Hakikat Kitabevi Toleo Namba 2

# DINI YA KIISLAM

MUANDAAJI
**HÜSEYN HİLMİ IŞIK**

**CHAPISHO LA SITA**

**Hakikat Kitabevi**
Darüşşefeka Cad. 53/A P.K.: 35
**34083** Fatih-ISTANBUL/TURKEY
Tel: 90.212.523 4556–532 5843 Fax: 90.212.523 3693
http://www.hakikatkitabevi.com
e-mail: info@hakikatkitabevi.com
-2022-

**BASKI:**
Ihlas Gazetecilik A.Ş.
Merkez Mah. 29 Ekim Cad. İhlas Plaza No: 11 A/41
34197 Yenibosna-İSTANBUL Tel: 90.212.454 3000

ISBN: 978-975-8883-91-2

# NJIA YA PEPONI

**Sifa njema ni za Allahu taala aliyetuweka miongoni mwa wanaotafuta mema na wenye kupenda elimu. Sala na salamu zimshukie mtume Muhammad, ambaye alitumwa hali ya kuwa rehma kwa walimwengu na masahaba zake wote.**

## UISLAMU: ALLAHU TAALA YUPO NA NI MMOJA

Allahu taala aliumba viumbe wote. Kila kitu mwanzoni hakikuwepo. Allahu taala pekee ndiye aliyekuwepo. Yeye huwepo daima. Yeye si kiumbe aliyezuka baadae. Kama asingekuwepo kabla, basi pangelazimika kuwepo nguvu zilizomuumba yeye. Kwani kutokuwepo kwa nguvu zinazoumba kitu kisichokuwepo humaanisha kuendelea kwa kutokuwepo kwa kitu hicho kisichokuwepo, hivi kwamba hakiwezi kuwepo. Ikiwa mwenye uwezo wa kukiumba alikuwepo, basi Allahu taala ni wa azali na milele na ndiye ambaye humiliki nguvu hizo. Kinyume na hayo, inawezekana kuhoji kwamba hizo nguvu za kuumba zilikuja baadae, hivyo kabla yake nguvu nyinginezo zilipaswa kuumba, jambo ambalo litakubalisha kuwepo kwa waumbaji kadhaa ambao idadi yao haina kikomo. Hata hivyo, hii ina maana kwamba hakuna mwanzo kwa waumbaji. Kutokuwepo kwa muumbaji wa mwanzoni husababisha kukosekana kwa uumbaji ambao ungetekelezwa. Ikiwa muumbaji atakosekana, basi viumbe wote hawa wa kimwili na kiroho ambao tunawaona au kuwasikia katika mazingira yetu wasingekuwepo. Lakini, kwa vile viumbe wa kimwili na kiroho wapo, basi lazima wawe na muumbaji mmoja wa azali na anayeishi milele.

Allahu taala aliumba kwanza madutu sahali, ambavyo ndio viundio vya viumbe vyote vya kimwili, kiroho na malaika. Madutu sahali leo hutambulika kama elementi/ vipashio. Kuna vipashio vipatavyo mia moja na tano ambavyo leo hii vinajulikana. Allahu taala ameumba, na kila uchao anaendelea kuumba, kila dutu na kila kitu kutokana na vipashio hivi mia moja na tano. Chuma, salfa, kaboni, gesi ya oksijeni, gesi ya klorini, kila kimoja wapo ni kipashio. Allahu taala hakusema ni miaka milioni ngapi iliyopita ndipo alipoviumba vipashio hivi. Wala hakutufahamishani lini alianza kuumba ardhi, mbingu na viumbe hai, ambavyo ni natija ya vipashio hivi. Kila kitu, kiwe kiumbe chenje uhai au kisicho na uhai, kina umri fulani ambao kitaishi. Allah hukiumba muda ukiwadia na hukiangamiza umri wake ukifikia mwisho. Yeye haumbi kitu kutokana na kutokuwepo tu kwa kitu hicho, lakini pia

hukiumba kitu kingine kutokana na kingine, pole pole au ghafla, na kile cha mwisho kuumbwa kikija maishani, cha mwanzo husita kuishi.

Allahu taala alimuumba mwanaadamu kutokana na madutu sahali na roho. Mwanaadamu hakuwepo kabla. Wanyama, mimea, majini na malaika walikuwa wameumbwa kabla ya mwanaadamu huyo wa kwanza kabisa. Huyo mwanaadamu wa kwanza aliitwa Adamu, amani ya Allah iwe juu yake. Kutokana naye, Allahu taala alimuumba mwanamke. Kutokana na hawa wawili, watu walizaana. Tunaona kwamba vitu vyote vilivyo na uhai na visivyokuwa na uhai sawia, vinabadilika. Kile ambacho ni cha milele hakipaswi kubadilika. Kuna mabadiliko miongoni mwa maumbile, hali na madutu. Tena mifanyiko ya kikemikali hubadilisha dhati na hali yake. Madutu yanasita kuishi huku mengine yakija kwenye uhai. Kwa upande mwingine, katika matukio ya kinyuklia, hata elementi/ vipashio vya kinyuklia hubadilika na kuwa nishati. Mchakato huu wa vitu kujitokeza vikitokana na vingine hauwezi kuwa wa azali usiokuwa na mwanzo. Lazima vilitokana na madutu ya mwanzo kabisa yaliyoumbwa na hayakuweko kabla. Kwani azali ina maana ya kutokuwa na mwanzo.

Maadui wa Uislamu wanajifanya wanasayansi na wanasema kwamba wanaadamu waliumbwa kutokana na kima. Wanasema kwamba daktari wa Kizungu anayeitwa Darwin alisema hivyo. Ni waongo. Darwin Charles [1809-82] hakusema hivyo. Alianzisha harakati za jinsi ya kuendelea kuishi miongoni mwa viumbe hai. Katika kitabu chake kiitwacho **The Origin of Species** aliandika kwamba viumbe hai viliendeleza tabia zilizoendana sana na mazingira yao na kwa kufanya hivyo vikapitia mabadiliko muhimu. Hakusema kwamba atomi moja hubadilika na kuwa nyingine. Katika kikao ambacho Jumuia ya Uingereza ya kuendeleza Sayansi iliandaa huko Salford mwaka wa 1980, Prof. John Durant wa Chuo cha Swansea alisema kwamba mtazamo wa Darwin wa kimageuzi kuhusu asili ya mwanaadamu umegeuzwa katika kisasili/uongo/ubunifu wa kisasa, jambo ambalo lina madhara kwa sayansi na maendeleo ya kijamii, kiasi kwamba uongo wa kisekula (elimu ya sekula) kuhusu mageuzi ulikuwa na taathira kubwa kwa utafiti wa kisayansi, ambazo zilisababisha upotoshaji , mgogoro usiohitajika na matumizi mabaya sana ya sayansi. Alihitimisha kwamba nadharia ya Darwin sasa imeenda mbali sana na hali ya kuwa imeacha nyuma marundo ya mawazo haribifu na danganyifu. Matamko haya aliyoyatoa Prof. Durant kumuhusu mwenzake ni miongoni mwa majibu yenye kuvutia sana yaliyotolewa kwa wana Darwin kwa jina la sayansi. Sababu kuu iliyojificha nyuma ya

jitihada zilizopo za kujaza watu shauku na nadharia hii ya kimageuzi katika ngazi fulani ya kitamaduni ni itikadi kengeushi. Hazihimili matilaba ya kisayansi. Ile iitwayo nadharia inatumika kama chombo cha kuingizia falsafa ya kiyakinifu. Hoja kwamba mwanaadamu alitokana na kima haina msingi katika elimu na ni mbali sana na sayansi. Wala si hoja ya Darwin. Inajikita katika uongo wa maadui wajinga wa Uislamu ambao hawana habari juu ya elimu na sayansi. Mtu mwenye elimu au mwanasayansi hawezi kutoa matamko ya kijinga na dhihaka kama hayo. Kama mtu aliyehitimu chuoni ataishi maisha ya upotovu na kusahau yale aliyosoma shuleni badala ya kujiendeleza na masomo yake katika taaluma aliyozamia, kamwe hawezi kuwa mtu mwenye elimu au mwanasayansi. Baya zaidi ni kuchukuwa kwake kinga ya Uislamu na kujaribu kusambaza maneno yake na maandishi ya uongo kwa jina la elimu na sayansi na hivyo yakaishia kuwa kama msingi danganyifu yenye madhara kwa jamii. Katika hali hiyo diploma yake, cheo na wadhifa wake vitakuwa mitego ya kujishaua ya kuwawinda vijana. Wanasayansi walaghai wanaosambaza uongo wao wenyewe na kashfa kwa jina la elimu na sayansi wanajulikana kama **walaghai wa sayansi**.

Allahu taala anachotaka ni watu kuishi kwa raha na amani duniani na wapate kujivunia huko akhera. Kwa sababu hii, anawaamrisha kufanya mambo yenye faida yatakayo wapelekea kupata raha na anawakataza yale yenye madhara yatakayosababisha maangamizi. Endapo mtu atatenda, bila kujali ni mshikadini au si mshikadini, muumini au sio muumini, aliyeshikamana na sheria za Kiislamu, yaani maamrisho na makatazo ya Allahu taala, hali ya kuwa anafanya hivyo kwa kujua au kutojua, kiwango cha raha na amani watakachopata katika maisha ya dunia hii yatakuwa sambamba na kiwango cha utiifu wao kwa mfumo huo wa sheria. Ni sawa na kaida isemayo kwamba (yeyote anayetumia matibabu muafaka atapona maradhi). Mafanikio ya hivi sasa wanayojivunia wasoshika dini ya Allah mengi ni kwa sababu ya kutenda matendo yao kwa namna ambayo imetokea kuafikiana na Quran tukufu. Hata hivo, kujivunia kwa milele kwa kutii Quran tukufu, huwezekana tu iwapo utiifu huo utatekelezwa na muumini kwa kujua.

Sheria ya kwanza ya Allahu taala ni kuwa na imani. Ukafiri ni jambo alililoliharamisha kabla ya uovu wowote mwingine. Imani maana yake ni “kuamini ukweli kwamba Allahu taala ni mmoja asie na mshirika wala mfano na Muhammad rehma na amani ziwe juu yake ni mtume wa Allahu Taala wa mwisho”. Allahu taala alimpa yeye maamrisho yake kupitia ufunuo. Yaani aliteremsha kwake sheria zake za Kiislamu

kupitia malaika, naye akazifafanua zote kwa watu. Neno lililoteremshwa kupitia kwa malaika linajulikana kama Quran tukufu. Kitabu ambacho kina matini yote ya Quran iliyoandikwa inajulikana kama **mas-hafu** (nakala ya Quran tukufu). Quran tukufu si matamko ya mtu binafsi aliyoyatoa mtume Muhammad rehma na amani ziwe juu yake, bali ni neno la Allahu taala. Hakuna mwanaadamu anayeweza kutoa tamko hata moja ambalo linafanana na aya zake katika ukamilifu. Sheria zilizofundishwa katika Quran tukufu, kwa pamoja zinajulikana kama Uislamu. Mtu mwenye kuziamini kwa moyo wake anajulikana kama muumini na Muislamu. Kuchukia hata sheria moja tu ni **ukafiri**. Kuamini kufufuliwa baada ya kifo, uwepo wa majini na malaika, ukweli kwamba Adam ni baba wa binaadamu wote na ni mtume wa kwanza kabisa, ni kazi ya moyo tu. Mambo haya ya ukweli yanaitwa mafundisho ya **imani** au **akida**. Ama kuhusu maamrisho ambayo yanapaswa kutekelezwa na makatazo ambayo yanapaswa kuepukana nayo kwa matendo na kwa moyo, ambayo ni lazima kuyaamini na kuyatenda au kuyaacha hayo huitwa mafundisho ya sheria za Uislamu. Kuyaamini ni miongoni mwa vitendo vya imani pia. Kuyaweka vitendoni au kuyaacha ni ibada. Ni kitendo cha ibada kutekeleza sheria za Kiislamu kwa kuleta nia kwanza. Maamrisho na makatazo ya Allahu taala yanaitwa sheria za Kiislamu ama sheria za kiibada/ kiungu. Maamrisho yanaitwa fardh na makatazo yanaitwa haram. Ni dhahiri kwamba mtu anayekana na kuchukia hata kitendo kimoja kati ya vitendo hivyo huwa kafiri (adui wa Allahu taala). Mtu anayeamini sheria hizo lakini akawa na udhaifu katika kuzitilia maanani hawi kafiri bali ni Muislamu ambaye ni **fasik** (mtenda madhambi). Muumini ambaye huyaamini mafundisho ya Uislamu na akayatekeleza kwa uwezo wake wote huitwa Muislamu mwema (**Muslimun salih**). Muislamu anayetii Uislamu akampenda murshid (muongozaji) kwa ajili ya kupata huruma na mapenzi ya Allahu taala huitwa mtu mwema. Muislamu ambaye ameshapata huruma ya Allah na mapenzi yake huitwa ʻarif au walii. Walii ambaye hutoa huduma kama njia mojawapo ya wengine kupata mapenzi Allah anaitwa murshid (muongozaji). Watu hawa wote wateule kwa pamoja huitwa watu wa kweli. Wote ni watu wema. Muumini mwema kamwe hataingia motoni.

**Kafiri** (adui wa Allahu taala) bila shaka ataingia motoni. Hatatoka motoni kamwe na atapewa adhabu zisizo na kikomo. Endapo kafiri atakuwa na imani (atakuwa muumini), madhambi yake yataghufiriwa mara moja. Endapo muasi atatubia kisha aanze kutenda vitendo vya ibada, ima hataingia motoni kamwe, na ataenda peponi moja kwa

moja kwa kupata maombezi au pasina njia yoyote katikati; au atachomwa motoni kadri anavyostahiki kutokana na madhambi yake na aingie peponi baadae.

Quran tukufu ilipoteremshwa, sarufi yake inalingana na lugha ya Kiarabu iliyokuwa ikizungumzwa na watu wa zama hizo, na katika umbo la kishairi. Yaani ina mizani kama ushairi. Imesheheni Kiarabu ambacho ni kigumu kutambulika. Ni bora katika sayansi za lugha ya Kiarabu na balagha kama vile elimu ya al-badi'i (taaluma inayochunguza ujumi wa lugha), elimu ya albayani na elimu ya al ma'ani. Kwa hiyo, ni ngumu kuielewa, mtu asiyekuwa na asili ya Kiarabu hawezi kuelewa vyema Quran tukufu, hata kama ni mjuzi wa Kiarabu. Hata wale waliokuwa na uasili huo hawakuweza kuifahamu, kwa hiyo bwana wetu mtume alieneemeshwa, alieleza sehemu kubwa (ya Quran). Ufafanuzi wa mtume wa Quran tukufu unaitwa **hadithi sharif**. Masahaba wa mtume "radiyallahu anhuma" ziwe juu yao wote, walifikisha mafundisho waliyoyasikia kutoka kwa mtume "swallallahu alaihi wa sallam" (rehma na amani ziwe juu yake) kwa vizazi ambavyo vilikuwa vidogo kabisa. Katika kipindi fulani nyoyo za watu ziliingiwa kiza kiasi kwamba baadhi ya Waislamu wapya walijaribu kuitafsiri Quran tukufu kwa maoni na mawazo yao finyu, na kwa kufanya hivyo wakatoa maana zisizokubaliana na ufafanuzi wa bwana mtume. Kutokana na uchochezi wa nyufa uliofanywa na maadui wa Uislamu, palizuka madhehebu sabini na mbili ya uongo. Waislamu wanaofuata madhehebu hayo wanaitwa wanabid'a au waliopotea. Kwa yakini makundi hayo yote sabini na mbili ya bid'a yataenda motoni lakini kwa vile ni Waislamu, hawataishi motoni milele, hatimae wataingia peponi. Kama imani anayoishikilia mtu itatofautiana na ile iliyoko kwenye mafundisho ya Quran tukufu na hadithi tukufu, mtu huyo huwa hana Imani na huaitwa **mulhid** (anae pinga kuwepo kwa mungu). Mulhid anajidhani kwamba ni Muislamu.

Wanazuoni wa Kiislamu Allah awarehemu waliojifunza mafundisho ya akida, yaani mihimili ya imani kwa usahihi kutoka kwa sahaba watukufu "radiyallahu anhuma" ziwe juu yao wote na wakayaandika mafundisho hayo yaliyo sahihi katika vitabu wanajulikana kama **Ahl as-Sunna.** Wao ni wanazuoni waliofikia kiwango cha ijtihad katika mojawapo ya madhehebu manne. Wanazuoni hawa walishikilia imani kama walivyojifunza kutoka kwa masahaba watukufu wala hawakujaribu kuelewa maana ya Quran tukufu kulingana na maoni na mitazamo yao binafsi. Walisambaza mafundisho ya ukweli waliyojifunza kutoka kwa mtume wetu, badala ya kufuata uelewa wao

binafsi. Dola la Uthman lilikuwa dola la kiislamu na lilishikilia imani ya kisunni.

Kama inavyoeleweka kutokana na yaliyoandikwa mpaka sasa, na yaliyoandikwa kwenye vitabu vingi vyenye thamani, ili kusalimika kutokana na maafa ya dunia hii na akhera, na kuishi maisha yenye raha na furaha, ni muhimu kushikilia imani iliyofundishwa na wanazuoni wa Ahl as-Sunna na watu walioongoka, yaani kujifunza mihimili yake na kuiamini yote. Mtu asiyeshikamana na imani ya kisunni na ya walio ongoka huitwa mwanabid'a, yaani Muislamu muasi au kafiri. Wajibu wa pili wa Muislamu mwenye imani ya kweli na akida sahihi ni kuwa salih, yaani kufikia huruma na mapenzi ya Allahu taala. Kwa kuzingatia lengo hilo, lazima mtu apate mafundisho ya Uislamu yanayohusu ni nini ambacho kinapaswa kufanyika na yale yanayopaswa kuachwa, kimwili na kiroho na aishi kulingana na muongozo huo. Kwa maneno mengine mtu anapaswa kutekeleza vitendo vya ibada. Wanazuoni wa Ahl as-Sunna na watu walioongoka walielezea vitendo vya ibada kwa namna nne tofauti. Hali hiyo basi ilipelekea kujitokeza kwa madhehebu manne yanayotambulika katika Uislamu. Kwa vile masuala ambayo wao wanahitilafiana ni madogo na si muhimu sana, wanahurumiana na kuheshimiana madamu mihimili inayowaunganisha ni sawa. Kila Muislamu anapaswa kutekeleza vitendo vyao vya ibada kwa kutii moja wapo ya madhehebu haya manne na ya watu walioongoka. Kusema kwamba mtu asiyeshikamana na madhehebu yoyote kati ya madhehebu hayo manne na ya watu walioongoka atakuwa ameacha njia pekee iliyosahihi ya Ahl as-Sunna na ya watu walioongoka ni ukweli usiopingika ambao umeandikwa pia katika sura iitwayo **Dhabaih**, sherehe ya Ahmad bin Muhammad bin Ismail Tahtawi [aliyefariki dunia mwaka wa 1221 (1815 A.D.) Allahu taala amrehemu] ya kitabu cha Alauddin Haskafi (1021-108 [1677 A.D.]) kiitwacho **Durr ul-Mukhtar**.

Kafiri akisema "Nimesilimu", ni lazima kumuamini hata kama ni mateka wa vita au amesema hivyo wakati wa amani. Lakini anapaswa kujifunza nguzo za imani na kuziamini haraka iwezekanavyo. Baadaye atajifunza na kutekeleza maamrisho ya Uislamu yaitwayo fardh na kuepukana na makatazo yake yajulikanayo kama haram kila inapomuajibikia na endapo atapata fursa ya kufanya hivyo. Wasipojifunza mambo hayo, au wakidharau na kupuuza hata jambo moja kati ya mambo hayo baada ya kuwa wamejifunza, watakuwa wamepuuza dini ya Allahu taala na watapoteza imani yao. Watu wanaopoteza imani yao kwa namna hii wanaitwa **murtad** (waasi). Murtadi ambao wanajigamba kuwa washikadini lakini wakawa

wanawapotosha Waislamu wanajulikana kama **zindik.** Hatupaswi kuwaamini mazindik wala uongo wao. Kama ilivyoandikwa katika ukurasa wa mia moja na sitini wa kitabu kiitwacho Siyar-i-kabir cha Kituruki, na pia katika sehemu ya mwisho ya kitabu kiitwacho Dur ul-Mukhtar sura inayohusu ndoa ya kafiri, mtu akibaleghe pasi na kusilimu au kutambua katika moyo wake kwamba ni Muislamu, ikiwa kwa sababu ni mbumbumbu haujui Uislamu na sio kutokana na kuzama kwake katika matamanio ya dunia, basi atahukumiwa kuwa murtad (mkanaji dini/ muasi). Imeandikwa katika sehemu ya mwisho ya Durr ul-Mukhtar sura inayohusu ndoa ya kafiri kwamba msichana Muislamu aliyeolewa katika ndoa ya Kiislamu akibaleghe bila kuujua Uislamu, ndoa yake huwa batili. [Kwa maneno mengine yeye huwa murtadi]. Itabidi afunzwe sifa za Allahu taala. Itabidi arudie/ akariri yale anayosikia na aseme, “Naziamini”. Ibn Abidin "rahmatullahi alaih" anafafanua suala hili kama ifuatavyo, “Msichana akiwa mdogo (yaani akiwa haja baleghe), anakuwa Muislamu, kwa vile dini yake hutambulika kutokana na ile ya wazazi wake. Akibaleghe hatategemea tena dini ya wazazi wake. Akibaleghe akatoka kwenye Uislam hali ya kuwa mbumbumbu katika Uislamu, atakuwa murtadi. Mtu asiyeamini nguzo za Uislamu pamoja na kwamba amezisikia, akitamka tu neno la tawhidi, yaani iwapo atasema, **“La ilaha illaallah Muhammadun rasulullah”,** kitendo hicho hakitamfanya kuwa Muislamu. Mtu anayeamini nguzo sita zilizoelezewa katika tamko, “Aamantu billahi” na anayesema, “Nimekubali kufuata maamrisho na kuacha makatazo ya Allahu taala,” huwa Muislamu. Kwa hiyo, Waislamu wote wanapaswa kuhakikisha kwamba watoto wao wanahifadhi nguzo sita za imani zilizotajwa katika tamko, **“Aamantu billahi wa malaaikatihi** (na malaika wake) **wa kutubihi** (na vitabu vyake) **wa rusulihi** (na mitume wake) **wal- yaumil akhiri** (na siku ya mwisho) **wa bil- qadari khairihi wa sharrihi minallahi taala** (na kheri na shari zinatokana na Allahu taala) **wal-baathu baadal mauti haqqun** (na kufufuliwa baada ya kufa ni haki) **Ash- hadu an Laailaahailla Allahu wa ash-hadu anna Muhammadan ‘abduhu wa rasuuluh‘.”** (Na nashahadia kwamba hakuna mola anayepaswa kuabudiwa kwa haki isipokuwa yeye Allah taala na mtume Muhammad "swallallahu alaihi wa sallam" juu yake ni mja wake na mtume wake) na ajifundishe maana yake sawa sawa. Mtoto asipoamini nguzo hizi au mojawapo ya maamrisho na makatazo ya Allahu taala na asiposema anaziamini, atakuwa murtadi, na siyo Muislamu, akibaleghe.”

Maelezo kamili kuhusu nguzo hizi sita hupatikana katika kitabu kiitwacho “Imani na Uislamu” (mojawapo ya machapisho ya Hakikat Kitabevi katika maktaba ya Istanbul). Kila Muislamu anahimizwa kukisoma kitabu hicho, yeye na watoto wake, ili kuimarisha imani, na pia wajitahidi kadri ya uwezo wao kuwahimiza marafiki zao kukisoma. Ni muhimu kuchukua tahadhari ili watoto wetu wasikuzwe wakiwa murtadi (wasikulie katika hali ya uasi/kumkana Allah). Katika hatua za kwanza za utoto, tunapaswa kuwafunza imani, Uislamu, kutawadha, kuoga na sala. Kazi muhimu ya wazazi ni kuwalea/ kuwakuza watoto wetu kama Waislamu (juu ya msingi wa Uislamu).

Imetajwa katika kitabu kiitwacho **Durer wa Ghurer** kwamba “Mwanaume anayeritadi anapaswa kuambiwa asilimu”. Lazima aachane na shaka zake. Akiomba apewe muda wa kufikiria, atawekwa jela kwa siku tatu. Akitubia (yaani akitubu juu ya dhambi zake kubwa akamuomba Allah msamaha), huku akimuahidi kuwa kamwe hatatenda tena dhambi hiyo kubwa, toba yake itakubaliwa. Asipotubia, basi atauliwa na hakimu wa kiislamu. Mwanamke anayeritadi hatauwawa. Atatiwa mbaroni na kuwekwa gerezani mpaka atakaposilimu. Akitorokea katika nchi ya vita (iliyotangaza vita dhidi ya nchi ya kiislamu), madhali yumo katika nchi hiyo, hatakuwa jariya (mtumwa). Akichukuliwa mateka atakuwa jariya (mtumwa). Akisharitadi ndoa yake itabatilika. Mali yake yote itatoka kwenye milki yake (yaani haitakuwa tena milki yake). Akisilimu tena itakuwa milki yake. (Mwanamke) akifariki dunia au akitorokea katika darul harb nchi ya vita [au akiritadi akiwa katika nchi ya vita], mali yake itakuwa turathi ya warithi wake. [Kama hana warithi, mali hiyo itarithiwa na watu wanaostahiki kupewa kitu kutoka kwenye mfuko wa baitul maal]. Murtadi hairithi mali ya murtadi mwingine. Mali inayomilikiwa na murtadi (mwanamume au mwanamke) haitakuwa milki yake. Itakuwa milki (fey) ya Waislamu. (Neno fey limetafsiriwa katika sura ambayo kichwa chake ni **NDOA YA MAKAFIRI** na imeambatanishwa kwenye sura ya kumi na tano ya kitabu kijulikanacho kama **Endless Bliss**). Vitendo vyake vyote vya kijamii kama vile kununua na kuuza, mikataba ya kupangisha, na sadaka, vitakuwa batili. (Tafadhali tazama sura ya thelathini na moja ya Endless Bliss kwa maelezo ya ‘batil’). Itarejea katika hali yake ya kwanza na kuwa sahihi ikiwa atakuwa Muislamu tena. Hatatakiwa kufanya kadhaa kwa vitendo vyake vya ibada vilivyotangulia, isipokuwa kitendo cha hija, ambayo atapaswa kuitekeleza upya. Vitendo vitatu vya kwanza vya ibada ambavyo

muumini mpya anapaswa kujifunza ni namna ya kutawadha, kuoga na kusali.

Nguzo sita za imani ni; kuamini kwamba Allahu taala yupo na ni mmoja na kuamini sifa zake, kuamini malaika, mitume, vitabu vilivyoteremshwa kutoka mbinguni, matukio yatakayo tokea Akhera, qadhaa na qadar. Baadaye, tutafafanua kila mojawapo ya nguzo hizo.

Kwa ufupi, lazima tutekeleze maamrisho ya Allahu taala na tuepukane na makatazo yake kiroho na kimwili na nyoyo zetu lazima ziwe katika tahadhari ili zisije zikazama katika mghafala (usahaulifu, ujinga, uvivu). Moyo wa mtu usipokuwa chonjo (yaani asipotambua uwepo na ukubwa wa Allahu taala na ladha ya fikra za baraka katika mbingu na hisia kali za adhabu ya moto wa jahannam), itauwia vigumu mwili wa mtu huyo kushikamana na Uislamu. Wanafiqhi hutoa fatwa kadhaa wa kadhaa (yaani majibu ya wanazuoni wa Kiislamu ambao ndio wenye mamlaka juu ya kujibu maswali yanayohusu namna ya kutekeleza vitendo vya ibada). Hunakiliwa kwa waja wa Allahu taala ili ziwe rahisi kutekelezeka. Ili watu washikamane na Uislamu kwa hima, wepesi na kuridhika, kuna haja ya kuwa na nyoyo safi. Hata hivyo, ikiwa mtu atazingatia tu usafi wa moyo na uzuri wa tabia ilhali anapiga kikumbo utiifu wa sheria za kiislamu, basi mtu huyo ni **mulhid**. Mafanikio ya kimaajabu ya watu kama hao [kama vile kutoa utabiri wa yale yasiyojulikana na kuwaponya wagonjwa kwa kuwapulizia] yanachukuliwa kama istidraj (kupewa muda mtu aendelee kufanya madhambi yake ili kuzama katika dimbwi la maasi) na yatawakokota/ buruta wenyewe pamoja na wale wanaopendezwa nayo hadi motoni. Dalili ya moyo ulio msafi na nafsi tulivu (tiifu) ni kushikamana na maamrisho na kuachana na makatazo ya Allah na kuwa mtu wa Uislamu kwa hiyari. Kujigamba kwa watu wasioelekeza hisia na miili yao kwa Uislamu ni maneno matupu (yasiyokua na mashiko). Kwa kusema hivyo, wanajidanganya na kuwadanganya watu waliowazunguka.

# SIFA ZA IMANI

Wanazuoni wanasema kwamba imani ina sifa sita.

**Aamantu billahi**; Naamini kwamba Allahu taala yupo na ni mmoja. Hana mshirika wala nadhwir. (Hana mshirika wala anayemfanana). Yeye ni munazzah (yuko huru, ametakasika) kutokana na makan (mahali). Hayuko katika mahali mahsusi.

Yeye ni muttasif (anasifika) na sifa zake za ukamilifu (kamal), yuko mbali na sifa za upungufu. Yeye hana sifa hizo. Sifa za ukamilifu zipo kwenye dhati yake na sifa za upungufu zipo kwetu sisi wanaadamu. Sifa za upungufu tulizo nazo ni mapungufu kama vile kuwa na mikono na/ au miguu na/ au macho, ugonjwa na siha, kula na kunywa, na mengine mengi kama hayo.

Sifa alizonazo Allahu taala ni za ukamilifu kama vile kuumba kwa ardhi na mbingu na viumbe wote wapigao mbizi, waishio angani, majini, ardhini na chini ya ardhi, kuwahifadhi wakati wote viumbe wengi tunao watambua baadhi yao na wengine wengi tusiowatambua kutokana na uwezo wa mwanaadamu uliowekewa mipaka, riziki yake kwa viumbe hawa wote (chakula, kujikimu), na sifa zake nyingine za ukamilifu. Yeye ni qadir-il-mutaq (Mwenye nguvu). Kila kiumbe ni zao linalotokana na sifa za ukamilifu wa Allahu taala.

Kuna sifa ishirini na mbili zinazomhusu Allahu taala na ni wajibu kwetu kuzijua. Aidha, kuna sifa nyingine ishirini na mbili ambazo ni muhali (haifikiriki, haiyumkiniki kwake yeye kusifika nazo).

Wajibu maana yake ni lazima. Sifa za aina hii anazo Allahu taala. Allahu taala hana sifa zilizo muhali. Muhali ni kinyume cha wajibu. Maana yake ni “Haiwezekani kuwepo”.

Kuna sifa moja inayomhusu Allahu taala ijulikanayo kama sifat-i-nafsiyya na ambayo ni wajibu juu yetu kuijua: Wujuud, ambayo ina maana ya “kuwepo”.

Ushahidi wa kuthibitisha kwamba Allahu taala yupo ni kauli tukufu isemayo: “innani ana Allahu”. Ushahidi wa kuthibitisha kiakili ni kwamba bila shaka muumbaji yupo aliyeumba viumbe hawa wote. Ni muhali kwake yeye kutokuwepo.

Sifat-i-nafsiyya ina maana kwamba kwa dhati pasi na yeye ni jambo ambalo haliwezi kutambulika wala kufikirika.

Kuna sifa tano zinazohusika na Allahu taala zinazorejelewa kama sifat-i-dhatiyya na ambazo ni wajibu juu yetu kuzijua: zinajulikana pia kama **Sifaat za Uluhiyya** (sifa za Uungu).

1- **Qidam**, ambayo inamaanisha kuwa uwepo wa Allahu taala hauna mwanzo.

2- **Baqaa**, humaanisha kuwa uwepo wa Allahu taala hauna mwisho. Hurejewa pia kama wajibul wujuud. Ushahidi wake kutokana na Quran tukufu ni aya ya tatu ya Sura al-Hadyd. Ushahidi wake wa kiakili ni kuwa uwepo wake ungalikuwa na mwanzo au mwisho angalikuwa asie na uwezo na angekuwa mwenye upungufu. Na asie na uwezo na mwenye upungufu asingeliweza kuwaumba viumbe wengine. Hivyo basi, ni muhali (haiwezekani uwepo wake kuwa na mwanzo au /na mwisho).

3- **Qiyam binafsihi**, ambayo humaanisha kuwa Allahu taala hana haja na yeyote katika dhati yake, sifa zake wala vitendo vyake. Ushahidi wake kutokana na Sura Muhammad, aya ya mwisho. Ushahidi wa kiakili ni kwamba asingelikuwa na sifa hizi asingelikuwa mwenye uwezo na angekuwa mwenye upungufu. Kutokuwa na uwezo au kuwa mwenye upungufu ni muhali kwake yeye Allahu taala.

4- **Mukhaalafat-un-lilhawaadith**, humaanisha kwamba Allahu taala hafanani na mtu yeyote katika dhati yake na pia katika sifa zake. Ushahidi wake kutokana na andiko takatifu ni tangazo lake Allahu taala katika aya ya kumi na moja ya Sura Ash-Shuara. Ushahidi wake kiakili ni kwamba asingelikuwa na sifa hizi asingelikuwa na uwezo na angalikuwa na upungufu. Kutokuwa na uwezo na kuwa na upungufu ni muhali kwa Allahu taala.

5- **Wahdaaniyyat**, humaanisha kwamba Allahu taala hana mshirika wala amfananaye, sio katika dhati yake tu bali pia katika sifa na vitendo vyake. Ushahidi kutokana na Quran tukufu aya ya kwanza ya Suratul Ikhlas. Ushahidi wa kiakili ni ukweli kwamba angalikuwa na mshirika viumbe wote wasingalikuwepo. Kwani mmoja wao angalipenda kuumba kitu na wakati huo huo mwengine angelizuia kisiumbwe.

[Kwa mujibu wa wanazuoni wengi wa Kiislamu, Wujuud, yaani uwepo, ni sifa bainifu. Hivyo basi, kuna sifa sita chini ya dhana ya **Sifaat adh-Dhaatiyya**].

## SIFAAT-U-THUBUUTIYYA

Kuna sifa nane zinazomuhusu Allahu taala ambazo ni wajibu kwetu kuzijua na ambazo huangukia katika sifati dhati zijulikanazo kama Sifaat-u-Thubuutiyya nazo ni Hayat - uhai, Ilmu - elimu (yaani ujuzi au maarifa ya uwelewa), Sam'u - kusikia, Baswar - kuona, Irada - kutaka, Qudrat - kukadiria au kupanga, Kalam - kuzungumza au kuongea, Takwin - kuumba.

**Maana ya sifa hizi ni kama ifuatavyo;**

1- **Hayat -** humaanisha kwamba Allahu taala yupo hai. Ushahidi wake ni sehemu ya kwanza ya aya ya mia mbili hamsini na tano ya Suratul Baqarah. Ushahidi wa kiakili ni ukweli kwamba Allahu taala asingelikuwa hai, viumbe hawa wasingelikuwepo.

2- **Ilmu-** humaanisha kwamba Allahu taala ana ujuzi. Ushahidi wake ni aya ya ishirini na mbili ya Sura al-Hashr. Ushahidi wa kiakili juu yake ni ukweli kwamba Allahu taala asingelikuwa na uwezo na ukamilifu kama hakuwa na ujuzi. Kutokuwa na uwezo na ukamilifu ni muhali kwa Allahu taala.

3- **Sam'u-** humaanisha kwamba Allahu taala anasikia. Ushahidi juu yake ni aya ya kwanza katika Suratul Israa.

4- **Baswar -** humaanisha kwamba Allahu taala anaona. Ushahidi wake pia ni aya ya kwanza ya Suratul Israa. Ushahidi wa kiakili ni kwamba kama Allahu taala angekuwa hana uwezo au ukamilifu asingekuwa na sifa ya kuona. Kutokuwa na uwezo na ukamilifu ni muhali kwa Allahu taala.

5- **Irada -** humaanisha kwamba Allahu taala alitakalo hua. Hakuna litokealo pasina yeye kutaka liwe. Alitaka viumbe wawepo akawaumba. Ushahidi wake ni aya ya ishirini na saba ya Sura Ibrahim. Ushahidi wa kiakili ni asingekuwa na uwezo na ukamilifu kama hakuwa na sifa ya kutaka liwe liwalo. Kutokuwa na uwezo na ukamilifu ni muhali kwa Allahu taala.

6- **Qudrat -** humaanisha kwamba Allahu taala ni Mwenye nguvu. Ushahidi ni aya ya sitini na tano ya Sura Aali-Imran. Ushahidi wa kiakili ni kwamba asingekuwa mwenye nguvu basi asingekuwa mwenye uwezo na ukamilifu. Ni muhali kwa Allahu taala kutokuwa mwenye nguvu na ukamilifu.

7- **Kalam -** humaanisha kuwa Allahu taala ana uneni yaani kuongea. Ushahidi wake ni aya ya mia moja sitini na nne ya Suratul Nisaa. Ushahidi wa kiakili ni kwamba asingelikuwa na uneni yaani kuongea asingelikuwa na uwezo na ukamilifu. Kutokuwa na uwezo na ukamilifu ni muhali kwa Allahu taala.

8- **Takwiin -** humaanisha kwamba Allahu taala ni Muumbaji, (yaani ana nguvu za kuumba, kwa hiyo anaumba). Yeye pekee ndiye anayeumba kutokana na hali ya kutokuwepo. Ushahidi ni aya ya sitini na mbili ya Sura Az-Zumar. Ushahidi wa kiakili ni kwamba yeye ameumba viumbe anuwai aina tofauti tofauti vyenye kustaajabisha ardhini na mbinguni, na ni muumbaji pekee wa viumbe wote. Ni kitendo cha ukafiri kusema "uumbaji" ukimrejelea yeyote ambaye si Allahu taala. Mwanaadamu hawezi kuumba kitu chochote.

Allahu taala ana sifaati maanawiyya (sifa zisizokuwa za mguso) ambazo ni wajibu juu yetu kuzijua nazo ni Hayyun, Aliimun, Samiiun, Baswiirun, Muriidun, Qaadirun, Mutakallimun, Mukawwinun.

**Maana za sifa hizi ni;**

1- Hayyun: Allahu taala yu hai.

2- 'Aliim: Ana ujuzi wa milele unaorejelewa kama 'ilmil qadiim.

3- Samiiun: Allahu taala anasikia na kusikia kwake ni kwa milele (sam'il qadiim).

4- Baswiirun: Allahu taala anaona.

5- Muriidun: Allahu taala anataka na kutaka kwake ni kwa milele (Iraadatil qadiima).

6- Qadiirun: Allahu taala ni mwenye nguvu na nguvu zake ni za milele (Qudratil qadiima).

7- Mutakallimun: Allahu taala ni mwenye kuzungumza na kuzungumza kwake ni kwa milele (Kalaamil qadiim).

8- Mukawwinun: Allahu taala ni Muumbaji na anaumba kila kitu.

Sifa ambazo ni muhali kwa Allahu taala ni kinyume cha zile zilizotajwa hapo awali.

**WA MALAAIKATIHI**: Na kuamini pia malaika wa Allahu taala. Allahu taala ana malaika kadha wa kadha. Aliwaumba kutokana na nuru. Ni wenye miili (ajsaam). Mwili (jism) uliotajwa katika muktadha huu si ule uliotajwa kwenye vitabu vya fizikia. Hawali wala hawanywi. Hawana jinsia. Huteremka na kupanda mbinguni. Hujitokeza katika sura mbalimbali. Hawamuasi Allahu taala hata kiasi cha kufumba na

kufumbua jicho wala kutenda madhambi kama sisi. Miongoni mwao kuna muqarrab [2] na mitume.

**WAKUTUBIHI**: Na kuamini pia vitabu vya Allahu taala. Allahu taala ana vitabu. Kuna vitabu mia moja na nne vilivyotajwa katika Quran tukufu. Mia moja kati yao ni vitabu vidogo vidogo. Vinajulikana kama 'Suhuf'. Vinne kati yao ni vitabu vikubwa. Taurat iliteremshwa kwa Nabii Musa "alaihis-salaam", Zabuur ikateremshwa kwa Nabii Daud "alaihis-salaam", Injiil ikateremshwa kwa Nabii Issa "alaihis-salaam", na Quran kwa bwana wetu mtume Muhammad "swallallahu alaihi wa sallam". Chapisho letu moja hutoa taarifa kamili kuhusu vitabu vinavyojulikana kama Taurati na Biblia ambavyo husomwa na Mayahudi na Wakristo wa siku hizi.

Kati ya suhufi mia moja, kumi ziliteremshwa kwa Adam "alaihis-salaam", hamsini kwa Seth "alaihis-salaam", thelathini kwa Idris "alaihis-salaam", na kumi kwa Ibrahim "alaihis-salaam". Suhufi zote ziliteremshwa na Jibriil "alaihis-salaam". Quran tukufu ni kitabu cha mwisho kati ya vitabu vilivyoteremshwa kutoka mbinguni. Kuteremshwa kwa Quran, kwa muda tofauti tofauti kulingana na matokeo na mahitaji kwa sura nzima na aya, kulichukuwa miaka ishirini na mitatu na sheria zake zitadumu hadi mwisho wa dunia. Imehifadhiwa kutokana na hali ya kutiwa mkono, kubadilishwa na kufanyiwa mageuzi na binadamu [kutokana na kubadilishwa na kunajisiwa na mwanaadamu].

**WA RUSULIHI**: Na kuamini pia mitume wa Allahu taala.

Allahu taala ana mitume (Amani iwe juu yao). Mitume wote ni wanaadamu. Adam amani iwe juu yake ni mtume wa kwanza na Muhammad rehma na amani iwe juu yake ni mtume wa mwisho. Kati ya mitume hawa wawili kuna mitume wengine wengi waliokuja. Allahu taala ndie anayejua idadi yao.

Kuna sifa tano ambazo tunapaswa kuzijua kuhusu mitume amani iwe juu yao. Nazo ni Swidiq (ukweli), Amana (uaminifu), Tabligh (ufikishaji), I'iswimat (kuhifadhiwa na kulindwa na kutofanya maasi) na Fatwana (uhodari wa akili ya vipawa vya juu).

1- Swidiq: Mitume wote amani iwe juu yao ni waaminifu katika yale wayasemayo, Yote wanayosema ni ya ukweli.

2- Amanat: Ni waaminifu kwani hawavunji ahadi.

3- Tabligh: Wanayapokea na kuyafahamu maamrisho na makatazo ya Allahu taala yote na huyafikisha kwa wafuasi wao.

4- I‘iswimat: Inamaanisha kwamba wameepukana na madhambi makubwa na madogo sawia. Hawafanyi madhambi. Mitume amani iwe juu yao ni kundi pekee la watu ambao hawana madhambi. [Mashia wanadai kuwa kuna kundi jingine la watu ambao hawafanyi madhambi].

5- Fatwaanat: Inamaanisha kwamba mitume wote amani iwe juu yao ni werevu kuliko watu wengine.

Kuna sifa tano ambazo zinafaa kwa mitume kuwa nazo: Wanakula na kunywa, wanaugua maradhi na wanakufa, wanahama kutoka dunia hii na kuelekea katika dunia nyingine ambayo ni akhera, hawapendi sana dunia hii.

Kuna mitume wapatao ishirini na tano ambao wametajwa katika Quran tukufu. Kuna kauli ya wanazuoni isemayo kwamba kuyajua majina yao ni jambo la lazima kwa kila mtu.

Majina ya mitume Amani iwe juu yao:

**Adam, Shith (Seth), Idris, Nuh, Hud, Swalih, Ibrahim, Lut, Ismail, Ishaq, Yaqub, Yusuf, Ayyub, Shua’ib, Musa, Harun, Khidr, Yusha ibn Nun, Ilyas, Alyasa, Dhul-kifl, Shamun, Ishmoil, Yunus ibn Meta, Daud, Sulaiman, Loqman, Zakariya, Yahya, Uzair, Issa ibn Mariam, Dhul-qarnain na Muhammad "swallallahu alaihi wa sallam".** Kuna kutofautiana kuhusu Uzair, Loqman na Dhulqarnain. Baadhi ya wanazuoni walisema kwamba watu hawa pamoja na Khidr pia walikuwa mitume, huku wengine wakisema kwamba walikuwa mawalii. Imeandikwa katika barua ya thelathini na sita toleo la pili la Maktubat-i-Ma’thuumiyya kwamba kuna kauli ya kisomi yenye kuridhisha isemayo kwamba Khidr amani iwe juu yake alikuwa mtume. Kama ilivyotajwa katika barua ya mia moja themanini na mbili, kujitokeza kwa Khidr kwa sura ya mwanaadamu, na kutenda matendo fulani fulani hakuoneshi kwamba yuko hai. Allahu taala aliruhusu roho yake pamoja na roho za mitume wengi na mawalii kuonekana katika sura za wanadamu. Kuwaona haina maana kwamba wako hai.

Kwa hiyo, unapaswa kusema Alhamdulillahi mimi ni kizazi cha Adam "alaihis-salaam" na ni miongoni mwa umma wa mtume wa mwisho, Muhammad swala na salamu ziwe juu yake. Mawahabi wanakana kwamba Adam amani iwe juu yake alikuwa mtume. Kwa hiyo na kwa vile wanawaita Waislamu washirikina, wao ni makafiri.

**WALYAUMUL AKHERA:** Aidha, naamini siku ya mwisho kwa vile Allahu taala katupa taarifa juu yake. Siku ya Qiyama inaanza wakati watu wanapofufuka kutoka makaburini mwao. Kuendelea hadi

wanapoenda kwenye mahali pao (ima) peponi au motoni. Sote tutakufa halafu baadae tutafufuliwa. Pepo, moto na mizani na Daraja la Siraat na hashr [mkusanyiko] na nashr [mtawanyiko kutoka kwenye mkusanyiko kuelekea peponi au motoni] na adhabu za kaburini na kuulizwa maswali na malaika wawili Munkar na Nakiir yote hayo ni ya ukweli. Bila shaka yatapitiwa.

**WABILQADARI KHAIRIHI WA SHARRIHI MINALLAHI TAALA:** Nakuamini pia kwamba matukio yote yaliopita na yatakayo kuja mbeleni, mazuri na mabaya ni sawa, yaliyotokea na yatakayotokea kutokana na kudura ya Allahu taala, yaani yanalingana na ujuzi wake na maamuzi yake yaliyokwisha fanywa, na kutokana na kuyaumba kwake na kuyaamulia yatokee katika nyakati maalumu na kuyaandika kwake kwenye Lauhin-Mahfudh. Hakuna hata chembe ya shaka moyoni mwangu.

Ashhadu an lailaaha illallah, wa ashhadu anna Muhammadan abduhu wa rasuluh.

Nguzo za imani zinazoshikiliwa na makundi mengine ishirini na nne ni ya uongo na ni ya uzushi na wataenda motoni. Waislamu wanao wapenda masahaba watukufu ["radiyallahu anhuma" ziwe juu yao] wanajulikana kama Ahl as-Sunna. Masahaba wote watukufu walikuwa wasomi na Waislamu waadilifu. Walikuwa na usuhuba na Bwana mtume (yaani mtume wa Allahu taala swala na salamu ziwe juu yake) na walimsaidia. Hata sahaba aliyepata usuhuba ule (wenye thamani) ulio mdogo zaidi humshinda walii ambae ni wa kiwango cha juu zaidi miongoni mwa mawalii ambao si sahaba. Hali aliyekuwamo sahaba mmoja na tawajjuh za kipenzi cha Allahu taala rehma na amani ziwe juu yake na ukamilifu ulofikiwa chini ya athari za mitazamo yake na pumzi zake zenye baraka havikumwangukia mtu yeyote asiyepata ukuruba na baraka zake. Masahaba wote watukufu walinusuriwa kutokana na matamanio ya nafsi zao punde tu baada ya kupata usuhuba wa mtume wa Allahu taala. Tumeamrishwa kuwapenda wote. Imeandikwa katika kurasa za mwanzo za maelezo juu ya kitabu kijulikanacho kama Shir’at al Islam kwamba unapo zungumza kuhusu masahaba watukufu [Radhi za Allahu taala ziwe juu yao] unapaswa kufanya hivyo kwa uangalifu kadri inavyowezekana. Usimkashifu yeyote kati yao.

Kuhusu makundi sabini na mbili yaliyopotea huku baadhi yao yakienda mbali sana katika upotofu, baadhi yalizingatia uaminifu wao, ilhali mengine yakiangukia upande wa falsafa na wanafalsafa wa

Kigiriki. Hivyo, walifanya mambo yasiyokuwa ya Kiislamu na yanayopingana na Uislamu. Walikumbatia bid'a (yaani imani na matendo yasiyohusiana kwa vyovyote vile na Uislamu na ambayo yamezuliwa kwa jina la imani za Kiislamu na matendo yake). Waliipa kisogo Sunna. Watu waliochukia vigogo wa Kiislamu kama vile Abu Bakr as-Siddiq na Umar bin Khattab (Radhi za Allahu taala ziwe juu yao) ambao ni wa daraja la juu zaidi miongoni mwa maswahaba watukufu kwa mujibu wa ijmaa (makubaliano ya wanazuoni wa Kiislamu), walijitokeza. Kusema kweli, hisia za chuki walizoonyesha baadhi yao kuhusu maswahaba zilimuhusu pia mtume rehma na salamu za Allahu taala ziwe juu yake. Palijitokeza watu waliokana ukweli kwamba bwana wetu, mtume, alikuwa amechukuliwa mbinguni kimwili na kiroho katika usiku unaojulikana kama Miraj [ambao umeelezewa kwa tafsili (upana) katika sura ya sitini ya sehemu ya tatu ya Endless Bliss].

Inasikitisha kuwaona baadhi ya Wanazuoni wa Kiislamu wa kisasa wakihudumu kama wazungumzaji wa kundi linalojulikana kama Ismaa'iliyya, kundi ambalo ni hatari zaidi kati ya makundi sabini na mbili (ya uzushi). Wanakazana kuyapotosha na kuyapa sumu marika ya vijana kwa kuandika na kueneza uwongo kama kusema kwamba wahenga wa bwana wetu mtume wa kiume na wa kike waliobarikiwa hawakuwa waumini na kwamba bwana wetu mtume rehma na salamu za Allahu taala ziwe juu yake alikuwa akitoa wanyama kama sadaka kwa masanamu kabla hajateuliwa kama mtume na wananukuu baadhi ya vitabu vya Kishi'a kuthibitishia upotovu wao. Inaonekana wazi kwamba lengo la watu waoga kama hawa ni kujaribu kuionea dini ya kiislamu, kuwapokonya vijana imani na kuwaingiza kwenye ukafiri. Aya moja ya Quran tukufu inasema kwamba yeyote anayetafsiri Qurani kulingana na fikra zake atakuwa kafiri.

Wanazuoni wa Kiislamu walikuwa na adabu (walipambwa na tabia njema kama ilivyopendekezwa na Uislamu). Walikuwa wakiongea na kuandika kwa uangalifu (diligence). Huwa makini sana ili wasije wakasema maneno ya uongo. Kuongea pasina kuchuja, kwa mfano kujaribu kuwasilisha maoni ya mtu binafsi ambayo ni ya uongo na upotovu kwa jina la Uislamu badala ya kutoa taarifa sahihi kutoka kwenye misingi ya sheria, yaani misingi mikuu minne ya elimu ya Kiislamu, si jambo linalofaa kufanywa na Muislam wa kawaida, ukiachilia mbali mwanazuoni wa Kiislamu. Tunapaswa kuchukulia maneno na maandishi haribifu na yenye uchafu ya watu wajinga kama hao ambao hawajatambua umuhimu wa mtume wetu rehma na

salamu ziwe juu yake, kama sumu (inayoweza kumuua mtu papo hapo).

Mshororo wa persion katika Kiingereza:

I shudder like a willow leaf if they should assault my iman (Natetemeka kama jani la mti ulioota karibu na maji wanaposhambulia imani yangu).

Allahu taala aongeze katika nyoyo zetu upendo wa wapendwa wake. Atunusuru kutokana na kuanguka katika fitna ya kuwapenda maadui zake. Dalili ya uwepo wa imani katika moyo ni kuwapenda wale awapendao Allahu taala na kuwachukia maadui zake. Katika utekelezaji wa amali yoyote ya ibada kwa upande wa kisuni kuna madhehebu manne. Nayo ni madhehebu ya Imam mkuu Abu Hanifa, Imam Shaafi'i, Imam Malik, na Imam Ahmad bin Hanbal rehma za Allahu taala ziwe juu yao.

Inafaa kushikamana na moja wapo ya madhehebu haya manne ili uwe sunni. Hapa ijulikane ya kwamba sunni sio maana ya dhehebu moja tu la kishafi kama ilivyozoeleka katika sehemu kama vile Tanganyika, Zanzibar na Kenya bali ni mchanganyiko wa madhehebu manne. Madhehebu ya maimamu hawa wanne yote ni ya ukweli na sahihi. Yote ni miongoni mwa madhebu ya Ahl as-Sunna.

Waislamu wanaomfuata Abu Hanifa madhehebu yao wanajulikana kama wahanafi. Tunasema "Madhehebu ya Imam mkuu ni swawab na sahihi. Kuna uwezekano pia kwamba yanaweza kutokuwa sahihi. Madhehebu mengine matatu si sahihi. Kuna uwezekano pia kwamba yanaweza kuwa sahihi".

Ili imani ya mtu kudumu, inategemea masharti sita:

1- Tunapaswa kuamini yaliyo ya ghaib. Tunaamini mambo ya ghaib (yasiyojulikana ama yasiyoonekana), ambayo si dhahiri. Kwani hatujawahi kumuona Allahu taala kwa macho yetu. Hata hivyo, tumeamini kama kwamba tumemuona. Hatujawahi kutilia shaka jambo hilo.

2- Hakuna kiumbe hata kimoja ardhini na mbinguni miongoni mwa wanaadamu, majini, malaika na mitume (amani iwe juu yao) ambaye ana elimu ya ghaib. Allahu taala peke yake ndiye aliye na ujuzi wa yale yaliyojificha na hutoa elimu aitakayo ya ghaib kwa viumbe wateule. [Ghaib humaanisha kile (kitu) ambacho hakiwezi kutambulikana kwa kutumia ala za hisi ama kueleweka kwa kupiga mahesabu au kufanya majaribio].

3- Kujua mambo ya haramu kama ni haramu na kuamini hivyo.

4- Kujua mambo yaliyo halali kama ni halali na kuamini hivyo.

5- Kutokuwa na hisia kwamba umesalimika kutokana na adhabu za Allahu taala na kumcha Allahu taala daima.

6- Kutokata tamaa kutokana na rehma za Allahu taala pasina kujali kiasi cha madhambi uliyotenda.

Iwapo mtu atashindwa kutimiza masharti haya sita, hata kama ametimiza matano au ikiwa atatimiza sharti moja tu na asitimize matano yaliyobaki, imani na Uislamu wa mtu huyo hautakuwa sahihi.

Kuna mambo arubaini [40] yanayoweza kumpelekea mtu aliye na imani kuipoteza baadae.

1- Kufanya mambo ya bid’a (uzushi), yaani kuwa na dosari katika imani ya mtu. [Ukiukaji mdogo wa nguzo za imani zilizofundishwa na wanazuoni humfanya mtu mwanabid’a au kafiri]. Ikiwa mtu atakana kitu ambacho ni lazima kukiamini, mtu huyo hua amekufuru hapo hapo. Ni bid‘a au upotofu (dhalala) kukana kitu ambacho ni lazima kukiamini. Bid’a au dhalala humpelekea mtu kufa imani au kudhoofika.

2- Imani dhaifu, yaani imani isiyoambatanishwa na amali (vitendo vya ibada).

3- Kuvifanya viungo sita vya mwanaadamu viepukane na njia iliyo sahihi.

4- Kuendelea kufanya madhambi makubwa. [Kwa hiyo, Muislamu hapaswi kunywa pombe, na wanawake na wasichana Waislamu hawapaswi kuonyesha vichwa vyao, nywele zao na vifundo vya mikono yao kwa wanaume wasio maharam wao.]

5- Kutokuwa na shukrani kwa neema ya Uislamu.

6- Kutohofia uwezekano wa kuenda akhera bila imani.

7- Kueneza ukatili.

8- Kutosikiliza adhana inayofanyika kwa mujibu wa sunna. [Mtu anayepuuza adhana huwa fasiki]. (Adhana na jinsi inavyoadhiniwa kulingana na sunna, yaani Uislamu, imeelezewa kwa tafsiri katika sura ya kumi na moja ya juzuu ya nne fascicle ya Endless Bliss).

9- Kutowatii wazazi. Kukataa kijeuri amri zao zinazowiana na Uislamu na ambazo ni mubah.

10- Kuapa mara kwa mara hata kama viapo vyenyewe ni vya ukweli.

11- Kupuuza tumaanina (kutulia) katika nguzo za sala (yaani katika rukuu, i'itidaal, baina ya sijda mbili, na juluus (kukaa baina ya sijda mbili). Taa'dil il arkaan maana yake ni kuwa katika hali ya utulivu (tuma'nina) kwa kipindi kinacho mtoshelezea kusema "Subhanallah".

12- Kufikiria kwamba sala si muhimu. Kutojali kujifunza na kuwafundisha sala watu wa familia na watoto, na kuwazuia watu wengine kuswali.

13- Kunywa pombe au kinywaji kingine kinacholewesha kikitumika katika kiasi kikubwa. Sheria hiyo hiyo inatumika hata kama pombe ni kidogo.

14- Kuwatia waumini mashakani.

15- Kujifanya walii au msomi katika mambo ya Uislamu. Kujifanya mshikadini, muhubiri, bila kupata mafundisho ya Uislam. [Vitabu vya uongo vilivyoandikwa na waongo kama hao havistahili kusomwa. Hutuba na mahubiri yao hayafai kuhudhuriwa].

16- Kuyasahau madhambi yake mtu, kuyachukulia kama jambo dogo.

17- Kiburi (yaani kuwa na kiburi kingi).

18- Kujikweza au kujiona (kujifaharisha), yaani kujifakharisha kwa usomi na uchamungu.

19- Kuwa mnafiki, yaani unafiki, kuwa na nyuso mbili.

20- Husda (kumhasidi ndugu yako Mwislamu).

21- Kutotii amri za serikali au bwana wako ikiwa amri zao hazipingani na Uislamu. [Haifai kutii amri zinazopingana na Uislamu].

22- Kusema kwamba fulani na fulani ni mtu mwema kabla hujampa mtihani.

23- Kuwa muongo.

24- Kuwakwepa wasomi. [Kutosoma vitabu vilivyoandikwa na wanazuoni wa kiislamu wa ahlu haqih].

25- Kufuga masharubu na kuyarefusha kupindukia kiasi kilichopendekezwa na sunna.

26- Wanaume hairuhusiwi kuvaa hariri.

27- Kuwa mwenye tabia ya kusema uongo.

28- Kuwasababishia majirani zako matatizo hata kama si waumini.

29- Kudhihirisha hasira nyingi juu ya mambo ya dunia.

30- Kupokea na kutoa riba.

31- Kuvaa mavazi yalio marefu sana kwa mashauo.

32- Kufanya mambo ya uchawi.

33- Kutomtembelea jamaa ambaye ni Muislamu (mwema) mchamungu.

34- Kutompenda mtu ambaye hupendwa na Allahu taala na kumpenda mtu ambae unajua kwamba anauchafulia jina Uislamu.

35- Kumkasirikia ndugu yako Muislamu kwa zaidi ya siku tatu.

36- Kuwa na tabia ya kuzini.

37- Kufanya liwati pasi na kutubia juu ya dhambi hilo baadaye. Liwati ni kuingiza dhakari kwenye sehemu ya kukidhia haja kubwa ya mtu mwingine.

38- Kuadhini katika nyakati zisizopendekezwa kwenye vitabu vya fiqhi / au kwa njia isiyoamrishwa na Sunna, au kutoipa adhana heshima inayostahiki wakati unapoisikia na inapowasilishwa kwa namna inayokubalika na Sunna.

39- Kutomkanya mtu umwonapo akitenda munkari [yaani kutomzuia mtu huyo asifanye hivyo] kwa kutumia lugha ya mvuto hali ya kuwa una uwezo wa kufanya hivyo.

40- Kuruhusu kutendeka kwa mambo yaliyokatazwa na Uislamu na aqiida ambayo mitume walikuja nayo. Kwa mfano wanawake ambao una haki ya kuwapa nasaha kama vile mke wako na binti yako, kuwaachia kutoka nje na hali hawajifuniki vichwa vyao, mikono yao na miguu yao, au kujipamba au kujitia marashi na manukato.

Imani humaanisha kutangaza kwa ulimi na kuthibitisha ukweli ambao mitume waliwasilisha kutoka kwa Allahu taala. Na Uislamu humaanisha kumwamini Muhammad rehma na salamu za Allahu taala ziwe juu yake na kutekeleza (amali) mafundisho yake.

Aidha, dini au millat ni itikadi yaani ni nguzo za kiimani ambazo mitume walileta kutoka kwa Allahu taala.

Uislamu ama sheria za Uislamu humaanisha amali, yaani nguzo za kimatendo alizozileta mtume wetu Muhammad kutoka kwa Allahu taala.

Aidha, iman-i-ijmaali (imani kwa muhtasari), humaanisha imani kwa ujumla wake, nayo humtoshelezea mtu (haja ya kuwa muumini, Muislamu). Si lazima kwenda katika tafsiri au ufafanuzi au kuijua imani kwa upana. Imani ya muqallid, yaani mtu anayeamini na hali haelewi,

itasihi (Hata hivyo, maelezo kamili huhitajika katika baadhi ya marahma).

Kuna viwango vitatu vya imani. Iman-i-taqliidii, Iman istidlaalii na Iman-i-haqiiqii.

**Iman-i-taqliidii** (imani ya kuigiza). Mtu mwenye kiwango hiki cha imani hajui faradh, wajib, sunna wala mustahab. Wanawaigiza tu wazazi wao katika imani na vitendo vyao vya ibada. Imani ya watu kama hao inaweza kusababisha matatizo.

**Iman-istidilaalii** (imani dokezi). Watu wenye kiwango hiki cha imani wanajua faradh, wajib, mustahab na haram, na hutii sheria za Kiislamu. Wana ujuzi na uwezo mkubwa wa kuwasilisha mihimili ya imani. Wamejifunza mihimili hiyo kutoka kwa walimu wa kidini na kwenye vitabu. Imani ya watu kama hawa ni thabiti.

**Iman-i-haqiiqii** (imani ya kweli ama halisi). Kama viumbe wote wangeungana na kukubaliana kumkana Mola wao (Allahu taala), mtu aliyoko katika kiwango hiki cha imani asingemkana Allahu taala. Watu wa namna hii hawana hata chembe ya shaka katika nyoyo zao. Imani yao hufanana na ile ya manabii (mitume). Kiwango hiki cha imani ni cha juu zaidi kuliko vile vingine viwili.

Aidha, sheria za kiislamu zinahusiana na amali (matendo ya ibada) na sio imani. Imani, peke yake, haimtoshelezi mtu kuingia peponi. Na vile vile, haiwezekani kuingia peponi kwa kutegemea amali (yaani kwa kutekeleza matendo ya ibada). Imani bila amali inakubalika. Kwa upande mwingine amali bila imani haina faida yoyote. Matendo ya ibada yanayofanywa, matendo ya uchamungu yanayotendwa na zaka inayotolewa na watu wasiokuwa na imani, vitu hivyo vyote havitowafaa lolote akhera. Imani haiwezi kutolewa kama zawadi kwa mtu mwingine, ijapokuwa thawabu zinazochumwa kutokana na amali zinaweza kuzawadiwa. Mtu hawezi kutoa wala kuandika agizo kuhusu imani kwenye wasia wake wa mwisho. Ingawa mtu anaweza kuwaagiza warithi wake kutenda amali kwa niaba ya mtu mwingine (baada ya mtu huyo kuaga dunia). Mtu anayepuuza kutenda amali hatakuwa kafiri. Lakini yule anaetupilia mbali imani au kuichukulia amali kama jambo lisilokuwa na maana atakuwa kafiri. Mtu mwenye udhuru au yule asiekuwa na uwezo wa kutenda amali atasamehewa. Lakini hakuna namna ambayo mtu atasemehewa katika suala la imani.

Kuna aina moja tu ya imani ambayo mitume wote waliwasilisha kwa wafuasi wao. Pamoja na hayo wanatofautiana katika sheria, utekelezaji na matendo ya kidini.

Halikadhalika kuna aina mbili za imani. Moja ya aina hizo ni iman-i-khalqii na nyingine ni iman-i-kasbii.

**Iman-i-khalqii** ni ile ya kiuzawa yaani kukubali kwa mja ahadi ya kukiri kuwa Allahu taala ndiye Mola wake.

**Iman-i-kasbii** ni imani anayoipata mtu baada ya kubaleghe. Imani ya waumini wote ni sawa. Ingawa wanatofautiana katika amali.

Imani ni faradh-i-daaim (ni faradhi ya kudumu), huku amali ikiwa faradh (faradhi) muda wake ukiwadia. Imani ni jambo la faradhi kwa kafiri na Muislamu ni sawa. Amali ni faradhi kwa Muislamu pekee.

**Na vile vile kuna vigawanyo nane vya imani;**

**Iman-i-matbuu'** ni imani ya malaika.

**Iman-i-ma'suum** ni imani ya mitume.

**Iman-i-maqbul** ni imani ya waumini.

**Iman-i-mauquuf** ni imani batilifu ya watu wa bid'a.

**Iman-i-marduud** ni imani ya uongo ambayo wanafiki hujigamba kuwa nayo.

**Iman-i-taqliidii** ni imani ambayo watu waliipata kutoka kwa wazazi wao na ambayo hawakufundishwa na walimu wa kidini. Imani ya watu hao inaweza kumsababishia mtu matatizo.

**Iman-isdilaalii** ni imani ya mtu anayemjua Mola Mtukufu kwa kurejelea ushahidi unaothibitisha uwepo wake. Imani ya mtu huyo ni imara.

**Iman-i-haqiiqii**. Mtu mwenye aina hii ya imani hawezi kumkana Mola wake (Allahu taala) hata kama viumbe wengine wangekubaliana kumkana Mola wao na hakutakuwa na chembe ya shaka ama kusitasita katika moyo wa mtu huyo. Kama tulivyotaja hapo awali katika matini hii, aina hii ya imani ndiyo bora kuliko nyingine zote.

**Umuhimu wa imani umejikita katika mambo matatu:**

**Kwanza**, huiokoa shingo ya mtu kutokana na upanga.

**Pili**, huiokoa mali ya mtu kutokana na kodi zijulikanazo kama jizya na kharaj (malipo wanayo lipia makafiri wakiwa katika ulinzi na usimamizi wa kiislam).

**Tatu**, huokoa mwili wa mtu kutokana na moto wa milele wa jahannam.

"Amantu billaahi...", hujulikana pia kama Sifaat-i-imaan au mu'minuuna bih dhaat-i-iimaan au asl-i-iimaan, kutokana na heshima yake na taadhima. (Ni tamko la nguzo za imani ambalo ni kama

ifuatavyo: “… wa malaaikatihi, wa kutubihi, wa rusulihi, walyawmil-aakhiri, wa bil- Qadari khayrihi wa sharrihi min Allaahi taala, wal-ba’athu ba’adal-mawt haqqun, ash-hadu anlaa ilaaha ill-Allah wa ash-hadu anna Muhammadan ‘abduhu wa rasuuluhu”).

Aidha, kuna madaraja mawili ya imani, yaani nyakati ambazo kwanza inamwajibikia mtu kuwa na imani:

Pili umri wa kutoa maamuzi na umri wa kubaleghe.

Pia, kuna sababu mbili za kuamini: kuumbwa kwa viumbe wote pili na kuteremshwa kwa Quran tukufu. Halkadhalika, kuna aina mbili za ushahidi: Daliil-i-aqlii (ushahidi wa kiakili) na daliil-i-naqlii (ushahidi unaotokana na maandiko).

Imani pia ina rukn mbili (mihimili), asl (asili): Ikraar bil-lisaan (kukiri kwa ulimi) na tasdiiqun bil jinaan (kuthibitisha kwa moyo). Na kuna masharti mawili yaliyowekewa rukn hizo:

Sharti iliyofunganishwa moyo ni kwamba usiwe na shaka yoyote wala wasiwasi na sharti inayohusu ulimi ni kutambua yale ambayo mtu huyatamka.

Aidha, tunaweza kujiuliza je, imani ni kiumbe? Jibu ni kwamba imani si kiumbe kwa vile ni hidayat (uongofu) kutoka kwa Allahu taala. Kwa upande mwingine, ni kiumbe kutokana na mtazamo kwamba ni uthibitisho na azimio la mja kimaumbile.

**Yaqiin** humaanisha kuijua dhati ya Allahu taala na ukamilifu wake.

**Khawf** humaanisha kumcha Allahu taala.

**Rajaa** humaanisha kutokata tamaa na rehma ya Allahu taala.

**Mahabbatullah** humaanisha kumpenda Allahu taala na mtume wake rehma na salamu za Allahu taala zimshukie juu yake na kuipenda dini ya Uislamu na waumini.

**Hayaa** humaanisha kuona haya mbele ya Allahu taala na mtume wake rehma na salamu zimshukie juu yake.

**Tawakkul** humaanisha kutegemea mambo yote kwa Allahu taala. Kuweka imani yako kwa Allahu taala wakati unapoanza kufanya jambo lolote.

Ni nini maana ya Uislamu, imani na ihsani?

Imani maana yake ni kuamini ukweli ulioelezewa na mtume Muhammad "swallallahu alaihi wa sallam" juu yake.

**Uislamu** ni kutekeleza maamrisho ya Allahu taala na kuepukana na makatazo yake.

**Ihsani** ni kutenda matendo ya ibada kama kwamba Allahu taala unamwona. Na kama wewe humuoni basi yeye anakuona.

**Maana ya imani** kila siku ni uthibitisho. Katika Uislamu (kitaaluma) neno hilo humaanisha kuamini nguzo sita za Imani.

**Ma'rifat** ni kutambua kuwa Allahu taala ana sifa za ukamilifu na kwamba yupo mbali na sifa za upungufu.

**Tawhiid** maana yake ni kuamini kuwa Allahu taala ni mmoja na hana mshirika.

**Uislamu** (sheria za Kiislamu) ni maamrisho na makatazo ya Allahu taala.

Dini na millat ni azimio linalohusiana na nguzo za imani analolifanya mtu muda wa uhai wake.

**Imani vile vile inalindwa katika ngome tano:**

1- Yaqiin

2- Ikhlaas

3- Kutenda matendo ya faradh na kuepukana na haramu.

4- Kushikamana na Sunna.

5- Kuimarisha adabu na kuwa mwangalifu nayo.

Yeyote anayekuwa imara katika ngome hizi atakuwa imara pia katika imani. Kupuuza ngome yoyote kutampelekea adui kupata ushindi. Mwanaadamu ana maadui wanne: rafiki mbaya kuliani, matamanio ya nafsi yake kushotoni, upendeleo wa dunia mbele yake na shetani nyuma yake. Maadui hawa hupania kuichukuwa imani. Marafiki wabaya si wale wanaomdhulumu mtu mali yake, pesa zake na mambo mengine ya dunia. Marafiki wabaya na walio hatari zaidi ni wale wanaokazana kuondoa dini ya mtu, imani, adabu, haya na uungwana na kwa kufanya hivyo, wamevamia furaha ya mtu duniani na kujivunia kwa milele huko akhera. Tunamuomba Allahu taala ailinde imani yetu kutokana na uovu wa maadui kama hao na upotofu unaopangwa na maadui wa Uislamu.

Maana ya Kalima-i-tawhid, yaani tamko "Lailaaha illa-Allah", ni "Hakuna anayestahiki kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allahu taala. Hana mshirika wala anayelingana naye. Hafungamani na wakati wala mahali maalum".

**"Muhamadun Rasulullah"** maana yake ni bwana wetu.

Muhammad Al-Mustafa sala na salamu zimshukie juu yake, ni mja na mtume wa Allahu taala wa haki. Alhamduli-l-Allahi sisi ni umma wake.

**Tamko la Tawhidi lina majina nane;**

1- Kalimat us-shahada.

2- Kalimat ut-tawhiid.

3- Kalimat ul-ikhlaas.

4- Kalimat ut-taqwaa.

5- Kalimat ut-twayyiba.

6- Da'wat ul-haqq.

7- Urwat ul-wuthqaa.

8- Thamarat ul-janna.

Masharti ya Suratul Ikhlas ni; Nia. Kujua maana yake na kuisoma au kuikariri kwa heshima.

Mtu anayefanya dhikri anahitaji mambo manne: Tasdiiq, ta'adhwiim, halaawat na hurmat.

Mtu anayeacha tasdiq anakuwa mnafiki, anaeacha ta'adhwiim hua mwanabid'a, anayeacha halaawat hua mnafiki na anaeacha hurmat hua fasik.

**Kuna aina tatu za dhikr:**

1- Dhikrul-awaam.

2- Dhikrul-khawaas.

3- Dhikrul-akhas.

Dhikrul-awaam ni ile ya wasiosoma. Dhikrul-khawaas ni ya wanazuoni wa Kiislamu na dhikrul-akhas ni ya mitume.

**Viungo vya binadamu vinavyohusika katika dhikr ni vitatu;**

1- Ulimi hufanya dhikr kwa kutoa tamko la shahada.

2- Kumpwekesha Allahu taala, kumhimidi na kusoma Quran tukufu.

3- Dhikr inayofanywa na moyo.

**Moyo hufanya dhikri ya aina tatu;**

1- Kuzingatia juu ya ushahidi na ishara zinazomwongoza mtu katika utambuzi wa sifa za Allahu taala.

2- Kuzingatia kuhusiana na ushahidi juu ya sheria za Allahu taala.

3- Kuzingatia kuhusiana na miujiza ya Allahu taala.

Wanazuoni wa tafsiiri wanaielezea aya ya mia moja na hamsini (150) ya Suratul-Baqarah kama ifuatavyo. Quran tukufu hutangaza kwamba "Enyi waja wangu! Mkinidhukuru kwa kunitii (kwa kutenda

matendo ya kumtii Allahu taala), na mimi nitakudhukuruni kwa neema zangu (janna). Mkinidhukuru katika hali ya upweke, basi nitakudhukuruni katika mkusanyiko mkubwa (yaani mahali pa mahshari). Mkinidhukuruni nyakati za ukiwa/ufukara, nitakudukuruni kwa msaada wangu. Mkinidhukuru kwa kuitikia wito wangu, (yaani kwa kutekeleza maamrisho yangu), basi nitakudhukuruni kwa kuwapeni hidaya (uongofu). Mkinidhukuru kwa ukweli na ikhlasi, basi nitakudhukuruni kwa nia ya nusura na uokovu. Mkinidhukuru kwa Al-Fatiha tukufu na kwa rububiyya ilioko kwenye Al-Fatiha tukufu, basi nitakudhukuruni kwa rehma zangu". Hivyo, wanazuoni wametaja mamia ya faida za kufanya dhikri. Tutataja tu baadhi yake.

Muislamu anapofanya dhikri, Allahu taala humfurahikia. Malaika watamfurahikia. Shetani atahuzunika. (Moyo wa mtu huyu utalainika). Watafanya ibada kwa kupenda na hamasa. Dhikri itaondoa huzuni katika nyoyo zao, itaweka uchangamfu katika nyoyo zao, na itang'arisha nyuso zao kwa nuru. Mtu huyo atakuwa shujaa na atajinyakulia upendo wa Allahu taala. Mlango wa maarifa utafunguliwa kwa ajili yake ili wapokee faydh kutoka kwa mawalii. Watapambwa na sifa sitini za tabia njema.

**Ash-hadu anna Muhammadan abduhu wa Rasuuluhu"**. Maana ya tamko hili ni: mtume wetu Muhammad al-Mustafa "swallallahu alaihi wa sallam" juu yake, ni mja wake na mtume wake alikula, akanywa na alioa wanawake. Alikuwa na watoto wa kiume na wa kike. Wote walikuwa watoto wake Bi. Khadija radhi za Allah zimshukie juu yake, isipokuwa Ibrahim ambaye mamake ni **Maariyat**. Alifariki akiwa mdogo. Watoto wake wote walifariki kabla yake isipokuwa Fatuma radhi za Allahu taala zimshukie ambae alimuozesha Ali "karramallahu wajhah". Hasan na Husein ni watoto wa Hadhrat Ali na Hadhrat Fatuma radhi za Allahu taala ziwashukie. Fatuma alikuwa na hadhi ya juu miongoni mwa watoto wake wote. Alikuwa akipendwa sana na mtume "swallallahu alaihi wa sallam" juu yake. Mtume "swallallahu alaihi wa sallam" alikuwa na wake kumi na mmoja ambao ni: Khadija, Sauda, Aisha, Hafsa, Ummu Salama, Ummu Habiba, Zainab bint Jahsh, Zainab bint Khuzaima, Maimuuna, Juwairiyya na Safiyya radhi za Allahu taala ziwashukie.

Dalili za kisheria zimeundwa na Kitabu (Quran), Sunna, Ijmaa na Qiyas. Kutokana na vyanzo hivyo vinne wanazuoni wa Kiislamu walipanua elimu yao ya kidini. Neno la Allahu taala linajulikana kama 'Kitab (kitabu)'. Sunna ni kauli za mtume (matamko ya mtume wa Allahu taala), af'al-ur Rasuul (matendo na tabia za mtume wa Allahu

taala) na taqriir-u-Rasuul (idhini ya mtume). Ijmaa ni makubaliano yaliyofikiwa na mujtahidin ambao waliishi katika karne moja, kwa mfano masahaba watukufu radhi za Allahu taala ziwe juu yao, au ma imamu wa madhehebu manne. Qiyas ni malinganisho yaliyofanywa na mujtahidin kati ya mambo mawili yanayotofautiana.

Maana za kilaksia zilizoelezewa na madhehebu mbalimbali ni za namna mbili tofauti: ya kwanza ni mkondo wetu wa kiitikadi na nyingine ni ule wa kimatendo.

Imamu wetu, yaani kiongozi, katika itikadi ni Abu Mansur Maturidi "rahmatullahi alaih". Mkondo wake unajulikana kama Ahl as-Sunna. Kiongozi wetu katika mkondo wa matendo ni Imam Abu Hanifa "rahmatullahi alaih". Mkondo wake unajulikana kama madhehebu ya Hanafii.

Abu Mansur Maturidi, jina lake ni Muhammad, jina la babake ni Muhammad na jina la babu yake ni Muhammad.
Mwalimu wake ni Abu Nasr al-iyaad "rahmatullahi alaih".

Jina la mwalimu wa Abu Nasr al-iyad ni Abu Bakr-aljurjaani ambaye alisomeshwa na Abu Sulaiman aljurjaani, aliyesomeshwa na Abu Yusuf na Imam Muhammad Shaybani. Na mwalimu wa hawa magwiji wawili ni Imam Abu Hanifa "rahmatullahi alaih". Kwa hiyo, Imam mkuu ndie kiongozi mkuu wa madhehebu yetu kiitikadiame na kimatendo.

Waislamu wote wana maimamu watatu (viongozi), kuwajua ni jambo la lazima. Imamu wetu anayetuhimiza kutekeleza maamrisho na kuepukana na makatazo ni Quran tukufu. Imamu wetu anayetuambia mambo hayo, yaani Uislamu ni Bwana mtume "swallallahu alaihi wa sallam". Imamu wetu anayesimamia utekelezaji wa mafundisho hayo kwa niaba ya mtume, yaani anayehakikisha kuwa yanafuatwa, ni kiongozi wa taifa la Kiislamu.

Mwalimu wa Imamu mkuu anaitwa Hammad ambae alisomeshwa na Ibrahim an-Nahaaii aliefundishwa na ‘Alqama bin Qays ambae mjomba wake Imam An-nahaaii. Mwalimu wa ‘Alqama ni ‘Abdullahi bin Masoud "rahmatullahi alaih" aliyepata elimu yake kutoka kwa mtume wa Allahu taala rehma na salamu za Allahu taala zimshukie.

Ama mtume wa Allahu taala rehma na salamu zimshukie, alipokea elimu yake kutoka kwa Jibriil rehma na salam ziwe juu yake ambae aliamrishwa na Allahu taala.

Allahu taala amemjaalia mwanaadamu majohari manne: Akili (moyo, busara, hoja), imani, haya na utendaji wa matendo mema.

Sala na matendo mema hukubalika iwapo masharti matano yatatimizwa. Masharti hayo ni imani, ‘ilm, niyya, ikhlas na kuwapa watu haki zao. Kwanza kabisa, lazima mtu ajue masharti ya kusihi katika kutekeleza matendo ya ibada yanayopaswa kufanywa. [Usahihi wa tendo fulani hutofautiana na ukubalifu wake. Matendo ya ibada yenyewe yana masharti yake na furudhu zake zinazopaswa kutimizwa ili yachukuliwe kuwa sahihi. Sharti hata moja likikosekana, tendo la ibada linalofanywa halitosihi. Itakuwa sawa na kutotendwa kwa tendo hilo la ibada na mtu hatanusurika na adhabu na mateso (kwa vile huhesabiwa kaliacha). Hakuna adhabu itakayomkumba mtu kutokana na tendo la ibada ambalo ni sahihi hata kama si kubalifu. Pamoja na hayo, mwislamu hatopata thawabu (ujira maalum) kwa ajili ya ibada yake isiyotakabaliwa. Ili itakabaliwe lazima kwanza isihi, yaani masharti matano yaliotajwa hapo awali yawe yametimizwa. Haki zilizoelezewa, ni miongoni mwa masharti haya. Imamu Rabbani mungu amrehemu alitaja katika barua ya ishirini na saba, mjeledi wa pili wa maandishi yake yanayojulikana kama Maktubat. “Endapo mtu atatenda tendo lifananalo na la mtume halafu akazuia haki ya mtu (hata kama ni chembe ndogo sana), hataingia peponi mpaka ailipe”. [Sala zake hazito kubaliwa].

Ibn Hajar al-Haytami al-Makki "rahmatullahi alaih", akielezea tendo la maasia la mia moja themanini na nane, katika kitabu chake Zawajir, alisema kwamba: “Aya ya mia moja themanini na nane ya suratul-Baqarah inasema: wala msichukuliane mali zenu kwa batili…”. Maana ya tamko ‘kwa batili’, ni udanganyifu unaofanyika kupitia riba, kamari, wizi, ulaghai, uhaini, kutoa ushahidi wa uongo, na uhalisia kuna hadithi tukufu isemayo “Muislamu asiyekula halali ya watu, akatenda matendo ya faradh, akaepukana na haramu na kuwadhuru watu, ataingia peponi” na “Mwili unaolishwa haramu utachomwa moto” na ikiwa watu hawatasalimika kutokana na kuonewa na kuudhika, mtu huyo hatapata manufaa yoyote katika imani yake au rehma au zaka” na “Ikiwa kanzu iliyovaliwa na mtu ilipatikana kwa njia ya haramu, basi sala anayosali haitotakabaliwa”. [Jilbaab ni vazi refu livaliwalo na wanawake. Jilbaab pia ni kanzu inayovaliwa na wanaume]. Hadithi ambayo ameinukuu kuelezea dhambi la mia mbili inasema “Mtu anayeuza bidhaa iliyochafuliwa si miongoni mwa umma wetu. Marejeo yake ni motoni”. Imetajwa katika hadithi inayozungumzia dhambi la mia mbili kumi na saba kwamba: “Motoni ni marejeo kwa mtu amdhuruye (anaemfanyia ubaya) jirani yake kwa ulimi wake hata kama anasali na kufunga na kutoa zaka sana”. Hata kama majirani wa mtu

sio waumini, haifai kuwadhuru (kuwatendea ubaya). Bali kinachofaa ni kuwatendea wema na kuwaonea huruma. Imetajwa katika hadithi tukufu katika kuelezea tendo la dhambi la mia tatu na thelathini kwamba: “Mtu anayemuua kafiri kwa dhuluma wakati wa amani, hatoingia peponi”. Hadithi nyingine inasema: “Waislamu wawili wakipigana kwa ajili ya matamanio ya kidunia, basi aliyeua na aliyeuliwa wataingia motoni”. Imetajwa katika hadithi inayozungumzia dhambi la mia tatu kumi na saba kwamba: “Mtu anayechochea uadui kati ya watu ataadhibiwa hadi siku ya kiama”. Hivyo hivyo, ataadhibiwa endapo atachochea uadui (uhasama) kati ya makafiri. Katika hadithi inayozungumzia dhambi la mia tatu hamsini: “Watu aina tatu, dua zao bila shaka zinakubaliwa. Mwenye kudhulumiwa, msafiri na wazazi”. Na katika hadithi nyingine “Mtu aliedhulumiwa, dua yake haitokataliwa hata kama ni kafiri”. Katika hadithi inayoelezea dhambi la uhaini dhidi ya serikali, imetajwa kuwa adhabu yake haitocheleweshwa”. Mwisho wa tafsiri kutoka kwa kitabu cha Zawaajir.

Ewe Muislamu! Ikiwa unapenda kupata rehma za Allahu taala na matendo yako kutakabaliwa, hifadhi hadithi zilizonukuliwa hapo juu moyoni mwako. Usihujumu mali, maishani mwako na usivunje heshima ya mtu yeyote, Muislamu na asiyekuwa Muislamu. Usimdharau mtu yeyote. Wape watu haki zao. Ni mojawapo ya haki za kibinaadamu mwanamume kumlipa mahari mwanamke ambae amemuacha. Asipolipa mahari hiyo, atastahili adhabu kote kote duniani na akhera. Haki ya kibinaadamu iliyomuhimu zaidi na ambayo adhabu yake ni kali sana ikivunjwa, ni kuwacha kuwafundisha jamaa wa karibu Uislamu, hasa wakiwa chini ya usimamizi wa mtu na ulinzi wake. Mtu akizuia jamaa zake na watu wengine kujifunza Uislamu na kufanya ibada, kwa kuwaadhibu na kuwadanganya, atachukuliwa kuwa kama kafiri au adui wa Uislamu. Mfano wa muelekeo huo usio wa kidini ni kujaribu kuyachafua mafundisho ya Uislamu, mkakati unaofuatwa na wanabid’a wanao fanya uzushi katika dini na watu wasiofuata madhehebu maalum kwa kutoa matamko yanayolenga kuukashifu Uislamu na kuandika makala ya uchochezi. Usiipige vita serikali wala sheria zake. Lipa kodi. Ni hatia kuiasi serikali, hata kama ina udhia au matatizo kama alivyosema Muhammad Mustafa Hadimi "rahmatullahi alaih", aliyefariki mwaka wa 1176 [1762 A.D.] huko Haadim, Konya, Uturuki, katika kitabu kijulikanacho kama Beriqa. Hata kama uko katika Dar ul-harb, yaani moja wapo ya nchi za makafiri, usivunje sheria wala haki zao. Usizushe fitna. Usifanye urafiki na watu wanaouhujumu Uislamu, na wanabid’a wazushi katika dini au

wasiofuata moja wapo ya madhehebu yoyote yale katika madhehebu ya haki. Usisome vitabu vyao wala magazeti yao. Usiruhusu vipindi vya redio zao na televisheni kuingia nyumbani kwako. Amrisha mema (yaani mafundisho ya Uislamu), kwa wale wanaotaka kukusikiliza. Kwa maneno mengine, wape nasaha, kwa uso wenye tabasamu na maneno matamu na laini. Kwa kutumia tabia yako nzuri, onyesha utukufu na heshima ya dini ya Kiislamu kwa watu wote wanaokuzunguka.

Ibn Abidin "rahmatullahi alaih", anaeleza katika mjeleda juzuu ya kwanza kama ifuatavyo:

“Saw’atayn, yaani sehemu ya siri ya mbele nayo, ni aura ghaliidh (uchi mzito) kwa mujibu wa madhehebu yote. Ni faradhi kusitiri sehemu hizi kwa mujibu wa madhehebu hayo yote. Mtu asiyetilia maanani suala la kusitiri sehemu hizo, atakuwa muasi mwenye dhambi kubwa na laana. Mwanamume asiyesitiri magoti yake anapaswa kushauriwa ili ayasitiri. Pamoja na hayo, kuamrisha mema kunapaswa kufanyika kwa maneno laini. Na mtu akiitikia kwa ujeuri anapaswa kujibiwa kwa ukimya. Kwa upande mwingine, ujeuri wa mwanamume aliyeonesha mapaja yake unapaswa kukabiliwa na kuadibhiwa/kuadhiriwa.

Endapo mwanamume atadhihirisha uchi wake kwa ujeuri (pamoja na kwamba ameonywa), basi anapaswa kushitakiwa kwenye mahakama ya kisheria ili alazimishwe kuusitiri. Ukiupa kipaombele huo hupewa katika hali ya ukiukaji wa sheria kwa anayeangalia sehemu za siri za mwanamume”. Katika madhehebu yote manne, ni lazima kwa wanawake kuisitiri miili yao yote, isipokuwa viganja vyao na nyuso zao, kwa wanaume ambao si maharimu wao na wanawake wasiokuwa waislamu; hii ina maana kwamba wanapaswa kusitiri miguu yao, mikono yao na nywele zao wakiwepo watu kama hao (yaani wanaume wasio maharimu wao na wanawake ambao si Waislamu). (Watu ambao si maharimu kwa jinsia zote mbili wameelezewa katika sura ya tano ya kitabu kiitwacho Endless Bliss).

Kwa mujibu wa madhehebu ya kishafi, ni lazima pia kwa wanawake kutoonyesha nyuso zao kwa watu hao waliotajwa hapo awali.

Ikiwa wanawake wenyewe au wazazi wao au ndugu zao au waume zao hawataitilia maanani sheria hii, basi watakufuru. Ni dhambi kubwa kwa wavulana kucheza densi ngoma au michezo huku mapaja yao yakionekana. Na ni dhambi kwa wasichana kufanya hivyo bila kusitiri vichwa vyao na mikono yao, na kuwatazama wakifanya hivyo. Muislamu hapaswi kupoteza muda wake wa faragha kwa kucheza

michezo au kufanya mambo yasiyokuwa ya manufaa ya aina yoyote, badala ya kujinufaisha na kujielimisha na kusali. Kwa mujibu wa Kimyaa-i-saadat: “kama ilivyo haramu kwa wanawake na wasichana kutoka nje hali ya kuwa vichwa vyao, mikono yao na miguu yao iko wazi, ni haramu pia kwao kutoka nje wakiwa wamevaa nguo nyembamba zinazowabana na zilizopambwa na kufukizwa kwa uturi au mafuta mazuri.

Na ikiwa Wazazi wao, waume zao na ndugu zao wanaridhika na kupenda vitendo hivyo watachukuliwa kama washirika wao katika dhambi hilo na kwa hivyo watapata sehemu ya adhabu ya dhambi. Kwa maneno mengine, watachomwa pamoja motoni. Lakini wakifanya toba wataghufiriwa madhambi yao na hawatachomwa. Kwani Allahu taala huwapenda watu wanaotubia.

## IMANI YA AHL AS-SUNNA SIO KAMA WALIVYO CHUKULIA KINA MAWAHABI ILI KUWATEKA WALE WASIO JUA KITU KATIKA UISLAMU

Naandika mistari hii baada ya kusalimisha mikono yangu kwa Allahu taala. ‘Hamd’ maana yake ni kuamini kwamba Allahu taala pekee ndie mwenye kila aina ya neema na hutushushia sisi, hivyo, tunapaswa kuelezea ukweli huu. Shukr (kushukuru, kutoa shukrani) maana yake ni kutumia neema zote kwa namna inayokubalika na sheria za Kiislamu (yaani maamrisho na makatazo ya Allahu taala). Neema hizo zimetajwa katika vitabu vya wanazuoni wa Ahl as-Sunna. Wanazuoni wa Ahl as-Sunna ni wale wanaojikita katika madhehebu manne.

Imam Muhammad al-Ghazali "rahmatullahi alaih" ametaja katika kitabu chake Kimyaa-i-sa’aadat kwamba “Mtu akisilimu, kimsingi inamuajibikia kujua na kuamini maana ya **KALIMATU** Laa ilaaha i-l-Allah, Muhammadun Rasuulullah. Neno hili linajulikana kama kalimat at-tawhiid. Inatosha kwa kila Muislamu kuamini maana ya kirai hiki bila ya kutilia shaka yoyote. Si lazima kwake kukitolea ithibati kwa dalili au kuiridhisha nafsi yake. Mtume wa Allahu taala hakuwaamrisha Waarabu kujua au kutaja uthibitisho au kutafuta au kufafanua mambo yanayoweza kutiliwa shaka. Aliwaamrisha tu kuamini na kutokuwa na shaka. Inamtosha mtu yeyote pia kuamini kwa pamoja bila ya kujua kiundani. Halafu ni faradh kifaaya (faradhi ya kutoshelezeana haja

yaani watakapofanya baadhi yao hua si lazima kwa wengine kufanya na kama hawakufanya wote basi hupata dhambi wote kwa pamoja) kwamba wawepo angalau wanazuoni wachache katika kila mji. Ni wajibu kwa wanazuoni hawa kujua ithibati, kuondoa shaka na kujibu maswali. Wao ni kama wachunga kwa Waislamu. Wanawafundisha imani kwa upande mmoja, na kwa upande mwingine wanatoa majibu ya kashfa za maadui wa Uislamu.

Quran Tukufu imetaja maana ya Kalimat at-tawhiid na mtume wa Allahu taala rehma na salamu zimshukie ameeleza yaliyoteremshwa kwake. Maswahaba wote walijifunza maelezo haya wakayawasilisha kwa watu waliokuja baada yao.

Wanazuoni wa daraja la juu ambao walitufundisha na kutueleza yale masahaba walio wafundisha kwa kuyaandika katika vitabu vyao bila ya kuyafanyia mabadiliko yoyote, wanajulikana kama Ahl-ul haqi. Watu wote wanapaswa kujifunza itiqadi (nguzo za imani) na kuungana na kupendana. Mbegu ya furaha imo katika itiqadi hii na muungano huu.

Wanazuoni wa Ahl as-Sunna wanaelezea maana ya Kalimat attawhiid kama ifuatavyo, “Watu hawakuwepo mwanzoni. Waliumbwa tu baadae. Wana muumba mmoja. Hana mshirika wala anayefanana nae. Amekuwepo tangu azali (maana ya azali uwepo usio na mwanzo) uwepo wake haukuwa na mwanzo. Atakuwepo milele, uwepo wake hauna mwisho. Hatosita kuwepo. Uwepo wake ni muhimu daima. Yeye kutokuwepo ni jambo lisilowezekana. Uwepo wake ni wa dhati yake. Hahitaji muongozo wowote. Hakuna kitu kisicho muhitaji. Yeye ndiye alieumba vitu vyote na kuvifanya viendelee kuwepo. Yeye si kitu cha kutumika kutengenezea vitu vingine. Yeye hayuko mahali fulani wala katika dutu maalum. Hana umbo na hawezi kupimika“. Haiwezekani kuulizwa jinsi alivyo, tunaposema “yeye”, hakuna kinachoweza kutokea katika fikra zetu wala tunachoweza kufikiria kuwa ni yeye. Yeye si kama vitu hivi. Vyote ni viumbe vyake. Yeye si kama viumbe wake. Yeye ni muumba wa kila kinachokuja katika kumbukumbu zetu, kilicho halisi na cha kufikirika. Yeye hayuko juu, chini wala upande mmoja. Hana mahali. Kila kiumbe kiko chini ya ‘Arsh. Na ‘Arsh iko chini ya mamlaka yake, chini ya kudra yake. Yeye yuko juu ya ‘Arsh. (Arshi ni vitu vyote vilivyoumbwa na allah kwa hio tukisema Allah yuko juu ya Arshi yake maana yake yuko juu kiutawala na kuviongoza na kuviamrisha anavyotaka) wala haimaanishi kuwa ‘Arsh humbeba yeye. ‘Arsh huwepo kwa ihsani yake katika kudura wake. Yeye ni kama alivyokuwa milele, katika kipindi cha milele

kilichopita. Atabaki yule yule wakati wote katika mustakbali wa milele kama alivyokuwa kabla ya kuiumba ‘Arsh. Hakuna kinachobadilika ndani yake. Ana sifa zake mwenyewe. Ana sifa nane zinazojulikana kama As-sifaat ath-Thubuutiyya ambazo ni uhai, ujuzi, usikivu, kuona, uwezo [omnipotent], kutaka [will], kunena na kuumba. Hakuna kinachobadilika katika sifa zake hizi. Kwani kubadilika humaanisha upungufu. Yeye hana upungufu wala hila. Ingawa hafanani na yeyote kati ya viumbe wake, inawezekana kumtambua katika dunia hii kadri anavyowawezesha viumbe kumtambua na kumuona yeye huko akhera. Hapa duniani anajulikana pasina kumtambua yukoje, na kule akhera ataonekana katika namna isiyotambulikana. [Tafadhali rejelea barua ya arubaini na sita ya mjalada wa kwanza wa Maktubat (kilichoandikwa na Walii mkuu na mwanazuoni Imam Rabbani Mujaddidi elfi-thaani Ahmad Faruqi Serhendi, "rahmatullahi alaih"). Tafisri ya Kituruki ya barua hiyo hupatikana katika sura ya ishirini na sita ya sehemu ya pili ya Endless Bliss].

Allahu taala alituma mitume, amani iwe juu yao, kwa viumbe wake (wanaadamu). Kupitia watu hawa waheshimiwa, aliwaonyesha wanaadamu matendo yanayoweza kuleta furaha na yale yanayosababisha maangamizi. Mtume wa hadhi ya juu zaidi ni Muhammad "swallallahu alaihi wa sallam", mtume wa mwisho. Alitumwa kama mtume kwa watu wote yaani si wa kabila au taifa au nchi au bara fulani bali ni mtume wa viumbe wote hata majini (na hadithi ya Ibnu Mas’ud inaelezea hivo,) mchamungu na asiyekuwa mshika dini, kwa kila sehemu na kila taifa katika ardhi hii. Yeye ni mtume wa wanaadamu wote, malaika na majini. Katika kila pembe ya dunia kila mtu anapaswa kumfuata na kushikamana na mtume huyu mwenye hadhi ya juu zaidi.

Sayyid Abdulhakim-i-Arwasi, "rahmatullahi alaih", alisema mtume wa Allahu taala rehma na salamu zimshukie alikuwa na majukumu matatu. La kwanza ni kuwasilisha na kutangaza sheria za Quran tukufu, yaani elimu ya imani na sheria za kifiqhi kwa wanaadamu wote. sheria za kifiqhi zimeundwa kwa matendo yaliyoamrishwa na yale yaliyokatazwa. Matawi haya mawili ya elimu huunda sheria za Kiislamu. Jukumu lake la pili lilikuwa kuwasilisha sheria za Quran za kiroho, elimu kumhusu Allahu taala mwenyewe na sifa zake katika nyoyo za wale walio juu zaidi miongoni mwa umma wake. Jukumu lake la kwanza lisichanganywe na lile la pili. Watu wasiofuata madhehebu, (yaani wanaokana madhehebu manne), wanakataa jukumu la pili. Hata hivyo, Abu Huraira "radiyallahu anhu", alisema: “Nilijifunza elimu ya

aina mbili kutoka kwa mtume "swallallahu alaihi wa sallam". Nimekwambieni moja wapo ya aina hizo. Kama ningeelezea ile ya pili, mngeniua”. Maneno haya ya Abu Huraira yameandikwa katika vitabu vya Bukhaari, Mishqaat, Hadiiqa na kwenye barua za Maktubat nambari 267 na 268.

Jukumu la tatu lilielekezwa kwa waislamu ambao hawakutii nasaha na mawaidha yanayohusiana na utekelezaji wa sheria za kifiqhi. Nguvu zilikuwa zikitumika kuwalazimisha kutii sheria hizo. Baada ya enzi za mtume "swallallahu alaihi wa sallam", kila mmoja wa makhalifa wanne, radhi za Allahu taala ziwashukie, alitekeleza kikamilifu majukumu haya matatu. Katika enzi za Hadhrat Hasan bin Ali "radiyallahu anhu", fitna na bid’a zilikithiri. Uislamu ulikuwa umesambaa katika mabara matatu. Mwangaza wa kiroho wa mtume "swallallahu alaihi wa sallam", ulikuwa umefifia kwenye ardhi hii. Idadi ya masahaba ilipungua. Baada ya kipindi hicho, hakuna mtu aliyekuwa na uwezo wa kutekeleza majukumu hayo matatu katika hali ya upweke. Kwa hiyo, majukumu hayo yalichukuliwa na makundi matatu ya watu. Jukumu la kuwasilisha imani na sheria za kifiqhi lilipewa viongozi wa Kiislamu wajulikanao kama Mujtahid. Miongoni mwa akina mujtahid hawa kuna waliowasilisha Imani na walijulikana kama mutakallimun. Nao ni wanazuoni wa elimu ya aqidah. Wale waliowasilisha fiqh wakajulikana kama fuqahaa. Jukumu la pili, yaani la kuwafanya Waislamu wanaotaka kuzipata sheria za kiroho za Quran tukufu lilipewa maaimamu kumi na wawili wa Ahl Bayt Allah awarehemu na wanasufi wakuu. Sirrii (Sarii) as-Saqatii (aliyefariki mwaka wa 251 H./876 A.D. huko Baghdad) na al-Junayd al-Baghdadi (aliyezaliwa mwaka wa 298 H./911 A.D. mjini Baghdad) ni wawili kati yao, Allahu taala awarehemu.

Jukumu la tatu, kuzifanya sheria za kiislamu zitekelezwe kwa nguvu, lilipewa masultani, yaani serikali mbalimbali. Jopo la watu wa tabaka la kwanza linalojulikana kama madhehebu. Jopo la pili linajulikana kama Tariiqa na la tatu ni ulindaji wa haki za watu (jurisprudence). Madhehebu yanayoelezea imani yanaitwa madhehebu ya Ahl as-Sunna. Yaani imani mtume wetu "swallallahu alaihi wa sallam" alisema kwamba waislamu watagawanyika kiimani katika makundi sabini na tatu. Kundi moja tu ndilo litakuwa la ukweli na mengine yatakuwa ya uongo. Na kweli ilitokea hivyo. Kundi lililobashiriwa kuwa litakuwa la ukweli ni la Ahl as-Sunna wal-Jamaa’a. Makundi mengine sabiini na mbili yaliyotangazwa kuwa ya uongo, yanajulikana kama makundi ya bid’a, yaani ya uzushi. Hakuna lolote kati yao ambalo ni la makafiri. Wote ni waislamu. Lakini iwapo Muislamu anasema kwamba amejikita

katika kundi lolote kati ya yale sabini na mbili akakana taarifa ambayo imetajwa waziwazi Quran tukufu, hadithi tukufu na ile iliyoenea (shamiri) miongoni mwa waislamu, basi atakufuru. Hivi leo, kuna waislamu wengi ambao, ijapokuwa wana majina ya Kiislamu, tayari wametoka kwenye madhehebu ya Ahl as-Sunna na kuwa wana bid'a au wasio waislamu". Mwisho wa kunukuu kutoka kwa Bwana 'Abdulkarim Efendi.

Waislamu wanapaswa kutafuta elimu udogoni hadi wakati pale wanapoingia kaburini. Elimu ambayo wanapaswa kujifunza inajulikana kama al-ulum al-Islamiyya ambayo imeundwa kwa sehemu mbili: I) Al-uluum an-naqliyya, ll) Al-uluum Al aqliiya.

**I) Al- uluum an- naqliyya** (ambayo pia inaitwa sayansi ya dini); Hii ni elimu inayopatikana katika vitabu vya wanazuoni wa Ahl as-Sunna. Wanazuoni wa Kiislamu waliitoa elimu hii kwenye vyanzo vikuu vinne. Vyanzo hivi vinajulikana kama adillat- ashshar'iyy Navyo ni: Quran tukufu, hadithi za mtume, Ijmaa al-umma na Qiyaas al-fuqahaa.

Elimu ya kidini imeundwa kwa matawi makuu manne:

1) 'Ilm at-tafsiir (sayansi au maelezo ya Quran tukufu). M taala mu wa tawi hili anaitwa mufassir, ni mtaala mu aliyebobea aliye na uwezo wa kuelewa anachokusudia Allahu taala katika maneno yake.

2) 'Ilm ul-usuul al-hadith. Tawi hili hushughulikia uainishaji wahadithi. Aina mbalimbali za hadithi zimeelezewa katika Endless Bliss, sehemu ya pili, sura ya sita.

3) 'Ilm al-hadith. Tawi hili huchunguza kwa makini matamko (hadith), mwenendo (sunna) na tabia za mtume wetu sala na salamu zimshukie.

4) 'Ilm usuul al-kalaam. Tawi hili huchunguza mbinu ambazo chanzo 'Ilm al-kalaam hunyambuliwa kutokana na Qurani na Hadithi.

5) 'Ilm al-kalaam. Tawi hili huangazia dhana za 'Kalimatu tawhiid na 'Kalimat ash-shahada' na nguzo sita za imani zenye mwegemeo wa dhana hizo. Haya ni mafundisho ambayo inapaswa kuyaamini kwa yakini. Wanazuoni wa kalaam mara kwa mara waliandika 'ilm usuul al-kalaam' na 'ilm al-kalaam' pamoja. Kwa hiyo, mtu wa kawaida anayachukulia matawi haya kuwa kitu kimoja.

6) 'Ilm usuul al-fiqhi. Tawi hili huchunguza unyambuaji wa mbinu za fiqh kutokana na Qurani na Hadith.

7) 'Ilm al-fiqh. Tawi hili ni la af'aal al-mukallafiin, yaani inazungumzia jinsi watu waliokomaa na kubaleghe wanavyopaswa

kushughulikia mambo yanayohusu miili yao. Af'aal al-mukallafiin matendo ya watu walio kuwa washafikia balaghe na ni wazima wa akili yana sehemu nane: Faradh, wajib, sunna, mustahabb, mubaah, haram, makruuh na mufsid. Hata hivyo, yanaweza kuainishwa kwa urahisi katika makundi matatu: Matendo yaliyoamrishwa, matendo yaliyokatazwa na yanayoruhusiwa (mubaah).

8) 'Ilm at-tasawuf. Tawi hili hujulikana pia kama' Ilm al-akhlaaq (maadili). Halielezei tu mambo yanayopaswa kufanywa na yasiopaswa kufanywa bali huchangia katika kuifanya imani ihusike moyoni, na kuwasaidia waislamu kutekeleza majukumu yao kulingana na mafundisho ya fiqhi na pia kupata maarifa. Kati ya matawi haya manane, ni faradh 'ain kwa Waislamu wote, wanawake na wanaume, kujifunza kalaam, fiqh na tasawuf, kadri inavyowezekana, na ni hatia ama dhambi kutojifunza mambo hayo.

**II) Al-uluum al-aqliyya** (hujulikana pia kama elimu ama sayansi za kimajaribio). Elimu hizi zimegawika katika makundi mawili: Elimu ya kiufundi na elimu ya kiubunifu. Ni faradhi kifaaya kwa waislamu kujifunza sayansi hizi. Ama elimu ya kiislamu, ni faradh 'ain (ni kila amali ambayo mtu inamlazimu aifanye kwa ulazima na kuifanya kwake ataandikiwa thawabu na kutoifanya kwake ataandikiwa dhambi) kujifunza elimu hiyo kadri inavyohitajika. Kujifunza mengi zaidi ya inavyohitajika, yaani kubobea katika elimu ya Kiislamu, ni fardh kifaaya. Iwapo hakutakuwa na mwanazuoni hata mmoja katika mji, wakazi wake na serikali iliyoko madarakani watapatwa na dhambi.

Mafundisho ya kidini hayabadiliki katika mapito ya wakati. Hakuna udhuru kwa mtu kufanya makosa wakati akizungumzia ilmul kalaam, ni hatia au kosa lisilosameheka. Hairuhusiwi hata kidogo kufanya mabadiliko katika mambo ya dini kwa kutumia maoni au mtazamo wa mtu binafsi. Kitendo hiki kinaweza kumpelekea mtu kutoka kwenye Uislamu. Mabadiliko na maendeleo katika ulum al-aqliyya yanaruhusiwa. Ni muhimu kuiendeleza kwa kuzitafiti na hata kujifunza kutoka kwa watu ambao si Waislamu.

Makala ifuatayo imenukuliwa kutoka katika kitabu cha al-Majmu'at az-zuhdiyya. Ilikusanywa na aliyekuwa waziri wa elimu, Sayyid Ahmad Zuhdu Pasha, "rahmatullahi alaih".

Neno 'fiqh' likitumika katika umbo la faqiha yafqahu, yaani katika kategoria ya tano, lina maana ya kujua Uislamu. Mtaalamu katika uwanja wa fiqh anajulikana kama faqiih. 'Ilm al-fiqh inashughulikia matendo ambayo watu wanapaswa kuyatenda. Elimu ya fiqh

imeundwa kwa Quran tukufu, Hadithi za mtume, Ijmaa na Qiyaas. Makubaliano ya masahaba watukufu na mujtahidiin waliokuja baada yao yanajulikana kama ijmaaul umma. Sheria za dini zinazotokana na Quran tukufu, Hadithi na Ijmaaul umma huitwa Qiyaas al-fuqahaa.

Ikitokea kwamba kuna jambo ambalo hukumu yake haieleweki katika Qurani au hadithi, liwe la halali au haramu, basi jambo hilo litalinganishwa na lile ambalo hukumu yake inaeleweka. Ulinganishaji huu ndiyo unaojulikana kama Qiyaas (analojia). Ili kutumia Qiyas jambo la pili lilihitajika kuwa na kigezo sawa na lile la kwanza ambacho kilipelekea lile la kwanza kuwa halali au haramu na hukumu hii hutolewa tu na wanazuoni waliobobea katika elimu na ambao wamefikia kiwango cha ijtihad.

Elimu ya fiqhi ni pana sana. Imegawika katika sehemu kuu nne:

1) Ibadaat, ambayo ina sehemu ndogo tano: Salat, Saum, Zakat, Hajj na Jihad. Kila moja kati ya hizo ina sehemu kadhaa. Kama tulivyoona ni kitendo cha ibada kufanya maandalizi kwa jihadi. Mtume wetu sala na salamu zimshukie alisema kuna aina mbili za jihadi dhidi ya maadui wa Uislamu: Jihadi kwa maneno na kwa matendo. Ni faradhi kujifunza jinsi ya kuunda na kutumia silaha mpya ili kujiandaa kwa jihadi ya matendo. Jihadi hufanywa na taifa. Ni faradhi kwa watu kujiunga na jihadi kwa kutii sheria za serikali zinazohusiana na jihadi. Siku hizi uvamizi wa maadui kupitia machapisho, filamu, vipindi vya redio na kila nyenzo ya propaganda- aina ya pili ya vita- umekithiri. Kwa hiyo, ni jihadi pia kupambana na maadui katika uwanja huu.

2) Al usrat (Munakahat), ambayo una vigawanyo vidogo vidogo kama vile ndoa, talaka, masurufu (baada ya mume kumuacha mke) na mambo mengine [yaliyoandikwa kwa upana kuhusu minasaba mbalimbali katika sehemu ya sita ya Endless Bliss. Tafadhali soma sura ya 12 sehemu ya tano na sura ya 15 sehemu ya sita].

3) Muamalaat, ambayo ina vigawanyo vidogo vidogo kama vile kununua, kuuza, kupangisha, ushirika, riba, urithi, na kadhalika. [Tafadhali tazama aya nne za mwisho za sura ya 6 sehemu ya nne na pia sura 19 za mwisho, sehemu ya 5 ya Endless Bliss].

4) ‘Jinaayati (kanuni ya adhabu) ambayo ina sehemu ndogo Qiswaas (ulipizaji kisasi), sarqat (wizi), zina (uzinifu), qadhf (kashfa) na ridda (kuritadi).

[Tafadhali tazama sura za 11, 12, 13, na 14 za Endless Bliss].

Ni faradhi kwa kila Muislamu kupata ujuzi wa kutosha wa fiqhi inayohusu ibada. Ni faradhi kifaaya kujifunza usrat na muamalat, kwa

maneno mengine, taaluma hizi mbili lazima watu wajifunze kadri wanavyozihitaji. Baada ya ‘ilm at-tafsiir, ‘ilmul hadiith na ilmul kalaam, taaluma muhimu zaidi ni ‘ilm al-fiqhi. Hadithi 6 zifuatazo zinadhihirisha umuhimu wa ‘ilm al-fiqhi:

“Allahu taala akimtakia mja wake kheri, humpa ujuzi wa dini (humfanya faqiih)”.

“Mtu anapopata ujuzi wa dini (akishakuwa faqiihi) Allahu taala humtimizia matakwa yake”.

“Mwenye hadhi ya juu ni yule aliye na ujuzi wa dini (faqiih katika mambo ya kidini)”.

“Faqiih (mjuzi wa fiqh) ni imara zaidi dhidi ya shetani kuliko ‘aabid (anayeabudu Allahu taala) mara elfu moja”.

“Kila kitu kina muhimili na muhimili wa dini ni ujuzi wa fiqhi”.

“Ibada bora na yenye thamani ni kujifunza na kufundisha fiqhi”.

Ubora wa Imamu mkuu Abu Hanifa, "rahmatullahi alaih", unaweza pia kudhihirika kwa kurejea hadithi hizo. Mafundisho ya Kiislamu katika madhehebu ya Kihanafi yaliwasilishwa kupitia kwenye silsila au mtiririko iliyoanza na ‘Abdullah ibn Masuud, radhi za Allahu taala zimshukie, ambae alikuwa sahaba. Hii ina maana kuwa Imamu mkuu Abu Hanifa, "rahmatullahi alaih", muasisi wa madhehebu hayo, alipata elimu ya fiqhi kutoka kwa Hammad, naye Hammad aliipata kutoka kwa Ibrahim an-Nakhai. Ibrahim al-Nakhai alisomeshwa na ‘Alkama na ‘Alkama akajifunza kutoka kwa ‘Abdullahi ibn Masuud, aliyefundishwa na Mtume wa Allahu taala rehma na salamu zimshukie”.

Abu Yusuf, Imam Muhammad As-Shaibaani, Zufar ibn Hudhail na Hasan ibn Ziyaad walikuwa wanafunzi wa Imam mkuu, rehma za Allahu taala ziwashukie. Kati ya hawa, Imam Muhammad aliandika vitabu vipatavyo elfu moja vya mafundisho ya Uislamu. Alizaliwa mwaka wa 135 H. na akafariki huko Rayy, nchini Iran mwaka wa 189 H. (sawa na 805 A.D.). Kwa vile alimuoa (mjane) mamaake as-Shaafi’i, mmoja wa wanafunzi wake, vitabu vyake vyote viliachwa kwa Shaafi’i baada ya kifo chake, jambo ambalo lilichangia kuongezeka kwa elimu ya Ash-shaafi’i. Kutokana na sababu hii, Imamu As-Shaafi’i, rehma za Allahu taala zimshukie alisema “Naapa kwamba elimu yangu ya fiqhi iliongezeka kwa kusoma vitabu vya Imamu Muhammad. Wale ambao wangetaka kuzama katika elimu ya fiqhi wanapaswa kuandamana na wanafunzi wa Imamu Abu Hanifa”. Na alisema “Waislamu wote ni kama familia (watoto) ya Imamu mkuu”. Kwa maneno mengine kama ambavyo mwanamume huchuma riziki kwa ajili ya mke na watoto

wake, Imam mkuu alihakikisha kuwa anapata elimu ya dini ambayo watu waliihitaji katika mambo yao. Kwa kufanya hivyo akawarahisisishia waislamu kazi ngumu.

Imam Abu Hanifa rehma za Allahu taala zimshukie, alikusanya elimu ya fiqhi, akaiainisha katika matawi makuu na madogo na akaiwekea usuli kadhaa (mbinu). Aidha alikusanya mafundisho ya aqida kwa namna inayolandana na mawaidha ya mtume na masahaba, akayafundisha kwa mamia ya wanafunzi wake. Baadhi ya wanafunzi wake walikuwa wanazuoni wa ‘ilm alkalaam, yaani walifundisha Imani. Abu Bakr al-Jurjaani, mwanafunzi wa Imam Muhammad ash-Shaibaani ni mmoja wa wanazuoni hao waliopata umaarufu. Abu Nasr al-Iyaadi ni mmoja wa wanafunzi wake alimfundisha Abu Mansur al-Matruudi ‘ilm al-kalaam. Abu Mansur aliandika kwenye vitabu vyake mafundisho ya kalaam kama alivyoyapokea kutoka kwa Imamu mkuu, rehma za Allahu taala zimshukie. Aliweza kuimarisha imani ya Ahl as-Sunna kwa kupingana na wanabid’a na aliisambaza katika maeneo ya karibu na mbali. Alifariki huko Samarkand mwaka wa 333 H. (sawa na 944 A.D.). Mwanazuoni huyu mkuu na mwengine Abul Hasan al-Ash’ari, wanajulikana kama maimamu wa madhehebu ya itikadi (mtazamo wa) ya kisunni.

Wanafiqhi wamegawanyika katika viwango saba. Kamal Pashazade Ahmad ibn Sulaiman Efendi, rehma za Allahu taala zimshukie, alieleza katika kitabu chake Waqf an-niyyaat kama ifuatavyo.

1) Mujitahid wa Uislamu ambao walibuni mbinu na sheria zilizofuatwa katika kuibua mihimili kutokana na vyanzo vinne vya dini (al-adillat al-arba’a) na kuibua mihimili kutokana na kanuni walizoweka. Mfano wa wanazuoni hawa ni Maimam wa madhehebu (yaani Imam mkuu Abu Hanifa, Imam Malik, Imam Ash-Shaafi’i na Imam Ahmad ibn Hanbal, vinara wa madhehebu manne).

2) Mujtahid ndani wa madhehebu, ambao kwa kufuata sheria zilizowekwa na maimamu wa madhehebu, waliibua kanuni kutokana na vyanzo hivyo vinne. Hao (katika madhehebu ya Kihanafi) walikuwa: Imam Abu Yusuf na Imam Muhammad, rehma za Allahu taala ziwashukie.

3) Mujtahid katika marahma ya kidini ambayo hayakugusiwa na mwasisi wa madhehebu. Waliibua kanuni kwa kutumia mbinu na kanuni za madhehebu. Pamoja na hayo, walilazimika kumfuata Imam. Miongoni mwao ni At-Tahawi (aliyeishi kati ya miaka ya 238-321H, nchini Misri), Hassaaf Ahmad ibn Umar (aliyefariki mwaka wa 261 mjini

Baghdad), Abdullahi ibn Husein al Kerkhi (340 H.), Shams al-a'imma AL-Halwaani (483 H.), Fakhr ul Islam Ali ibn Muhammad al-Pazdawi (400-483 H., huko Samarqand), Qadhi Khan Hasan ibn Mansur al-Farghaani (592 H.) na kadhalika, rehma za Allahu taala ziwashukie wote.

4) As haab at-takhriij, ambao hawakutakiwa kutumia ijtihad. Walikuwa wanazuoni walioelezea kwa ufupi sheria zilizowekwa na mujtahid ambazo hazikuwa wazi. Mmoja wao ni Hasan ad-Diin ar Raazi Ali ibn Ahmad. Anajulikana pia kwa lakabu kama 'Jessaas'. Alifariki mwaka wa 370 H.

5) Ar-Baab at-tarjiih, waliopendelea riwaya moja kati ya zile zilizopokelewa kutoka kwa mujtahid. Hao walikuwa Abul Hasan Al-Quduuri (362-428 H. mjini Baghdad) na Burhan ud-diin Ali al Marginaani, muandishi wa al-Hidaaya aliyeuliwa na majangili wa Cengiz katika mauaji ya Bukhaara mwaka wa 370 H. (1193 A.D.).

6) Wanazuoni walioandika riwaya kadhaa kuhusu jambo fulani kulingana na mpangilio wake (kama jambo lililotokana na misingi ya kutegemewa) walijulikana kama muqallid na hawakuweka riwaya yoyote iliyokataliwa katika vitabu vyao. Nao ni Abul Barakaat Abdullahi ibn Ahmadan-Nasafi (aliyefariki mwaka wa 710 H.), muandishi wa Kanz ad-daqaaiq na Abdullah ibn Muhammad al Musuli (aliyefariki mwaka wa 683 H.), muandishi wa Mukhtaar, Burhaan ash-Shari'a Mahmud ibn Sidras-Shari'a Ubaidullah (aliyefariki mwaka wa 673), mwandishi wa al-Wiqaaya na Ibn as-Saa'aati Ahmad ibn Ali al-Baghdaadi (aliyefariki mwaka wa 694), mwandishi wa Majmaa' al-Bahrain, rehma za Allahu taala ziwashukie.

7) Wapo pia na muqallid wasioweza kutofautisha kati ya riwaya dhaifu na halisi.

Baada ya kujiingiza katika jambo kubwa asilolimudu, mleta mabadiliko katika dini sasa anaanza kuchanganyikiwa. Maskini ambaye hawezi kuvumilia mshikamano wa waislamu na maimamu wa madhehebu kwa kutii hadithi zilizonukuliwa hapo juu au aya zilizonukuliwa mara kadhaa hapo awali. Kwa vile ameshindwa kupata sababu yoyote ambayo imejengwa kwenye misingi ya elimu na akili ya kuilaumu taqliid. Anasema kwamba taqliid huzuia elimu na maarifa. Tulilijibu dai lake hili katika makala yaliyotangulizwa. Je, maamrisho ya aya au hadithi husababisha madhara? Jibu twaliachia uelewa na mantiki ya wasomaji wetu.

Bw. 'Abdul Wahhab ash-Sha'raani aliandika katika kitabu chake al-Mizaan al-Kubra:

“Ndugu zangu Waislamu! Kuweni wenye kuzingatia. Kama mtume wa Allahu taala hakufafanua yale yaliyoteremshwa kwa mukhtasari au kitaashira katika Quran tukufu ingebaki katika hali ya kutojulikana hadi leo hii. Kama maimamu wetu wa madhehebu ambao ni warithi wa mtume "swallallahu alaihi wa sallam" hawakuelezea hadithi fupi fupi sunna za mtume zingekuwa katika hali ya kuto julikana hadi leo hii. Kwa hivyo, wanazuoni wa kila karne, kwa kufuata mtume "swallallahu alaihi wa sallam" walifafanua hadithi zilizokuwa zimejitokeza kwa muhtasari. Katika Sura An-Nahl Allahu taala anaelezea kwamba aliiteremsha Qurani kwa mtume ili awabainishie watu yaliyoteremshwa kwao. Bayan maana yake ni kuelezea aya za Allahu taala. Kwa njia nyingine ama kwa namna tofauti. Kama wanazuoni miongoni mwa umma wangeweza kuelezea aya za Quran na kutoa tafsiri za aya fupi na kuona sheria kwenye Qurani tukufu, Allahu taala angalimwambia mtume “wambie yale yaliyoteremshwa kwako kupitia malaika” na asingemwamrisha kutoa maelezo.

Shaikhul Islamu Zakaria "rahmatullahi alaih" alisema: “kama mtume "swallallahu alaihi wa sallam" hakufasiri yaliyotangazwa kwa muhtasari katika Quran tukufu na kama maimamu wa madhehebu hawakueleza yaliyowasilishwa kiishara, hakuna mtu yeyote kati yetu angezielewa. Kwa mfano kama mtume "swallallahu alaihi wa sallam" hakuelezea jinsi ya kutawadha katika hadithi zake, tusingeweza kufikia mahitimisho kwenye Quran kuhusu jinsi ya kufanya hivyo. Vivyo hivyo, idadi ya rakaa katika sala, sheria, kesi na kiwango cha nisaab, masharti na vitendo vya faradhi na sunna vinavyohusu kufunga, hija na zaka, visingeonekana kwenye Quran tukufu. Hakuna sheria yoyote iliyoteremshwa kua ishara ambayo ingeeleweka kama hazikuelezewa katika hadithi.

“Ni dalili ya unafiki kupambana dhidi ya wanazuoni wa Kiislamu kwani inamaanisha kupinga tu bila sababu na kukataa ushahidi wao. Allahu taala alitangaza katika aya ya 46, Suratun Nisaa: **“hakika hawatakuwa waumini mpaka watakapokufanya hakimu katika yale yaliyojiri baina yao, kisha wasitilie wasiwasi katika hukumu uliyotoa na wajisalimishe kweli kweli”**.

Aya hii inamaanisha kuwa wale wasioridhika na maamuzi ya mtume au maamrisho ya Quran si waumini. Hadithi inasisitiza kuwa “Msigombane wala kubishana mbele ya mtume. Kwa vile wanazuoni ni warithi wa mtume, kugombana au kubishana na wanazuoni wa dini yake, kujaribu kukosoa jitihadi zao ambazo ni sahihi, hujamaanisha kugombana naye (yaani mtume). Kama ambavyo tunapaswa kuamini

na kuyakinisha wahyi aliouleta hata kama hatuwezi kupata sababu zake na ushahidi wake, hivyo tunapaswa kuamini na kuyakinisha elimu iliyotujia kutoka kwa maimamu wa madhehebu, hata kama hatuelewi ushahidi wao wa kimaandishi, kwani kuwapinga wao ni kuupinga Uislamu. Ijapokuwa kuna sheria tofauti katika dini za mitume "Alaihim us salaam", sisi Waislamu tunaamini na kuwatambua wote kama mitume wa Allahu taala, kwa vile wameungana juu ya jambo hilo. Madhehebu nayo yanapaswa kutambuliwa. Watu ambao si mujtahid wamefarakana. Madai ya mtu asiye mujtahidi, kwamba madhehebu fulani yana kasoro, hayapelekei madhehebu hayo kuwa na kasoro. Imam Ash-Shaafi´i alisema: “Kujisalimisha ni nusu ya imani”. Naye Bw. Rabii’ akadakia na kusema: “Hapana. Bali ni imani kamili”. Imam Ash-Shaafi´i akakubali maoni hayo. Aidha Imam Ash-Shaafi’i alisema: “Mtu mwenye imani kamili hasemi lolote kuhusu elimu ya usuul. Yaani haulizi kwa nini ni hivi kwa nini siyo vile?” alipoulizwa elimu ya usuul ndio ipi? Alijibu: “Hufunua Qurani, Sunna na Ijmaa al umma”. Kauli hii hudhihirisha kuwa tunapaswa kusema kwamba tunaamini elimu yote iliyokuja kutoka kwa Allahu taala na mtume wake kama alivyoiteremsha. Vile vile, tunapaswa kuamini yaliyopokelewa kupitia kwa wanazuoni wa kiislamu, yaani pasi na ubishi. Kwa hiyo, Imam ibn ‘Abdul Barr (aliyefariki mwaka wa 463 H./1071 A.D.) alisema: “Hakuna Imamu wetu yeyote ambaye amesikika akiwaamrisha wanafunzi wake kufuata madhehebu fulani. Waliwaambia kufuata fatwa za madhehebu wanayopenda, kwa vile madhehebu yote yapo kutokana na rehma za Allahu taala. Haikutajwa katika hadithi yoyote, iwe sahihi au dhaifu, kwamba mtume "swallallahu alaihi wa sallam" amemwamrisha mtu yeyote miongoni mwa umma wake kupendekeza madhehebu fulani.

Imam al-Quraafi anasema “kama ilivyoshuhudiwa na masahaba wote, mtu aliyemfuata Hadhrat Abu Bakr na Hadhrat Umar radhi za Allahu taala ziwashukie kwa kushikamana na fatwa zao“, alikuwa pia akiuliza sahaba mwingine kuhusu tabia zake zingine na angetekeleza yale aliyojifunza. Hakuna mtu ambaye angekataa ushahidi au maandiko. Kwa mujibu wa maridhiano ya wanazuoni, inafaa kwa Muislamu mpya kujifunza na kutenda (vitendo vya ibada) kwa kumuuliza mwanazuoni wa madhehebu fulani, pasi na kuomba uthibitisho, na iwapo hakuwapata wanazuoni wa madhehebu, amuulize mwanazuoni yeyote lakini baadae, ajifunze mojawapo ya madhehebu ya ahlu haqi na ayafuate. Mtu jeuri anayekataa maridhiano haya, anapaswa kuleta uthibitisho kwa kukanusha kwake.

Allama Sayyid Ahmad at-Tahtaawi, mwanazuoni mkubwa wa Kihanafi wa kutoka Misri, aliandika katika mada ya Dhabaayh katika Hashiyatu Durr ul-Mukhtar “Kulingana na wanazuoni wa Tafsiiri walio wengi, aya isemayo “Hakika wale waliofarakanisha dini yao wakawa makundi”. Huwarejelea watu wa bid’a ambao wangejitokeza katika umma huu. Katika Hadithi iliyopokelewa na Bw. Umar radhi za Allahu taala zimshukie, amesema mtume "swallallahu alaihi wa sallam" alisema, akimwambia Aisha radhi za Allahu taala zimshukie: “aya inayohusu kugawanya katika makundi katika dini huwaelekea watu wa bid’a na wafuasi wa matamanio ya nafsi zao ambao watajitokeza katika umma huu”. Katika Sura al-An`am, aya ya 153 Allahu taala anasema: “Na kwa hakika hii ndiyo njia iliyonyooka. Basi ifuateni.” (Yaani Wayahudi na Wakristo na makundi mengine ya waasi waliacha njia ya kweli, msigawanyike kama wao). Katika Sura Aali-Imran, aya 103, Allahu taala alitangaza “Na shikamaneni nyote kwenye kamba (yaani dini ya Allah) ya Allahu taala wala msifarakane!”. Baadhi ya wanazuoni wa tafsiri walifafanua kwamba: ‘kamba ya Allahu taala’ ni jama’a (muungano ama umoja)”. Amri isemayo: ‘Msifarakane’, huonesha kwamba ndivyo mambo yalivyo na kwamba jama’a ndio wenye fiqhi na elimu. Mtu anayekhitilafiana na fuqahaa (wanafiqhi) kadri ya shubiri hujikita katika uasi, hunyimwa msaada wa Allahu taala na anastahili moto wa Jahannam, kwa sababu wasomi (fuqahaa) wako kwenye njia ya kweli na wameshikamana na sunna za mtume "swallallahu alaihi wa sallam" na njia ya makhalifa waongofu radhi za Allahu taala ziwashukie. Waislamu walio wengi wako kwenye njia ya fuqahaa. Wale wanaotoka kwenye njia yao wataingizwa katika moto wa Jahannam. Enyi mlioamini, fuateni kundi lililo pekee lililokingwa kutokana na Jahannam. Na kundi hili ni lile linaloitwa Ahl as-Sunna wal-Jamaa’a. Kwani msaada, kinga na uongofu wa Allahu taala ni wa wale wanaofuata kundi hili, na ghadhabu na mateso yake yameandaliwa kwa wale wanaojitenga na kundi hili. Siku hizi, kundi hili liloongoka huunganishwa kwenye madhehebu manne ambayo ni Hanafii, Malikii, Shaaf’i na Hanbalii. Wakati huu, yeyote asieshikamana na mojawapo ya madhehebu haya manne ni mtu wa bid’a na ameandaliwa Jahannam. Wanabid’a wote hudai wako kwenye njia ya kweli. Suala hili haliwezi kuhukumiwa kwa madai tu au udhanifu bali kwa ripoti za wa taala mu katika uwanja huu na wanazuoni wa hadithi, ambao ripoti zao zimejengwa juu ya msingi wa ukweli [1].

Maimamu wanne wa madhehebu ndio vinara wa dini ya Kiislamu. Maulamaa wa Kiislamu wameandika vitabu kadhaa wa kadhaa kuhusu

wasifu na ubora wao, kama vile, sehemu zifuatazo za kitabu cha Kiarabu zenye vichwa ‘Ashadd ul-Jihaadi fii ibtwaali Da’watil-Ijtihaad’, ‘al-Minhat ul-Wahbiyyatu fir-raddi ‘ala Wahabiyya’, na vitabu vyenyewe vijulikanavyo kama ‘Hidaayat ul-Muwaffiqiin’ na ‘Sabiil un-Najaat’ vilivyochapishwa Istanbul. Ifuatayo ni tafsiri ya ‘Ashadd ul-Jihaad’ ambayo imelenga kuwaahidi na kuwaongoza vijana:

1) Imam wa kwanza miongoni mwa maimamu wa Ahl as-Sunna Imam mkuu Abu Hanifa an-Nu’maan ibn Thaabit ("rahmatullahi alaih"). Alizaliwa mwaka wa 80 H. (699 A.D.) akafariki mwaka wa 150 H. (767 A.D.) mjini Baghdad. Yeye ni muasisi wa madhehebu ya Kihanafi. Wa ottoman (wana wa makhalifa wa dola la Uthman), Waislamu wa India, Siberia na Turkistan wamekuwa wakitekeleza ibada kulingana madhehebu ya Hanafi. Kuna Hadithi inayoelezea kwamba: ‘Abu Hanifa ni nuru ya umma’. Hakuna haja ya kusisitiza uchamungu wake (wara’), upaji dunia kisogo (zuhud), ukarimu, uhodari, na busara, sifa ambazo zinajulikana sana. Robo tatu ya elimu ya fiqhi ni yake. Na anashirikiana na maimamu wengine wa madhehebu katika robo iliyobaki. Imam Shaafi’i alinukuliwa akisema “Vyanzo vya fiqhi walivyonavyo watu ni Abu Hanifa na wanafunzi wake“. Yeyote anayetaka kujifunza fiqhi anapaswa kukimbilia kutegemea elimu ya Abu Hanifa na wanafunzi wake. Nilipomuuliza Imam Malik iwapo amewahi kumwona Abu Hanifa, alisema, Ndiyo. Nimewahi kumuona Abu Hanifa. Alikuwa mtu ambae hata kama angalidai kuwa nguzo hii imeundwa kwa dhahabu angetoa ithibati sahihi kwa madai hayo. Hakuna mtu ambae angethubutu kumpinga. Watu walikuwa usingizini kuhusiana na taaluma ya fiqh, Abu Hanifa akawaamsha wote. Isa ibn Musa mmoja wa wale waliojitenga kwa minajili ya ibada na kuipa dunia kisogo zama hizo, alipokuwa ameandamana na Abu Ja’far Mansuur, aliyekuwa Amirul mu’miniin, Abu Hanifa aliingia chumbani. Isa akamwambia Mansuur kuwa mgeni huyo alikuwa mwanazuoni mkubwa wa kimataifa. Mansuur akamuuliza Imam ni nani alimuelimisha. Akamjibu kwamba alisomeshwa na wanafunzi wa Hadhrat Umar "radiyallahu anhu". Mansuur akasema “hakika una tegemeo jema”.

Imam mkuu Abu Hanifa alikuwa akisali kila usiku. Siku moja, alipokuwa amelala ndani ya Kaaba, akaamshwa na sauti: “Ewe Abu Hanifa! Umenitumikia kwa uaminifu. Umenitambua ipasavyo. Kulingana na imani yako na shukrani zako, nimekusamehe na wale watakaokufuata mpaka siku ya kiama”. Ni habari nzuri ilioje kwa Abu Hanifa na wafuasi wa madhehebu yake. Tabia na sifa zake nzuri

anayeweza kuwa nazo si mwingine isipokuwa mjuzi na Imam wa madhehebu ambaye alikuwa mujtahid. Kati ya maimamu wote waliokuwa mujtahid na wasomi wakomavu aliowaelimisha, Abdullahi ibn Mubaarak, Imam Malik, Imam Mis'ar, Abu Yusuf, Muhammad Ash-Shaibaani na Imam Zufar ndio wanaotoa ushuhuda wa hadhi yake ya juu. Ingawa alitamani sana kujitenga na watu aingie utawani au upweke kwa sababu alikuwa mwenye staha na haya, alianza kutoa fatwa kadhaa alipoamrishwa na mtume wa Allahu taala katika ndoto yake kutangaza madhehebu yake. Madhehebu yake yalienea katika sehemu nyingi. Idadi ya wafuasi wake iliongezeka. Palijitokeza watu waliomwonea wivu, lakini wote walishindwa na wakafedheheka. Wanazuoni wengi walijifunza usuuli na furuu' (shina na matawi/ mbinu) za madhehebu yake na wakaandika vitabu vingi. Wale ambao walikuwa na uwezo wa kuchunguza na kufahamu maandiko yenye ithibati naqlii (yenye kutegemea vyanzo kama vile Quran na Hadith) na aqlii (yenye kuzingatia akili ama mantiki) waliandika mambo kadhaa kuhusu ubora wake.

Ijapokuwa Abul Faraj ibn al-Jawzii amenukuu baadhi ya visa vinavyomdunisha Imam mkuu kwenye kitabu chake, yeye aliviandika si kwa shabaha ya kumdunisha Imamu bali kuonyesha kuwa kulikuwa na watu waliokuwa wakimwonea wivu. Katika kitabu hicho hicho alimsifu Imam mkuu kuliko wale wengine. Babake Imam mkuu Thabit, alikuwa amemtembelea Hadhrat Ali "radiyallahu anhu", aliyemuombea yeye na wanawe baraka. Dua hiyo ilibainika kwa Imamu mkuu. Alieanza na kuwa mmoja wapo wa Taabi'un kutokana na kupata suhba ya baadhi ya masahaba hususani Anas ibn Malik "radiyallahu anhu" (yaani radhi za Allah ziwe juu yake).

2) Imam Malik ibn Anas "rahmatullahi alaih" alizaliwa Madina mwaka wa 95 H. (715 A.D.) akafariki huko huko mwaka wa 179 H. (795 A.D.). Alisema kwamba alianza kutoa fatwa baada ya shinikizi la maimamu 70. Alisema, "Kati ya mabwana zangu walionifundisha, kuna wachache mno ambao hawajachukuwa fatwa kutoka kwangu" kama kauli ya Imam Shaafi'i, kauli hii ya Imamu haikukusudia kuonyesha majigambo. Ilikusudiwa kuonesha neema ya Allahu taala. Az-zarqaani ameandika katika sherehe yake juu ya Muwatta. Imam Malik ni imam maarufu wa madhehebu. Alikuwa wa juu zaidi katika wanazuoni wa zama zake. Alikuwa mwanamume mwenye akili timamu na maadili dhahiri. Alikuwa mrithi wa hadithi za mtume "swallallahu alaihi wa sallam". Alieneza dini ya Allah miongoni mwa wanadamu. Alikuwa rafiki wa maulamaa mia tisa na alinufaika sana. Alikusanya na kuandika

hadithi 100,000. Alianza kufundisha akiwa na umri wa miaka kumi na saba. Waliohudhuria mihadhara yake walikuwa wengi zaidi kuliko wale waliohudhuria mihadhara ya walimu wake. Walikusanyika mbele ya mlango wa nyumba yake ili kujifunza hadithi na fiqhi. Ilibidi amwajiri bawabu (mlinda geti la mlango wa kuingilia). Aliwaruhusu wanafunzi wake kwanza halafu watu wengine kuingia ndani. Alikuwa akienda msalani mara moja katika siku tatu. Alikuwa akisema, “Naona haya kukawia (kuchukuwa mda mrefu) msalani”. Alipoandika kitabu chake kiitwacho Muwatta, alianza kushuku uaminifu wake. Aliweka kitabu hicho ndani ya maji akasema “Kama kitabu hiki kitarowana, sitokihitaji”. Hata hivyo, hakuna sehemu ya kitabu hicho japo ndogo hivi iliorowana. Abdurrahman ibn Anas alisema “Hakuna mtu katika ardhi hii ambae anategemewa zaidi katika elimu ya Hadithi kuliko Malik. Sijamwona mtu mwerevu kuliko yeye. Sufyaan ath-Thauri ni imam katika Hadithi, lakini si Imam katika Sunna. Al-Awzaa’i ni Imam katika Sunna na siyo katika Hadithi. Imam Malik ni Imamu katika Hadithi na Sunna pia”. Yahya ibn Said alisema “Imam Malik ni shahidi wa Allahu taala kwa viumbe wake (wanadamu). Imam Shaafi’i alisema “Popote Hadithi inapochunguzwa, Malik ni kama nyota ya mbinguni. Hakuna mtu ambae angeweza kumfikia Malik katika kuhifadhi, kuelewa na kutunza Hadithi. Maoni yangu ni kwamba Malik hana kifani katika uaminifu. Shahidi kati yangu na Allahu taala ni Malik. Kama si Malik na Sufyan ibn Uyaina kufikia sasa elimu ingekuwa imetoweka katika eneo la Hijaz”. ‘Abdullah alipomuuliza babake Ahmad ibn Hanbal ni nani ndie mjuzi zaidi miongoni mwa wanafunzi wa Zahrii, babake alisema kwamba Malik ndie mjuzi zaidi katika kila tawi la elimu. Ibn Wahab alisema, “Kama si Malik na Laith sote tungeenda kombo”. Al-Awzaa’I alikuwa akisikia tu jina la Malik likitajwa, alisema `Yeye ni msomi sana miongoni mwa wasomi`. Alim mkubwa wa Madina na mufti wa Haram mbili. Aliposikia habari ya kifo cha Imam Malik, Sufyan ibn ‘Uyayna alisema “ Hivi sasa dunia haina mtu kama yeye, alikuwa Imam wa dunia. Alim wa Hijaz, shahidi wa zama zake na jua la ummat Muhammad "swallallahu alaihi wa sallam". Tushikamaneni na njia yake”. Ahmad ibn Hanbal alisema kwamba Imam Malik alikuwa mbora kuliko Sufyan Aththaurii, Laith, Hammad na al-Awzaa’ii. Sufyan ibn ‘Uyayna alisema aliyekusudiwa katika hadithi isemayo kwamba “ Watu wakimuhitaji mtu kwa haraka, hawatampata mtu mwengine anayemzidi mwanazuoni wa Madina ni Imam Malik. Imam Malik alisema kwamba alikuwa akimwona mtume "swallallahu alaihi wa sallam" kila usiku kwenye ndoto. Mus’ab alisema kwamba alimsikia

babake akisema, “Malik na mimi tulikuwa katika Masjid an-Nabawii. Mtu mmoja akaja karibu nasi akauliza ni nani kati yenu ni Abu Abdillahi Malik? Tukamuonyesha. Akamkaribia akarusha mkono na kuuzungusha kwenye shingo lake kisha paji la uso wake. Akasema “Nilimuona mtume wa Allahu taala "swallallahu alaihi wa sallam" kwenye ndoto akiwa amekaa hapa. Akasema, ‘mwite Malik’. Akaja na hali anatetemeka. ‘Tuliza nafsi yako ewe Aba ‘Abdillahi. Kaa kitako na ufungue kifua chako’, alitoa amri. Kifua chake kilifunguka kikasambaza manukato yenye kupendeza kila mahali. Imam Malik alilia akasema kwamba ndoto hiyo hufasiriwa kama elimu”.

3) Imam ash-Shaafi’i (rahmaullahi alaih rehma za allah ziwe juu yake). Jina lake ni Muhammad ibn Idris ibn Abbaas ibn Uthmaan ibn Shaafi’i. Ukoo wake una asili ya kutoka kwa Hashim ibn Abd al-Muttalib kama babu yake wa nne ambaye ami yake Hashim alikuwa miongoni mwa mababu wa mtume wa Allahu taala. Babu yake wa tano Saayib, alikuwa katika jeshi la maadui kwenye vita vya Badr, lakini baadaye yeye na mwanae Shaafi’i walisilimu wakawa masahaba. Kwa hiyo Imamu huyu alipewa jina la Shaafi’i. Mama yake ni Sharifa aliyetokana na kizazi cha Hadhrat Hasan "radiyallahu anhu". Alizaliwa Gaza mwaka wa 150 H. (767 A.D.) akafia Misri mwaka wa 204 H. (820 A.D). Alipokuwa na umri wa miaka miwili, alipelekwa Makkat al-Mukarrama, ambapo alihifadhi Qurani akiwa mtoto mdogo na kitabu cha Imamu Malik al-Muwatta’ akiwa na umri wa miaka kumi. Alianza kutoa fatwa akiwa na umri wa miaka kumi na tano. Alienda Madinatul-Munawwara mwaka huo huo akapata elimu kutoka kwa Imam Malik. Alienda Baghdad mwaka wa 185. Baada ya miaka miwili alienda Makka kufanya hija. Alirejea Baghdad mwaka wa 198 akapata makazi huko Misri mwaka wa 199. Baada ya kipindi kirefu tokea kifo chake kulikuwa na watu waliotaka kuupeleka mwili wake huko Baghdad na kaburi lake lilipochimbwa, harufu ya miski ilijitokeza ikawalewesha watu waliokuwepo wakakata tamaa.

Kuhusu elimu na ujuzi wake, alikuwa mbora kuliko maimamu wa zama zake na mbora pia kuliko watu wengi waliomtangulia. Madhehebu yake yalienea katika sehemu nyingi. Wakazi wote wa Haramu mbili (Makka na Madina na ardhi takatifu Palestine) walikuwa wafuasi wa Shaafi’i. Hadithi isemayo kwamba, “Mwanazuoni wa Kiquraishi ataijaza dunia kwa elimu” ilibainika kumhusu Imam as-Shaafi’i. Abdullahi alipomuuliza babaake Ahmad ibn Hanbal kwa nini anamuombea sana Imam Shaafi’i, babaake alimjibu, “Ewe mwanangu, Nafasi ya Imam Shaafi’i miongoni mwa watu ni kama ile ya jua

mbinguni. Yeye ni mponyaji wa nafsi”. Zama hizi, Muwatta ilkuwa na hadithi 9500, lakini baadae ilifupishwa na kubakiza hadithi zilizopo sasa ambazo idadi yake ni 1700. Alipewa jina la kupanga (lakabu) la Naasir as-Sunna (mwokozi wa sunna/ dini). Jambo lililowashangaza wengi ni kwamba alianzisha madhehebu mapya katika kipindi kifupi sana cha miaka minne. Zaidi ya vitabu 40 vimeandikwa kwa madhumuni ya kudhihirisha wadhifa na ubora wake.

4) Imam Ahmad ibn Hanbal as-Shaibaanii al-Maruuzii (rahmatullahi alaih) alizaliwa Baghdad mwaka wa 164 H. (780 A.D) akafia huko huko mwaka wa 241 H. (855). Alikuwa Imam katika taaluma mbili, Hadithi na Fiqh. Aidha, alikuwa mahiri katika mambo yaliyokuwa magumu kueleza na shupavu katika kuelezea mambo ya sunna ya ndani sana. Alijulikana kwa zuhd na wara (kujitenga na mapambo ya dunia). Alienda, Basra, kwenye miji mitakatifu ya Makka na Madina, Yemen, Damascus na Mesopotamia ili kukusanya Hadithi. Alijifunza fiqh kutoka kwa Imam ash-Shaafi’i aliyejifunza Hadithi kutoka kwake. Ibrahim al Harbii alisema, “Niliwahi kumuona Ahmad ibn Hanbal. Kama Imam Ahmad angeishi katika enzi ya ath-Thauri, al-Awzaa’I, Malik na Laith ibn Sa’d, angewazidi wote kiwango”. Alihifadhi Hadithi milioni moja. Imam ash-Shaafi’i alimtumia barua kutoka Misri. Alipoisoma, alilia. Alipoulizwa kwa nini alilia, alisema “alimwona mtume wa Allahu taala "swallallahu alaihi wa sallam" kwenye ndoto, akamwamrisha, “Mwandikie Abu ‘Abdillahi Ahmad ibn Hanbal barua na uweke ndani yake salamu zangu. Atakuja kuulizwa iwapo Qurani ni kiumbe. Mwambie asijibu swali hilo. Wanaume 800,000 na wanawake 60,000 walihudhuria mazishi yake. Siku ya kufariki kwake, wayahudi na wakristo 20,000 walisilimu. Maimamu hawa wanne wa Ahl as-Sunna walikuwa wabora katika Hadithi kwenye karne ya pili.

Abd al-Ghani an-Nabluusii ameandika mambo yafuatayo:

“Kuna aya isemayo kwamba Allahu taala hawatakii waja wake wepesi na hawatakii ugumu. Na katika hadithi kama ambavyo Allahu taala anataka kuondokana na makatazo yake, anataka vile vile tutumie rukhsa aliotoa. Yaani anataka tufanye vitendo ambavyo ameruhusu waja wake kuvifanya. Jambo hili lisieleweke vibaya. Imam al-Manaawi aliandika katika sherehe yake ya al-Jaami’ as-Saghiir, ‘Hairuhusiwi kukusanya rukhsa za madhehebu yote ukaunda madhehebu mapya ya rukhsa kitendo ambacho kinampelekea mtu kukaidi Uislamu’. Abdussalam alisema kwamba ingeruhusiwa kwa sharti kwamba usiuache Uislamu. Imam as-Subki alisema, ‘Inaruhusiwa kuhamia kwenye madhehebu ambayo ni mepesi zaidi kwa mtu wakati wa haja

na dharura kubwa. Lakini hairuhusiwi kama hakuna dharura kubwa kwani katika hali hiyo itakuwa kwa manufaa ya mtu na siyo kwa ajili ya kuilinda dini ya mtu. Hairuhusiwi kubadili madhehebu mara kwa mara. Nimetoa maelezo kamili kuhusu taqliid ya madhehebu katika kitabu changu Khulaasat atitahqiiq fii bayaani hukmi 't-taqliid wat-talfiiq.

Hairuhusiwi kufanya hila katika sheria ili kuifanya halali kuwa haramu, yaani, hiyo si ruhusa iliotolewa na Allahu taala. Ibn al-Izz, katika kuelezea taqliid ya madhehebu mengine, aliandika 'Mtu anapaswa kujiepusha na kufanya hila katika mambo ya kisheria kama njia ya kuridhisha matakwa yake binafsi bila kuelewa maneno ya maimamu wa madhehebu au kuzijua hila za kisheria'. Ni jambo lililo wazi kwamba muqallid hawazijui hila za kisheria na wanatumia neno 'hila' walilosikia kutoka kwa maimamu wa madhehebu kulingana na matakwa yao. Imamu mkuu Abu Hanifa alisema kwamba mamufti wale waliofundisha hila za kisheria wangeadhibiwa.

Ruhusa anayopenda Allahu taala ni ile aliyoitoa kwa wale wanaojikuta kwenye dhiki wakati wanapokuwa wakitekeleza amri yake. Pamoja na hayo, hairuhusiwi kukwepa kutekeleza amri au kutafuta ruhusa zinazoafiki uelewa wa mtu. Najm ad-Diin al-Ghazali aliandika katika kitabu kinachoitwa Husnut-tanabbuhi kwamba, shetani hamuachi mtu kutumia ruhusa ya Allahu taala. Kwa mfano, hamruhusu kufanya mash kufuta au kupangusa badala ya kuosha kwenye khuf (ni aina maalum ya viatu). Humfanya anawe miguu yake. Mtu anapaswa kutumia ruhusa na siyo kutafuta ruhusa za madhehebu wakati wote kwa sababu ni haramu kukusanya ruhusa za madhehebu mbalimbali. Ni njia ya shetani.

Wasalaf as-Saalih walio wengi (Waislamu wa karne mbili za kwanza za Uislamu) walipata usumbufu mwingi. Walitekeleza ibada ngumu. Usifanye jinsi walivyofanya. Fuata njia ya ruhusa iliyotajwa katika Quran tukufu na Hadithi. Lakini usiwakashifu watu hao wakubwa, Walikuwa wameelimika sana na wenye akili kuliko wewe. Huyajui waliokuwa wakiyajua. Usiingilie mambo usiyoyajua au kuyaelewa na usiwafuate. Jitahadharishe na kuwapinga watu hao wakubwa kwa kutegemea yale unayoelewa kutoka kwenye Qurani na Hadithi. Waliielewa Qurani na Hadithi vizuri sana kuliko unavyoelewa. Kwa vile walikuwa karibu zaidi na enzi ya mtume "swallallahu alaihi wa sallam" kuliko wewe, kwa vile akili zao ziliongolewa na maarifatullah (kumjua Allahu taala), kwa vile walishikamana kikamilifu na sunna na kwa vile ikhlas yao, imani, tawhidi na zuhd ilikuwa ya kiwango kikubwa zaidi, waliyajua mambo mengi kuliko wewe na wengine wanaokufanana.

Ewe mtu maskini mwenye wadhifa wa kidini mchana na usiku (muda wote) umekuwa ukikimbilia matamanio ya tumbo lako na nafsi. Umepata baadhi ya maalumaati ya kidini ili kuviridhisha/kuvishibisha. Kwa kutegemea ujuzi wako kidogo unajichukulia kuwa ni bingwa wa Uislamu. Unajaribu kushindana na Salaf as-Saalihiin. Usiwakashifu watu hao wenye umaarufu wa Uislamu waliojitolea kujifunza na wakafundisha elimu na wakatakasa nyoyo zao kwa matendo mema na ambao walijiepusha na mutashabiihaat mambo yalio fanana au kuwa baina ya halali na haramu, ili wale chakula cha halali na waepukane na haramu! Walikuwa juu zaidi kuliko wewe. Hali yako hii ni kama ile ya shorewanda anayeshindana na kipanga katika kula na kunywa. Mujaahada, riyaada, ibaada, ijtihaad na maneno ya watu hao wakubwa yalieandana na mafundisho ya Qurani na Hadithi. Salaf as-Saalihiin wenyewe walitekeleza amri, lakini wakatoa fatwa ili Waislamu watumie ruhusa.

Maulamaa wa Ahl wa kiislamu walio wengi walisema kwamba imani kwa kukubali tu ni sahihi (faafu), hata kama muqallid wa imani kama huyo ni muasi na mwenye madhambi. Kwa sababu ameacha istidlaal (kujiridhisha kwa hitimisho za kimantiki). Kwa maneno mengine, mtu anayeamini kutokana na mafundisho aliyopata kwa mtu mwingine bila kufikiria au kufahamu, ni muumini, Muislamu. Karama (miujiza) ya awliyaa ni ya ukweli. Wanaweza kuwa na miujiza wakiwa wafu au hai. Karaamaat ya Hadhrat Mariam, Ashaab ul-Kahf na Aasaf ibn Barhiyaa na ya waziri mkuu wa nabii Sulaiman "alaihis-salaam" imeonyeshwa katika Quran. Karaamaat ni mambo yanayofanywa na wanazuoni wa Ahl as-Sunna na ambayo hayawezi kutambulika kwa kutumia mantiki au sayansi.

Mujtahid hakosei wakati anapotafuta na kuchagua aya au hadithi kama ushahidi. Lakini anaweza kukosea wakati anapofikia mahitimisho ya sheria kutokana na ushahidi alioupata. Kwa hiyo, mujtahid ambaye hakukosea atapewa thawabu kumi na yule aliyekosea atapewa thawabu moja. Mtume wa Allahu taala "swallallahu alaihi wa sallam" alimuamrisha Hadhrat ‘Amr ibn al-Aas “Wewe mwenyewe unafikia mahitimisho kuhusu sheria! Usipokosea utapata thawabu kumi, ukikosea utapata moja”. Kuhusu mambo ambayo hujayapatia ufumbuzi, thawabu hiyo moja si ya bidii uliyofanya katika ijtihad lakini ni kwa sababu ya usumbufu katika kupata ushahidi. Akifanya makosa katika kupata ushahidi, hatopata thawabu yoyote lakini wale wanaofuata ijtihadi kama hizo hawataadhibiwa. Mbele ya Allahu taala ni moja tu kati ya ijtihad nyingi (kuhusu rehma makhsusi) ndiyo sahihi.

Nyingine zote si sahihi. Kwa mujibu wa wanazuoni wa kundi la Mu’tazila, mujtahidi hakosei na yale ambayo ni sahihi ni ya namna nyingi. Maelezo kamili kuhusu ijtihad yametolewa katika sherehe ya Mir’aat al-Usuul na Mirqaat al-wusuul ambazo ziliandikwa na Mulla Khusraw.

Imetajwa katika hadithi kwamba uongo na uzushi vitakithiri baada ya karne ya tatu. Bid’a na uasi vitaongezeka. Idadi ya wale wanaoacha njia ya salaf as-Saalihiin katika mas’ala ya imani na ibada itaongezeka. Wanafiqhi na watawa wanaofuata mkondo wa tasawuf, ambao wanashikamana na Qurani, Sunna na Ijmaa’ ya salaf as-saalihiin wataokolewa huku watu wengine wakiteseka milele. Wanafiqhi na wajuzi wa tasawuf watakuwepo mpaka mwisho wa dunia utakapofika. Lakini haitajulikana kwa yakini wao ni akina nani. Hata hivyo, wale ambao waislamu watataja sifa zao watajulikana.

Ni fardh ‘ain (faradhi kwa waislamu wote) kujifunza ‘ilm al haal (mafundisho ya dhehebu moja). Allahu taala anasema: “Basi ulizeni wanazuoni ikiwa hamjui”. Kwa hiyo, inafaa wale wasiojua kupata elimu kutoka kwa wanazuoni au kwenye vitabu vyao. Vivyo hivyo, hadithi huwahimiza watu, wanaume kwa wanawake, kutafuta elimu. “Kutafuta elimu ni jambo la faradhi kwa kila Muislamu”. Maamrisho haya hudhihirisha kuwa ni muhimu kujifunza mambo yanayohusu mwili na moyo kutoka kwenye vitabu vya ‘ilm al-haal na kwamba haifai kuamini yale wasemayo wajinga wasiofuata madhehebu (hususani wanaodai kuwa ni waleta mabadiliko katika dini).

Kwa mujibu wa makubaliano ya wanazuoni wa njia iliyo sahihi, ni fardh ‘ain kwa Muislamu kujifunza ipasavyo, imani, halali, haramu na ibada. Wasipojifunza haya kutoka kwenye vitabu vya ‘ilm al-haal, watakuwa ima wanabid’a Ni fardh kifaaya (fardh ambayo ikitekelezwa na baadhi ya waumini, wengine hawapati dhambi) kujifunza mambo mengine zaidi ya hayo yaliyotajwa, kwa mfano, matawi kumi na mbili ya lugha ya kiarabu, tafsiri, hadithi, sayansi, tiba na hisabati. Mtu mmoja wa mji fulani akitenda kitendo cha fardh kifaaya, basi kitendo hicho kitakuwa mustahab na siyo fardhi kwa wakazi wa mji huo. Kutunza vitabu vya fiqh katika mji wowote ni kama kutunza maulamaa wa Kiislamu. Si fardhi kwa mtu yeyote katika mji kama huo kujifunza tafsiri, hadithi na fiqhi inayozidi kiwango kinachohitajika, bali ni mustahab. Si fardhi kwa mtu yeyote kupata ushahidi juu ya sheria au kujifunza sheria hizo, lakini ni mustahab kwa wanazuoni. Kujifunza matawi hayo ya elimu ni bora zaidi kuliko kufanya ibada ya sunna. Pale ambapo hakuna khalifa, wanazuoni hutekeleza majukumu yake. Ni

wajibu kuwa watiifu kwa wanazuoni hao ambao maisha yao huafikiana na elimu yao.

Tangu enzi za masahaba, maadui wa Uislamu wamekuwa wakiwadanganya waislamu kwa kujifanya watu wenye majukumu ya kidini ili wauvunje Uislamu kutoka ndani. Maadui wa namna hii wanaitwa ‘mazindiki,’ ‘wafanya mageuzi,’au ‘washikiliaji wa itikadi ya kisayansi’. Wamewadanganya wajinga na kuwatoa kwenye Uislamu katika kila karne, japokuwa wameshindwa kuudhuru Uislamu, kwa sababu kumekuweko wanazuoni wengi wa fiqh na tasawuf katika kila karne ambao wamekuwa wakiwaonya Waislamu kwa mihadhara yao na makala ili wasidanganywe. Lakini leo hii, idadi ya wanazuoni wa kiislamu imepungua jambo ambalo limewapa maadui fursa ya kuuhujumu Uislamu. Wamekuwa wakiupiga vita Uislamu wakijifanya watu wenye nafasi katika dini. Wanao weza Kugundua madhara haya ya kisirisiri, ni waislamu wenye sifa za wanazuoni wa kiislamu.

Hadhrat Muhammad Ma’thuum al-Faruuqi as-Sirhindi "rahmatullahi alaih" alielezea sifa za wanazuoni wa kiislamu kama ifuatavyo: “Usifanye urafiki na mtu asietii maamrisho ya kiislamu au yule aliyeacha njia ya haki na kufuata njia ya bid’a! Jitahadharishe na watu wenye vyeo katika dini ambao wanafanya mambo ya bid’a! Hadhrat Yahya ibn Ma’adh ar-Raazi (Quddisa sirruh) alisema, ‘epukana na watu wa aina tatu. Jitenge nao: Aliyeghafilika (anayejishughulisha na matamanio ya nafsi yake akamsahau Allahu taala) na wenye vyeo vya kidini ambao wamepotoka katika maadili, wasomi (waliohifadhi Qurani wakawa wanaikariri) wanaojipendekeza kwa matajiri na masufi wasiojua lolote kuhusu Uislamu. Ikiwa atajitokeza mtu akawa ni mwenye mamlaka katika dini na si mwenye kumtii mtume "swallallahu alaihi wa sallam", yaani sunna zake, na asieshikamana na Uislamu, tunapaswa kujitenga naye na tusinunue wala kusoma vitabu vyake. Tunapaswa kuwa mbali nao. Hata kuwasifia kidogo kutaharibu imani yako. Yeye si mtu mwenye mamlaka juu ya Uislamu, bali ni adui mwenye madhara kwa Uislamu. Anachafua dini na imani yako. Yeye ni hatari zaidi kuliko shetani. Matamko yake yanaweza kuwa matamu na yenye kuvutia na anaweza kujifanya mtu asiyependa dunia hii (zaahid). Pamoja na hayo unapaswa kumkimbia kama ambavyo ungemkimbia mnyama mkali. Al-Junaid al-Baghdaadi (Quddisa sirruh), mwanazuoni wa kiislamu, alisema: “Kuna njia moja tu itakayonipeleka kwenye furaha ya milele nayo ni kushikamana na sunna za mtume "swallallahu alaihi wa sallam". Usimfuate mtu mwenye vyeo vya kidini ambae hasomi vitabu vya wanazuoni wa Ahl as-Sunna au yule asiyefuata njia

iliyobainishwa katika hadithi, kwani mwanazuoni wa kiislamu anapaswa kufuata njia iliyooneshwa na Qurani na hadithi.

Salaf as-Saalihiin walikuwa kwenye njia ya haki. Walikuwa waaminifu. Walipata upendo wa Allahu taala na ridhaa zake. Njia yao ilikuwa ile iliyobainishwa katika Qurani na Hadithi. Walishikamana na njia ya kweli.

Vigogo wa tasawuf na maulamaa wa fiqh walikuwa kwenye njia ya salaf as-saalihiin. Wote walishikamana na Uislamu. Walipata heshima ya kuwa warithi wa mtume wa Allahu taala. Hawakuuwacha Uislamu hata kidogo, katika matamko yao, matendo yao na tabia zao.

Nasisitiza tena kwamba usidhani kwamba wale wanaolegeza kamba katika kumtii mtume wa Allahu taala au wanaopotoka katika njia yake, kwamba ni wenye mamlaka juu ya mambo ya dini! Usiamini matamko yao ya uongo au maandiko yao yanayovutia! Wayahudi, Wakristo, Wabudha na Wabrahama wamekuwa wakitumia matamko matamu na yenye kusisimua na kughilibu ili kueneza propaganda kwamba wako kwenye njia ya kweli na huwashawishi watu kufuata njia ya kheri na furaha.

Njia inayompelekea mtu kufikia kila aina ya furaha katika Uislamu, njia ya uokovu, ni sunna za mtume "swallallahu alaihi wa sallam". Kumtii mtume ni ishara inayotofautisha kati ya ukweli na uongo. Neno lolote, maandishi au kitendo kinachopingana na dini yake, hakina thamani. Abdullah ibn Mubarak "rahmatullahi alaih" alisema “atakaelegeza kamba au kutokutilia umuhimu katika kufanya vitendo ambavyo ni mustahab, hawezi kutenda kitendo cha sunna.” Ulegezaji kamba na kuto kutilia umuhimu katika kufanya sunna humfanya mtu asiwe na hima bidii katika kutenda kitendo cha faradhi. Na anaelegeza kamba katika faradhi hawezi kupata maarifa ayapendayo Allahu taala’. Kwa sababu hiyo imebainishwa katika hadithi kwamba ‘kufanya dhambi humpeleka mtu kwenye ukafiri’. Hadhrat Abu Sa’iid Abul kheir (aliyefariki mwaka wa 440 H. /1049 A.D.), mmoja wapo wa mawalii mashuhuri, aliulizwa, ‘Fulani anatembea juu ya maji. Unasemaje kuhusu rehma hiyo? Akasema, ‘Halina maana’. Hata bata anaweza kuelea juu ya maji’. Akaulizwa, ‘Fulani anaruka angani. Akajibu, ‘Thamani yake ni kama ya nzi’. Akaulizwa, ‘Fulani anatoka kwenye mji mmoja na kwenda kwenye mji mwingine papo hapo. Akasema, ‘Shetani naye hutoka mashariki na kwenda magharibi kwa ghafla’. Mambo kama hayo hayana thamani katika dini yetu. Mwanamume halisi huishi na watu, akaenda kununua bidhaa na akaoa, pamoja na hayo hamsahau Allahu taala hata kidogo’. Hadhrat Abu Ali ar Rodbaari

(aliyefariki mwaka wa 321 H./933 A.D. huko Misri), mmoja wapo wa mawalii wakuu na mwanafunzi wa al-Junaid al-Baghdaadi, aliulizwa, ‘Mwanaume mwenye majukumu ya kidini ambae husikiliza ala za muziki [au kufanya urafiki na wasichana wasio maharimu zake, au kumruhusu mke wake au binti zake kutoka nyumbani bila ya kujifunika kama ilivyoelezewa na Uislamu] na ambae husema kwamba moyo wake umetakasika na kwamba moyo ni muhimu, unasemaje kuhusu mtu huyo?’ Alisema, ‘makao yake ni Jahannam,’ Akasema, Abu Sulaiman ad-Daaraani, aliyekaa katika kijiji kinachoitwa Darya huko Damascus na akafia huko mwaka wa 205/820, alisema, ‘Kwanza nalinganisha fikra na nia zangu na Qurani na Sunna. Halafu nasema na kufanya matendo yanayowiana na vyanzo hivyo viwili vya sheria.’

Sheikh ibn Abi bakr Muhammad ibn Muhammad al-Andaluusi, aliyeishi Misri na kufariki mwaka wa 734 H./1334 A.D., alisema katika kitabu chake Ma’arij al-Hidaaya, jifunze jambo la kweli na uwe mkweli! Kila kitendo, wazo, neno na tabia ya mtu mkamilifu huafikiana kikamilifu na zile za mtume "swallallahu alaihi wa sallam", kwani kila aina ya furaha inaweza kupatikana kwa kumfuata mtume.

Kumfuata mtume maana yake ni kushikamana na Uislamu ipasavyo’.

Je, tunamfuata vipi mtume wa Allahu taala? Vifuatavyo ni vipengele muhimu katika kumfuata mtume:

Unapaswa kufanya toba punde tu baada ya kutenda dhambi. Kutubia dhambi iliyotendwa hadharani hufanyika hadharani na kutubia dhambi iliyofanyika kwa siri hufanyika kwa siri. Toba haipaswi kuwakhirishwa. Kiraaman kaatibiin (malaika wanaoandika vitendo vya mtu) hawaandiki dhambi mara moja. Kama mtu atatubia dhambi haitoandikwa. Itaandikwa ikiwa toba haikufanyika. Ja’far ibn Sinaan (Quddisa sirruh) alisema, ‘Kuwacha kufanya toba juu ya dhambi ni kubaya zaidi kuliko kutenda dhambi’. Na yule ambae hakufanya toba pale pale, anapaswa kufanya hivyo kabla ya kifo chake. Tusipuuze wara’ na taqwa. Taqwa ni kuacha kutenda jambo lililoharamishwa, na wara’ ni kutofanya mambo yanayotiliwa shaka. Inafaa zaidi kuepukana na yaliyoharamishwa kuliko kufanya mambo yaliyoamrishwa. Wakubwa zetu wanasema, ‘waovu na wema hutenda fadhila. Lakini ni siddiiq (wasema kweli) na wema pekee ndio wanaoepukana na madhambi’. Hadhrat Ma’ruuf al-Karkhii alisema, Acha kuwaangalia sana wanawake wasio mahram! Usimuangalie hata kondoo! Kwa mujibu wa hadithi, ‘Wachamungu na wale wanaoipa dunia kisogo ndio

watakaokuwa mbele ya Allahu taala siku ya kufufuliwa kwa fadhila na ubora. Dua ya mchamungu inatakabaliwa haraka na kufuatana na mchamungu ni ibada. Anayezungumza naye hupata baraka kama yule anayetoa sadaka'. Usifanye jambo lolote ambalo moyo wako hutetemeka wakati wa kulifanya. Usifuate matamanio ya nafsi yako! Ishauri nafsi yako juu ya mambo unayotilia shaka! Kwa mujibu wa hadithi, 'Tendo lolote litulizalo na kuifariji nafsi ya mfanyaji ni zuri. Tendo lolote linalosisimua nafsi ni dhambi'. 'Hakika halali iko wazi na haramu iko wazi, na baina yake kuna mambo yasiyodhahiri yaliojificha. Basi epukana na yale yasiyodhahiri (ufanye yale ambayo huyatilii shaka)! Hadithi inadhihirisha kuwa haifai kufanya jambo ambalo linaisisimua nafsi na kutiliwa shaka. Inaruhusiwa kufanya jambo lisilotiliwa shaka. Hadithi nyingine inasema, 'Mambo ambayo Allahu taala ameyahalalisha katika Qurani ni ya halali. Alisamehe yale ambayo hakuyataja katika Qurani. Tukikumbana na jambo la kutilia shaka tunapaswa kuweka mkono wetu juu ya moyo wetu. Ikiwa moyo haupigipigi (hautetemeki), tunapaswa kulifanya. Lakini ukipigapiga, tuliache. Kwa mujibu wa hadithi, 'Weka mkono wako kwenye kifua chako! Moyo utatulia iwapo jambo (unalotaka kufanya) ni halali. Lakini utakapo piga jua kuwa kama (jambo hilo) ni haramu. Ukliitilia shaka jambo lolote basi usilifanye! Usilifanye hata kama watu wenye vyeo katika dini wametoa fatwa.' Mwenye imani hujiepusha na madhambi madogo ili kukwepa kutenda madhambi makubwa.

Tunapaswa kuchukulia ibada zetu na matendo mema (tuliyofanya) kuwa yana walakini. Tunapaswa kufikiria kuwa hatujaweza kutekeleza amri za Allah ipasavyo. Abu Muhammad 'Abdullahi ibn Manaafil (Quddisa sirruh) alisema, 'Allahu taala ameamrisha kutenda aina kadhaa za ibada. Ameamrisha waja wake kuwa na subira, moyo wa ibada, kusali, kufunga, na kuomba kughufiriwa madhambi kabla ya mapambazuko. Kughufiriwa madhambi kumetajwa mwisho. Kwa hio, ni muhimu kwa wanadamu kuchukulia kuwa ibada zao na matendo mema waliyofanya yana kasoro na waombe msamaha ili kughufiriwa madhambi'. Jaafar ibn Sinan (Quddisa sirruh) alisema, 'Kitendo cha wanaofanya ibada kujichukulia kuwa ni wabora kuliko watenda madhambi, ni kibaya zaidi kuliko madhambi yao'. Siku moja, Hadhrat Ali Murteza (Quddisa sirruh) aliacha Itikaafu akatoka msikitini baada ya tarehe ishirini katika mwezi wa Ramadhan. Alipoulizwa kwa nini alitoka nje, alisema, 'Nilipowaona wasoma Qurani wakiisoma Qurani kwa maghani na wanajisifia kwa hilo, niliona nisiendelee kukaa ndani'.

Tunapaswa kufanya kazi ili familia zetu na sisi wenyewe tupate kujikimu maishani kwa njia ya halali. Biashara na kazi za mkono ni muhimu. Wasalaf as-Saalihiin walikuwa wakifanya kazi na kuchuma pesa kwa njia hii. Kuna hadithi nyingi sana zinazoelezea thawabu za kujikimu maishani kwa njia ya halali. Hadhrat Muhammad ibn Salim aliulizwa: 'Tufanye kazi na tuchume mali, au tufanye ibada na kumtegemea Allahu taala?' Alisema, 'Kumtegemea Allahu taala (tawakkul) ilikuwa kawaida yake mtume "swallallahu alaihi wa sallam" na kuchuma mali kwa kufanya kazi ilikuwa sunna yake. Mtafanya kazi na kumtegemea kwa Allahu taala!' Abu Muhammad ibn Manaazil alisema, 'Bora kufanya kazi na kumtegemea Allahu taala kuliko kujitenga kwa ajili ya ibada'.

Lazima tukadirie katika kula. Tusile sana kiasi cha kutufanya tukawa wavivu, wala tusile sana kiasi cha kutuzuia kufanya ibada. Hadhrat Shah an-Naqshaband (Quddisa sirruh), mmojawapo wa mawalii maarufu, alisema, 'Kula vizuri na ufanye kazi vizuri!' Kwa ufupi, kitu chochote kinacho saidia katika kufanya ibada na kutenda mema ni kizuri na kimebarikiwa na vile ambavyo huvipunguza vimeharamishwa. Lazima tuangalie (tupeleleze) na tuwe waangalifu katika nia zetu au jambo lolote zuri tunalofanya. Nia isipokuwa nzuri, tusilifanye.

Tunapaswa kuepukana na kujitenga na watu wasiotii sheria za kiislamu na wale wanaofanya bid'a na madhambi ['Uzla]. Kwa maneno mengine, tusifanye urafiki na watu hao. Kwa mujibu wa Hadithi, 'Hikma imeundwa kwa sehemu kumi, tisa kati yake huunda 'uzla (kujitenga) na moja ni kunjamaa'. Lazima tuingiliane na watu kama hao inapohitajika. Tutumie muda wetu katika kufanya kazi, kufanya dhikri, kutaamali na watu na kufanya ibada. Wakati wa kufurahika furaha ya uhakika na kudumu ni baada ya kifo. [Tusisome vitabu na magazeti yenye madhara, wala kusikiliza redio au kutazama vipindi vya television visivyo na tija wala faida. Vitabu, magazeti, redio na runinga (television) za maadui wa Uislamu zimepania kisirisiri kuuangamiza Uislamu. Wamekuwa wakifanya mipango ya kuwafanya vijana wapinge dini na wakose maadili].

Tunapaswa kumkaribisha kila mtu kwa uso wenye uchangamfu, pasi na kujali ni wazuri au wabaya. [Tusiamshe fitna. Wala tusifanye watu kuwa maadui. Tufuate maneno ya Hafidh Shiraz, 'Waambie watu ukweli na uwakaribishe maadui kwa uso ulio jaa uchangamfu na utumie lugha nzuri na maneno laini']. Tunapaswa kuwasamehe wale wanaoomba msamaha. Tunapaswa kuonyesha tabia nzuri kwa kila mtu. Tusipinge maneno ya mtu yeyote au kuzozana na mtu Tusiongee

ovyo ovyo bali tuongee kwa upole. Sheikh ‘Abdullah Bayal (Quddisa sirruh).

Alisema, ‘Tasawuf haimaanishi rehma, kufunga, au kufanya ibada nyakati za usiku. Haya ni majukumu ya kila mtu kama mja. Tasawuf humaanisha kutomdhuru mtu yeyote.

Yeyote anaeweza kufanya jambo hili hupata lengo (lake). Hadhrat Muhammad ibn Salim aliulizwa jinsi ya kumtofautisha walii na watu wengine. Akasema, ‘Atatofautishwa kwa maneno yake matamu, tabia zake zenye kupendeza na fadhila zake nyingi. Akiongea na mtu habishani na huwasemehe wale wanaoomba msamaha na humhurumia kila mtu’. Abu abdillahi Ahmad al-Makkaari alisema, ‘Futuwwat humaanisha kumtendea fadhila mtu aliyekuudhi, kumpa zawadi mtu usiempenda na kumchangamkia mtu uliyemchoka’.

Tunapaswa kuongea kidogo, kulala kidogo na kucheka kidogo. Kucheka sana hufifiza moyo. Tunapaswa kufanya kazi, lakini ujira wake tuutarajie kutoka kwa Allah peke yake. Tunapaswa kufurahia utekelezaji wa amri zake. Endapo tutamtegemea Allahu taala peke yake, atatukirimu kwa kuturahisishia matakwa na malengo yetu. Kwa mujibu wa hadithi, Allahu taala hutoa matilaba (matakwa au malengo) yote ya mtu anaemtegemea. Huwafanya watu wengine wamsaidie’. Yahya ibn Maadh ar-Raazi aliyefariki mwaka wa 258 H./878 A.D. huko Nishapur) alisema, ‘watu watakupenda kadri unavyompenda Allahu taala. Watu watakuogopa kadri unavyomuogopa Allahu taala. Watu watakusaidia kulingana na kiwango cha ibada yako kwa Allahu taala’. Usikimbilie faida zako binafsi! Abu Muhammad ‘Abdulla ar-Raasibii aliyefariki mwaka wa 367 H./978 A.D. huko Baghdad alisema, ‘Pazia kubwa zaidi lililopo kati ya Allahu taala na mtu ni kujifikiria na kumtegemea mtu asiye na uwezo kama yeye. Tunapaswa kufikiria juu ya kujipendekeza kwa Allahu taala badala ya kujipendekeza kwa watu’.

Tunapaswa kutumia lugha tamu na kudhihirisha uso wenye bashasha kwa wake zetu na watoto wetu. Tunapaswa kukaa nao kadri tunavyoweza ili tuwape haki zao. Tusiwe karibu sana nao kiasi cha kuwafanya wawe mbali na Allahu taala.

Tusitafute ushauri wa wajinga na watu wenye vyeo vya kidini waliopotoka, kuhusu mambo yetu ya dini. Tusikae pamoja na wale wanaopendelea dunia hii. Tunapaswa kufuata sunna katika kila jambo tufanyalo na kuepukana na bid’aa. Tukiwa tumefurahika tusikiuke mipaka ya Kiislamu. Wala tusikate tamaa na msaada wa Allahu taala tukiwa kwenye shida. Tunapaswa kuwa katika hali ile ile wakati wa

vyakula vingi na wakati wa kuadimika kwa chakula. Kwa hakika, tunapaswa kupunguza wasiwasi wakati wa uhaba na kuwa na wasiwasi wakati wa vyakula vingi. Kubadilika kwa mambo kusitubadilishe sisi.

Badala ya kutafuta makosa ya watu wengine, tutafute makosa yetu wenyewe. Tusijichukulie kuwa wabora kuliko waislamu wengine. Tunapaswa kumuenzi kila Muislamu kuliko kujienzi wenyewe. Tunapokutana na Muislamu, tunapaswa kuamini kuwa furaha yetu inaweza kutegemea baraka atakazotuombea.

Tunapaswa kuwa kama watumishi kwa wale ambao tunalazimika kuwasimamia. Kwa mujibu wa hadithi, 'Muislamu anayetenda vitendo vitatu vifuatavyo ana imani kamili: kuitumikia jamii yako, kukaa pamoja na maskini [sio ombaomba] na kula na watumishi'. Katika Qurani mambo haya matatu huchukuliwa kuwa sifa za waumini. Tunapaswa kujifunza tabia za salaf as-salihiin na tujaribu kuiga mienendo yao. Tusiseme jambo baya kuhusu mtu ambaye hayupo. Tunapaswa kumzuia msengenyaji [Ghiiba (kusengenya) ni kusema kitu nyuma ya mgongo wa mtu wakati hayupo mahala hapo kwa namna ambayo ingemuudhi kama angesikia na hata kama tunalosema ni la ukweli]. Kama ni uongo, basi hiyo ni iftirau (kashfa/kumsingizia mtu jambo ambalo hakulifanya). Yote mawili huchukuliwa kuwa madhambi makubwa. Iwe kawaida yetu kuamrisha mema na kukataza mabaya. Muhammad ibn Alyan'a aliulizwa jinsi unavyoweza kuelewa kwamba Allahu taala anakupenda. Akasema, 'Inaeleweka wakati ambapo twaa (kufanya mema) huwa tamu na kutenda madhambi kukawa chungu kwako'. Tusisononeshwe na kuogopa kuwa maskini. Shetani humdanganya mtu kwa kusema kwamba atakuwa maskini na kumshawishi kuzini. Kwa mujibu wa hadithi, 'Mtu anayekuwa na watu wengi katika nyumba yake na chakula kidogo, akaswali sala yake vizuri na akaacha kuwasengenya waislamu, atakuwa pamoja nami siku ya kufufuliwa.

Muislamu mwenye sifa hizo nzuri zilizoandikwa hapo juu anaitwa mtu mwenye mamlaka ya kidini. Tunapaswa kutambua kwamba mtu asiekuwa na sifa hizo, na ambae hazitaki, na hudunisha walio nazo, basi huyo si mtu mwenye mamlaka ya kidini, bali ni adui wa Uislamu na hatupaswi kuamini maneno yake wala maandishi.

Bid'a humaanisha nini? Katika barua ya 54, 165, 186, 255, 260 na 313, mjalada wa kwanza wa kitabu kiitwacho Maktubat, Imam ar-Rabbani Ahmad al-Faruqi "rahmatullahi alaih" alielezea maana ya bid'a na madhara ya kufanya bid'a. Tumetafsiri barua zote 313 katika

mjalada wake wa kwanza kutoka Kifarsi hadi Kituruki, na sehemu yake kwa Kiingereza, na tukazichapisha mwaka wa 1387 (1968). Aidha kuna taarifa kamili kuhusu bid'a katika sehemu ya kwanza ya kitabu cha Kiarabu kiitwacho Hadiiqat an-Nadiyya kilichoandikwa na 'Abd al-Ghanii an Nabuluusii. Na sehemu hii pia ilichapishwa mwaka wa 1399 H. (1979 A.D.) huko Istanbul. Tafsiri ya sehemu ya maandishi yake yamewasilishwa kama ifuatavyo:

Bid'a maana yake ni imani, kitendo au neno lisilowiana na sunna [yaani mafundisho ya kidini ya mtume Muhammad "swallallahu alaihi wa sallam"]. Allahu taala aliwaumba waja wake ili wapate kumuabudu. Ibada maana yake ni kunyenyekea na kujishusha hadhi. Kwa maneno mengine, ni mtu kuonesha unyenyekevu wake kwa muumba wake. Yaani kutotilia maanani uzuri au ubaya unaoshurutishwa na fikra za mtu au nafsi na mila zake, ili kujisalimisha kwa maelekezo ya muumba kuhusu kile ambacho ni kizuri au kibaya, na kuamini na kutii kitabu na mtume alietumwa na muumba. Endapo mtu atatenda kitendo kwa hiyari yake bila kuzingatia yale ambayo muumba wake amemruhusu, basi mtu huyo hatakuwa amedhihirisha unyonge wake kwake na atakuwa hajatimiza masharti ya kuwa Muislamu. Ikiwa kitendo hicho kinahusu imani na ni mojawapo ya mambo ambayo yametangazwa kwa itifaki ya wanazuoni kuamini, imani yake hii ni bid'a inayosababisha kukufuru. Ikiwa kitendo hicho hakihusu imani lakini kinahusu maneno na vitendo vyenye uhusiano na dini, basi hayo yatakuwa ni fisq, dhambi kubwa. Imetangazwa katika hadithi kwamba, 'Yeyote anaezua jambo katika dini yetu lisilokuwemo, basi litakataliwa'. Hadithi hii huonyesha kuwa iwapo imani, neno, tendo au au tabia isiyokuwepo katika Uislamu itazuliwa na iaminike kuwa imo katika dini au kuwa ni ibada, au iwapo kutakuwa na kuongeza au kufuta katika yale yaliyowasilishwa na Uislamu na iwapo imetarajiwa kuwa kufanya hivyo kutaleta thawabu, uzushi au badiliko kama hilo ni bid'a, hivyo wafanyaji hawatakuwa watiifu na sheria za Kiislamu zitakuwa zimekiukwa.

Mambo mapya yanayofanyika sio katika Uislamu lakini katika mila, yaani, yale ambayo mtendaji hatarajii thawabu wakati wa kufanya, si bid'a. kwa mfano, dini yetu haikatai mambo mapya na mabadiliko yanayofanyika katika kula, kunywa, kusafiri na uchukuzi au ujenzi wa nyumba. Kwa hiyo, kulia mezani au kwa kutumia mabakuli tofauti kutumia vijiko au nyuma, kusafiri kwa honda na pikipiki gari au ndege, kutumia aina yoyote ya jengo, nyumba au vifaa vya jikoni na kila namna ya elimu ya kiteknolojia, ala au ujenzi havichukuliwi kama bid'a katika

Uislamu. Inaruhusiwa kuvitumia katika nyanja zenye manufaa. Kwa mfano, inaruhusiwa kutengeneza redio, vipaza sauti, au mashine za kielektroniki na kuvitumia katika mambo yasiyokuwa ya ibada. Matumizi ya vipaza sauti katika mambo ya kidunia huruhusiwa, lakini kuvitumia katika kuadhini, kusoma Qurani au maulidi ni mabadiliko katika ibada. Ili adhana isikike kwa mbali, isifanywe kwa kutumia kipaza sauti, lakini tunapaswa kujenga misikiti katika kila wilaya na kila muadhini anapaswa kuadhini katika kila msikiti.

Siku moja, Anas ibn Malik "radiyallahu anhu" aliulizwa kilichomliza. Akasema, ‘Kati ya ibada nilizojifunza kutoka kwa mtume "swallallahu alaihi wa sallam", ni sala peke yake ndio ilikuwa haijabadilika. Na sasa ninalia kwa sababu naona imeshabadilishwa pia’. Alichokusudia ni kwamba alilia kwa sababu watu wengi wa zama zake hawakutimiza masharti ya sala, wajibu wake, sunna zake, mustahab zake wala hawakuepukana na makruhu zake, mufsid zake na bid’a zake. Hao wasiofanya hayo ni watu ambao hawakutambua hadhi ya mitume, mawalii, au waislamu wachamungu. Waliacha njia yao wakabadili ibada kulingana na mitazamo yao binafsi na matamanio ya nafsi zao. Kwa kuiacha njia ya kheri, walirudia tena kwenye hali ya maangamizi. Sababu ya kulia kwake ni kwamba walibadilisha sala kwa kuiongezea (mambo yasiyokuwemo kabla) na kufuta baadhi (ya mambo yaliyokuwemo). Kwa kufanya hivyo ndio wakiweza kubadilisha sunna, [yaani Uislamu].

Kwa mujibu wa Hadithi, ‘Endapo umma utazua jambo (bid’a) katika dini hii baada ya kifo cha mtume, basi utapoteza sunna inayolingana nazo’. Kwa maneno mengine, wakifanya bid’a ambayo haisababishi ukafiri, watapoteza sunna.

Tunaambiwa katika Hadithi nyingine kwamba, ‘Allahu taala hatompa mwanabid’a fursa ya kufanya toba, mpaka atakapoiacha bid’a yake’. Yaani, iwapo mtu atatengeneza bid’a mwenyewe au afanye ile iliyotengenezwa na mtu mwingine, basi hawezi kufanya toba kwa sababu anaichukulia bid’a hiyo kuwa jambo jema na kwa hiyo, anaifanya akitarajia kwamba atapata thawabu. Na kutokana na ubaya wa bid’a hiyo, ambao unaweza hata kumpelekea kukufuru, hatopata fursa ya kufanya toba juu ya madhambi yake.

Katika Hadithi tukufu, imeelezewa pia kwamba, ‘Allahu taala hatokubali tendo lolote (zuri) la mtu anayezua jambo (anayefanya bid’a) katika dini, mpaka atakapoliacha jambo hilo kwa ajili ya (kumtii) Allahu taala’. Kwa maneno mengine, mtu anayeendelea kufanya

jambo ambalo ni la uzushi (bid'a) katika imani, matendo, maneno au maadili, Allahu taala hatokubali ibada yoyote kati ya ibada zake za aina hiyo hata kama ni sahihi. Ili ibada zake zikubalike, anapaswa kuachana na bid'a kwa kumcha Allahu taala na kutarajia thawabu kutoka kwake au kupata ridhaa yake.

Imeelezewa pia katika Hadithi kwamba, 'Allahu taala hatokubali funga (saum), hija, umra, jihad, kujizuia kufanya madhambi na kutenda haki kwa mtu anayeshikamana na bid'a na atatoka kwenye Uislamu kwa wepesi'. Yaani, ibada yake haitokubaliwa hata kama matendo yake ni sahihi na hatopata thawabu kwa sababu anaendelea kufanya bid'a isiyosababisha ukafiri. Ama akifanya bid'a inayosababisha ukafiri, basi ibada zake anazozifanya hazitakuwa sahihi kwa njia yoyote ile atakazozifanya. Hakuna lolote kati ya matendo yake ya ibada yalio faradhi au sunna yatakayokubaliwa. Kwa vile bid'a hufanywa kwa kufuata matamanio ya nafsi na shetani, anayeshikamana nayo hutoka kwenye Uislamu, kwenye kujisalimisha kwenye maamrisho ya Allahu taala.

Imani ni tendo la moyo. Nguzo tano za Uislamu ni tendo la moyo na ulimi kwa pamoja. Imani inahusiana na moyo. Lakini Uislamu hujumuisha hayo yote: moyo, ulimi na mwili. Imani iliyoko ndani ya moyo na Uislamu ulioko ndani ya moyo hufanana. Kinachomtelekeza mwanabid'a ni Uislamu kwenye ulimi na mwili. Yule anayeendelea kufanya bid'a ni mtu anayetii nafsi yake na shetani. Mtenda madhambi huwa muasi. Yeye haitwi mwanabid'a. Lakini mwanabid'a huwa muasi na mwenye dhambi na huchukulia kwamba bid'a yake ni ibada na hutarajia kupata thawabu kwa hio bid'a yake. Kutenda dhambi nje ya ibada [tafauti na bid'a] hakuzuii matendo ya ibada kukubalika/ kuidhinishwa.

Kwa mujibu wa Hadithi, 'Hakika watakaokuwa hai baada yangu miongoni mwenu (umma), wataona tofauti nyingi. Shikamaneni basi na sunna zangu na sunna za makhalifa wangu waongofu! Epukaneni na uzushi. Kwani kila jambo la uzushi ni bid'a na kila bid'a ni upotofu na kila upotofu humuelekeza mtu kwenye moto wa Jahannam'. Hadithi hii tukufu hudhihirisha kuwa kutakuwepo tofauti kadhaa katika umma huu, kati ya mirengo hiyo tofauti, tunapaswa kufuata ule wa mtume "swallallahu alaihi wa sallam" na makhalifa wake wanne. Sunna maana yake ni matamko yake, matendo yote ya ibada, imani na mienendo, na mambo ambayo mtume aliidhinisha kwa kuyanyamazia alipoona yakitendwa.

Katika Hadithi imeelezwa kwamba, ‘Ufisadi utakapoenea (utakapokithiri) miongoni mwa umma wangu, wale watakaoshikamana na sunna zangu watapewa thawabu za mashahidi mia moja’. Yaani, watu watakapochupa mipaka ya Uislamu kwa kufuata matamanio ya nafsi, bid’a za akili zao, yule atakayefuata sunna za mtume atapewa thawabu za mashahidi mia moja siku ya kiama. Hii ni kwa sababu wakati wa mfarakano na ufisadi, itakuwa vigumu kufuata mafundisho ya Uislamu kama kupambana na makafiri.

Imeelezwa katika Hadithi kwamba, ‘Uislamu ulikuja hali ya kuwa ni mgeni na utarudi ukiwa ni mgeni. Basi wamejivunia wale ambao ni wageni. Watakaoihuwisha sunna yangu iliyochafuliwa na watu wangu’. Yaani, katika kipindi cha machafuko ya Uislamu, watu wengi hawakuuelewa Uislamu na walichukulia kama jambo geni. Hivyo hivyo, katika nyakati zilizopo au zijazo wajuzi wa Uislamu watakuwa wachache. Ili kuhakikisha kuwa wanatimiza jambo hilo, wataamrisha mema na kukataza mabaya. Watakuwa mfano bora kwa watu wengine katika kufuata sunna, yaani Uislamu. Watayaandika mafundisho ya Uislamu kwa usahihi na watafanya jitihada za kusambaza vitabu vyao. Ni watu wachache mno ndio watakaowasikiliza na watakuwa na maadui wengi. Wakati huo, mwenye cheo cha kidini aliye na waungaji mkono wengi atakuwa ndiye mtu anayechanganya maneno matamu lakini ya uongo na yale ambayo ni ya ukweli. Kwani, yule atakayesema ukweli atakuwa na wapinzani (maadui) wengi.

Imebainishwa katika Hadithi tukufu kwamba, ‘Wana wa Isra’ili waligawanyika katika makundi sabini na mbili. Umma wangu utagawanyika katika makundi sabini na tatu. Sabini na mbili kati yao wataungua motoni na kundi moja tu ndilo litakalonusurika. Hao ni wanaonifuata mimi na masahaba zangu’. Kwa maneno mengine, wana wa Isra’il waligawanyika katika makundi sabini na mbili kuhusiana na mambo ya dini. Lakini Waislamu watagawanyika katika makundi sabini na tatu. Yaani, watagawanyika katika makundi mengi. Hakuna kati yao atakayekuwa kafiri, lakini wataungua katika moto wa jahannam kwa muda mrefu. Kundi moja tu ambalo litakuwa na imani sawa litekeleze ibada sawa na yake na masahaba zake, ndilo halitoingia motoni. Ikiwa wanazuoni hao wa Kiislamu wanaofanya ijtihad katika mafundisho ya imani ya mtume "swallallahu alaihi wa sallam" na masahaba watukufu watakiuka imani ambayo ni ya kimsingi katika dini na ambayo inajulikana na wanazuoni walo wengi, basi watakuwa makafiri. Watajulikana kama **mulhidiin**. Ikiwa watakosea katika imani iliyowasilishwa na itifaki ya wengi na ambayo si ya kimsingi,

hawatakuwa makafiri bali wanabid'a katika imani. Wao pia wanajulikana kama **Ahl al-qibla** (watu wa kibla/waislamu). Aidha, katika matumizi ya ijtihad kwenye matendo na ibadaat, wale ambao hawaamini kuwa ibada hizo ni za kimsingi kulingana na makubaliano ya wanazuoni walio wengi, huchukuliwa kuwa makafiri au mulhidiin. Lakini wanazuoni wanaokosea katika ibada ambazo si za kimsingi wala hazikuwasilishwa kwa itifaki huwa wanapata thawabu kama wao ni mujtahidiin. Kama si mujtahidiin basi huchukuliwa kuwa **la madh-habii** (wasiofuata madhehebu). Kwani hairuhusiwi kwa asiekuwa mujtahid kufanya ijtihad, anapaswa kufuata madhehebu ya mujtahid. Katika Hadithi imeelezwa kuwa, 'Mtu anayesema laa-ilaaha illallah, asiitwe kafiri kutokana na kufanya dhambi! Amuitae kafiri atakuwa kafiri mwenyewe'. Mtu ambae hapaswi kuingia motoni kutokana na imani yake sahihi anaweza kuingia motoni kutokana na madhambi aliyotenda. Akiwa mtu salih (mwema, mcha mungu), yaani akitubu au kughufiriwa au kupata maombezi (shafaa'a) kamwe hatoingia motoni. Kwa sababu, mtu anaekanusha imani au kitendo ambacho kimewasililishwa kutokana na makubaliano ya walio wengi na ambacho ni cha msingi, yaani kinachotambulikana hata kwa mjinga, atakuwa kafiri au murtadi, hatoitwa muumini wa 'laa ilaaha illallah' wala mtu wa Qibla, hata kama atasema laa ilaaha illallah, akafanya kila aina ya ibada na kuepukana na kila namna ya madhambi.

**Swali:** Mtume wetu alitangaza kuwa 'Bid'a zote ni upotofu'. Lakini baadhi ya wanazuoni wa kifiqhi walisema kwamba baadhi ya bid'a ni mubahu (zinaruhusiwa), baadhi yake zikawa mustahab huku zingine zikiwa wajib. Je, kauli hizo mbili zinatafsiriwaje?

**Jibu:** Neno bid'a lina maana mbili. Maana ya kwanza ni ya kilugha ambayo ni ya kiujumla. Kwa maana hiyo, kila aina ya uzushi, ima katika mila na desturi au katika ibada ni bid'a. Mila na desturi ni matendo ambayo thawabu hazitarajiwi na ambayo hufanyika kwa manufaa ya kidunia. Lakini ibada hufanyika ili kuchuma thawabu huko akhera. Kileksia, neno bid'a humaanisha kila aina ya uzushi/ ubunifu uliojitokeza katika kipindi cha kwanza, kinachojumuisha enzi za salaf as-salihiin, yaani masahaba watukufu, mataabi'iin na mataabi't-taabi'iin. Mambo yaliyoanzishwa katika enzi zao si bid'a.

Bid'a ni yale mambo yaliyoanzishwa katika kipindi cha Mataabi'iin na Mataabi't-taabiin. Maana ya pili ya neno bid'a ni uzushi katika dini ulioanzishwa baada ya as-sadr ul awwal (enzi ya kwanza). Mabadiliko haya yanaweza kuwa katika imani au ibada. Kubuni ibada mpya au kuongezea jambo au kufuta jambo la ibada ni bid'a katika ibada. Kati

ya bid’a hizo, zile ambazo zilianzishwa bila idhini kimaneno au kimatendo, yaliyo wazi au ya ishara kutoka kwa mwenye dini -yaani idhini ya kutoka kwa mtume Muhammad "swallallahu alaihi wa sallam", zinaitwa bid’at sayyi’a (bid’a mbaya). Hakuna bid’a yoyote kati ya zile zilizomo katika mila na desturi, ambayo ni sayyi’at (mbaya) kwa sababu hazifanyiki kwa ajili ya ibada lakini hufanyika kwa manufaa ya kidunia. Uzushi unaofanyika katika kula, kunywa, kuvaa na ujenzi wa makazi ni bid’a katika mila na desturi. Bid’a zote za kiimani ni bid’a mbaya. Imani ya madhehebu katika ibada si bid’a kwa sababu hutokana na mantiki inayotoka kwenye adillat ashshar’iyya (hoja za kisheria). Si nyongeza kwa matini lakini ni maelezo ya matini. Ikiwa kutoa takbirat al-iftitaah mara kadhaa wakati wa kuanza sala kutakusudiwa kupata thawabu za ziada, basi tendo hilo ni bid’a. Lakini ikiwa kutafanywa kwa kughafilika kwa sababu ya kuona haya, ni dhambi. Ikiwa bid’a zilizofanyika katika ibada ziliruhusiwa na mtume kwa njia dhahiri au kwa ishara, basi zinajulikana kama bid’a hasana (bid’a nzuri), ambazo ni mustahab au wajib. Ni mustahab kujenga minara ya miskiti. Mtu hupata thawabu kwa kuijenga minara hiyo na hapati dhambi kutofanya hivyo. Mnara unaitwa mi’dhana. Mama yake Zaid ibn Thabit "radiyallahu anha" alisema, ‘Nyumba ndefu zaidi karibu na msikiti Masjid an-Nabawi ilikuwa yangu. Mwanzoni, Hadhrat Bilal al-Habashi "radiyallahu anhu" alikuwa akiadhini akiwa kwenye paa la nyumba yangu. Baada ya msikiti wa mtume kujengwa, aliadhini huku akiwa amepanda sehemu ya juu ya msikiti’. Hii inaonyesha kuwa ni sunna kwa waadhini kutoa adhana wakiwa wamepanda mnarani. [Inasikitisha kuona kwamba bid’a ya kuadhini kwa kutumia vipaza sauti imetokomeza sunna hii]. Kujenga shule za kidini na kuandika vitabu vya kidini ni bid’a ambazo ni wajib. Kufanya hivyo humpatia mtu thawabu na ni dhambi kuacha kufanya hivyo. Hupata thawabu vilevile kuwaonya kwa kutoa ushahidi dhidi ya shaka walizo nazo wanabid’a na mulhidiin kwamba ni ukafiri kufanya bid’a hizo.

Bid’a zote zilizotajwa katika hadithi zilizoandikwa hapo juu ni bid’a mbaya zilizoingizwa katika Uislamu. Hazina umuhimu kwa ibada. Bid’a nzuri, zenye manufaa katika ibada na ambazo hufanywa kwa idhini ya mwenye dini si uzushi. Hadithi tukufu inayohimiza kwamba, ‘Shikamana na sunna za makhalifa waongofu’, humaanisha kwamba ‘tupilia mbali mabadiliko ambayo utayafanya katika Uislamu kwa kufuata akili yako na nafsi yako na ushikamane na njia yangu’ na huonyesha kuwa bid’a katika mila na desturi si uzushi. Kwani njia ya mtume "swallallahu alaihi wa sallam" inahusiana na mafundisho ya

kidini. Hakusema chochote kuhusu mila. Alikuja kuwajulisha binadamu mambo yanayohusu dini yao. Hakutumwa kuwaambia lolote kuhusu mambo yao ya kidunia. Kwa sababu, walikuwa wakiijua dunia yao vizuri, ilhali walikuwa hawawezi kufanya makisio kuhusu matlaba na maamrisho ya Allahu taala.

Siku hizi, neno bid’a humaanisha uzushi katika dini. Wanaoshikilia imani ya kiuzushi kama hiyo huitwa mubtadi’ na ahl al-hawaa (wanauzushi na wafuata matamanio ya nafsi). Kwani hawafuati Uislamu, lakini wanafuata nafsi zao. Madhehebu ya kiuzushi sabini na mbili yako kwenye kundi hili. Imani za baadhi yao husababisha ukafiri. Wale ambao hawaamini kufufuka baada ya kufa, wakakana sifa za Allahu taala, au matabaka ya viumbe ni ya milele, huangukia kwenye kundi hili pia. Imani kama hizo, zinazosababisha ukafiri, huitwa ilhad. Wale wanaoshikilia imani kama hiyo wanaitwa mulhidiin. Imani haisababishi ukafiri iwapo mwenye kuishikilia aliipata kutokana na kuifasiri kimakosa aya au hadithi ambayo maana yake haikuwa wazi na kwa hiyo, ikafafanuliwa kwa kuchagua maana inayofaa zaidi kati ya maana kadhaa wa kadhaa. Wale wasioamini adhabu ya kaburini au wasioamini miiraji wako hivyo hivyo. Lakini bid’a hizi zisizosababisha ukafiri, ni zenye kuleta hatari zaidi kuliko madhambi makubwa kama vile kuua muumini kwa udhalimu na kuzini. Hawawi makafiri kwa sababu wanapata imani zao za uongo kwa makisio kutoka kwenye Qurani na Hadithi. Leo hii, watu wengi hawaamini mambo haya ya ukweli si kutokana na (ta’wil) tafsiri potofu lakini kwa kusema kwamba hawaridhiki na mantiki na sayansi. Watu wa namna hiyo wasiojenga imani zao juu ya msingi wa Uislamu na badala yake wanazingatia mantiki na sayansi huwa murtadi. Mulhidiin ambao imani zao husababisha ukafiri hujidhani kwamba ni Waislamu, wakatenda vitendo vya ibada na wakaepuka madhambi, lakini hakuna kitendo chochote kati ya vitendo hivyo ambacho ni hafifu.

Bid’a sayyi’a katika ibada si mbaya sana kama bid’a katika imani, ingawa nazo hazikubaliki na ni uzushi. Inafaa mtu aepukane nazo zaidi kuliko kuepukana na utendaji maovu. Hususani, ikiwa bid’a kwenye ibada inasababisha kupuuza sunnat muakkada, bid’a huwa yenye kuchuma madhambi zaidi.

Imani ambayo ni kinyume na bid’a katika dini inaitwa Ahl as-Sunna wal-Jamaa’a. Kinyume cha bid’a katika ibada ni sunnat alhudaa. Ile iliotajwa mwanzo huwakilisha imani ya mtume wa Allahu taala "swallallahu alaihi wa sallam", na iliotajwa mwisho ni ibada alizokuwa akizifanya mtume siku zote lakini akaziacha wakati mwingine na

ambazo huwaambia wengine wasiziache. Zile ambazo aliwaambia watu wasiziache zinajulikana kama wajib. Si dhambi kuacha sunnat ul-hudaa pasina udhuru. Yule anayeziacha daima basi atafedheheka siku ya kufufuliwa. Mfano wa vitendo hivyo ni, kuadhini, kukimu, kusali katika jamaa na sunna za sala tano za kila siku. Hata hivyo, kama wakazi wote wa eneo fulani wataviacha (vitendo hivyo), itabidi wapigwe vita.

Kufanya bid'a katika mila na desturi si tendo la uasi lakini kutozifanya ni tendo la wara' na bora. Kujenga majumba marefu zaidi kuliko invyohitajika, kula shibe ya mtu, kunywa kahawa na majani chai na kuvuta sigara ni bid'a katika mila. Hatuwezi kusema kwamba vitendo hivyo ni haramu au makruhu. Maamrisho na makatazo ya Sultani yanayoendana na maamrisho na makatazo ya Allahu taala ni hafifu. Kutii amri anazotoa kulingana na matamanio ya nafsi yake na akili yake si wajibu ingawa hairuhusiwi kuvunja amri zake. Bali ni wajibu kumtii sultani dhalimu kusalimika kutokana na dhulma na mateso yake. Kwani hairuhusiwi kujiweka hatarini. Ulul amr ambaye Qurani inaamrisha kwamba atiiwe ni sultan, kiongozi, au hakimu Muislamu. Ni wajibu kutimiza na kutii haki na amri zao zilizo sawa. Kinyume cha bid'a katika vitendo ni sunnat az-zaaida ambazo huhusisha vitendo vya mtume vya kawaida. Mfano wa vitendo hivyo ni mustahab kama vile, mitindo ya nguo zake, kuanza na upande wa kulia wakati anapovaa nguo, kula, kunywa, kutoa na kupokea kitu kwa mkono wake wa kulia, kufanya istinjaa kwa mkono wa kushoto baada ya kujisaidia, na kuingia chooni ukianza na mguu wa kushoto. [Kama inavyobainika, mabadiliko yanayojitokeza katika mavazi ya wanaume na wanawake, kuvaa nguo kama wakosefu ni desturi za kibid'a. Nguo za wanawake ambazo ni kubwa kiasi cha kufunika mwili mzima isipokuwa mikono na nyuso zao si bid'a katika dini. Nao si wakosefu. Wanapaswa kufuata desturi za nchi zao katika matumizi ya nguo kama hizo. Kutumia nguo zinazokiuka desturi zinaweza kusababisha ukosefu wa heshima na fitna mambo ambayo ni haramu].

Kama inavyobainika katika yale tuliyoelezwa mpaka sasa, bid'a kwa ujumla, katika maana yake ya kileksia, ni za aina mbili: bid'a katika mila na desturi na bid'a katika dini.

Dhana hiyo ikitumika peke yake, huwa inamaanisha bid'a katika dini. Bid'a katika dini huhusu imani na ibada. Bid'a zote zinazohusiana na imani ni sayyi'a (mbaya). Kuna aina mbili za bid'a katika ibada: sayyi'a na hasan (mbaya na nzuri). Bid'a sayyi'a ni bid'a zinazojikita katika imani lakini hazimpelekei mtu kukufuru na zile za ibada

haziuhudumii Uislamu. Bid'a iliyojikita katika imani ikisababisha ukafiri, itajulikana kama ilhaad.

Bid'a hasana ni uzushi unaohudumia Uislamu. Bid'a hizi ni za aina mbili mustahab na wajib. Kujenga mnara wa msikiti ni bid'a hassan ambayo ni mustahab, kwani ni sunna kwa muadhini kuadhini akiwa amepanda sehemu ya juu. Mnara huhudumia sunna hii. Si sunna kuadhini kwa sauti kubwa sana kuliko sauti asilia ya mwanamume.

Allahu taala ameshatangaza kuwa dini imekamilika. Vitendo vya uzushi ambavyo ni hasana huruhusiwa, na hata kuamrishwa, kwenye sheria ya mtume "swallallahu alaihi wa sallam".

**Swali**: Kwa nini masahaba watukufu, Taabi'iin na Taabi'ttaabiin hawakufanya bid'a hasana ambayo ni mustahab na wajib?

**Jibu:** Hawakuwa na haja ya baadhi yake. Kwa mfano, hawakujenga misikiti wala hawakuwa na uhitaji wa kuandika vitabu. Kwani kulikuwepo wanazuoni na mujtahid wengi. Ilkuwa rahisi kwa kila mtu kuuliza na kujifunza. Zaidi ya hayo, hawakuwa na pesa nyingi wala mali ya kujengea majumba makubwa na minara. Lakini sababu iliyo muhimu zaidi ni kwamba walitekeleza majukumu yenye umuhimu mkubwa sana, ambayo hayakuwaachia muda wa kufanya mambo hayo. Mchana na usiku walipambana na makafiri, na madola na madikteta waliozuia kuenea kwa Uislamu. Walitoa fedha zao na mali yao yote kwa ajili ya jihadi hizo. Walifanikiwa katika kunusuru mamilioni ya watu kutoka kwenye makucha ya nchi dhalimu, kwa kutwaa nchi na miji mbalimbali na wakawasilimisha na kuwawezesha kupata furaha kubwa zaidi duniani na akhera. Waliwasilisha nidhamu na maadili ya kiislamu kwa waja wa Allahu taala. Hawakuwa na muda wa kufanya mambo mengine.

Mtume wa Allahu taala "swallallahu alaihi wa sallam" alisema, **'Yeyote anayefanya sunna hasana (sunna nzuri), atapata ujira wake na ujira wa yule anayeitekeleza pasi na kuwa na upungufu wowote katika ujira wake. Na yeyote anayefanya sunna sayyi'a (sunna mbaya), atapata adhabu yake na adhabu ya yule anayeitekeleza pasi na kuwa na upungufu wowote katika adhabu yake'**. Bid'a hasana zote zimegubizwa katika sunna hasana iliyotajwa katika hadithi hiyo tukufu. Ili astahiki kupata ujira au adhabu ya wale wanaotekeleza sunna mpya aliyoianzisha mpaka siku ya kiama hutegemea iwapo alikusudia kwamba watu wengine waitekeleze pia. Hivyo hivyo, ikiwa Imam wa sala ya jamaa hakunuwia kuwa imam wa sala ya jamaa, basi atapata

thawabu za kusali peke yake- sio zile za mara ishirini na saba zaidi. Kwani ili apate thawabu za jamaa ilikuwa anuwie kuwa imam.

Madhara ya kufanya bid'a sayyi'a ni makubwa zaidi kuliko madhara ya kuacha sunna na hata wajibu. Kwa maneno mengine, pale ambapo kuna shaka kuhusu iwapo jambo fulani ni sunna au bid'a, ni lazima kuliacha.

**Swali:** Dini imekamilishwa na Qurani na Sunna. Ibada zisizoruhusiwa na vitu hivyo viwili ni bid'a. Sasa, inafaaje kusema kwamba adillat ash-shar'iyya (hoja za kisheria/ vyanzo vya sheria) ni vinne?

**Jibu:** Wanazuoni wa ahlusunna walisema kwamba adilla asshar'iyya ni nne: Kitabu (Qurani), Sunna, Qiyaas na Ijmaaul umma. Kwa vile zile mbili za mwisho hutokana na mbili za mwanzo, hivyo basi, kimsingi ziko mbili: Kitab na Sunna. Sheria iliyowekwa kwa Ijmaa ni kwamba kwa itifaki, ijmaa inapaswa kujengwa juu ya msingi wa ushahidi, hati inayotokana na Kitab au Sunna. Aidha, Qiyaas inaweza kutumika kama ushahidi wa kufaa kwa ijmaa. Mfano ni ijmaa iliyotumika kumteua Abu Bakr as-Siddiq "radiyallahu anhu" kuwa khalifa. Hadithi tukufu iliyopokelewa na mtu mmoja pia inaweza kutumika kama ushahidi. Kwani uandikaji wa hati kwa ijmaa hauhitaji ushahidi wake kuwa wa uhakika. Ni hati kwa sababu ni ijmaa. Kama ingeshurutishwa kwamba ushahidi, uwe wa yakini basi ijmaa isingefaa, ushahidi ungekuwa hati hiyo. Kuhusu Qiyaas, ushahidi ama kaida kutoka kwenye Kitabu au sunna ni muhimu. Hii ni kwa sababu qiyaas hufichua lililojificha, katika Kitab na sunna. Haiongezei sheria juu yake. Yaani haibuni sheria bali huzidhihirisha. Hufafanua sheria ya kiujumla kwa furuu' (matawi ya taaluma ambayo inapaswa sio tu kuyaamini lakini pia kuyazingatia katika utendaji). Ijmaa inaweza kuisaidia Qiyaas kama chanzo chake. Sunna ni ufasiri na maelezo ya kitabu cha Allahu taala.

Leo hii, baadhi ya mashekhe wa uongo, watu wadanganyifu wa tasawuf, wakilaumiwa kutokana na tabia zao ambazo ni kinyume na mafundisho ya Kiislamu, wanasema, 'Hivi ni haramu kwa elimu iliyo dhahiri (wazi). Sisi tuna ilm al-baatin (elimu ya ndani). Kwa hiyo, ni halali kwetu'. Kusema hivyo ni ukafiri. Mtu anayesema hivyo au anayeidhinisha kauli kama hizo ni kafiri. Kufafanua mambo au kuyasema bila kujua maana yake ni jambo lisilosamehewa. Mazindiki hawa wanasema, 'Nyinyi mnapata elimu kutoka kwenye vitabu. Lakini sisi tunaipata kutoka kwa mwenyewe, yaani moja kwa moja kutoka kwa Muhammad "swallallahu alaihi wa sallam". Tusiporidhika nalo,

tunauliza na kujifunza kutoka kwa Allahu v. Hatuhitaji kusoma vitabu au kujifunza kutoka kwa waalimu. Ili kufika kwa Allahu taala inafaa kuacha elimu iliyo dhahiri na kutojifunza Uislamu. Kama njia yetu ingekuwa ya uongo, tungefikiaje miujiza ya hali ya juu kama hiyo au kuona nuru na roho za mitume?

Tunapofanya kitu chenye dhambi, tunaarifiwa kwenye ndoto. Katika ndoto zetu Allahu taala huturuhusu kufanya kitendo mnachokichukulia kuwa haramu na hali tunajua kwamba ni halali kwetu'. Maneno kama hayo, yanayolenga kuuhujumu Uislamu, ni ya ilhad. Yaani hukusudiwa kubadilisha maana za Qurani na Sunna zilizo wazi. Huo ni udhalaala (upotofu). Haifai kuziamini kauli potofu kama hizo. Hata kutia shaka kwamba labda si kauli za uongo ni ukafiri. Yeyote anayesema au kuamini hivyo ni **zindiiq**. Hupaswi kumwita mtu **zindiiq** kwa kusikia kutoka kwa mtu mwingine tu kwamba yuko hivyo. Huwezi hitimisha hivyo mpaka ieleweke wazi wazi kutokana na ushahidi wa watu wawili waadilifu. **Zindiiq** maana yake ni **dahrii**, yule ambaye huabudu maada na nguvu za asili na hamuamini Allahu taala na siku ya kiama.

Sheria za Kiislamu haziwezi kusomwa kwa ilhamu. Ilhamu waliopewa mawalii haiwezi kuwa ushahidi. Ilhamu maana yake ni elimu inayokuja kwenye moyo wa mtu kutoka kwa Allahu taala. Ilhamu za mawalii ni za kweli. Ukweli wake huhukumiwa na uwiano wake na mafundisho ya kiislamu. Lakini kuwa walii kunahitaji kujifunza na kutii mafundisho ya Uislamu. Aya inayoelezea kuwa Allahu taala huwapa wachamungu elimu inathibitisha jambo hili. Ilhamu haiji kwenye moyo wa mtu ambae hashikamani na sunna au asiyeepukana na bid'a. Matamko yake ni mambo ya uasi yanayotokana na nafsi na shetani. Kauli zetu hizi hazikinzani na mazungumzo baina ya nabii Musa na Khidr "alaihis-salaam", kwa sababu si za umma uliotangulia. Hakuamrishwa kumfuata. Hata hivyo, Muhammad "swallallahu alaihi wa sallam" ni mtume kwa watu na majini wote duniani kote mpaka siku ya kiama. Ilm al-ladunnii na ilham hupewa wale ambao hujirekebisha na wakamfuata Muhammad "swallallahu alaihi wa sallam". Waliojaaliwa neema hii huielewa vyema Qurani na Sunna. Mafundisho ya kiislamu hayawezi kueleweka kwa ndoto vile vile. Ndoto isiyowiana na Uislamu huhukumiwa kuwa ya kishetani.

Al-Junaid al-Baghdadi (aliyefariki mwaka wa 298H/910 A.D. mjini Baghdad), mmoja wapo wa mawalii mashuhuri alisema, 'Njia pekee ya kumuongoza mtu ni ile ya kupata ridhaa za Allahu taala na kumfuata Muhammad "swallallahu alaihi wa sallam". Alisema tena, 'Asiyetii

Qurani au Hadithi hawezi kuwa kiongozi'. Wasiokuwa mujtahid hawawezi kuielewa Qurani au Hadithi. Wanazuoni wale ambao waliasisi makundi sabini na mbili ya uasi hawakielewi kitabu na sunna kwa sababu wao si mujtahid. Walipotosha mamilioni ya Waislamu.

Ili kuwa mtiifu kwa Qurani na hadithi, inafaa kufuata mojawapo ya madhehebu manne. Ndiyo, mtu asiyejua kusoma na kuandika anaweza kuwa 'aarif (mjuzi), lakini hawezi kuwaongoza wengine. Ili kuwa kiongozi, inafaa ujifunze sheria za Qurani na sunna kutoka kwa mwalimu [au kwenye vitabu vya fiqh vya moja wapo ya madhehebu manne], kwa sababu njia ya salaf assalihiin na warithi wao ni njia ya Qurani na sunna.

Sirrii as-Saqatii (alieyefariki mwaka251 H./865 A.D. mjini Baghdad), mmoja wapo wa mawalii maarufu, mwanafunzi wa Ma'ruuf al-Karkhi na mjomba na mwalimu wa al-Junaid al-Baghdadi, alisema, 'Tasawuf ina maana tatu: Kuwa na waraa, kutotamka maneno yoyote yasiyoendana na Qurani na sunna na kutofanya haram unapokuwa na karaamaat. Waraa maana yake ni kuepukana na matendo yanayotiliwa shaka. Imam al Ghazali (aliyefariki mwaka wa 505 H./1111 A.D., mjini Tus/Mashhad, Iran) aliandika katika kitabu chake **Mishkaat al-anwaar**, kwamba, 'Moyo ni nyumba ya malaika'. Tabia mbaya kama vile, ukali, tamaa, wivu na kiburi ni kama mbwa mwitu. Malaika hawaingii mahali ambapo kuna mbwa. Imetajwa katika Hadithi kwamba, 'Malaika hawaingii ndani ya nyumba ambamo kuna mbwa na picha'. Sisemi kwamba neno nyumba katika hadithi hii ni moyo wala kwamba neno mbwa maana yake ni tabia mbaya. Naamini maana yake iliyo wazi na pia maana za hapo juu. Haya maneno yangu hutofautisha kati ya Ahl as-Sunna wal Jamaa'a na kundi la kibid'a liitwalo Baatiniyya. Baatini hupuuza maana dhahiri na kuibua maana kinzani au maana isiyo fahamika. Ikiwa maana dhahiri ya aya hukinzana na maana dhahiri za aya nyengine, basi maana yake dhahiri lazima itupiliwe mbali na inapaswa kuzingatia ta'wiil, yaani, maana inayofaa zaidi lazima ielezewe. Wale wanaosisitiza maana dhahiri wakati ta'wili inapohitajika wanaitwa Hashwii au mujasima kwa umaarufu ni mawahabi. Kwa sababu hiyo, imesemekana kwamba Qurani ina maana dhahiri na maana ya ndani.

Wale ambao daima wanatoa maana dhahiri hujulikana kama Hashwi. Na wale wanaotoa maana zisizo za kawaida huitwa Batinii. Wale wanaotoa maana zote mbili kama inavyohitajika hua waislamu kamili. Ni gwiji katika matawi ya kielimu ya Batin na dhahir ndiye anayeweza kuelewa ikiwa kauli ya mwanatasawuf huwiana na Uislamu

au la. Wale ambao hawana ujuzi wa maana za maneno yanayotumika na wanazuoni wa tasawuf hawawezi kuzielewa. Watu kama hao kama ibn Taimiyya na Muhammad ibn Abdulwahhab, ambao wako mbali na ukamilifu, wanafikiria kwamba kauli ya Bayazid al-Bistaami, isemayo kwamba, 'Subhaanii maa a'dhama sha'nii', haiwiani na Uislamu. Muhyiddin ibn al-Arabi alitoa ufafanuzi kamili kwamba maana ya kauli hiyo ilikuwa kamaal-I tanziih. Mtu asiyetii sheria za Kiislamu anaweza kufanya maajabu. Haya hayaitwi "karaamaat" bali ni "istidraaj". Bayazid al-Bistaami alimuona mtu aliyejulikana kama walii akitema mate akiyaelekeza upande wa kibla akasema, "Bwana huyu amepuuza moja wapo ya tabia njema za mtume wa Allahu taala "swallallahu alaihi wa sallam". Kwa hiyo, hawezi kuwa walii".

Bayazid al-Bistaami alisema, "Hata kama mtu atadhihirisha karaamaat, kama vile kutembea juu ya maji, kwenda kwenye sehemu za mbali katika muda mfupi na kuruka angani, usimchukulie kuwa ni walii mpaka awe mwenye kutii Uislamu!" kwani kutii Uislamu, ni sharti kufuata mojawapo ya madhehebu ya haki. Yametangazwa kwa itifaki kuwa hairuhusiwi kwa wasio kuwa mujtahid kuwafuata masahaba watukufu. [Kwa sababu madhehebu yao hayajulikani]. Ijtihad itatumika hadi mwisho wa dunia. [Hata hivyo, ni wanazuoni wachache ndio wanaotimiza sharti ya kuwa na uwezo wa kutumia ijtihad. Aidha, hakuna haja ya wao kutumia ijtihad mpya. Suluhisho kwa kila jambo litakalojitokeza hadi mwisho wa dunia ipo katika mojawapo ya madhehebu ya haki]. Ibada aipendayo Allahu taala zaidi ni kutenda faradhi. Ibada za sunna zenye thamani ni zile zinazoenda sambamba na fardhi zilizomo ndani ya Qur' an na sunna. Muhammad ibn Fadhl al-Babalkhi (aliyefariki mwaka wa 319 H./931 A.D.) alisema, "Vipengele vinne ambavyo huifanya nuru iondoke kwenye nyoyo na nyoyo ziwe na giza ni mtu kutotumia elimu yake kwenye utendaji, kutenda bila ujuzi, kutojifunza yale ambayo mtu hayajui na kuzuiwa watu wengine kusoma". Watu wengine husoma ili wajulikane kuwa wasomi na kupata mali na vyeo. Hutumia fursa ya kuwa watu wenye vyeo vya kidini kama njia ya kujikimu kwa ajili ya siasa. Hawasomi ili waweze kutenda amali njema. Watu wa dini ni lazima wafuate kitabu na sunna [lakini hawa sivyo walivyo]. Hawa huyafuata mafundisho kama wanavyoyafuata wajinga. Hutenda madhambi makubwa wakidai kwamba Allahu taala ni mwingi wa rehma na hupenda kurehemu. Hutenda matendo kulingana na akili zao na matakwa yao. Bali pia wanataka watu wengine wafanye kama wao. Huwalaumu Waislamu wa kweli kwa kutowafuata. Zaidi ya hayo, wanadhani kwamba wako

kwenye njia ya kweli na kwamba watapata wa kuwaokoa na kuwatetea siku ya qiyamah. Hawasomi vitabu vya kweli vilivyoandikwa kutokana na vitabu vya wanazuoni wa Ahl as-Sunna wala hawawaruhusu watoto wao kuvisoma. Tamaa zao ni mbovu na maneno yao ni yenye udanganyifu na uongo. Kila siku wanajitokeza katika sura tofauti. Huonyesha uso wenye bashasha kwa watu, lakini huwasengenya wakiwapa kisogo. Huzuia vitabu vya kweli ambavyo havijachafuliwa na bid'a kusomwa. [Wanasema, 'msisome vitabu hivi. Vina madhara']. Huwatishatisha wale wanaochapisha vitabu na kuvisoma. Huvisifu vitabu vyenye madhara vya "La madhhabi" kwa matangazo yenye udanganyifu. Huyatusi mafundisho ya Uislamu. Wanayoandika kwa kutoona mbali huwasilishwa kwa vizazi vichanga kwa jina la elimu na sayansi. Kama inavyoeleweka katika yale yalioandikwa hadi sasa, wanazuoni wote na wanatasawuf walishikamana na Uislamu jambo ambalo hatimaye liliwafikisha kwenye viwango vya juu. Inafaa ieleweke kuwa wanaowasengenya ni wajinga katika mambo yanayohusu Uislamu. Tusiamini maneno ya uongo ya watu wajinga kama hao. Wao ni wezi wa imani. Wao ni laa-madh-habi au mazindiiqi wanaoweka vizuizi kwenye njia ya kheri.

Asemaye kwamba haamini adhabu za kaburi huwa kafiri, kauli yake hudhihirisha kuwa hauheshimu Uislamu.

Wale wanaojikita katika kundi la Qadariyya, waitwao pia Mu'tazila, ni wapotofu kwa sababu wanasema kwamba "Allahu taala haumbi maovu wala madhambi. Mwanaadamu huumba dhambi lake mwenyewe".

Wale wanaojikita kwenye dhehebu la Baatiniyya ni wapotofu kwa sababu wanaamini kuwa roho za marehemu huingia katika miili ya watu wengine na kwamba mwanaadamu hurejea katika dunia baada ya kifo, kwamba roho ya Allahu taala imeingia katika (miili ya) maimamu kumi na wawili, kwamba si muhimu kuutii Uislamu mpaka wakati maimamu kumi na wawili watakapozaliwa upya katika miili ya viumbe wengine (roho zao zitakapoingia katika miili mipya) na kwamba Jibril "alaihis-salaam" alikuwa ameamrishwa kumletea Ali ("radiyallahu anhu") wahyi, lakini alikosea na kuuleta kwa Muhammad "swallallahu alaihi wa sallam".

Wakhaariji wanaowaita waislamu wote "makafiri" pasi na kutegemea ta'wiil au wale wanaowashutumu Ali, Uthman, Talha, Zubair na 'Aisha ('radiyallahu anhum) kuwa wamekufuru ni wapotofu.

Wale walio katika dhehebu la Najariyya na Mu’tazila ni wapotofu kwa sababu hawaamini sifa za Allahu taala.

Jabriyya ni wapotofu kwa sababu wanasema kwamba mwanaadamu hawezi kufanya lolote, kwamba Allah huumba kila kitu pasina kujali iwapo mwanaadamu amekiomba au la na kwamba kwa sababu hii wale wanaotenda madhambi wana udhuru.

Baadhi ya watu wa dhehebu la Mu’tazila wamekuwa wapotofu kwa sababu wanasema kwamba Allahu taala haonekani na kitu chochote na hataonekana peponi.

Qadariyya wamekuwa wapotofu kwa sababu wanakana sifa ya Allahu taala ya “Ujuzi” na wanasema kwamba Allahu taala hajui lolote kabla ya kutokea.

Miongoni mwa watu wanaofuata dhehebu la Murji’a, wanaosema kwamba Allahu taala atawasamehe baadhi ya makafiri na atawaadhibu milele baadhi ya waumini kama apendavyo, wale wanaosema kwamba ibada zao zitakubaliwa bila shaka na madhambi yao yatasamehewa bila shaka, na wale wasemao kwamba faradhi zote ni ibada za sunna, na kwamba si dhambi kutozifanya, wamekufuru.

Khaariji huangukia katika dhehebu la kibid’a kwa sababu wanasema kwamba vitendo na ibada vimegubika katika imani na anayeacha faradhi huwa kafiri, kwamba atendae dhambi kubwa hupoteza imani yake, na kwamba imani yake itarejea pindi atakapoacha kutenda madhambi.

Kufanya mas-h kufuta kwenye miguu mitupu badala ya mas-h kwenye khufu mbili si kitendo cha ukafiri bali ni bid’a. Sala inayosaliwa nyuma ya imam ambae amefanya mas-h hiyo ya miguuni haisihi. Hairuhusiwi kufanya urafiki na wanabid’a. Kwa mujibu wa hadithi, “Ikiwa mtu ataepukana na mwanabid’a, Allahu taala ataujaza moyo wake amani na imani. Ikiwa mtu ataacha kuwaenzi wanabid’a, Allahu taala atamkinga kutokana na khofu ya siku ya kufufuliwa”.

Jukumu la kwanza kwa Muislamu ni kujifunza imani ya Ahl as-Sunna kwa usahihi na kufanya jitihada kuhakikisha kuwa familia na marafiki zake hujifunza pia. Anapaswa kumuomba Allahu taala kumjaalia miongoni mwa wanaoshikamana na imani ya dini ya kiislam katika uhai wao. Anapaswa kujitahadharisha sana ili asije akadanganywa na watu na majini yenye fikra za kishetani, na marafiki wabaya au maandishi yenye upotofu.

Imeelezwa katika hadithi tukufu kwamba, ‘Karne bora ni karne yangu. Kisha ni wale wanaowafuatia. Kisha wale wanaowafuatia.

Baada ya hawa uongo utaenea”. Hadithi hii inaonesha kuwa uongo ulianza kujitokeza katika maneno, tabia na vitendo mwishoni mwa karne ya tatu ya majio ya Uislamu. Watu walikuwa hawaaminiki tena kwani bid’a zilikuwa zimekithiri miongoni mwao. Waliandama mkondo au mafundisho tofauti na yale ya Salaf as-Saalihiin. Wanatasawuf maarufu na maimamu wa fiqh walilingania njia ya Salaf as-Saalihiin.

Asiyeamini hadithi iliyopokelewa na mtu mmoja hawi kafiri bali ni mwanabid’a. Lakini Yule asemaye kwamba Abu Bakr hakuwa sahaba huwa kafiri kwa sababu kwa kufanya hivyo amekana aya tukufu”. Kwa mujibu wa kitabu cha fatwa kiitwacho Zaahiriyya, ‘Ni kweli kwamba mtu asiyeamini ukhalifa wa Abu Bakr au Umar al-Faaruuq "radiyallahu anhuma" hua kafiri kwa uteuzi wao kwa sababu makhalifa ni rehma iliyowasilishwa kama Ijmaa’ (itifaki ya umma)”. [Kwa mujibu wa Ahl as-Sunna, Ijmaa’ (itifaki) ni uthibitisho wa hati. Anayekana uthibitisho huu huwa kafiri. Kwa vile ijmaa’ si uthibitisho kwa khawaarji, washi’a na mawahabi, walisema kwamba yeyote anayekana jambo lililoripotiwa kupitia Ijmaa hatokuwa kafiri].

Ibn Abidin, akiizungumzia murtadi, katika sura ya tatu, katika kitabu kiitwacho Radd-al mukhtaar, aliandika: “Wananchi wasio Waislamu, waishio katika Dar al Islam hujulikana kama Dhimmiyyiin. Hairuhusiwi kuchukuwa mali, kuua au kushusha hadhi ya dhimmi au ile ya makafiri wanaokuja katika nchi kwa ajili ya biashara au utalii. Wana uhuru sawa na ule waliopewa waislamu. Ama Mulhid, hali ni tofauti. Mulhid wanaowadanganya waislamu wanatakiwa kuomba msamaha. Wakikataa wote huuliwa kwa amri ya kiongozi wa dola. Wakitubu, toba yao hukubalika. Wanabid’a ambao bid’a yao haisababishi ukafiri hupewa nasaha. Wakikataa wanaadhibiwa na dola kwa ta’ziir. Kama kuna haja, wanalazimishwa kufanya toba kwa kuwaweka kwenye jela au kuwachapa viboko. Ikiwa kiongozi wao anayethubutu kuwadanganya waislamu, hakufanya toba baada ya kutiwa mbaroni na kuchapwa viboko, inaruhusiwa kwa dola kumuua. Ingawa yule anayewapelekea waislamu kuwacha dini ya kiislam na kutokufuata njia sahihi na kuwa waasi wa laa madh-habi na kwa kufanya hivyo, akajaribu kueneza bid’a hawi kafiri, inaruhusiwa kwa kiongozi wa dola kumuua ili kuwahami watu wasije wakapoteza amani na umoja wao.

## UWAHABI NA KUKATALIWA KWAKE NA AHL AS-SUNNA

Ingawa wanasema kwamba wao ni Waislamu, mawahabi ambao pia wanaitwa Wanajdi, ni mojawapo ya makundi yaliyojitenga na Ahl as-Sunna.

Ahmad Cevdet Pasha, aliekuwa afisa wa jeshi la majini chini ya makamu wa mkuu wa jeshi la majini katika enzi ya Sultan wa dola la Wauthumani wa thelathini na nne Abdul Hamid Khan II aliyetawala miaka ya 1258-1336H/1842-1918 na ambaye amezikwa kwenye makaburi ya Sultan Mahmud, huko Istanbul, rahmatullahi alaihim, kila mmoja wao aliandika kitabu cha historia ambapo waliuelezea Uwahabi kikamilifu. Yafuatayo ndiyo yaliyonukuliwa kutoka kwenye kitabu cha Sabri, aliyetafsiri maalumati kutoka kwenye kitabu cha Ahmad Zayni Dahlan kinachoitwa **"Fitnat al-Wahhabiyya"**. [Alifariki mwaka wa 1308H/1890 A.D.].

Uwahabi uliasisiwa na Muhammad ibn Abdulwahhab. Alizaliwa Huraimila huko Najd mwaka wa 1111H/1699 A.D., akafariki mwaka wa 1206H/1791. Hapo awali, alikuwa Basra, Baghdad, Iran, India na Damaski kwa madhumuni ya matembezi na kufanya biashara. Alikuwa Basra alipouponyoka mtego wa Hempher, aliyekuwa mmojawapo wa makachero wa Uingereza na aliyetumika kama chombo katika mipango ya Uingereza ya kuuangamiza Uislamu. Alichapisha mambo ya upuuzi yaliyoandaliwa na kachero huyo kwa jina la Uwahabi. Kitabu chetu kiitwacho **Confessions of A British Spy** hutoa taarifa kamili kuhusu uanzilishi wa Uwahabi. Huko alipata vitabu vilivyoandikwa na Ahmad Ibn Taimiyya wa huko Harraan (aliyeishi katika miaka ya 661-728H/1263-1328 A.D., akafia huko Damaski), ambavyo mambo yaliyomo hayakuwiana na Ahl as-Sunna, akavisoma. Kwa vile alikuwa mtu mjanja, alijulikana sana kama Ash-Shaikh an-Najdi. Kitabu chake kiitwacho **Kitab at-tawhiid**, alichoandaa kwa kushirikiana na kachero wa Uingereza, kilifasiriwa na mjukuu wake Abdulrahman na sherehe yake **Fath al-Majiid** na uchapishaji ukafanywa na muwahabi Muhammad Hamiid huko Misri. Mawazo ya Muhammad ibn Abd al-Wahhab yaliwavutia wanavijiji, wakazi wa Dar'iyya na kiongozi wao Muhammad ibn Su'ud. Waliokubali mawazo yake, wanajulikana kama Wawahabi au Wanajdi. Idadi yao iliongezeka na alijitangaza kuwa kadhi na Muhammad ibn Suud akawa amir. Walitoa azimio lililohakikisha kuwa vizazi vyao pekee ndio wanaowarithi.

Babaake Muhammad, aliyekuwa Muislamu mchamungu na mwanazuoni wa Madina, alitiwa wasiwasi na maneno ya Ibn Abdul-

Wahab kiasi kwamba alichukuwa hatua za kumpeleka kwa washauri na kuwataka watu wote kutoongea naye kutokana na maneno yake. Lakini aliutangaza uwahabi mwaka wa 1150 H./1739 A.D.. Alisema vibaya kuhusu ijtihad za wanazuoni wa kiislamu. Alifikia hatua ya kuwaita Ahl as-Sunna makafiri. Alisema kwamba yeyote anaetembelea kaburi la mtume au walii akasema, “Yaa Nabiyy Allah” (Ewe nabii wa Allahu taala), au “yaa Abdul-Qaadir” (Ewe Abdul-Qaadir) angekuwa mshirikina (mushrik).

Mtazamo wa wawahabi ni kwamba anaesema kwamba mtu yeyote asiekuwa Allahu taala hufanya kitu fulani, ni kafiri. Kwa mfano asemae kwamba, ‘Dawa fulani hupunguza maumivu’, au ‘Allahu taala alinitakabalia dua yangu karibu na kaburi la mtume au walii fulani, huwa mushrik. Ili kuyatolea mawazo haya uthibitisho, wanatoa ushahidi wa aya isemayo kuwa, “Iyyaaka nasta’iin” (Wewe pekee ndie tunaekuomba msaada) ya sura Al-Fatihah na aya nyengine zinazoelezea tawakkul.

Kitabu kiitwacho Al-Usuul al-Arba’a fi tardiid al-Wahhabiyya, mwishoni mwa sehemu yake ya pili kinasema: mawahabi na walaa madh-habii wengine hawaelewi maana za majaz na istiara. Mtu anaposema kwamba alifanya kitu fulani, wanamwita mushrik au kafiri ingawa tamko lake ni la kimajazi. Hatahivyo, Allahu taala ameeleza kwenye aya nyingi za Qurani kwamba yeye ndio mtengenezaji wa kweli wa kitendo chochote na mtu ni mtengenezaji wa kimajazi. Katika sura Al-An-am, aya ya 57 na katika Sura Yusuf, anasema: “Hukumu (maamuzi) ni ya Allahu taala pekee”, yaani Allahu taala ni muamuzi pekee. Katika aya ya 64, Sura An-Nisaa, anasema: “…hawatakuwa waumini mpaka watakapofanya maamuzi katika yale yaliyojiri baina yao na wajisalimishe kweli kweli”. Aya iliyotangulia husema kwamba Allahu taala ndie muamuzi (Hakiim) wa kweli na iliyoifuata hutaja kuwa mwanaadamu anaweza akaitwa kimajazi kama muamuzi (hakiim).

Kila Muislamu anajua kwamba Allahu taala pekee ndie anayejaalia uhai na kuuondoa, kwani ametangaza katika Sura Yunus, aya ya 56 kwamba, “Yeye anahuisha na kufisha”; katika Sura Az-Zumar, aya 42 anasema, “Allahu taala hufisha nafsi wakati wa kufa kwao”. Katika Sura As-Sajdah, aya ya 11, anasema, “Sema, hukufisheni malaika wa mauti”.

Allahu taala pekee ndie anayejaalia uzima kwa mgonjwa. Katika Sura ash-Shuuara, aya ya 80 anasema, “Na nikiuguwa yeye ndie anaeniponyeshaa” na katika Sura Aali-Imran, aya ya 49 Isa ananukuliwa akisema, “Na ninawaponesha vipofu wa tangu kuzaliwa

na wakoma, na ninafufua maiti kwa idhini ya Allahu taala …". Anayemjalia mwanaadamu mtoto kwa kweli ni Yeye. Katika Sura Maryam, aya ya 19, malaika Jibril anasema: "Malaika akasema: Hakika mimi ni mwenye kutumwa na Mola wako Mlezi ili nikubashirie tunu ya mwana alietakasika".

Mwanaadamu kwa kweli ni milki yake Allahu taala. Sura Al-Baqarah, aya ya 257 inataja hilo waziwazi: "Allahu taala ni walii (rafiki) wa walioamini" na katika Sura Al-Maidah, aya ya 56, "Hakika walii (rafiki) yenu ni Allahu taala na mtume wake" na kwenye Sura Al-Ahzab, aya ya 6, "Ila muwe mnawafanyia wema marafiki zenu". Anamaanisha kwamba mwanaadamu nae kitaashiria, ni Walii. Hivyo hivyo, msaidizi wa Kweli ni Allahu taala ingawa huwaita wanadamu mu'in (msaidizi) kimajazi. Katika Sura Al-Maidah, aya ya 2, kwamba "Saidianeni katika wema na uchamungu wala msisaidiane katika uovu na kuzozana". mawahabi hutumia neno mushrik wakimrejelea Muislamu amwitae mtu 'abd (mtumishi, mtumwa) wa fulani badala ya kumwita Abdullahi, kwa mfano "Abd an-Nabii" au "Abd ar-Rasuul lakini katika Sura An-Nur aya ya 32, Allahu taala anasema "Na waozesheni wajane miongoni mwenu na wajakazi wenu. Wakiwa mafakiri Allahu taala atawatajirisha kwa fadhila yake". Rabb wa kweli wa wanadamu ni Allahu taala, lakini mtu mwengine anaweza kuitwa rabb kimajazi katika Sura Yusuf, aya ya 42 Yusuf amesema "nitaje mbele ya rabb wako''.

Istighatha au kutaka msaada ni kitu ambacho mawahabi hupinga zaidi, kuomba msaada au hifadhi ya asiekuwa Allahu taala. Kusema kweli kama wanavyojua waislamu wote, istighatha halisi ni kutoka kwa Allahu taala. Lakini inaruhusiwa kusema kimajazi kwamba mtu anaweza kuomba istighatha (msaada, auni, ghauthi) kutoka kwa mtu mwingine, kwani katika Sura Al-Qasas, aya ya 15 tunaelezwa kuwa: "…Akakuta humo watu wawili wanapigana, mmoja ni katika wenzake, na mwengine katika maadui zake. Yule mwenzake alimtaka msaada kumpiga adui yake." Kwa mujibu wa hadithi, "Katika mahshar wataomba msaada (watafanya istighatha) kutoka kwa Adam". Aidha hadithi iliyonukuliwa kutoka katika kitabu kiitwacho Hisn al-Hasiin, inasema: "Yeyote anayehitaji msaada anapaswa kusema, "Enyi waja wa Allahu taala! Nisaidieni!" Hadithi hii tukufu hutuamrisha kuitisha msaada kutoka kwa mtu aliye mbali nasi". Mwisho wa tafsiri kutoka kwenye kitabu cha Al-Usuul al-Arba'a.

Kila neno lina maana bainifu ambayo hujulikana kama maana halisi ya neno hilo. Maana ya neno fulani hua ya kimajazi iwapo halikutumika kwa uhalisi wake bali kwa maana husihi. Ikiwa neno ambalo

linamuhusu Allahu taala tu limetumika kimajazi kuwarejelea wanadamu, mawahhabi hufikiria kuwa neno hilo limetumika kwa maana yake halisi. Kwa hiyo watamwita mtu anayetumia neno hilo mushriki au kafiri. Lakini wanapaswa kuzingatia kuwa maneno haya yametumika kimajazi katika aya na hadithi mbalimbali kuwarejelea wanadamu.

Kutafuta maombezi kutoka kwa mtume wa Allahu taala na mawalii si kumwepuka Allahu taala au kusahau kuwa yeye ndie muumbaji wa kila kitu. Ni kama kutarajia mvua kutoka kwake kupitia kwenye mawingu, kutarajia kupona kutoka kwake kwa kutumia dawa, kutarajia ushindi kutoka kwake kwa kutumia mizinga, mabomu, roketi na ndege. Hizi ni sababu. Allahu taala hukiumba kila kitu kupitia visababu. Si kitendo cha ushirikina kushikamana na visababu. Mitume (alaihimus-salaam) walishikamana daima na visababu. Kama ambavyo tunaenda kwenye chemchem kunywa maji aliyoyaumba Allahu taala na kwenye tanuri kuchukuwa mikate ambayo ameiumba pia, na kama ambavyo tunaunda silaha na kuwapa askari mafunzo kamili yenye mazoezi mengi yanayohusu matumizi ya silaha ili Allahu taala atupe ushindi, hivyo hivyo tunaunganisha roho zetu na ile ya mtume au walii ili Allahu taala atutakabalie dua zetu. Kutumia redio ili kuisikia sauti aliyoiumba Allahu taala kupitia kwenye mawimbi ya sumaku za kielektroniki haina maana kwamba tumemsahau na kulikimbilia boksi, kwani ndie anayetoa maajabu haya na nguvu hizi kwa ala hiyo iliyomo kwenye boksi la redio. Allahu taala ameificha kudura yake ndani ya kila kitu. Mshirikina huabudu masanamu lakini hamfikirii Allahu taala. Muislamu, anapotumia visababu na njia kadhaa, humfikiria Allahu taala anaejalia visababu hivyo na viumbe mafanikio na maajabu. Hutarajia kupata matakwa yake yote kutoka kwa Allahu taala. Anajua kwamba chochote akipatacho hutoka kwa Allahu taala. Maana za aya zile zilizotajwa hapo juu hudhihirisha kuwa huu ni ukweli. Yaani, muumini anaposoma Sura Al-Fatihah katika kila rehma, anasema, “Ewe Mola wangu! Nashikilia njia za kimaada na sababu za kisayansi ili nipate matamanio yangu na mahitaji ya kidunia, na kuwaomba waja wako kunisaidia. Ninapofanya hivyo, naamini kuwa wewe pekee ndie unayetoa na ndie Muumba wa matamanio. Matumaini yangu ni kwako pekee!”. Waumini wanaosema haya kila siku hawawezi kuchukuliwa kuwa washirikina. Kuomba msaada kutoka kwa roho za mitume na mawalii ni sawa na kushikamana na visababu hivi vilivyoumbwa na Allahu taala. Aya hiyo ya Sura Al-Fatihah huelezea wazi wazi kuwa wao si washirikina bali ni waumini wa kweli. Mawahabi pia hushikilia njia za

kimaada na kisayansi. Huridhisha matamanio yao kwa njia yoyote ile. Lakini huchukulia kitendo cha kuwakimbilia mitume na mawalii kama wapatanishi kuwa ushirikina.

Kwa vile maneno ya Muhammad ibn Abdul-Wahhab yalilingana na matamanio ya nafsi, watu wasiokuwa na elimu ya kidini waliyakubali kwa wepesi. Walidai kuwa wanazuoni wa Ahl as-Sunna na waislamu wa kweli walikuwa makafiri. Amiri (viongozi) waligundua kuwa uwahabi uliwiana na matamanio yao ya kuongeza nguvu zao na kupanua maeneo yaliyokuwa chini ya himaya yao. Waliyalazimisha makabila ya waarabu kuufuata uwahabi. Waliwaua watu ambao hawakuwaamini. Wanavijiji walimtii amir wa Dar'iyya Muhammad ibn Su'ud kwa kuogopa kuuwawa. Kujiunga na jeshi la amir kuliwafaa kwani kuliwawezesha kuridhisha matakwa yao ya kushambulia, kuua na kuchukuwa mali ya wasiokuwa mawahabi.

Sheikh Sulaiman, ndugu yake Abdul-Wahhab, alikuwa mwanazuoni wa kisunni. Mtu huyu, mwenye kheri, aliupinga uwahabi katika kitabu chake kiitwacho as-Sawa'iq al-Ilaahiyya fir-raddi 'alal-Wahhabiyya na akazuia kuenea kwa mihimili yake ya kichochezi. Kitabu hiki chenye thamani kilichapishwa mwaka wa 1306H. Kilichapishwa pia huko Istanbul mwaka wa 1395 H./1975 A.D. kwa kufidia. Walimu wake Muhammad ibn Abdul-Wahhab waliogundua kuwa amefungua njia ya uovu, walipinga vitabu vyake vilivyochafuliwa. Walitangaza kuwa ameacha njia ya kweli. Walithibitisha kuwa mawahabi walitoa maana potofu kwa aya na hadithi kadhaa. Hata hivyo, hatua hiyo iliongeza chuki za wanavijiji na uhasama dhidi ya waumini.

Uwahabi haukuenezwa kwa elimu bali ulienezwa na wajinga kwa ukatili na umwagaji damu. Miongoni mwa watu waliorowesha mikono yao na damu kwa njia hii, ni Amir wa Dar'iyya Muhammad ibn Su'ud. Bwana huyu alitoka kwenye kabila la Bani Hanifa, mmoja wa vizazi vya wapumbavu waliomuamini Musailama kuwa mtume. Alifariki mwaka wa 1178 na kurithithiwa na mwanawe Abdul Aziiz, ambae aliuliwa na Mashi'a mwaka wa 1217H. Alirithiwa na mwanawe Sa'ud aliyefariki mwaka wa 1231H. Mwanawe Abdullah alichukuwa mahala pake lakini aliuliwa huko Istanbul mwaka wa 1240. Mahala pake palichukuliwa na Tarki ibn Abdullah, mjukuu wa 'Abdul Aziiz. Aliyemrithi, mwaka wa 1254, alikuwa mwanawe Faisal ambae pia alirithiwa na mwanawe 'Abdullah mwaka wa 1282. Ndugu yake 'Abdur-Rahman na mwanawe 'Abdul Aziiz walipata makazi nchini Kuwait. Mnamo mwaka wa 1319H/1901 A.D., 'Abdul Aziiz aliend Riyadh akawa amir. Mwaka wa 1918 aliishambulia Makka akishirikiana na Waingereza. Katika mwaka

wa 1351H/1932 A.D., alianzisha taifa la Saud Arabia. Tunasoma katika magazeti yaliyotolewa mwaka wa 1991 A.D., kwamba Fahd, amir wa Saud alikuwa ametuma bilioni nne za dola kama msaada kwa makafiri wa Urusi ambao wamekuwa wakipambana na mujahidin nchini Afghanistan.

Mawahabi hudai kuwa wako kwenye njia ilionyooka katika kumuamini Allahu taala pekee na kuepuka ukafiri, na kwamba waislamu wote walikuwa washirikina kwa miaka mia sita, na kwamba wamekuwa wakijaribu kuwaokoa kutokana na ukafiri. Ili kuthibitisha kuwa ni wakweli, walitaja Sura Al-Ahqaf, aya ya 5 na Sura Yunus aya ya 106 kama ushahidi. Hata hivyo, tafsiri zote za Qurani husema kwa itifaki kwamba aya hizi mbili na nyingi nyinginezo zimekusudiwa mushrikina. Aya ya kwanza ni: "Na nani mpotofu mkubwa kuliko hao wanaowaomba, badala ya Allahu taala, ambao hawatawaitikia mpaka siku ya kiama, na wala hawatambui maombi yao, na nyingine ni: "Na wala usiwaombe wasiokuwa Allahu taala ambao hawakufai kitu wala hawakudhuru. Ukifanya hivyo basi utakuwa miongoni mwa waliodhulumu!"

Kitabu kinachojulikana kama "Kashf ush-shubhaat" huvuruga (kwa hila) aya iliyoko katika Sura Az-Zumar, inayosema kwamba: "Aya hii tukufu hunukuu maneno ya mushrikina wanaoabudu masanamu." Qurani huwafananisha wale wanaotafuta maombezi kutoka kwa mushrikina kama hao na husema kwamba masanamu yao hayaumbi kitu lakini Allahu taala ndie muumba. Katika tafsiri ya aya hii, kitabu kinachoitwa Ruuhl Bayaan kinasema: "Wanadamu huumbwa wakiwa na uwezo wa kumtambua muumba, aliewaumba wao na kila kitu. Kila mwanaadamu huhisi shauku ya kumuabudu Muumba na kuwa karibu nae. Lakini uwezo na shauku hio haina thamani kwa nafsi. Shetani au marafiki wabaya wanaweza kumdanganya mwanaadamu, na matokeo yake, shauku hii ya kimaumbile itaharibika, na mwanaadamu ima atakuwa asiemuamini muumba na siku ya kiama kama vile wakomunisti na wanafreemason (wanachama wa chama cha siri cha kusaidiana) au washirikina (waabudu miungu mingi). Mshirikina hawezi kumkaribia Allahu taala na hawezi kumjua. Kitu chenye thamani ni ma'rifa, ile elimu inayoimarika baada ya kuutokomeza ushirikina na kuikumbatia tawhidi. Dalili zake ni kuwaamini mitume (alaihimus-salaam) na vitabu vyao na kuwafuata. Hii ndio njia pekee ya kumkaribia Allahu taala. Aliyepewa zawadi ya kumsujudia mtu ni shetani, lakini alikataa kusujudu katika namna ambayo haiwiani na nafsi yake. Wanafalsafa wa Kigiriki wa enzi za kale walikufuru kwa

sababu walitaka kumkaribia Allahu taala si kwa kuwafuata mitume (alaihimus-salaam), bali kwa kufuata mantiki na nafsi zao. Waislamu wanapaswa kushikamana na Uislamu ili waweze kuwa karibu na Allahu taala. Wanapofanya hivyo, nyoyo zao hujawa na mwangaza wa kidini. Washirikina hawamfuati mtume wala Uislamu, bali huzifuata nafsi zao, nyoyo zao zenye maasi na bid'a, ili waweze kuwa karibu na Allahu taala, hivyo nyoyo zao hupata weusi na huwa na kiza. Allahu taala ametaja mwishoni mwa aya tukufu kwamba wanatoa kauli ya uwongo wanaposema, "Hatuyaabudu masanamu kutokana na sababu nyingine isipokuwa yapate kututetea". Kama inavyobainika, ni dhuluma kubwa kuchukulia aya tukufu ya 25 ya Sura Luqman, inayosema kwamba, "Na ukiwauliza Nani alieumba mbingu na ardhi? Bila shaka watasema Allahu taala", kama ushahidi na kusema kwamba 'washirikina pia walijua kwamba muumba alikuwa Allahu taala peke yake. Waliyaabudu masanamu ili yapate kuwatetea siku ya hukumu. Ni kwa sababu hiyo ndio wakawa washirikina na makafiri'.

Sisi, Waislamu, hatuabudu mitume "alaihis-salaam" wala mawalii (rahmatullahi alaihim) tunasema kwamba wao si wenzake wala washirika wake Allahu taala. Tunaamini kuwa walikuwa viumbe na wanaadamu na kuwa hawastahiki kuabudiwa. Tunaamini kuwa wao ni waja wapendwa wa Allahu taala na atawahurumia waja wake kwa ajili ya huba ya vipenzi vyake. Allahu taala pekee ndie huumba hasara na faida. Yeye pekee ndie anaestahiki kuabudiwa. Tunasema kwamba anawahurumia waja wake kwa ajili ya vipenzi vyake. Ingawa washirikina kutokana na ujuzi wa kimaumbile wanasema masanamu yao si yenye kuumba kitu, na kwa vile hawakuuendeleza ujuzi huu kwa kufuata mitume "alaihis-salaam", wanaamini kuwa masanamu yanapaswa kuabudiwa, wanakuwa washirikina kwa vitendo vyao hivyo. Lakini hawawi washirikina kwa kusema kwamba walitaka uombezi. Kama inavyobainika, kuwafananisha Ahl as-Sunna na makafiri wanaoabudu masanamu si kweli hata kidogo. Aya hizi zote ziliteremshwa kwa ajili ya makafiri wanaoabudu masanamu na washirikina. Kitabu hicho kiitwacho 'Kashf ash-shubhaat' kinatoa maana potofu kwa aya hizo, hutumia hoja potofu na kusema kwamba waislamu wasunni ni washirikina.

Hadithi mbili zilizonukuliwa na Abdullah ibn Umar "radiyallahu anhu" zinasema: "Wameacha njia ya kweli. Wamewatuhumu waislamu kwa aya zilizoteremshwa kwa ajili ya makafiri" na "miongoni mwa mambo ninayohofia umma wangu, jambo baya zaidi ni kufasiri kwao Quran tukufu kulingana na mitazamo na yao". Hadithi hizi mbili

zilitoa ubashiri kuwa wasiofuata madhehebu watajitokeza na kwa kutoa tafsiri potofu za aya zilizoteremshiwa makafiri watazitumia dhidi ya waislamu.

Mtu mwingine aliyetambua kwamba Muhammmad ibn Abd al Wahhab alikuwa na maoni potofu na yangekuwa yenye hatari baadae na ambae alimshauri, alikuwa Sheikh Muhammad ibn Sulaiman al-Madani "rahmetullahi alaih" [aliyefia Madina mwaka wa 1194 H./1780 A.D.] mmoja wapo wa wanazuoni wa Madina. Alikuwa mwanazuoni wa Kishaafi katika fiqhi na aliandika vitabu vingi. Ufafanuzi wake ya kitabu cha ibn Hajar al-Haytami al-Makki kiitwacho Tuhfat ul-Muhtaaj, sherehe ya kitabu kiitwacho Minhaaj, umepata umaarufu mkubwa. Katika kitabu chake cha juzuu mbili, kinachoitwa al-Fataawa, anasema: “Ewe Muhammad ibn Abd al Wahhab! Usiwakashifu waislamu! Nakushauri kwa ajili ya Allahu taala. Ndio, mtu anaposema kwamba mtu mwingine asiekuwa Allahu taala anaumba vitendo, mwambie ukweli! Lakini wale wanaoshikilia visababu wakaamini kuwa visababu na nguvu zenye athari ndani yake zimeumbwa na Allahu taala hawawezi kuitwa makafiri. Wewe pia ni Muislamu. Ingekuwa kweli zaidi kumuita Muislamu mmoja muasi kuliko kuwaita Waislamu wote hivyo anayeacha jumuiya hii huelekea kwenye upotevu. Aya ya 115 ya Sura An-Nisaa inathibitisha maneno yangu “Na anaempinga mtume baada ya kumdhihirikia uongofu, na akafuata njia isiyokuwa ya Waumini, tutamwelekeza alikoelekea, na tutamwingiza katika Jahannamu. Na hayo ni marejeo mabovu”.

Ingawa mawahhabi wana mihimili potofu isiyohisabika, mihimili hiyo imejengwa juu ya kanuni tatu:

1- Wanasema kwamba amali au vitendo vya ibada vimegubika katika imani na yeyote asiyetenda kitendo cha faradhi hata kama anaamini kuwa kitendo hicho ni cha faradhi, kama vile sala kutokana na uvivu, au zaka kutokana na ubakhili, hua kafiri na anapaswa kuuliwa na mali yake lazima igawanywe miongoni mwa mawahhabi.

Ash-Shirstani anasema: “Wanazuoni wa Ahl as-Sunna kwa pamoja wanasema kwamba ibada haiingizwi katika imani. Iwapo Muislamu ataacha kitendo fulani cha ibada ya faradhi kutokana na uvivu ingawa anaamini kuwa kukitenda ni faradhi, hatakuwa kafiri. Kwa mujibu wa madhehebu ya kihanbal, hakuna itifaki kuhusu yule asiyeswali kutokana na uvivu, kwamba huwa kafiri. [Thanaaullah Paanipuutii (rahmatullahi alaih) katika mwanzo wa kitabu chake kijulikanacho kama **Maa laabudda** anasema “Muislamu hakufuru kwa kutenda

dhambi kubwa. Akiwekwa motoni, atatolewa humo mapema au baadae, kisha ataingizwa peponi na ataishi humo milele”. Kitabu hiki kipo katika lugha ya Kifursi na kilichapishwa Delhi mwaka wa 1376 H./ 1956 A.D.] na kilitolewa tena na Hakikat Kitabevi mjini Istanbul mwaka wa 1410H/ 1990 A.D.. Katika madhehebu ya Kihanbali ilisemekana kuwa yule ambae ameacha sala ndie kafiri. Hayo hayakusemwa kuhusiana na aina nyingine za ibada. Kwa hiyo, kuhusu jambo hili si sawa kuwachukulia mawahabi kuwa wafuasi wa Hanbali. Kama ilivyoelezewa hapo juu, watu wasiojikita katika jumuia ya Ahl as-Sunna hawawezi kuwa wahanbali kwa vyovyote vile. Wasiojikita katika dhehebu lolote kati ya madhehebu manne hawawezi kujikita katika Ahl as-Sunna.

2- Wanasema kwamba atafutae uombezi kutoka kwa roho za mitume "alaihis-salaam" au mawalii "rahmatullahi alaihim" au anaehudhuria makaburi akaomba dua huku akimtaja Allah hua kashakufuru. Wanaamini pia kwamba maiti hawana hisia.

Kama mtu azungumzae na maiti aliomo kaburini atakuwa kafiri, mtume wetu "swallallahu alaihi wa sallam", wanazuoni wakuu na mawalii wasingeomba dua kwa namna hiyo. Ilikuwa kawaida yake mtume wetu "swallallahu alaihi wa sallam" kutembelea makaburi ya Baqii mjini Madina na mashahidi wa Uhud. Kwa kweli, imeandikwa katika ukurasa wa 485 wa kitabu cha mawahhabi kiitwacho **Fath al-majid** kwamba aliwatolea salamu na kusemezana nao.

Mtume wetu "swallallahu alaihi wa sallam" daima alikuwa akisema katika dua zake: “Allahumma innii as’aluka bihaqqi-ssaa’iliina ‘alaika” (Yaa Rabbi! Nakuomba kwa ajili ya watu hao ambao umewapa yale yote waliyokuomba) na akapendekeza kwamba tuombe hivyo. Alipozikwa Fatima, mamaake Hadhrat Ali (radiyallahu anhuma), kwa mikono yake mwenyewe yenye kheri, alisema. (Yaa Rabbi! Mughufirie Mama Fatima madhambi yake! Umpanulie mahala alimoingizwa! Kwa haki ya nabii wako na manabii waliotangulia! Hakika wewe ni mbora wa wanaorehemu”.) Katika hadithi iliyopokelewa na Uthman ibn Hunaif "radiyallahu anhu", mmoja wapo wa maansaari mashuhuri, tunaambiwa jinsi mtume "swallallahu alaihi wa sallam" alivyomuamrisha kipofu mmoja aliyemuomba dua ili apone, atawadhe na kusali rakaa mbili kisha aseme:

Allahumma inni as’aluka wa atawajjahu ilaika binabiyyika Muhammadin nabiyyir rahma, yaa Muhammad inni atawajjahu bika ilaa Rabbii fii haajatii haadhihi litaqdhiya lii’ Allahumma shaffi’hu

fiyya”. Katika dua hii, kipofu aliamrishwa kupata kimbilio kwa Muhammad "swallallahu alaihi wa sallam" kama mpatanishi ili dua yake ipate kutakabaliwa. Masahaba watukufu daima walikuwa wakiomba dua hii ambayo imenukuliwa katika juzuu ya pili ya kitabu kiitwacho Ashi’at al-lam’aat na pia katika al-Hisn al-Hasiin na marejeleo yake na maana inayokusudiwa: “Naelekea kwako kupitia kwa mtume wako”.

Dua hizi hudhihirisha kuwa inaruhusiwa kuwawasilisha wale awependao Allahu taala katika upatanishi na kumwomba kwa kusema “Kwa ajili yao”. Sheikh Ali Mahfudh aliyefariki mwaka wa 1361H/ 1942 A.D. mmoja wapo wa wanazuoni wa Chuo cha Azhar huwasifu sana Ibn Taymiyya na ‘Abduh katika kitabu chake al-Ibaada. Hata hivyo, anasema kwenye ukurasa wa 213 wa kitabu hicho hicho kwamba: “Si sahihi kusema kwamba mawalii maarufu "rahmetulllahi alaihim" hawatendi matendo ya kidunia baada ya kifo, kama vile kuwaponya wagonjwa, kuwanusuru wale ambao wamekaribia kufa majini, kuwasaidia wale wanaopambana na adui na kupatikana kwa vitu vilivyopotea. Si sahihi kusema hivyo, kwa sababu mawalii ni watu maarufu sana, Allahu taala kawaachia majukumu haya au hua wanafanya wayatakayo au kwamba mtu anayeshikamana nao hatakosea. Lakini rehma ya wao kuwa hai au maiti si hoja, kwa sababu Allahu taala humjalia baraka zake yeyote aliyemteua miongoni mwa mawalii zake na kupitia miujiza yao huwaponya wagonjwa, huwanusuru waliokaribia kufa majini, huwasaidia wanaopambana na adui na Allahu taala huvirejesha vilivyopotea. Haya ni ya kimantiki. Kwa kweli, Quran tukufu hudhihirisha mambo haya ya ukweli”.

Abdul-Ghanii an-Nablusii "rahmetullahi alaih" anaandika: “Hadith Qudsi aliyoipokea al-Bukhari kutoka kwa Abu Huraira "radiyallahu anhu", inasema, Allahu taala anasema, “Mja wangu hanikaribii na chochote nikipendacho zaidi kuliko kitendo cha fardhi. Na mja wangu hanikaribii na chochote miongoni mwa ibada za sunna ila ninampenda. Na nikishampenda, mimi huwa sikio lake ambalo husikia nalo na jicho lake ambalo huona nalo na mkono wake ambao hushika kwake. Na akiniomba nitampa atakacho bila shaka. Na akiniomba kinga, nitampa kinga bila shaka”. Vitendo vya ibada vya sunna vilivyotajwa hapa [kama ilivyoandikwa waziwazi katika **Maraaq al-Falaah** na **Shereh At-Tahtaawi**], ni sunna na ibada zisizo za faradh zinazofanywa na watu ambao tayari wameshatekeleza vitendo vya ibada vya faradhi. Hadithi hii hudhihirisha kuwa mtu anayetenda ibada za sunna baada ya kutekeleza zile za faradhi atapendwa na Allahu taala na dua yake

itatakabaliwa. Watu kama hao wanapowaombea dua watu wengine, wale walioombewa watapata yale wanayotamani. Watu kama hao husikia hata kama wameshakufa. Wanaowaomba hawaambulii patupu kama ambavyo hawakufanya hivyo walipokuwa hai; wanawaombea dua. Kwa sababu hii, hadithi inasema “Mkipata shida katika mambo yenu, ombeni msaada kutoka kwa wale walioko makaburini!” maana ya hadithi hii ni wazi na ufasiri wake kwa namna nyingine tofauti hairuhusiwi. Ufasiri wa ‘Aluusi ni potofu.

Kwa kweli, “Waislamu ni waislamu wakiwa maiti, kama wanavyokuwa wakiwa wamelala. Mitume wangali mitume baada ya kufa kama ilivyo wakiwa wamelala kwani roho ndio Muislamu. Mwanamume anapofariki, roho yake huendelea kuwa hai. Ukweli huu umeandikwa katika kitabu kiitwacho **Umdat al‘aqaa’id** cha Imam Abdullah an-Nasafi (kilichochapishwa London mwaka wa 1259 H./1843 A.D.). Hivyo hivyo, mawalii wangali mawalii wakiwa maiti kama wanavyokuwa wakiwa usingizini. Asiyeamini haya ni mkaidi. Nimethibitisha katika kitabu kingine kuwa mawalii huwa pia na karaamat (miujiza) baada ya kifo. Mwanazuoni wa kihanafi Ahmad ibn Sayyid Muhammad al-Makki, mwanazuoni wa Kishaafi Ahmad ibn Ahmad as-Sujaa’i na Muhammad as-Shaubari al-Misri waliandika vijitabu ambamo walithibitisha kwa ushahidi kuwa mawalii walikuwa na karaamat na kuwa karaamaat hizo ziliendelea baada ya kufa kwao. Na kwamba tawassul au istighaatha kwenye makaburi yao kunaruhusiwa.

Muhammad Haadimii Efendi "rahmatullahi alaih" wa Konya (aliyefariki mwaka wa 1176 H./ 1762 A.D. mjini Konya) aliandika: “Karaamaat za mawalii ni za kweli. Walii ni Muislamu amjuaye sana Allahu taala na sifa zake (**‘aarifun billahi**). Anafanya ibada na vitendo vingi vya utiifu. Anajitahadharisha sana na madhambi na matamanio ya nafsi yake. Vitu anavyoviumba Allahu taala kwa njia iliyoko nje ya sheria ya usababishi na sheria za kisayansi hujulikana kama ‘Khaariq al‘aada’ (maajabu) ambavyo ni vya aina nane: Mu’jiza, karaama, I’aana, ihaana, sihr, ibtilaa, isaabat al’ayn, na irhaas. Karaama ni tukio lisilo la kawaida litokealo kupitia kwa muumini mwenye bidii anaemjua sana Allahu Taala (‘aarifun billah). Yeye hua walii na sio mtume. Ibrahim ibn Ishaaq al-Isfaraa’ini, mwanazuoni wa Kishaafi, alikana baadhi ya karaama huku Wamu’tazila wakikana karaama zote. Wanasema kwamba zinaweza kuchanganywa na muujiza na hivyo kuamini mitume kunaweza kuwa jambo gumu. Hata hivyo, walii ambae karaamaat hutokea kupitia kwenye vitendo vyake, hadai utume wala hapendi

karaama kutokea tu. Inaruhusiwa kumwomba Allahu taala kupitia kwa mitume au mawalii hata baada ya kufa kwao kwa sababu mu'jiza na karaama hazikomi baada ya kifo. Ali Ajhuri, mwanazuoni mashuhuri wa Kimaliki, anasema: 'Walii akiwa hai huwa kama upanga katika ala yake. Baada ya kufa kwake, taathira zake huwa kali zaidi kama upanga ulioko nje ya ala yake'. Kauli hii imenukuliwa pia na Abu Ali Sanji katika kitabu chake kiitwacho Nuur al-Hidaaya.

Qurani, Sunna na Ijmaa huthibitisha kuwa karaama ni jambo la kweli. Karaamaat nyingi sana za mawalii zimeripotiwa kwenye vitabu vingi vyenye thamani. Mwisho wa tafsiri kutoka kwenye kitabu kiitwacho **Beriiqa**. Hadithi iliyo sahihi iliyopokelewa na ibn Khuzaima, ad-Daar qutni na at-Tabraani kutoka kwa Abdullah ibn Umar "radiyallahu anhu" inasema **"Imeniwajibikia kuwatetea wale watakaotembelea kaburi langu"**. Imam al-Manaawi pia ameinukuu hadithi hii katika **Kunuuz ad-Daqaa'iq**. Aliandika pia hadithi isemayo **"Kutembelea kaburi langu baada ya kufa kwangu ni kama kunitembelea nikiwa hai"**. Iliyopokelewa kutoka kwa ibn Hibbaan na hadithi iliyopokelewa kutoka kwa at-Tabraani inasema **"Nitamtetea mtu atembeleaye kaburi langu"**. Hadithi mbili zifuatazo, ambazo ni za kiwango cha marfuu ya kwanza iliyonukuliwa na al-Bazzaar na ya pili ikanukuliwa katika Sahih Muslim, zote zikiwa zimepokelewa kutoka kwa Abdullah ibn Umar "radiyallahu anhu", zajulikana takribani na kila Muislamu **"Ni halali kwangu kuwatetea wanaotembelea kaburi langu" "Siku ya kiama nitawatetea wale wanaokuja Madina kutembelea kaburi langu"**.

Ni habari muhimu sana ambazo zimenukuliwa katika hadithi kwamba **"Mtu anaehiji kisha akatembelea kaburi langu, atakuwa kama amenitembelea nikiwa hai"**. Imenukuliwa na at-Tabraani, ad-Daara Qutni na Abdur-Rahman ibn al-Jawzi. Hadithi nyingine iliyonukuliwa na ad-Daara Qutni inayozungumzia wale wanaopuuza kulitembelea kaburi la mtume "swallallahu alaihi wa sallam" baada ya kufanya hija na hali hawana udhuru wa kufanya hivyo anasema **"Mtu asienitembelea baada ya kuhiji atakuwa ameniudhi"**.

'Abd al-Aziiz, mkuu wa chuo cha Kiislamu cha Madinat ul-Munawwara aliandika katika Tahqiiq al-Iidhaah kwamba "Hakuna yoyote kati ya hadithi zilizotajwa hapo juu [zinazopendekeza ziara hiyo] ambayo inaegemezwa kwenye uthibitisho maalum". Sheikh al-Islam ibn Taymiyya alisema kwamba zote ni mawdhuu". Hata hivyo, silsila ya mapokezi yake imetajwa kwa ukamilifu katika juzuu nane za **Sherehe al-Mawahib** na mwishoni mwa juzuu ya nne ya **Wafaa' al-**

**Wafaa'** ya as-Samuudi. Katika vitabu hivi, imetajwa pia kuwa hadithi hizi ni (za kiwango cha) hasan na kwamba maelezo ya Ibn Taymiyya hayana msingi maalum.

Mkuu wa chuo na walimu wa chuo kikuu cha Madina wanajaribu kuyazulia upungufu maandishi ya Ahl as-Sunna na badala yake waeneze mihimili ya kiwahabi dunia nzima kwa kutumia vitabu vyao. Ili kuyaridhisha mataifa ya kiislamu, wanafuata sera mpya. Wanaanzisha kituo cha Kiislamu kijulikanacho kama Rabita al-Alam al-Islaami huko Makka na wanawakusanya watu wajinga wanaoweza kuchukuwa rushwa, wenye elimu ya kidini, wakiteuliwa kutoka katika kila nchi na ambao wanawalipa mishahara inayofikia mamia ya sarafu za dhahabu. Wanaume hawa wajinga wenye vyeo vya kidini, kwa vile hawana ujuzi juu ya vitabu vya Ahl as-Sunna, hutumiwa kama vibaraka. Wanasambaza mihimili yao kutoka kwenye kituo hiki, ambayo wanaichukulia kuwa fatwa za umoja wa mataifa ya kiislamu, kwa dunia nzima. Katika fatwa ya uongo iliyotolewa katika mwezi wa Ramadhani mwaka wa 1395 H./1975 A.D., walisema: “Ni faradhi kwa wanawake kusali sala ya Ijumaa. Khutuba za Ijumaa na Idi zinaweza kuwasilishwa kwa lugha za kienyeji katika kila nchi”. Muasi ajulikanae kama Sabri mmojawapo wa wafuasi wa Mawdudi na mwanachama wa kituo hicho cha fitna na uharibifu kilichopo Makka, aliipeleka fatwa hiyo mara moja huko India ambako wanaume wanaopokea mishahara, matajiri na wajinga waliwalazimisha wanawake kwenda misikitini na wakaanzisha kitendo cha kuwasilisha khutuba kwa lugha mbalimbali. Ili kuzuia kitendo hiki, wanazuoni wa Ahl as-Sunna na wanadini wa kweli nchini India "rahmetulllahi alaihim" waliandaa fatwa kutokana na vyanzo vinavyothaminiwa wakazisambaza. Wawahabi hawakuwa na uwezo wa kupinga fatwa hizi ama ukweli huu. Mamia ya wanaume wenye elimu ya kidini kutoka Kerala, kusini mwa India, walipotambua kwamba walikuwa wamedanganywa, walitubu wakarejea kwenye njia ya Ahl as-Sunna. Nne kati ya fatwa hizo ambazo zimejengwa juu ya vyanzo vyenye kutegemewa, zilizochapishwa kupitia mchakato wa kufidia zikatumwa kwa nchi kadhaa za kiislamu. Wenye mamlaka halisi ya kidini katika kila nchi huwatolea waislamu wito wa kuwa waangalifu na kujaribu kuzima uchochezi unaougawa Uislamu ndani kwa ndani.

Tunamshukuru Allahu taala, kwa vile vijana wasio na hatia na walio macho katika kila pembe ya dunia, wanaweza kutofautisha kati ya ukweli na uongo. Alipokuwa akielezea mada zinazohusu khutuba ya Ijumaa, takbiirat al-iftitaahi na swala, Ibn Abidin "rahmatullahi alaih" aliandika katika kitabu chake kiitwacho Radd al Muhtaar kwamba:

“Kuwasilisha khutuba kwa lugha isiyokuwa ya Kiarabu ni kama kutoa takbiirat al-iftitaahi (Allahu Akbar) kwa lugha nyingine wakati wa kuanza swala. Takbiirat al-iftitaahi ni kama adhkaari za swala na ni makruhu ya uharamisho kufanya adhkaari na kusali kwa lugha nyingine isiyokuwa Kiarabu kama ilivyoharamishwa na Hadhrat Umar "radiyallahu anhu". Katika sura inayozungumzia wajibu za salat, aliandika: “Kutenda jambo la makruhu ya uharamisho ni dhambi ndogo. Iwapo mtu ataendelea kulitenda, atapoteza adaala yake (istiqaama yake katika dini na uungwana)”. Imeandikwa katika kitabu cha at-Tahtaawi kwamba mtu anaetenda dhambi ndogo kwa mfululizo hua faasiq na kwamba mtu anaweza kukimbilia kwenye msikiti mwingine ili asisalie nyuma ya Imamu ambae ni faasiq na mwanabid’a. Kwa vile kuwasilisha khutuba nzima au sehemu yake kwa lugha nyingine ni makruhu tena bid’a, ambayo huchukuliwa kama dhambi kubwa, masahaba watukufu na Tabi’uun daima waliwasililisha khutuba kwa Kiarabu huko Asia na Afrika, hata kama wasikilizaji hawakuwa na ujuzi wa Kiarabu na hawakuelewa khutuba hizo. Ingawa elimu ya kidini ilikuwa haijaenea na walipaswa kufundishwa, waliisoma khutuba yote kwa Kiarabu. Ni kwa sababu hiyo ndio masheikh wa dola la Kiuthumani na wanazuoni wa kiislamu mashuhuri duniani kote, kwa miaka mia sita, hawakuruhusu uwasilishaji wa khutuba kwa Kituruki pamoja na kwamba walikuwa na hamu kubwa ya kufanya hivyo ili yaliyomo yapate kueleweka kwani walijua kwamba ilikuwa hairuhusiwi kuwasilisha khutuba kwa Kituruki. Hadithi tukufu iliyopokelewa na Imamu al-Baihaqi kutoka kwa Abu Huraira "radiyallahu anhu" inasema: **“Mtu anaponitolea salamu, Allahu** taala **huirejesha roho yangu kwenye mwili wangu nikaisikia salamu yake”**. Kwa kutegemea hadithi hii, Imamu al-Baihaqii "rahmatullahi alaih" alisema kwamba mitume "alaihis-salaam" walikuwa hai katika makaburi yao katika maisha yasiyojulikana kwetu.

Pamoja na hayo, Abd al-Aziiz ibn ‘Abdullah wa Madina huinukuu hadithi hii katika ukurasa wa 66 kwenye kitabu chake kiitwacho Al-Hajj wal-Umra na anafafanua kwamba inelezea kifo cha mtume "swallallahu alaihi wa sallam" wakati, katika ukurasa huo huo, anasema kwamba yuko hai katika kaburi lake kwenye maisha yasiyojulikana kwetu. Matamko yake hupingana. Kwa kweli, hadithi hii hudhihirisha kuwa roho yake yenye baraka hurejeshwa kwenye mwili wake na huitambua salamu.

Zaidi ya hayo, hadithi mbili zilizonukuliwa kwenye ukurasa wa 73 wa kitabu hicho hutoa taarifa kwamba mtu anayeifanya ziara kwenye

makaburi anapaswa kusema “Assalalaamu alaikum ahl ad-diyaar minal mu’miniin’. Hadithi hiyo hutuamrisha kuyatolea salamu makaburi ya waislamu wote. Asiesikia anaweza kusalimiwa au kuongeleshwa. Ingawa wasiofuata madhehebu huzinukuu hadithi hizi, wanadai kuwa maiti hawawezi kusikia na huwachukulia wanaoamini kuwa wanasikia kama washirikina. Hawazifasiri aya na hadithi kwa usahihi.

Kuna hadithi nyingi zinazoelezea kuwa mtume "swallallahu alaihi wa sallam" yuko hai katika kaburi lake kwenye maisha yasiyojulikana. Uwepo wa hadithi nyingi huashiria kuwa ni sahihi. Kati ya hadithi hizo, hadithi mbili zifuatazo zimeandikwa katika vitabu sita vinavyotambulika kote **“Nitasikia salawaat zinazotolewa kwenye kaburi langu, nitaarifiwa kuhusu salawaat zilizotolewa kwa mbali”; “Mtu anapotoa salawaat kwenye kaburi langu, Allahu** taala **humtuma malaika akanipa taarifa kuhusu salawaat hizo na nitamtetea siku ya kiama”**. Muislamu akienda kwenye kaburi la maiti Muislamu ambae alikuwa anamjua wakati wa uhai wake akamtolea salamu, maiti huyo atamtambua na kuitikia salamu. Hadithi iliyonukuliwa na ibn Abid-dunia huelezea kuwa Muislamu aliyekufa humtambua na kumjibu anae mtolea salamu tena hufurahi.

Mtu anapowasalimia waliokufa ambao hakuwajua, hufurahi na kumshukuru kwa salamu hiyo. Ikiwa waislamu walio wema na mashahidi "rahmetullahi alaihim" huwatambua na kuwajibu wale wanaowatolea salamu, inawezekanaje mtume "swallallahu alaihi wa sallam" asifanye hivyo? Mtume "swallallahu alaihi wa sallam" huzijibu salamu zote hapo hapo kama mfano wa jua linavyotoa mwangaza duniani kote.

Kwa mujibu wa hadithi tukufu mtume anasema: **“Baada ya kufa kwangu, nitasikia jinsi ninavyosikia nikiwa hai”**. Hadithi nyingine iliyonukuliwa na Abu Ya’la inasema: **“Mitume wako hai ndani ya makaburi yao, wanaswali”**. Ibrahim ibn Bishar na Sayyid Ahmad ar-Rifaa’i na mawalii wengine wengi "rahmetullahi alaihim" walisema kwamba walisikia jibu baada ya kumtolea mtume "swallallahu alaihi wa sallam" salamu. Mwanazuoni wa Kiislamu mashuhuri Hadhrat Jalalud-Diin as-Suyuuti aliandika kitabu kiitwacho Sherh al-Muhkam kama jibu kwa swali aliloulizwa ‘Ni kweli kwamba Sayyid Ahmad ar-Rifaa’i aliubusu mkono wa mtume? Katika kitabu hiki hiki, alithibitisha kwa ushahidi wa kiakili na kimapokeo kwamba mtume wa Allahu taala "swallallahu alaihi wa sallam" yuko hai kwenye kaburi lake katika maisha yasiyojulikana na kwamba husikia na kuitikia salamu. Aidha

alieleza katika kitabu hiki kwamba usiku wa Mi'raaj mtume alimwona Musa "alaihis-salaam" akisali ndani ya kaburi lake.

Katika hadithi iliyopokelewa na mama yetu Aisha As-Swiddiiqa "radiyallahu anha" mtume alisema: **"Naumia kutokana na nyama ya sumu niliyokula huko Khaybar. Kwa sababu ya sumu hiyo, mkole wangu karibu ushindwe kutenda kazi"**. Hadithi hii hudhihirisha kuwa zaidi ya utume, Allahu taala amempa Muhammad mwenye hadhi ya juu miongoni mwa wanadamu hadhi ya ushahidi. Allahu taala anaielezea katika Sura Aali-Imran aya ya 169 "Wala kabisa usiwadhanie waliouliwa katika njia ya Allahu taala kuwa ni maiti. Bali hao ni wahai, wanaruzukiwa kwa Mola wao". Bila shaka mtume huyu maarufu "swallallahu alaihi wa sallam" aliyepewa sumu akiwa katika njia ya Allahu taala, ni wa juu zaidi miongoni mwa watu na ndie ambae hadhi yake ilinyanyuliwa katika aya hiyo tukufu. Hadithi iliyonukuliwa na ibn Hibbaan inasema **"Miili ya mitume "alaihis-salaam" haiozi. Mtu anaponitolea salamu, malaika huifikisha kwangu na kusema Fulani bin fulani ametuma rehma na salamu kwako"**. Hadithi iliyopokelewa na ibn Maaja inasema **"Nisalieni tena na tena siku ya Ijumaa Swala zenu zitawasilishwa kwangu punde tu baada ya kutolewa".** Abu Dardaa' "radiyallahu anhu" aliyekuwa na mtume wakati huo aliuliza, **"Je, itawasilishwa kwako pia baada ya kufa? Mtume akasema Ndio. Nitaarifiwa kuhusu swala hiyo baada ya kufa pia. Kwani imeharamishwa kwa ardhi kuifanya miili ya mitume ioze. Wako hai baada ya kufa na hulishwa"**. Hadithi hii imeandikwa pia katika sehemu ya mwisho ya kitabu kiitwacho muwataa wal-qubuur cha Senaullahi Pani Puti. Kitabu hiki ni cha Kifursi na kilichapishwa Delhi mwaka wa 1310 H./ 1892 A.D. na kilitolewa upya na Hakikat Kitabevi mjini Istanbul mwaka wa 1990].

Hadhrat Umar "radiyallahu anhu" baada ya kupata ushindi huko Baytil maqdis, alienda kufanya ziara kwenye kaburi la mtume "swallallahu alaihi wa sallam" akamtolea salamu. Hadhrat Umar ibn Abd al-Aziiz aliyekuwa walii maarufu, alikuwa akiwatuma maafisa mara kwa mara kutoka Bait al-Maqdis kwenda Madina ili wamsalie mtume. Hadhrat 'Abdullah ibn Umar alikuwa akienda moja kwa moja kwenye Hujrat as-Sa'ada, baada ya kutoka safarini akatembelea makaburi akianza na kaburi la mtume halafu lile la Abu Bakr halafu lile la babaake akawatolea salamu. Imamu Naafi' alisema "Nilimuona Hadhrat 'Abdullahi ibn Umar zaidi ya mara mia, akienda kwenye kaburi la mtume na kusema 'Assalamu alaika yaa Rasul Allah!' Siku moja Hadhrat 'Ali "radhiallahu anhu" aliingia katika msikiti mtukufu akalia

alipoona kaburi la Fatima ("radiyallahu anha") na akalia zaidi alipoenda kwenye Hujrat as-Sa'ada. Kisha akawatolea salamu mtume "swallallahu alaihi wa sallam", Hadhrat Abu Bakr na Hadhrat Umar "radiyallahu anhuma" akisema: 'Assalaamu alaika ya Rasuul Allah. Assalaamu alaikumaa enyi ndugu zangu wawili".

Kwa mujibu wa Imam mkuu Abu Hanifa ("rahmatullahi alaih"), mtu anapaswa kufanya hija kisha aende Madinat al-Munawwara amtembelee mtume "swallallahu alaihi wa sallam". Hayo pia yameandikwa kwenye fatwa ya Abu-l-Laith as-Samarqandi.

Qadhi Iyaadh, muandishi wa kitabu kiitwacho Shifaa'; Imam an-Nawawi, mwanazuoni wa Kishaafi na ibn Humaam, mwanazuoni wa Kihanafi "rahmetullahi alaihim", walisema kwamba kuna Ijmaa ya umma kuhusiana na kutembelea kaburi lenye baraka. Wanazuoni wengine wanasema kwamba ni wajibu. Kwa kweli ni sunna kutembelea makaburi jambo ambalo limeandikwa pia katika kitabu cha mawahabi Fath al-Majid. Sura An-Nisaa, aya ya 64 inasema kwamba **"Na lau pale walipojidhulumu nafsi zao wangelikujia, wakamwomba Allahu taala msamaha, na mtume akawaombea msamaha, hapana shaka wangelimkuta Allahu taala ni Mwenye kupokea toba na Mwenye kurehemu"**. Aya hii huashiria kuwa mtume "swallallahu alaihi wa sallam" atafanya utetezi na utetezi wake utakubaliwa. Aidha, inatuamrisha kutoka katika sehemu za mbali tutembelee kaburi lake na tuombe utetezi wake.

Kwa mujibu wa hadithi: **"Haifai kufunga safari na kutembea kwa masafa marefu kutembelea misikiti mingine isipokuwa misikiti mitatu"**. Hadithi hii hudhihirisha kuwa kusafiri safari ndefu kwa ajili ya kutembelea msikiti mtukufu mjini Makka, msikiti wa mtume mjini Madina na msikiti wa Al-Aqsa mjini Jerusalem ni kitendo ambacho kukifanya mtu hupata thawabu. Kwa sababu hii, Waislamu wanaoenda kufanya hija na wakakosa kutembelea kaburi la mtume lililoko kwenye al-Masjid an-Nabawi watakosa ujira huu.

Imam Malik "rahmatullahi alaih" alisema kwamba ni makruhu kwa wanaotembelea makaburi kukaa karibu na Hujrat as-Sa'ada kwa muda mrefu. Imam Zain al-Abidiin "rahmatullahi alaih" alipokuwa akifanya ziara, alisimama karibu na nguzo ilioko upande wa Raudha tukufu na hakuenda mbele zaidi. Ziara ilikuwa ikifanyika kwa kusimama, kwa kuelekea kibla kwenye mlango wake wa Hujrat as-Sa'ada hadi Hadhrat Aisha alipofariki dunia.

Katika hadithi mtume anasema: **“Msilifanye kaburi langu mahali pa sherehe”**. Hadhrat ‘Abd al-Aziim al-Munziri, m taala mu wa hadithi, alielezea maana ya hadithi hii kuwa: **‘Msione kuwa inatosha kutembelea kaburi langu mara moja katika mwaka kama kwenye siku za Idi. Jitahidini kunitembelea mara kwa mara**. Na hadithi isemayo kwamba **“Msiyafanye majumba yenu makaburi”**, humaanisha kuwa tusiyafanye majumba yetu yaonekane kama makaburi kwa kutosaliwa ndani yake. Kwa hiyo, maelezo ya Hadhrat al-Munziri ni sahihi. Kwa kweli hairuhuhusiwi kusali makaburini. Ilisemekana kuwa hadithi hii inaweza kumaanisha kwamba **‘Msitenge siku maalum kwa ajili ya kutembelea kaburi langu kama siku ya sherehe’**. Wayahudi na Wakristo, wakati wakiitembelea mitume yao, kwa kawaida walikusanyika pamoja, wakawa wanapiga ngoma zao huku wakicheza, na kuimba nyimbo pamoja na kufanya sherehe. Hadithi hizi zinamaanisha kwamba tusiwe kama wao yaani tusifurahikie wala kutenda yaliyoharamishwa siku za sherehe au kucheza matete au ngoma au kukusanyika kwa ajili ya kushereheka katika ziara yetu. Tunapaswa kufanya ziara, kutoa salamu na kuomba dua kisha tuondoke kimya kimya pasi na kuchukua muda mrefu.

Imamu mkuu Abu Hanifa "rahmatullahi alaih" alisema kwamba kutembelea kaburi la mtume ni sunna inayothaminiwa zaidi, na kuna wanazuoni waliosema kwamba ni wajibu. Kutokana na sababu hii, kutembelea kaburi la mtume kunaruhusiwa kama nadhiri kwa mujibu wa dhehebu la Kishaafi’.

Kwa kweli, “Allahu taala amedokeza katika tamko lake, “Nisingalikuumba wewe, basi nisingaliumba chochote” kuwa Muhammad "swallallahu alaihi wa sallam" ni kipenzi chake anayempenda zaidi. Hata mtu wa kawaida hatokataa kitu kinachoumbwa kwa ajili ya mpenzi wake. Mtu akisema, ‘Ewe Allahu taala! Nakuomba kwa ajili ya mtume wako Muhammad "swallallahu alaihi wa sallam", ombi lake halitokataliwa. Hata hivyo, mambo madogo madogo ya kidunia hayapaswi kuhusisha huruma ya mtume wa Allahu taala kama mtetezi”.

Imamu mkuu Abu Hanifa "rahmatullahi alaih" alisema “Nilikuwa mjini Madina. Sheikh Ayyub as-Sahtiani mmoja wapo wa watu wema alienda kwenye msikiti mtukufu. Nilimfuata hadhrat Sheikh alielekea kwenye kaburi. Alisimama huku mgongo wake ukiwa kwenye kibla. Kisha akaenda nje”.

Hadhrat ibin Jamaa'a aliandika katika kitabu chake al-Mansak al-Kabiir "Wakati wa ziara, baada ya kusali rakaa mbili na kuomba dua karibu na mimbari, unapaswa kuja kwenye Hujrat as-Sa'ada, upande wa kibla na kichwa cha mtume "swallallahu alaihi wa sallam" kikiwa upande wa kushoto, utasimama katika masafa ya mita mbili kutoka kwenye ukuta wa al-Marqad ash-Shariif (kaburi la mtume) kisha ukiuacha upande wa nyuma wa ukuta wa kibla na kugeuka polepole mpaka uelekee Muwajjahat as-Sa'ada, basi mtolee salamu. Hivi ndivyo ilivyo katika madhehebu yote manne".

'Abd al-Ghanii an-Nabluusii "rahmetullahi alaih" akielezea 'afa la ishirini na tatu miongoni mwa maafa ya ulimi', anaandika; "Ni makruhu ya uharamisho kusema wakati wa kuomba dua, "Kwa haki ya mitume" au "Kwa haki ya walii [fulani ambae yuko hai au amekufa] au kumuomba Allahu taala kitu huku ukisema hivyo, kwani inasemekana kuwa hakuna kiumbe ambae ana haki zozote juu ya Allahu taala, yaani si lazima kwake kumpa mtu yeyote matakwa yake. Huu ni ukweli, hata hivyo, aliwaahidi waja wake wapendwa na kutambua haki yao kwake, yaani atakubali matakwa yao. Ameeleza katika Quran tukufu kwamba ameweka haki ya waja wake juu yake, kwa mfano, 'Ni haki juu yetu kuwasaidia waumini'. Imetangazwa katika fatwa za al-Bazzaaziyya kwamba "Inaruhusiwa kumuombea mtu kwa ajili ya mtume au walii aliye hai au ambae amefariki dunia kwa kutaja jina lake". **Sherh Shir'a** inaeleza kuwa: "Mtu anapaswa kumuomba Allahu taala kwa kuwafanya mitume au waumini wema watetezi. Ukweli huu umeandikwa pia katika **Hisn al-Hasiin**". Kama tunavyoona wanazuoni wa Kiislamu walisema kwamba inaruhusiwa kumuomba Allahu taala kwa kutumia haki au upendo aliowajaalia vipenzi vyake na hakuna mwanazuoni hata mmoja aliyesema kwamba ingekuwa ushirikina kuomba na fikra kwamba watu wana haki kadhaa juu ya Allahu taala. Mawahabi peke yao ndio wanaosema hivyo.

Ingawa wanasifu fatwa za al-Bazzaziyya katika **Fath al-Majiid** na kuzichukulia kama ushahidi, wanampinga katika rehma hizi. Aidha, Haadimi akielezea 'maafa yanayosababishwa na ulimi', aliandika: "Tamko 'kwa haki ya mtume wako au walii' humaanisha kwamba utume wake au uwalii wake ni wa kweli. Mtume wetu "swallallahu alaihi wa sallam", nae akiwa na nia hii alisema "Kwa haki ya mtume wako Muhammad na nyakati za vita alimuomba Allahu taala kumsaidia kwa haki ya maskini miongoni mwa Muhaajiriin. Aidha, kulikuweko wanazuoni wengi wa kiislamu walioomba: "kwa ajili ya watu hao ambao umewapa yale yote waliokuomba", na "Kwa haki ya

Muhammmada al-Ghazali”, na waliandika dua hizi katika vitabu vyao”. Kitabu kiitwacho **Hisn al-Hasiin** kimejawa na dua kama hizo. Tafsiri ijulikanayo kama **Ruuhul Bayaan** ikielezea aya ya themanini ya Sura Al-Maidah inasema kwamba hadithi iliyopokelewa na Umar al-Faaruuq inasema **“Adam "alaihis-salaam" alipokosea, alisema: “Ewe Mola wangu, nisamehe kwa ajili ya Muhammad "alaihis-salaam". Na Allahu** taala **akasema; ‘Sijamuumba bado Muhammad. Unamjuaje? Alisema: “Ewe Mola wangu! Uliponiumba na ukanipa roho yako, nilitazama nikaona tamko ‘Laailaaha ill- Allahu Muhammadun Rasuulullah’ limeandikwa kwenye pambizo za Arsh. Ni jina la umpendae zaidi ndilo ambalo lingeandikwa karibu na jina lako. Kwa kuzingatia jambo hilo, nilijua kwamba unampenda sana’. Kutokana na jibu hilo, Allahu** taala **alisema: “Ewe Adam! Unasema ukweli. Miongoni mwa viumbe wangu, yeye ndie nimpendae zaidi, hivyo nimekusamehe kwa ajili yake. Asingalikuwapo Muhammad, nisingalikuumba wewe”**. Hadithi hii imenukuliwa na Imam al-Baihaqi katika kitabu chake kiitwacho **Dalaa’il** na Aluusi katika **Ghaaliyya**.

Mawahabi wameeleza kuwa “Imam Zayn al-‘Abidin ‘Ali "rahmetullahi alaih" alimuona mwanamume akiomba dua karibu na kaburi la mtume "swallallahu alaihi wa sallam" akamkataza kwa kumnukulia hadithi, **“Nisalieni popote mlipo. Hakika rehma zenu zitanifikia”**. Huelezea tukio hilo kimakosa na huendelea kusema. ‘Kwa hio, imeharamishwa kukaribia kaburi la mtume kwa ajili ya kuomba dua na kumsalia, jambo ambalo hufanana na kuyafanya makaburi mahala pasherehe.

Imeharamishwa kwa hao ambao wanaenda kusali katika msikiti wa mtume kukaribia kaburi hilo kwa ajili ya kutoa salamu. Hakuna yeyote miongoni mwa maswahaba aliefanya hivyo na waliwazuia wale waliotaka kufanya hivyo. Hakuna kitendo kingine kitakachowasilishwa kwa mtume isipokuwa rehma na salamu zitolewazo na umma wake”. Alieleza pia kuwa Serikali ya Saudi Arabia iliwaweka askari karibu na kaburi la mtume "swallallahu alaihi wa sallam" ili kuwazuia Waislamu kufanya hivyo.

Hadhrat Yusuf an-Nab‘hani alikanusha uongo huo katika sehemu nyingi za kitabu chake. “Imam Zayn al-‘Abidiin "rahmatullahi alaih" hakuharamisha kitendo cha kufanya ziara kwenye kaburi la mtume "swallallahu alaihi wa sallam". Lakini aliharamisha tabia ya utovu wa heshima ambayo sio ya kiislamu wakati wa ziara. Mjukuu wake Imam Ja’faras-Siddiiq, alikuwa akitembelea Hujrat as-Sa’ada na kutoa salamu na kusema kwamba ‘kichwa chake chenye kheri kiko upande huu’,

akiwa amesimama karibu na nguzo iliyoko upande wa Raudhat al Mutwahhara. Maana ya tamko “Msifanye kaburi langu mahala pa sherehe” ni ‘msitembelee kaburi langu katika baadhi ya siku kama vile siku kuu. Nitembeleeni mara kwa mara’. Abu Abdillahi al-Qurtubi ameandika katika kitabu chake kiitwacho at-Tadhkira kwamba “Vitendo vya umma wa mtume "swallallahu alaihi wa sallam" huwasilishwa kwake kila asubuhi na kila jioni”. Khalifa Mansur, alipokuwa akitembelea kaburi la mtume "swallallahu alaihi wa sallam" alimuuliza Imam Malik, ‘Je, niangalie kaburi au kibla?’ Imam Malik akasema: ‘Unawezaje kumpa kisogo mtume wa Allahu taala "swallallahu alaihi wa sallam" ilhali kughufuriwa kwako na kwa babaako Adam ni kwa ajili yake?’ (Taz. Kurasa za 88 na 106). Hadithi isemayo “Tembeleeni makaburi”, ni amri. Kama kuna haramu ambayo hufanyika wakati wa ziara, basi haramu hio ndio inayokatazwa na sio ziara yenyewe. (Taz. Kurasa za 89, 116). Imam an-Nawawi anasema katika **Adhkaar** kwamba ‘Ni sunna kutembelea makaburi ya mtume na waislamu wachamungu mara kwa mara na kukaa karibu na mahali hapo pa ziara kwa muda fulani’. (Taz. Ukurasa wa 92). Ibn Humaam katika Fath al-Qadiir huinukuu hadithi iliyopokelewa na Dara Qutni na Al-Bazzaar isemayo kwamba “Mtu akinitembelea kwa nia ya kunitembelea tu na sio kufanya kitu kingine, atastahiki utetezi wangu siku ya kiama”. (Taz. Ukurasa wa 98). Allahu taala aliwafadhili mawalii kwa karaamat. Karaamat zao hushuhudiwa mara kwa mara hata baada ya kufa kwao. Wanaweza kuwa wenye manufaa hata baada ya kufa. Inaruhusiwa kuwafanya watetezi mbele ya Allahu taala. Hata hivyo, wanapaswa kuombwa msaada kwa njia inayowiana na Uislamu. Hairuhusiwi kusema ‘Nitakupa kiasi fulani kama utanipa ninachoomba’, au ‘Ukimponya jamaa yangu’, kauli ambazo hutolewa mara kwa mara na wajinga. Pamoja na hayo, jambo hili haliwezi kuchukuliwa kuwa ni kitendo kinachoweza kusababisha kukufuru au ushirikina kwani hata zuzu hawezi kumtarajia walii kuumba kitu. Anamtaka walii awe sababu katika uumbaji wa Allahu taala. Anadhani kwamba walii ni mwanaadamu ambae hupendwa na Allahu taala na humuomba: ‘Tafadhali! Niombee kwa Allahu taala ili aniwezeshe kufikia matamanio yangu; kwani hawezi kukataa dua yako’ (Taz. Ukurasa wa 100). Kwa kweli, mtume "swallallahu alaihi wa sallam" alisema: “Kuna watu wengi wanaochukuliwa kuwa wenye hadhi ya chini na kwa hiyo si wenye kuthaminiwa lakini ni waja wa Allahu taala awapendao. Wakitaka kitu, Allahu taala hukiumba’. Waislamu huwaomba mawalii kuwatetea kwa kufuata hadithi kama hizo. Imam

Ahmad, Imam ash-Shaafi'i, Imam Malik na Imam mkuu Abu Hanifa "rahmetullahi alaih" walisema kwamba inajuzu kutabaruku kupitia makaburi ya wachamungu. Wanaodai kuwa ni wa Ahl as-Sunna au kwamba wanafuata dhehebu fulani kati ya madhehebu ya Ahl as-Sunna, wanapaswa kufuata maoni ya maimamu hawa na kama si hivyo tutawachukulia kuwa waongo na sio wasunni" (Taz. Ukurasa wa 118).

Imeandikwa katika al-Fataawa al-Hindiyya, chini ya mada inayohusu kumfanyia hija mtu mwingine kwamba: 'Inaruhusiwa kumzawadia thawabu za ibada mtu mwingine. Kwa hiyo, thawabu za sala; saumu; zaka; hija kusoma Quran; dhikri; kutembelea makaburi ya mitume, mashahidi, mawalii waislamu watenda wema; kutoa sanda kwa ajili ya maiti na thawabu za zawadi zote na matendo mazuri yanaweza kutolewa kama zawadi". Kinachoeleweka katika aya hii pia ni kwamba kutembelea makaburi ya mawalii huleta thawabu.

Ushahidi wa yale yaliyoandikwa kufikia sasa, umeandikwa kwa mapana katika vitabu vyetu vya Kiarabu na Kiingereza. Allahu taala anawaamrisha Waislamu kuungana. Kwa hiyo, Waislamu wote wanapaswa kujifunza imani ya Ahl as-Sunna wal Jamaa'a na waungane kwenye njia ya kweli kwa kuamini kama inavyofundishwa katika vitabu vya wanazuoni hawa wa ahlusunna. Njia pekee iliyo sahihi ni njia ya Ahl as-Sunna. Tunapaswa kuwa waangalifu sana tusitoke kwenye umoja wa Ahl as-Sunna wala tusidanganyike na maandishi ya waasi wanaotaka kuwadanganya waislamu.

Allahu taala ameeleza waziwazi katika Sura An-Nisaa aya ya 114 kwamba wale wanaupa kisogo umoja wa Waislamu wataingia katika moto wa Jahannam. Ni wazi kutokana na nyaraka na marejeleo kwamba yeyote asiyejiunga na moja wapo ya madhehebu ya ahlu al haqaii huwa kajitenga na umoja wa Ahl as-Sunna na kwamba mtu kama huyo, asiyefuata madhehebu atakuwa muasi au kafiri. Kitabu cha at-Tawassulu bin-nabii wa Jahaalat al-Wahhabiyiin huthibitisha kwa mifano na ushahidi kuwa Ibn Taymiyya alijitenga na Ahl as-Sunna wa al-Jamaa'a. Uwahabi ni mchanganyiko wa kaulii za Ibn Taymiyya na uongo na kashfa za Hempher, kachero wa Uingereza.

3- Mawahhabi husema kwamba kujenga kuba juu ya kaburi, kuwa washia taa za mafuta wale wanaoabudu na kutumikia kwenye makaburi na kutoa nadhiri kwa kutolea sadaka roho za wafu ni ukafiri na ushirikina! Wakazi wa Haramu mbili (Makka na Madina) wamekuwa wakiabudu kuba na kuta hadi sasa". Kujenga kuba juu ya kaburi ni haramu ikiwa ni kwa ajili ya kuonyesha ufahari na kupamba. Ikiwa ni

kwa ajili ya kuhifadhi kaburi kutokana na uharibifu, basi kitendo hicho huwa makruhu. Ikiwa imekusudiwa kwamba lisije likavunjwa na mwizi au mnyama, basi inaruhusiwa. Lakini pasifanywe mahali pa kutembelewa, yaani mtu asiseme kwamba panapaswa kutembelewa nyakati kadhaa wa kadhaa.

Ni haramu kuzika maiti katika jengo lililojengwa kabla. Masahaba walimzika mtume "swallallahu alaihi wa sallam" na makhalifa wake wawili ndani ya jengo. Hakuna yeyote kati yao aliyepinga kitendo hicho. Hadithi hutueleza kuwa makubaliano yao hayakujengwa juu ya uasi. Mwanazuoni wa Kiislamu maarufu, Ibn Abidin aliandika: “Ni makruhu kufunika kaburi kwa nguo na kuweka juu yake vilemba vya Waislamu wachamungu au mawalii. Kitabu kiitwacho Fataawa al-Huja kinasema kwamba ni makruhu kufunika kaburi kwa nguo. Lakini maoni yetu ni kwamba si makruhu ikiwa imekusudiwa kuonyesha kila mtu ukubwa wa yule alioko kaburini au kuzuia kuudhiwa au kuwakumbusha wale wanaomtembelea wawe na heshima na adabu. Vitendo visivyo haramishwa katika al-adillat ash-shari‘yya vinapaswa kuhukumiwa kulingana na kilichokusudiwa. Ijapokuwa katika enzi ya masahaba hakuna kuba zililojengwa kwenye makaburi wala kuweka juu yake majeneza ya mawe au nguo, lakini hakuna yeyote kati yao aliyepinga maziko ya mtume "swallallahu alaihi wa sallam" na makhalifa wake wawili ndani ya chumba. Kwa sababu hiyo, na kwa ajili ya kutekeleza amri isemayo ‘Msikanyage makaburi’ na ‘Msionyeshe utovu wa heshima kwa maiti zenu‘. Na kwa vile vitendo hivyo havikuharamishwa, haviwezi kuwa bid’a eti kwa sababu vilitendwa na vizazi vya baadae. Vitabu vyote vya fiqhi hueleza kuwa punde tu baada ya tawaaf ya mwisho inafaa kutoka kwenye al-Masjid al-Haraam ili kuiheshimu Kaaba tukufu. Hata hivyo, masahaba hawakupaswa kufanya hivyo kwa sababu daima walikuwa wakionesha heshima kwa Kaaba. Lakini kwa vile vizazi vilivyofuatia havikuweza kuonesha heshima, wanazuoni wetu walitangaza kuwa ilifaa kuonesha heshima kwa kuondoka kwenye msikiti. Hivyo, walituwezesha kuonesha heshima kwa masahaba watukufu. Hivyo Hivyo, iliruhusiwa kufunika makaburi ya watu wema (swaalihiin) na mawalii kwa nguo au kujenga kuba juu yake ili kuonesha heshima kama walivyofanya masahaba. Mwanazuoni mkuu ‘Abd al-Ghanii an-Nabluusi ameeleza haya kwa ukamilifu katika kitabu chake Kashf an-Nuur”. Huko Uarabuni, makaburi yanaitwa ‘mashhad’. Mjini Madinat al-Munawwara, kulikuwa na mashhad mengi kwenye makaburi ya Baqii. Wale wasiofuata madhehebu waliyaharibu. Hakuna mwanazuoni wa

kiislamu aliewahi kusema kwamba ingekuwa ukafiri au ushirikina kujenga kuba juu ya makaburi au kuyatembelea. Hakuna aliewahi kuonekana akivunja makaburi.

Ibrahim al-Halabi "rahmatullahi alaih" aliandika mwishoni mwa kitabu kiitwacho al-Halabii al-Kabiir “Mtu akiamua kwamba ardhi yake itakuwa mahali pa kuzika maiti (makaburini) na kama ndani yake kuna mahali patupu, inaruhusiwa kujenga kaburi lenye kuba ndani yake kwa nia ya kumzika maiti fulani. Ikiwa hakuna mahali patupu, kaburi hili litavunjwa na makaburi ya kawaida yatachimbwa mahali pake.

Hii ni kwa sababu ni mahali pa wakfu palipotengewa kwa ajili ya makaburi”. Kama kujenga makaburi yenye kuba ingekuwa shirk (ushirikina), au kama makaburi yenye kuba yangechukuliwa kuwa masanamu, ingekuwa ni lazima kuyavunja. Kaburi la kiislamu la kwanza kuwepo duniani ni la al-Hujrat al-Mu’attara ambapo mtume wa Allahu taala alizikwa. Bwana wenu mtume alifia katika chumba cha mpenzi wake, mama yetu Aisha "radiyallahu anha", siku ya Jumatatu kabla ya adhuhuri, tarehe 12 Rabi’ ul-Awwal, mwaka wa 11H. Alizikwa katika chumba hicho majira ya usiku. Hadhrat Abu Bakr na Hadhrat Umar "radiyallahu anhuma" walizikwa katika chumba hicho hicho. Hakuna sahaba aliepinga kitendo hicho. Sasa, itifaki hii ya masahaba watukufu inapingwa. Hata hivyo, kukanusha Ijmaa ya umma kutokana na ufasiri potofu wa ushahidi hausababishi ukafiri, bali husababisha bid’a.

Chumba cha Hadhrat ‘Aisha kilikuwa na urefu wa mita tatu, upana upatao mita tatu na kilijengwa kwa matofali yaliyokaushwa kwa jua. Kilikuwa na milango miwili, mmoja upande wa magharibi na mwingine upande wa kaskazini. Khalifa Umar "radiyallahu anhu" alikizungushia chumba hicho (Hujrat as-Sa’aada) ukuta wa mawe. ‘Abdullah ibn Zubair "radiyallahu anhu" aliuvunja ukuta huo akaujenga upya kwa kutumia mawe meusi kisha akaupiga plasta. Ukuta huu haukuwekewa paa na ulikuwa na mlango mmoja upande wa kaskazini. Hadhrat Hassan "radiyallahu anhu" alipofariki dunia, mwaka wa 49H, ndugu yake Hussein "radiyallahu anhu" aliupeleka mwili wake kwenye Hujrat as-Sa’aada, kulingana na wasia wake wa mwisho, na akataka upelekwe mwili wake kwenye kaburi kwa ajili ya maombezi lakini baadhi ya watu walimzuia wakifikiria kwamba maiti angezikwa katika makaburi hayo. Kwa hiyo, ili kuzuia ghasia, maiti hakupelekwa ndani ya makaburi hayo na badala yake alipelekwa na kuzikwa kwenye makaburi ya Baqii. Ili kuzuia tukio kama hilo, milango yote (ile miwili ya chumbani na mmoja uliokuwa kwenye ukuta) ilizibwa.

Walid, Khalifa wa sita wa dola la Umayya, alipokuwa Gavana wa Madina, aliinua ukuta na kuuzungushia chumba huku akikifunika kwa kuba dogo. Alipokuwa Khalifa, alimuamrisha Umar ibn Abdul- Aziiz, akiwa Gavana wa Madina, kuupanua msikiti mtukufu mwaka wa 88H/ 707 A.D.. Hivyo, chumba hicho kilizungushwa na ukuta wa pili. Ukuta huu ulikuwa wenye umbo la pembe tano na paa na haukuwa na milango.

Kwa mujibu wa “Fath al-Majiid“ atafutae baraka kutoka kwenye mti, jiwe, kaburi, au kitu kinginecho hua mshirikina. Makaburi yamefanywa masanamu kwa kujengewa kuba juu yake. Watu wa enzi za Jahiliyya waliwaabudu wachamungu na masanamu pia. Leo hii, watu kama hao hutenda vitendo zaidi ya hivyo kwenye madhabahu na makaburi. Kutafuta baraka kutoka kwa makaburi ni sawa na kuabudu sanamu liitwalo Laat. Washirikina hawa wanadhani kuwa mawalii husikia na kujibu dua zao. Wanasema kwamba huwakaribia maiti kwa kuweka nadhiri na kutoa sadaka kwa makaburi. Vitendo hivi vyote ni vya ushirikina mkubwa. Mshirikina hua mshrikina hata kama atajiita kitu kingine. Kumuomba maiti kwa utiifu na unyenyekevu, kuwachinjia wanyama, kuweka nadhiri, na vitendo vingine vyote ni ushirikina hata kama vitapewa majina mengine. Leo hii, mshirikina huadhimisha na kutafuta baraka kutoka kwa makaburi wakidai kuwa inaruhusiwa kufanya hivyo. Hayo ni makisio ya uongo.

Tumeshatafsiri majibu yaliyotolewa na wanazuoni wa Kiislamu kwa kashfa hizo zenye kuchukiza zinazowalenga waislamu wa Ahl as-Sunna na kuyaandika kwenye vitabu vyetu kadhaa. Aya ifuatayo imetafsiriwa kutoka katika sura ya kwanza ya kitabu kiitwacho Al-Usuul al- arba’a fii tardiid al-Wahhaabiyya ili kumuonyesha msomaji muangalifu kwamba mawahhabi wamejidanganya na watasababisha maangamizi:

“Quran tukufu, Hadithi, kauli za Salaf as-Saalihiin na nyaraka nyingi za wanazuoni hudhihirisha kuwa inaruhusiwa kumuadhimisha mtu. Aya ya 32 na Sura Al-Hajj inasema: “Ndiyo hivyo! Na anayetukuza ibada za Allahu taala, basi hayo ni katika unyenyekevu wa nyoyo”. Kwa hiyo, ni wajib kuziheshimu sha’aair za Allahu taala. Sha’aair maana yake ni ishara. Abdulhaqq ad-Dahlawi "rahmatullahi alaih" alisema: “Sha’aair ni wingi wa sha’iira ambayo humaanisha ishara (alama). Chochote kinachomkumbusha mtu mola wake ni sha’iira ya Allahu taala. Aya ya 158 ya Suratul Baqarah inasema “Hakika vilima vya Safaa na Marwa ni katika alama za Allahu taala ”. Aya hii hudhihirisha kuwa milima ya Safaa na Marwa si ishara pekee za Allahu taala, lakini pia kuna ishara nyiginezo na sehemu kama vile ‘Arafa, Muzdalifa na Mina haziwezi

kusemekana kuwa ni ishara pekee za Allahu taala. Shaah Waliyyullah ad-Dahlawi "rahmatullahi alaih" ameeleza katika kitabu chake kiitwacho Hujjat Allahi al-Baaligha, ukurasa wa 69 kwamba “Sha’air za Allahu taala ambazo ni kubwa zaidi ni Quran tukufu, Kaaba tukufu, mtume "swallallahu alaihi wa sallam" na ibada ya sala”. Na katika kitabu chake kiitwacho Altaaf al Quds, Shah Waliyyullahi ad-Dahlawi "rahmatullahi alaih" anasema “Kupenda Sha’aair za Allahu taala maana yake ni kuipenda Quran tukufu, mtume "swallallahu alaihi wa sallam" na Kaaba au kupenda kitu chochote kinachoweza kukukumbusha Allahu taala. Ni sawa na kuwapenda mawalii”. Ikiwa milima miwili iliyoko karibu na msikiti mtukufu, yaani Saffa na Marwa ambapo Hadhrat Hajira, maamake mtume Ismail alitembea, ni miongoni mwa Sha’aair za Allahu taala na zinaweza kumpelekea mtu kumkumbuka mama huyo aliebarikiwa, kwa nini mahali alipozaliwa mtume Muhammad mbora wa viumbe na kipenzi cha Allahu taala, akalelewa, akamwabudu Allahu taala, akahamia, akaswalia, akafia na kaburi lake na mahali walipo jamaa zake na maswahaba zake pasichukuliwe kuwa miongoni mwa sha’aair? Kwa nini wanaharibu sehemu hizi.

Quran ikisomwa kwa makini na bila upendeleo, itabainika kwa wepesi kwamba aya nyingi huelezea rehma ya kumuadhimisha mtume "swallallahu alaihi wa sallam". Sura Al-Hujurat inasema “Enyi mlioamini! Msitangulie kitu chocote kile mbele ya Allahu taala na mtume wake, na mcheni Allahu taala. Hakika Allahu taala ni mwenye kusikia, mwenye kujua. Enyi mlioamini! Msinyanyue sauti zenu kuliko sauti ya nabii, wala msiseme nae kwa kelele kama mnavyosemezana nyinyi kwa nyinyi, visije vitendo vya amali njema mnazo zifanya vikaharibika na hali hamtambui. Kwa hakika wanaoteremsha sauti zao mbele ya Mtume wa Allahu taala, hao ndio Allahu taala amezisafisha nyoyo zao kwa uchamungu. Hao watakuwa na maghfira na ujira mkubwa. Hakika hao wanaokuita nawe uko nyuma ya vyumba, wengi wao hawana akili. Na lau wao wangelingojea mpaka ukatoka nyumbani kwako ingelikuwa kheri kwao. Na Allahu taala ni Mwenye maghfira, Mwenye kurehemu”. Inambainikia wazi mtu anayesoma na kuzingatia aya hizo tano jinsi Allahu taala anavyomsifu na kumwadhimisha kipenzi chake Mtume na jinsi anavyouamrisha umma kumheshimu na kutokuwa na majivuno mbele yake. Kiasi cha umuhimu wake unaweza kukadiriwa na ukweli kwamba matendo ya wale wanaopiga kelele wakiongea naye yatabatilishwa. Aya hizi ziliteremshwa kama adhabu kwa watu sabini wa kabila la Bani Tamiim waliomwita mtume huko Madina kwa kupiga kelele hali ya kuwa hawamuoneshi heshima.

Leo hii kuna wanaodai kuwa wao ni kizazi cha Bani Tamiim. Hao ndio mtume aliwakusudia aliposema “Watu wakali na watesaji wako mashariki”, na “Shetani atazua mfarakano kutoka kule”. Alisema hivyo huku akiashiria kwa kidole chake eneo la Najd [lililoko katika kisiwa cha Uarabuni.] Baadhi ya watu wasiofungamana na madhehebu ni Wanajid walioenea kutoka huko. Mfarakano uliobashiriwa kwenye hadithi hiyo ulijitokeza baada ya miaka elfu moja mia mbili. Walitoka Najd, wakaelekea Hijaz huku wakipora mali za waislamu, wakiua wanaume na kuwachukuwa mateka wanawake na watoto. Walitenda maovu mengi sana kuliko makafiri.

**KUNA NINI ZAIDI**. Katika aya zilizotajwa hapo juu, kauli iliyorudiwa rudiwa isemayo kwamba “Enyi mlioamini”, hudhihirisha kuwa waislamu wa karne zote hadi siku ya kiama, wamehimizwa kumheshimu mtume wa Allahu taala "swallallahu alaihi wa sallam". Amri hiyo ingalikuwa kwa masahaba "radiyallahu anhum ajma’in" peke yao, ingalielekezwa kwao “Enyi masahaba”. Kwa kweli, kauli zisemazo “Enyi wake za mtume!” na “Enyi watu wa Madina!” ni za Qurani. Kauli hiyohiyo “Enyi mlioamini hutumika katika aya zinazotaja sala, kufunga, hija, zaka na vitendo vingine vya ibada ambavyo ni fardh kwa waislamu hadi siku ya kiama. Ama wazo la wawahhabi kwamba mtume "swallallahu alaihi wa sallam" alipaswa kuheshimiwa alipokuwa hai na kwamba hapaswi kuheshimiwa au kuombwa msaada baada ya kufariki kwake dunia, wazo hili halina ukweli kwa mujibu wa aya hizi.

Aya zilizotajwa hapo juu huashiria kuwa ni muhimu pia kumuadhimisha asiyekuwa Allahu taala. Katika Sura Al-Baqarah, aya ya 104 tunaambiwa kwamba “Enyi mlioamini! Msiseme ‘Raa’ina’ (tamko lenye maana ya kuapa, kutia ila katika lugha ya Kiyahudi. Wayahudi walitumia neno hili kumkejeli mtume kwa maana hio. Kutokana na maana hiyo mbaya, Allahu taala aliwazuia waumini kutumia neno hilo).

Sura Al-Anfal, aya ya 33 inasema “Na Allahu taala hakuwa mwenye kuwaadhibu hali ya kuwa na wewe umo pamoja nao, wala Allahu taala si mwenye kuwaadhibu na hali ya kuwa wanaomba msamaha” na ameahidi kwamba hatowaadhibu mpaka siku ya kiama itakapowadia. Aya hii hupinga madai ya mawahhabi kwamba mtume alitoweka na kuwa udongo.

Suratul Baqarah aya ya 34 inasema “Na kumbuka tulipowaambia malaika ‘Msujudieni Adam’, wakasujudu wote isipokuwa Iblisi”. Aya hii hudhihirisha kuwa Adam "alaihis-salaam" anapaswa kuadhimishwa. Shetani alikataa kuonesha heshima kwa asiyekuwa Allahu taala

akawakashifu mitume na kwa kufanya hivyo akawa ameasi amri hii. Wawahhabi wamefuata nyayo za shetani. Wazazi wa Yusuf "alaihis-salaam" na ndugu zake, pia walimwonesha heshma kwa kumsujudia. Kama kumheshimu kiumbe ungekuwa ushirikina, basi asingewaadhimisha waja wake kwa tamko ‘sajda’ (kusujudu) akielezea mambo yanayowahusu.

Kwa mujibu wa Ahl as-Sunna, kumsujudia asiyekuwa Allahu taala ni haramu kwa sababu kitendo hicho hufanana na kusujudu kunakojikita katika ibada na sio ishara ya heshima! Shetani alikuwa akijitokeza mara kwa mara mbele ya mtume "swallallahu alaihi wa sallam" katika umbo la mzee wa kutoka Najd. Makafiri walipokusanyika mahali pajulikanapo kama Dar un-Nadwa huko Makka, wakaamua kumuua mtume, shetani alijitokeza akiwa kwenye umbo la mzee wa Najd akawafundisha jinsi ya kutekeleza mauaji na wakakubali kufanya jinsi alivyowambia mzee huyo wa Najd. Tangu siku hiyo, shetani amekuwa akiitwa sheikh an-Najdi. Hadhrat Muhyiddin Ibn Al-‘Arabi ameandika katika kitabu chake kiitwaacho **al-Musaamaraat** kwamba: “Makafiri wa Kiquraish walipokuwa wakiifanyia ukarabati Kaaba, kila mmojawapo wa viongozi wa makabila alisema yeye ndie atakayeliweka tena jiwe lenye thamani lijulikanalo kama Hajarul-Aswad mahali pake. Baadae wakakubaliana kuwa mtu atakaekuja mapema asubuhi ndie atakaempendekeza mtu wa kuliweka jiwe hilo mahala pake akimchagua mmoja wao. Mtume wa Allahu taala ndie alikuwa wa kwanza kuwasili. Wakati huo alikuwa na umri wa miaka ishrini na tano na walisema kwamba wataufuata ushauri wake kwa sababu alikuwa mwaminifu (Amiinu). Alisema: “Leteni zulia na mueke jiwe juu yake. Shikilieni pembe za zulia halafu mlibebe mpaka mahali ambapo jiwe hilo litawekwa”. Baada ya kufika mahali hapo, alilichukuwa kutoka kwenye zulia kwa mikono yake yenye baraka akaliweka mahali pake kwenye ukuta. Wakati huo, shetani alijitokeza akiwa kwenye umbo la sheikh an-Najdi akasema huku akiashiria jiwe fulani “Wekeni hili pembezoni mwake ili liegemee juu yake”. Kusudio lake hasa lilikuwa lile jiwe baya aliloashiria likianguka siku za mbele, lilifanye al-Hajar al-Aswad lisiwe imara na kwa hiyo limtie doa mtume "swallallahu alaihi wa sallam". Alipotambua njama hio, mtume alisema “Audhu billahi minashshaitwanir-rajiim”, shetani akatoweka mara moja’. Kwa vile Muhyiddin Ibn al-Arabi "rahmatullahi alaih" aliujulisha ulimwengu kwamba sheikh An Najdi alikuwa shetani, watu wasioegemea madhehebu humchukia walii huyu mkuu. Kwa kweli, wanamwita kafiri. Kinachoeleweka kutokana na aya hizo ni kwamba kiongozi wao alikuwa shetani. Kwa sababu hio, wanaharibu

sehemu takatifu zilizorithiwa kutoka kwa mtume wa Allahu taala "swallallahu alaihi wa sallam". Wanasema kwamba sehemu hizo huwafanya watu washirikina. Kama kusalia katika sehemu takatifu kungekuwa ushirikina, Allahu taala asingetuamrisha kuhiji, mtume wa Allahu taala asingebusu jiwe jeusi (al-Hajar al-Aswad) alipokuwa akifanya tawaf, hakuna mtu ambae angesalia Arafa na Muzdalifa, mawe yasingetupwa huko Mina na waislamu wasingetembea baina ya Safa na Marwa. Sehemu hizi tukufu zisingeheshimiwa kiasi hicho.

Sa’d ibn Mu’adh, kiongozi wa waansari alipofika mahali ambapo walikuwa wamekusanyika, mtume "swallallahu alaihi wa sallam" aliwambia “Simameni kwa ajili ya (kumheshimu) kiongozi wenu” Amri hii ilikusudiwa kuwahimiza wote wamuheshimu Sa’d. Ni kosa kusema kwamba Sa’d alikuwa mgonjwa. Kilichokusudiwa ni kwamba wamsaidie kuteremka kutoka kwenye mgongo wa mnyama wake aliemtumia kama chombo cha kusafiria kwa sababu amri ilielekezwa kwa wote. Ingalikuwa kwa ajili ya kumsaidia basi amri ingewahusu tu mtu mmoja au wawili na wangeambiwa wasimame ‘kwa ajili ya Sa’d’ na sio ‘kwa ajili ya kiongozi wenu’.

Ilikuwa kawaida yake Abdullahi ibn Umar "radiyallahu anhu" kila alipokuwa akitoka Madina kwenda Makka kwa ajili ya hija, kusalia katika sehemu alikokuwa akikaa mtume "swallallahu alaihi wa sallam". Alikuwa akipata baraka kutoka kwenye sehemu hizi. Alikuwa akiweka mikono yake kwenye minbari ya mtume "swallallahu alaihi wa sallam" kisha akapangusa uso wake. Imam Ahmad ibn Hanbal "rahmatullahi alaih" alikuwa akiibusu Hujrat as-Sa’aada na minbari kwa ajili ya kupata baraka. Kwa hio, wale wasioegemea madhehebu mara wanasema kwamba wanafuata madhehebu ya Hanbali na mara nyingine wanayachukulia aliyokuwa akiyafanya Imamu huyu kuwa ni ushirikina. Hivyo, inabainika kwamba madai yao kuwa ni wafuasi wa Hanbali ni ya uongo. Imam Ahmad ibn Hanbal aliweka sharti Imam ash-Shaafi’i "rahmatullahi alaih" kwenye maji akanywa maji hayo kwa ajili ya kupata baraka. Abu Ayyub al-Ansaari "radiyallahu anhu" alipangusa uso wake kwenye kaburi la mtume "swallallahu alaihi wa sallam" na akaja akitaka kumnyanyua lakini alimwambia ‘Niache! Sikuja hapa kwa ajili ya mawe wala udongo bali kwa ajili ya hadhira ya mtume "swallallahu alaihi wa sallam".

Masahaba watukufu walikuwa wakipata baraka kutokana na vitu alivyokuwa akimiliki mtume "swallallahu alaihi wa sallam". Walipata baraka kutokana na maji aliyokuwa akitumia kutawadha na kutokana na jasho lake, shati lake, bakora yake, upanga wake, viatu vyake, bilauri

(glasi) yake, pete yake, ilimradi kutokana na kila kitu alichokuwa akitumia. Ummu Salama "radiyallahu anha" mama ya waumini alikuwa akiweka ndevu za mtume. Wagonjwa walipoenda kwake, alikuwa akiweka ndevu hizo kwenye maji ili wanywe kwa ajili ya kupata siha. Kaburi la Imam al-Bukhari "rahmatullahi alaih" lilikuwa likitoa harufu ya marashi na watu walikuwa wakichukuwa udongo kutoka kwenye kaburi hilo ili kupata kubarikiwa nao. Hakuna mwanazuoni au mufti hata mmoja ambae hakuridhia hayo. Wanafiqhi na wanahadithi waliruhusu matendo hayo. Tafsiri kutoka kwenye kitabu kiitwacho **al-Usuul al-Arba'a** huishia hapa. [Katika enzi za masahaba watukufu na Taabi'in, na hata kufikia mileniam ya kwanza, kulikuweko mawalii na swalihiina wengi. Watu walikuwa wakiwatembelea na kupata baraka kutoka kwao na kuombewa dua. Hapakuwa na haja ya kuwafanya wafu watetezi au kutafuta baraka kutokana na vitu visivyokuwa na uhai. Kwa vile matukio haya hayakujitokeza sana, zama hizo, haimaanishi kuwa yalikuwa yameharamishwa. Yangalikuwa haramu, pangalikuwepo watu wa kuyazuia. Hakuna hata mwanazuoni mmoja alieyazuia. Hata hivyo, zama za mwisho zilipoingia, bid'a na dalili za ukafiri zikakithiri. Vijana wamedanganywa na maadui wa Uislamu wanaojifanya wenye mamlaka ya kidini na wanasayansi, na kwa vile kupinga dini na kuritadi huafikiana na malengo yao, madikteta na wakandamizaji, watumwa wa nafsi zao, wameunga mkono kundi hili. Idadi ya wanazuoni na mawalii imepungua kwa hakika, hapakujitokeza yeyote katika miongo ya hivi majuzi na kwa hiyo, ni lazima kutafuta baraka kwenye makaburi na vitu vilivyorithiwa kutokana na mawalii. Pamoja na hayo, kama ilivyo katika mambo yote na vitendo vya ibada, matendo haya yamechafuliwa kwa kuingizwa ndani yake vitendo vya haramu. Kulingana na itifaki ya wanazuoni wa kiislamu, ni muhimu kutakasa matendo ya halali kutokana na bid'a iliyoingizwa ndani yake badala ya kuyapiga marufuku matendo yenyewe. Tazama kitabu kiitwacho 'Advice for the Muslims', mojawapo ya machapisho ya Hakikat Kitabevi, Istanbul Uturuki. Kurasa zake za mwisho hutoa taarifa kuhusu ukatili na mateso ya mawahabi dhidi ya waislamu huko Hijaz. Waislamu huweka mawe juu ya makaburi. Wanaandika majina ya waislamu waliokufa kwenye mawe hayo. Waislamu husoma Suratul Fatihah na dua nyinginezo kwa ajili ya roho za watu ambao majina yao yameandikwa kwenye mawe hayo. Endapo Muislamu atatembelea kaburi la walii, atasoma dua nyingine ambamo ataiomba roho ya walii huyo kumtetea na kumwombea baraka.

# JAMAA’AT TABLIIGH

Kuna kundi la watu ambao wamekuwa wakitembelea nchi mbalimbali za kiislamu na kutoa mawaidha na nasaha kwa waislamu chini ya mwamvuli wa Jamaa’at Tabliigh. Watu hawa wamekuwa wakiizunguka dunia kutoka India na Pakistan wakiwa kwenye makundi ya watu watatu na watano. Wanasema kwamba wanafanya jitihada ya kuueneza Uislamu. Wanadai kwamba wameandama njia ya masahaba. Baadhi yao hudai pia kwamba wanafuata dhehebu la Kihanafi na kuvutiwa na Ibn Taymiyya. Ijapokuwa mengi wasemayo ni yenye manufaa na ni sahihi, kwa vile hawataji asilani majina na maneno ya wanazuoni wa kiislamu, na inaonekana kana kwamba wanaficha baadhi ya elimu ya Ahl as-Sunna, ni suala ambalo huzua wasiwasi na dukuduku. Katika ibara zifuatazo kuna maandishi ya baadhi ya wenye mamlaka wanaoishi India na Pakistan kuwahusu: “Wao ni waasi. Wanajinadi kuwa Jamaa’at Tabligh. Makao yao yako Delhi [wakiwa na matawi makubwa huko Karachi na Lahore nchini Pakistan]. Popote waendapo, huwa wanasisitiza kusali. Hutoa maalumaati yenye manufaa na umuhimu mkubwa. Shughuli hizi zinarejelewa kama ‘kast’ kwa lugha ya Kiurdu. Inasemekana kuwa, shirika lao liliasisiwa na Mhindi ajulikanaye kama Mawlana Ilyaas. Bwana huyu alizaliwa Kandla mnamo mwaka wa 1303 H./ 1886 A.D.. Alikuwa mwanafunzi wa Rashid Ahmad Gangohi. Imeelezwa katika kitabu kiitwacho Maulana Ilyas Uranki Dini Da’wat kilichoandikwa na mmoja wa wanafunzi wa Ilyaas, kwenye ukurasa wa 43 na 49 kwamba alikaa naye kwa miaka kumi. Rashid Ahmad alipofariki, mwaka wa 1346 H./ 1905 A.D., alifundishwa na Khalil Ahmad Saharanpuri. Katika kitabu chake cha Kiurdu, Khalil Ahmad [aliyefariki mwaka wa 1346 H./ 1928 A.D., mjini Madina] anasema kwamba shetani ni mwenye ujuzi zaidi kuliko mtume wa Allahu taala. Rashid Ahmad alisema kwenye kitabu kiitwacho **Baraahin Qat’iyya** ukurasa wa 51 kwamba kitabu cha Khalil Ahmad kilikuwa kimebarikiwa na alikiweka mahali panapojulikana kama **‘Baitul ’ain-I Islam’**. Rashid Ahmad alikuwa Khalifa wa Haji Imdadullah al-Madani [aliyefia Makka mwaka wa 1317 H./ 1899 A.D.] na mwanzoni alifundishwa na Isma’il Dahlawi aliyeandika kwenye kitabu kiitwacho Taqwiyat al-Iman ambacho ni tafsiri ya Kiurdu ya Kitabut Tawhid cha Ibn Abdul Wahhab, ukurasa wa 38 kwamba mtume alikufa na mwili wake ukaoza akawa udongo. Yeyote anayeamini kuwa atawatetea watu siku ya kufufuka huwa mshirikina. Mwalimu mwingine wa Ilyas

alikuwa Ashraf Ali Tahanawi aliyekuwa khalifa wa Haji Imdadullah wa Tariiqa ya Chishtiyya. Katika sehemu ya kwanza ya kitabu chake cha Kiurdu kiitwacho **Hifz al-Iman**, ameandika mambo ya kuchukiza yanayoshusha hadhi ya Mtume hadi kiwango cha chini cha mtoto, mwendawazimu au wanyama. Walimu wote wa Ilyas walikufuru kwa sababu ya maandishi yao. Ilyas huwasifu, huwaadhimisha na kuwaheshimu kupita kiasi makafiri hawa.

Anasema kwamba wao ni mawalii watukufu zaidi wa zama hizo. Ukurasa wa 114 wa kitabu chake kiitwacho **Malfuzaat Hadhrat Mawlana Ilyas rahmatullahi alaihi** kimejawa na sifa kama hizo. Kuhusu mwalimu wake Ahmad, anasema "Nisingalimwona, moyo wangu usingalipata utulivu. Kila nilipoamka usiku, nilikuwa nikienda chumbani kwake nikautazama uso wake kisha nikarudi nikaenda kulala. Upendo wake umepenya katika kila sehemu ya mwili wangu kama damu kwenye mishipa yangu" (Taz. Mawlana Ilyas Uranki, ukr 44 na 49). Allahu taala amesema katika aya ya mwisho ya Sura Al-Mujadilah kwamba "Huwakuti watu wanaomuamini Allahu taala na siku ya mwisho kuwa wanawapenda wanaompinga Allahu taala na Mtume wake, hata wakiwa ni baba zao, au watoto wao, au ndugu zao, au jamaa zao". Wafuasi wote wa Jamaa'at Tabliigh hutilia chumvi na kumsifu sana Ilyas na walimu wake na wanapotaja au kusikia majina yao wanasema: 'rahmatullahi alaih'. Wanasambaza vitabu vyao vilivyotajwa hapo juu kila mahali.

Ilyas alipofarki dunia mwaka wa 1363 H./ 1949 A.D., alirithiwa na mtoto wake Muhammad Yusuf Kandlavi [aliyezaliwa mwaka wa 1335 H./1917 A.D. mjini Delhi na kufariki dunia mwaka wa 1394 H./ 1974 mjini Lahore akazikwa Delhi]. Kitabu chake cha juzuu nne kiitwacho Hayat as-Swahaba kilitafsiriwa kwa Kituruki kikachapishwa mwaka wa 1395 H./ 1975 A.D.. Kwa vile maswahaba walisifiwa sana katika kitabu hiki kinaibua shauku kwa msomaji. Hata hivyo, kuna msemo mashuhuri kwamba "Mtu anapaswa kuhukumiwa kulingana na vitendo vyake na siyo maneno yake". Yoyote anayeamini kuwa masahaba ni wabora na akawa anawapenda ni sharti afuate njia yao ambayo ndio njia iliyooneshwa na wanazuoni wa Ahl as-Sunna. Dalili ya kuwapenda masahaba ni kujifunza vitabu vya fiqhi vya moja ya madhehebu manne ya Ahl as-Sunna, kupania kusambaza mafundisho yao na kuishi maisha yanayowiana nayo.

Muhammad Yusuf alirithiwa na mtoto wake Shaikh In'am al-Hasan aliyekuwa mwalimu wa hadithi kwenye madrasa ya Mazahir al-Ulum mjini Sahranpur nchini India. Abul Hasan Ali Nadvi, mudiri wa Nadwat

al-Ulamaa [Jumuiya iliyoasisiwa Lucknow, nchini India [mwaka wa 1310 H./ 1891 A.D.] anamsifu al Imam ar-Rabbani Ahmad as-Sirhindi na huduma zake katika kitabu chake kiitwacho ad-Da'wat al-Islaamiyya [Lucknow, 1395H / 1975 A.D.] na husifu zaidi Isma'il Dahlawi [aliyefariki mwaka wa 1320H], Madrasa iliyoko Diobend iliyoasisiwa na Muhammad Qasim Nanawtawi [aliyefariki dunia mwaka wa 1317 H/ 1899 A.D.], Jumuiya ya Tabligh na muasisi wake Muhammad Ilyas. Mwandishi wa kitabu hiki ambaye ni mnyonge mbele ya Allahu taala, amesoma kitabu kiitwacho Taqwiimul Bayaan, tafsiri ya Kifursi ya kitabu cha Isma'il Dahlawi kiitwacho Taqwiyat ul-Iman [kilichochapishwa Pakistan mwaka wa 1396H / 1976 A.D.].

Katika mwezi wa Shawwal mwaka wa 1399H/ 1979 A.D. na kufuatia matoleo ya kila mwezi yaitwayo al-Muallim yanayochapishwa na Jamiyat al-Ulamaa iitwayo 'Samasta' iliyopo Malappuram mji wa taifa la Kerala, kusini mwa India, Mawlawi Abu Ahmad, mmoja wa wanazuoni wa Ahl as-Sunna, aliandika makala yenye anuani "Disclosure of the suspicions about Jamaa'at at-Tabligh" (Ufichuaji wa tuhuma kuhusu Jamaa'at Tabligh).

Makundi mbalimbali ya watu wanaosema kwamba wataihuisha dini na kuisambaza kila mahali, yamejitokeza kaskazini mwa India. Kwa kuzingatia matamko yao ya juu juu, watu wengi huwafuata bila ya kufanya udadisi ama kuchunguza imani ya waasisi wake. Baada ya kuona hali zao za ndani, wameanza kujitenga nao na kudhihirisha uwongo na hila zao. Historia ilishuhudia waasi kama hao ambao hutumikia nafsi zao na fikra zao mbaya. Wameyafasiri kimakosa maandiko ya Uislamu. Huwafiki misimamo mibovu ya Ibn Taymiyya na Muhammad ibn Abd al Wahhab wa Najd. Wenye ujuzi mdogo wa kidini hudhani kuwa wako kwenye njia ya ukweli na kwamba wanatumikia Uislamu.

Huizunguka dunia nzima. Wanaonekana kama washikadini na wachamungu ukiangalia ibada yao, hotuba zao zenye kuvutia, na mavazi yao. Hawazungumzii kamwe imani yao na njia wanayoandama nayo. Walianza kueneza mbegu zao. Wametangaza vita dhidi yao kwa kudhihirisha vitabu vyao, imani yao, asili yao na wasifu wa waasisi wao. Walipovichunguza walielewa hila zao na kugundua kuwa ni watu wa bid'a. Walitoa fatwa kwamba watu hao wameacha njia ya kweli ya Ahl as-Sunna wal Jamaa'a na kuandamana na njia ya bid'a na upotofu. Fatwa hizi za maulamaa wa India kusini na kaskazini na kisiwa cha

Ceylon zilichukuliwa kuwa itifaki ya maulamaa yaani Ijmaa. Nasi tukifuata mwongozo wa Allahu taala na nyayo za salaf as-Salihiin, tutaelezea imani yao mbovu na njia yao potofu.

Muasisi wa kundi hili alikuwa Muhammad Ilyas ibn Isma'il aliyezaliwa mwaka wa 1303 H./ 1886 A.D. na kufariki dunia mwaka wa 1363 H./1944 A.D.. Aliwahi kufundisha kwenye madrasa ya Mazahir al-Ulum. Aliposhindwa hapo, alianza maisha ya usheikh. Alipata kipato chake kutokana na kuandika hirizi na kuwaombea wajinga dua. Wakati huo huo aliasisi Jumuiya ya Tabligh. Jamal Muhammad Sahib, mkuu wa madrasa ijulikanayo kama 'kulliyyat kaid millat' iliyoko Madras, alitoa maelezo kamili kuhusu jumuiya hii katika gazeti la Jandaraka, toleo la Julai mwaka wa 1976. Kiongozi wa Jamaat at-Tabligh yenye makao yake huko Delhi na rafiki yake Muhammad Idris al-Ansaari anaeleza sababu za kuanzishwa kwa jumuiya hii katika kijitabu kiitwacho Tabligh Dustur al- Amal (kilichochapishwa na shirika la uchapishaji la Jamal mjini Delhi). Ukifikiria kwa makini na kuchunguza historia, utagundua kuwa watu hawangeweza kupata amani na furaha kutokana na nguzo nne za kimsingi. Hali hii hueleweka kutokana na aya ya 139 ya Sura Aali-Imran isemayo kwamba "Wala msilegee, wala msihuzunike, kwani nyinyi ndio wa juu mkiwa ni waumini". Kwanza, Uislamu unalenga kubadilisha kipengele cha ndani, yaani imani potofu na tabia. Pili, kuvibadilisha vipengele hivi itawezekana iwapo njia iliyochaguliwa na mitume itazingatiwa. Tatu, kazi zilizokwishafanywa na waislamu hadi sasa katika kiwango cha mtu mmoja mmoja au kwa pamoja hazikuwa kwa ajili ya kutimiza lengo hili na hawakufuata njia ya mitume. Nne, kwa sababu hii, ni muhimu kuanzisha jumuiya ya watu wema (wachamungu), yaani jumuiya ya kiislamu ambayo inapaswa kufanya kazi kulingana na njia (muongozo) iliyodhihirishwa na Uislamu. Sasa, kazi hii hufanyika na Muhammada Ilyas, mmoja wapo wa watumishi wa Allahu taala. Alianzisha jumuiya ijulikanayo kama Jamaa'at Tablighiyya kwa kuwakusanya watu wanaotaka kutoa huduma zao katika njia ya Uislamu. Tazama maneno haya! Kwa mujibu wa kiongozi wa Jamaa'at at-Tabligh, kazi iliyofanywa na umma wa Muhammad na mtu mmoja mmoja au kwa pamoja, kwa kipindi cha miaka elfu moja na mia nne haikufanyika kulingana na mwogozo wa mitume "alaihis-salaam" wala haikulenga kubadilisha imani potofu iliyokuwa imetanda miongoni mwa wanadamu. Kwa hiyo, ilIbidi ianzishwe jumuiya mpya! Wale waliokuwa na hamu ya kuutenganisha umma wa Muhammada na kuanzisha kundi jipya la waasi linalopinga Ahl as-Sunna wamekuwa wakisema maneno kama hayo mara kwa mara wakidai kuwa umma wa

kiislamu umeacha njia ya haki na uokovu, wameasisi makundi mapya. Wameshikilia mitazamo yenye ufisadi na maasi waliyoizua kwa namna hii. Mwengine anayewafanana ni Abu A'la Mawdudi, ambaye hivi majuzi alianzisha jumuiya ijulikanayo kama Jamaa'at Islami nchini Pakistan. Katika ukurasa wa kumi na tano wa kitabu chake cha Kiurdu kiitwacho 'Min Muslimanur maujuduhu siyasi, anaelezea sababu za kuanzishwa kwa Jumuiya hiyo kama ifuatavyo:

Nimefanya uchunguzi na kujifunza mambo mengi. Niliamua kuondoa hazama ya Uislamu iliyoko sasa kwenye shingo yangu. Kama nisingalifanya hivyo, mimi pia ningefuata nyayo za wanaokana dini. Ilhad na Dahriyya [anaturejelea dini za mababu zake kama ilhad na dahriyya]. Kwa hiyo, nimechagua dini mpya inayowiana na maana ya kalimat at-Tawhiid". Alijidai kuwa yeye ndie Muislamu wa kweli wa zama zake na aliilingania dini hii mpya kwa watu wote, waislamu na wasio waislamu. Muhammad Ilyas alisema hayo hayo, akidai kuwa yale yote ambayo umma wa Muhammad uliyafanya haukufuata mwongozo wa Mtume. Muhammada Manzur an-Nu'man, katika ukurasa wa kumi na mbili wa kitabu chake **Malfuzaat** humnukuu akisema: "Yote yale unaofanya umma wa Muhammad hivi sasa unayafanya kulingana na ada na desturi. Wale waliofundisha na kuwaongoza watu katika mambo ya kidini walitegemea mila na desturi. Muhammad Hasan Khan mmoja wapo wa viongozi wa Jama'at at-Tabligh aliandika dibaji ya **Miftah at-Tabligh** ambapo alisema: "Kwa vile mambo ya kidini hayaendeshwi vizuri wakati uliopo, watu wengi wamenaswa na ushirikina uliopo, ukafiri na ukanaji kuwepo kwa Allah (ilhad). Kwa kuwahurumia watu walio kwenye hali hii, Allahu taala alimtuma Sheikh Muhammad Ilyas kama muujiza ili awaamshe waislamu kutoka kwenye ujinga na wapate mwelekeo wa kidini. Mujahid huyu alifanya jitihada ya kuwaamsha watu katika mji wa Mivat, kusini ya Delhi, kadri ilivyoruhusu hali ya zama zake'. Haikuwawia rahisi kujibu swali, je, Ilyas alipata wapi njia ya kweli na hali umma wote ulikuwa kwenye ukafiri na upotofu?

Kwa mukhtasari, kundi la Jama'at at-Tabligh kama mengine yaliyonyanyuliwa hadhi ghafla, linadai kuwa umma wa Muhammad umepotea na kuacha njia ya kweli. Maneno haya ni kinyume na aliyowasilisha mtume wetu "swallallahu alaihi wa sallam" kwa vile alisema katika hadithi iliyopokelewa na Tirmidhi kwamba "Umma wangu hautaungana juu ya upotofu." Hadithi hii huthibitisha kuwa mambo ambayo mujtahidina ama wanazuoni wa kiislamu

wanakubaliana juu yake ni ya ukweli daima. Mtu yeyote mwenye akili timamu, hata kama si mwanazuoni, ataelewa jambo hili.

Yafuatayo ni maelezo kamili kuhusu jama'at at-Tabligh.

"Abul Hasan Ali Nadvi, m taala mu maarufu wa mambo ya kidini na historia nchini India humnukuu mwasisi wa Jama'at Tabligh akisema "nilianza kazi hii nikiwa Madina mwaka wa 1345 H. / 1926 A.D.. Nilipewa habari njema kuwa ufanisi wa jumuia hii utapitia mikononi mwangu". Haya yameandikwa kwa Kiurdu katika kitabu kiitwacho **Mawlana Ilyas Uranki dini Da'wat**, ukurasa wa 77. Katika ukurasa wa 78 imeandikwa kwamba alianza kulingania dini baada ya kurudi India kutoka Madina. Kutokana na mistari miwili iliyonukuliwa, anadai kuwa aliitikia mwaliko huu baada ya kupata amri na habari njema kutoka kwa Allahu taala. Hali ya ndani ya jumuiya hii imeelezewa kwa ukamilifu katika **Malfuzaat Ilyas**. Katika ukurasa wa 50 wa kitabu hiki, Manzur an-Nu'man, mwanafunzi wake, hutoa habari hizi njema kwa marafiki zake "Ru'yaa (ndoto) ni mojawapo ya sehemu 46 za utume. Kupandishwa cheo (taraqqi) ambako inawezekana kusipatikane kupitia riyadha wala mujaahada kunaweza kujitokeza kwa watu wateule kupitia ru'yaa. Mafundisho wanayoyapata kupitia ru'yaa ni sehemu ya utume. Je, kupandishwa cheo hakuwezekani kutokana na mambo haya? Elimu huongeza maarifa na maarifa humsogeza mtu karibu na Allahu taala. Hivyo, Allahu taala alituamrisha kumwomba tukisema "Ewe Mola wangu! Niongezee elimu!" Mwanaadamu hupewa elimu ya kweli akiwa katika ru'yaa. Kwa hiyo, ombeni dua ili kiongozi wenu alale sana. Nikilala kidogo kwa sababu ya kukasirika, nakimbilia kwa tabibu na kutumia dawa anazonipa ili kuongeza usingizi wangu. Njia hii ya kulingania dini kupitia tabligh ilinibainikia kupitia kwenye ndoto. Niliambiwa tafsiri ya aya isemayo kwamba, "Nyinyi mmekuwa umma bora waliotolewa watu kwa kuwa mnaamrisha mema na mnakataza maovu", nikiwa kwenye ndoto. Kama mitume, nimeumbwa kwa ajili ya kulingania dini. Tamko "nimeumbwa" lililoko kwenye aya huashiria kuwa ulinganiaji huu hauwezi kukamilika kwa kuufanyia katika sehemu au mji mmoja, kwamba inafaa kutoka katika sehemu moja kuelekea miji mingine na kutembelea miji kadhaa". Tazama maneno haya! Qurani inatafsiriwa kwenye ndoto na haiwezi kupatikana kupitia riyadha wala mujaahada. Kutokana na neno 'ukhrijat' lililoko kwenye aya anaibua maana ambayo haijaelezewa na mfasiri yeyote. Anawaambia wafuasi wake kufanya jitihada ya kulala sana na anawafundisha mambo mengine mengi kama inavyobainika katika maandishi yake. Je, hiyo si mifano ya kuitafsiri Qurani kulingana na

mtazamo wake binafsi? Mtume wetu aliwaonya waislamu wasifanye tafsiri kama hiyo katika hadithi isemayo: “Jahannamu ni makao ya yule anayeitafsiri Qurani kulingana na maoni yake”. Hadithi hii ilipokelewa na Tirmidhi. Wale ambao hawaoni tofauti kati ya kushoto na kulia wala kutambua faradhi na sunna, husafiri kwa ajili ya kufanya tabligh kulingana na tafsiri hii ya ndotoni. Baada ya Uislamu kuenea kila mahali kutoka mashariki hadi magharibi, kwenda kwao kutoka nyumba hadi nyumba nyingine pia kuliamrishwa kwenye ndoto. Mwanazuoni Ibn Jariri at-Tabariy na wafasiri wengi miongoni mwa Salaf as-Salihiin, waliifasiri aya hii na mwanazuoni Imam as-Suyuuti alizielezea katika kitabu chake Durar al-Mansur. Kwenye ukurasa wa sitini na nne sehemu ya pili ya kitabu hiki, imeelezwa kwamba, “Abdul Hamid ibn Jariir at-Tabariy na ibn Mundhir waliripoti kutoka kwa Imam Mujahid kwamba katika aya “Nyinyi mmekuwa umma bora walioteuliwa miongoni mwa watu”, ‘watu’ ni wale wote ambao si Waarabu na “umma bora” walikuwa Waarabu”. Ni wazi kwamba hakuna m taala mu yeyote wa tafsiri aliyewahi kuitafsiri aya hii jinsi alivyofanya Ilyas. Kwa hio, jumuiya yake ya Tabligh haiafikiani na njia ya Qurani, hadithi na salaf as-Salihiin. Imejengwa juu ya msingi wa tafsiri inayofanyika kwenye ndoto (usingizini). Huu ni uzushi katika Uislamu (bid’a). Mtume wetu "swallallahu alaihi wa sallam" alitangaza kuwa “Azuaye jambo katika dini yetu hii ambalo halimo basi litatupiliwa mbali”. Hadithi hii imenukuliwa katika Sahihain za Bukharin a Muslim. [An-Nablusi pia hutoa maelezo kamili kuhusu mada hii katika ukurasa wa 128 wa **al-Hadiiqa**. Ameeleza kwenye ukurasa wa 168 kwamba: “Ndoto kama ilhamu ya kiroho, haziwezi kuwa sababu ya kutunga sheria za Uislamu”. Kwenye ukurasa wa 170 anaandika “Inawezekana kwa Allahu taala kuufungua moyo wa mtu ambae hakusoma kitabu chochote na kuujaza na maarifa na uhakika. Mtu huyu anapoisikia aya yoyote au hadithi, anaitafsiri na kuwashangaza maulamaa. Lakini haifai kumtegemea. Yeye ni walii na sio imamu wala murshid.

Ili kuwa mwanazuoni wa kiislamu, ni sharti kuwa na uelewa kamili wa sheria za hadithi”. Kwenye ukurasa wa 187 anasema “Kusahau mambo yanayohusu Uislamu, yaani, Uislamu kuchukuliwa kama mila, au kufuata mantiki na maoni ya mtu binafsi na sio Uislamu, huchangiwa na mambo manne: kwanza, kutotilia maanani elimu aliyoipata mtu, pili kufanya jambo lolote bila elimu, [Yaani, badala ya kujifunza maamrisho ya Allahu taala, hufanya anavyoona na kufikiria tu, bali pia huwashawishi watu wengine kufanya hivyo na kuamini kuwa ni wachamungu na wenye faida huku akiwachukia

wasiowapenda]. Tatu, kutojifunza mapema sheria zinazotawala mambo ambayo atayafanya kuwazuia watu kujifunza mambo ya kidini na kuwakashifu wanaotaka kujifunza au kufundisha vijana mambo hayo kwa kusema kuwa yamepitwa na wakati. Wakuu wa tasawuf, mawalii na murshid wamekuwa daima wakifuata miongozo yake minne ambayo ni Quran, sunna, ijmaa na qiyas. Wale wanaoshikamana na vitu visivyokuwa marejeo hayo manne watapelekwa kwenye mateso ya jahannamu. Wanaonesha uwongo kama ukweli na ukweli kama uwongo na wakaziba njia ya furaha isiyokuwa na mwisho ni waongo".

Hafidh Ibn Hajar al-Asqalaanii alisema "Ndoto za watu wasiokuwa mitume haziwasilishi sheria za kiislamu ambazo hueleweka kupitia wahyi au ijtihad". Ikiwa ndivyo ilivyo, inawezakanaje aya zikatafsiriwa kupitia kwenye ndoto ya mtu? Watu wanaweza kutawaliwa vipi kupita kwenye ndoto? Watu wanawezaje kutumwa katika kila sehemu ya dunia kwa kutegemea ndoto? Je, suala hili halikubadilisha sheria za kiislamu? Hata mtu mwenye elimu kidogo anaelewa vyema jambo hili.

Allahu taala alisema kwamba aliiteremsha Qurani ili ibainishwe kwa watu. Hata hivyo, kiongozi wa Tabligh anasema kwamba Qurani ilifasiriwa kwake kupitia kwenye ndoto. Kulingana na kiongozi huyu na jinsi ilivyodaiwa katika **Tanbiihaat** cha Abul a'la Maududi ambae ana mtazamo sawa na wake, kufafanua Qurani kwa kutumia kitabu cha tafsiri kinachotambulikana si muhimu, ilhali makamusi ya Kiarabu hutosheleza haja ya kuelewa yanayooneshwa kwenye ndoto. Hawa wawili, hawataleta mabadiliko ya kidini, kama wanabid'a wote, hueleza maana ya Qurani kulingana na mitazamo yao binafsi huku wakidai kuwa wanafuata Qurani na sunna. Huu ni uongo ulio wazi.

Katika kitabu chao kiitwacho **Dustur al-Amal**, inasemekana kuwa malengo ya wanachama wa Tabligh ni matatu:

1- Kuinua neno la Allahu taala.

2- Kueneza Uislamu.

3- Kuwaunganisha wale walio na imani hii.

Kuleta mabadiliko kwenye madhehebu, maadili na elimu. Ili wapate uelewa wa imani yao, inafaa kusoma vitabu vyao. Baadhi ya mambo wanayoamini yamejadiliwa kama ifuatavyo "Muhammad Ilyas, kiongozi wa jumuiya ya Tabligh alisema. 'Lengo letu ni kufundisha yale Mtume aliyowafundisha masahaba. Ni hatua ya kwanza ya jumuiya hii kuizunguka kila nchi kuelezea yanayohusu sala na kutoa nasaha'(Taz. Malfuuzaat, uk: 31). Maneno haya humaanisha kuwa wanaelezea

mafundisho ya Mtume wa Allahu taala kulingana na uelewa na mitazamo yao. Alimwambia rafiki yake Zaahir Hasan, ‘Jumuiya yetu inapaswa kuwa kundi linalofundisha sala tu . Naapa kwa jina la Allahu taala kwamba jumuiya yetu hailengi kufundisha sala. Tunafunza taifa jipya’ (Taz. Dinii Da’wat, uk: 205). Maneno haya hudhihirisha waziwazi lengo lake. Ni dhahiri kuwa wafuasi wa Ilyas si waaminifu katika kile wanachodai kuwa wanamuhimiza kila mtu kuswali. Tabia hii ni kisingizio tu, ni mtego wa kumnasa kila mtu kujiunga nao. Ukweli ni kwamba tamko, ‘Tabligh yetu imegubiza Uislamu, tariiqa na haqiiqa’, (Makaatib, uk:66) huonesha kwamba jumuiya hii iliyoasisiwa juu ya msingi wa ndoto ya Ilyas, ili kuwa na Uislamu na tariqa mpya. Kwa kweli dini imejengwa juu ya misingi hiyo mitatu. Dini mpya iliyojengwa juu ya msingi wa ndoto ilianzishwa na hali imefichwa nyuma ya Uislamu. Ni wazi kuwa tamko lao lililotajwa hapo juu hutokana na bid’a na upotofu.

Muhammad Idris Ansaari, mmoja wa wafuasi wa Ilyas alisema, “Imani ya jumuiya hii ni Laa ilaaha ill-Allah Muhammadun Rasulullah” (Dustuur, uk:4). Hii ni nguzo ya kimsingi ya Uislamu. Waqadiani na wabahai ambao kwa itifaki wametangazwa kuwa si waislamu walidai kwamba wanaamini hivyo na hawa pia walianzisha makundi mapya ya uzushi yaliyodai hivyo. Kwa kusema kwamba ‘ili kufanya jambo au ibada, au kukataza jambo, lazima iwe imetangazwa na mtume wa Allahu taala. Hakuna andiko jingine linalohitajika’, Ilyas alikana Ijmaa na Qiyaas ambavyo ni miongoni mwa dalili za kisheria (adillat ash Shar’iyya) (Taz. Dustuur, uk: 5). Hata hivyo, kamwe hakudai kuwa mujtahid. Angalifanya hivyo, hakuna mtu miongoni mwa waliokuwa wanajua usuli na elimu yake ambaye angemwamini.

Masharti ya kujiunga na jumuiya hii yameelezwa katika Dustuur al-‘Amal kama ifuatavyo: ‘Yeyote anayesema kwamba anaamini maana ya kalimat ash-Shahaada huwa mwanachama wa jumuiya hii. Kundi, taifa au nchi anamoishi haina athari juu ya suala hili’ (Taz. Uk:5). Aya hii hudhihirisha kuwa yeyote anaejisema kwamba ni Muislamu, hata kama ni mqadiani au mwanachama wa makundi mengine ya kibid’a kama vile, khaarijiyya, qaadiriyya, mu’tazila, au mawduudiyya, anaweza kuwa mshirika wa kundi hili na kufanya ibada yake akitegemea tu hadithi. Hawazingatii yale walioyafanya Salaf as-Salihiin ya Ijmaa na Qiyaas. Hawafuati mojawapo ya madhehebu manne. Kwa upande mwengine, wanadai kuwa wameshikamana vilivyo na Uislamu, tariiqa na haqiiqa. Huu ni upotofu uliowazi na kuchanganyikiwa.

Jumuiya hii ya Jamaat at-Tabligh hufanana na kundi la uasi liitwalo Jama'at al-Islami la Abul A'la Mawdudi.

Akizungumzia uchaguzi wa kiongozi wa Jamaa'a alisema, "Katika nidhamu ya kiislamu, hadhi ya amir ni muhimu sana. Amir anayeteuliwa kutokana na wanachama wa Jamaa'at attabligh ndie Ulu 'l amr aliyeelezewa na Uislamu. Ni fardhi kwa kila mtu kutii amri zake jinsi ambavyo amri za Allahu taala na mtume wake zinavyotiiwa. Ni wajibu kutii amri hizo za amir pasi na pingamizi. Hairuhusiwi kuchunguza hati za amiri. Ni dhambi kubwa kutofuata amri zake na kufanya yaliyo kinyume na matakwa yake Hayo husababisha adhabu na mateso ya Allahu taala (Taz. Uk:6-7). Kama inavyobainika, wanampandisha cheo amir wao hadi kufikia hadhi ya utume. Katika ukurasa wa nane, wanasema "Kabla ya amir kutoa amri, ni lazima atafute ushauri wa watu maarufu wa Jama'a na baadae wanachama wa halmashauri kuu. Ikiwa watakuwa na maoni tofauti, atachagua yale anayotaka na aamrishe yazingatiwe (uk:7)". Kama ilivyoelezewa, wanamtii amiri wao tu na wanachukulia kuwa wale wasiomfuata yeye, Allahu taala atalipiza kisasi dhidi yao. Wanakiri kuwa ni lazima kumtii amiri hata kama hakubaliani na yale wayasemayo wanachama wa halmashauri. Viongozi, wanachama wa halmashauri hii na amiri watakuwa miongoni mwao, yaani miongoni mwa wale wanaoungana juu ya kalimat ush-Shahaada pasi na kuchunguza madhehebu elimu au kutafuta sharti nyingineyo. Hata hivyo, salaf as-Salihiin, yaani wanazuoni wa Ahl as-Sunna, wameelezea sifa za mtu anayefaa kuwa Ulul-amr. Mwanazuoni Abu Suudi Efendi alisema kwamba, Ulul-amr ni viongozi wanaofuata njia ya tawhidi na hakimu waadilifu. Wao ni makhalifa waongofu (khulafaa ar-raashiduun), makhalifa wanne na wale wanaofuata nyayo zao. Imam al-Karkhi alisema "Wao ni makamanda wa zama za mtume "swallallahu alaihi wa sallam" na waliokuja baada yao. Hakimu na wakuu wa jeshi ni kama wao. Wengine huona kwamba Ulul-amr ni wanazuoni wa kiislamu. Ni wazi kwamba Amir wa Jamaa'at at-Tabligh ambae wanamteua kutoka miongoni mwao hayumo ndani. Aidha, madai kwamba ni waajib kumtii amiri na kwamba kutotii amri zake ni dhambi kubwa, hayana msingi.

Akielezea yatayoukumba umma wake, mtume wa Allahu taala "swallallahu alaihi wa sallam" alisema: "Watoto wa Israil walifarakana katika makundi sabini na mbili na umma wangu utafarakana katika makundi sabini na tatu. Kundi moja tu kati yao ndilo litakalonusurika na mengine yote yataenda motoni." Maswahaba waliposikia haya waliuliza, "Ewe mtume wa Allahu taala! Ni kundi lipi hilo? Alijibu: "Ni

wale waliofuata njia yangu na ile ya masahaba zangu". Hadithi hii ilipokelewa kutoka kwa Abdullah Ibn Umar "radiyallahu anhu". Hadithi iliyopokelewa kutoka kwa Muawiya "radiyallahu anhu" na Ahmad na Abu Daud inasema kwamba mtume alisema "Kati yao, makundi sabini na mbili yataingia motoni na lililobaki litaingia peponi. Nalo ni Jama'a". Hadithi hii imenukuliwa katika sura inayozungumzia I'tisaam, kitabu kiitwacho Mishkaat. Enyi Waislamu. Lazima tulitafute na tulipate kundi hilo moja litakalonusurika lililotajwa katika hadithi hii na imani ambayo ni sababu ya kuingia peponi na tujitahadharishe na makundi ya waasi yanayopingana na kundi hili. Kwa kufanya hivyo tutakuwa tumefanya jitihada ya kunusurika na kutoingia kwenye moto wa Jahannamu na ulimi wake. Hadhrat Gawth al-A'zam Abd al-Qadir al-Jiilaani alielezea hadithi iliyotajwa hapo awali na neno 'Jama'a lililojitokeza katika hadithi ya pili kama ifutavyo. 'Muumini anapaswa kushikamana na sunna na Jama'a. Sunna ni mwenendo alioubainisha mtume "swallallahu alaihi wa sallam". Jama'a imeundwa kwa mambo ambayo yalifanywa kwa itifaki na masahaba watukufu walioishi katika zama za makhalifa wanne wajuulikanao kama Khulafaa ar-Raashiduun. Waislamu wanapaswa kuzuia ongezeko la wanabid'a na waepukane nao na hawapaswi kuwasalimia. Ahmad ibn Hanbal, Imamu wa dhehebu letu alisema kwamba kumsalimia mwanabid'a ni kumpenda kwa vile imetajwa kwenye hadithi kwamba "Sambazeni salamu!" haya yameandikwa kwenye ukurasa wa 90 wa Ghunyat at-taalibiin. Mwanazuoni maarufu Ahmad ibn Hajar al-Hitmi, muhaqqiq wa mwisho, amezungumzia maada hii kwa upana kwenye ukurasa wa 149 wa kitabu chake Sawaaiq al-Muhriqa na kusema 'Wanaojitenga na imani ya Ahl as-Sunna ni mubtadi'in. Walianza kujitokeza katika karne ya kwanza (ya majilio ya Uislamu).

Hadhrat Ibn Hajar al-Hitmi alisema katika kitabu chake kiitwacho **Fath al-Jawaad** kwamba **Mubtadi** ni mtu asiyekuwa na itikadi inayoshikiliwa na Ahl as-Sunna kwa itifaki. Itifaki hiyo iliwasilishwa na maimamu maarufu wawili. Abul Hasan al-Ash'ari na Abu Mansuur al-Matruudi na wanazuoni waliofuata njia yao. Kwa mujibu wa Al-Fataawa al-Hadiithiyya, ukurasa wa 205, 'Mwanabid'a ni yule ambae imani yake hutofautiana na ile ya Ahl as-Sunna. Imani ya Ahl as-Sunna ni ile ya Abul Hasan al-Ash'ari, Abu Mansuur al-Matruudi na wafuasi wao. Yeyote anayezua jambo lisiloidhinishwa na Uislamu, hua mwanabid'a. Shaafi´i Alim Ahmad Shihaab ad-Diin Kalyubi al-Misri kwenye kitabu kiitwacho Kanz ar-Raaghibin, Juzuu ya nne ameandika maneno yafuatayo:

‘Yeyote asiyezingatia mafundisho ya Abul Hasan al-Ash’ari na Abu Mansuur al-Matruudi, basi mtu huyo si msunni. Maimamu hawa wawili walifuata nyayo za mtume "swallallahu alaihi wa sallam" na maswahaba wake. “Kwa mujibu wa ibara zilizotangulia, inaeleweka kwamba ni kundi moja tu kati ya makundi sabini na tatu, lililoibuka kutokana na mfarakano ndilo litakalonusurika dhidi ya moto wa Jahannamu. Ni jukumu la kila Muislamu kulitafuta, kulipata na kushikamana na kundi hilo ambalo wafuasi wake wanamfuata Abul Hasan al-Ash’ari na Abu Mansuur al-Matruudi. Haifai kwa mtu kuasisi kundi jipya zama hizi akaona kwamba Laa ilaaha illallahu inatosha akajitenga na imani ya Ahl as-Sunna wal jamaa’a. Hotuba na maandishi ya kundi la wanaodai kuwa Jamaa’at atTabligh yanabainisha kuwa sharti pekee inayomtoshelezea mtu kujiunga na kundi hili ni kutamka neno ‘Laa ilaaha illallah Muhammadun rasuulullah’. Mtu yeyote hata kama ni mfuasi wa kundi la waasi au hamtii yeyote isipokuwa Mtume wa Allahu taala huwa mwanachama wa jumuiya hii punde tu baada ya kutamka kauli hii hata kama hakuwatii swahaba na mujtahidiin. Watu wanaowakilisha Maqadiani, Nijaari, Uwahhabi, Umauduudi na makundi mengine ya wasiokuwa waislamu huonekana wakiwa katika jumuiya hii. Kusudio lao ni nini hasa kama si kuufarakanisha umma?

Je, wanawakosoa waasi baada ya kujiunga na jumuiya yao? Kinyume cha haya hubainika katika vitabu vyao na tabia zao. Wanawazuia watu kuzungumzia madhehebu. Wanampa kila mtu uhuru katika itikadi zake. Kwa mujibu wa Dustuur al-Amal, ukurasa wa saba, ‘Maada za mfarakano na zisizofaa hazipaswi kuzungumziwa. Kiini cha tawhidi na nguzo za Uislamu zinapaswa kudurusiwa’. Mambo hayohayo yameandikwa kwenye ukurasa wa 218 wa **Miftaah at-tabligh**. Kiongozi wao Muhammad Ilyas aliandika katika ukurasa wa 116 wa **Malfuuzaat**, msingi wa jumuiya yetu ni kuimarisha imani. Haifai kuupanua ujuzi unaohusiana na imani. Tukifanya hivyo, tutaamsha uchochezi na wasiwasi nyoyoni’. Kwenye ukurasa wa 142 anasema ‘Wakati mwingine mnatumia neno ‘bid’a. Msitamke maneno kama hayo. Maneno kama hayo yanaweza kusababisha mfarakano baina ya watu’.

Hatimae, hawana imani ya Ahl as-Sunna. Makundi yote sabini na mbili yanaweza kuungana bila kizuizi. Wasiokuwa waislamu wanaweza kujiunga nao pia. Hawashughuliki na ujuzi wa imani, wanawazuia watu kiijfunza mambo yanayohusu imani. Husema kwamba wanamfuata mtume tu. Hawachunguzi njia pekee ya ukweli iliyotajwa katika hadithi. Wanasema ikichunguzwa itasababisha mfarakano. Hawatumii

neno ‘bid’a au mengine kama hilo wakidai kuwa husababisha uchochezi. Pamoja na tabia hizi za kiasi, wanadai kuwa wao ni Ahl as-Sunna wal jamaa’a. Hata hivyo, kulingana na mtazamo wa njia hii ya ukweli, uasi wao hautiliwi shaka.

Wanazuoni wa Kiislamu wamewakataza waislamu kufanya urafiki na wanabid’a. Hadhrat Qutb al-Aqtab Abd al Qadir al-Jiilaani alisema kwamba thawabu nyingi zaidi hupatikana kutokana na kuamini kuwa madhehebu ya wanabid’a ni potofu, hayafai kufuatwa na yanapaswa kupigwa vita. Mtume wetu "swallallahu alaihi wa sallam" alisema Allahu taala huujaza amani na imani moyo wa mtu anaemwangalia mwanabid’a kwa jicho la uadui. Amchukuliaye mwanabid’a kuwa habithi, Allahu taala humuokoa kutokana na hofu za siku ya kufufuliwa. Anayemuudhi mwanabid’a Allahu taala humpandisha daraja mia peponi. Akutanaye na mwanabid’a na uso wenye tabasamu ama kumtendea wema atakuwa ameuchukia Uislamu ulioteremshwa na Allahu taala kwa Muhammad "swallallahu alaihi wa sallam". Hadithi iliyopokelewa na Mughiira kutoka kwa Abdullah ibn Abbaas "radiyallahu anhuma" inasema, “Allahu taala hatokubali ibada ya mwanabid’a asipoachana na bid’a yake” Fudhail ibn Iyad alisema, ‘Allahu taala hubatilisha ibada na kuondoa imani kutoka kwenye moyo wa mtu anayependa bid’a. Inatarajiwa kuwa anayemchukia mwanabid’a, ataghufiriwa madhambi yake hata kama ana madhaifu katika vitendo vyake vya ibada. Ukikutana na mwanabid’a, badili muelekeo! Hadithi na nasaha zilizotolewa hapo juu zimeandikwa katika Ghunyat at-taalibiin, ukurasa wa 90. Muislam yeyote anaweza kujiunga na jumuiya yao akiwa ni wa Ahl as-Sunna au hata mwanabid’a. Pamoja na utatanishi huu, bado wanadai kuwa wako kwenye njia ya kweli. Hali hii hufanana na kuweka vinyume viwili pamoja, kama vile moto na baruti, jambo ambalo haliwezekani.

Huku muasisi wa Jamaa’at at-tabligh Muhammad Ilyaas akiwasilisha aliyoyaona kwenye ndoto kama dini mpya, alikuwa pia akitoa chanjo za vijidudu alivyopata kwa wafuatao madhehebu. Katika kitabu kiitwacho Madhaahib, ukurasa wa 90, anasema ‘Ni jambo jema kuhudhuria vikao vya hatm al-Qurani na dhikr. Wanadini maarufu walisema hivyo. Hata hivyo, kwa vile kuna kuhofia hatari ya kuwa kama wanabid’a, ni bora kutohudhuria vikao hivyo. Kuna hatari kama hiyo katika kumsalia Mtume kwa kufikiria kuwa yupo na anakuona na kutoa salamu kama wanavyotoa wanabid’a. Ndio, hata kama inaruhusiwa kuitoa kwa upendo uliovuka mipaka, shetani anaweza kuingilia kati na kuharibu imani. Na hii ni hatari kubwa’.

Angalia maneno haya. Haruhusu kumsalia na kumtolea salamu Mtume huyu maarufu ukiwa na fikra kwamba yupo na huona, hata kama kufanya hivyo kungetokana na hisia za kumpenda sana kiasi cha kuvuka mipaka. Hii ni imani ya Kiwahhabi. Kuzuia kwake kitendo hicho hata katika hali ya kuonyesha upendo uliopindukia kiasi ni uasi unaozidi ule wa mawahabi. Muislam hawazi kitendo hicho. Anafikiria nini kuhusu waislamu wote wanaposema wakiwa katika sala “Assalamu alaika ayyuhan Nabiyyu”? Tazama Hujjat al-Islam aliyoandika Imam al-Ghazali "rahmatullahi alaih" katika kitabu chake **Ihyaa al-Uluum** (Juzuu ya kwanza, uk:129): ‘Kwanza vuta sura ya mtume "swallallahu alaihi wa sallam" moyoni mwako. Halafu sema Assalaamu alaika ayyuhan Nabiyyu na uamini kuwa anakusikia na kukujibu’. Ottoman Alim Muhammad Hakki Efendi (Aliefia Makka mwaka wa 1301 H./ 1884 A.D.) aliandika katika makala yake kwenye ukurasa wa 166 wa kitabu chake kiitwacho Haziinat al-Asraar, ‘Muislam anapaswa kufikiria kuwa yuko kwenye hadhara ya mtume "swallallahu alaihi wa sallam" na aseme kwa heshima na akinuia kuwa yeye ni mtetezi, wasila na mwokozi kati yake na Allahu taala, ‘Assalaamu alaika ayyuhan Nabiyyu’.

Al-‘Arifu bi ‘llah Sayyid Muhammad ‘Uthman al-Mirghaani al Makki al-Hanafi (aliefia Makka mwaka wa 1268 H./ 1852 A.D.) alisema ‘Fikiria juu ya kuwepo kwa mtume "swallallahu alaihi wa sallam" huku akikuangalia, akikuona na kukusikia. Hata kama upo mbali, Allahu taala huifanya sauti yako isikike na hukufanya uonekane waziwazi. Hapa, kuwa karibu au mbali ni sawa’. Ibara hizi zote hudhihirisha kuwa mtume wa Allahu taala "swallallahu alaihi wa sallam" anaona na kuwasikia wale ambao hufikiria kuwa wanamtazama. Mwasisi wa Jamaa’at attabligh haamini haya. Kuyakataza hata kama yangefanyika kwa kumpenda sana Mtume na husema kwamba Mtume hawaoni wala hawasikii wanaofikiria juu yake. Kauli yake hii huchimba kwenye muhimili wa kimsingi wa mawahabi usemao kwamba, ‘Maiti hawasikii’. Maelezo yaliyo sahihi zaidi juu ya maada hii ni fatwa ya Ahmad Ibn Hajar al-Hitaami, mwanazuoni maarufu yaliyoandikwa katika al-Fataawa al-Kubra, Juzuu ya pili, ukurasa wa tisa.

**Swali**: Je, anayeitukuza roho ya mtume wa Allahu taala "swallallahu alaihi wa sallam" humuona? Inasemekana kuwa akionekana huulizwa angesema nini kuhusu mtu huyo. Neno ‘mtu huyo’ hutumika kumrejelea mtu huyo aliyopo mbele yake. watu wengi hufariki dunia kwa wakati mmoja. Kwa vile ‘mtu huyo’ hutumika kuwarejelea wote,

inaeleweka kuwa anaonekana katika sehemu nyingi kwa wakati mmoja. Je, jambo hili hutokea vipi?

**Jibu**: Ni kweli kwamba mtume anaonekana na kila mtu anayekaribia kufa, na anaulizwa, “Unasema nini kuhusu mtu huyo?” jambo hili hudhihirisha nguvu za Allahu taala. Neno ‘huyo’ hutumika kuashiria mtu aliyopo mbele yake. Kauli hii ni jibu kwa mtu asiyeamini kuwa Mtume hawezi kuonekana kwa namna mbalimbali kwenye sehemu mbalimbali na kwa wakati moja. Kwa hakika jambo hili linaweza kuaminika pia kwa kutumia akili. Dhati yake tukufu huwa kama kioo na kila mtu huiona sura ya ujamali au ubaya wake kwenye kioo hiki. Hakuna mabadiliko yanayojitokeza kwenye ujamali uliomo ndani ya kioo. Maisha ya kaburini na yale ya siku ya kiama hayafanani na yale ya dunia. Kila mtu ana sura moja hapa duniani. Imeshuhudiwa mara kadhaa kwamba mawalii wamekuwa na sura mbalimbali katika maisha ya dunia pia. Inajulikana sana kwamba Kadiid al-Baan Hasan al-Mussuli na wengine wameonekana hivyo’.

Katika al-Fataawa al-Kubra, ukurasa wa 29 aliandika ‘maiti huwatambua watu wanaowatembelea. Hadithi iliyopokelewa na ibn Abid-Dunya inasema ‘mtu anapotembelea kaburi la ndugu yake Muislam akakaa pembezoni mwake, maiti humtambua na kuitikia salamu yake’. Hadithi nyingine inasema, ‘Mtu anapopitia karibu na kaburi la ndugu au rafiki yake Muislam akatoa salamu, maiti humtambua na kuitikia salamu yake’. katika fatwa yake ya pili, anasema, ‘Maiti huzisikia sauti za walio hai. Hadithi iliyopokelewa na Imam Ahmad inasema, ‘Maiti huwatambua wale wanaomkosha, wanaombeba na kumweka kaburini’. Hadhrat Sayyid Abdul Hakim Arwasi mwanazuoni na walii maarufu aliyefariki dunia mjini Ankara mwaka wa 1362 H/ 1943 A.D. alisema ‘Ibn Hajaral-Makki alikuwa mmoja wa wanazuoni bora wa kiislamu. Maneno yake yote yameandikwa na huchukuliwa kama hoja’.

Inakuwaje mtu akawa na shaka katika kuwepo na kuona kwa Mtume wa Allahu taala "swallallahu alaihi wa sallam"? Hadhi ya mitume na mawalii hunyanyuliwa baada ya roho zao safi kutengana na miili yao. Wao huwa na tasarruf (mamlaka) timilifu kama malaika. Haya yameelezewa kwa itifaki ya wanazuoni wa Ahl as-Sunna lakini yamepingwa tu na Muhammad ibn Abd al Wahhab ambae ameachwa na Allahu taala kwenye uasi. Ilyas, kiongozi wa Jamaa’at at-Tabligh amenaswa na mkondo huu wa uasi. Ufuatao ni mfano mwingine, unaotokana na kauli za wanazuoni, ambao pengine unaweza kutoa

mwanga kwa wanaomwamini na kuwafedhehesha mulhidiin (wakana Mungu).

Shah Walii-Allah ad-Dahlawi, mmoja wa wanazuoni maarufu wa India, aliandika kwenye kitabu chake kiitwacho Hujjatu ‘llahi ‘l-Baaligha (Juzuu 1: 35), “Mwanaadamu anapofariki dunia, hakuna uhusiano unaobaki baina ya roho yake na ulimwengu wa maada. Roho hurejea kwenye asili yake, huwa kama malaika, na hutoa wahyi na misaada kwa watu kama malaika. Husaidia katika kueneza na kuimarisha dini ya Allahu taala. Hutoa msaada kwa haraka kwa wale wanaotumika katika njia hii. Imeshuhudiwa kwamba wao hutoa msaada wakiwa kwenye makundi”. Ibara hii huelezea kuwa roho zenye kheri hufanya kazi jinsi malaika wanavyofanya. Je, maneno haya hayatoshi kuwakosoa wale ambao hawaamini kuwa Mtume wa Allahu taala "swallallahu alaihi wa sallam" huwepo na husikia? Wanazuoni wa kiislamu wameelezea kwa itifaki kuwa yeye ndie sababu ya kuwepo kwa viumbe wote na kupata ukaribu na Allahu taala.

Kwa mujibu wa ar-Rawd an-Nadir, kilichoandikwa na Allama Abd ar-Rauuf al-Manaawi: “Baada ya nyoyo safi kutengana na maisha haya na kupandishwa vyeo vyao, hakuna kizuizi chochote mbele yao. Wao huona kila kitu, au kufunzwa na malaika. Jambo hili ni la ajabu sana kiasi kwamba ni wachache mno wanaolijua. Ikiwa roho zilizobarikiwa tu huwa katika hali kama hii, basi inapaswa mtu kufikiria kwa makini jinsi alivyo yule mwenye hadhi ya juu kabisa.

Hadhrat Ahmad Zaini Dahlani alisema katika kitabu Taqriib al-Usuul, ukurasa wa 58, kwamba “Arif walio wengi walisema kwamba baada ya walii kufariki dunia uhusiano wa roho yake na muriidi wake huedelea kuwepo. Kwa baraka ya roho hiyo, nuru na faida kadhaa hujitokeza. Maelezo kamili yametolewa na Hadhrat Qutb al-Irshad Abdhullah al-Haddaad aliyesema “Baada ya walii kufariki dunia, huwaachia marafiki zake wa karibu mambo yake. Mambo hayo huzidi yalivyokua alipokuwa hai. Kwani alikuwa akijishughulisha sana katika dunia na kazi za kumtumikia Allahu taala, wakati mwingine kazi hizo zilimhangaisha zaidi. Aghlabu kwa namna hii na hususan nyakati hizi ambapo mteule anafariki dunia, ndipo maumbo na miili yao hutoweka lakini haqiiqa [uhalisia wao] huendelea kuwepo. Wako hai kwenye makaburi yao. Kwa vile walii yuko hai kwenye kaburi lake, ujuzi, akili na nguvu zake za kiroho hazibadiliki hata kidogo. Kwa hakika, vyote huongezeka zaidi baada ya kufa”. Ikiwa hali ndivyo ilivyo kwa mawalii, basi ni lazima ikadiriwe jinsi inavyopaswa kuwa kwa mitume, na hasa yule ambae ni mbora wao. Ukweli ulio dhahiri, waweza tu kupingwa na

waliochafuliwa nyoyo na sumu ya wasiofuata madhehebu na wale walionaswa kwenye mtego wa wamkanao Allah na walioacha Uislamu. Allahu taala awanusuru waislamu wote kutokana na maangamizi haya makubwa. Amin".

## MASHARTI YA KUWA MUISLAMU WA KWELI

Neno Islam ni la Kiarabu ambalo maana zake ni 'kujitolea kufanya kitu, kujisalimisha, uokovu na amani'. Imam Abu Hanifa (rahmatullahi alaih) amefasiri neno 'Islam' kama 'kujisalimisha na kutii maamrisho ya Allahu taala'.

Mambo yaliyotajwa hapo juu yakisomwa kwa uangalifu, itabainika wazi jinsi Muislam anavyopaswa kuwa. Tutayarudia tena kama ifuatavyo.

Kwanza kabisa, Muislamu ni msafi kimwili na kiroho. Lakini acha tuanze na usafi wa kimwili.

Katika sehemu mbalimbali za Quran tukufu, Allahu taala anasema "Allahu taala huwapenda wale wanaotubu na huwapenda wasafi". Waislamu hawaingii misikitini wala ndani ya nyumba zao wakiwa wamevaa viatu vyao. Mazulia yao na sakafu zao huwa safi. Kila Muislam ana choo ndani ya nyumba yake. miili yao, nguo zao na chakula chao huwa kisafi daima. Kwa hiyo, hawasambazi vijidudu vya maradhi na ugonjwa.

Kasri ya Versailles, ambayo Wafaransa hujifaharisha nayo, hawana hamu nayo.

Katika enzi za kati, Mfaransa wa Paris akiamka asubuhi, alikuwa akikojoa na kwenda haja kubwa kwenye chombo cha kuendea haja. Kwa vile hapakuwa na choo ndani ya nyumba yake, akipeleka chombo hicho na chupa ya kunywea maji kwenye mto Seine. Kwanza akichota maji yake ya kunywa kutoka kwenye mto huo, na kisha kumwaga mkojo huo na kinyesi ndani ya mto. Mistari hii imetafsiriwa kiasisi kutoka kwenye kitabu cha Kifaransa kijulikanacho kama 'Drinking water' (L'eau Potable). Padre wa Ujerumani aliyekuja Istanbul katika enzi za Sultan Sulaiman, alisema maneno yafuatayo katika kitabu alichoandika mnamo mwaka wa 967 H./ 1560 A.D.:

“Nimependezwa na usafi uliopo hapa. Kila mtu hunawa mara tano kila siku. Maduka yote ni masafi. Hakuna uchafu mitaani. Hakuna madoa kwenye nguo za wauzaji. Aidha, kuna majumba yaitwayo ‘hammam’ yenye maji ya moto ambamo watu huoga, tofauti na watu wetu ambao ni wachafu hawajui namna ya kujiogesha”. Wazungu walijifunza kuoga baada ya karne kadhaa.

Lakini siku hizi, wageni wanaotembelea nchi za kiislamu huandika katika vitabu vyao wanavyochapisha “Ukienda katika nchi za Mashariki, kwanza, harufu ya samaki waliooza na takataka hushambulia pua yako kwa ghafla. Kuna uchafu kila mahali. Mitaa imejaa na mate na kamasi. Unaweza kuona marundo ya takataka hapa na pale na mizoga. Unapata hisia za karaha unapotembea katika nchi za mashariki na kutambua kuwa waislamu si wasafi kama wanavyodai”. Tunasikitika kuwa huo ni ukweli. Hakika nchi zinazobeba bendera ya Uislamu hivi leo, hawakusahau tu ujuzi wa imani lakini pia hawatilii maanani suala la usafi. Lakini kosa ni la wale ambao wamesahau kuwa msingi wa Uislamu ni usafi. Umaskini si udhuru wa kuwa wachafu. Kutema mate na kuchafua mahala fulani hakuhusiani kwa vyovyote na pesa. Watu wachafu kama hao ndio wahuni ambao wamesahau maamrisho ya Allahu taala yanayohusu usafi. Kama kila Muislamu angeijua dini yake ipasavyo na kushikamana nayo, uchafu huo ungetoweka wenyewe. Hivyo, wageni wanaotembelea nchi za kiislamu wangependezwa na usafi, kama walivyopendezwa na waislamu wa enzi za Kati.

Muislamu wa kweli huwa msafi na kujali siha yake. Hatumii vinywaji vinavyolevya kwa sababu ni aina moja wapo ya sumu. Hali nyama ya nguruwe, kwa vile imeharamishwa kutokana na hatari na madhara yake anuwai. Imegunduliwa kwamba kirusi kinachosababisha UKIMWI, ugonjwa hatari unaoambukizwa na mashoga hutokana na nguruwe.

Mtume wetu "swallallahu alaihi wa sallam" aliisifu sayansi ya tiba kwa namna mbalimbali. Mfano wa kauli yake isemayo “ Kuna aina mbili za elimu, elimu ya mwili na elimu ya dini”. Yaani, aina hizi mbili ni muhimu zaidi. Kwa kusema ‘Elimu ya dini’ inayohifadhi roho na ‘elimu ya tiba’ inayouhifadhi mwili, alitaka tufanye jitihada ya kuifanya miili na roho zetu kuwa zenye nguvu. Kwani kila aina ya matendo mazuri huweza kufanyika na mwili wenye siha na afya.

Hivi leo, vyuo vikuu vyote hufundisha kwamba tiba ina matawi mawili. La kwanza ni elimu ya siha, kuufanya mwili uwe na siha, na tawi la pili ni utabibu, kutibu magonjwa. Tawi la kwanza limepewa umuhimu

wa kwanza. Jukumu la kimsingi la tiba ni kuwakinga watu dhidi ya magonjwa kuwafanya wenye afya nzuri. Hata kama mgonjwa atatibiwa, anaweza kuwa asiejiweza na mwenye upungufu. Na sasa acha turudi kwenye hoja yetu, elimu ya siha na jukumu la kwanza la tiba ni kukubaliwa na Uislamu. Katika sehemu ya pili ya kitabu kiitwacho Mawaahib al-laduniyya, imethibitishwa kuwa Qurani hukuza aina zote mbili za tiba kama inavyoelezewa katika baadhi ya aya.

Mtume wetu "swallallahu alaihi wa sallam" alianzisha uhusiano wa karibu sana na Mfalme mkuu wa Byzantine Heraclius. Walikuwa wakiwasiliana na kutumiana wajumbe. Siku moja, mfalme Heraclius alimtumia zawadi nyingi. Daktari wa tiba alikuwa miongoni mwa zawadi hizo. Alipowasili, alienda kwa Mtume "swallallahu alaihi wa sallam" akasema, “Bwana, mtukufu mfalme amenituma kwako kama mtumishi wako. Nitawatibu wagonjwa wako bure”. Mtume "swallallahu alaihi wa sallam" alikubali huduma zake. Daktari alipewa nyumba kama ilivyoamrishwa. Kila siku walimnunulia chakula na kinywaji kitamu. Siku na miezi kadhaa ilipita na hapakuwa na Muislamu aliyeenda kumuona. Hatimaye, aliona haya akaomba ruhusa ya kwenda zake, akasema “Bwana, nilikuja hapa kukuhudumia. Hadi sasa hakuna mgonjwa aliyenijia. Nimekuwa nikikaa bure nikila na kunywa kwa furaha. Sasa naomba nirudi nyumbani”. Mtume wetu "swallallahu alaihi wa sallam" alimjibu “Ni juu yako. Ukitaka kubaki, ni jukumu la waislamu kumhudumia na kumheshimu mgeni wao. Hata hivyo, ukitaka kuondoka sasa, nakutakia safari njema. Lakini wapaswa kujua kuwa hata kama ungeishi hapa kwa miaka kadhaa, hakuna muislam ambae angekuja kukuona. Hii ni kwa sababu sahaba zangu hawaugui. Dini ya Kiislamu imebainisha namna ya kupata afya njema. Sahaba zangu wako makini sana katika mambo ya usafi. Hawali chochote mpaka wanaposikia njaa na husitisha kula kabla ya kushiba”.

Kwa matamko hayo, hatukusudii kusema kwamba muislamu haugui. Hata hivyo, muislamu anaekuwa makini katika mambo ya siha na usafi wake huwa mwenye afya njema kwa muda mrefu. Ni nadra sana kuugua.

Kifo ni ukweli usioepukika. Kila kitu huwezekana kwa kuzingatia maamrisho ya Uislamu tu kuhusu usafi. Katika enzi za kati, Ukristo ulipofikia kilele chake, wataalamu maarufu wa tiba walikuwa wakipatikana miongoni mwa waislamu tu. Wazungu walikuwa wakija Andalusia Hispania ambayo ilikuwa ni nchi ya kiislam, ili kupata elimu ya tiba. Wale waliogundua chanjo ya kupata kinga dhidi ya ndui walikuwa waislamu Waturuki. Bwana Janner aliyejifunza jinsi ya

kutengeneza chanjo hiyo kutoka kwa Waturuki aliipeleka Ulaya mwaka wa 1211H/ 1796 A.D. na bila kustahili, akapewa jina la heshima la ‘mgunduaji wa chanjo ya ndui’. Zama hizo, bara la Ulaya lilikuwa lenye ukatili na magonjwa yalikuwa yakiwaangamiza watu. Mfalme wa Ufaransa, Louis wa kumi na sita alikufa kutokana na ndui mwaka wa 1774 A.D. Maradhi ya tauni na kipindupindu yalisababisha maangamizi kwa muda mrefu. Napolion wa kwanza alipoizingira ngome ya AKKA mwaka wa 1212 H./ 1798 A.D., tauni ilizuka miongoni mwa wanajeshi wake na kwa vile hakuwa na namna ya kuondokana nayo, ilimbidi aombe msaada kutoka kwa maadui zake waislamu Waturuki.

Imeandikwa katika kitabu cha Kituruki kama ifuatavyo “Waturuki walituma madaktari baada ya kukubali ombi letu. Walivaa nguo safi sana na nyuso zao zilikuwa zenye mng’ao. Kwanza, waliomba dua halafu wakanawa mikono yao kwa muda mrefu wakitumia sabuni na maji. Walikata uvimbe uliokuwa kwenye miili ya wagonjwa kwa kisu kidogo na kusababisha mbubujiko wa usaha halafu wakaosha vizuri vidonda hivyo. Baadaye, waliwaweka wagonjwa kwenye vyumba tofauti wakawaamuru walio wazima kutochanganyika nao. Walichoma nguo za wagonjwa wakawavisha nguo mpya. Hatimaye, waliosha tena mikono yao, wakachoma vichaka vya mishubiri katika sehemu ambapo maiti walikuwa, wakaomba dua tena wakaondoka huku wakikataa yale yote tuliyotoa kama malipo na zawadi”.

Hii ina maana kwamba wenyeji wa magharibi ambao hawakuwa na uwezo wa kupambana na maradhi hadi karne mbili zilizopita, walijifunza tiba iliyopo leo hii kwa kusoma, kufanya majaribio na kazi kama ilivyopendekezwa katika Quran tukufu. Kuhusu usafi wa kiroho, bila shaka waislamu wanapaswa kuwa na maadili na uungwana wa hali ya juu. Uislamu kwa ujumla ni maadili na uungwana. Kiasi cha wema, uadilifu na ukarimu ni vitu ambavyo Uislamu unaamrisha kuwatendea maadui na marafiki kwa usawa mkubwa sana.

Matukio ya karne ya kumi na tatu zilizopita huonyesha waziwazi ukweli huu kwa maadui wa Uislamu. Tutaelezea ithibati moja iliyo dhahiri kabisa kati ya nyingi zisizohesabika. Kama ilivyoandikwa katika moja wapo ya kumbukumbu za miaka mia mbili katika nyaraka zilizoko kwenye jumba la makumbusho la Basra. Waislamu walijenga msikiti kwenye ardhi iliyokuwa karibu na mtaa wa Wayahudi huko Altiparmak. Wayahudi walidai umiliki wa ardhi wakasema kwamba waislamu hawapaswi kujenga msikiti pale. Mvutano ulizua malalamiko ambayo yalipelekwa kwenye mahakama ya kisheria. Baada ya kusikilizwa kwa kesi, mahakama ilitoa uamuzi kwamba eneo hilo lilikuwa la Wayahudi

na kwamba msikiti ulipaswa kubomolewa na ardhi irejeshwe kwa Wayahudi. Uamuzi ulitekelezwa. Bila shaka uamuzi huo ulikuwa wenye uadilifu mkubwa.

Mtume wetu "swallallahu alaihi wa sallam" alisema “Hakika nilitumwa kwa ajili ya kutimiza maadili mema”, na hadithi nyingine inasema “walio na imani miongoni mwenu ni wenye tabia nzuri”. Kwa hiyo, imani pia hupimwa kwa kuzingatia maadili.

Usafi wa kiroho ni muhimu kwa Muislam.

Muongo, laghai, mdanganyifu, katili, dhalimu, asiyewasaidia waumini, mwenye kiburi, anayefikiria juu ya manufaa yake tu si Muislam wa kweli hata kama anafanya sana ibada.

Maana ya aya tatu za kwanza za Suratul-Maun ni, ‘Ewe Mtume wangu. Umemuona yule anayekana siku ya hukumu, ambae hawajali mayatima, hawapi haki zao wala hawahimizi watu wengine juu ya kuwapa maskini chakula’. Ibada ya watu kama hao haikubaliwi.

Katika Uislamu, kuepukana na haramu hupewa kipaumbele ikilinganishwa na kufanya matendo ya faradhi. Muislamu wa kweli ni mtu kamili na mkomavu. Ana uso wenye tabasamu. Ni mtu mwenye lugha tamu na ambae husema ukweli. Hakasiriki kamwe.

Mtume alisema: “Aliyejaaliwa upole, kajaaliwa wema duniani na akhera”. Muislam huwa mpole sana. Humsikiliza kila mtu anayetafuta ushauri wake na huwasaidia kadri ya uwezo wake.

Muislamu ni mwenye heshima na ni mpole. Mtume wetu "swallallahu alaihi wa sallam" alisema “Kupenda nchi yako ni sehemu ya imani”. Ndiyo maana Muislamu anatoa huduma za kijeshi kwa hiari serikali inapopambana na wavamizi.

Mnamo mwaka wa 1560, kasisi (mchungaji au padri) wa Kijerumani akisema ‘Sasa naelewa kwa nini waislamu Waturuki walitushinda katika mapambano yetu yote. Jihadi ikitokezea, waislamu huchukuwa silaha mara moja, wakapigana na wakafa kwa hiari kwa ajili ya nchi na dini yao. Wanaamini kuwa wale wanaouliwa katika vita vitakatifu wataenda peponi. Tofauti na hayo, katika nchi yetu, pakiwepo uwezekano wa vita, kila mmoja hutafuta mahali pa kujificha akihofia kusajiliwa jeshini na wale wanaoandikishwa jeshini kwa kulazimishwa hawataki kupigana”.

Allahu taala ameelezea kwa undani waja wake katika Qurani tukufu, Suratul-Furqan aya 63-69: **“Na waja wa Arrahman mwingi wa rehma ni wale wanaotembea ulimwenguni kwa staha, na wajinga**

**wakiwasemeza hujibu, salama. Na wale wanaokesha kwa ajili ya Mola wao Mlezi wakisujudu na kusimama. Na wale wanaosema Mola wetu Mlezi tuondolee adhabu ya Jahannamu. Hakika adhabu yake ikimpata mtu haimwachi. Hakika hiyo ni kituo na makao mabaya. Na wale ambao wanapotumia hawatumii kwa fujo wala hawafanyi ubakhili, bali wanakuwa katikati baina ya hayo. Na wale wasiomwomba mungu mwengine pamoja na Allahu** taala**, wala hawaui nafsi aliyoiharamisha Allahu** taala **isipokuwa kwa haki, wala hawazini. Na atakayefanya hayo atapata madhara. Atazidishiwa adhabu siku ya kiama, na atadumu humo kwa kufedheheka"**.

Katika sura hiyo pia aya 72-74 waja hao wema: **"Na wale ambao hawatoi ushahidi wa uongo, na pindi wapitapo penye upuuzi, hupita kwa heshima yao. Na wale ambao wanapokumbushwa ishara za Mola wao Mlezi hawajifanyi viziwi wala vipofu na hizo aya "**.

Zaidi ya hayo, Sura As-Saaffat aya 2-3 hubainisha kuwa mtu akiweka nadhiri au kuahidi kitu asichoweza kutimiza huwa amefanya jambo baya.

Muislam wa kweli huwaheshimu wazazi wake, waalimu, makamanda, sheria na wenye mamlaka katika nchi yake. Hachezi kamari wala kupoteza wakati.

Muislam wa kweli hufanya ibada yake kwa ukamilifu humshukuru Allahu taala. Ibada haipaswi kufanywa kwa kujikalifu au bila kujijua. Inapaswa kufanwa kwa hiyari na kwa kumuonyesha Allahu taala upendo. Kumcha Allahu taala maana yake ni kumpenda sana. Umpendaye sana, hutaki kumkasirisha kwa kuhofia kuwa unaweza kuvuruga akili yake. Hivyo hivyo, ibada zetu zinapaswa kufanywa kwa namna ambayo inathibitisha upendo wetu kwake. Neema alizotujaalia Allahu taala ni nyingi mno kiasi kwamba kulipa deni la shukrani kwa kumpenda sana na kumuabudu kwa moyo safi. Kuna aina kadhaa za ibada. Baadhi ya aina za ibada ni baina ya Allahu taala na mja wake.

Pengine Allahu taala atawasamehe madhambi wale ambao hawamuabudu vya kutosha. Kuheshimu haki za watu wengine ni ibada pia. Lakini hatawaghufiria wale ambao wamewatukana watu na kuvunja haki zao mpaka wapate msamaha wa wenye haki hizo. Hadithi zifuatazo ziko katika Juzuu ya nne ya kitabu kiitwacho Ashi'at-ul-Lammat kilichoandikwa kwa Kifursi na maelezo ya kitabu mashuhuri kiitwacho Mishkaat al-Masaabih.

1- Asiewahurumia watu, Allahu taala hamhurumii.

2- Ukizuia ukatilii, utakuwa umemnusuru dhalimu na aliyedhulumiwa.

3- Ikiwa tisa kati ya kumi ya pesa zilizotumika kununua shati ni halali, moja kati ya kumi ikawa haramu, Allahu taala hatokubali sala inayosaliwa kwenye shati hilo.

4- Muislam ni ndugu yake Muislam. Hamdhulumu. Hamnyimi msaada. Hamdharau. Ni jambo baya lilioje kumvunjia heshima ndugu yake Muislamu.

5- Hatokuwa muumini wa kweli mpaka ampendelee ndugu yake jambo analolipenda yeye kwenye nafsi yake.

6- Naapa kwa jina la Allahu taala kwamba mtu ambae jirani yake hasalimiki kutokana na udhia wa mkono wake na ulimi wake si muumini.

7- Asiekuwa na huruma, hana imani.

8- Allahu taala huwahurumia wanaowahurumia watu.

9- Si katika waislamu yule ambae hawahurumii wadogo wetu wala hawaheshimu wakubwa wetu.

10- Mtu akiwaheshimu na kuwasaidia wazee, Allahu taala humtumia wasaidizi akizeeka.

11- Nyumba aipendayo sana Allahu taala ni ile inayomlea na kumtunza yatima na inayomhudumia yatima kwa ukarimu.

12- Allahu taala atamsaidia yule anayemnyamazisha msengenyaji hapa duniani na Akhera. Asipomnyamazisha msengenyaji na hali ana uwezo wa kufanya hivyo, Allahu taala atamwadhibu kote hapa duniani na Akhera.

13- Anayemsitiri ndugu yake Muislam, huwa kama ameokoa maisha ya msichana ambae kazikwa akiwa hai kwa kumtoa kaburini.

14- Mbora wa watu mbele ya Allahu taala ni yule anaemtendea wema zaidi mwenzake.

15- Uzuri wa mtu au ubaya wake unajulikana kwa kuangalia iwapo majirani zake wanampenda.

16- Anayewaudhi majirani zake kwa ulimi wake, ataingia motoni hata kama anaswali, anafunga na anatoa zaka sana. Lakini ikiwa hawaudhi majirani zake kwa ulimi wake, ataingizwa peponi.

17- Allahu taala amewapa vipenzi vyake na maadui zake vitu vyenye thamani. Lakini amewajalia vipenzi vyake tu tabia njema. [Sasa inaeleweka kwamba kauli isemayo ‘inatarajiwa kuwa makafiri wenye

tabia nzuri watajaaliwa imani mara moja kabla ya kufariki dunia, ni sahihi].

18- Thawabu za mtu anayeingilia heshima ya au mali ya mtu mwingine zitapewa yule aliyedhulumiwa. Ikitokezea kwamba ibada za mkiukaji na matendo yake yaliyo mema hayatoshi kulipia, basi atapewa madhambi ya mdhulumiwa.

19- Moja wapo ya madhambi ya kiumbe yaliyo mabaya zaidi ni kuwa na tabia mbaya.

20- Mtu anayefurahi kumuona yule anayemchukia kwenye shida, Allahu taala naye atamjaalia udhia kama huo.

21- Watu wawili walienda msikitini wakaswalia huko. Walipopewa chakula walisema kwamba walikuwa wamefunga. Walizungumza kwa muda fulani na walipotaka kuondoka Mtume (swallllahu alaihi wa sallam) akawaambia, ‘Swalini na mfunge tena kwa sababu mulikuwa mukimsengenya mtu katika mazungumzo yenu. Kusengenya huondoa thawabu kwenye ibada’.

22- Epukaneni na husda. Hakika husda hula matendo mema kama moto unavyokula kuni.

23- Kuwa na husda maana yake ni kumuhusudu mtu. Yaani kutamani aondokewe na neema aliyoipata. Si husda kutamani kupata neema kama ile aliyoipata mtu mwengine bila kutaka yeye imuondokee. Hali hii hujulikana kama ghibta.

24- Mpole hupata kheri duniani na Akhera.

25- Allahu taala hatamuingiza mja wake aliyemjalia uso mzuri na tabia njema kwenye moto wa jahannamu.

26- Abu Huraira aliambiwa na mtume "swallallahu alaihi wa sallam" “Kuwa mpole. Akauliza: ‘ Nini maana ya kuwa mpole’? mtume akamjibu “Mkaribie aliye mbali umpe nasaha, umsalimie anayekutesa, anaekataa kukupa mali yake, au elimu, au msaada, mpe (ayatakayo)“.

27- Pepo ni makao ya mtu anayejitakasa kutokana na kiburi, udanganyifu na madeni.

28- Mtume hakupenda kuswalia jeneza ya mtu aliyefariki duniani akiwa na madeni. Sahaba Qataada alichukuwa madeni kwa malipo. Kwa hiyo, mtume alikubali kuswalia jeneza yake.

29- Usiwapige wake zako. Wao si watumwa wako.

30- Mbora wenu mbele ya Allahu taala ni aliye mbora kwa wake zake. Na mie ni mbora wenu katika kuwatendea wema wake zangu.

31- Mbora wenu katika imani ni mwenye tabia nzuri zaidi na alie mpole kwa wake zake.

Hadithi nyingi kati ya hizo zilizotajwa hapo juu hupatikana katika kitabu kiitwacho Zawaajir kilichoandikwa na mwanazuoni maarufu Ibn Hajar. Ni chimbuko la maadili mema ya kiislamu. Wanazuoni wameunda kaida kadhaa kutokana na hadithi hizo.

1- Ni haramu kwa Muislam anayeishi katika nchi za makafiri kuvuruga mali yao, maisha na heshima au kuiba. Hapaswi kukaidi sheria zao wala kulaghai au kuwa mdanganyifu katika kununua na kadhalika.

2- Kunyang'anya mali ya kafiri au kumuudhi ni jambo baya zaidi kuliko kunya'nganya mali ya Muislamu. Kuwafanyia ukatili wanyama ni kitendo kibaya zaidi kuliko kuwafanyia ukatili wanadamu na kufanya kitendo hicho kwa makafiri ni kibaya zaidi kuliko kuwafanyia unyama.

3- Ni haramu kuchukuwa na kutumia mali ya mtu mwingine bila ya idhini hata kama utairejesha ikiwa haikuharibiwa.

4- Mtu akiahirisha kulipa deni na hali ana uwezo wa kulipa, atachukuliwa kuwa dhalimu na mkaidi. Ataendelea kupata laana. Kutolipa deni la mtu ni dhambi linalosajiliwa kwenye faili la matendo hata kama mtu amelala. Mtu akilipa deni lake kwa pesa au thamani ya chini au kwa vifaa visivyokuwa na faida, au ikiwa mwenye deni atarejesha mali yake pasina kuridhika, ataendelea kuwa na dhambi. Hatanusurika na dhambi mpaka amridhishe mwenye deni.

Kwa miaka elfu moja mia nne, wanazuoni wa Kiislamu wamekuwa wakitoa mafunzo kwenye mihadhara yao na vitabu kuhusu maadili mema yaliyoamrishwa na Uislamu. Kwa kufanya hivyo, wanajaribu kuwafundisha vijana tabia nzuri zilizopendekezwa na Uislamu. Vitabu vifuatavyo ni mfano tu wa vitabu vingi sana ambavyo vinaeneza maadili haya mema.

**Maktubat** kilichoandikwa na mwanazuoni maarufu Imamu Rabbani Ahmad Faaruuqi (rahmatullahi alaih), aliyekuwa walii na mujaddid wa milenia ya pili, ni kitabu chenye thamani. Sayyid Abdulhakim Arwasi, aliyekuwa Profesa wa saikolojia katika Madrasat al-Mutahassisiin, iliyokuwa madrasa kuu katika enzi za Wauthumani, alikuwa akisema mara kwa mara "Hapajaandikwa kitabu kingine kinachothaminiwa zaidi kuhusu Uislamu", na "Kitabu muhimu na kinachothaminiwa zaidi, baada ya Qurani na hadithi za mtume "swallallahu alaihi wa sallam" ni kitabu cha Imamu Rabbani''. Imamu Rabbani alizaliwa katika mji wa Serhend nchini India mwaka wa 971 H./ 1563 A.D. na akafariki dunia

huko mwaka wa 1034 H./ 1624 A.D.. Naye Abdulhakim Effendi alizaliwa Van, mji ulioko mashariki mwa Uturuki mwaka wa 1281 H./ 1874 A.D. na akafariki dunia mwaka wa 1362 H./ 1943 A.D. mjini Ankara. Katika barua ya 76 ya **Maktubat** imeandikwa: Maana ya aya ya 7 ya Sura Al-Hashr: “yote aliyokuleteeni Mtume yachukueni, na yote aliyokukatazeni epukaneni nayo”.

Ili kuepukana na maangamizi duniani na akhera, ni muhimu kuzingatia mambo mawili: Kushikamana na maamrisho na kuondokana na makatazo. Kati ya haya mawili jambo la pili ni kuu na muhimu zaidi nalo ndilo huitwa wara’ na taqwaa.

Mtu aliyefanya sana matendo ya ibada alitajwa kwa mtume. Lakini alipotajwa mtu mwingine aliyejitenga na makatazo, alisema “Hakuna jambo linaloweza kulinganishwa na wara”. Yaani kujitenga na makatazo ni jambo linalothaminiwa zaidi. Hadithi nyingine inabainisha kuwa “Wara’ ni nguzo ya dini yako”. Watu wamekuwa wabora kuliko malaika kutokana na wara’ na maendeleo yao au kutukuzwa kwao ni kwa sababu ya wara’. Malaika hutii amri. Lakini hawaendi mbali.

Hivyo kushikamana na wara’ na kuwa na taqwa ni muhimu zaidi kuliko kitu kingine. Katika Uislamu jambo linalothaminiwa zaidi ni taqwaa.

Wara’ na taqwaa maana yake ni kuachana kabisa na haramu. Ni muhimu kuachana na mubaah zisizohitajika. Tunapaswa kutumia mubaah tu kadri inavyohitajika. Mtu akitumia mubaah kama atakavyo, yaani yale mambo ambayo sheria imeruhusu, au kutumia mubaah kupita kiasi kinachohitajika, basi ataanza kufanya yanayotiliwa shaka. Na yanayotiliwa shaka ni karibu sana na haramu. Nafsi ya mwanaadamu ni yenye tamaa kama ya mnyama. Anayetembea karibu na lindi anaweza kuanguka ndani yake. Ili kudumisha wara’ na taqwa sawasawa, mtu anapaswa kutumia mubaah kadri inavyohitajika na daima asizidishe kiasi cha mubaah hasa nyakati hizi. Angalau aachane na haramu na afanye jitihada za kuachana na mubaah iliyozidi kiasi cha haja. Akifanya yaliyo mubaah kwa kiwango kisichohitajika, ni vyema afanye toba na kuomba msamaha. Anapaswa kuchukulia matendo haya kama mwanzo wa kufanya haramu. Anapaswa kurudi mbele ya Allah na kuomba msamaha. Toba hii, kuomba msamaha na ku nyenyekea kunaweza kufidia kuachana na mubaah isiyohitajika na hivyo akapata kinga dhidi ya madhara ya vitendo kama hivyo.

Kuna njia mbili za kuepukana na haramu:

**Kwanza** kuepukana na madhambi ambayo huvuruga haki za Allahu taala.

**Pili**, kuepukana na madhambi ambayo huvuruga haki za watu au viumbe wengine.

Aina ya pili ni muhimu zaidi. Allahu taala hana haja na kitu chochote. Yeye ni mwenye kurehemu. Kwa upande mwingine, wanaadamu hawahitaji tu vitu vingi, lakini pia ni wenye choyo. Mtume "swallallahu alaihi wa sallam": "Aliyevuruga haki za wanaadamu wenzake, au mali au heshima ya viumbe, anapaswa kulipa haki hizo ili asamehewe kabla ya kufa. Kwa sababu siku hiyo, dhahabu na mali havitakuwa na thamani. Siku hizo thawabu zake zitaondolewa mpaka haki itakapolipwa. Isipolipwa hatopata thawabu yoyote na atabebeshwa madhambi ya mwenye haki".

[Ibn Abidin, katika maelezo yake ya kitabu **Durr ul-Mukhtar** alisema "Mwenye haki atakapo acha kudai haki yake na mdaiwa akaendelea na kutolipia deni, sala zake za faradhi mia saba alizoziswali katika jamaa'a zikakubalika, thawabu zake zitamalizika kabisa, atabebeshwa madhambi ya mdai kisha arushwe motoni, zifidie deni hilo kama malipo ya deni". Deni moja ni sudusi ya dirhamu moja, karibu nusu ya gramu ya fedha ambayo ni sawa na kurushi ishirini na tano].

Siku moja, mtume aliwauliza sahaba: **"Mnamjua muflisi?" walisema: "Ni Yule asiyekuwa na dirhamu wala dinari (asiyekuwa na mali yeyote)". Akasema: "Muflisi katika umma wangu, ni yule atakayekuja siku ya kiama na thawabu za sala, zaka na saumu. Lakini kamtukana huyu, kamkashifu huyu na kala mali ya huyu. Basi thawabu za matendo yake mema zitachukuliwa na kupewa huyu, nyingine zipewe huyu na nyingine zipewe huyu. Thawabu zake zikimalizika kabisa, atabebeshwa madhambi yao kisha atatupwa motoni"**.

Kwa mujibu wa Maktubat, ukurasa wa 98, mtume "swallallahu alaihi wa sallam" alisem: **Allahu** taala **ni mpole. Hupenda upole. Huwapa watu wapole yale ambayo hakuwapa walio wakali au mtu mwingine"**. Hadithi hii inapatikana katika Sahih Muslim.

Aidha, mtume "swallallahu alaihi wa sallam" anasema katika hadithi iliyopokelewa na Aisha "radiyallahu anha" kwamba: **"Kuwa mpole. Tahadhari ukali na mambo yanayochukiza. Upole humpamba mtu na kuondoa ubaya"** (Muslim).

Katika hadithi nyingine inayopatikana katika Sahih Muslim, Mtume anasema. Asiyekuwa na upole katika mambo ayafanyayo, hajafanya

tendo lolote zuri”. Hadithi nyingine iliyoko katika Sahih Bukhari inasema **“Mtu nimpendaye zaidi miongoni mwenu ni mwenye upole”.**

Kwa mujibu wa Imamu Ahmad na Tirmidhi "rahmetullahi alaih": **“Aliyejaliwa upole kajaliwa kheri duniani na Akhera”**.

Kwa mujibu wa Ahmad, Tirmidhi, Hakim na Bukhari "rahmetullahi alaih" **“Haya hutokana na imani. Mwenye Imani ni mtu wa peponi. Tendo baya (fahsh) ni uovu. Na waovu ni watu wa motoni”**.

Hadithi iliyonukuliwa na Ahmad na Tirmidhi inasema: **“Nikwambieni mtu ambaye ni haramu kwa moto kumchoma. Sikilizeni kwa makini. Ni yule aliye mwepesi na mpole kwa watu”**.

Hadithi iliyonukuliwa na Tirmidhi na Abu Daud inasema: **“Watu ambao ni wapole na huwatuliza wengine ni kama mtu anayeshikilia hatamu ya mnyama wake. Akitaka kumsimamisha mnyama huyo atamtii. Akitaka kumuendeshea juu ya majabali, mnyama huyo atayaelekea kwa haraka”**.

Hadithi iliyonukuliwa na Bukhari inasema: **“Mtu akidhibiti hasira zake pamoja na kwamba ana uwezo wa kufanya analotaka, Allahu** taala **atamuita siku ya kiama akiwa miongoni mwa watu wengine, amwambie “Nenda peponi uchague hural-ain umpendaye”.**

Kwa mujibu wa hadithi [iliyonukuliwa katika vitabu vyote vya hadithi] kuna mtu aliyemuomba Mtume kumpa nasaha, akasema “Usikasirike” Mtu huyo aliporudia swali hilo, jibu likawa sawa na lilitolewa mwanzo “Usikasirike”.

Hadithi iliyonukuliwa na Tirmidhi na Abu Daud inasema: **“Sikilizeni. Niwaelezee sifa za wale watakaoingia peponi. Ni wale wasiokuwa na nguvu (mamlaka), wasiokuwa na uwezo. Wakiapa kufanya jambo, Allahu** taala **hutimiza kiapo chao. Sikilizeni. Niwaelezee sifa za wale watakao ingia motoni. Ni wale wakali, wanaotoa uamuzi kwa haraka (bila kufikiria) na ni wenye kiburi”**.

Hadithi iliyowasilishwa na Tirmidhi na Abu Daud "rahmetullahi alaih" inasema **“Mtu akikasirika na hali amesimama, anapaswa kukaa kitako. Ikiwa hawezi kupunguzaa hasira akiwa amekaa, basi na alale chini”.**

Hadithi iliyowasilishwa na Tabraani, Baihaqi na Ibn Asaakir "rahmetullahi alaih" inasema: “**Mshubiri huifanya asali chungu, hasira huchafua imani pia”.**

Hadithi iliyowasilishwa na Baihaqi na Abu Nu’aym inasema: **“Allahu** taala **humpandisha cheo anayenyenyekea kwa ajili yake”.** Mtu huyo hujidunisha na kujifanya ni mtu wa chini lakini ni mwenye hadhi ya juu mbele ya wengine. Ikiwa mtu atajichukulia kuwa mbora kuliko wengine Allahu taala atamshusha hadhi na atachukuliwa na wengine kuwa mwenye hadhi duni. Yeye ni mkuu, kwa maoni yake, lakini kwa hakika, anaonekana kuwa mwenye hadhi ya chini kuliko mbwa na nguruwe”.

Hadithi iliyowasilishwa na Bayhaqi "rahmetullahi alaih" inasema, Musa alihis- Salaam alipouliza, **“Ewe Mungu wangu. Ni nani anayethaminiwa zaidi miongoni mwa waja wako? Allahu** taala **alisema “Ni yule anayesamehe japo ana uwezu wa kumuadhibu”.**

Hadithi iliyowasilishwa na Abu Ya’laa inasema: **“Mwanaadamu akidhibiti matamko yake, Allahu taala atasitiri mapungufu yake. akidhibiti hasira zake, Allahu taala atafuta madhambi yake siku ya kufufuka. Akimuomba Allahu taala, atakubali maombi yake.”**

Kwa mujibu wa Tir-midhi, Mua’wiya alimwandikia Hadhrat Aisha "radiyallahu anha" barua akimuomba amwandikie nasaha akaandika akisema “Assalamu alaikum, Nilimsikia mtume "swallallahu alaihi wa sallam" akisema “Mwanaadamu akimridhisha Allahu taala hata kama watu watakasirika, Allahu taala atamkinga kutokana na madhara ya watu. Akiwaridhisha watu hata kama jambo hilo litasababisha ghadhabu za Allahu taala, Allahu taala humwachia watu”.

Tunamuomba Allahu taala kutuwezesha sote kushikamana na hadithi hizi zilizosemwa na aliyesema ukweli daima. Jaribu kutenda amali kulingana na matlaba yake, maisha duniani humu ni mafupi. Lakini adhabu za Akhera ni kali sana na hazina kikomo. Wenye busara wanapaswa kufanya maandalizi mapema. Tusidanganywe na urembo na ladha ya dunia. Kama heshima na thamani ya mtu ingekadiriwa na mambo ya dunia, wanaomiliki mali nyingi ndio wangekuwa wenye thamani na wabora kuliko watu wengine. Kudanganywa na uzuri wa dunia ni upumbavu.

Tuchukulie muda huu mfupi kama neema kubwa na tujitahidi kufanya ayapendayo Allahu taala. Tuwe wakarimu kwa waja wa Allahu taala. Kuna njia kuu mbili za kuepukana na mateso siku ya kufufuliwa. Njia ya kwanza ni kuyaadhimisha na kuyaheshimu maamrisho ya Allahu taala na njia nyingine ni kuwatendea wema na kuwahurumia waja wa Allahu taala. Aliyosema Mtume ni ukweli mtupu. Hakuna vichekesho, mzaha wala kupayuka katika mafundisho yake. Kulala huku macho yakiwa wazi kama sungura kutaendelea mpaka lini?

Usingizi kama huu huaibisha na kufedhehesha ni kuambulia patupu na ufukara. Maana ya aya ya 115 ya Sura Al-Muuminun ni “Je, mlidhani ya kwamba tulikuumbeni bure na kwamba nyinyi kwetu hamtarudishwa?"

Najua kwamba huna hamu ya kusikiliza maneno kama haya. Ungali kijana mtanashati na mwenye kufurahia maisha. Wategemea neema za kidunia. unatumikiwa na wanaokuzunguka. Waweza kufanya mambo yote unayotaka. Lakini haya yote yameandikwa kwa sababu tunakuonea huruma na tunataka kukufanyia kitu chenye maana namaslahi baada ya kufa kwako. Hujachelewa hata kidogo bado. Huu ni wakati wa kufanya toba. Na kumuomba Allahu taala ”. Mwisho wa tafsiri ya barua ya 98.

Akielezea tasawuf katika kitabu chake kiitwacho Ar-riyaadh at-tasawufiyya, Sayyid Abdulhakim Arwasi alisema “Tasawuf maana yake ni kutupa sifa za kibinaadamu na kujaliwa sifa kama za malaika na tabia za utukufu”. Na alinukuu kauli ya Abu Muhammad Jariir: “Tasawuf ni kujaaliwa tabia zote nzuri na kutakaswa kutokana na tabia zote mbaya”. [Abu Muhammad Jariir Ahmad ibn Muhammad ibn Husein alifariki dunia mwaka wa 311/ 923 A.D.. Alikuwa mwanafunzi wa Junaid al-Baghdadi].

Muhammad Ma’thum "rahmetullahi alaih" bin Imam Ahmad Faaruuqi "rahmatullahi alaih", mwanazuoni na mujaddid maarufu alimuandikia Mir Muhammad Hafii, mmojawapo wa magavana wa India barua iliyoko kwenye kitabu chake Maktubat, nayo ni ya 147, mambo yafuatayo: “Namuomba Allahu taala Muumba Mkuu atukinge dhidi ya kupotea njia ya Bwana wetu Muhammad "swallallahu alaihi wa sallam", kipenzi chake na mbora wa mitume yote. Ndugu yangu aziizi. Maisha ya mwanaadamu ni mafupi. Yatakayo tukumba katika maisha ya milele huko Akhera hutegemea jinsi tunavyoishi katika dunia hii. Mwenye busara katika maisha haya mafupi hapa duniani, hufanya mambo yatakayo mpelekea kuishi vizuri na kwa raha katika Akhera. Huandaa yaliyo muhimu kwa msafiri anayeelekea Akhera. Allahu taala amekupa fursa ya kutawala watu wengi, jambo ambalo linakupa fursa ya kuwatekelezea mahitaji yao. Mshukuru sana Allahu taala kwa kukuneemesha kwa jukumu hilo lenye thamani na faida. Jitahidi sana kuwahudumia waja wa Allahu taala, utapata Baraka duniani na Akhera.

Ujue kwamba ili kupendwa na Allahu Taala, unapaswa kuwa mpole kwa waja wake, kuwatendea wema, kuwasaidia na hali ya kuwa una

tabasamu na ukunjufu kwenye uso wako, na kutumia maneno laini na mepesi.

Usitilie shaka kwamba kufanya hivyo kutakuokoa kutokana na mateso ya a khera na kukuongezea neema peponi. Mtume "swallallahu alaihi wa sallam" aliyaelezea vyema mambo haya katika hadithi ifuatayo, Allahu taala ameumba na kusambaza vitu wanavyohitaji waja wake. Mja wa Allahu taala anayependwa zaidi ni Yule anayetumika kama njia ya kufikisha neema zake kwa waja wake".

Hadithi chache zilizoandikwa hapo chini, hudhihirisha faida ya kukidhi mahitaji ya Waislamu, kuwafurahisha na kukufanya uwe na subira.

Na pia zinasifia na kuhimiza upole, makini na uvumilivu, zielewe vyema. Ikiwa huwezi kuelewa baadhi yake, jifunze hadithi hizo kwa kuwauliza watu wanaojua dini yao na wanaoishi kulingana na matlaba ya elimu yao. Matamko matukufu ya mtume wetu yanaitwa hadithi. Soma hadithi zifuatazo kwa uangalifu! Tafadhali! Fanya jitihada ya kuzitilia maanani katika maneno yako na matendo.

1- Waislamu ni ndugu. Hawaumizani wala kukorofishana. Amsaidiaye ndugu yake mwislamu, Allahu taala humrahisishia mambo yake. Amwokoae mwislamu kutokana na shida za dunia, Allahu taala atamwokoa kutokana na shida za siku ya kiama. Amsitiriae mwislamu, Allahu taala atamsitiri siku ya Kiama". [Bukhari na Muslim]

2- Allahu taala humsaidia mja wake atakapokuwa anamsaidia ndugu yake Muislamu. [Muslim]

3- Allahu taala amewaumba baadhi ya waja wake ili wawatekelezee haja zao na kuwasaidia watu wengine. Wenye kuhitaji msaada watakimbilia kwa watu hawa. Waja hawa hawatahofia mateso siku ya kiama. [Tabraani]

4- Allahu taala amewajaalia baadhi ya waja wake neema nyingi. Amewaumba ili wawasaidie waja wake wengine. Wakigawanya neema za Allahu taala kati ya waja wake hakutakuwa na upungufu katika mali yao. Wasipotoa neema hizi kwa waja wa Allahu taala, atachukuwa neema zake awape watu wengine". [Tabraani na Ibn Abi Dunyaa]

5- Kumsaidia ndugu yako Muislamu haja yake ni bora kuliko kufanya itikafu kwa miaka kumi. Na hali ya kuwa siku moja ya itikafu kwa ajili ya Allahu taala, humweka mtu mbali sana na moto wa Jahannamu. [Tabraani na Haakim]

6- Mwanaadamu akimsaidia ndugu yake Muislamu, maelfu ya malaika watamuombea dua. Akienda kufanya kazi hiyo, dhambi moja litafutwa kwa kila hatua na atapewa neema siku ya kiama. [Ibn Maaja].

7- Anayemsaidia Muislam katika shughuli zake, kwa kila hatua atapewa thawabu sabini na ataghufuriwa madhambi sabini. Hali hii itaendelea mpaka kazi hiyo itakapomalizika. Ikimalizika madhambi yote yataghufiriwa. Akifariki dunia akiwa anafanya kazi, ataenda peponi bila kuhesabiwa. [Ibn Abi Dunyaa]

8- Anayepambana na mamlaka ya dola ili kumuokoa ndugu yake kutokana na shida na akampatia raha, Allahu taala atamuezesha kupita haraka kwenye siraat watu wengine watakapoteleza. [Tabraani]

9- Kitendo akipendacho Allahu taala ni kumfurahisha Muislam kwa kumpa nguo na chakula au kumkidhia haja nyenginezo. [Tabraani]

10- Kitendo akipendacho Allahu taala baada ya vitendo vya faradhi ni kumfurahisha Muislam. [Tabraani]

Maamrisho ya Allahu taala yanaitwa faradh. Hivyo, kutokana na hadithi hii tukufu, inaeleweka kuwa wanaotenda vitendo vya ibada vilivyo vya faradhi hupendwa zaidi na Allahu taala. Mambo yenye madhara na uovu ambayo Allahu taala ameyakataza kufanywa yanaitwa haram. Allahu taala huwapenda wale wanaepukana na haram kuliko wale wanaofanya vitendo vya faradhi. Ni faradhi kuwa mvumilivu na ni haramu kuwa mwepesi wa kukasirika.

11- Mtu akimhudumia vyema Muislamu, Allahu taala huumba malaika kutokana na kitendo hicho kizuri. Malaika huyu atamuabudu Allah wakati wote na thawabu za ibada yake zitamuendea mtu huyu. Akifariki na kuzikwa kaburini, malaika huyo atakuja kwenye kaburi lake kwa uso wenye mng'ao na urafiki. Atakapomuona, malaika atatulia na kuchangamka. Atamuuliza "Wewe ni nani?" jibu litakuwa "Mimi ni wema uliomtendea fulani na fulani na furaha uliyomletea moyoni mwake. Allahu taala amenituma nije nikufurahishe leo na nikutetee siku ya kiama na nikusindikize hadi peponi".

12- Mtume "swallallahu alaihi wa sallam" aliulizwa "Ni mambo yapi yaliyo muhimu yatakayompelekea mtu kuingia peponi?" Akajibu: "Uchangamfu na uvumilivu". Na alipouliuzwa sababu kuu zinazowapelekea watu kuingia motoni alisema: "Kusikitika sana unapoharibikiwa na neema za kidunia, kufurahi ukipata neema hizi na kuvuka mipaka". [Tirmidhi, Ibn Hibbaan na Baihaqi]. Dalili ya uchamungu ni kuwacha makatazo yake.

13- Mwenye imani thabiti miongoni mwenu ni yule mbora zaidi katika tabia na mpole kwa mke wake. [Tirmidhi na Hakim]

14- Mwanaadamu atapata madaraja ya juu peponi kutokana na tabia yake nzuri.

Hasira zitamburuta mwanaadamu kwenye lindi la Jahannamu. [Tabraani]

15- Ibada iliyo rahisi na nyepesi zaidi ni kusema kidogo na kuwa mvumilivu. Nasema tilia maanani rehma hili! [Ibn Abi Dunyaa]

16- Mtu mmoja alimuuliza mtume "swallallahu alaihi wa sallam" “Amali nzuri ni zipi?” mtume akajibu “Kuwa mvumilivu”. Mtu huyo aliondoka na baada ya sekunde chache alirejea na kuuliza swali hilo hilo. Mtume alisema tena “Kuwa mvumilivu”. Mtu huyo aliend zake na baada ya muda mfupi tu akarejea na akamuuliza suala lile lile tena mtume “ Amali ipi ndiyo aipendayo Allah zaidi?”. Mtume alitoa jibu hilo hilo, “kuwa mvumilivu (kutokasirika)”. Mtu huyo alimuuliza tena mtume ”Kitendo gani ndicho huthaminiwa zaidi?” mtume alimgeukia na kumwuliza “Huelewi kinachokusudiwa na ‘kuwa mvumilivu? Jitahidi sana. Usimkasirikie mtu yeyote”.

17- Nakuahidini kuwa Muislamu asiyegombana na mtu yeyote, asiemkasirisha mtu yeyote kwa ulimi wake, hata kama yale ambayo angesema yangekuwa ya kweli, ataingia peponi. Nakuahidini kuwa asiyedanganya wala kufanya utani au kuwachekesha watu wengine ataingia peponi. Nakuahidini kuwa mvumilivu atapata madaraja ya juu peponi. [Abu Daud, Ibn Maaja na Tirmidhi]

18- Katika hadithi kudsi Allahu taala anasema “Naupenda Uislamu niliokuteremshieni. [yaani nawapenda watu waliokubali dini hii na kushikamana na maamrisho yake]. Kuwa kwenye dini hii hujalizwa [hukamilishwa] tu na kuwa mkarimu na mvumilivu. Kila uchao, toa ilani kuwa umeikamilisha dini yako kwa mambo haya mawili”. [Tabraani]

19- Uvumilivu huyayusha na kuangamiza madhambi jinsi maji yanavyoyeyusha theluji. [Tabraani]

20- Allahu taala huwapenda na kuwasaidia walio wapole. Hawasaidii wakali. [Tabraani]

21- Ni watu aina gani walioharamishwa kuingia Jahannamu na kuchomwa na moto wa Jahannamu? Sikilizeni kwa makini ni wale wote ambao ni wapole wasiokasirika. [Tirmidhi na kwenye barua iliyotajwa hapo juu]

22- Kufanya amali kwa utulivu na upole ni kipaji kikubwa sana kutoka kwa Allah. Kukosa subira na kuwa na pupa ni mbinu ya shetani. Kuwa mvumilivu na makini ni mambo ayapendayo Allahu taala. [Abu Ya'laa]

23- Kutokana na upole wake na ulaini wa maneno yake mtu anaweza kupata vyeo vya wanaofunga mchana na kuswali usiku. [Ibn Hibbaan]

24- Allahu taala humpenda mtu ambae akikasirika huwa mpole na hivyo akadhibiti hasira zake. [Isfahan]

25- Tafadhali sikilizeni kwa makini nakwambieni. Anayependa kufikia madaraja ya juu peponi anapaswa kuwa mpole kwa mtu asiye na adabu. Anapaswa kumsamehe mtu atendae mambo yake kwa dhuluma. Anapaswa kuwa mkarimu kwa mwenye choyo. Anapaswa kuwatunza marafiki au jamaa ambao hawamuonei huruma. [Ibn Abi Dunyaa]

26- Sio mwenye nguvu yule anayewaangusha chini wenzake wakati wa kupigana. Bali Mwenye nguvu ni yule anayedhibiti nafsi yake anapokasirika. [Bukharii na Muslim]

27- Amsalimiaye mtu kwa uso wenye bashasha, atapewa thawabu kama zile wanazopewa watoa sadaka.

28- Kutabasamu mbele ya ndugu yako Muislam, kumfunza mambo mema na kumkataza mabaya, kuwasaidia wageni kufika wanakoelekea, kuondoa mawe, miba, mifupa na vitu vingine ambavyo vinaudhi na vyenye madhara njiani, na kuwapa watu maji ya kunywa ni sadaka. [Tirmidhi]

29- Kuna makasri (majumba makubwa ya kifahari ambayo hukaa wafalme) peponi. Mtu aliye ndani ya mojawapo ya makasri hayo anaweza kuona sehemu yoyote anayotaka na kuonekana katika sehemu yoyote achaguayo. Abu Mali al-Ash'ari (rahmatullahi alaihi) alipouliza ni nani ambao wangepewa makasri kama hayo, mtume "swallallahu alaihi wa sallam" alisema “watakao kuwa na lugha ya kuvutia, wakarimu na wanaotafakari uwepo na ukubwa wa Allahu taala na wakamuomba wakati watu wengine wamelala”.

30- Nimezinukuu hadithi hizo kutoka kwenye kitabu cha hadithi kijulikanacho kama Targhiib wa Takriib, kitabu kimoja wapo kati ya vitabu vya hadithi vinavyothaminiwa. Abdu al Adhim Mundhir (rahmatullahi alaih), mwandishi wa kitabu hicho ni mmoja wapo wa wanazuoni maarufu wa hadithi. Alizaliwa mwaka wa 581 H./ 1185 A:D, akafariki dunia mwaka wa 656 H. / 1258 A.D. nchini Misri.

Allahu taala atuwezeshe kushikamana na hadithi zilizoandikwa hapo juu maishani mwetu. Jiangalie! Ikiwa matendo yako yanalingana nazo, mshukuru Allahu taala. Ikiwa una tabia zisizolingana na matlaba ya hadithi hizo, muombe Allahu taala akurekebishe. Ikiwa matendo ya mtu yanaenda kinyume na matlaba ya hadithi hizo, bado kuna fursa kubwa kwake yeye kujua makosa yake na kumuomba Allahu taala kumwezesha kujirekebisha. Yule ambaye hashikamani na mafundisho hayo wala hasikitiki kwa kushindwa kufanya hivyo, basi huyo hautilii maanani Uislamu. Tunapaswa kumuomba Allahu taala kutukinga kutokana na hali mbaya kama hiyo!

Pongezi kwa wale waliofanikiwa,

Fedheha kwa maskini, waliokosa!

Mwisho wa tafsiri kutoka kwa Maktubat Ma'thuumiyya.

Hadithi zilizoandikwa hapo juu huwaamuru waislamu kuwa na maingiliano ya upole, huruma na udugu. Ambae sio Muislamu huitwa kafiri. Imeandikwa kwenye ukurasa wa thelathini na tatu kwamba Muislamu anapaswa kuwa mpole kwa makafiri pia na asiwaudhi. Hivyo, makafiri watakuwa wameonyeshwa kuwa Uislamu huamrisha kuwa na uvumilivu, kuishi kwa udugu na kufanya kazi kwa bidii. Hali hii itawapelekea walio waaminifu kusilimu kwa hiari.

Jihadi ni faradhi. Dola hupambana na maadui sio tu kwa kutumia mizinga na panga lakini kwa kutumia pia mbinu za vita baridi, propaganda na machapisho. Kila Muislasmu hufanya jihadi kwa kuonesha tabia nzuri na kutenda mema. Kufanya jihadi maana yake ni kuwalingania watu kuingia katika dini ya Uislamu. Inaeleweka pia kuwa kuonyesha ukarimu kwa makafiri, na kutowaudhi ni jihadi. Kwa hiyo ni faradhi kwa kila Muislamu kuishi na watu kwa tabia nzuri".

Hadhrat Muhammad Ma'thuum Faaruuqi (rahmatullahi alaih) mwandishi wa barua hiyo ndefu, ni mmoja wa wanazuoini na mawalii maarufu. Alizaliwa mjini Serhand, huko India mwaka wa 1007 H., akafariki dunia mwaka wa 1079 H. / 1668 A.D.. Amezikwa katika kaburi kubwa lililoko kwenye masafa ya mita chache kutoka kwa kaburi la babaake. Alitoa nasaha kwa Waislamu, viongozi wa serikali, mtawala wa zama zake, Sultan Alamghir Evrengzib "rahmetullahi alaih" kupitia kwenye barua zake na ziliwapelekea kuwa na udugu, uvumilivu, huruma, na raha na utulivu duniani na furaha kubwa zaidi akhera.

Zaidi ya watu 140,000 walihudhuria makongamano na mihadhara yake. Matokeo yake ni kwamba walipata madaraja ya juu katika tasawuf na uwalii. Mbali ya wanafunzi wake wateule, idadi ya watu

waliorekebisha imani na tabia zao iliongezeka na kufikia laki kadhaa wa kadhaa. Zaidi ya mawalii mia nne waliosomeshwa nae walifikia kiwango cha irshad.

Kila mmoja wapo aliwaokoa maelfu ya watu kutokana na maangamizi, ujinga na upotofu katika miji walikotumwa. Vijana wake watano wote walikuwa wanazuoni na mawalii. Na vizazi vyao wote vimekuwa hivyo. Waliandika vitabu vingi vyenye thamani vinavyo waelimisha watu.

Muislam wa kweli haamini mambo ya kimaajabu. Anapuuza vitu kama vile uchawi, kisrani, upigaji ramli, na hirizi zenye maandishi yasiyotokana na Qurani. Hupuuza pia shanga za bluu, uwekaji kandili, nyaya na nyuzi kwenye mawe ya makaburi na wale wote wanaodai kuwa wanafanya miujiza. Kwa kweli mambo mengi kama hayo yamewasilishwa kwetu kutoka kwenye dini nyingine.

Mwanazuoni mkuu Imamu Rabbani "rahmatullahi alaih" huwajibu wanaotarajia miujiza kutoka kwa wanadini kama ifuatavyo.

“Watu huwatarajia wanadini kufanya miujiza. Inawezekana baadhi yao wasifanye miujiza laikini bado wako karibu sana na Allahu taala kuliko watu wengine? Muujiza mkuu ni kujifunza Uislamu na kuishi kulingana na mafundisho yake.

Utafiti wa hivi karibuni uliofanywa katika chuo kikuu cha Stanford Marekani umedhihirisha kuwa baadhi ya watu, ukali na ukubwa wa hisia zao za sita zinawawezesha kufanya mambo kama vile kuhesabu vitu vilivyoko kwenye boksi, kusoma maandishi yaliyomo ndani ya bahasha iliyofungwa, kuwasiliana na mtu aliye kuwa mbali sana au kusoma fikra za mtu. Watu wa mbali na dini zote walishiriki katika jaribio hilo na kupata mafanikio sawa. Wakati mwingine, huko mashariki ya mbali, katika nchi za China na India, watabiri wa Kichina na Fakirwav wa India, wameweza kutushangaza kwa kuonyesha stadi zisizofikirika. Baadhi yao huonekana kana kwamba wanaruka angani huku wengine wakikwea kamba zilizotupwa juu pasina kutegemea kwenye kitu chochote. Kwa upande mwengine Ubudha, mfumo wa imani inayoshikiliwa na Wachina, ni kama mfumo wa falsafa. Buddha, (563-483 KK), Confucius (531-479 KK) na Loatse walikuwa wanafalsafa mashuhuri. Misimamo waliyofundisha ilikuwa kaida za kimaadili. Buddha aliwafundisha watu kutupilia mbali tamaa, kuwa na tabia ya kujinyima raha, kutenda mema, kuwa mvumulivu, kusaidiana na kupambana dhidi ya maovu. Anasema “Tenda jinsi unavyotaka utendewe”. Lakini hamtaji Allahu taala. Ingawa Buddha alisema kuwa

alikuwa mwanaadamu tu, wanafunzi wake walimfanya mungu baada ya kifo chake. Walimjengea mahekalu na Ubudha ukabadilishwa na kuwa aina fulani ya dini.

Dini ya Kiasli ya Wahindi (ya kuabudu moto) ni aina fulani ya kuabudu masanamu. Waliabudu baadhi ya wanyama (kama vile ng'ombe) licha ya kuabudu masanamu. Ubudha na kuabudu moto si dini. Lakini ukweli uliopo ni kwamba baadhi ya wahusika huonyesha uwezo unaofanana na miujiza. Hupata uwezo huo kupitia mafunzo maalum ya nidhamu ambayo yanahusu kujizuia na matamanio ya kimwili, mafunzo maalum ya kimwili, na kufanya kazi ngumu kwa muda mrefu. Hivyo hivyo, usumaku ambao unaweza kumgandisha mtu na uhiponozi ambao kwao mtu hupewa amri kupitia ufunuo na matendo yake hudhibitiwa, ni aina fulani ya nguvu walizojaaliwa baadhi ya watu.

Tunachoona ni kwamba hiyo si miujiza. Ni vipawa tu vya kiajabu. Leo, wanasayansi wamegundua kuwa karibu watu wote wana vipaji vya namna hii kwamba baadhi yao wanavyo katika umbo lililoendelea zaidi kwamba baadhi ya watu wanaweza kuendeleza uwezo wao kupitia kwenye mifumo maalum na kwamba kila mtu ataweza kuamsha hisia yake ya sita kwa kutumia mbinu mpya na rahisi ambazo hatimaye zitagundulika.

Basi mtu aliyepewa aina fulani ya hisia ya sita iliyoendelezwa akiionyesha kama miujiza na siyo stadi, basi huu lazima uchukuliwe kama ulaghai.

Imam Ahmad Rabbani "rahmetullahi alaih" katika barua yake ya 293 aliandika "Maajabu na miujiza ni ya aina mbili. Aina ya kwanza ni elimu na maarifa ambayo ni ya dhati ya Allahu taala sifa zake na matendo yake. Elimu hii haiwezi kupatikana kwa kufikiri au kutumia akili. Allahu taala huwajaalia vipenzi vyake elimu hii.

Aina ya pili huhusu mambo ya dunia yasiyoelezeka. Miujiza ya aina hii inaweza kupewa makafiri na vipenzi vyake Allah pia.

Aina ya kwanza ya miujiza ni yenye thamani. Hupewa wale walio kwenye njia ya ukweli na wapendwao na Allah. Lakini wajinga hudhani kuwa aina ya pili ndiyo yenye thamani.

Yeyote anayeitakasa nafsi yake kwa kujitenga na watu, na kujinyima chakula anaweza kuelewa maajabu ya viumbe. Lakini kwa vile watu wengi hutilia maanani mambo ya kidunia, huwachukulia walio na aina ya pili kuwa mawalii. Hawawatambui mawalii wa kweli. Wanasema kwamba wangelikuwa mawalii halisi wangekuwa na uwezo

wa kutoa habari juu ya hali yetu. Wanawakataa waja wa Allahu taala awapendao”.

Katika barua ya 260, aliandika “Kuwa walii maana yake ni kuwa karibu sana na Allahu taala.

Miujiza inayohusiana na viumbe inaweza kupewa wale waliofikia cheo hiki. Wingi wa miujiza si ithibati kwamba walii (anayeifanya) ni wa cheo cha juu. Walii si lazima ajue kwamba miujiza inatokea kwake. Allahu taala anaweza kuidhihirisha sura ya mawalii katika nchi mbalimbali kwa wakati mmoja. Anaonekana akifanya mambo yanayostaajabisha katika maeneo yaliyo tofauti kabisa. Lakini huwa hatambui mambo haya. Mawalii wengine wanaweza kutambua hali yao, lakini hawawaambii wageni kwa sababu hawawathamini”.

Ibn Hajar Makki "radiyallahu anhu", kipenzi cha wanazuoni wa Ahl as-Sunna na ambae maneno yake huzingatiwa kama ushahidi huwasilisha hadithi zifuatazo kabla ya sura inayoitwa ‘Ihtiqaar’ katika kitabu chake kiitwacho Zawaajir  “Naapa kwa jina la Allahu taala kwamba ibada ifanywayo na wale waliokula chembe ya haramu haitokubaliwa kwa muda wa siku arubaini”, na “Anaesali akiwa amevaa shati aliyonunua kwa kutumia pesa za haramu sala yake haitokubaliwa”, na “Zaka inayotolewa kutokana na pesa za haramu haitokubalika. Madhambi yake hayatapunguzwa”. Sufyan Thawri anasema kwamba: “kufanya mambo mema na kuweka misingi kwa kutumia pesa za haramu ni kama kuondoa uchafu kwa mkojo”.

Muislam wa kweli hafanyi ibada kwa ria. Ibada hufanyika kwa siri au kwa jamaa misikitini. Muislam mzuri akitaka kufanya jambo zuri au kumpa mtu sadaka, hufanya hivyo kwa siri na hamuudhi wala kumvunjia mtu heshima kwa kumkumbusha kitendo alichomfanyia. Allahu taala amesisitiza jambo hili katika Qurani tukufu.

Kwa ufupi, Muislamu wa kweli ni mwanaadamu kamili aliye na sifa zote za tabia nzuri, ni mwenye heshima, ni msafi sana kimwili na kiroho na huwa muaminifu kwa kila hali.

Imamu Ghazali, mwanazuoni maarufu (rahmatullahi alaihi) [450 H. (1058 A.D.)-505 H. (1111 A.D.)], katika kitabu chake kiitwacho Kimyaa Sa’adat kilichochapishwa miaka 900 iliyopita kwa Kifursi, aliwaainisha wanadamu katika makundi manne: “Kundi la kwanza ni wale wasiojua lolote isipokuwa kula, kunywa na kufurahia starehe za kidunia katika kundi la pili kuna wale wanaotumia mabavu, wakawadhulumu watu na wakawa wakatili kundi la tatu ni la wale wanaowaghilibu watu na kundi

la nne ni la waislamu wanaoshikamana na maadili yaliyotajwa hapo awali".

Jambo linalopaswa kukumbukwa ni kwamba kuna njia inayounganisha moyo wa mwanaadamu na Allahu taala. Ni muhimu kufikiria juu ya namna ya kuwasambazia watu nuru ya Uislamu. Mtu anayehisi nuru ya Uislamu moyoni mwake, hua na majuto kwa madhambi yake na huipata njia ya ukweli. Kama watu wangeukubali Uislamu, wangetokomeza maovu, udanganyifu, vita, dhuluma, na ukatili. Kwa hivyo, ni wajibu wetu sote kuwalingania watu dini ya Uislamu duniani kote, huku tukiwabainishia umuhimu wake na mambo yote yanayoihusu. Ni jihadi kufanya hivyo.

Wahutubie watu daima kwa lugha nzuri na laini na uelewa wa hisia zao, hata kama ni wa dini nyingine. Hii ni amri ya Allahu taala katika Qurani tukufu. Imeandikwa katika vitabu vya fiqhi kwamba ni dhambi kudhuru hisia za wale wasio waislamu au kumdhihaki mtu kwa vile ni kafiri. Muislamu anayefanya hivyo ataadhibiwa. Lengo letu ni kumfundisha kila mtu ubora wa Uislamu na ukweli kwamba jihadi hii inaweza kufanyika tu kwa kutumia lugha yenye kuvutia, elimu, uvumilivu na imani. Anayetaka kumridhisha mtu juu ya jambo lolote anapaswa kuliamini mweyewe kwanza.

Muislam hua mwenye subira daima. Asipofanya hivyo atapata shida katika kuelezea imani yake. Hakuna dini nyingine iliyo wazi na yenye mantiki kama Uislamu. Anayejua umuhimu wa dini hii anaweza kumthibitishia mtu yeyote kwamba dini hii ndio dini pekee ya ukweli. Tusiwachukulie watu wa dini nyingine kama watu wenye hasira. Ni kweli kwamba kukufuru ni jambo baya daima. Kwa vile ukafiri ni mwenendo wa maisha wenye madhara na ufisadi usababishao maangamizi duniani na Akhera, Allahu taala aliwajalia watu dini ya Uislamu ili waishi kwa udugu, raha na amani katika dunia hii na waepukane na mateso ya siku ya kiama. Makafiri ni maskini waliokosa njia hii ya furaha. Tunapaswa kuwahurumia na tusiwadhuru hata kidogo.

Hata kuwasengenya ni haramu. Haiwezekani kujua wazi iwapo mtu ni wa peponi au motoni mpaka atakapotoa pumzi zake za mwisho.

Dini zote za mbinguni humuamini Mungu mmoja isipokuwa zile ambazo zimechafuliwa. Katika Qurani, Allahu taala huwahimiza watu wote kufuata njia ya ukweli. Anaahidi kuwa atamsamehe madhambi yake yaliyopita mwanaadamu anayeshikamana na njia hii. Walio katika dini nyingine ni maskini waliodanganywa na shetani au wasiojua lolote

kuhusu Uislamu. Wengi wao wana bahati mbaya. Ijapokuwa wanamuamini Mungu mmoja kama sisi na wanajaribu kupata upendo wake, wamepotoshwa. Tunapaswa kuwaonyesha njia ya kweli kwa kutumia subira, lugha yenye mvuto, hoja na mantiki.

Kabla ya kuchafuliwa na mwanaadamu, dini zote zinazofundisha uwepo wa Mungu mmoja, zilikuwa sawa katika misingi ya imani. Dini kuu tatu za Uyahudi, Ukristo na Uislamu humuamini Mungu mmoja na huamini kuwa mitume wote walikuwa wanadamu kama sisi. Lakini Wayahudi walimkataa Hadhrat Issa na Muhammad "alaihimus-salaam" na Wakristo ambao hawakujiokoa kutokana na kuabudu masanamu, walidhani kuwa Hadhrat Issa "alaihis-salaam" alikuwa mwana wa mungu ijapokuwa Issa "alaihis-salaam" aliwaambia kuwa “Mimi ni mwanaadamu kama nyinyi”, “Mimi si mwana wa mungu”. Bado wanaabudu miungu watatu wajulikanao kama baba, mwana na roho mtakatifu.

Papa waliotambua kuwa huu ulikuwa uongo, kama vile Papa Honorius, walijaribu kuufanyia marekebisho mtazamo huo. Lakini urekebishaji wa imani hii potofu unaweza kufanyika tu na Uislamu ambao Allahu taala alimfunulia mtume wake wa mwisho Muhammad "swallallahu alaihi wa sallam". Hivyo, hakuna anayeweza kukana ukweli kwamba Uislamu ambao una misingi yote ya dini tatu na ambao umezitakasa kutokana na ushirikina uliopenyezwa ndani yake, ndio dini pekee ya kweli.

Bwana Fellowes, Mzungu aliyesilimu, alisema “Martin Luther alijaribu kuifanyia marekebisho imani potofu ya Ukristo bila kujua kwamba Muhammad "swallallahu alaihi wa sallam" alikuwa amefanya hivyo tayari kwa kuutangaza Uislamu miaka 900 kabla yake. Ndiyo maana ni muhimu kuukubali Uislamu kama chapa ya Ukristo iliyotakaswa kikamilifu na kuamini kuwa mtume Muhammad "swallallahu alaihi wa sallam" ni mtume wa mwisho”.

# HOJA ZISIZOPINGIKA

[Kitabu HUJAJ QAT'IYYA kilichoandikwa na Abul barakat Abdullah Suwaydi wa Baghdad kwa lugha ya Kiarabu. Kilipigwa chapa nchini Misri mwaka wa 1323H [1905 A.D.], na toleo jipya likafanywa kwa mchakato wa kufidia huko Istanbul.

Tafsiri yake ya Kituruki, iliyofanywa na Allama Yusuf Suwaydi, ilipigwa chapa katika jumba la kupiga chapa la Kurdistan lililoko Misri mwaka wa 1326H [1908 A.D.]. Suwaydi Abdullah Efendi alizaliwa huko Baghdad mwaka wa 1104H. Baada ya kuhiji mwaka wa 1137H, alipewa ijaza kutoka kwa Abdulghani Nablusi [1050-1143H] (1730 A.D.) mjini Damascus, na ijaza nyingine alipewa na Ali Efendi wa Istanbul [1099-1149 H.]. Alifundisha kwa miaka mingi huko Baghdad. Aliandika vitabu vingi vyenye thamani. Babu yake wa thelathini ni Abu Ja'far Abdullah Mansur, mmoja wa Makhalifa wa dola la Waabbasi.

Nadhir Shah [1099-1160 (1746 A.D.)], mtawala wa Irani, aliwaitisha mkutanoni wasomi wa Iran na Bukhara akawaamuru kujadiliana na kufikia hitimisho la pande mbili kuhusu ni lipi kati ya makundi ya Kisunni na Kishi’a ni la ukweli na wakamteua kuwa kiongozi wa mjadala huo. Kitabu kiitwacho HUJAJ QAT’IYYA, kinachotoa maelezo kuhusu mazungumzo yaliyofanyika katika mkutano huu, ni chenye thamani kubwa. Baada ya kuzungumza kwa muda mrefu na wanazuoni wa Kishi’a katika mkutano huo, yeye (Abdullah Suwaydi) alithibitisha kuwa kundi la Wasunni ndilo lilikuwa la ukweli. Shah alipendelea uamuzi huu na kumpongeza. Alifariki dunia siku ya Jumamosi, tarehe kumi na moja Shawwal mwaka 1174H [1760 A.D.]. Alizikwa karibu na kaburi la Hadhrat Ma'ruf Kerhi 'rahmatullahi alaih ', ambae alifariki dunia mwaka wa 200H [815 A.D.].

Alipouliwa Shah Huseyn Safawi, mfalme wa tisa na wa mwisho wa dola la Safawi nchini Iran, na Waafghani mwaka wa 1142H [1729 A.D.], hali ya fujo ilianza huko Uajemi. Mwana wa Shah, Tahmasib II, alikuwa mtu asiye na uwezo na mpenda mambo ya anasa. Kwa hiyo, waziri wake aitwaye Nadhir akachukuwa hatamu za uongozi. Aliwafukuza Waafghan kutoka Iran na kuuteka tena mji mkuu, Isfehan. Aliizingira Baghdad, ambayo ilikuwa ikiongozwa na Ahmad Pasha. Miezi minane badae jeshi lililoongozwa na Uthman Pasha, ambae lakabu yake ilikuwa Lame, liliwasili kutoka Istanbul na kulifukuza jeshi la Irani.

Nadhir Shah alikuwa Shah wa Iran mwaka 1148. Aliuteka mji wa Delhi. Akamwaga damu nyingi sana. Kisha akaziteka nchi za Afghanistan na Bukhara. Baada ya kuandaa jeshi kubwa, alielekea Baghdad na Musul. Lakini aliposhindwa kuiteka miji hiyo, alirudi Najaf.

Alipewa jina la utani Shahinshah yaani mfalme wa wafalme. Aliwatuma mabalozi kwenye dola la Wauthumani na kupendekeza kupanga mjadala wa kisomi ili kuamua ni kundi lipi kati ya makundi ya Kisunni na Washi'a Waimamiyya lilikuwa la ukweli.

Ili kuondokana na mitazamo tofauti tofauti ya kiimani kati ya Wasunni na Washi'a na kuyaunganisha makundi hayo, kwa kushikilia lile linaloonekana kuwa la ukweli, wanazuoni kutoka kwenye makundi hayo mawili walikutana kwa amri ya Nadhir shah. Abdullah Efendi aliwasilisha hotuba akaelezea mambo kiuwazi na kiundani, huku akitoa hoja za ki taala mu hivi kwamba Washi'a waliduwaa na kushindwa kumjibu. [Maswali yaliyoulizwa na majibu yaliyotolewa na pande zote mbili yaliandikwa na kuchapishwa katika kitabu kiitwacho HUJAJ QAT'IYYA.

Gavana wa Baghdad Ahmad Pasha aliniita. Nilipofika huko, Ahmad Agha, mmoja wapo wa maafisa wa Ahmad Pasha, aliniambia kwamba Pasha alitaka kunituma kwa Nadhir Shah. Nilimuuliza kwa nini. Alisema, "Shah alimuomba msomi wa Sunni.Utafanya mjadala na wanazuoni wa Kishi'a ili kuona iwapo mihimili ya Kishi'a ni sahihi. Ikiwa hivyo, basi Ushi'a utatangazwa kuwa dhehebu la tano".

Nikasema, "Ewe Ahmad Agha. "Hujui kwamba Waajemi ni wakaidi, watu wenye vichwa vigumu?

Je, unafikiri watakubali maneno yangu? Hasa Shah wao, ni mwenye ukatili na kiburi. Nitawezaje kutoa hati zinazoonyesha kwamba njia yao si sahihi. Mtu anawezaje kuthubutu kuongea nao. Wao tayari wamekataa hadithi ambazo ni lazima nizitoe kama ushahidi. Wanakataa vitabu vya kidini. Wanafafanua aya tukufu kwa namna ambayo inaendana na malengo yao. Nitawezaje kuthibitisha kwao ukweli kwamba inaruhusiwa kufanya masah kwenye soksi mbili wakati wa kutawadha. Wepesi wa kupangusa kwenye soksi (masah) umeidhinishwa na sunna tukufu. Hadithi inayoelezea ruhusa hii ilisimuliwa na masahaba wanaozidi sabini. Mmoja wao ni Hadhrat Ali "karramallahu wajhah". Nikiwaambia ukweli huu, watasema kuwa zaidi ya sahaba mia moja wameripoti kuwa jambo hili haliruhusiwi. Ikiwa nitawaambia kwamba maneno wanayoyachukulia kuwa hadithi yamezuliwa, wataniambia hayo hayo. Watasema, tutakujibu yale yote

utakayowasilisha.' Kwa sababu hii, naomba Hadhrat Pasha aniwie radhi kutokana na wasiwasi wangu kuhusu wajibu huu”.

Alisema, “Haiwezekani. Pasha amekuteua wewe kutekeleza wajibu huu. Ni lazima umtii. Usithubutu kupinga amri yake”.

Asubuhi iliyofuata nilikuwa na mazungumzo marefu na Ahmad Pasha. Alisema, "Nenda ukashughulikie suala hilo". Naomba Allahu taala akujalie ufanisi kwenye majadiliano na utoaji hoja Ikiwa wanaonyesha ukaidi na majivuno wakati wa mjadala, toa maelezo kwa ufupi. Lakini usiwaache waondoke bila kupata jibu. Wakikubali ukweli na kuzungumza kwa busara, usisite kusema mambo yote unayoyajua. Usikubali kamwe kushindwa. Nadhir Shah atakuwa Najaf sasa. Jitahidi kufika huko siku ya Jumatano” Mimi na watu wengine wachache tuliondoka. Nikiwa safarini, nilifikiri juu ya majibu na ushahidi ambao ningetoa. Watu niliokutana nao njiani waliniambia kwamba Shah alikuwa amewaalika karibu mufti wa Kishi’a sabini.

Niliwaza na kuwazua. Nikijizuia kusema ukweli mbele yao nitakuwa nimekosea. Na bado kulikuwa na hofu ya kuwa wangeweza kubadilisha maneno yangu kabla ya kuwasilishwa kwa Shah. Niliona kwamba ni bora kumuomba Shah ahudhurie mjadala. Masaa mawili yalikuwa yamesalia kufika Najaf, alipotujia mtu akasema, "Kwa nini mmekawia? Shah anakusubirini". Nilitaka kujua iwapo ilikuwa kawaida yake kuwatuma watu kwa ajili ya kuwalaki wageni wake njiani. Alisema, "Hapana. Wewe ni mtu wa kwanza ambaye Shah amemtumia ujumbe na kumuomba afanye haraka." Baada ya kusikia maneno hayo, nilijiambia, "Shah amekusudia kunilazimisha kukubali mihimili ya mtazamo wa Waimamiyya (Washi’a). Atanishinikiza na pengine anilazimishe. Lakini sitowaruhusu kuniweka katika hali ngumu, siwaogopi. Sitosita kusema ukweli hata kama ningejua kwamba wangeniua. Hadi sasa, waislamu wamekuwa katika hali ngumu mara mbili. Mara ya kwanza ni wakati mtume "swallallahu alaihi wa sallam" alipofariki dunia. Halafu Abu Bakr as-Siddiq "radiyallahu anhu" akawaokoa na kuwatuliza. Mara ya pili, ni wakati Al-Ma´mun [(Mtoto wa Harun Rashid) alipenda Shia] aliposema kwamba Qurani ni kiumbe. Ahmad bin Hanbal [164H-241H, Baghdad] "rahmatullahi alaih" aliwaokowa Waisilamu kutokana na fitna hii. Na sasa imebainika kuwa fitna ya tatu inataka kuzuka. Nikikosea au kusita, inaweza kuendelea mpaka mwisho wa dunia. Maendeleo ya Uislamu au kudhoofika kwake hutegemea njia moja au nyingine. Sasa nitaandama njia ya kukomesha fitna hii”. Niliamua kujitahidi na kuwa mvumilivu. Nilijitolea muhanga.

Bendera mbili zilionekana kwa mbali. Tulipofika karibu, niliona mahema ya kifalme. Hema la Shah lilikuwa limejengeka juu ya mihimili saba. Kulikuwepo maelfu ya washika gadi. Mmoja wao alitufuata. Aliulizia hali ya Ahmad Pasha na maafisa waliokuwa chini ya amri yake, akitaja majina yao moja baada ya lingine. Nilishangazwa na kuuliza kwake kana kwamba alikuwa anawajua. "Nilimtumikia Pasha pia kama Balozi wa Irani kwenye dola la Wauthumani. Jina langu ni Abdulkarim Beg", alielezea. Kisha watu wengine tisa walikuja. Abdulkarim Beg alisimama kwa heshima walipofika. Nilijua kuwa walikuwa watu wa nafasi za juu. Tulisalimiana. Wakasema, "Tunakualika kwenye kitala cha Shah". Waliinua pazia iliyokuwa mbele ya hema kubwa. Tulitembea tukipitia kwenye njia nyembamba, mpaka tulipoingia kwenye ukumbi wa Shah. Nadhir Shah aliponiona, alisema, "Abdullah Beg, karibu! Njoo karibu". Tulichukuwa hatua kumi, na akasema tena, "Njoo karibu" Nilisogea karibu nikasimama kwenye umbali wa mita mbili kati yetu. Alikuwa amekaa kitako. Ungebaini kuwa alikuwa mrefu. Kulikuwa na mapambo ya tepe tele kwenye kichwa, shingo, na mikono yake. Alikuwa mwenye kujivunia na kinaa. Alionekana mchovu na mzee. Ndevu zake zilikuwa za rangi nyeusi na alikuwa kapoteza meno ya mbele. Macho yake yalikuwa mazuri na yenye nyusi zilizoonekana kama pinde zilizo wazi. Alikuwa mtu mwenye kulazimisha na mwenye bashasha. Nilipomuona, hofu iliyokuwa moyoni mwangu ilipungua. Aliuliza kwa Kituruki, “Vipi hali ya Ahmad Pasha? Nikamjibu, “Alikuwa mzima”.

[Wakati huo Sultan Muhammad Khan I, mfalme wa ishirini na nne wa dola la Wauthmani, ndie alikuwa kwenye arshi. Pamoja na hayo, Ahmad Khan III, Sultan aliyemtangulia, alikuwa hai bado. Alizaliwa mwaka wa 1083H na kufariki dunia mwaka wa 1149H/ 1736 A.D.. Amezikwa kwenye makaburi ya Sultan Turhan; babu yake mzaa baba, yaliyoko Bahcekapi, kati ya Yeni Cami’ (msikiti mpya) na Misir Carsisi (soko). Alipanda arshi ya ufalme mwaka wa 1115H akapinduliwa kutokana na maasi ya Janissary. Mtoto wa kaka yake, Sultan MahmudI, akachukuwa nafasi yake. Ushindi dhidi ya mwenda wazimu Petro na mauaji ya Ibrahim Pasha wa Nevsehir mwaka wa 1143H yalitokea wakati wa utawala wake.

Katika juzuu ya kwanza ya kitabu kiitwacho **Sijill Uthmanii** imetajwa “Ahmad Pasha ni mwanawe Eyyubi Pasha. Alikuwa gavana wa Konya mwaka wa 1129H, gavana wa Basra mwaka wa 1130H, gavana wa Baghdad mwaka wa 1136H wakati alipofariki babaake, halafu akatumwa Iran kama Serasker (Amiri jeshi mkuu). Mnamo mwaka wa

1149H aliteuliwa tena kuwa gavana wa Baghdad. Alifariki dunia mwaka wa 1160H katika mwezi wa Dhulqa'da. Ugavana wake wa Baghdad wa mara mbili ulidumu kwa miaka ishirini na mbili.

Alisema "Unajuwa kwa nini nilikuita hapa?" Nikasema "Hapana. Sijui".

Alieleza "Kama ujuavyo, nchi yangu ni ya kanda mbili. Moja wapo ya kanda hio ni Turkistan na Afghanistan. Watu wa mikoa hii hudai kuwa Wairani ni makafiri. Si jambo jema kwa watu walioko chini ya utawala wangu kuitana makafiri. Nakuteua kuwa naibu wangu. Utajadiliana nao kisha uamue ni kundi lipi ndilo la ukweli. Utatokomeza mfarakano huu. Nataka nijue utakayoona na kusikia kwenye kongamano. Mpe ripoti Ahmad Khan pia".

Baada ya kuruhusiwa niliondoka. I'timad ud-daula, yaani Waziri mkuu aliniomba nimtembelee na nikutane na Mulla, yaani mkuu wa mambo ya dini, baada ya Sala ya adhuhuri. Nilifurahi sana nilipotoka hapo. Wakati wa chakula cha mchana, nilipelekwa kwa Waziri mkuu. Waziri alinisalimia na hali amekaa kitako. Hakunyanyuka wala kuonyesha heshima yoyote. Nilipokaa, alinyanyuka akasema "Karibu". Kulingana na desturi yao, mwenyeji husimama mgeni anapokaa. Kwa vile sikujua desturi hiyo, nilikasirika mwanzoni. Kwa hakika nilikuwa nimepanga kumwomba Shah amwadhibu Waziri mkuu kwa kutomheshimu mwanazuoni kama hatua ya mwanzo ya kutokomeza ukosefu wa imani ambao shah alikuwa ameniamrisha. Lakini nilipojifunza desturi yao hii, niligundua kwamba alikuwa na adabu. Baada ya kumaliza chakula cha mchana, tulipanda wanyama tukaelekea kwa Mulla. Njiani, nilikutana na Mwafghani. Alinitolea salamu. Nlipomuomba ajitambulishe, alisema "Mimi ni Mulla Hamza, Mufti wa Waafghani". Nilipomuliza iwapo alijua Kiarabu, alisema "Ndio". Nilisema "Shah ameniamuru kurekebisha mihimili ya uasi na uovu inayoshikiliwa na kufuatwa na Wafursi. Lakini waking'ang'ania imani zao kwa inadi na kuficha baadhi ya mihimili yao, nitafanyaje? Sijui mengi kuhusu watu hawa. Niambie yote uyajuayo ili nipate kujua la kufanya".

Alisema, "Usimuamini Shah! Anakutuma kwa Mulla mkuu ili uongee naye peke yake. Kuwa muangalifu wakati wa mazungumzo." Nilisema "Naogopa. Inaelekea kuna njama".

Alisema "Hapana. Usiogope hayo. Shah aliwatuma watu waaminifu ambao wataripoti kwake yatakayojiri katika kila hatua ya majadiliano. Haiwezekani kumdanganya Shah".

Nilikaribia hema la Mulla Mkuu. Alitoka nje kunipokea. Alikuwa mfupi. Alinionyesha kiti kilichokuwa karibu naye na juu yake kidogo. Katikati ya mazungumzo, alisema “Leo nilimuona Hadi Khodja, Mufti wa Waafghani. Yeye ni bahari ya elimu.” Hadi Khodja alikuwa Qadhi wa Bukhara. Alikuwa msomi sana. Kwa sababu hiyo aliitwa Bahr ul-‘Ilm (bahari ya elimu). Alikuwa hapa kwa siku kadhaa kabla ya kuwasili kwangu akiwa na wanazuoni wengine kutoka Bukhara.

Mulla huyo alisema “Inawezekanaje ajichukulie kuwa bahr al‘ilm wakati hana elimu? Ningalimpa ushahidi wa aina mbili kuthibitisha kuwa Imam Ali alistahiki kuwa Khalifa wa kwanza, asingelikuwa na jibu. Si yeye peke yake. Hata kama wanazuoni wa kisunni wangeungana, wasingeweza kutoa jibu”.

Nilisema, “Ushahidi huo usiojibika ni upi?”

1- Alisema “Kwanza, ningependa kukuuliza swali, “Bwana Mtume alisema yafuatayo kuhusu Ali ibn Abi Twalib "radiyallahu anhu" “Uhusiano uliokuwepo baina ya Harun na Musa ni kama ule uliopo baina yangu na wewe. Tofauti pekee iliyopo ni kwamba hakuna mtume atakayekuja baada yangu”. “Wewe pia unajua hadithi hii”.

Nilisema, “Ndiyo. Kwa hakika inajulikana sana. Alisema “Hadithi hii huonyesha kuwa Imam Ali alistahiki kuwa khalifa wa mtume Muhammad”.

Niliuliza, “Inakuwaje?”

Alisema “Inaeleza kuwa nafasi ya Imamu Ali kwa kumlinganisha na mtume hufanana na ile ya Harun na Musa. Tofauti pekee iliyopo imetajwa “Lakini hakuna mtume atakayekuja baada yangu”. Kwa sababu hii Ali alipaswa kuwa Khalifa wa kwanza. Harun asingalifariki dunia angalimrithi Musa. “Wewe unadai waziwazi kuwa matamko haya yana urejeleo wa kijumla kwa mujibu wa mantiki. Unafikiaje hitimisho kuwa yana maana ya kijumla?”

“Katika mambo ya kipekee, kiambatisho hudokeza uwepo wa maana ya kijumla”.

“Harun "alaihis-salaam" kama Musa "alaihis-salaam" alikuwa mtume. Kwa upande mwengine, kama ujuavyo, Hadhrat Ali hakuwa mtume, ima kabla au baadae. Aidha, Harun "alaihis-salaam" alikuwa ndugu halisi wa Musa "alaihis-salaam". Kwa upande mwingine, Hadhrat Ali hakuwa ndugu halisi wa mtume. Upekee katika ile ambayo ni ya ujumla hurejelea udhanifu kwa mujibu wa mantiki. Kwa hiyo, maana ya tamko inapaswa kutafutwa kama nafasi au mahali. Sauti /t/ mwishoni mwa neno [manzila] huashiria maana ya umoja. Idhaafa

(uhusishaji) kama ule wa nafasi ya Harun ni idhaafa al-ahadiyya kama ilivyo katika aina nyingi za uhusishaji. Kwa maneno mengine, hauashiria maana ya kijumla. Maana ya kipekee ya neno hilo ni 'isiokuwa'. Kwa hiyo, tamko hilo hubeba maana dhanifu, siyo bainifu. Katika tamko kama hili, jambo lisilokuwa wazi linaweza kueleweka kwa kutumia taarifa nyingine. Yaani, kama uhusiano baina ya maneno 'manzila' na 'Harun' unavyoashiria kwamba alikuwa Khalifa wa Wana wa Israil tu, hivyo unaashiria kuwa Hadhrat Ali "radiyallahu anhu" aliachwa Madinat al-Munawwara kama khalifa wakati wa vita vitukufu vya Tabuk. Alisema: "kuachwa huko kama khalifa huonyesha kuwa alikuwa mbora zaidi. Kwa hivyo lazima awe Khalifa wa kwanza".

Nilisema: "Hivyo basi, Abdullahi ibn Umm Maktuum lazima awe Khalifa pia. Kwani mtume "alaihis-salaam" alimuacha, kama alivyowaacha watu wengine, kama Khalifa, yaani, muakilishi wake huko Madinat al-Munawwara. Sasa, kwa nini umemchagua Hadhrat Ali "radiyallahu anhu" kama khalifa wa kwanza badala ya kumtunukia heshima hiyo mmoja wapo wa wale wengine? kwa mfano yule aliyetajwa hapo juu? Zaidi ya hayo, kama kumuacha kama mwakilishi ingekuwa sababu ya ubora, Ali "radiyallahu anhu" asingeelezea wasiwasi wake kwa kulalamika kwamba, "Utaniacha hapa na wanawake, watoto na wasiojiweza?" na Bwana wetu Fahari wa viumbe asingesemtuliza kwa kusema, "Hupendi kuwa na nafasi nami kama Harun na Musa?".

Alisema: "Kulingana na tawi la elimu la kisunni lijulikanalo kama 'usuul', jambo muhimu si kutofautiana kati ya sababu lakini muhimu ni ujumla wa tamko".

Nilisema: "Sichukulii tofauti kati ya sababu kama ushahidi. Lakini nasema kwamba kipashio kisicho dhahiri katika hadithi hii tukufu ni dalili inayodokezea umahsusi wake". Alinyamaza kimya!

Niliendelea, "Zaidi ya hayo, hadithi hii haiwezi kutolewa kama ushahidi. Kwa sababu haikupokelewa kwa pamoja. Baadhi ya wanazuoni walisema ni **sahih**, wengine wakasema ni **hasan** na wengine wakaielezea kuwa **dha'ifu**. Kwa mfano, Ibn al-Jawzi alisema kwamba hadithi hii ni **maudhuu'**. [Abulfaraj Jamalud-diin Hafidh Abdur-Rahman Ibn Aliyyu al-Jawzi (rahmatullahi alaih) ni mwanazuoni maarufu wa hadithi. Alizaliwa mjini Baghdad mwaka wa 508H na akafariki dunia mwaka 597 H./ 1201 A.D.. Aliandika zaidi ya vitabu mia moja vya hadithi. Tafsiri yake iitwayo Mughni inajulikana sana]. Hadithi hii inawezaje kuthibitisha kuwa Imam Ali "radiyallahu anhu" alipaswa

kuwa Khalifa wa Kwanza, licha ya ukweli kwamba ushahidi lazima ujulikane sana kutokana na matini (aya au hadithi iliyotajwa waziwazi)?

Alisema “Ndiyo. Huo ni ukweli. Hadithi hii sio ushahidi wetu pekee. Hadithi isemayo, “Msalimieni Ali kama Amir al-Mu’minin”, ni ushahidi. Ni ukweli usiopingika kwamba hadithi hii tukufu huashiria haki ya Ali kuwa Khalifa wa kwanza. Kama si utume wake”.

Nilisema: “Kadri tujuavyo, hadithi hii ni mawdhuu’. Vitabu vya wanazuoni wa Ahl as-Sunna (rahmatullahi alahim) havina hadithi kama hii”. Alifikiria kidogo halafu akasema kwa ghafla “nitataja ushahidi mwingine ambao haiwezekani kuufasiri vinginevyo. Aya isemayo ‘Njooni‘. Tuwaite watoto wenu na watoto wetu’ ni ushahidi wangu”.

Nilihoji, “Aya hii tukufu, ambayo ni aya ya sitini na moja ya Sura Aali-Imran, inawezaje kuwa ushahidi?”

Alisema “Wakristo waliokuja Madina kutoka Najran walipokufuru, mtume "swallallahu alaihi wa sallam" aliwaambia, “Nakukaribisheni kwenye mashindano. Acha tumuombe Allahu taala alaani kundi linalosema uwongo”. Halafu akajitokeza huku Ali, Fatima, Hasan na Husein wakiwa pamoja naye. Bila shaka, mtu aliyejiunga na mtume katika dua hii ni mbora kuliko yule ambae hakufanya hivyo”.

Nilisema, “kile ulichosema sasa ni kisa tu. Hakiashirii ubora. Kwa sababu kuna kisa kinachohusu kila sahaba wa mtume na kinachomtofautisha na wengine. Wasomi wa historia wanauelewa ukweli huu. Aidha, Qurani iliteremshwa kwa Kiarabu. Kwa mfano, tuchukulie kuwa makabila mawili yalitaka kupigana na chifu wa moja ya makabila hayo akasema, “Nitaandamana na mashujaa wa kabila”, tamko hili haliwezi kuwa uthibitisho kwamba makabila hayo hayakuwa na mashujaa wengine isipokuwa wale waliojitokeza. Mtu kuwa na jamaa zake wa karibu kwenye dua ni ishara ya huzuni na kusudio lake ni kutaka dua hiyo ikubalike”.

Alisema, “Hili huonyesha kwamba wanapendwa sana”.

Nilisema, “Haya ni mapenzi ya kiuzawa yaliyoko katika maumbile ya mtu. Ni kama mtu kujipenda, kuwapenda watoto wake. Haifai kutafuta ubora katika jambo hili”.

Alidai, “Kitu kingine. Mtume "swallallahu alaihi wa sallam" alimueka Hadhrat Ali katika nafasi sawa na yake”.

Nilisema, “Wewe huna ujuzi wa taalima ya usuul, na labda hata Kiarabu hukijui. Neno ‘anfus’, unalochukulia kuwa ushahidi, ni jam’ qillat (wingi-uchache). Limeambatanishwa na kiambishi ‘Naa’,

ambacho ni kipashio cha wingi. Wingi unapoambatanishwa na wingi mwingine, husababisha mgawanyo wa (idadi) moja kwa elfu. Kwa mfano, ukisema ‘kampuni ya askari farasi limepanda farasi’ unakusudia kusema kwamba wapanda farasi wote walioko kwenye kampuni hiyo wamepanda farasi wao. Jam’u humaanisha ‘zaidi ya moja’. Aya ya ishirini na sita ya Sura An-Nur inayosema, “Hao wameepushwa na hayo wanayosema”, huashiria Hadhrad Aisha (radiyallahu anha) na Safwan (radiyallahu anhu hivyo, tamko, ‘Nyoyo zenu”, katika aya ya nne ya Sura At-Tahrym, ni la wingi, na hali kulingana na taaluma ya mantiki humaanisha ‘mioyo miwili, kwa sababu limeambatanishwa na kiwakilishi nafsi ya pili. Kwa kutumia dalili hiyo hiyo, tamko, ‘watoto wetu’, linalohusu Hasan na Husein (radiyallahu anhum) na urejeleo wa wingi ‘wanawake’, uliomkusudia Hadhrat Aisha pekee, ni balagha. Kama aya hiyo ingeashiria kuwa Hadhrat Ali alipaswa kuwa Khalifa wa kwanza, basi, Hasan, Husein, na Fatima wangekuwa makhalifa. Hata hivyo, hakuna namna ambavyo Hadhrat Fatima angekuwa Khalifa”.

Alisema, “Nina ushahidi mwingine. Aya ya hamsini na tano ya Suratul Maidah inasema: “Hakika rafiki yenu mlinzi ni Allahu taala na mtume wake na walioamini, ambao hushika Sala na hutoa zaka nao wananyenyekea”. Kama ilivyoelezewa kwa itifaki na wanazuoni wa tafsiri (ya Qurani), Hadhrat Ali, alipokuwa akisali, alitoa pete yake na kumpa maskini kama sadaka, ndipo aya hii tukufu ikateremshwa. Tamko ‘Innamaa’ katika aya humaanisha ‘yeye peke yake’. Yaani, humrejelea yeye pekee. Na neno ‘walii’ katika aya hiyo humaanisha ‘yule ambae aliashiriwa kuwa kiongozi’, unasemaje kuhusu masahaba?

Jibu langu lilikuwa, “Elimu tuliyo nayo kuwahusu masahaba ni kwamba walikuwa wakweli kwa nafsi zao na katika maneno.

2- Alisema, “Aya nyingi za Qurani huwalaumu. Kuna aya nyingi zinazosema kwamba wao ni wanafiki, kwamba walimuudhi mtume. Mfano ni aya ya nane ya Suratul Mujadilah, ya kwanza ya Suratul Munaafiquun, ya kumi na sita, ishirini, ishirini na tisa na thelathini za Sura Muhammad. Zaidi ya hayo, aya ya mia moja na mbili ya Sura at-tawba, kumi na moja, kumi na mbili na kumi na tano za Surat al-Fat-h na aya ya nne ya Suratul Hujurat zimeeleza kwamba wanafiki walijificha sana mjini Madina kiasi kwamba mtume na watu wengine hawakuwatambua. Imetajwa katika Suratul Anfal kwamba, “Hakika waliompinga mtume, ni wale waliokwepa vita vya Badr, siku waumini walipojitolea muhanga”. Ni kwa sababu hii ndiyo Allahu taala, Mjuzi wa siri, anafichua nia mbaya za wanafiki katika aya ya sita ya Al-Anfal.

Ni wanafiki hawa waliotoroka vita vya Hunayn na waliotegemea kuwa idadi kubwa waliyokuwa nayo ingewapatia ushindi, ndio waliopelekea kuteremshwa kwa aya ya kumi na mia moja kumi na sita za Sura Al-Imraan. Katika maafa ya Uhud walikimbilia milimani, wakimwacha Mtume mikononi mwa maadui. Walisababisha kujeruhiwa kwa uso wake, kun'golewa kwa meno yake mawili na kuanguka kwake kutoka juu ya farasi. Hakika waliombwa msaada lakini walijifanya viziwi na kwa hiyo walilaumiwa na Allahu taala katika aya ya mia moja hamsini na tatu ya Sura Aali-Imran. Kutokana na tabia mbaya waliyoonesha huko Tabuk, walikemewa na kuonywa katika aya ya thelathini na tisa ya Sura Tawba.

(Aliendelea), "Kama ukweli huu unavyoonesha, masahaba wa mtume walimpinga. Aya inayozungumzia kutoroka kwao huonesha kwamba wote walimkimbia na si wachache wao. Kwani aya ya arubaini na tatu ya Sura Tawba inaelezea kwa urefu na uwazi kwamba walipata mateso na kukemewa, wakasababisha kuteremshwa kwa aya ya arubaini na nne ya Sura Tawba, inayomlaumu mtume kwa sababu aliwaruhusu kujiunga tena na waumini. Zaidi ya hayo, katika vita vya Ahzaab au Khandaq vilivyotokea mwezi wa kumi na moja mwaka wa 5H, walikemewa na kulaumiwa kupitia aya ya kumi na tatu na kumi na tano ya Suratul Ahzab na aya nyingine nyingi.

Inawezekanaje, watu kama hao wasemekane kuwa wakweli? Vitendo vyao na maneno yao yanaweza kuthaminiwa vipi kama ushahidi katika mambo ya dini? Hawaaminiki kimantiki na kisayansi.

Nilichukuwa zamu yangu "Aya zote ulizotaja kama ushahidi ili kuwakashifu masahaba watukufu (ridhwanullahi alaihim ajma'iin) zilikusudiwa wanafiki. Hakuna anayetilia shaka ukweli huu. Hakika Washia, kwa itifaki, hutambua ukweli huu. Kujaribu kuwalimbikizia masahaba watukufu, waliosifiwa katika aya kadhaa, lawama zilizotajwa katika aya hizi ambazo inajulikana wazi kuwa ziliteremshwa kuwakemea wanafiki, na hivyo kujaribu kuwaharibia jina, si jambo la haki na mantiki. Mwanzoni kulikuweko wanafiki wengi. Baadaye idadi yao ikapungua. Katika kipindi cha mwisho cha uhai wa mtume "swallallahu alaihi wa sallam" wanafiki walijitenga na waumini wa kweli. Allahu taala aliwatenga wazuri kutokana na wabaya kwa aya ya mia moja sabini na tisa ya Sura Aali-Imran. Bwana wetu, mtume "swallallahu alaihi wa sallam" alisema: "Madina huwachuja watu wema kutokana na wabaya, kama moto kwenye karakana ya mhunzi inavyochuja chuma kutokana na taka". [Yaani kama karakana zinazotumika na wahunzi na kalibu zinavyotenganisha taka liitwalo

mavi ya chuma kutokana na chuma, hivyo, mji wa Madina huwatenganisha watu wazuri kutokana na wabaya]. Uhalali wa kuwasingizia masahaba yaliyomo kwenye aya tukufu yanayoelezea wanafiki, unawezaje kuthibitishwa? Aya ya mia moja na kumi ya Aali-Imran inasema: “mmekuwa umma bora “. Inawezekanaje watu hao waliosifiwa na aya hii kulinganishwa na wanafiki?

(Niliendelea), “Allahu taala anawasifu masahaba katika aya nyingi. Katika vitabu vyote vya Tafsiri vimeandikwa kwamba aya ya 59 ya Sura Tawba iliteremshwa kwa ajili ya Ibn Dhil Huwaysira ibn Zuhayr, aliyekuwa kiongozi wa Khawarij. Haifai kwa mtu mwenye elimu kuwasingizia masahaba watukufu (ridhwanullahi alaihim ajma’iin) uovu uliotajwa kwenye aya hii. Inafaa wakati huu kufafanua mafungu ya maneno yaliyonukuliwa kuelezea tukio hili katika kitabu cha Bukhari. Abu Sa’idal Khudhri "radiyallahu anhu" anasimulia: “Nilikuwa na mtume "swallallahu alaihi wa sallam". Nilikuwa nikifurahia uso wake wenye mng’ao. Alikuwa anagawanya ngawira zilizotekwa kutoka kwa makafiri katika vita vitukufu vya Hunayn.Huwaysira mwenye asili ya ukoo wa Bani Tamiim aliingia na kusema: “Ewe mtume wa Allahu taala. Fanya uadilifu! Mtume akasema, “Hebu, ona aibu! Nisipofanya uadilifu, nani mwingine ataufanya? Nisingetoa haki, mngekumbwa na madhara mengi!” wakati huo, Umar al-Faruq alisimama na kusema: “Tafadhali! Niruhusu nimwue mjinga huyu”. Mtume akasema: “Muache kwa sababu mtu huyu ana marafiki. Wanasali jinsi unavyosali. Wanafunga, wanasoma nawe Qurani. Pamoja na hayo, neno la Allah halipiti kwenye koo zao. Wataacha dini kama mshale unavyoacha upinde. Akiangalia mshale wake na shabaha na chupa, hawezi kuona chochote kati yao. Kumbe mshale huo umefika kwenye chupa, ukaichoma na kumwaga damu. Miongoni mwao kutakuwa na mtu mwenye rangi nyeusi. Mkono wake mmoja ni kama kiwele cha mnyama. Kinatonesha bila kikomo.”. abu Sa’id al-khudhriy anasimulia: “Hadhrat Ali alipambana na Khawarij katika enzi ya ukhalifa wake. Tulimuona mtu wa namna hii miongoni mwa mateka. Alikuwa kama mtume alivyomuelezea. Imetajwa kuwa sababu ya kuteremsha kwa aya hii, ilikuwa kutokana na kauli ifuatayo iliyotolewa na mnafiki ajulikanaye kama Abul Hawaat: “Enyi marafiki zangu. Kwa nini msimwangalie bwana wenu? Anataka kuonyesha uadilifu kwa kuwapa wachunga kondoo haki yenu”.

Niliendelea, “hivyo hivyo, aya ya nane ya Suratul Mujadilah iliteremshwa kwa ajili ya Mayahudi na wanafiki. Kwani walikuwa wakipanga mikutano ya kisiri huku wakiwadanganya masahaba.

Waumini waliwaonea huruma wakidhani kuwa mikutano hiyo ilifanywa kwa kuhofia balaa fulani ambalo lingewakumba. Hata hivyo, kurefushwa kwa vikao vyao kulidhihirisha malengo yao. Masahaba walilalamika kwa mtume "swallallahu alaihi wa sallam" wakaomba mikutano hiyo isitishwe. Kwa hiyo, mtume alitoa amri ya kusitisha mikutano hiyo. Pamoja na hayo, wanafiki walikaidi amri wakaendelea na uhaini wao. Kutokana na tukio hilo, aya ya nane ya Suratul Mujadilah iliteremshwa "Kwani hawaoni wale waliokatazwa kunong'onezana kisha wakayarudia yale waliyokatazwa, na wakanong'ona juu ya mambo ya dhambi, na ya uadui, na ya kumwasi mtume? Na wakikujia hukuamkia sivyo anavyokuamkia Allahu taala".

Kukaidi amri na kuitisha tena mkutano kuliashiria kuwa walikuwa wakimpinga mtume.

(Niliendelea), "Maana ya aya ya nane ya Suratul Mujadilah ni "Na wakikujia hukuamkia sivyo anavyokuamkia Allahu taala". wayahudi hulaumiwa na aya hii. Walipokutana na Mtume, walisema, "Assaamu alaiku" badala ya kusema, "Assalamu alaikum". Na Mtume alikuwa akiwajibu, "Wa alakumus saam! Hivyo, badala ya kusema 'salaamu', yaani amani, walisema 'saamu' yaani 'mauti'. Walidhani kwamba wangemdanganya Fahari wa viumbe, mbora wa viumbe wote, wanadamu waliotangulia na watakaokuja hapo mbeleni. Walipotengana naye, walisema kwamba wamemdanganya na kwamba angalikuwa mtume wangaliadhibiwa kutokana na maovu yao. Kwa sababu hiyo, ilitajwa mwishoni mwa aya kwamba "Unawatosha moto wa Jahannamu na ni makao mabaya". Bukhari alitaja katika kitabu chake kwamba, kama kawaida yao Wayahudi walikuwa wakimtolea mtume salamu mbovu. Aisha (radiyallahu anha) alielewa walichokuwa wakikikusudia kwa salamu hiyo, hivyo alikasirika. Mtume akamwambia kwamba hapakuwa na haja ya kukasirika kwa sababu Allahu taala alikubali ombi lao ambalo ni 'wa alaikus saam'. Tamko 'wanapokujia wanafiki...' katika aya ya kwanza ya Sura Al-Munaafiqun, humtaja Abdullahi ibn Salulu na marafiki zake. Haiwahusu masahaba.

(Niliendelea), "Maana ya aya ya kumi na sita ya Sura Muhammad ni, "Na wapo miongoni mwao wanaokusikiliza, mpaka wakiondoka...". aya hii pia iliteremshwa kwa ajili ya wanafiki. Wanaohudhuria vikao vya mtume wakasikiliza kauli kadhaa, lakini hawakuwa tayari kuzingatia aliyokuwa akisema.

Imam Muqaatil [wa Belh, aliyefia Basra mwaka wa 150H] anasema katika tafsiri yake: Mtume "swallallahu alaihi wa sallam" alipokuwa

akitoa hotuba, Wayahudi walijifanya kuwa hawaelewi anayoyasema. Walikuwa wakimuuliza Abdulla ibn Abbas ("radiyallahu anhu") “je, mtu huyu anamaanisha nini?” Abdullahi ibn Abbas anasema, walikuwa wakimuuliza mara kwa mara.

Allahu taala ni muadilifu. Aliteremsha aya ya kumi na sita ya Sura Muhammad ili kuwatofautisha waumini wanaomtumikia kwa moyo mkunjufu, na wanafiki.

Maana ya aya hii ni, “Hao ndio Allahu taala amewapiga muhuri nyoyo zao, na wakafuata pumbao lao”. Kisha akawapa masahaba habari njema zinazohusu uongofu na uwokovu. Sa’id ibn Jubair, "radiyallahu anhu" alisema: Tamko “The hast seen those with ailing hearts”, linalojitokeza katika aya ya kumi na mbili ya Sura Muhammad, huwafichua wanafiki. Kwani kuna nyoyo za aina tatu: Wa aina ya kwanza ni moyo wa muumini ambao ni msafi na umefungamanishwa na Allahu taala kwa upendo. Aina ya pili ni moyo mgumu na uliokufa. Hautakuwa na hisia za huruma kamwe. Watatu ni moyo wenye maradhi. Maradhi haya ni mojawapo ya sifa za wanafiki. Allahu taala kaelezea aina zote tatu katika aya ya hamsini na moja ya Suratul Hajj. Aina mbili za nyoyo hizo zitaadhibiwa. Mmoja tu ndio utapata uokovu. Moyo mbora ndio **saliim** (mzima). Moyo wa muumini ni **saliim**. Allahu taala ameusifia moyo ulio **saliim**.

Aya ya themanini na nane ya Sura Ash-Shuaraa inasema: “Siku ambayo mali wala watoto hazitosaidia kitu. Isipokuwa mwenye kumjia Allahu taala kwa moyo safi”.

Bani Anbar walikuwa makafiri. Si sawa, kwa mujibu wa mantiki na sayansi kuwachukulia kuwa masahaba.

Kuhusu vita vitakatifu vya Badr, kama ilivyofafanuliwa kwenye vitabu vyenu na vitabu vyetu, vilikuwepo kama ilivyotajwa katika aya ya kwanza ya Suratul Anfal.

(Niliendelea), kutawanyika kulikotokea katika vita vya Hunayn si kutoroka. Bali kulikuwa kufanya hadhari ambayo ni mbinu ya kivita. Kila vita huwa na harakati za kurudi nyuma na kwenda mbele. Hata hivyo, wale waliotawanyika hawakuwa masahaba wakuu. Walikuwa watumwa walioachiliwa baada ya kutekwa kwa Makka miezi michache kabla (ya vita hivyo). Ilikuwa wazi kwamba matokeo yake yatakuwa ushindi. Katika Sura Tawba aya ya ishirini na saba imeelezwa kuwa kurudi nyuma kulichangia ushindi, “Kisha baada ya hayo Allahu taala atawasamehe awatakao”.

Mtume "swallallahu alaihi wa sallam" alipewa habari kuhusu ushindi huu. Kwa sababu hiyo, hakuwalaumu wale waliotawanyika. Hakukasirishwa na yeyote kati yao. Kwa hiyo, haifai kuwakemea kwani imetajwa kwamba “inaruhusiwa kutoroka vitani maisha ya mtu yanapokuwa hatarini” katika kitabu cha mwanazuoni wa Kishia ajulikanaye kama Abul qasim kiitwacho kitabush-Sharaayi’. Huoni kwamba ni muhimu kwa mtu kuuzuia ulimi wake usije ukawakashifu masahaba waliorudi nyuma katika vita vya Hunayn.

“Ama kuhusu kutoroka vita vitakatifu vya Uhud. Vita hivyo vilitokea kabla ya kuharamishwa kwake. Imeelezewa katika aya ya 155 ya Aali-Imran kwamba Allahu taala amewasamehe. Imetajwa katika vitabu vyote vya tafsiri kwamba habari njema zinazoelezea kuwa Allah kawasamehe ambayo imezungumziwa kabla ya aya ya 153 ya Sura Aali-Imran imefungamanishwa na aya hii inayoifuata.

Maana ya aya ya 99 si karipio kwao. Huwaeleza kwamba wamelegeza kamba. Tena inawahusu masahaba wote, akiwemo Ali ibn Abi Talib "radiyallahu anhu".

Baada ya kusema hayo Mulla alianza kuongea:

3- Je, inasihi kumteua mtu kama Khalifa wakati ukhalifa wake ulizua mabishano? Bani Hashim walikuwa wenye sifa miongoni mwa masahaba watukufu. Ni baada ya kusita kwa muda mrefu na kulazimishwa ndipo walitambua ukhalifa wake. Je. Hii ndiyo njia ya kumkubali khalifa?

Nilijibu, “Masahaba wote (ridhwanullahi alaihim ajma’iin) walikubaliana kwa pamoja juu ya ukhalifa wa Hadhrat Abu Bakr "radiyallahu anhu" na masahaba wachache ndio waliochelewa kutangaza utiifu wao, si kwa sababu walimpinga bali kwa vile hawakualikwa kwenye uchaguzi. Kwa hiyo hawakuwepo. Licha ya hayo, kupinga kwa watu walio wachache kusingebadilisha upendeleo wa walio wengi. Jambo kama hilo lingaliwezekana, lingalitokea kwa Hadhrat Ali (Karramallahu wajhah) aliyeteuliwa kuwa Khalifa wa nne baadaye na hatimaye ukhalifa wake usingekuwa wenye haki.

4- Mulla mkuu alibadilisha maada, “Abu Bakr alimnyima Hadhrat Fatma haki yake. Akitumia hadithi isemayo, “Sisi kundi la mitume haturithiwi. Na mali tunayoacha huwa sadaka, hakumpa haki yake. Katika vita vya Khaybar Jibril aliteremsha aya isemayo, “ Nampe aliye jamaa yako haki yake”. Mtume alipouliza, “ni nani jamaa yangu?” aliambiwa, “Alikuwa Fatma”. Imesimuliwa na Ummu Ayman na Asmaa bint Uways na Ali ibn Abi Talib kwamba kutokana na tukio hili, Fatma

alipewa shamba la mitende lijulikanalo kama Fadak. Pamoja na ushahidi huu, alimnyima haki yake kwa kutumia hadithi iliyopokelewa naye, ni nini huu kama si ukatili? Je, inaruhusiwa katika Uislamu kumkubali khalifa ambae tabia yake na matendo yake ni kama haya?"

Nilimjibu, "Kuna sababu mbili ambazo inawezekana zilimfanya Hadhrat Fatma kudai shamba la mitende liitwalo Fadak. Labda alisema alikuwa amelirithi. Na pengine alidai kuwa ni haki yake aliyopewa na mtume kabla ya kifo chake. Madai yako ni kwamba aliliomba kwa sababu ilikuwa mali yake. Hakuna mwanazuoni yeyote wa a Ahl as-Sunna aliyesema kwamba Mtume alimpa Fatma shamba la Fadak au kwamba lilikuwa mali yake. Wala haikuandikwa kwenye kitabu chochote cha kiislamu. Vitabu vyote husema kwamba aliliomba shamba hilo kwa sababu ilikuwa mirathi kutoka kwa baba yake. Inawezekana vipi hadithi hii iliyosimuliwa katika Sahih Bukhari, kubadilishwa kuwa "Lilichukuliwa kwa nguvu?" hadithi ziko wazi kabisa kiasi kwamba haiwezekani kustahmili upotofu kama huo. Kwani shamba la mitende la Fadak lilikuwa likimilikiwa na mtume "swallallahu alaihi wa sallam". Alipofariki dunia, milki ikahamishiwa kwa Abu Bakr, khalifa wake. Fatma alipolidai kama mirathi, alimjibu kama ilivyoelezewa katika hadithi na akaapa kuwa aliwaheshimu jamaa zake mtume kuliko jamaa zake mwenyewe. Ukweli huu umeandikwa katika Sahih Bukhari. Hadithi iliyopokelewa pia na Umar, Uthman, Ali, Talha, Zubair, Abdur-Rahman, Abbas na wake zake mtume "swallallahu alaihi wa sallam". Imam Abu Ismail Bukhari anasema: Ishaq aliniambia, nilisikia hadithi hii kutoka kwa Malik Ibn Anas. Alisema: Aliisikia kutoka kwa Ibn Shihab az-Zuhri, ambae alisema kwamba aliisikia kutoka kwa Malik Ibn Aws. Nilimtembelea Malik ibn Aws nikamuuliza. Akaniambia `Siku moja nilikuwa nimekaa mbele ya nyumba yangu kabla ya adhuhuri aliponijia mtu kutoka kwa Umar akaniambia kwamba Khalifa alitaka kuniona. Nilienda huko nikaingia. Khalifa alikuwa amekaa kwenye kitanda. Hapakuwa na godoro kwenye kitanda hicho. Alikuwa ameegemea kwenye mto. Nilimsalimia na kukaa kitako. Akaniambia: Baadhi ya watu kutoka kwenye kabila lako walikuwa hapa. Nilitoa amri kwamba wapewe pesa. Nilikuita kwa sababu ningependa uwagawie pesa hizo. Zichukue uwagawie". Nilimuomba Khalifa aniwie radhi na ampe mtu mwingine pesa hizo ili atekeleze amri hiyo. Lakini aliposisitiza nilikubali. Wakati huo bawabu (mlinda mlango) aliingia akasema kwamba Uthman, Abdur-Rahman, Zubayr, Sa'id ibn Abi Waqqaas (ridhwanullahi alaihim ajma'in) waliomba ruhusa. Khalifa akasema, "Wanaweza kuingia". Waliingia

wakakaa kitako. Muda mfupi baadae, bawabu aliingia tena na kusema kwamba Hadhrat Ali na Abbas walikuwa wakisubiri nje. Waliporuhusiwa, waliingia na kukaa kitako. Hadhrat Abbas alianza kuongea. Akasema, "Mimi na Ali tulikuja hapa kwa ajili ya utanzuaji wa mgogoro baina yetu kuhusu mali ya Bani Nadhiir ambayo Allah alimzawadia mtume. Alitaka rehma hili lijadiliwe ili wale waliotangulia kuja waridhike pia. Khalifa alianza kuongea akasema.

"Nakuomba useme ukweli kwa haki ya Mola Mwenye enzi na utukufu. Muumba wa mbingu na ardhi na kuvijalia kuwepo kila wakati: Je, Mtume wa Allahu taala alisema kwamba, "Sisi mitume haturithiwi? Na chochote tunachoacha nyuma ni sadaka? Mnajua kwamba alisema hivyo?" Uthman na wenzake waliofika mapema walisema, "Ndio. Tunajua. Mtume alisema hivyo". Halafu khalifa akageuka upande wa Ali akarudia swali hilo hilo. Wote wakabubali na kusema, "Ndio". Akasema, "Basi mnapaswa kuwa tayari kusikiliza hukumu kuhusu rehma hili. Mola wa walimwengu alitoa mali hii kama ngawira. Imetajwa katika Sura Al-Hashr aya ya sita kwamba Allahu taala alitoa zawadi hii kwa kipenzi chake na siyo mtu mwingine. Bwana wetu, fahari ya viumbe alitoa mali ya namna hii akaigawa kulingana na mafundisho ya Kiislamu. Ikabaki ile iliyopo leo. Baada ya kutenga sehemu yake kwa ajili ya matumizi yake ya nyumbani, alikuwa akitoa iliyobaki kwa wale waliopewa ruzuku kutoka kwenye Bayt al mali (banki kuu ya kiisalam) Mtume hakufanya hivyo?" Mnasema nini kuhusu rehma hili? Masahaba wote walijibu kwa kusema, "Ndio".

Khalifa aliendelea, "Mtume alipofariki, Abu Bakr as-Siddiq "radiyallahu anhu" alichukuwa hatamu za uongozi. Alifuata sera ya mtume akafanya vile vile, hadi kifo chake bila ya kukosea. Sasa nyinyi wawili mko pale mnataka niseme.

Mnauliza swali. Kwa vile nyote mnauliza swali hilo hilo, lazima jibu liwe moja. Wewe Hadhrat Abbas uko hapa kuulizia haki ya binami yako, na wewe Hadhrat Ali uko hapa kuulizia haki ya mke wako ambayo ni mirathi kutoka kwa baba yake. Nimenukuu hadithi kwa ajili yenu, "Hatuachi mirathi nyuma yetu...", ambayo mmekubali kuwa mliisikia. Halafu nimekuelezeni sera iliyofuatwa na Abu Bakr as-Siddiiq, ambae alikuwa Khalifa. Niliwapeni kazi ya kushughulikia rehma hili, nikisisitiza kuwa mfuate sera iliyotumika kabla". Hivyo, khalifa alijibu swali la Hadhrat Ali na Abbas mbele ya Hadhrat Uthman na marafiki zake., akataja kwamba walikuwa wamepewa kazi hii kwa sharti hilo. (Akaendelea kusema), "Sasa ikiwa mmekuja hapa kutafuta rukhsa ya kufanya jambo ambalo ni kinyume na sharti hili, naapa kwa utukufu wa

Muumba wa ardhi na mbingu kwamba sitatoa rukhsa ya kufanya jambo linalokinzana na matakwa ya Allahu taala na mtume wake. Ikiwa hamuwezi kufanya kazi hii, niachieni! Nitashughulikia mahitaji yenu". Urwat ibn Zubair alipoulizwa kuhusu hadithi hii alikiri kwamba aliisikia kutoka kwa Malik ibn Aws "radiyallahu anhu". Akaongea hadithi iliyopokelewa kutoka kwa Aisha "radiyallahu anha", mke wa mtume "swallallahu alaihi wa sallam" inayosema: "Siku moja, wake zake mtume "radiyallahu anhunna" walinituma kwa baba yangu Hadhrat Abu Bakr as-Siddiiq aliyekuwa Khalifa wakati huo, niende nikamuulize kuhusu mirathi ambayo walipaswa kupata kutokana na nyara. Alisema, "Hammuogopi Allahu taala? Hadithi ya Bwana wetu Mtume inayosema, "Sisi mitume hatuachi mirathi", hudhihirisha kuwa hamna mirathi yoyote. Je, mnaikumbuka hadithi hii?" Alipokataa, niliikumbuka hadithi hiyo nikarudi nyumbani.

"Niliinukuu hadithi hiyo tukufu kama inavyojitokeza katika Sahih Bukhari, ili kubainisha kwamba pamoja na ushahidi huu uliodhahiri, wanaobishana kiukaidi ni wenye nia mbovu. Hadhrat Abu Bakr as-Siddiq aliisikia hadithi hii kutoka kwa mtume wa Allahu taala "swallallahu alaihi wa sallam". Ni ushahidi unaotegemewa zaidi. Kwani kuna njia tatu za kujifunza jambo: Kwanza, kwa kulitambua. pili, kwa kulisikia kutoka kwa watu wote. na tatu, kwa kulisikia kutoka kwa mtume wa Allahu taala. Kwa vile Fatma hakuisikia hadithi hii, haimaanishi kuwa haipo. Kuthibitisha kwa Hadhrat Ali na Abbas na Hadhrat Aisha kusisitiza ushawishi wake, hakuwachi shaka yoyoyte kuhusu ukweli wake.

"Ulikosea katika madai yako kwamba Hadhrat Fatma "radiyallahu anha" alileta wanawake wawili kama mashahidi. Yeye alipendekeza Hadhrat Ali na Umm Ayman "radiyallahu anhuma" kama mashahidi. Ni mmoja tu kati ya mashahidi hawa ndie alikuwa mwanamke. Ukweli huu uliandikwa vizuri kwa uwazi zaidi katika **Nahjul Haqq** cha Ibn al-Mutahhir Hasan ibn Yusuf al Hulli, mwanazuoni wa Kishi'a. Hata hivyo, huu si ubishani wa kiislamu. Tukio lifutalo litathibitisha kwa nini hauko hivyo: Hadhrat Ali "radiyallahu anhu" alimshtaki Myahudi juu ya nembo na akapendekeza mwanawe Hassan na mtumwa wake Qanbar kuwa mashahidi. Kadhi Shurayh akawakataa kwa sababu si kitendo cha kiislamu kwa mtu kuwa shahidi kwa babaake. Imamu Ali ambae alikuwa Khalifa wakati huo, aliufuata Uislamu na mantiki kwa kukubali uamuzi.

[Ibn Mutahhir Hulli alizaliwa mwaka wa 684 H. na kufariki dunia mwaka wa 726 H./1226 A.D.. Alikuwa mmoja wa wanazuoni wa kundi

la Kishi’a la Imaamiyya. Aliandika mamia ya vitabu. Kadhi Shurayh aliteuliwa na Hadhrat Umar "radiyallahu anhu" kuwa kadhi wa Kuufa. Alihudumia Uislamu kama Kadhi kwa karibu miaka sitini. Alifariki dunia mwaka wa 87 H., akiwa na umri wa miaka mia moja. Huyu asidhaniwe kuwa ndiye yule Kadhi Shurayh aliyekuwa rafiki ya Imam mkuu Abu Hanifa ambae Khalifa Mansur alimteua kuwa Kadhi wa Kufa na ambae alizaliwa mwaka wa 95 H., akafia Kuufa mwaka wa 177 H./793 A.D.].

“Tukichukulia kuwa ushahidi huu wote umepuuzwa na bado inadhaniwa kuwa Khalifa Abu Bakr as-Siddiiq alichukuwa shamba la mitende la Fadak kwa nguvu, kwa nini Hadhrat Ali "radiyallahu anhu" hakuwapa Hassan na Hussein shamba hilo alipokuwa khalifa na hali ya kuwa kila kitu kilikuwa mikononi mwake, chini ya amri yake? Kwa nini hakubadilisha yaliyokuwa yamefanyika na makhalifa watatu waliotangulia? Kufuata sera ile ile iliyofuatwa na makhalifa waliomtangulia, inayohusu shamba la mitende ni ushahidi ulio wazi wa kuthibitisha ukweli kwamba Abu Bakr hakulichukuwa kwa nguvu”.

Kutokana na ushahidi huo, Mulla mkuu alisema:

5- Je, inaswihi kwa mtu aliyefanya jitihada ya kukataa amri ya mtume, kuwa khalifa?

“Hapana. Haiswihi”. Nilisema.

Alisema, “Ilikuwaje Umar aliyempiga Abu Huraira "radiyallahu anhu" na kumkataza kutekeleza amri aliyopewa kuwa khalifa? Mtume "swallallahu alaihi wa sallam" alimpa Abu Huraira kandambili zake zenye baraka, akamwambia, “Nenda na hizi. Wapashe watu habari njema kwamba wale wanaoamini kalimat shahada wataingia peponi Alipokuwa njiani kutekeleza amri hii, alikutana na Umar. Akamuuliza unatoka wapi na unakwenda wapi. Abu Huraira alipomhadithia wajibu ambao alikuwa anakwenda kuutimiza, alimpiga kofi kifuani na akamwamuru arudi alikotoka. Abu Huraira alichukizwa sana. Aliporudi, alimwambia mtume yaliyojiri. Kama ilivyoandikwa katika kitabu kiitwacho **Al-jam’u Bayna as-Sahihayn** cha Hafidh Muhammad ibn Abi Nasr Hamidi Andalusi Maliki [aliyefariki mwaka wa 488H/1095 A.D.], Abu Huraira alisema: Abu Bakr, Umar na mimi tulikuwa tumekaa na mtume wa Allahu taala. Mtume alisimama akaenda zake. Tukapata wasiwasi. Tukatoka nje ili kumtafuta. Niliwatangulia wengine nikafululiza mpaka kwenye ukuta wa Bani Najjar. Nikaanza kuuzunguka nikitafuta mlango. Nikamuona Rabi’a akiingia kwa kupitia kwenye mlango mdogo, nikamfuata. Nlimuona mtume ndani. Akaniambia nisogee karibu. Akanipa kandambili zake zenye baraka akasema,

“Nenda na hizi! Wapashe habari njema wale wote utakaokutana nao kwamba wanaoamini **Laa Ilaaha illallahu Muhammadun Rasuulullah** (Kalimat Shahad), wataingia peponi!” Nilitoka nje kama alivoniamrisha.

Kwanza nilimkuta Umar. Akaniuliza, “Unaenda wapi?” Nilipomwambia kwamba nilikuwa nikienda kuwapasha waumini habari njema, alinipiga. Akaniamuru nirudi nilikotoka. Nilirudi nikilia machozi. Nilipokuwa nikimweleza mtume wa Allahu taala, Umar aliingia akasikiliza. Mtume wa Allahu taala akamuuliza alichofanya. Akasema, “Ewe mtume wa Allahu taala! Niko tayari kuwatoa muhanga wazazi wangu kwa ajili yako! Je, ulimpa Abu Huraira kandambili zako zenye baraka ukamwambia akawapashe wale wanaoamini kalima Shahada habari njema ya kuingia peponi?” mtume aliposema, “ndio”, Umar alisema, “Ewe mtume wa Allahu taala! Usifanye hivyo tafadhali! Nahofia kwamba watakaosikia habari hizo, watategemea hilo walegeze kufanya ibada katika kufanya matendo yao. Tafadhali waache!” Hivyo, mtume alisema, “Sawa. Waache”.

“Ukichunguza mambo hayo kwa makini, huoni kwamba Umar alikataa amri ya Allahu taala na Mtume wake? Inaruhusiwa vipi kumfanya mtu kama huyo khalifa na kuyaacha mambo ya Waislamu mikononi mwake?”

Nilijibu. “Tabia hii ya Hadhrat Umar haikusudii kukataa amri ya mtume wa Allahu taala. Wala haiashirii kutotii amri. Yeye huwasilisha fikra yake kwa mtume. Fikira yake inaweza kukubaliwa au kukataliwa kutegemea amri ya mtume ya mwisho. Kusema, “Ewe mtume wa Allahu taala niko tayari kuwatoa mhanga wazazi wangu” ni dalili ya kuonyesha heshima, upole na upendo na kwamba yuko tayari kutekeleza amri yake. Kwa upande mwingine, mtume wa Allahu taala hamkemei Hadhrat Umar kutokana na tabia yake na badala yake anakubali maoni yake akiyachukulia kuwa ni yenye manufaa kwa waislamu. Anamuamrisha Abu Huraira kuacha kandambili na kutotoa habari hiyo.

Tabia ya aina hii si ya Hadhrat Umar pekee. Masahaba wengi walifanya mambo yaliyo sawa na mtume wetu akakubali mengi kati yake. Imeelezwa katika Sahih Bukhari na Muslim kwamba Bwana wetu mtume "swallallahu alaihi wa sallam" alisema, “Kila mtu ajaye katika ardhi hii ana sehemu aliyotengewa ima peponi au motoni”. Mtu mmoja kutoka kwenye hadhira akauliza, “Ewe mtume wa Allahu taala. Tunaweza kusubiri mpaka tutakapoenda kwenye sehemu tulizotengewa na Allahu taala kuliko kufanya ibada?” Mtume

"swallallahu alaihi wa sallam" akamwambia, “Usiache ibada yako. Kwani wale watakaoingia peponi watatenda mambo yatakayo wapeleka peponi na wale watakaoenda motoni watafanya matendo yatakayo wapeleka motono”. Kisha akasoma aya ya tano ya Sura Al-Layl. Kauli ya Umar hufanana na jibu hili la mtume "swallallahu alaihi wa sallam". Yaani alikusudia kusema kwamba, “Ewe mtume wa Allahu taala, tumejifunza kutoka kwako kwamba haingefaa kutoa habari njema kama hizi kwa wajinga. Nahofia kuna wengi wao wanaoweza kutegemea kalimat ash-shahaada wakapuuza ibada ambazo ni faradhi au wajibu wakalegeza katika ibada zao katika kushikamana kwao na Uislamu”. Mtume alitambua kwamba Umar alikuwa na nia nzuri kwa hiyo, alikaribisha ushawishi wake.

Hadhrat Ali alitoa matamko kama hayo ambayo yangechukuliwa kuwa utovu wa heshima. Kundi la Kharijiyya lijulikanalo kama Nawaasib lilimkashifu kutokana na matamko hayo. Abdulhamid Naaji alijaribu kumdunisha Hadhrat Ali kwa kunukuu matamko hayo kwenye kitabu chake. Ali ibn Ahmad ibn Hazm (384H-456/ 1064 A.D.) mwanazuoni wa Andalusia, katika kitabu chake kiitwacho Tafsiir na Sharif Murtadhaa, mwanazuoni wa Kishia katika kitabu chake Tanziihul Anbiyaa, walitoa majibu kwa kashifa hizi wakampinga Naaji. Ukitaka naweza kukupa mifano mingi ya majibu haya”.

Mulla mkuu hakusema kitu. Aliuliza swali lingine:

6- Je, ni sawa kwa mtu anayejiita Amir ul-Mu’miin kuharamisha kitu kilichohalalishwa na Allahu taala na mtume wake?

“Ni kitu gani hicho?” niliuliza.

Alisema, “Umar aliharamisha ndoa ya mut’a iliyohalalishwa na Allahu taala na mtume wake na ambayo imeelezewa katika Quran tukufu na Sunna. Kama huku si kupinga amri za Allahu taala, inawezekana vipi kuelezea rehma hilo vinginevyo?”

Nilitoa jibu lifuatalo kwa Mulla mkuu: “Kama ilivyoelezewa katika Musnad na Ibn Maaja [manahadithi Muhammad ibn Yazid aliyezaliwa Qazvin mwaka wa 209H akafariki dunia mwaka wa 273 H./886 A.D.] “Umar "radiyallahu anhu" alipokuwa Khalifa alisema: “Mtume "swallallahu alaihi wa sallam" alituhalalishia ndoa ya mut’a mara tatu na akaiharamisha mara tatu. Naapa kwa jina la Allah, nilisikia kwamba mtu ambae ameoa na amemfungia mwanamke katika nyumba yake kwa njia ya mut’a nitamuua kwa kumpiga mawe”. Hadithi hii haionyeshi kuwa ndoa ya mut’a iliharamishwa na Hadhrat Umar. Lakini

huonyesha kuwa hakuruhusu mut’a kwa vile ilikuwa imeharamishwa na mtume "swallallahu alaihi wa sallam".

Masahaba wote isipokuwa Hadhrat Abdullah ibn Abbas waliunga mkono kauli hii ya khalifa. Lakini naye baadaye alikubali pia, ikawa kwamba masahaba wote wamekubaliana kwa pamoja. Bukhari anatuhadithia hadithi iliyopokelewa kutoka kwa Hadhrat Ali kwamba, Hadhrat Ali alimwambia Ibn Abbas, “Umekosea. Bwana wetu fakhari ya walimwengu alikataza ndoa ya mut’a”. Kutokana na kauli hii ya Hadhrat Ali, Abdullah ibn Abbas alikubaliana na uamuzi akakiri kuwa ndoa ya mut’a iliharamishwa baadae.

(Nliendelea), Sulaiman ibn Ahmad Tabraani mwanahadithi maarufu, [aliyezaliwa Tabariyya mwaka wa 260 H., akafia Isfihan mwaka wa 360 H./971 A.D.] na Sulaiman ibn Daud Tayaalisi [aliyefariki dunia mwaka wa 202 H./817 A.D.] humnukuu Said ibn Jubair kwenye vitabu vyao akisema, “Nilimwambia Abdullah ibn Abbas ‘Nisingeweza kusema hata kidogo kwamba ndoa ya mut’a ni halali. Unaweza kufikiria juu ya madhara ambayo yatajitokeza kutokana na kusema hivyo? Ukisema kwamba imeruhusiwa, itaenea kila mahali na watu wengine watatumia kauli yako hii kama ushahidi wa kuhalalishia ndoa ya mut’a.” Baada ya kusema hivyo, Abdullah ibn Abbas alisema, “Kwa kusema hivyo sikumaanisha kwamba ndoa ya mut’a daima ni halali kwa kila mtu. Nilisema kwamba ingeruhusiwa tu katika hali ya dharura ili kuzuia madhara yasiyoepukika. Nilisema hivyo nikidhani kwamba kwa vile Allahu taala ametoa ruhsa ya kula nyama ya nguruwe kadri ya kuondoa madhara katika hali ya dharura, ndoa ya mut’a inafaa iruhusiwe”.

Kama itakavyobainika katika maelezo haya kwamba mut’a kuruhusiwa kwa kila mtu hayakuwa maoni ya Abdullah ibn Abbas. Maoni yake yalikuwa kwamba ingeruhusiwa kukidhi haja isiyoweza kuepukika, la si hivyo madhara yangejitokeza kama ilivyo katika mambo yote yaliyoharamishwa. Abu Bakr ibn Huseyn Bayhaqi [384H-458H/1067 A.D.] mwanahadithi, anaeleza wazi kuwa Abdullah ibn Abbas "radiyallahu anhu" alighairi mtazamo wake. Imeripotiwa na Tabraani na Bayhaqi pia kwamba Abdullah ibn Abbas alisema, “Ndoa ya mut’a mwanzoni ilikuwa halali. Lakini iliharamishwa baada ya kutetremshwa kwa aya isemayo, “Mama zenu ni haramu kwenu”. aya tukufu iliyoko katika Suratul-Muuminun inayosema, “Ni wake zenu tu na vijakazi mnaomiliki ndio halali”, husisitiza ukweli kuwa ndoa ya mut’a imeharamishwa. Kwani imeashiriwa kwenye aya hii kwamba ni wake na vijakazi tu ndio walio halali na wengine ni haramu”.

Imesimuliwa na maswahaba wote akiwemo Hadhrat Ali kwamba ndoa ya mut'a ni haramu.

Katika Sahih Bukhari imetajwa kuwa Hadhrat Ali "radiyallahu anhu" alimwambia Abdullah ibn Abbas kwamba mtume "swallallahu alaihi wa sallam" alikataza ndoa ya mut'a na kula nyama ya punda katika vita vya Khaybar. Kwa upande mwingine, imeandikwa katika Sahih Muslim na Sunan ibn Maaja kwamba mtume "swallallahu alaihi wa sallam" alisema, "Enyi waislamu! Nilikuruhusuni kuwaoa wanawake kwa ndoa ya mut'a, lakini sasa nimeiharamisha. Yeyote aliye na mwanamke aliyemuoa kwa namna hiyo, basi anapaswa kumtaliki na kuchukuwa mali yake aliyokuwa amempa!" Aidha, katika Sahih Bukhari na Muslim imetajwa kuwa, "mtume "swallallahu alaihi wa sallam" alihalalisha ndoa ya mut'a mara tatu na kuiharamisha mara tatu".

Nilimuliza Mulla mkuu, "Je, mwanamke aliyeolewa katika ndoa ya mut'a anaweza kumrithi mwanamume? Na ikiwa mwanamke huyu amezaa watoto na mume huyu, watoto hawa wanaweza kumrithi baba yao?". Mulla mkuu alijibu, "Hapana!".

"Hivyo basi, mwanamke huyu si mke wa mtu wala kijakazi. Una maoni gani kuhusu aya tukufu isemayo, "Waumini tahadharini wanawake wasio wake zenu wala vijakazi?" Yaani aya hii ilihalalisha tu wachumba na vijakazi. Huelezea waziwazi kwamba mtu hawezi kumkaribia mwanamke yeyote isipokuwa hawa wawili. Huoni kwamba kudai kuwa ni halali kuingiliana na mwanamke asiye mke wake wala jariya (kijakazi) na ambae mtu kafunganae ndoa ya muda ijulikanayo kama mut'a ni kuipinga amri hii ya Qurani iliyo dhahiri?"

Na huoni kwamba ni kupambana kwa ukaidi, kwa makusudi? Zaidi ya hayo, mnatoa kauli za upuuzi ambazo haziwezi kuhalalishwa. Kwa mfano, mmoja wapo wa wanazuoni wenu ajulikanaye kama ibn al-Aal, ameandika kwamba inaruhusiwa kwa mwanamke kujamiiana na wanaume kumi na wawili katika usiku mmoja na kwamba akishika mimba baba ya mtoto wake atatambulika kwa bahati nasibu. Ufisadi gani mwingine na uadui ambao ungekuwa wenye uharibifu zaidi kwa Uislamu kuliko huu? Jibu langu hili liliondoa uwezo wa kufikiri kwenye kichwa cha Mulla mkuu. Alifikiria kwa muda mrefu akitarajia kuukwepa utata. Halafu akauliza swali lingine:

7- "Je, ni wajib (lazima) kwa kila mtu kumtii khalifa na kutekeleza amri zake. Na mtu anayetiiwa awe maasumu asiyekosea. Licha ya hayo, imejulikana kwa pande zote mbili, (wanazuoni wa Kishia na Kisunni) kwamba imamu ni mtu asiye na hatia (maasumu). Mtu yeyote

mwenye akili anasema hivyo pia. Kwa sababu imamu maana yake ni mtu anayetiiwa. Kama shati inayovaliwa inavyoitwa ridaa, hivyo hivyo mtu anayetiiwa huitwa imamu. Kama imamu angetarajiwa kusema au kufanya makosa, angeaminika, angetarajiwa kusema au kufanya jambo linaloweza kuwapeleka watu kwenye maangamizi na ambalo lingepingana na amri za Allahu taala. Kwa vile utiifu kwa imamu umeamrishwa na Allahu taala, kukosea kwa imamu kungemaanisha kwamba Allahu taala alituamrisha kumtii mtu muovu. Na hili ni jambo linalokinzana na mantiki na dini".

Nilimjibu kama ifuatavyo "Madai yako kwamba kuna itifaki katika umaasumu na kutokosea kwa imamu na kwamba hili ni jambo lililoamrishwa katika Uislamu si sahihi hata kidogo na ni yenye upotofu. Nyinyi mashi'a hampendi ijmaa. Mnasema kwamba ijmaa haiwezi kuwa ushahidi wa kuthibtishia amri katika Uislamu. Kulingana na imani yenu, ijmaa si dalili ya kisheria (dalil shar'i). Kutokana na sababu hiyo, hoja inayoegemezwa kwenye msingi wa ijmaa haifanani na imani yenu.

Kwa upande mwingine, ikiwa kwa kusema 'kuna itifaki' unakusudia kuwa Washi'a wamekubaliana na imani hii, hiyo ina maana hii ijmaa yote iliyokuwepo kabla ya kujitokeza kwa kundi la Waismailiyya ingekuwa jambo lisilokuwa na mashiko. Zaidi ya hayo, kwa vile hapakuwepo jina 'Ushi'a' wakati Hadhrat Ali alipochaguliwa kuwa khalifa, ijmaa ambayo ilitekeleza uteuzi huu ingekuwa potofu, jambo ambalo lingalimaanisha kuwa hakuteuliwa kwa haki kuwa khalifa. Ukhalifa wa Hadhrat Muawiya ulitambuliwa na Hadhrat Hassan na waislamu wote likiwemo kundi la washi'a.

Imamu maana yake ni mtu anayepaswa kutiiwa. Lakini hakuna ushahidi unaodhihirisha kuwa anapaswa kuwa mtu asiye na hatia au asiyekosea. Ushahidi wowote ambao ungetolewa kuthibitisha madai haya ungekataliwa na tabaini za dalili tano zifuatazo:

I- Ni wajibu kutii tu amri za amiri au hakimu. Si lazima mtu anayetiiwa kuwa asiyekosea katika mambo yote anayofanya.

II- Kwa mujibu ya washi'a, mufti hukosea. Hata hivyo, ni wajibu kwa kila mtu kutekeleza amri za mufti.

III- Hakimu atakubali ushahidi wa mtu yeyote achukuliwaye kuwa ni muadilifu. Shahidi ambae hakimu anatoa hukumu kwa kuzingatia ushahidi wake si lazima awe asiyekosea.

IV- Mtumwa anapaswa kutii amri za bwana wake isipokuwa akimuamrisha kufanya kitendo kilicho haramishwa. Lakini haimaanishi kuwa bwana wake si mwenye kukosea.

V- Katika sala zote, walioko kwenye jamaa wanapaswa kumfuata imamu. Hata kama imamu anaswali kwa manufaa ya kidunia au anamfanyia rukuu au kumsujudia mtu mwingine badala ya kufanya hivyo kwa ajili ya Allahu taala, jamaa (maamuma) bado watalazimika kumfuata.

Kwa hiyo, wale wanaotiiwa katika hali hizo tano si lazima wawe wasiokosea".

Mulla mkuu akaanza kuzungumza:

"Sisi hatukutilia maanani maana hizi za twaa na ufuasi. Tulizingatia maana inayohusu utiifu wa vitu kwa kutegemea kiwango fulani. Kinachotegemewa zaidi ni kauli ya mtume, "Je, mimi si awla (mwenye kuthaminiwa zaidi) kwenu kuliko maisha yao?" kwa wale waliokuwa wamemzunguka waliposema, "Ndiyo ewe mtume wa Allahu taala! Alisema, "Basi yeyote ambaye mimi ni mawla wake, Ali pia, anapaswa kuwa mawla wake". Kwa hiyo, twaa katika muktadha huu humaanisha kumfanya mtu kuwa bwana wako. Hata kama tungezingatia maana yake ya kijumla kama katika vipengele vitano ulivyotaja, bado usingekuwa kama unavyodhani. Ndiyo. Ni wajibu kuwatii Amiri na Hakimu. Lakini ni wajibu kuwatii tu wale walioteuliwa na Imamu ambae si mkosefu [yaani khalifa], si wajibu kuwatii wasiokuwa hao. Kauli ya shi'a kwamba mufti wanapaswa kutiiwa haikusudii kumaanisha kuwatii mufti wenyewe. Twaa hii huchimbuka kutokana na ukweli kwamba waliteuliwa na Imamu aliye maasumu (asiekosea). Madhali wao ni wawakilishi wake, amri yao ni amri ya Imamu. Pamoja na hayo, si lazima kutii amri zao wenyewe. Ama kuwatii watu wengine, inafaa kuwatii tu ikiwa amri zao huruhusiwa na Uislamu, kwa sababu twaa hii imeamrishwa na Allahu taala. Hata hivyo, utiifu kwa Imamu [Khalifa] ni wa kiujumla sana kuliko mifano iliyotajwa hapo juu".

Jibu langu lilikuwa kama ifuatavyo: "Twaa au ufuasi haufichi shaka. Neno hili ni mojawapo ya maneno yanayojulikana kama mutawaatir [Maana ya mutawaatir imeelezwa kwa upana katika sura ya nne, sehemu ya pili ya kitabu iitwacho Sa'aadat Abadiyya]. Kwani twaa maana yake ni mfuasi kumfuata yule anayemtii. Ikiwa mtu anamfuata yule ambae ni mwenye hadhi ya juu, mfuasi anaitwa 'taabi'' na yule mwenye hadhi anaitwa 'matbuu'. Kitendo hiki cha kufuata ni cha aina tofauti na hutegemea kiwango au muda wa twaa. Kwa maneno mengine, sifa yake iliyo muhimu ijulikanayo kama mutwawaati haitobadilika. Kwani inaelezewa kwa itifaki na wanazuoni wa usuul na

wanazuoni mwengine kwamba tofauti inayosababisha tashqiiq (mfarakano) ni tofauti katika kiini cha jambo.

Tofauti hii haikujengwa juu ya msingi wa wakati wala kiasi. [Tashqiiq imeelezewa kwa upana katika Sa'aadat Abadiyya].

(Niliendelea), "Ikiwa maana ya 'iqtidaa' hufahamika kutokana na neno 'it-tibaa' kufuata, hii pia ni mutwawaati. Kwani iqtidaa maana yake ni kufuata katika kila jambo. Ikiwa mtu atafanya jambo mwenyewe, liwe jambo muhimu au lisilo la muhimu, hatachukuliwa kuwa amefanya iqtidaa. Kufuata kwa namna moja kunaweza kuchukuliwa kuwa iqtidaa kwa uhalisi wake, lakini mtu aliyefanya hivyo hasemekani kuwa ametekeleza iqtidaa kwa maana yake kamili. Kwa hiyo, fikra yenu kwamba "mtu anayefuatwa hupendwa sana na mfuasi wake" ambacho ndicho kitovu cha mvutano katika hoja yenu, ni bure, ni kama zoezi la kuendesha mtumbwi. Kwani huku si kufuata hata kidogo. Na maana uliyoitaja haihusiani lolote na upendo ulioamrishwa na Uislamu na ambao ni sawa na ule unaopaswa kuonyeshwa kwa bwana wetu mtume "swallallahu alaihi wa sallam" kama ilivyotajwa katika hadithi. "Hatakuwa muumini kamili mpaka anipende mimi kuliko nafsi yake, wazazi wake, na watu wengine wote".

Mlifikiria visivyo kuwa upendo uliotajwa katika hadithi ulikuwa uteuzi wa khalifa na mkawalinganisha makhalifa na Bwana mtume. "swallallahu alaihi wa sallam" Ulinganishi huu haufai kwa vyovyote vile. Mulla mkuu alinyamaza kisha akabadilisha mada.

8- Alisema, 'Ni ukweli unaojulikana sana kwamba Bwana mtume alikuwa mwenye huruma sana kwa umma wake na kwamba alijaribu kutetea haki zao kwa amani. Hakuna haja ya kusema haya. Ni kutokana na huruma yake hii ndipo alikuwa akimteua mtu kuchukuwa nafasi yake akiwa amesafiri kutoka kwenye mji wa Madina kwenda kwenye mji mwengine. Katika hali kama hii, ingewezekanaje kwake yeye kutomteua imamu, mwakilishi atayeendesha shughuli za umma huu na kukidhi mahitaji ya watu hawa wote ambao idadi yao imefikia milioni kadhaa baada ya kifo chake na kuwaacha bila udhibiti hadi mwisho wa dunia?

Kwa upande mwingine, kama inavyobainika katika khutuba iitwayo Ghadiir Hum, iliyoandikwa kwenye vitabu vyenu vilivyothibitika kuwa vya kweli na kwenye ripoti zingine mtume alimteua Hadhrat Ali kuchukuwa nafasi yake akifariki dunia kwa kutoa matamko yaliyo wazi na kwa vidokezi. Kwa hakika, kwa vile ilikuwa wajibu kwa Mola wa Walimwengu kumteua Imamu wakati mtume alipokarikbia kifo chake,

alitaka kuandika wasia ili kushughulikia wajibu huu na kuwazuia wakaidi kuukwepa. Aliomba kalamu na karatasi. Umar, aliyekuwa mmoja wapo wa hadhira, alimshawishi asifanye jambo hilo. Kwa matamko yenye kuudhi na kuchukiza ambayo hata watovu wa adabu wasingeweza kuyatoa”.

Nilimjibu, “Tamko lisemalo kwamba ‘Ilikuwa wajibu kwa Mola wa walimwengu kumteua Imamu, hufanana na hoja ya kundi la wamu’tazila wanaosema kwamba, “Ni wajibu kwa Mola wa walimwengu kufanya mambo fulani. Kutofanya hivyo huenda kinyume na hekima ya Allahu taala. Kauli yao hii ni yenye upotofu na uongo. Kwa sababu twajua kwamba ingawa vitendo vya Allahu taala huwafikiana na hekima na ni muhimu daima, lakini si wajibu kwa Allahu taala kufanya jambo eti kwa sababu huafikiana na hekima na ni muhimu. Aya ya Qurani isemayo, “Haulizwi juu ya kitu chochote lakini wao huulizwa”, huonyesha wazi kuwa kauli yako si sahihi. kama ingekuwa wajibu kwa Allahu taala kumteua Imamu, isingefaa kwa wanadamu kumkosa Imamu.

Ni lazima kwa Imamu huyo kujulikana na kila mtu, kuwa na uwezo na nguvu, kuwa na sifa za uimamu, kuweza kukomesha kabisa maovu na desturi mbaya, kufanya matendo mema na kuwahami waislamu kutokana na madhara. Mkidai kuwa dunia haiwezi kumkosa Imamu na kuwateua watu wachache akiwemo Hadhrat Ali kwa ajili ya nafasi hiyo, mkadai pia kuwa ni wajibu kwa Allahu taala kuwafanya maimamu kuwa na upendo mwingi mkashikillia kuwa hakuna kati yao aliye na sifa za imamu. Mnataja kuwa wote waliishi katika hali ya unyonge, kutokuwa na uwezo, shida na mateso, bila kuweza kufanya lolote au kuwa na athari yoyote. Ni faida au hekima gani hiyo inayoweza kutarajiwa kwa kumfanya imamu mtu kama huyo asiye na uwezo, anayejisalimisha kwa nguvu za wengine?

“Ushikiliaji wenu huu wa kikaidi hukusudia kumfanya Allahu taala mdhaifu na asiye na uwezo; Allahu taala atukinge kutokana na imani kama hiyo! Kwani kulingana na fikra zenu ameshindwa kufanya jambo fulani! Allahu taala yuko mbali na hana mfungamano na makisio kama hayo.

“Njia nyingine ya kupinga fikra zenu ni: “Je, kuwafikiana na hekima au kuwa na manufaa huhitajika daima au la?

Ukisema kuwa na hekima si jambo zuri daima, utakuwa umekubaliana nasi. Katika hali hiyo tunaweza kusema kwamba hekima uliyoitaja hapo juu, haikuwepo wakati mtume alipokaribia kifo. Kwani

kama inavyosemekana kuwa kuwepo kwa hekima hakuleti tofauti yoyote, basi pia kuwepo kwake hakuwezi kuwa bora kuliko ukosekanaji wake.

Kwa upande mwingine, ukisema kwamba kuwepo kwa hekima ni bora, hekima hii lazima iwepo katika dhati ya Allahu taala au mahali pengine. Kama haipo katika dhati yake basi kiumbe kingine kitakuwa katika dhati yake na hili haliwezekani kabisa.

“Kama inavyobainika, kusema kwamba ni wajibu kwa Allahu taala kumteua Imamu, si sahihi kabisa na ni upuuzi. Ndio, wanadamu huhitaji imamu, kwa ajili ya kuuhami Uislamu, kuwaadhibu wakoseaji, kulinda haki na kutekeleza jukumu muhimu la kuamrisha mema na kukataza mabaya, kama wanavyoshikilia Ahl as-Sunna, ni wajibu kwetu kuwa na imamu ama raisi. Lakini si wajibu kwa Allahu taala kumteua mtu yoyote. Kwasababu hiyo, Bwana mtume "swallallahu alaihi wa sallam" alipofariki dunia, masahaba watukufu waliungana pamoja wakamchagua Abu Bakr as-Siddiiq "radiyallahu anhu" kama imamu wao. Uislamu ulipata kinga dhidi ya vurugu.

(Niliendelea), “Kwa mujibu wa wamu’tazila, kilicho muhimu ni iwapo akili zinatofautisha kitu kuwa kizuri au kibaya. Wanaachia akili jukumu la kuamua ni vitu gani vilivyoumbwa na Allahu taala ni vizuri na vipi kati yake ni vibaya. Wanasema kwamba Allah anapaswa kuumba vitu vizuri. Hakuna madai yenye kuchukiza kama kusema kwamba Allahu taala anapaswa kuumba vitu ambavyo akili ya mtu huviona vizuri. Madai yenu hufanana na haya. Kama ilivyoelezewa kwa uwazi kabisa, Allahu taala huumba chochote anachopenda. Na wala si lazima kwake kuumba kitu chochote. Vitu vyote anavyopenda kuumba ni vyenye manufaa na huviumba kulingana na hekima. Hakuna chochote kati ya viumbe hivyo ambacho ni kibaya. Kulingana na wamu’tazila, humaanisha kitendo kinachosababisha adhabu kikiachwa. Hivyo basi, ikiwa mtu hawezi kulaumiwa kwa kutofanya jambo fulani, haiwezi kusemekana kuwa kufanya jambo hilo ni wajibu.

Ukisema kwamba Allahu taala anapaswa kuumba kitu fulani, humaanisha kuwa inafaa kumlaumu na kumuadhibu asipokiumba. Na ingemaanisha kuwa Allahu taala ana mapungufu na kwamba ataepuka adhabu endapo ataumba kitu hicho. Hakuna maasi mengine ambayo mtu angethubutu kuyafanya kwa ujeuri mbele ya Allahu taala bila ya kuwa na hofu kuliko haya na hakuna tamko lingine ambalo ni kinyume na sifa zake za ukamilifu ambalo lingechukiza zaidi kuliko hilo.

Tamko lako hilo lisilo na thamani lingeweza kupingwa na majibu mengi pia. Tamko hilo hukusudia kumlinganisha Muumba na viumbe vyake kwa kutumia kigezo sawa kinachotumika katika ukadiriaji. Na jambo hili haliwezekani kwa vyovyote vile.

Aidha, kama ingekuwa wajibu kwa Allahu taala kumuweka imamu asiyekosea, basi ingekuwa wajibu kwake kumtuma mtume katika kila karne, kumweka imamu asiyekosea katika kila mji, na kumfanya kila mtawala mwadilifu na mkweli. Ndio, kila mtu awe ni mzuri au mbaya, asingependa kuona mazingira ambapo Allahu taala amewaacha waja wake bure bila kiongozi au imamu, wakiishi katika ujinga na upotofu wakigaragara kizani.

Ili kuzuia hali kama hiyo, Allahu taala aliteremsha kitabu kinacho waongoza kwenye raha na amani na akamjalia mwanaadamu kipawa cha kiakili kinacho mtoshelezea haja ya kutambua thamani yake.

Ukisema Allahu taala daima amekuwa akituma imamu asiyekosea na akamkabidhi uongozi wa mambo yanayowahusu waja wake, haya yatakuwa madai mengine ya kipuuzi yasiyo na maana. Licha ya upuuzi kwamba imamu huyu asiyekosea angeishi kwa miaka hii elfu kipindi ambacho watoto wake wote, wajukuu na ndugu na marafiki wangekufa, angekuwa na manufaa gani kwa kuendelea kuwa kwenye furaha pamoja na kwamba idadi ya washi'a imeongezeka, badala ya kujitokeza awaongoze watu kwenye njia ya kweli, awazindue na kueneza Uislamu? Angesemekana vipi kuwa ana wajibu kama ule wa kuwaongoza watu kwenye njia ya kweli, kuhakikisha kuwa wenye haki wanapata haki zao, na kufanya mambo mengine mengi? Ni nini kinachostaajabisha au kuonekana kuwa ni chenye ujanja zaidi kuliko kushikilia imani kama hiyo? Allahu taala asipomjaalia mtu uongofu hakuna awezaye kumhidi kwenye njia ya kweli. Mambo haya yote ya hakika hudhihirisha kuwa Allahu taala halazimishwi kufanya au kutofanya jambo.

Kwa mujibu wa Nahj al Balaagha, Hadhrat Ali "radiyallahu anhu" alitaja ukweli huu kwa uwazi katika hotuba yake aliyoitoa katika vita vya Siffiin. Alisema, "kwa kuwa mimi ni kiongozi wenu, nina haki juu yenu. Nanyi mna haki juu yangu na juu ya wenzenu. Madhali kuna haki ambazo mtu huwadai wengine, kutakuwa na haki anazodaiwa. Allahu taala ndiye peke yake asiyedaiwa haki yoyote ingawa kuna haki anazodai. Kwani anaweza kufanya kila kitu.

Kila jambo analofanya ni la uadilifu. Haki ya Allahu taala kwa waja wake ni kumuabudu na kumtii. Kwa vile ni mwenye huruma anatoa

ujira kwa waja wake kama malipo kwa kitendo hicho”. Ukizingatia hotuba hiyo, utaona kwamba matamko yako hukinzana na yale ya Hadhrat Ali.

“Kauli yako isemayo kwamba Bwana yetu, mtume "swallallahu alaihi wa sallam" aliagiza kuwa Hadhrat Ali anapaswa kuchaguliwa kama Khalifa si sahihi pia.

Masahaba walipaswa kutekeleza maamrisho ya mtume sambamba na yale yaliyofaradhishwa. Kauli yako humaanisha kuwa walipuuza wajibu huu kwa kuficha agizo hili la mtume. Kwa upande mwingine, haiwezekani kwa idadi hiyo kubwa ya watu kukubaliana juu ya uhalifu. Zaidi ya hayo, kauli yako haiwezi kuwa sahihi kwa vile imekinzana na hadithi tukufu.

(Niliendelea), “Hadithi iliyopokelewa kutoka kwa Anas ibn Malik na ibn Abi ‘Asim na Alqaa’i, wanazuoni wa Kishi’a inasema: “Allahu taala ameukinga umma wangu kutokana na kukubaliana juu ya upotofu”. Hakim ibn Uyayna, mwanazuoni wa hadithi "rahmatullahi alaih" ameinukuu hadithi inayosema, “Allahu taala hatawaunganisha umma wangu kwenye maasi”. Na neno mkono katika hadithi isemayo kwamba “Mkono wa Allahu taala huwa pamoja na jamaa” maana yake ni “nguvu” ama “msaada”. Kama inavyobainika katika hadithi hizo na hadithi nyingine nyingi zinazo fanana, umma wa Muhammad (waislamu) hawatakubaliana milele juu ya upotofu. Kusema yale yaliyo kinyume na hadithi hizo ni kuzipinga.

“Unadai kuwa bwana wetu mtume "swallallahu alaihi wa sallam". aliomba kalamu na karatasi ili aandike wasia. Kauli yako hii haiwafikiani na madai yako yaliyotangulia, yanayohusu hotuba ya Ghadiir Hum. Angalitoa amri kama hiyo, isingalihitajika tena kuandika wasia. Hii inamaanisha kuwa wasia unaodai kuwa mtume alitaka kuwaandikia huko Ghadiir Hum ni uzushi mtupu. Ukweli ni kwamba masahaba watukufu akiwemo Hadhrat Ali "radiyallahu anhum" na Bani Hashim wote kwa pamoja walimchagua Abu Bakr kuwa khalifa. Itifaki hii na hadithi zilizotajwa hapo juu huthibitisha kuwa ukhalifa wake uliongozwa kwa usawa na kauli zako ni batili. Wasia kama huo ungalikuwapo, wakati wa utawala wa makhalifa hao wengine (yaani Abu Bakr, Umar na Uthman) ambao wangekuwa wamemdhulumu Hadhrat Ali, Hadhrat Ali angalidai haki yake la si hivyo angalipambana nao. Hakika alipochaguliwa kuwa Khalifa, alichomoa upanga wake akapambana na walioasi kulingana na amri ya Uislamu kushughulikia marahma ya kidini na kidunia kama khalifa. Kama tujuavyo, sote,

aliendeleza vita vilivyoteketeza miji kadhaa na kusababisha umwagaji damu ya maelfu ya waislamu. Mtu mwenye nguvu na heshima. Aliyekuwa mkali kwa wasiomtii, sasa ndie anayeonekana kuwa alikaa kimya ijapokuwa aliona haki yake aliyopewa na Uislamu ikinyakuliwa na asijiunge na baraza la wazee ili kufanya uamzi juu ya nani alipaswa kupewa haki hiyo. Je, madai kama hayo yanaweza kukubalika?

(Niliendelea), ikiwa kama inavyodaiwa katika kitabu cha washi’a, kwamba Hadhrat Ali "radiyallahu anhu" aliacha kudai haki kwa sababu hakuwa na watu wa kutosha kumuunga mkono (Allahu taala atukinge kutokana na kusema hivyo), basi angekuwa kapuuza amri ya Allahu taala kwa sababu angekuwa ameogopa kutekeleza jukumu alilopewa na Allahu taala na mtume wake. Hata hivyo, ukweli unaojulikana kote ulimwenguni ni kwamba Hadhrat Ali "karramallahu wajhah" ambae alikuwa binamu wa kwanza wa mtume "swallallahu alaihi wa sallam" na mkwe wake na pia simba wa Allahu taala, angalichagua kifo kuliko kumwacha mtu kumharibia jina kwa kumhusisha na kitendo chenye kuaibisha kama woga, bila kujali adui yake angekuwa nani na katoka sehemu gani duniani. Sasa mnaona kuwa kitendo kibaya kama hicho inafaa kihusishwe na Amir al- Mu’minin Ali "karramallahu wajhah" aliyekuwa bwana wetu.

Kauli yenu hii huuelekeza uhasama kwake, badala ya kuelezea upendo wenu kwake. Kwa hiyo, naona kuwa nina deni la kubainishia watu waliopo hapa ukweli kuwa imamu huyu ametakasika kutokana na hayo wanayomhusisha nayo na hana mapungufu kama inavyofikiriwa.

(Niliendelea), “Kauli yako kwamba mtume "swallallahu alaihi wa sallam" aliomba kalamu na karatasi ili aandike wasia lakini Umar akamshawishi kuachana na jambo hilo, si sahihi madhali hakuna ushahidi kuthibitisha kuwa mtu huyu aliye na hadhi ya juu (Hadhrat Umar) angeonyesha tabia kama hiyo. Kwani Abdulla ibn Abbas anasema, kama ilivyosimuliwa kwenye Maghaazi, sehemu ya Sahih Bukhari: ilikuwa Alhamisi ugonjwa wa Bwana wetu mtume ulipozidi. Alisema, “Niletee karatasi! Nitaandika kitabu (wasia) ili msipotee baada yangu. Watu waliokuwepo wakaanza kuzungumza. Mtume akasema: “Haifai kuongea kwa sauti mbele ya mtume! “ mtu mmoja akauliza, “Je, yuko kwenye weweseko? Muulize”. Tena Abdullah alisimulia kuwa mtume "swallallahu alaihi wa sallam" alikuwa mgonjwa. Tuliokuwa naye tulikuwa wachache. Akasema, “Nitakuandikieni kitabu (wasia) ili msije mkapotea baada yangu”. baadhi yetu tukasema, “Maumivu yake yamezidi. Tuna Qurani tukufu.

Kitabu cha Allahu taala kitatutoshelezea haja”. Hatukukubaliana. Baadhi yetu walisema, “hebu tulete karatasi! Acha aandike ili tusipotee baadae!” wengine wakasema, “mambo mengine. Kauli tofauti ziliongezeka. Mtume akasema “Simameni!”

“Kwahiyo, kama ilivyosimuliwa katika Sahih Bukhari, kitabu chetu kinachothaminiwa na kutegemewa zaidi baada ya Qurani, ukinzani unaosemekana kutokea haukutokana na mtu maalum. Watu wachache walijiuliza iwapo ingekuwa vyema kutofanya jambo waliloambiwa. Kwani usimulizi wa Bukhari uko katika hali ya wingi, “walisema’ jambo linaloashiria kuwa wale walioitikia walikuwa zaidi ya mmoja. Kwa hiyo, si sawa kujaribu kutumia tukio hili kama msingi wa kumlaumu Hadhrat Umar "radiyallahu anhu" peke yake. Kama pangekuwepo watu wa kulaumiwa katika tukio hili, basi watu wote waliokuwepo wangegawana sawasawa lawama hiyo ya kufikirika. Ali na Abbas "radiyallahu anhuma" walikuwa miongoni mwao. Kwa hiyo, wao pia wangelaumiwa. Sasa, kwa misingi yoyote ambayo washi’a wangewatetea Hadhrat Ali na Abbas, tungependa kupendekeza sababu hizo hizo ili kumtetea Hadhrat Umar.

(Niliendelea), “Wanahadithi hutoa maelezo tofauti kuhusiana na hotuba iliyotolewa huko Ghadiir Hum. Kwa vyovyote vile, hotuba hii haiungi mkono fikra yenu. Zaidi ya hayo, madai yako kwamba aya ya kumi na saba ya Suratul Maidah inayosemwa iliteremkia huko Ghadiir Hum ni ya uongo. Kwani madai yako haya hutoa picha kwamba mtume "swallallahu alaihi wa sallam" hakuwasilisha maamrisho ya Allahu taala kwa masahaba (Allahu taala atukinge na matamko kama hayo)! Katika hali hii, ingemaanisha kuwa kwa vile hakutaka kuwasilisha amri hii na badala yake akamwomba Jibril "alaihis-salaam" katika hotuba hii amuombe Allahu taala amsamehe, alikuwa ameacha kutekeleza amri kwa kuwaogopa masahaba. Hapana shaka kwamba bwana wetu Muhammad "swallallahu alaihi wa sallam" hakuwa na hatia yoyote katika mambo ya namna hii.

“Ushahidi wetu wa pili, ni kwamba madai yako hudokezea kwamba Allahu taala hakumkinga Mtume dhidi ya watu wengine hadi wakati alipowasilisha hotuba hii kabla ya kifo chake. Kwa upande mwingine, ilikuwa ikijulikana kabla ya hotuba hii kwamba Allahu taala alikuwa akimpa kinga. Kwa hiyo, madai yako ni ya uongo kwa sababu hukinzana na ukweli uliokwisha wekwa bayana.

“Ushahidi wa tatu, ni kwamba madai yako hukusudiwa kuonyesha kwamba mtume "swallallahu alaihi wa sallam" alikuwa akiwaogopa waumini hadi siku hiyo na kwamba alikuwa akiwaogopa masahaba pia.

Kwa upande mwingine, ukweli ulioripotiwa kupitia kwenye masimulizi tofauti ni kwamba masahaba watukufu "ridhwanullahu alaihim ajma’in" hawakusita hata kidogo kujitolea na kuwatoa wazazi wao muhanga kwa ajili ya mtume "swallallahu alaihi wa sallam". Kufikiria kuwa masahaba waliungana kutoa tishio kwa mtume "swallallahu alaihi wa sallam" ni jambo linalopingana na mantiki na mafundisho ya kiislamu. Inajulikana wazi jinsi mtume alivyoeneza Uislamu kwa ujasiri bila ya kuhofia lolote, akitii aya tukufu isemayo “Wambie watu waliyoamrishwa, usipofanya hivyo hutokuwa umefikisha ujumbe wake” alipokuwa katika hali ya upweke na maadui zake pamoja na makafiri wa Kikuraishi walioonyesha ukatili wao. Kusema kwamba aliogopa kuwasilisha maamrisho kwenye tukio la Ghadiir, baada ya kuuteka mji wa Makka na kusilimu kwa makundi ya watu kutoka kila pembe wakiwemo mashujaa wa Banii Hashim na Bani Abdu Muttwalib, na baada ya kuteremshwa kwa Sura An-Nasr ili kutoa habari njema ya ushindi mpya, na kwa kuzingatia ukweli kwamba walikuwa katika sehemu ambapo Ansar na Muhajirun ndiyo waliokuwa wengi, ni kumkashifu vibaya sana na ni utovu wa heshima kwa mtume "swallallahu alaihi wa sallam" aliyepambwa na sifa zilizo bora. Isitoshe, kusema kwamba aliwaogopa masahaba ni sawa na kuikanusha aya ya mia moja na kumi ya Sura Aali-Imran inayosema, “Nyinyi mumekuwa umma bora (kuliko wengine) waliotolewa miongoni mwa watu”. Kwa vyovyote vile, hakuna namna ya kuthibitisha madai hayo.

“Ushahidi wa nne. Madai yako kwamba Bwana mtume "swallallahu alaihi wa sallam", baada ya kumuasi Allahu taala kwa kutowasilisha amri yake kwa masahaba, alirejea Madina. Alipougua, alimteua Abu Bakr kuchukuwa nafasi yake kama Imamu kwa siku kadhaa. Kwa kufanya hivyo alipuuza amri ya Allahu taala kwa mara ya pili kwa kumwacha Ali. Kulingana na madai yenu, Allahu taala alikuwa amemwamrisha kumteua Hadhrat Ali kuwa Imamu. Ingawa alimteua Abu Bakr kuwa Imamu baada ya kuamrishwa na aya kuwambia masahaba kumfanya Ali imamu baada yake (kama mnavyodai) katika aya iliyoteremkia Ghadiir Haum, ukweli ni kwamba aya hiyo iliteremkia Arafa na iliwalenga washirikina makureshi kama inavyoelezewa kwa itifaki ya wanazuoni. Kama Mtume angalijua kuwa Hadhrat Ali alipaswa kuwa khalifa wa kwanza, angalitaja jambo hilo. Hapakuwa na sababu ya kuogopa kutaja jambo hilo. Kwani watu wa Makka, hususani Bani Abdul Muttwalib walikuwa jamaa zake, wangefurahi na hakuna mtu ambae angeogopa wala kudhurika.

“Licha ya hayo yote, hotuba hiyo duni, yenye kina kifupi, ikichunguzwa kwa makini, na kwa jicho lisilokuwa na upendeleo wala ukaidi, haiwezekani kuwa matamko haya yalitolewa na mtu ambae ni mweledi wa fasihi ya Kiarabu, licha ya kutoka kwenye kinywa cha mtume "swallallahu alaihi wa sallam" ambae alikuwa na ujuzi wa kipekee wa ufasaha na balagha. Hivyo, kauli hizo zote ni uongo na zimezuliwa na watu wa nje (wasio Waarabu). Hata kama kauli isemayo, “Basi yeyote ambae mimi ni mawla (msaidizi kipenzi kiongozi) wake, Ali anapaswa kuwa mawla wake pia”, ambayo ni mojawapo ya kauli hizo, (hata kama ingekuwa hadithi ya kweli), isingemaanisha kuwa Hadhrat Ali ndiye alipaswa kuwa Imamu wa kwanza.

Kwani neno ‘mawla’ lina maana mbalimbali. Maana ishirini za neno hilo zimeandikwa kwenye kamusi ya Kiarabu. Maana ya neno la aina hii hutambulikana kulingana na muktadha wa matumizi yake (katika matini fulani) na inaweza kuwa maana halisi au maana dokezi. Si sahihi kutoa ufasiri wake bila kuzingatia ishara kama hiyo. Haijulikani wazi iwapo ingekuwa sawa kutoa maana zake au baadhi yake hata hivyo, baadhi ya wanazuoni wanasema kwamba si sawa. Tuchukulie tu kwa ajili ya kuridhia kimya kimya kwamba tungesema ingekuwa sawa. Tumekubaliana nanyi katika kulifasiri neno ‘mawla’ kama ‘mpenzi’ na ‘msaidizi’. Halafu tuchukulie kuwa haifai kutoa maana nyengine. Katika hali kama hii, tunapaswa kutoa maana tunazokubaliana juu yake. Na kwa sababu hii ndipo Abdul Ghafiir ibn Ismail Faaris (451H-529H/ 1135 A.D. huko Nishapur), alielezea neno ‘walii’ katika kitabu chake **Majma’ul Gharaib**, huinukuu hadithi hii kama, “Ikiwa mtu ananipenda na kunitambua kama msaidizi wake, lazima amtambue Ali kama msaidizi wake pia”. Suala hili likifikiriwa kwa makini, itabainika kuwa hadithi hii haiashirii ukhalifa wala ubora wa Ali hata kidogo. Kwa sababu isingesihi kuelezea maana ya ‘walii’ kama ‘awla’, kilugha wala kiislamu. Ni dhahiri kwamba tafsirii kama hiyo si ya kiislamu. Ama kilugha, maneno yenye kategoria (Wizani) ya ‘maf’al’ hayajatumika kabisa katika kategoria ya ‘af’al’ katika mofolojia ya Kiarabu”.

Mulla mkuu akasema, “Abu Zaid, mwanalekskografia alisema kwamba yalitumika katika tafsiri ya Abu Ubayda. Na hulitafsiri tamko “ni mawla wenu” kama “ndiye anayefaa kwa ajili yenu”.

Nilisema, “Kauli yake haiwezi kutumika kama ushahidi. Kwa sababu, hakuna m taala mu wa Kiarabu aliyekubali kauli yake hiyo. Kama yangalikuwa visawe, ingalikuwa sawa kusema “fulani ni mawla (msaidizi, mpenzi) wako! Lakini wanalekskografia wanasema haitosihi kamwe. Kauli ya Ubayda imepingwa na njia nyingine pia. Tumeona

kwamba neno ‘awla’ haliwezi kutumika badala ya ‘mawla’. Tuchukulie kuwa tumekubali kuwa linaweza kutumika, bado lisingetumika kumaanisha ‘kuwa na, kutumia’. Labda awla humaanisha “anayefaa zaidi kuheshimiwa na kupendwa”. Hata kama ingekubalika linamaanisha kutumia, isingewiana na maana ya aya tukufu. Je, neno ‘awla’ linalojitokeza katika Sura Aali-Imran, aya ya sitini na nane inayosema, “Watu wanaomkaribia zaidi Ibrahim ni wale waliomfuata” linaweza kusemekana kumaanisha, “kutumia Ibrahim?” Awla katika muktadha huu sana sana linaweza kumaanisha “Anayefaa zaidi kupendwa”.

Zaidi ya hayo, neno ‘walii’ lililotumika mwishoni mwa hadithi humaanisha ‘kupenda’. Kama lingemaanisha ‘kufaa zaidi kutumika juu ya mtume wa Allahu taala” basi, Mtume angalisema, “yeyote anayefaa kutumika”. Kwa vile hakusema hivyo, tamko lililoko kwenye hadithi humaanisha, “kumpenda Hadhrat Ali na kutokuwa na uhasama naye” na sio “kufaa kutumika”. Kwa kweli, Abu Nua’ym Ahmad ibn Abdullah "rahmetullahi alaih" [aliyefia Isfihan mwaka wa 430H], husimulia kutoka kwa Hasan: Hasan aliuliza juu ya jambo hili. Wakasema: “Je, hadithi tukufu “...yeyote ambae mimi ni mawla wake...” huonyesha kuwa Ali anapaswa kuwa Khalifa wa kwanza? Jibu lake lilikuwa, “Kama mtume angekusudia kusema kwa hadithi hii kwamba Hadhrat Ali anapaswa kuwa khalifa wa kwanza, angesema, “Enyi watu! Mtu huyu ndie walii wa wajibu wangu. Atakuwa khalifa baada yangu. Sikilizeni na mtii amri hii! Naapa kwa jina la Allahu taala kwamba kama Allahu taala na mtume wake "swallallahu alaihi wa sallam" wangependelea kwamba Ali awe khalifa wa kwanza, basi Ali angekuwa amekaidi amri ya Allahu taala inayohusu suala hili na kwa kufanya hivyo angekuwa ametenda dhambi kubwa”. Msikilizaji mmoja aliposema, “Kwa nini mtume hakusema kwamba yeyote ambae mimi ni mawla wake, Ali pia, anapaswa kuwa mawla?” Hasan akasema, “Hapana! Wallahi mtume wa Allahu taala angalipenda Ali Kuwa khalifa wa kwanza, angalitoa amri hii kwa uwazi kabisa kama alivyowaamrisha Waislamu kudumisha sala na kufunga”. Kwa hio, kauli hizi za Hasan, alie miongoni mwa Ahl Bayt na mtoto wa Hadhrat Ali, hudhihirisha kuwa kauli zenu ni za uongo na upotofu”.

9- Mulla alinyamaza. Kisha akabadili mkondo: “Utasema nini kuhusu hadithi isemayo ukweli kwamba siku ya kiama kila Muislamu ataulizwa iwapo alimpenda Ali na wanawe na pia juu ya tabia yake kuhusu mambo ya dunia na akhera? Kwani Ali ibn Muhammad ibn Sabbaagh Maliki (aliyefariki dunia mwaka wa 855H/ 1451 A.D.) katika

kitabu chake **Fusuul ul-muhimma**, kinachotokana na **Manaaqib** humnukuu ibn al-Muayyad akisema, “Abu Burayda alisema: “Siku moja nilikuwa nimekaa mbele ya mtume. Bwana Mtume akasema, “Naapa kwa jina la Allahu taala ambae nguvu zake zimeshikilia roho yangu kwamba siku ya kiama maswali ya kwanza ambayo watu wataulizwa ni: Mlitumia vipi maisha yenu? Mliichakaza vipi miili yenu na mlifanya mambo gani? Mliipata wapi mali yenu na mliitumia wapi? Mlimpenda mtume wangu?” Hadhrat Umar aliyekuwa amekaa upande wangu alisema “Dalili ya kukupenda ni ipi ewe mtume wa Allahu taala? Mtume "swallallahu alaihi wa sallam" akaweka mkono wake juu ya kichwa cha Hadhrat Ali aliyekuwa amekaa karibu nae, akasema, “Kunipenda mimi (baada ya kifo changu) ni kumpenda huyu”. Kama ilivyoandikwa katika kitabu hicho hicho, Hadhrat Ali alisema, “Wallahi Bwana Nabiyyul ummiyy "swallallahu alaihi wa sallam" alisema kwamba watakaonipenda ni waumini na wasionipenda ni wanafiki”. Sasa, huoni kwamba mtu ambae watu wataulizwa juu ya upendo wao kwake siku ya kiama lazima awe mbora kuliko wengine na kizazi chake hustahili ukhalifa kuliko watu wengine?”

Nilimjibu, “Ibn Sabbaagh ambae unamwita Maliki si mfuasi wa madhehebu ya Malik. Vitabu na maandishi yake hudhihirisha kuwa ni mduasi wa madhehebu ya Kishi’a. Ni ukweli ulioelezewa na wanazuoni kwamba Ibn Muayyad, maarufu kwa lakabu “Mtoto wa Harzem” ni mshi’a pia. Tena hakuna haja ya kutafuta ushahidi mwingine.

Baadhi ya mashia hubadili hadithi na kuzifungamanisha na mwanazuoni maarufu wa hadithi. Wanajaribu kuwapotosha waislamu kwa uongo kama huo. Ni wazi kuwa abadilishaye au kupotosha hadithi iliyoandikwa kwa matini yake sahihi kwenye vitabu ni muongo kweli kweli. Matini sahihi ya hadithi imenukuliwa hapa na Imam muhammad ibn Isa at-Tirmidhi (209 H./ 892 A.D.) “Mwanaadamu ataulizwa juu ya mambo manne. Atulizwa juu ya jinsi alivyotumia muda wa uhai wake, elimu yake aliifanyia nini, mali yake aliichuma vipi na mwili wake aliuchakaza vipi”. Tabrani vilevile ameinukuu hadithi hii tukufu, lakini kishazi cha mwisho ni kama ifutavyo “Jinsi alivyotumia ujana wake”. Kwa hiyo matini sahihi ya hadithi hii imenukuliwa hivyo. Upendo wa Ahl al-Bayt au jina la Hadhrat Umar halikutajwa ndani yake. Hii ina maana kwamba ibn Sabbaagh na ibn Muayyad walikuwa waongo. Hata hivyo, hadithi hiyo haihusiani kwa vyovyote na ukhalifa.

Hata kama tungekubali matini iliyopotoshwa kuwa sahihi, ingemaanishisha ‘kuwapenda sana Ahl Bayt’. Madhehebu ya kisunni hutuamrisha kuwapenda sana Ahl al- Bayt, upendo unaoendana na

hadhi ya kila mmoja wao bila ya kupunguza wala kuzidi mipaka kwa hali yoyote. Ili uwe msunni wa kweli, lazima uwapende Ahl al-Bayt kwa namna inayoendana na heshima yao. Lakini wewe unatoa matamko yanayo kinzana na Uislamu ili kuendeleza kampeni ya kuwapenda. Mwenye chembe ya imani moyoni mwake hawezi kutoa matamko kama hayo. Unasema, ‘Ampendae Ali, hakuna baya litakalomdhuru’. hivyo hivyo, baadhi yenu huzua hadithi. Kwa mfano, tunawezaje kumuamini mtu anayemkashifu Bwana mtume "swallallahu alaihi wa sallam" kwa kumsingizia kuwa alisema, “Kundi la Ali halitoulizwa juu ya madhambi madogo na makubwa. Maovu yao yatabadilishwa kuwa mazuri?” Ibn Babaawayh huizua hadithi ambamo alimnukuu Ibn Abbas akisema kwamba mtume wetu alisema, “Allahu taala hatowachoma moto vipenzi vyake”. Hadithi nyingine wanayoizua ili kuwapotosha watu, “Ampendaye Ali ataingia peponi hata kama ni Myahudi au Mkristo”.

Je, huo si udhalimu kumkashifu Bwana mtume "swallallahu alaihi wa sallam" kwa kumzulia matamko kama hayo kwa jina la hadithi?

[Jina halisi la Abu Ja’far ibn Baabawayh ni Muhammad ibn Ali. Ni mmoja wa wa taala mu wa Fiqhi na Tafsiri wa Kishi’a. Ana Kitabu cha Tafsiri na kingine cha Fiqh kinachoenziwa na kundi la Kishi’a la Imaamiyya. Alizaliwa Khurasan akafariki dunia mwaka wa 381 H./ 991 A.D.].

“Kumsingizia mtu si kitendo cha Uislamu wala mantiki. Katika Sura An-Nisaa aya ya 121 Allahu taala anasema, “Hao makao yao ni Jahannamu, na wala hawapati makimbilio kutoka humo”. Sura Az-Zilzal aya ya mwisho inasema, “Na anayetenda chembe ya uovu atauona!”

Kashifa zisizokuwa na msingi wowote hushindana na aya hizo tukufu.

Zaidi ya hayo, ni kitendo cha ibada kuwapenda Ahl al-Bayt. Jambo hili hutegemea kuwa na imani kama katika aina nyingine za ibada. Sura Al-Anbiyaa, aya ya 94 husema, “Na atendae mema naye ni muumini basi haitakataliwa juhudi yake. Na hakika sisi tunamwandikia”. Si kitendo cha kiislamu kusema kwamba watu wasiokuwa na heshima hii ya imani, kama vile Wayahudu na Wakristo wataingia peponi kwa kuwapenda Ahl al-Bayt tu, au kuamini kuwa kuwapenda watu hawa kutabadilisha madhambi madogo kwa makubwa kuwa matendo mema. Katika vitabu vya Kishi’a imetajwa kuwa Ali (Karramallahu wajhah) alikuwa akitoa nasaha mara kwa mara kwa watu wa nyumba

yake, “Msiwategemee mababu zenu! Musiache kutekeleza amri za Allahu taala hata kidogo!”

‘Matamko aliyotoa hayana thamani kwa sababu yanakinzana na nasaha ya Hadhrat Ali na ripoti nyingine nyingi.

Kupata furaha duniani na Akhera na nidhamu katika mambo ya dunia hutegemea kuwazuia watu kutenda madhambi na matendo yaliyokatazwa, ni kweli kama kusema kwamba, “Madhambi yatabadilika kuwa thawabu”. Kauli hii itawachochea wenye nia mbaya na hata washi’a kufanya maovu, madhambi na dhuluma, ambayo itachangia kuuvunja Uislamu. Ni wazi kuwa mwenye uwezo fulani wa kiakili hatageuka kuyaangalia matamko hayo, licha ya kuyaamini”.

Baada ya maneno hayo, watu waliohudhuria kikao hicho walipendekeza kuwa maswali yaliyokuwa yameandaliwa yaulizwe na yatolewe majibu. Lakini baadhi ya washi’a walimwambia Mulla mkuu, “Tahadhari kubishana na bwana huyu. Kwani ni mwanazuoni mwenye elimu nyingi kama bahari. Ushahidi wote uliotoa amethibitisha kuwa ni uongo. Yumkini ukapoteza umaarufu na heshima yako”.

Baada ya haya, Mulla mkuu aliniangalia huku akitabasamu. Alisema, “Wewe ni mwanazuoni hodari. Ungeweza kujibu swali lolote kama ulivyoyajibu haya. Lakini Bahr al-Ilm wa Bukhara asingeweza kupinga hoja zangu”.

Nilisema, “Mwanzoni mwa mazungumzo haya ulisema kwamba wanazuoni wa Ahl as-Sunna (rahmatullahi alaihim ajma’iin) hawawezi kukanusha ushahidi wako. Ni tamko lako hili ndilo lilitupa msukumo wa kuongea”.

“Kwa vile mimi ni Mwirani, sina ukwasi katika uhodari wa matawi ya taaluma ya Kiarabu. Labda nilitumia maneno yasiyofaa. Sikukusudia hilo”.

Nilisema, “Hebu nikuulize maswali mawili. Acha wanazuoni wenu wote waungane na watoe majibu”. “Maswali hayo ni yepi?” Aliuliza.

10. “Swali langu la kwanza ni hili, Nyinyi washi’a mnasema nini kuhusu masahaba watukufu?”

“Masahaba wote, isipokuwa watano tu, waliritadi kwa sababu hawakumchagua Hadhrat Ali kuwa khalifa. Walitoka kwenye Uislamu. Masahaba hao watano ni Ali, Miqdad, Abu Dharr, Salman na Ammar ibn Yasir”, alijibu.

Nilisema, “Tukichukulia kuwa uliyosema ni sahihi, ilikuwaje Ali akamuozesha Hadhrat Umar binti yake Umm Kulthuum?” “Ndoa hiyo ilifanyika bila yeye kupenda”. Alijibu.

Nilisema, “Naapa kwa jina la Allahu taala kwamba unamshushia hadhi Hadhrat Ali kwa namna ambayo hata Mwarabu wa chini kabisa angelalamikia kitendo hicho. Matusi mabaya kama hayo yaliyomlenga Hadhrat Ali lazima yawe sehemu ya mpango hafifu. Kama ajuavyo Allahu taala, Mwarabu mwenye hadhi ya chini kabisa, anayejiamini angetetea utukufu na heshima yake kiasi cha kujitolea muhanga. Seuze mtu mashuhuri kutoka kwenye ukoo wa Bani Hashim waliokuwa wenye hadhi ya juu na waadilifu zaidi kuliko makabila mengine ya Kiarabu katika nasaba, uungwana, heshima na umaarufu na ingewezekana vipi kwa kabila lote kukubali fedheha kama hiyo? Unasemaje kuhusu mheshimiwa na shujaa maarufu ambaye sifa yake ya “simba wa Allahu taala” imeenea duniani kote?”

Alisema, “Pengine jini jike lilimpenda Umar na likajitokeza mbele yake katika sura ya Umm kulthum”.

Jibu langu lilikuwa, “Kauli hiyo huondoa ile iliyotanguliwa kwa kuhongwa. Akili inawezaje kukubali upuuzi kama huo? Njia hii ya kuelezea ukweli ingegeuza sheria zote za Uislamu kichwa chini. Kwa mfano, mtu anayerudi nyumbani akitoka kazini anaweza kujikuta kazuiwa na mke wake kuingia ndani ya nyumba yake akidai kuwa yeye ni jini na siyo mume wake. Tuchukulie kuwa ameungwa mkono na mashahidi wawili kuthibitisha kuwa ni yeye na sio mwingine. Mara hii mwanamke anaweza kukataa mashahidi akidai kuwa wao pia ni majini. Hivyo, kila kitu kitavurugika kabisa sio tu katika nyumba moja lakini pia kila mahali. Muuaji au mwizi anaweza kukataa kanuni ya adhabu ya Kiislamu isitekelezwe kwa kusema kwa mfano, “Mimi si mtu yule mnayemtafuta”. Anaweza kuwa jini pia”. Kwa kweli, Ja’far as-Siddiiq "rahmatullahi alaihi" mnayedai kuwa ndie kiongozi wa madhehebu yenu, labda alikuwa jini”. Mulla mkuu alikanganyika. Akanyamaza. Kutokana na hali hiyo, nilisema, “Sasa nauliza swali la pili”.

11. “Je, kwa mujibu wa madhehebu yenu, amri za khalifa katili zinakubalika?”

“Hapana! Si sahihi. Hazipaswi kukubalika”. Alijibu.

“Mama yake Muhammad ibn Hanafiyya mtoto wa Ali, alikuwa nani?”. Niliuliza.

Alisema, “Alikuwa Hanafiyya bint Ja’far”.

Niliuliza, “Ni nani alimtia mbaroni Hanafiyya?”

Alisema kwamba hakumjua. Alijua lakini akasema hakumjua ili kudhoofisha hoja. Baadhi ya hadhira walisema kwamba alitiwa mbaroni na Abu Bakr "radiyallahu anhu".

Nikasema, “Kila mtu anajua umuhimu wa kuwa mwangalifu katika kumchagua mchumba. Mbona Hadhrat Ali alimwoa kijakazi na kuzaa nae watoto, mtu aliyetiwa mbaroni na Hadhrat Abu Bakr mnayemchukulia kuwa hakuwa Imamu muongofu na khalifa wa haki?”

Alisema, “Labda Hadhrat Ali aliwaomba marafiki zake kumpa kijakazi kama zawadi, wakamuozesha kijakazi huyo”.

Nilisema, “Unaweza kutoa ushahidi kuthibitisha madai haya?” Mulla mkuu hakuwa na la kusema. Baada ya kunyamaza kidogo, niliendelea.

Ili kuepuka kurefusha mjadala, sikunukuu aya na hadithi kwa sababu hadithi yoyote ambayo ingenukuliwa ingeibua usaili. Kambi zote mbili zingeomba kutoa ushahidi jambo ambalo lingerefusha mjadala.

Wakati huohuo, mazungumzo yaliyojiri kwenye mjadala yaliripotiwa kwa usahihi kwa Shah. Hivyo, Shah aliwaamrisha wanazuoni wa kutoka Irani, Bukhara na Afghanistani kuungana, kuondosha dalili za uasi na kuandika ripoti isiyotenguka akaniteua kuwa mwakilishi wake na raisi wa halmashauri hii ya wanazuoni inayowakilisha mataifa matatu tofauti. Tulitoka nje ya mahema. Waafghani, Wauzbeki na Waajemi walikuwa wakininyooshea vidole. Wanazuoni sabini wa Irani walikusanyika nyuma ya kaburi la Ali (karramallahu wajhah). Ali Akbar, Mulla Mkuu ndiye aliyekuwa kiongozi wa wanazuoni wa Irani. Mulla mkuu alinionyesha Mulla Hadi Khodja, aliyekuwa Bahr I-Ilm kutoka Bukhara, akamuuliza iwapo alinijua. Alipomjibu kwamba hanijui, alisema, “Mtu huyu ni Suwaydi Zade Shaikh Abdullah Efendi, mwanazuoni mashushuri wa Kisunni. Shah alimuomba Ahmad Pasha kumtuma hapa kuhudhuria mjadala wetu na kutuongoza kama mwakilishi wa Shah. Tukifikia makubaliano ya pamoja, atakuwa shahidi wetu sote na atatufanyia uamzi wa mwisho. Sasa, hebu tuondoe dalili zozote za uasi. Hebu tuziondoe mbele yake. Hata hivyo, Abu Hanifa hatuiti makafiri. Pamoja na hayo, hebu tufikirie kwa makini juu ya kadhia hii. Kwa mujibu wa **Sherh al-Mawaaqif** Waimaamiyya si makafiri. Abu Hanifa ameeleza katika kitabu chake kiitwacho **Fiqh Akbar**, “Hatuwaiti watu wanaoswali wakielekea kibla makafiri”. Na imeandikwa katika kitabu kiitwacho **Sherh al-Hidaya** kwamba kundi la Waimamiyya ni kundi mojawapo la

Waislamu. Hata hivyo, vizazi vya Wasunni vya siku hizi vimetuita makafiri. Na vizazi vyetu vya siku hizi vimekuiteni makafiri pia. Sisi si makafiri wala nyinyi. Sasa, hebu tuchunguze matamko yaliyopelekea vizazi vyenu kutuita makafiri ili tuyakomeshe”. Hadi Khodja alisema, “Mmekufuru kwa sababu ya kuwalaani masheikh wawili (Shaykhayn), yaani Abu Bakr na Umar "radiyallahu anhuma"”.

Mulla mkuu akasema, “Tumeacha kuwalaani masheikh hao wawili”.

Hadi Khodja alisema, “Mlikufuru kwa kuwaita masahaba watukufu (ridhwanullahi alaihim ajma’iin) makafiri”.

Mulla mkuu akasema, “Sasa tunasema, masahaba wote "ridhwanullahi alaihim ajma’iin" ni Waislamu na ni wakweli pia”.

“Mnasema kuwa ndoa ya mut’a ni halali”.

“Ni haramu, waliofedheheka peke yao ndio wanaweza kufanya hivyo”.

“Mnamchukulia Hadhrat Ali kuwa mbora kuliko Abu Bakr na mnasema kuwa ilikuwa ni haki ya Ali kuwa Khalifa wa kwanza”.

“Mtu aliyembora zaidi baada ya mtume "swallallahu alaihi wa sallam" ni Abu Bakr Siddiiq. Anayemfuata ni Umar. Halafu Hadhrat Uthman. Hadhrat Ali huja baada yake "ridhwanullahi alaihim ajma’iin". Haki yao ya ukhalifa ipo katika mpangilio nilioutaja”. Bahrul ilm aliuliza, “Mtazamo wenu ni upi katika imani?”

Mulla mkuu alijibu, “Imani yetu ni ya Abul Hasan al-Ash’ari”.

Sasa, ni muhimu kujua mambo yote yaliyotajwa na Uislamu kuwa halali na haramu na kuyaamini hivyo, kwa maneno mengine, usiharamishe yaliyo halali wala kuhalalisha yaliyo haramu”.

“Tunakubali kaida hii”. Alisema. Bahrul ilm akasema, “Haifai kutenda yale ambayo madhehebu yote ya Ahl as-Sunna yaliyataja kwa itifaki kuwa ni haramu”.

Mulla mkuu akasema, “Tunakubali hili pia”. Halafu akaongezea, “Tunakubali haya yote. Sasa mtuchukulie kuwa miongoni mwa makundi ya kiislamu”. Bahr ul-ilm akasema, “Anayewalaani masheikh wawili huwa kafiri”.

“Tumekomesha kitendo hicho cha kuwalaani masheikh hao wawili "radiyallahu anhuma". Tumekubali kaida zingine pia. Sasa huwezi kutuchukulia kuwa waislamu?” Bahr ul-ilm alirudia kauli yake, “Ni ukafiri kuwalaani masheikh wawili”. Kusudio lake lilikuwa kudokezea kwamba, “kulingana na madhehebu ya Kihanafi, kama mtu atawalaani

masheikh hao wawili, toba yake haitokubalika. Wairani walikuwa wakifanya hivyo. Kwa hiyo, wamekufuru. Kuacha sasa kuwalaani hakutawatoa kwenye hali hiyo ya ukafiri”. Mulla Hamza, Mufti wa Waafghani alisema, “Ewe Hadi Khodja! Kuna ushahidi wowote unaothibitisha kuwa Wairani waliwalaani masheikh hao kabla ya kikao hiki?”

Hadi Khodja alisema, “Hapana! Hakuna ushahidi”.

Mulla Hamza aliuliza, “Ikiwa hawatawalaani kuanzia sasa, kuna sababu gani nyingine ya kuacha kusema kwamba hawa ni waislamu?”

Hadi Khodja akasema, “Wao ni Waislamu madhali wamefanya hivyo. Hii ina maana kwamba tunakubaliana juu ya halali na haramu, mazuri na mabaya”.

Baada ya haya, wote walinyanyuka wakakumbatiana. Waligeuka upande wangu wakasema, “Kuwa shahidi wetu”. Halafu tukatawanyika. Ilikuwa Jumatano jioni, tarehe 24 Mwezi wa Shawwal. Palikuwepo Wairani wapatao elfu kumi, wote wakituangalia.

Kama kawaida, I’timadu ud-Dawla (Waziri mkuu) alimwacha Shah akaja kwangu saa kumi za usiku akaniambia “Mtukufu Shah amekutumia Shukrani na salamu zake. Ameamuru kuwa wanazuoni wale wale wakutane tena kesho waandike na kutia sahihi uamuzi uliofikiwa”. nilisema kwamba nitafanya hivyo.

Alhamisi jioni, nilienda kwanza kwenye kikao. Wairani wapatao elfu sitini walikuwa wamekusanyika huko, hivi kwamba kulikuwa na msongamano mkubwa ulioenea sehemu zote kuanzia kwenye kaburi la Ali hadi sehemu za mbali. Nilipowasili, nilikaa kitako.

Mkataba mrefu ukaletwa. Kwa amri ya Mulla mkuu, Mufti Aqa Heseyn aliusoma kwa sauti. Ulikuwa umeandikwa kwa Kiajemi. Ifuatayo ni tafsiri yake.

Ni kawaida na hekima ya Allahu taala kuwatumia watu mitume ili wawaamrishe mema na wawakataze mabaya. Miongoni mwa mitume, zama za mwisho ilikuwa ya mbora wao, mtume Muhammad "swallallahu alaihi wa sallam". Kama mtume wa mwisho, alitimiza wajibu wake wa kufundisha maamrisho na makatazo ya Allahu taala na akaaga dunia. Baada yake, masahaba walikusanyika na kwa itifaki walikubaliana juu ya ubora wa Abu Bakr as-Siddiq katika uchamungu, wema na kushikamana na dini, wakamteua kuwa khalifa. Hadhrat Ali pia alikuwa miongoni mwa waliomchaguwa. Alipiga kura yake kwa hiari bila kulazimishwa wala kutishwa. Kwa hiyo, ukhalifa wa Abu Bakr

ulikuwa kulingana na makubaliano ya pamoja ya maswahaba watukufu. Maswahaba wote waliomchagua walikuwa waadilifu na waislamu wa kweli (ridhwanullahi alaihim ajma'iin). Wamesifiwa katika Quran tukufu, kwenye aya inayosema, "Muhajir anda Ansar who are ahead of and above all others..." na pia "Verily Allah taala loves those believes who promised thee under a tree" amewaridhia Allah wale waumini walio chukuwa ahadi ya utii chini ya mtii na pia "mbora wa viumbe "swallallahu alaihi wa sallam" aliwasifu, "Masahaba wangu ni kama nyota mbinguni, ukimfuata yeyote utaongoka".

Baada ya Abu Bakr as-Siddiq, Hadhrat Umar alikuwa Khalifa baada ya kupendekezwa naye. Hadhrat Ali pia alikuwa miongoni mwa waliohudhuria. Hadhrat Umar alipendekeza watu sita kabla ya kufariki dunia na akatoa ushauri kwamba baada yake watu hawa sita wanapaswa kumchagua mmoja wao kuwa Khalifa. Hadhrat Ali alikuwa mmoja wapo wa watu hao sita. Watano kati yao walimchagua Uthman kwa pamoja kuwa Khalifa. Hadhrat Uthman hakutoa ushauri wake katika uchaguzi huu. Baada ya kifo chake cha kishahidi, masahaba wote kwa pamoja walimchagua Hadhrat Ali kuwa Khalifa. Watu hawa wanne waliishi pamoja kwa amani na hapakutokea mgogoro kati yao. Daima walipendana na kusifiana. Kwa hakika, Hadhrat Ali alipoulizwa alikuwa na maoni gani kuhusu Shaykhayn yaani Abu Bakr na Umar, alisema: "watukufu hawa wawili ni maimamu waliochaguliwa kwa uadilifu na haki". Aidha, Hadhrat Abu Bakr alipokuwa Khalifa aliuliza, "Je, Ali alikuwa miongoni mwa walonichaguwa?"

Enyi Wafarsi! Ubora na ustahilifu wa ukhalifa miongoni mwa makhalifa hao wanne ni wa mfuatano huo.

Yeyote anayewalaani, akawakemea au kuwasema vibaya, kaya yake na damu yake itakuwa halali kwa Shah. Watu kama hao wamelaaniwa na Allahu taala, malaika, vitabu vitukufu na mitume! Nilipochaguliwa kuwa Shah kwenye mraba wa Megan mwaka wa 1148, niliweka masharti kadhaa. Na sasa naongezea masharti haya: nakukatazeni kuwalaani Shaykhayn. Munapaswa kukomesha kitendo hicho. Yeyote atakaejihusisha na kitendo hicho kibaya cha kuwalaani, familia yake itatiwa mbaroni, mali yake itanyakuliwa na atauliwa. Zamani kitendo hiki cha kufedhehesha hakikuwepo katika nchi ya Irani.

Kitendo hiki kibaya kilizuliwa na Shah Ismail Safawi na wanawe waliofuata mkondo wake. Kimeshikiliwa kwa miaka ipatayo mia tatu.

Mkataba huu ulisainiwa na kupigiwa muhuri na wanazuoni wote. Kisha (Ferman-i-aali), agizo lililotolewa na Nadhir Shah kushughulikia

marahma ya taifa zima, lilisomwa kwa sauti. Lifuatao ni toleo lake la Kituruki.

**AGIZO**

Kwanza naikabidhi nafsi yangu kwa Allahu taala. Yafaa ijulikane kuwa Shah Isma'il Safawi alijitokeza mwaka wa 906 H. [1500 A.D.]. Alikusanya baadhi ya watu waliokuwa wajinga karibu naye. Ili kupata matakwa ya dunia hii na kufikia mahitaji yake, alichochea mfarakano na uovu miongoni mwa watu. Yeye alizua kitendo cha kuwapa kwa Shaikhayn (jambo ambalo lilipelekea kuibuka kwa dhehebu linaloitwa Shiah). Hivyo, alipanda mbegu za ugomvi mkubwa kati ya Waislamu. Alisababisha bendera za unafiki na uchochezi kupeperuka sana kiasi kwamba, wakati makafiri wakiishi maisha ya faraja yasiyokuwa na wasiwasi, waislamu walikuwa wakiudhiana. Wanauana na kuvunjiana heshima. Kutokana na mkutano uliofanyika huko Megan Square, mkasema kwamba nikikubali ombi lenu, mtaacha imani zote potofu na matamko ya kiwendawazimu ambayo yalikuwa yameota mizizi huko Iran tangu wakati wa Shah Isma'il. Mliahidi kuwa mngeamini na kutamka kwa ndimi zenu kwamba makhalifa wanne ndio wanaostahiki ukhalifa na ni wa kweli huo ndio uliokuwa mtazamo (Madhhab) wa mababu zenu wachamungu na ni sunna yetu yenye baraka, na kwamba mngewapenda wote wanne na kuacha kuwatusi. Na sasa, ili kusisitiza jambo hili jema, nimechunguza suala hili na kuwauliza wanazuoni na washika dini. Wote kwa pamoja wameelezea kuwa tangu siku mtume wetu "swallallahu alaihi wa sallam", na ahli zake na masahaba zake wote, walilingania njia ya ukweli, kila mmoja kati ya makhalifa wanne radhi za Allahu taala ziwashukie, ambao walikuwa sahaba waongofu, walijitolea muhanga wakatoa mali zao, wakaacha wake zao, watoto, na ami zao, na kuvumilia kila aina ya matusi, uovu, na mishale kwa ajili ya kulingania (watu) dini (Uislamu). Kwa sababu hiyo, walitunukiwa usahaba (**suhbat**) maalum wa bwana wetu, mtume wa Allahu taala "swallallahu alaihi wa sallam". Ni kwa sababu hiyo tena, ndiyo walipata sifa iliyoelezewa katika aya tukufu isemayo kwamba "Waheshimiwa miongoni mwa Muhajirina na Ansar...”. Baada ya kufariki kwa bwana wa wema, Abu Bakr as-Siddiq "radiyallahu anhu", rafiki yake wa pangoni, aliteuliwa khalifa wa kwanza kwa kura za sahaba wote, ambao walikuwa wenye kufanya maamuzi kuhusu mambo ya waislamu. Baada yake, aliyechaguliwa kuwa khalifa na kuidhinishwa na sahaba watukufu alikuwa Umar Faruq radhi za Allahu taala zimshukie, akawa khalifa, na baada yake 'Uthman bin Affan, dhu nurayn, radhi za

Allahu taala zimshukie, ambae kati ya wagombea sita (waliochaguliwa na Umar), alichaguliwa katika ofisi ya ukhalifa pasina upinzani wowote, na baada yake Amirul Mu'minin Ali ibn Abi Talib 'karramallahu wajhah', simba wa Allahu taala, chaguo la wale wanaomtafuta mtu (kuwaongoza), hazina ya maadili yasiyo kifani, akawa khalifa. Wakati wa ukhalifa wao, makhalifa wote hawa wanne walikuwa na utangamano na maafikiano baina yao. Walikuwa na udugu na umoja kati yao. Kila mmoja wao alitetea nchi za kiislam dhidi ya ushirikina na uovu wa washirikina. Baada ya zama za makhalifa hawa wanne, waislamu walihifadhi umoja wao katika marahma yanayohusu imani. Kulingana na mabadiliko katika nyakati na hali, wanazuoni wa kiislamu walikuwa na fasiri tofauti katika mambo yanayohusu kufunga, hija, zaka na aina nyingine za ibada, pamoja na hayo, hapakuwa na kukosea au upungufu au ubatilifu katika nguzo za imani au katika kumwenzi mtume wa Allahu taala "swallallahu alaihi wa sallam wa alaa aalihi wa swahbih" au katika kuwachukulia kama waislamu wa kweli. Nchi zote za kiislamu zilihifadhi usafi huu bora hadi pale alipojitokeza Shah Isma'il. Kwa bahati nzuri, kutokana na busara zenu na uongofu wa nyoyo zenu safi, mmetupilia mbali mienendo kama vile kuapa kwa sahaba watukufu na kuwa mashi’a, iliyozuliwa badae. Mmepamba nyoyo zenu kwa upendo wa makhalifa wanne, ambao ni nguzo kuu nne za kasri ya Uislamu. Kwa hiyo, ninaahidi kuwa nitaripoti ahadi hizi tano kwa Padishah, mwenye uluwa, mtumishi wa haramayn-i-sherifayn (miji miwili yenye heri, Makka na Madina), Dhulqarnayn wa pili katika ardhi hii, ndugu yetu, na Sultan wa ardhi ya Wagiriki ya Byzantine. Acha tutimize suala hili kwa namna inayoendana na matakwa yetu. Naomba kwamba yale tuliyoandika hapa yatekelezwe kwa haraka sana, kwa msaada wa Allahu taala! Sasa, ili kuimarisha jitihada hii yenye baraka, Gwiji wa maulamaa (Hadhrat Ali Akbar), kiongozi mkuu, na wasomi wengine wameandika kumbukumbu. Kwa kufanya hivyo, wamevunja mapazia yote ya shaka. Imetambulikana kwamba udanganyifu huu wote na uhasama ulianza na fitna (uovu, uchochevu) uliozuliwa na Shah Isma'il. Kabla yake.

Waislam wa nyakati zote, hasa wale wa siku za mwanzo za Uislamu, walikuwa na imani sawa, mtazamo mmoja. Kwa hiyo, kutokana na msaada wa Allahu taala na ufunuo aliopamba nyoyo zetu kwao, tumefikia uwamuzi huu. Tangu kuja kwa Uislamu mpaka wakati alipojitokeza Shah Isma'il, waislamu wote waliwachukulia makhalifa wanne waongofu kuwa makhalifa wanaofaa na wa kweli. Walijua kwamba waliteuliwa katika wadhifa wa ukhalifa kwa njia ya haki.

Waliepukana na kuwatusi na matamko ya kuwaudhi. Mabingwa katika fani ya uzungumzaji na wahubiri wakuu walielezea wema, sifa na ubora wa makhalifa hawa katika hotuba na mazungumzo yao. Walipotaja au kuandika majina yao yenye kheri, walikuwa wakiongezea tamko 'radiyallahu anhuma' (radhi za Allahu taala ziwashukie). Nimemwamuru muadham mtukufu na mwanazuoni mashuhuri Hadhrat Mirza Muhammad Ali, kulitangaza agizo hilo katika miji yote ya Iran, ili watu wangu walisikie na kulikubali. Kutolitii au kulipinga kutasababisha adhabu ya Allahu taala na hasira za Shah-an-shah (Mfalme). Ijulikane hivyo.

Baada ya kusomwa kwa agizo hili na kueleweka, niliruhusiwa kwenda mbele ya Shah, ambapo nilipongezwa kwa dhati. Nadir Shah alifurahia sana mafanikio haya, na akatoa shukrani zake za dhati. Aliamuru kwamba sala ya Ijumaa iswaliwe katika msikiti wa Kufa. Nikamwambia I’timad-ud-dawla (mtegemewa katika dola/ Mtukufu Mfalme) kwamba sala hiyo haitokubaliwa, kwani watu watatu ambao ni wakazi wa mji ndio wanaohitajika kuhudhuria sala hiyo kwa mujibu wa madhehebu ya Kihanafi, na kwamba idadi hiyo (inayopelekea sala ya Jum’a kusihi) kwa mujibu wa madhehebu ya Kishaafi’i ni (angalau) watu arubaini. Kiongozi mkuu akasema kwamba (watu) wangealikwa tu kuhudhuria khutuba. Nilienda msikitini. Kulikuweko wanazuoni wapatao elfu tano na maafisa. Ali Meded, Imamu wake Shah, alikuwa kwenye minbari. Wakati huo huo, Mulla mkuu na wanazuoni wa Kerbela walionong’onezana wenyewe, na Meded alitolewa kwenye minbari. Mmoja wapo wa wanazuoni wa Kerbela alichukuwa nafasi yake akapanda minbari. Baada ya kumhimidi Allahu taala na kumsalia Mtume, alitaja majina ya makhalifa wanne akisema, "radiyallahu anhu", baada ya kila jina. Hata hivyo, ilipofika zamu ya Umar, alitamka jina Umar kwa kulititilia silabi ya mwisho irabu /i/, ijapokuwa alikuwa mjuzi sana wa Kiarabu (ujuzi unaompa kinga ya kutofanya kosa). (Yaani, alisema *Umari'* badala ya *Umara'*). Kwa hiyo alikiuka kaida zinazolifanya jina Umar ‘ghayr munsarif’ (lisikubali kuwekewa irab /i/ na tanwin). Ilikuwa dhahiri kwamba kulikuwa na hila katika tendo hili. Kulingana na amri ya Shah, maadili yalitangazwa, kwanza juu ya ustawi na utukufu wa Hadhrat Mahmud Khan bin Mustafa Khan, ambae alikuwa Khalifa-i-Muslimin, na kisha juu ya ustawi na utukufu wa Nadir Shah. Sura Al-Jumua ilisomwa katika rak'at ya kwanza. Baada ya sala, niliomba ruhusa kutoka kwa Nadir Shah nikarudi Baghdad. Nilimsimulia Ahmad Pasha matukio yote. Nilitoa nakala ya agano lililofanyika kati ya makundi mawili na nakala ya agizo, ambalo Nadir

Shah aliwatangazia Wafarsi. Hati hizi, na masimulizi ya tukio hilo yalipelekwa Istanbul na kukabidhiwa Khalifa.

Mtu huyu mnyonge (Hadhrat Abdullah Suwaydi mwenyewe) alitunzwa na mtukufu Khalifa kwa fadhila na zawadi nyingi, ambazo napaswa kukiri kuwa sitokuwa na uwezo wa kumlipa mtukufu huyo (deni la shukran anazostahikii) kwa ihsani yake, hadi kifo changu.

Sultan Mahmud I "rahmatullahi alaih" alizaliwa mwaka wa 1108 H., na akafariki dunia mwaka wa 1168 H. [1754 A.D.]. Alikuwa Khalifa mwaka 1143 H. [1730 A.D.]. Amezikwa kwenye makaburi yanayojulikana kama Valide Turhan Sultan, kando ya Yeni Camii '(Msikiti Mpya), huko Eminonu, Istanbul. Makaburini humu kuna (makaburi ya) Turhan Sultan na mwanawe, Mehmed IV, Mustafa II, Ahmad III, Osman (Uthman) III, na Murad V 'rehma za Allahu taala ziwashukie.

Toleo la asili la Kiarabu la kitabu kijulikanacho kama **Hujat Qat'iyya** mjini Istanbul mwaka 1400 [ 1980 A.D.].

## HILYA-I-SA'ADAT (PAMBO LA FURAHA)

[Hulka na sifa za mtume "**swallallahu alaihi wa sallam"**].

Maumbo ya viungo vyote vinayoonekana vya Bwana wetu, mtume, tabia zake mwenendo wake mzuri, maisha yake yote, pamoja na mazoea yake yote, yameandikwa kwa uwazi sana yakiambatanishwa na marejeleo ama vyanzo vyake.

Vitabu hivi vinajulikana kama vitabu vya siira. Kati ya maelfu ya vitabu vya siira, kile kilicho andikwa mwanzo kilikuwa kitabu cha Ibni Is-haqq kinachoitwa Sirati ur- Rasulillah, ambacho sherehe yake ilitolewa na Ibn Hisham Humayri na kikachapishwa na Westenfeld, mtaalamu wa Ujerumani. Allahu taala alimpa mtume Muhammad "swallallahu alaihi wa sallam" miujiza ambayo aliwapa manabii wote (Mitume). Miujiza mingi imeandikwa katika kitabu cha Kiarabu kijulikanacho kama **Al Mawahib-ul-Laduniyya** na kile cha Kifarsi kijulikanacho kama **Madarij-un-Nubuwwa** vingine ni **al-Anwar-ul-Muhammadiyya** (Kiarabu), ambao ni mukhtasar wa

**Mawahib** na **Hujjatullahi 'alal'alamin fi mu'jizati Sayyid-il-mursalin** (kwa Kiarabu).

Katika kijitabu hiki, tulifanya unukuzi kutoka kwenye kitabu chenye mijalada miwili ambacho kinaitwa **al-Mawahib-ul-laduniya** kilichoandikwa na Imam Ahmad Qastalani, mmoja wa wanazuoni wa kiislamu wa Misri. Abdulbaqi Efendi, mshairi wa kiislamu, alitafsiri kitabu hiki kutoka katika lugha ya Kiarabu kwenda kwenye lugha ya Kituruki. Kutokana na kitabu hicho, sehemu zilizochukuliwa kuwa muhimu kwa vijana zimeandikwa kwa mukhtasari kama ifuatavyo:

Uso wake wenye kheri, viungo vyote vilivyobarikiwa na sauti yenye kheri ya fahari kwa viumbe (Muhammad "swallallahu alaihi wa sallam") vilipendeza zaidi kuliko nyuso na miguu na sauti za watu wote. Uso wake uliobarikiwa ulikuwa wa umbo la duara. Alipokuwa katika hali ya uchangamfu, uso wake wenye kheri uling'ara kama mwezi. Ingeonekana wazi kwa kutazama paji la uso wake wenye kheri kwamba alikuwa amefurahi. Mtume "swallallahu alaihi wa sallam" alikuwa akiona wakati wa usiku jinsi alivyoona wakati wa mchana. Akiona nini kilichopo nyuma yake kama alivyoona yaliyokuwa mbele yake. Mamia ya visa vinavyothibitisha ukweli huu yameelezewa katika vitabu. Allahu taala, aliyejaalia neema ya kuona katika jicho ana nguvu za kuiumbia katika kiungo kingine neema hii ya kuona.

Alipoangalia upande mmoja au kutazama yale yanayomzunguka, hugeuka kwa mwili wake wote na kisha akaangalia. Aliangazia dunia zaidi kuliko alivyokuwa akiangazia angani. Macho yake yenye kheri yalikuwa makubwa. Nyusi zake zilizobarikiwa zilikuwa ndefu. Kulikuwa na kiasi fulani cha rangi nyekundu katika weupe ya macho yake yenye kheri. Mboni yake yenye baraka ilikuwa nyeusi sana. Fahari wa walimwengu alikuwa na paji pana. Kope zake zenye baraka zilikuwa nyembamba na zenye kuachana. Mshipa uliopo kati ya kope zake mbili ulivimba alipokuwa na hasira. Pua yake yenye kheri ilikuwa nzuri sana na ilikuwa juu kidogo katika sehemu ya kati. Kichwa chake chenye baraka kilikuwa kikubwa. Kinywa chake hakikuwa kidogo. Macho yake yalikuwa meupe. Meno yake ya mbele yalikuwa yameachana. Alipokuwa akielezea jambo, yalionekana kana kwamba nuru ilikuwa ikipenya kwenye meno yake. Miongoni mwa viumbe vya

Allahu taala, hakuna aliyewahi kutoa hotuba iliyo wazi zaidi na yenye utamu kuliko yake. Maneno yake yalieleweka kwa urahisi, huku yakifurahisha watu na kuzivutia roho. Alipokuwa akiongea, maneno yake yalivutia kama lulu. Kama mtu angejitokeza akitaka kuhesabu maneno yake, ingekuwa rahisi kuyahesabu. Wakati mwingine, angerudia jambo mara tatu ili liweze kueleweka vizuri. Peponi kila mtu atazungumza kama Bwana Muhammad. Sauti yake ikifika umbali ambao hakuna mtu mwingine angeweza kufikisha.

Fahari wa walimwengu "swallallahu alaihi wa sallam" alikuwa mchangamfu. Alikuwa akitabasamu kwa furaha. Alipokuwa akitabasamu, meno yake yalikuwa yakionekana. Akitabasamu, nuru yake ilikuwa ikitoa mwangaza kwenye kuta. Alikuwa akilia kiasi kama alivyokuwa akitabasamu. Kwa vile hakuwahi kucheka kwa sauti, hivyo hivyo hakulia kwa sauti kubwa, lakini macho yake yalitoa machozi na sauti ya kifua chake ikisikika. Alikuwa akilia machozi anapofikiria juu ya madhambi ya umma wake (yaani, Waislam), naye alikuwa akilia kwa kumcha Allahu taala. Pia alilia alipokuwa akiisikiliza Quran tukufu na wakati wa kusali.

Fakhari ya walimwengu "swallallahu alaihi wa sallam", vidole vyake vyenye baraka vilikuwa vikubwa. Mikono yake ilikuwa minene. Viganja vyake vilikuwa vipana. Harufu ya mwili wake ilikuwa ikinukia zaidi kuliko harufu ya manukato yanayosifika kwa uzuri. Mwili ulikuwa laini na wenye nguvu. Anas bin Malik anasema: "Nilimtumikia Rasulullah kwa miaka kumi. Mikono yake yenye kheri ilikuwa laini kuliko hariri. Jasho lake lilikuwa linatoa harufu nzuri zaidi kuliko manukato yanayonukia vizuri na pia kuliko maua yoyote. Mikono yake, miguu na vyanda vilikuwa virefu. Vidole vyake vilikuwa vikubwa. Uwazi uliokuwa kwenye mguu wake haukuinuka sana na ulikuwa laini. Mifupa ya mabega yake ilikuwa mikubwa. Kifua chake chenye baraka kilikuwa kipana, moyo wake wenye kheri ulikuwa nazargah-i ilahi.

Mtume wa Allahu taala rehma na salamu zimshukie hakuwa mrefu sana, wala mfupi. Mtu yoyote alipofika karibu naye, Mtume angeonekana kuwa mrefu kuliko mtu huyo. Akiwa amekaa, mabega yake hua juu kuliko ya wale wote waliokuwa wamekaa pamoja naye.

Nywele na ndevu zake hazikuwa zimepiga mawimbi sana, wala nyoofu sana, lakini zilikuwa zimepiga mapinde kutokana na jinsi

alivyoumbwa. Nywele zake zilikuwa ndefu. Awali alikuwa na masongo ya nywele upande wa mbele, baadaye akazitenganisha. Wakati mwingine alirefusha nywele zake na wakati mwingine alikuwa akizipunguza na kuzifupisha. Hakuweka rangi kwenye nywele na ndevu zake. Alipokufa mvi katika nywele na ndevu zake zilikuwa chini ya ishirini. Alikuwa akipunguza masharubu yake. Urefu na umbo la masharubu yake lilikuwa sawa na kope zake. Alikuwa na vinyozi wa binafsi waliokuwa wakimtumikia. [Ni sunna vilevile kwa waislamu kufuga ndevu zao na kuzirefusha kiasi cha kujaza ukufi na kupunguza masharubu yao].

Mtume "swallallahu alaihi wa sallam" daima alikuwa na mswaki wake na kitana chake. Alikuwa akitumia kioo wakati wa kuchana nywele na ndevu zake. Nyakati za usiku, alikuwa akiweka wanja kwenye vigubiko vyake.

Fakhari ya viumbe (Muhammad "swallallahu alaihi wa sallam") alikuwa na mazoea ya kutembea kwa haraka na kuangalia chini upande wake wa mbele. Akipita mahali fulani, alitambulika kwa harufu yake iliyonukia vizuri.

Fakhari ya walimwengu alikuwa na rangi nyeupe iliyochanganywa na nyekundu, na alikuwa mwenye jamali na umbo la kupendeza sana. Endapo mtu atathubutu kusema kwamba Mtume alikuwa muovu na sura mbaya na mweusi basi atakuwa muongo.

Yeye "swallallahu alaihi wa sallam" alikuwa Mwarabu. Katika kamusi neno Arab maana yake ni jamali. Kwa mfano, tamko *lisan al-Arab* lina maana ya lugha nzuri. Kijiografa, neno Mwarabu lina maana ya mtu aliyezaliwa kwenye rasi ya Uarabuni akakulia katika hali ya hewa ya huko ikiwa na maji yake na chakula na ambaye damu yake ni ya watu wa huko.

Kama ambavyo watu wa damu ya Anatolia wanaitwa Waturuki, watu waliozaliwa na kukulia nchini Bulgaria wanaitwa Wabulgaria na watu wa Ujerumani ni Wajerumani; hivyo basi, Mtume wa Allahu taala ni Muarabu kwa sababu alizaliwa Uarabuni.

Waarabu, wakati wa Mtume walikuwa weupe, wenye rangi ya mwanga. Familia ya Mtume wetu (Muhammad) hasa, ilikuwa yenye rangi nyeupe iliyopendeza sana. Kwa kweli, babu yake nabii Ibrahim alikuwa mwenye rangi nyeupe na alikuwa mwana wa muarabu

aliyeitwa Taruh, ambaye alikuwa mmojawapo wa wenyeji wa mji wa Basra. Azer, ambae alikuwa kafiri, hakuwa baba yake Ibrahim "alaihis-salaam" bali alikuwa mjomba na baba yake mdogo.

Umaarufu wa babaake 'Abdullah, ulikuwa umeenea hadi Misri kwa sababu ya uzuri wake na kwa sababu ya nuru kwenye paji la uso wake, wasichana takribani mia mbili walikuja Makka ili awaoe. Lakini nuru ya Bwana Muhammad ilimwangukia Amina.

Kwa muda wa karne moja, nchini Uturuki na katika nchi nyingi za kiislamu, usiku mtakatifu wa ‘Raghaib’ unajulikana kama usiku ambamo 'Abdullah alioa. Si sahihi kutoa maana kama hiyo kwa usiku wa ‘Raghaib’. Ingemaanisha kwamba Mtume aliitukuza dunia kwa kuwepo kwake kabla ya miezi tisa, jambo ambalo lina dosari. Kwa kuwa alikuwa mwenye hadhi ya juu kuliko watu wote katika kila hali, na kwa vile alikuwa mkamilifu katika kila namna, hivyo alikuwa mkamilifu vya kutosha wakati alipomuongoa mama yetu Amina. Dosari katika kipindi hiki cha ujauzito huchukuliwa kuwa dosari na upungufu katika sayansi ya tiba.

Usiku wa Ijumaa ya kwanza (usiku uliopo kati ya Alhamisi na Ijumaa) ya Rajab unaitwa usiku wa Raghaib, kwa vile Allahu taala anatoa raghibat, yaani baraka na zawadi kwa viumbe wanadamu usiku wote. Dua yoyote inayoombwa usiku huo itatakabaliwaliwa na vitendo vya ibada kama vile sala, kufunga na zaka, ujira wake utalipwa maradufu kuliko vile vinavyotendwa nyakati za kawaida.

Allahu taala atawasamehe wale wanaouheshimu usiku huo.

Katika zama za mwanzo za Uislamu na kabla ya Uislamu ilikuwa haramu kupigana vita katika miezi ya Rajab, Dhu'lqa'da, Dhu'lhijja na Muharram. Katika Riyad-un Nasihin sura ya pili aya ya nane katika Tafsir za Zahidi na Ali Jurjani na Tafsiri zote imeandikwa kwamba: “Kabla ya majilio ya Uislamu Waarabu walikuwa wakibadilisha sehemu ya miezi ili waweze kupigana vita katika miezi ya Rajab na Muharram kwa kuiweka mbele au nyuma.

Mtume "swallallahu alaihi wa sallam" alipokuwa akihiji hija yake ya kuwaaga akiwa na waislamu elf tisini katika mwaka wa kumi wa Hijra, alisema: “Enyi sahaba zangu! Tunahiji wakati wake (hasa wakati wa hija). Mwandama wa miezi ni kama ulivyokuwa wakati Allahu taala alipoumba”. Katika mwaka ambapo Abdullah alioa,

mahali pa miezi hiyo hapakuwa pa kweli, mwezi wa Rajab ulikuwa mahali pa Jumadal akhir. Yaani, ulikuwa mbele kwa mwezi mmoja. Hivyo basi, kipindi cha nuru yenye baraka iliyomtolea mwangaza mama yetu Amina kimo katika mwezi wa Jumadal akhir. Sio kwenye Usiku wa Raghaib.

Ami zake 'Abbas na mwanawe' Abdullah, rangi yao ilkuwa sawa na ile ya Mtume. Pia vizazi vya Mtume wetu vitakuwa na jamali na huruma mpaka mwisho wa dunia. Kwa mfano, Amir wa Jordan, marehemu 'Abdullah, aliyewahi kuja Istanbul, alikuwa mtu kama huyo. Ahmad Makki Efendi mja mwema, aliyekuwa mufti wa Kadikoy, alikuwa Sayyid (kizazi cha Mtume), na kama babu zake, alikuwa mwenye rangi nyeupe na kope nyeusi na macho makubwa meusi, mwingi wa huruma na bashasha. Sahaba zake Mtume walikuwa na huruma pia Bw. 'Uthman alikuwa mweupe mwenye nywele za rangi ya shaba. Dihya Kelbi, balozi ambaye Mtume alimtuma kwa Heraclius, mfalme wa Byzantine, alikuwa mzuri sana. Malaika Jibril mara nyingi alikuwa akijitokeza katika sura ya Dihya "radiyallahu anhu".

Lugha ya Kiarabu, lugha pekee ya elimu na ustaarabu katika enzi za kati na ambayo kwa kweli ni lugha iliyoendelea zaidi na ya kisasa kati ya lugha mia saba na sabini zinazozungumzwa ulimwenguni hivi leo na yenye utajiri katika sarufi ufasaha na fasihi iliingia na kutuama katika kila nchi pamoja na ustaarabu wa kiislamu. Katika nyakati hizo watu wa Ufaransa na Wazungu wengine ambao walijiunga na vyuo vikuu vya Kiarabu na shule za waislamu nchini Hispania kwa madhumuni ya kupata elimu, waliyapeleka maneno mengi ya Kiarabu, hasa maneno ya kiufundi yaliyotumiwa katika elimu na sayansi, katika nchi zao na kuyachanganya na lugha zao. Leo, katika lugha za Magharibi, maneno ya Kiarabu bado yanatumika.

Katika Injili ya lugha nyingi iliyochapishwa na British and Foreign Bible Society huko London mwaka wa 1947, kuna mistari michache iliyoandikwa kama vielelezo vya kila mojawapo ya lugha mia saba sabini.

Watu wa Misri wana rangi ya kahawia isiyoiva. Watu wa Ethiopia (Habashistan, al-Habasha) ni weusi na huitwa Habashi. Watu wa Zanzibar (Zain bar) wanaitwa Zain lenye maana ya uzuri, na pia ni weusi na walio changanya. Ni tendo la ibada kuwapenda na

kuwaheshimu jamaa zake Mtume, ambao ni Waarabu. Kila Muislamu anawapenda. Watu wote waliokuja Asia Ndogo kama wageni walijitambulisha kwetu kama Waarabu ili wapate kuheshimiwa na kuhurumiwa, hivyo waislamu wa Anatolia walikuwa wepesi kuwasadiki wakawaamini na kuwapenda. Hii ni kwa sababu watu weusi na weupe hawakubaguliwa katika rehma nzima ya upendo huu. Muislamu mweusi ni bora, huthaminiwa, na kupendwa zaidi kuliko kafiri mweupe. Kuwa mweusi hakupunguzi thamani ya imani kwa mtu yeyote. Baadhi ya sahaba za Mtume walikuwa weusi ingawa walikuwa Waarabu. Bw. Bilali al-Habashi na Usama kipenzi cha Mtume walikuwa weusi. Lakini makafiri kama vile Abu Lahab na Abu Jahl ambao uovu wao unajulikana na kila mtu walikuwa weupe. Allahu taala hamthamini mtu kwa rangi yake lakini humthamini kulingana na nguvu ya imani na uchamungu wake.

Hata hivyo, maadui wa Uislamu -Wayahudi- waliwatambulisha watu weusi kana kwamba walikuwa wa tabaka la chini na lisilopendeza.

Waliwafanya watumwa na walitaka kufuta upendo uliopo kati ya waislamu na kuuvunja udugu wao.

Kwa upande mwingine, kwa kuwaita wanyama wenye rangi nyeusi ‘Waarabu’ na kuwarejelea watu weusi kwenye picha, katuni na magazeti kama ‘Waarabu!’, walijaribu kuwahudhurisha Waarabu visivyo kuwa sahihi kwa vijana wetu ili kuwatenganisha watoto waislamu na mtume wetu "swallallahu alaihi wa sallam".

Leo, watu wanaoishi Uarabuni katika miji ya Makkat al-Mukarrama na Madinat al-Munawwara ni vizazi vya wageni waliokuja katika kipindi cha karne kadhaa kutoka Afrika, Asia na maeneo mengine na kuishi huko. Wageni hao walikuwa weusi na vipenzi vya Allahu taala na mtume "swallallahu alaihi wa sallam". Ayyuub Sabri Pasha "rahmatullahi alaih", mmoja wa wakuu wa jeshi la Sultan Abdulhamid Khan wa pili "rahmatullahi alaih", ameandika katika kitabu chake cha Kituruki chenye juzuu tano kiitwacho **Mir’a-ul-haramayn** kwamba katika jiji lote la Makka kuna familia za Waarabu mbili tu zilizobaki. Na leo hakuna waliobaki. Baada ya kifo cha Mtume, sahaba zake wote na vizazi vyake waliondoka Uarabuni kwa ajili ya jihadi, yaani ili kuueneza Uislamu duniani kote. Walisambaa katika Asia ya mbali, Afrika, Cyprus, Istanbul na kwa

ufupi kila mahali. Ili kufundisha dini ya Allahu taala kwa wanadamu, walipigana na kujitolea mhanga. Ardhi hii pana imejawa na mashahidi waliobarikiwa. Waliwapeleka vijana wao kwenye vituo vya Chuo Kikuu cha Baghdad ambacho kilikuwa wakati huo ndicho chuo kikubwa zaidi ulimwenguni kote na hayo yanaweza kushuhudiwa katika vitu vya kisanii vilivyobaki hadi sasa ambavyo walivifanyia majaribio na wakagundua mambo mengi mapya katika nyanja za fizikia, kemia, elimu ya sayari, jiografia na hisabati, ili waweze kupata elimu. Wakati Hulaghu, dhalimu mashuhuri, na mjukuu wa kafiri Genghis ambaye jina lake halisi ni Timüjin Khan, aliwatesa na kuwaua waislamu zaidi ya mia nane elfu wakiwemo wanawake na watoto akawachoma na kuiharibu Baghdad mwaka wa 656 H. (1258 A.D.) wale waliojificha katika visima na wale waliokimbilia Anatolia walinusurika. Kwa hiyo, vizazi vya Bwana wetu mtume "swallallahu alaihi wa sallam" na sahaba zake walipata makazi katika kila sehemu ya Anatolia, hususani sehemu ya Mashariki. Leo watu wenye akili, subira na bidii ya kusoma tunaowaita Wakurdi, wote ni vizazi vya watu hao. Kuna makundi mawili ya Wakurdi, mojawapo ya makundi hayo ni vizazi vya Yafethi, mwana wa tatu wa nabii Nuh. Kundi hili linajumuisha watu wafedhuli na wajinga ambao walikuja katika enzi za zamani Asia Ndogo kutoka sehemu za Asia ya kati na ambao wanaishi maisha ya kuhama hama. Mwanahistoria Xenophon, mwanafunzi wa Socrates, alieleleza kwamba aliwaona Wakurdi mashariki mwa Anatolia. Kundi la pili la watu wanaoitwa Wakurdi ni watu waliostaarabika na ambao ni wapole na wanaoishi mijini. Karibu wote ni vizazi vya Mtume wetu na sahaba zake. Kizazi cha Imam Hasan kinatambulika kwa jina la “Sharif” huku cha Imam Husayn kikitambulishwa kwa “Sayyid.” Katika enzi ya Waottoman (wana wa Uthuman), huko Aleppo kulikuwa na mahakama kubwa ya haki iliyohifadhiwa kwa Masayyid na Masharifu. Watu wa ukoo wao wote waliandikishwa huko na waongo hawakuweza kudai Usayyid. Mahakama iliondolewa na Mustafa Rashid Pasha, wakati wa mageuzi ya kisiasa yaitwayo Tanzimaat. Waislamu maarufu wa Irisan walioishi katika sehemu iliyoko kati ya Van na Hakkari, walikuwa wana wa makhalifa wa bani Abbas na idadi yao iliongezeka kutoka kwa mtoto mmoja aliyenusurika katika mauaji ya Hulaghu. Leo hii katika kila sehemu ya nchi yetu kuna vizazi vya

sahaba wa Mtume na masayyid. Tunapaswa kutambua thamani yao na kuwapa heshima wanayostahiki.

Mtume wa Allahu taala alikuwa na tabia nzuri sana. Aliyemjaalia tabia hiyo ni Allahu taala, si kwamba aliipata baadaye kwa kufanya bidii. Hakuwahi kumlaani mwislamu yeyote wala hakuwahi kumzaba kofi mtu yeyote. Hajapata kulipiza kisasi ili kuiridhisha nafsi yake. Alilipiza kisasi kwa ajili ya Allahu taala. Alikuwa akiwatendea wema jamaa zake, marafiki na watumishi. Alikuwa mpole sana na mwenye huruma nyumbani kwake. Alikuwa akiwatembelea wasiojiweza na kuhudhuria mazishi. Alikuwa akiwasaidia marafiki zake na kuwakalisha watoto wao kwenye paja lake. Pamoja na hayo, moyo wake haukushughulika nao. Roho yake ilikuwa katika dunia ya malaika.

Mtu ambaye angalimwona Mtume kwa ghafla angejawa khofu. Asingelikuwa mpole, hakuna mtu ambaye angalikaa karibu naye, hakuna mtu ambaye angalikuwa na nguvu za kumsikiliza kutokana na tabia zake za utume. Hata hivyo, yeye mwenyewe hakuweza kumtazama mtu yeyote kwenye uso kwa macho yake kutokana na kuona aibu.

Fakhari ya Uislamu "swallallahu alaihi wa sallam" alikuwa mtu mkarimu sana kuliko wanadamu wengine. Hajawahi kusikika akimwambia mtu aliyemwomba kitu, "Sina". Kama akiwa nacho kile alichoombwa hukitoa, kama hakuwa nacho basi hatoi jibu. Mtume alikuwa na sifa nyingi sana na alikuwa amewatendea wema watu wengi kiasi kwamba wafalme wakuu wa Byzantine na Mashah wa Ufursi hawakuweza kushindana naye. Aliishi katika hali kama hiyo kiasi ya kwamba hakuweza kukumbuka kula wala kunywa. Hakuwahi kutumia maneno kama "Lete chakula," au "Pika chakula fulani." Alikua akila wanapomletea chakula na alikuwa akikubali tunda lolote alilopewa. Wakati mwingine alikula kidogo katika kipindi cha miezi kadhaa na alipendelea njaa na wakati mwingine alikula sana. Alikuwa akila kwa vidole vitatu. Yeye hakunywa maji baada ya kula. Akinywa maji akiwa ameketi. Alipokuwa akila na watu wengine alikuwa akiacha kula baada ya kila mtu kumaliza. Alikuwa akikubali zawadi kutoka kwa mtu yeyote. Kama kiitikio kwa mtu aliyemletea zawadi, alikuwa akitoa zawadi zaidi sana.

Mnamo mwaka wa nane Hijria, siku ya Alhamisi tarehe ishirini Mwezi wa Ramadhani, Mtume wa Allahu taala pamoja na mashujaa

elfu kumi na mbili waliutwaa mji wa Makka baada ya kuondoka tarehe kumi Ramadani. Siku iliyofuata aliwasilisha khutuba akiwa amefunga kilemba cheusi kwenye kichwa chake. Baada ya kukaa Makka kwa siku kumi na nane alikwenda Hunayn. Alikuwa akiruhusu kikomo cha kilemba chake kuning'inia na alikuwa akisema, "Kilemba hiki hutofautisha kati ya waislamu na makafiri." Ilikuwa kawaida yake kuvaa nguo mbalimbali. Walipokuja mabalozi kutoka katika nchi za kigeni akijipamba. Yaani, akivaa nguo zenye thamani na nzuri na kuudhihirisha uso wake mzuri. Awali, alikuwa na pete ya dhahabu lakini baadaye alivaa pete ya fedha. Alitumia pete yake kama muhuri. Neno "Muhammadun Rasulullah" liliandikwa kwenye pete yake. Katika madhehebu yote manne hairuhusiwi kwa wanaume kuvaa pete za dhahabu. Kitanda chake kilikuwa cha ngozi kilichojazwa vipande vipande vya mti. Wakati mwingine alilala juu ya kitanda hiki na wakati mwingine juu ya ngozi iliyotandikwa chini, juu ya kitanda na wakati mwingine kwenye udongo mkavu. Alilalia upande wake wa kulia huku akiweka kiganja chake chini ya shavu lake la kulia.

Rasulullah "swallallahu alaihi wa sallam" hakukubali kuchukuwa zaka, na hakuwahi kula vitu kama vitunguu maji au vitunguu thomu, na hakusoma mashairi.

Rasul-i akram "swallallahu alaihi wa sallam" alizaliwa kwenye mji wa Makka, mnamo mwaka wa 571 A.D. usiku wa Jumatatu tarehe kumi na mbili mwezi wa Rabi'ul-awwal sawa na mwezi wa April. Kila mwaka waislam ulimwenguni wanasherekea usiku huu kama usiku wa Mawlid. Kila sehemu Rasulullah anakumbukwa kwa kusoma **Qasida za Mawlid**. Sultan wa Erbil, Abu Sa'id Muzaffarud-din Kukburi bin Zayuddin Ali alikuwa anaandaa sherehe na kutoa zawadi kwenye siku ya Mawlid. Tabia nzuri, huruma na vitendo vyema vya Sultan huyu vimeelezwa kwa upana katika kitabu cha historia kilichoandikwa na Ibn Khilligan, kwenye ukurasa 234 mlango **Hujjatullahi 'alal'alamin** na kwenye vipeperushi kwa jina **Mawlid-i sherif** kilichoandikwa na Sayyid Abdulhakim-i Arwasi. 'Mawlid' maana yake ni wakati wa kuzaliwa. 'Rabi'ul-awwal' maana yake ni majira ya masika. Siku hiyo ni siku ya furaha na sherehe. Alipewa jina lake **Muhammad** na babu yake **'Abdulmuttalib'**. Abdulmuttalib alipata ndoto kwamba jina Muhammad litaenea ulimwenguni kote na kwamba atasifiwa na kila mtu.

Jina Muhammad maana yake ni yule anaesifiwa sana. Kuja kwa Hadhrat Jibril mara ya kwanza kwake na kumjulisha kwamba amepewa utume, kuondoka kwake kutoka Makka kwenda kwenye kijiji Kuba cha Madinat al Munawwara (Hijira), kurudi kwake kuukomboa mji wa Makka na kifo chake vyote vilitokea siku ya Jumatatu. Wakati anazaliwa iligundulika kwamba kiunga mwana chake kilikuwa kisha katwa na alikuwa kisha tahiriwa. Inasemekana katika kitabu Zerkani cha **Mawahib**, wazazi wake; Hadhrat **Abdullah** na Hadhrat **Amina** wakati wanafunga ndoa, Abdullah alikuwa na umri wa miaka kumi na nane na Amina alikuwa na umri wa miaka kumi na nne. Hadhrat Amina alifariki dunia akiwa na miaka ishrini. Mwanzo alinyonyeshwa na mama yake kwa siku tisa, halafu akanyonyeshwa na **Thuwaiba** jariya wa Abu Lahab kwa siku kadhaa. Halafu alinyonyeshwa na **Halimatu Sa'diyya** kwa muda wa miaka miwili. Aliishi kwenye kijiji cha **Ban Sa'd bin Bakr** kwa muda wa miaka miwili tena alipokuwa na miaka minne aliletwa kwenye mji wa Makka.

Alipoanza kutembea alikuwa anawaangalia watoto wenzake wakicheza lakini hakujiunga nao. Alipokuwa na miaka sita, mama yake; Amina; alifariki dunia na alipokuwa na miaka nane, babu yake; Abd al-Muttalib; alifariki dunia. Alipokuwa na miaka ishrini na mitano, alimuoa Hadhrat Hadija 'radiyallahu anha'. Wakati ana miaka arubaini mnamo mwezi wa Ramadhani siku ya Jumatatu wakati yupo kwenye pango la mlima **Jabal-i-hira** na **Jabal-i-niir**, malaika Jibril alijitokeza na akambashiria kwa kumpa habari njema kwamba yeye ni nabii wa watu wote na majini.

Hadhrat Jibril alianza kuja kwake na kumpa utume kutoka kwa Allahu taala   pamoja na kitabu cha **Quran tukufu** kwa muda wa miaka ishirini na mitatu. JibrIl alijitokeza kwake mara laki mbili arubaini elfu ukilinganisha na mara kumi na mbili alizojitokeza mbele ya **Adama "alaihis-salaam",** mara hamsini kwa **Nuh** "alaihis-salaam", mara arubaini kwa **Ibrahim** "alaihis-salaam", mara mia nne kwa **Musa** (Moses) "alaihis-salaam" na mara kumi kwa **Issa** "alaihis-salaam".

Alipokuwa na umri wa miaka hamsini na mbili katika usiku wa ishirini na saba mwezi wa Rajab akiwa Makka, Jibril "alaihis-salaam" alijitokeza kwake na kumpeleka Masjidul Aqswa Yerusalemu akitokea Masjidul Haram badae akampeleka mbiguni kwenda

kwenye sidrati almuntahaa. Katika Miraj huko ndio alipewa sala tano za kila siku. Unaweza kusoma ukurasa wa mwisho wa mlango wa tano kwenye kitabu **Endless Bliss** (Furaha ya kudumu) toleo la pili.

Alipokuwa na miaka hamsini na mitatu, alihamia Madina kwa amri ya Allah. Aliacha nyumba yake asubuhi mapema siku ya Alhamisi tarehe ishirini na saba mwezi wa Safar. Alikuja nyumbani kwa Abu Bakr Siddiq alasiri. Baada ya muda mfupi yeye pamoja na Abu Bakr waliondoka. Walikwenda kwenye pango linalopatikana kwenye mlima **Thawr** kilomita tano na nusu kusini mwa Makka. Mlima huu una urefu wa mita 759 sawa na futi 2530. Walikaa kwenye pango hilo kwa muda wa siku tatu na waliondoka usiku wa Jumatatu.

Baada ya safari ya muda wa wiki waliwasili kwenye kijiji cha **Kuba** karibu na Madina siku ya Jumatatu, tarehe nane mwezi wa Rabi-ul-awwal, ambayo inalingana na tarehe ishirini mwezi wa Septemba. Imeandikwa katika kitabu cha Tafsir ya **Baydhawi** kwamba baada ya kukaa hapa hadi tarehe ishirini na tatu mwezi wa Septemba, waliondoka kuelekea Madina siku ya Ijumaa tarehe kumi na mbili mwezi wa Rabiul-awwal na waliwasili kwenye mji wa Madina siku hiyo hiyo. Baadae wakati wa utawala wa Umar alFaruq, siku ya mwezi wa Muharram wa mwaka huo, ikawa mwanzo wa kalenda ya kiislam ya **Hijri kamar**. Kulingana na wanahistoria siku ya mwanzo ilikuwa kwenye mwaka 622 A.D. Imeandikwa kwenye kitabu cha bwana Ahmad Ziya **Ilm-i Hey'at**, kilichochapishwa mwaka 1316 [1898 A.D.], kwamba ilikuwa sawa na siku ya Ijumaa tarehe kumi na sita mwezi wa saba. Mwanzo wa kalenda ya kiislam ni siku alipoingia kijiji cha Kuba ambapo ilikuwa tarehe 20 mwezi wa Septemba.

Alishiriki vita mara ishirini na saba, mara tisa alikwenda kama askari na mara nyengine alichukuwa nafasi ya kamanda mkuu. Alikuwa akitumia aina mbili za bendera kwenye vita vitakatifu, Raya yake ilikuwa nyeusi na Liwa yake ambayo ni ndogo zaidi kuliko Raya ilikuwa nyeupe. (**Raya** na **Liwa** ni bendera zilizokuwa zikipeperushwa vitani)

Alifariki dunia akiwa kwenye mji wa Madina mchana wa Jumatatu, Rabiul-awwal tarehe kumi na mbili mwaka 632 A.D. akiwa mwenye umri wa miaka 63. Bila kuvuliwa nguo zake,

alikoshwa na kuvalishwa sanda tatu na akazikwa kwenye sehemu ambako alifia.

Mtu anayemuona mtume kwenye ndoto yake, basi kweli anakuwa amemuona yeye kwa sababu shetani hawezi kujitia kwenye sura yake mtume.

Mtume alikuwa na watoto wa kiume watatu, wa kike wanne, wake kumi na moja, ami kumi na mmoja na shangazi sita. Mtume alioa mke wake wa kwanza akiwa na miaka ishirini na tano, alimuoa Khadija mwenye umri wa miaka arubaini na tano na alikuwa mjane. Lakini alikuwa mtu mwenye mali, mrembo, mwenye busara, heshima na elimu. Waliishi pamoja kwa muda wa miaka ishirini na tano, na alifariki dunia miaka mitatu kabla ya hijra katika mwezi wa Ramadhan kwenye mji wa Makka. Mtume hakuoa mke yeyote wakati Khadija yupo hai.

Ndoa yake mtume ya pili ilikuwa ya Hadhrat Aisha "radiyallahu anha", binti yake Abu Bakr, wakati ana umri wa miaka hamsini na miwili. Alifunga nae nikah mwaka mmoja baada ya kifo cha Khadija na aliishi naye kwa muda wa miaka nane hadi anakufa.

Alioa wake wengine wote baada ya kumuoa Hadhrat Aisha na alifanya hivyo kutokana na sababu aidha za kidini, kisiasa au huruma. Wanawake hawa wote walikuwa wajane pia walikuwa wazee. Kwa mfano, watu wa Makka walipozidisha mateso juu ya waumini, mtume aliliamrisha kundi moja kuhamia huko Habasha. Mfalme wa Habasha kipindi hicho akiitwa Najashi (Negus) alikuwa Mkristu lakini alikuwa mwenye elimu, hikma na huruma. Aliwauliza waislam maswali kadhaa, wakati wa kujibu maswali hayo alikuwa makini sana mpaka, aliridhika na majibu yao na akasilimu kama inavyotajwa katika riwaya mbali mbali.

Hata hivyo, Ubaydullah bin Jahsh kutokana na udhaifu wa iman yake, alikanusha Uislam na kubaki kwenye mila ya wazazi. Baadae alimlazimisha mke wake kuacha Uislamu lakini mke wake alikataa na kusema bora kufa kuliko kuachana na dini ya Mtume Muhammad "swallallahu alaihi wa sallam", na hatimae akamuacha. Na baada ya muda mfupi Ubaydullah bin Jahsh alifariki dunia.

Umm-i Habiiba alikuwa mtoto wa Abu Sufyan kiongozi wa ma Quraysh ndani ya mji wa Makka.

Starehe na neema za hapa duniani zote sio muhimu zikilinganishwa na habari hii njema. Nikaah yaani ndoa hii ni moja ya sababu ambazo zinachangia kumfanya Abu Sufyan 'radiyallahu anhu' kuheshimiwa na kuwa Muislam. Kama inavyoonekana hapa, hii nikahi sio tu inaonyesha ubaya wa makafiri, lakini pia inaonyesha kiwango cha hekima, akili, ujasiri, baraka na rehma za Mtume wa Allah.

Mfano mwingine ni ule wa Hadhrat Hafsa, binti wa Hadhrat Umar ambae alikuwa mjane. Katika mwaka wa tatu wa Hijra, Hadhrat Umar' aliwaambia 'Hadhrat Abu Bakr na Hadhrat' Uthman "radiyallahu anhuma", "Je, mutamuoa binti yangu?" kila mmoja wao akasema, "Nitafikiri juu ya jambo hili." Siku moja hao watatu na masahaba wengine walipokuwa pamoja, Rasulullah aliuliza, "**Ewe Umar! Kwa nini nakuona?** Kama ni rahisi kuona rangi ya wino ndani ya chupa?‘, hivyo Rasulullah kwa mtazamo wake wa kwanza alielewa mawazo ya kila mtu. Wakati mwingine alipoona kuwa ni lazima alikuwa anawauliza. Na hua ni lazima kusema ukweli kwa mtume hata na kwa watu wengine, Hadhrat Umar alijibu, "Ewe Rasulallah nilitamani binti yangu aolewe na Abu Bakr au na Uthman 'radiyallahu anhuma', lakini hawakukubali pendekezo langu la kumuoa binti yangu". Kwa sababu Rasulullah hakutaka hata mara moja kuumiza na kukasirisha wafuasi wake wapendwa, ili kumpendeza Umar hapo hapo Mtume alisema, "Ewe Umar! Je, ungependa binti yako kuolewa na mtu mzuri sana kuliko Abu Bakr na 'Uthman 'radiyallahu anhum'? Umar alishangaa. Kwa maana, alijua hakuna mtu alie bora zaidi kuliko Hadhrat Abu Bakr na Uthman. Kisha Umar akasema, "Naam, Ewe Rasulallah." Tena Rasullullah akasema, "Ewe Umar, nipe binti yako!" Kwa hivyo Hadhrat Hafsa akawa mama wa Abu Bakr, Uthman "radiyallahu anhuma" na waislam wote na wakawa watumishi wake, badaae Hadhrat Abu Bakr, Hadhrat Umar na Hadhrat' Uthman wakawa na urafiki na undugu wa karibu sana.

Mfano wa tatu, hebu tueleze kwa ufupi kwamba katika mwaka wa tano au sita wa Hijra, Juwayriyya, ambae alikuwa miongoni mwa mamia ya watumwa waliopatikana kutoka kabila la Banii Mustalaq, alikuwa ni binti wa Haris, mkuu wa kabila. Wakati Rasulullah alipo amua kumuacha huru na kumuoa, masahaba wote waliwaacha huru watumwa wao kutoka kabila hilo, na wakasema waliosema

"Tungeona aibu kuwatumia kama jariya na watumishi, jamaa za mke wa Rasulullah, mama yetu." Wote waliwaachia huru watumwa wao. Ndoa hii ilisababisha mamia ya wafungwa kuwa huru. Hadhrat Juwayriyya mara nyingi alitamka ukweli huu kwa kujivunia. Hadhrat 'Aisha alitamka na kusema, "Sikuona mwanamke mwenye heshima zaidi kuliko Juwayriyya."

Mfano wa nne ni ule wa Zaynab-bint-Huzeyma 'radiyallahu' anha'. Lakini kitabu chetu ni kidogo mno hakituruhusu kuandika mifano mingine. Mifano mitatu ya kwanza iliyotolewa inatosha kwa mtu mweye hekima, ufahamu wa haraka, na mwenye uwezo wa kutambua ukweli.

Pia tutaeleza ukweli kwamba ingawa Rasulullah alikuwa na nguvu zaidi kwa kila namna ukilinganisha na wanaume wengine, aliishi tu na wake zake tisa. Na alidumu katika hali hio kwa miaka michache. Na katika miaka hio alikuwa daima akifanya kazi na alishiriki kwenye vita. Siku alizokaa nyumbani zilikuwa chache sana. “nikah” ni (ndoa kwa namna iliyowekwa na Uislam)." Wakati alipoingia peponi katika usiku wa Miraj (kupanda kwake mbinguni), Rasulullah kamwe hakuwaangalia “hurlain” wake ndani ya pepo. Lakini moja ya maadui wa Uislamu, walitoa kashfa chafu ambayo haina msingi kwamba mtume alioa Hadhrat Zainab alipokwenda Miraj. Baadae, alipokea barua ya hongera kutoka kwa Papa, ambae alikuwa adui wake.

Ukweli huu umeandikwa katika **Kamus-ul-a'lam**. Chini ya kipengele cha **Zaynab**.

Katika tafsiri ya **Mawahib-i Ladunniyya**, kwenye ukurasa wa 459, imeandikwa: "Rasulullah "alaihis-salaam" alimpa Zaynab ambae ni binti wa shangazi yake ili afunge ndoa na Zayd. Baada ya muda mrefu, Zayd alisema kuwa alitaka kumtaliki mkewe. Alipoulizwa '**Kwa nini?**' Alisema, Sijaona jambo baya ndani yake, na siku zote nimeridhika na vitendo vyake vyote. Lakini, daima ananikumbusha mimi heshima yake na anajivunia na ukoo wake.' Rasulullah akamwambia Zayd, 'Hayo maneno sio muhimu katika ndoa yako. 'Usimuache mkeo kwa sababu hizo.' Hata hivyo, Allahu taala alimzuia kuepuka talaka hii. Kwa hivyo Zayd alimuacha (talaka) Zaynab na Allahu taala alimruhusu Rasulullah kumuoa Zaynab. Daud ''alaihis-salaam" 'alikuwa na wake mia moja na jariya mia tatu. Sulaiman "alaihis-salaam" alikuwa na wake mia tatu na

jariya mia saba. Lakini mtu aitwae “Voltaire” ambae ni muongo na mshawishi kwa kuzusha fitna katika Uislam, hakuzungumzia kuhusu ndoa za manabii hawa watakatifu, lakini akasema uongo juu ya Rasulullah kulingana na wake aliooa ambayo ilikuwa ni amri kutoka kwa Allah kutekeleza amri hii ilikuwa ni wajibu kwa Mtume.

Moja ya sababu muhimu kwa nini Rasulullah alioa wake kadhaa ilikuwa kufundisha Uislam. Kwa mfano, kabla Aya ya Hijab kuteremshwa, yaani, kabla ya wanawake kuamrishwa kujifunika, wanawake walikuwa wanakuja kwa Rasulullah kuuliza na kujifunza Uislam. Wakati Rasulullah "alaihis-salaam" alienda nyumbani kwa mmoja wao, wote walikuwa wanakuja na kukaa, na kusikiliza na kujifunza kutoka kwa Rasulullah. Lakini, baada ya aya ya Hijab, ikawa marufuku kwa wanawake na wanaume wasiokuwa mahaarim kukaa pamoja na kuzungumza, baada ya hapo Rasulullah hakuwaruhusu wanawake wasiokuwa mahram kuja kwake na kuuliza maswali. **Aliamuru** wanawake wote kuuliza na kujifunza Uislam **kutoka kwa mke wake** Hadhrat **'Aisha. Kulikuwa** na wana**wake** wengi vile na **maswali** mengi sana yaliulizwa kwa **Hadhrat** 'Aisha na kwa hivyo hakuweza kuyajibu yote.

**Ili** kufanya **kazi hii muhimu** iwe nyepesi, na **kupunguza uzito** kwa **Hadhrat 'Aisha**, Rasulullah alioa wake wengi. Akisaidiwa na wakewe waliobarikiwa, Rasulullah aliweza kuwasilisha ujumbe maridadi kuhusu wanawake kwenda kwa mamia ya wanawake wa Kiislamu.

Na kama angebaki na mke mmoja, ingekuwa vigumu, na haingewezekana, kwa **wanawake** wote **kujifunza kutoka kwa mke moja**.]

Rasulullah alikuwa ummi, yaani, alikuwa hawezi kusoma vitabu, hakufundishwa kuandika, wala hakupokea masomo kutoka kwa mtu yeyote. Rasulullah alizaliwa Makka na akakulia huko, alilelewa na watu tofauti, na licha ya kuwa hakusafiri sana katika ujana wake, alisimulia habari kutoka kwenye Taurat kuhusu matukio kadhaa (kitabu cha Hadithi za Musa), vile katika Injil, na katika vitabu vilivyoandikwa wakati wa karne za Gregory na Kirumi. Na ili kufundisha Uislam, alituma barua kwa waislam tofauti. Katika mwaka wa sita badaa ya Hijra, alituma barua kwa watawala wa Byzantine, Irani, na Abyssini na kwa wafalme wengine wa Kiarabu. Mtawala wa Irani (shah) Khosrow Parviz aliichana barua vipande

vipande, na akamuua sahaba ambae alikuwa amempelekea barua hio. Muda mfupi baada ya hayo, aliuliwa na mwanawe aitwaye Shfruya.

Majina ya Muhammad "swallallahu alaihi wa sallam" yaliandikwa katika Taurat na Injil. Wayahudi na Wakristo walimsubiri kwa hamu, hali ya kudhani kwamba atakuwa muyahudi ili wazidi kupata heshima ulimwenguni. Lakini alipo kuja, Wayahudi na Wakristo walikuwa na choyo na walimkataa, kwa sababu alitoka kwa Waarabu na hakutokea katika makabila yao. Hata hivyo, idadi kubwa ya wenye hekima walikuwa na busara ya kutosha kumuamini Muhammad "swallallahu alaihi wa sallam". Hata hivyo kukataa kwa mayahudi unabii wake au kushindwa kuutambua ukoo wake na ubora wake hautazuia thamani na heshima zake.

Allahu taala anasema katika Surah Al-Inshirah "**nimeunyanyua utajo wako/ yaani kukupa umaarufu na kusifika kwa utukufu wako**," ili jina lako litakuwa limeambatanishwa pamoja na jina langu kila mahali. Kila muda mwanzo wa wakati wa sala (maombi) huadhiniwa na kutajwa pamoja jina la mtume na la Allahu taala.

Mtu yeyote hawezi kuwa Muislamu halisi ila mpaka amfuate Rasulullah katika kila kitu anachofanya. Na imani yake haitakuwa kamili isipokuwa atakapo mpenda sana Rasulullah kuliko maisha yake mwenyewe.

Rasulullah yeye ni mtume wa watu wote na majini. Kwa hivyo ni wajibu kwa kila taifa kila karne kumfuata mpaka siku ya wisho.

Kila Muislam anapaswa kusaidia dini yake, kufuata tabia zake, kutaja jina lake la heshima mara nyingi, kumuombea sala na salam kwa ajili ya heshima na kwa upendo wakati wowote anaposema au kusikia jina lake lililobarikiwa.

Muislamu anapaswa kumpenda kwa upendo wa dhati, na kuiheshimu **Qurani** na Uislam, ambayo aliteremshiwa mtume Muhamadi swalah na salamu ziwe juu yake.

Kitabu **Mir'at-i Kainat** kinasema: "Watu wajinga na wavivu huandika maandishi ya awali (kama vile SAW) badala ya "swallallahu alaihi wa sallam".' Hii haikubaliki. Tunapaswa kuepuka hili kwa makini."

Imeelezwa kuhusu sala katika kitab cha **Ibni Abidin** kwamba "Ni fardhi kusema (rehma fulani) **Salawat** (hutamkwa kama baraka juu

ya nafsi yake mtume wetu) mara moja katika maisha ya mtu. Ni wajibu kusema "swallallahu alaihi wa sallam" kila mara moja kwa mtu anayesema, anayesikia, anayesoma au anaandika (jina lake la kheri) kwa mara ya kwanza, na ni mustahab kutamka hii baraka wakati wowote jina lake la kheri (la Mtukufu mtume) linaporudiwa."

## DINI YA UYAHUDI (JUDAISM) NA WAYAHUDI

Uchunguzi wa vitabu vitakatifu, ushahidi wa kihistoria na kazi zilizopatikana hadi zama zetu hizi unatuonyesha kwamba dini ambayo inaamrisha watu kumuamini Allah kuwa ni mmoja ni Uislam. Itambulike ya kwamba Uislam ulikuepo tangu enzi za mtume Adam "alaihis-salaam". Baada ya kuumbwa na kuanza kuishi ardhini, ingawa mitume wengi "alaihis-salaam" walipewa vitabu katika kipindi kati ya Hadhrat Adam na Hadhrat Abraham (Ibrahim "alaihis-salaam"), hawakupewa vitabu vikubwa. Allahu taala aliwatumia viijtabu vidogo vinavyoitwa "**Suhuf**." Suhuf hizi zilikuwa mia moja, kumi kati yake aliteremshiwa Ibrahim "alaihis-salaam".

Kulingana na wanahistoria, Ibrahim "alaihis-salaam" alizaliwa miaka 2122 kabla ya Issa "alaihis-salaam" kuzaliwa kwenye mji uliopo kati kati ya Mto Euphrates na Mto Tigris. Kama ilivyoelezwa awali, alifariki dunia baada ya kuishi miaka 175 kwenye mji unaoitwa "**Hulflurra-man**" karibu na Yerusalemu. Kulingana na kitabu **La Bible a Dit Vrai** (Bibilia tukufu inasema ukweli) kilichochapishwa na muandishi Marston, hivi karibuni miliki zilizokuwa za Hadhrat Ibrahim zimekutwa kwenye sehemu hizo. Hivyo, ni ukweli kwamba aliishi kwenye enzi zilizotajwa hapo juu. Baba wa kambo wake akiitwa **Azar na** baba yake mzazi akiitwa **Tarih** naye alikufa wakati Ibrahim bado mdogo. Azer alikuwa msanii na mshuhulukiaji wa sanamu. Wakati Ibrahim "alaihis-salaam" akiwa bado mtoto alijua kwamba sanamu hazipaswi kuabudiwa. Aliyavunja masanamu ambayo yalishughulikiwa na baba wa kambo wake vipande vipande na akaanza kujadiliana kwa hoja nzito juu ya uhalali wa kuabudu masanamu hayo na mkuu wa nchi yao, ambaye

ni Nimrod, mfalme wa Babel (Babylon). Nimrod alikuwa mtawala jeuri ambae hana huruma. Kama inavyosimuliwa, Nimrodi halikuwa jina lake halisi, ilikuwa lakabu tu kama Fir'aun. Nimrod wakati bado mdogo, kinyoka kidogo kilimuingia kwenye pua yake na kumsababisha kuwa na sura mbaya sana. Alikuwa mbaya sana kiasi kwamba baba yake alikuwa hawezi kuuangalia uso wake mbaya. Hatimae, aliamuwa kumuua. Lakini kutokana na maombi ya mama yake, hakuuliwa. Badala yake alisalimishwa kwa mchungaji. Mchungaji nae kwa kuwa hakumudu kuutazama uso wake mbaya naye pia alimtupa sehemu fulani kwenye mlima.

Chui ambae kwa maana ya lugha yao lilikuwa ni Nimrod alimuokoa mtoto kutokana na kufa njaa kwa kumnyonyesha. Jina Nimrod linatokana na chui. Baada ya kifo cha baba yake, Nimrod alimrithi ufalme wake na akajiita Mungu na aliwataka watu wamuabudu. Mtu huyu jeuri aliitwa na Ibrahim "alaihis-salaam" kwenye dini ya kweli. Ibrahim pia alijaribu kuwazuia watu kutokuabudu masanamu na Nimrod. Lakini hawakuwacha tabia hii waliendelea nayo. Watu wa Chaldean walikuwa na utamaduni wa kukusanyika pamoja kwenye sherehe za kila mwaka. Na walikuwa wanakwenda kwenye majumba ya masanamu na kusujudu mbele ya masanamu hayo. Baada ya sherehe wanarudi nyumbani kwao. Siku moja katika siku za sherehe, Ibrahim "alaihis-salaam" alikwenda kwenye chumba cha masanamu na kayavunja masanamu madogo yote kwa kutumia shoka. Halafu baadae akakimbia na kuliacha shoka kwenye shingo ya sanamu kubwa. Wakati watu wa Chaldean wanaigia chumba cha masanamu, walikuta masanamu madogo yote yamevunjwa. Walitaka kumkamata mtu alievunja masanamu yao ili wamuadhibu. Walimleta Ibrahim "alaihis-salaam" na wakamuuliza kama ndio yeye aliefanya kitendo hicho. Ibrahim "alaihis-salaam" alijiibu, "nadhani sanamu kubwa lenye shoka ndio limefanya hivyo kwa sababu halikutaka wengine nao kuabudiwa. Lakini kwa nini hamuliulizi sanamu kubwa?" Walimjibu," je! inakuwaje ukataka sisi tuliulize sanamu na unajua kwamba sanamu haliwezi kuongea?" sasa kutokana na majibu yao hayo akawajengea hoja, na kuwauliza suala la kimantiki, "sasa kwa nini mnaabudu masanamu ambayo hayawezi kuongea na hayawezi kujilinda wala kujitetea dhidi ya kuvunjwa? Ni aibu kubwa kwenu kwa kuabudu vitu dhaifu kiasi

hichi! Baada ya hapo aliwataka watu hao waache kuabudu masanamu. Lakini jaribio lake halikufanikiwa. Ukweli huu unaelezwa kuanzia sura ya hamsini na mbili na kuendelea. Waliripoti tukio hilo kwa Nimrod. Nimrod alitaka kumuona Ibrahim "alaihis-salaam". Alipokuwa mbele ya Nimrod, hakumsujudia. Nimrod alipomuuliza kwa nini hakumsujudia, alimjibu, "Namsujudia Allahu taala pekee, ambae aliniumba." Nimrod hakuwa na uwezo wa kukataa ushahidi uliotolewa na Ibrahim "alaihis-salaam". Ibrahim "alaihis-salaam" alipomuambia kwamba Allah ni mmoja, mwenye uwezo na wa milele na kwamba Nimrod sio kitu chochote zaidi ya kuwa binadam, Nimrod alikasirika sana. Baada ya kuhimizwa na wafuasi wake, aliamua kumkusanyia kuni na kumtupa Ibrahim "alaihis-salaam" kwenye moto ili amuadhibu adhabu kali zaidi ya kumuunguza akiwa hai. Ukweli huu umeandikwa katika Quran tukufu Suratul-Baqarah aya: 259 "**Je, hukumuona yule aliyehojiana na Ibrahimu juu ya Mola wake kwa sababu Allahu taala alimpa ufalme? Ibrahimu aliposema: Mola wangu ni yule ambaye huhuisha na hufisha, yeye akasema: Mimi pia nahuisha na kufisha. Ibrahimu akasema: Hakika Allahu taala hulileta jua toka mashariki, basi wewe ulilete toka magharibi, ndipo akafedheheka yule aliyekufuru, na Allahu taala hawaongozi watu wadhalimu**. Sura As-Saaffat aya: 98-99 "**Wakasema: Mjengeeni jengo kisha mtupeni motoni. Basi walitaka kumfanyia hila, lakini tukawafanya kuwa wadhalilifu**. Kama inavyosemwa, moto uligeuka na kuwa bwawa lenye samaki wengi. Samaki waliumbwa kutokana na kuni. Ukweli huu unatangazwa katika Quran al-kerim Sura Al-Anbiyaa aya: 69-70 "**Wakasema: Mchomeni ili muwasaidie miungu wenu, ikiwa nyinyi ni mnaweza kufanya hivo. Tukasema: Ewe Moto, uwe baridi na chanzo cha amani kwa ajili ya Ibrahimu**."

Jina Nimrod halikutajwa katika Quran al-kerim, lakin jina hilo lipo katika Torah ("Agano la kale" sehemu ya Bibilia). Leo kuna bwawa linaloitwa "Ayn-i Zalfka" au "Halilurrahman." Ni bwawa lenye upana wa mita za mraba hamsini kwa thelathini kwenye mji wa Urfa. Bwawa hili linachukuliwa kupatikana kwenye sehemu inayosemekana kuwa Hadhrat Ibrahim alitupwa kwenye moto, na inaaminiwa kuwa ndiyo sehemu ambayo samaki waliumbwa kutokana na kuni.

Hadhrat Ibrahim alioa mara mbili. Ingawa mke wake wa kwanza Sarah alikuwa na miaka sabini hakuwa na mtoto. Kutokana na hili, hadhrat Ibrahim alioa jariya anaeitwa Hajar ambae alipewa kama zawadi na Pharaoh (mfalme) wa Misri. Alipata mtoto kutoka kwake anaeitwa Ismael. Kwa sababu hio Sarah nae alimuomba Allahu taala ampatie mtoto. Allahu taala alimpa mtoto na akamuita Ishaq. Ismail na Ishaq salam ziwe juu yao ndio mababu wa Warabu na Wayahudi. Tunaweza kusema kwamba Warabu na Wayahudi ni ndugu wanaotoka kwenye baba mmoja lakini mama tofauti. Ibrahim ndio moja ya babu zake mtume Muhammad "alaihis-salaam".

Ibrahim "alaihis-salaam" alipata utume wakati ana umri wa miaka tisini. Alifundisha dini ya tawhid (upweke wa Mungu). Maana ya aya ya sitini na saba ya Sura Aali-Imran kwenye Quran tukufu ni: "**Ibrahim sio myahudi wala sio mkirisito. Yeye ni "hanif" maana yake ni mtu ambaye amefuata ukweli, na "Muislam" maana yake yule ambaye kajisalimisha kwake**."

Mtume aliewasilisha misingi ya uyahudi ni Hadhrat Musa. Musa "alaihis-salaam" ziwe juu yake alizaliwa miaka 1705 kabla ya Issa "alaihis-salaam" ziwe juu yake kuzaliwa kwenye mji wa Mempis, Misri.

Kwa kuwa kuna hadithi tofauti kuhusu tarehe ya kuzaliwa kwake, haijulikani vizuri mfalme gani aliekuwa anatawala Misri kipindi hicho. na kwa kuwa Pharaoh alipata ndoto kwamba mtoto wa kiume atakaezaliwa kwenye mwaka huo atakuwa sababu ya kuangamizwa kwa ufalme wake, alitoa amri kwa wanajeshi wake kuua watoto wa kiume wote waliozaliwa katika mwaka huo.

Allah akamuamrisha mama yake amuweke kwenye sanduku na kumuacha kwenye Mto Nile, na kumuomba Allahu taala kumlinda. Sanduku lililokuwa limebeba mtoto liliokotwa na "**Asiya**" mke wake Pharaoh. Pharaoh nae alimuona mtoto. Lakini wakati Pharaoh na mke wake walipoona sanduku kwenye mto waliambizana kwamba: "kilichopo kwenye sanduku kikiwa kiumbe hai atakichukuwa mke wake na kama ni mali itakuwa yake. Wakakubaliana hivyo." Na kwa kuwa alikubali wazo hilo hakumuumiza mtoto.

Jina la Musa maana yake ni "kuokolewa kutoka kwenye maji." Wakristo wanamuita Moses.

Mama wa Musa aliajiriwa kwenye jumba la ufalme wa Pharaoh kama mnyonyeshaji wa mtoto. Matokeo yake, alikuwa na uwezo wa kumlea mwanawe. Alipotimiza umri wa miaka thelathini alipata habari kwamba alikuwa na jamaa zake nje ya jumba la ufalme. Aliondoka kwenye jumba la ufalme na kuwatafuta jamaa zake ili kuishi nao. Alikutana na kaka yake Harun "alaihis-salaam" ambae alikuwa mdogo kuliko yeye kwa umri wa miaka mitatu. Musa "alaihis-salaam" aliandamana dhidi ya Pharaoh baada ya kumuona akiwatesa wayahudi. Musa "alaihis-salaam" alijitahidi kuwalinda. Siku moja kafir mmoja Mmisri alikuwa anamtesa Myahudi, lakini Musa "alaihis-salaam" alipokuwa anajaribu kumuokoa Myahudi, yule Mmisiri alifariki dunia. Kwa kweli Musa "alaihis-salaam" alitaka kuzuia mateso tu dhidi ya Wayahudi. Alilazimika kuihama nchi ya Misir. Alikwenda kwenye mji wa **Madyana**. Huko alimtumikia Shu'aib "alaihis-salaam" kwa muda wa miaka kumi na hilo lilikuwa ni sharti au makubaliano ya kumuozesha binti yake. Alimuozesha binti yake Safurar (Tsippore).

Baada ya kutimiza miaka kumi, Musa "alaihis-salaam" alirudi Misri. Wakati anarudi, aliona moto kwenye mlima wa Tur na akaufuata. Huko alisikia neno la Allahu taala. Wakati huo, alipewa risalat (utume) na ujumbe usemao kwamba Allahu taala ni mmoja, na kwamba Pharaoh sio mungu na mengine mengi aliyoteremshiwa.

Halafu alikwenda kwa Pharaoh kule Misri. Alimlingania juu ya kumwamini Mungu mmoja. Na alitaka uhuru wa Bani Israel (watoto wa Israel), lakini Pharaoh alikataa na alikasirika sana. Alisema "Musa ni mchawi mkubwa. Anataka kuchukuwa uongozi wa nchi yetu kwa kutumia hila zake." Halafu akawauliza washauri wake mtazamo wao. Walimshauri wakisema, "kusanyeni wachawi. Waambieni washindane nae Musa." Wachawi walikusanywa, na wakazi wa Misri walikusanyika kushuhudia kinachoendelea. Wachawi walitupa kamba zao chini. Kamba zote zikageuka kuwa nyoka na kuanza kumuelekea Musa "alaihis-salaam". Lakini Musa "alaihis-salaam" alipo tupa bakora aliyokuwa nayo mkononi mwake iligeuka kuwa nyoka mkubwa mwenye kutisha na kuanza kumeza wale nyoka wengine wote. Kutokana na miujiza hio wachawi walimuamini Musa na kusema:"Mtu huyu anayoyasema ni ukweli."

Tukio hili limetajwa ndani ya Quran tukufu Suratul Aaraf aya 111-123. Kisha, Pharaoh aliendelea kukasirika sana. Alisema, "huyu alikuwa mwalimu wenu sio? Nitakata mikono yenu na miguu yenu. kisha nikutundikeni kwenye matawi ya mitende." Walimjibu "Tumemuamini Musa. Tunataka kuwa chini ya ulinzi wa Mungu wake. Tunataka rehma zake na kutusamehe." Pharaoh alikataa kuwaachilia Bani Israel. Na kama angaliwaachilia angewakosa watu ambao walikuwa watumishi wake.

Na muujiza mwengine ni ule wa maji yaliotumika na makafiri yaligeuka na kuwa damu. Chura walitoka chini na kujazana kila sehemu. Ugonjwa wa ngozi na giza la siku tatu liliikumba nchi ya misri. Pharaoh alishituka baada ya kuona miujiza hii na akawaruhusu kuondoka. Wakati Musa "alaihis-salaam" na Bani Israel wanaondoka kuelekea Yerusalemu, Pharaoh alihuzunika sana. Pamoja na jeshi lake kubwa akaamua kuwafuata na alikuwa na nia ya kuwaua wayahudi wote. Wayahudi walipofika Red Sea, bahari hio iliwaruhusu kuvuka. Nabii Musa alimuomba Allah taala awape nusra kutokana na pharaoh na baada tu ya kumaliza dua yake bahari ilijifungua yenyewe na wakaweza kupita wana wa israail.

Na pale Pharaoh pamoja na jeshi lake walipo jaribu kuingia kwenye ufimbi wa bahari nyekundu ili kuwafukuzia wayahudi, bahari ilijifunga na kusababisha Pharaoh na jeshi lake kuangamia. Wakati wa kuhama Musa "alaihis-salaam" alimuomba Allahu taala kujitokeza akiwa Mlima Tur. Ombi lake halikukubaliwa na Allahu taala. Lakini, alizungumza nae tena kwenye Mlima Sinai. Musa "alaihis-salaam" alikaa kwenye Mlima Sinai kwa muda wa siku arubaini na usiku arubaini na akafunga. Allahu taala alimtumia kitabu kinachoitwa Torah (Taurat) kupitia malaika Jibril "alaihis-salaam", kitabu hicho kilikuwa kimeandikwa kwenye mbao. Mwanzo alikuwa ameshapewa amri kumi kufuatwa na wafuasi wake. Amri kumi hizo (**Awamir-i ashara**) zimo kwenye vitabu vya wayahudi. Zinaanza na aya ya mwisho wa sura ya tano ya kitabu cha kumbukumbu la Torati, na kumazilika na mwanzo wa sura ya ishirini kwenye kitabu cha Safari. Ziko kama ifuatavyo:

1. Mimi ni Bwana Mungu wako aliyekutoa kutoka nchi ya Misri kutoka kwenye nyumba ya utumwa.

2. Hamtakuwa na Mungu mwengine mbele yangu. Msiwafanye masanamu wa kuchonga au mfano wowote wa kitu kilichopo juu mbinguni, au kilicho chini ya ardhi, au kilicho ndani ya maji chini ya ardhi kuwa miungu yenu.

3. usitaje jina la Bwana Mungu wako bure bila sababu kama kuapa kiholela.

4. Itakase siku ya Sabato. Siku sita utafanya kazi, na fanya kazi zako zote. Lakini siku ya saba ndio Sabato ya Bwana Mungu wako. Usifanye kazi yoyote katika siku hiyo.

5. Mheshimu baba yako na mama yako.

6. Usiue.

7. Wala usizini.

8. Wala usiibe.

9. Wala usitoe ushahidi wa uongo dhidi ya jirani yako.

10. Wala usimtamani mke wa jirani yako, wala usitamani nyumba ya jirani, shamba lake, mtumishi wake, au mjakazi wake, au ng’ombe wake, au punda wake au kitu chochote ambacho kinamilikiwa na jirani yako.

Musa "alaihis-salaam" aliporudi kutoka Mlima Sinai, aliwakuta watu ambao aliwaacha chini ya ulinzi wa kaka yake Harun "alaihis-salaam", wamepotea na kutoka kwenye njia sahihi na kuanza kuabudu sanamu lililokuwa kwenye sura ya ndama alietengenezwa kutokana na dhahabu. Na hapo alimshika ndugu yake Harun kwa nini aliwaruhusu kuabudu sanamu? lakini alimjibu kwamba nilijitahidi kuwanasihi ila hawakunisikiliza baada ya hapo akawatenganisha waovu na wema. Musa "alaihis-salaam" alikuwa kiongozi mwenye busara. Alikuwa na athari kubwa juu ya watu alioishi nao. alipokuwa na mwaka mmoja tu, alimfanya Pharaoh kukasirika sana kwa sababu alichezea ndevu zake zilizokuwa zimepambwa kwa lulu. Alitaka kumuua, lakini mke wake Asia, aliingilia kati na kumpa mtihani wa kumjaribu akili zake. Alipewa tende na moto kwenye sahani ili achaguwe moja kati yake, aliponyanyua mkono wake kuchukua tende Jibril "alaihis-salaam" aliugeuza mkono wake na kuchukua moto. Alipotia moto kwenye mdomo wake, ulimi wake uliungua na akatupa moto. Ndio sababu alikuwa hazungumzi kwa utaratibu na ufasaha wa lugha yao, na ndio sababu alimtaka kaka yake Harun "alaihis-salaam" kuwa

karibu nae kwa sababu yeye alikuwa anasema kwa ufasaha. Musa "alaihis-salaam" alipowakuta watu wake wakiwa wamepoteza muelekeo alirudi tena kwenye Mlima Tur na kumuomba Allahu taala kuwasamehe watu wake. Watu wake walikua wamemuahidi kutorudia tena kosa la kumshirikisha Allah na kitu chengine. Alianza kuwaongoza kuelekea jangwani akiwa anatafuta **Arz-i mew'ud** (nchi alioahidiwa), ambayo aliwaahidi Allahu taala. Walikaa kwenye Jangwa la Tih kwa muda wa miaka arubaini. Wakiwa katika jangwa Allahu taala aliwalisha manna na salwa (nyama ya kwale).

Musa "alaihis-salaam" aliweza kusogelea kilima cha Ne'bo karibu na mji wa Ariha kutoka sehemu ambayo Arz-i mew'ud inaonekana. Aliishi hapo hadi kifo chake alipokuwa na umri wa miaka 120 kama inavyosemwa. Na alimchagua nabii Yusha kuwaongoza watoto wa Israel kuelekea Arz-i mew'ud. Kaka yake Harun "alaihis-salaam" alikuwa ameshakufa miaka mitatu kabla yake. Nabii Yusha ndie aliyewaongoza hadi ardhi ya "Ariha" inayoitwa Arz-i mew'ud.

Mwana historia na mwana habari mkubwa Ahmad Jawdat Pasha katika kitabu chake "**Qisas-i Anbiya**" anaeleza: "mtoto wa Hadhrat Ishaq alikuwa Hadhrat Ya'qub (Jacob). Jina lake asili lilikuwa "**Israel**." Watu kutoka kwenye kizazi chake wanaitwa "**Banu Israel**", maana yake "**watoto wa Israel**." Yusuf (Joseph) "alaihis-salaam" alikuwa mtoto wa Yaquub (Jacob) wa kumi na mbili, nae pia alikuwa nabii. Baada ya Yusuf "alaihis-salaam", watoto wa Israel walifuata sheria ya Yaquub na Yusuf alaihim salam, na waliishi Misr.

Kabila la "Kibt" ndio wakaazi wa mwanzo wa Misr. Walikua wakiabudu nyota na masanamu. Waliwafikiria wa Israel kuwa watumwa. Watoto wa Israel walitamani kuhama waende kwenye sehemu inayoitwa "Canaan" (Kan'an) ambayo ilikuwa nchi ya baba zao. Lakini Pharaoh hakuwaruhusu kwenda. Waliwalazimisha wa Israel kufanya kazi ngumu kama kujenga miji mipya na majengo. Daima walikuwa na ndoto ya kutoroka ukatili wa Pharaoh.

Kitabu **Mir'at-i-Kainat** kinasema "Musa "alaihis-salaam" alikwenda kwenye Mlima Tur mara tatu. Mara ya kwanza, alipewa risalat (unabi). Mara ya pili alipewa kitabu "Torah" (**Taurat**) na **Awamir-i ashara** (amri kumi). Taurat ilikuwa kwenye vipande arubaini. Kila kipande kilikuwa na sura elfu moja. Palikuwepo na aya elfu moja katika kila sura. Taurat ya sasa haina aya nyingi. Na

sababu ni kwamba, kama Quran tukufu inavyoeleza, Taurat na Bibilia vilibadilishwa na watu baadae.

Taurat ilioteremshwa na malaika Jibril "alaihis-salaam" kwa Musa "alaihis-salaam", kitabu hicho kilikaririwa na Musa, Harun, Yusha, Uzair na Issa "alaihis-salaam". Kitabu **Kamus-ul Alam** kinasema "Buhtunnasar wa Assyria alipoikamata Yerusalemu, alizichoma moto nakala zote za Taurat. Zaidi ya hayo, aliwateka watu sabini elfu miongoni mwao ni wanazuoni wa kiyahudi, akiwemo Daniel na Uzair "alaihis-salaam", na kuwasindikiza Babylon. Ukweli ni kwamba Uzair "alaihis-salaam" alikuwa anaitwa Ezra na wayahudi umeandikwa katika kitabu "**Munjid**." Hata hivyo, kitabu cha Ezra na baadhi ya vitabu vilivyomo kwenye agano la kale ya Bibilia takatifu ya leo, sio Uzair "alaihis-salaam".

Mtu anayeitwa Ezra alikuwa mchuganji wa kiyahudi. Wayahudi waliikataa Taurat na kuwa waovu. Hawakuwaamini mitume walio teremshiwa kwao. Waliwaua wengi wa manabii hawa. Bahman Khosrow, Shah wa Iran, aliwashinda wa Assyrian, na kuwachilia huru mateka wa kiyahudi, akiwemo Daniel "alaihis-salaam".

Idadi ya watu wanaoabudu kwenye msikiti wa Aqsa iliongezeka. Alexander the Great alipoukamata mji wa Jerusalemu, mtu wa kiume kutoka Jerusalemu kwa jina "Herodas" alipewa ugavana wa mji wa Jerusalemu. Governor mbaya huyu alimuua Yahya "alaihis-salaam". Alitesa sana watu. Baadae, mji wa Jerusalemu ulitekwa na watu wa kiroma. Mwaka wa 135 wa enzi za ukristu, baada ya wayahudi kuandamana, Adrian aliuteketeza mji wa Jerusalemu na kuwaua watu wa kabila la kiyahudi. Wayahudi walioweza kutoroka walikwenda sehemu mbalimbali, lakini hata hivyo walidhulumiwa na waliteswa sana na wakrisito.

Dini ya Uislam ilipotokea, walipata amani na utulivu.

Mji wa Jerusalemu ulirejeshwa na watawala wa kirumi na kupewa jina "**Ilia**" (Ilya). Mji wa Jerusalemu ulijengwa upya na Khalifa wa tano wa ummawi anayeitwa Abdulmalik bin Marwan. Mji huo uliharibiwa tena na wakrisito kwenye vita vya msalaba. Salahuddin aliukomboa tena. Makhalifa wa uongozi wa kiottoman waliukarabati na kuupamba mji huu.

Kitabu takatifu baada ya Taurat kilikuwa **Talmud**. Musa "alaihis-salaam" aliwafundisha Harun, Yusha na al-Ya'azar aliyoyasikia

kutoka kwa Allahu taala kwenye Mlima Tur. Maneno hayo yaliwasilishwa kwa manabii waliofuata baadae na hatimaye alifundishwa Yahuda Wakati wa karne ya pili ya zama za kikristo, maneno hayo yaliandikwa na kuwa kitabu kwa usaidizi wa Yahuda mtakatifu kwa muda wa miaka arubaini. Kitabu hiki kiliitwa **Mishna**. Maelezo ya aina mbili yaliandikwa kwenye **Mishna** wakati wa karne ya tatu na ya sita zama za kikrisito, kwenye mji wa Jerusalemu na mji wa Babylon kwa pamoja. Maelezo haya yalipewa jina la **Gamara**. Kila moja ya Gamara mbili hizi ilikusanywa na kuwekwa kwenye kitabu pamoja na **Mishna** na kupewa jina "**Talmud**." Talmud yenye Gamara ilioandikwa kwenye mji wa Jerusalemu pamoja na Mishna inaitwa **Talmud ya Yerusalemu**. Nyengine yenye Gamara ilioandikiwa kwenye mji wa Babylon pamoja na Mishna inaitwa **Talmud ya Babylon**. Wakristo ni maadui wa vitabu hivi vitatu. Wakristo wanaamini kwamba mtu aliyefundisha Mishna alikuwa Sham’un, ambae alibeba msalaba uliotumika kusulubiwa Issa. Baadhi ya maagizo hatari kwa watu yanayopatikana katika Talmud yameandikwa kwenye mwisho wa kitabu chetu cha kituruki "**Cevab Veremedi**," ambacho kimetafsiriwa kwa lugha ya kingereza na kuchapishwa kwa jina "**Could Not Answer**." Ukweli kwamba jina lilotajwa hapo juu "Al-Ya'azar" alikuwa mtoto wa Shuayb "alaihis-salaam" umeandikwa katika kitabu **Mir’at-i Kainat**. Bibilia takatifu ya wakrisito ina vipande viwili "Agano la Kale" na "Agano Jipya." Agano la Kale pekee ndicho kinachoaminiwa na Wayahudi kuwa Kitabu Kitakatifu. Hawapendi wazo la kuita kifungu hiki Agano la Kale. Wanapenda kiitwe "Torah." Wanasema "Torah" ina vipande vitatu. Kipande cha kwanza kinaitwa "Taurat. Taurat ina vipande vitano:

1. Mwanzo
2. Kutoka
3. Mambo ya Walawi
4. Hesabu
5. Kumbukumbu la Torati

Vitabu vitano hivi kwa ujumla vinaitwa: Pentateuch (vitabu vya sheria). Aya ya pili ya sura Isra katika Quran tukufu, hii imetangazwa "**Tumempa Musa Kitabu**." Lakini baada ya miaka maandishi ya kigeni yalianza kuingizwa kwenye Torah za sasa. Kwa hiyo, hakuna

uhusiano kati ya Torah aliyopewa Musa "alaihis-salaam" na Tora ya leo.

Ukweli ni kwamba Allahu taala atatuma nabii wa mwisho anayeitwa Muhammad "alaihis-salaam" imeandikwa kwenye Torah ya awali. Wakati Musa "alaihis-salaam" alipokwenda mlimani Tur kwa mara ya pili kuomba msamaha kwa ajili ya watu wake waliokua wamepotea, majibu aliyopewa na Allahu taala yameandikwa katika aya 156-158 ya sura Al-Aaraf: "**Na Musa akawachagua watu sabini katika kaumu yake kwa ajili ya miadi Yetu, na lilipowashika tetemeko la nchi akasema `Mola wangu, kama Ungetaka Ungaliwaangamiza wao na mimi zamani. Je, Utatuangamiza kwa sababu ya yale waliyofanya wapumbavu kati yetu? Sio haya ila ni majaribio Yako, kwa hivyo Humpoteza Umtakaye na Kumuongoza Umtakaye. Wewe ndie Mlinzi wetu, basi tusamehe na Uturehemu, nawe ndie Mbora wa kusamehe. Na Utuandikie mema katika dunia hii na katika Akhera, bila shaka tumeelekea Kwako`. Akasema: Adhabu Yangu Nitamfikishia Nimtakaye, na rehma Yangu imeenea kwenye kila kitu, basi Nitaiandika kwa ajili ya wale wanaoniogopa na kutoa Zaka na wale wanaoziamini Aya Zetu, Ambao wanamfuata Mtume, nabii asiejua kusoma wala kuandika, ambae wao humkuta ameandikwa kwao katika Taurati na Injili, Huwaamuru yaliyo mema na huwakataza yaliyo mabaya, na huwahalalishia vitu vizuri na huwaharimishia vitu vibaya, na huwaondolea mizigo yao na minyororo iliyokuwa juu yao. Ama wale waliomuamini yeye na kumheshimu na kumsaidia na wakaifuata nuru iliyoteremshwa pamoja naye, hao ndio wenye kufaulu**.

Na hakuna shaka kwamba Wayahudi walimuamini nabii wa mwisho na walimsubiri kutokea. Zaidi ya hayo, inasemwa katika tafsiri zengine kwamba wakati wa vita Wayahudi walikuwa wanaomba, wakisema "Ewe Mola wetu! Kwa ajili ya mtume wako wa mwisho ambae uliahidi kutuma, tafadhali tusaidie." Na walikuwa wanashinda vita kwa dua hiyo.

Hadhrat Daud na Hadhrat Sulaiman walikuwa miongoni mwa mitume waliotumwa kwa wayahudi baada ya Musa "alaihis-salaam" na walijitahidi kueneza dini ya ukweli. Tunaweza kuelezea dini ya kiyahudi kama ifuatavyo:

**Imani**: Kuna Mungu mmoja. Yeye ni mwenyewe, kuwepo uhai na umauti unatoka kwake. Anaona na anajua kila kitu. Hajazaliwa na hana mtoto, kusamehe na kuadhibu vipo chini ya nguvu zake.

**Maadili**: Misingi ya maadili yao ni amri kumi, tuseme, Awamiri ashara, watu wanafaa kushikamana na amri kumi hizo kama zilivyo. Roho na mwili wa wanadamu ni tofauti. Roho haina kifo hadi siku ya kiama. Ni muhimu kuamini maisha ya kiroho ya ulimwengu wa pili.

**Misingi ya Kidini**: Wasio Wayahudi wanaonekana kuabudu masanamu. Ni muhimu kukaa mbali nao. Ni muhimu kujitenga nao kwa kadiri iwezekanavyo. Ni muhimu kutoa sadaka ya damu au bila damu. Wanaadhibu kulingana na sheria za kisasi. Mtu mwenye kutenda dhambi huhukumiwa kutokana na kitendo chake. Watoto wa kiume wanatahiriwa kutokana na amri ya Rabbi. Wanyama wanaoliwa wanapaswa kuchinjwa. Nyama ya mnyama aliekufa bila kuchinjwa hailiwi. [Hata leo, Marekani na Ulaya kwenye bucha za wayahudi kuna ishara yenye muhuri "kosher", kuwashiria kwamba nyama inayouzwa hapa imechinjwa kulingana na sheria zilizoelezwa na Rabbi. Wayahudi wanakula nyama iliyoandaliwa kwa njia hii pekee. Waislamu wanakula nyama iliyochinjwa baada ya kutamka jina la Allahu taala. Waislamu hawali nyama ya nguruwe]. Wanawake wakiyahudi wanapaswa kufunika vichwa vyao baada ya kuolewa.

Leo, wanawake wakiyahudi wanaoishi Ulaya wanatekeleza amri hii kwa kuvaa wigi. Pia ni marufuku kwa Wayahudi kula nyama ya nguruwe.

Vitendo vya kuabudu vya Wayahudi kuna sherehe tofauti. Jumamosi ni siku yao takatifu. Hawafanyi kazi au hata kuwasha moto katika siku hiyo. Jumamosi huchukuliwa kuwa sikukuu na wanazisherekea, wanaiita "Sabatah". Zaidi ya hii, wana baadhi ya sikukuu nyingine kama, Pasaka, Shaw-wat, Rosh-ha-Shanah, Kepur, Sukkot, Purem, Hanuqa na kadhalika. Pasaka inachukuliwa kuwa kumbukumbu ya kuondoka kwao kutoka Misr. Shawwat inasemwa kuwa sherehe ya waridi, ambayo inachukuliwa kusherehekea kuteremshwa kwa Torah na Awamir-i Ashara. Kepur ni sherehe kuu, inayochukuliwa kuwa siku waliosamehewa baada ya kutubu. Sukkot ni sherehe ya maskani, inachukuliwa kuwa kumbukumbu ya maisha ya jangwa. Tofauti na padri, Rabbi hana mamlaka ya

kusikiliza maungamo. Wanatekeleza tu sherehe za ibada. Mbele ya Allahu taala wayahudi wote wako sawa, hakuna tofauti kati ya mmoja kwa mwengine.

Baada ya Hadhrat Musa, idadi ya sherehe za kidini na namna Rabbi wanavyozitekeleza ilibadilishwa au kanuni mpya ziliongezwa na manabii tofauti.

Baada ya Hadhrat Daud, waliongeza kusoma kitabu cha zaburi kwa kuambatanisha na muziki. Daud "alaihis-salaam" alizaliwa miaka elfu moja kabla ya Issa "alaihis-salaam" kuzaliwa.

Daud "alaihis-salaam" alikuwa mchungaji. Kwa kuwa alikuwa mwenye sauti ya kuvutia, alipelekwa kwa mkuu wa nchi Talut. Kwa miaka thelathini alimuua Goliath, ambae alikuwa mtu mkubwa sana, na watu wakampenda sana. Lakini Talut alitahadharishwa na akaanza kukaa mbali na Daud "alaihis-salaam". Hata hivyo, baada ya Talut kufariki dunia, kulingana na maombi ya watu, Daud "alaihis-salaam" alikuwa mrithi wake. Ndio wa mwanzo kuamrisha Jerusalemu kuwa mji mkuu.

Utawala wa Daud "alaihis-salaam" ulidumu kwa muda wa miaka arubaini. Ukweli ni kwamba alipewa kitabu cha Zabur umeandikwa kwenye aya ya 164 ya Sura An-Nisaa na aya ya 56 ya Sura Al-Isra katika Quran tukufu. Ni kweli kwamba Daud "alaihis-salaam" alimuomba Allahu taala rehma na msamaha.

Katika Zaburi ya leo, kwenye Bibilia, kuna nyaraka za uongo ambazo zimeongezwa. Kwa sababu ya maongezeko haya, imepoteza asili yake kabisa. Allahu taala alimpa Daud "alaihis-salaam" neema nyingi.

Maana ya aya ya 11 ya Sura Saba: **"Na kwa hakika Tulimpa Daudi fadhili kutoka Kwetu, enyi milima nyenyekeeni pamoja nae, na ndege (pia) na tukamlainishia chuma."** Na maana za aya ya 18-20 za Sura Sad: **"... E Muhammad! umkumbuke Mtumishi Wetu Daudi, mtu mwenye nguvu za kila aina, kwa yakini yeye alikuwa kila mara mwenye kumwelekea Allahu taala. Hakika sisi tuliitiisha milima kwake. Wakasherehekea kumtukuza Allahu taala pamoja naye jioni na asubuhi. Na Tuliwaitisha kwake ndege wakiwa wamekusanywa pamoja. Wote walimwelekea yeye.**"

Na maana ya aya ya 26 ya Sura Sad **"Mbele yetu Daud ni mwenye cheo cha juu na mahali pazuri."**

Hadithi mbaya ilioandikwa katika Taurat ya leo na Bibilia inayosema "Tukio kati ya mja na kamanda wake mke wa Uria kwa jina Bathseba" sio kweli. Hadhrat Ali "radiyallahu anhu", khalifa wa nne alitangaza kwamba atampiga bakora 160 yule ambae ataeneza uongo huo. Tafsiri ya aya ya 26 ya Sura Sad ilioandikwa katika kitabu cha tafsiri **Ma-wakib** ni "Urya alituma ujumbe kwa msichana anayeitwa Teshama kumueleza kwamba anataka kumuoa. Ingawa msichana alikubali, watu wake walikataa. Walitaja sifa mbaya mbele ya msichana. Wakati huo huo, Daud "alaihis-salaam" pia alitaka kumuoa Teshama. Baada ya Urya kufa kwenye vita, msichana aliolewa na Daud "alaihis-salaam". Hata hivyo, Allahu taala hakutaka jambo hili kwa sababu ya ukweli kwamba Teshama alikuwa kasha poswa. Daud "alaihis-salaam" baada ya kuelewa kwamba kafanya kosa, alitubu na Allahu taala alimsamehe." Hakuna ushahidi wa wazi kuhusu kisa hiki ndani ya Quran tukufu. Hata hivyo, ilielezwa kwamba Hadhrat Daud alikuwa mcha Mungu, alipewa elimu ya Sayansi na uwezo wa kutofautisha ukweli na uongo. Kwenye aya ya 25 ya Sura Sad, inasemwa kwamba alimsujudia Allahu taala na kumuomba busara ya kuhukumu kesi ya kondoo, mara kwa mara akimuomba Allahu taala rehma, na alikuwa anaswali sana. Wanazuoni wa kiislamu kwa ujumla wanakubaliana kwamba kisa cha Urya kiliongezwa kwenye Taurat na Bibilia baadae. Ingawa hadithi hizi za uzushi zinazoitwa "**Israeleyyat**" zimewaathiri waislam wasio na elimu, wanazuoni wa kiislam walitoa tamko kwa pamoja kwamba ni simulizi.

Sulaiman "alaihis-salaam" mtoto wa Daud "alaihis-salaam" alimrithi baba yake na kuwa nabii na kiongozi wa watoto wa Israel. Alikuwa na uwezo wa kuzungumza na majini, wanyama pori na ndege. Kipindi cha Sulaiman "alaihis-salaam" ndio bora zaidi kwa watoto wa Israel. Hadi enzi za Sulaiman "alaihis-salaam" viongozi wa Wayahudi hawakujua thamani ya jumba la ufalme. Nyumba ya Talut ilipotajwa hapo awali haikuwa na tofauti na nyumba ya mkulima wa kawaida. Ndio yeye kwa mara ya kwanza kuanzisha mji wa Jerusalemu na kujenga jumba la ufalme huko. Alikuwa na majengo mengi, vyumba vya ufalme, mabustani, mabwawa, sehemu za kuchinjia, na sehemu za ibada zilijengwa. Jina la hekalu lake kuu sana lililojengwa kwenye mji wa Jerusalemu ni Masjid-i Aqsa (Bayt-i Muqaddas). Aliwaalika wasanifu wa Foenician kujenga

msikiti huu. Na viumbe viitwavyo "jinn" walifanya kazi wakati wa ujenzi. Vifaa vya ujenzi vilivyotumiwa katika ujenzi huu vilikuwa vya thamani sana. Ukiangaliwa kwa mbali ulionekana kama kipande cha dhahabu yenye kung'a. Ujenzi ulidumu kwa miaka saba. Kwa bahati mbaya, msikiti huu mzuri ulichomwa na Nebukadreza II (Buhtunnasar), mfalme wa pili wa Assyrian (Waashuru) alipouteka mji wa Jerusalemu. Hata hivyo, Khosrow aliutengeneza, baadae wa Roma nao waliuchoma tena.

Inaelezwa kwenye kitabu **Kamus-ul Alam**, "Baada ya janga hilo, ukarabati, wa ujenzi na uboreshaji ndani ya Jerusalemu hayakufanyika tena na Waisrael.

Baadaye watawala wa Byzantine walitengeneza msikiti wa Aqsa na kuiita jina Jerusalemu. Mtume wetu "alaihis-salaam" aliwahi kuswalia kwenye Masjid-i Aqsa.

Mji wa Jerusalemu ulitekwa na Waislamu mnamo karne ya 16, wakati wa utawala wa Hadhrat Umar 'radiyallahu anhu'. Msikiti uliopo sasa ulijengwa wakati wa utawala wa Abdulmalik bin Marwani "rahmatullahi-alaih". Msingi wa ukuta uliobaki unaitwa "Ukuta wa kulia" na wayahudi wa sasa, nao huomba mbele ya ukuta huu. Wakati wa enzi za Sulaiman "alaihis-salaam" mji wa Jerusalemu ulikuwa mji bora na tajiri zaidi duniani. Hadithi zisizohesabika zimesimuliwa kwa watu kuhusu majumba ya kifalme yaliojengwa na Sulaiman "alaihis-salaam" kwenye mji wa Jerusalemu, na kuhusu vyumba vilivyo ndani na mapambo ya thamani yaliyotumika kupamba.

Inaweza kusemwa kwamba hadi leo, hakuna mfalme aliyeweza kuishi maisha ya kifahari kama Sulaiman "alaihis-salaam". Sulaiman "alaihis-salaam" alikuwa na wanawake wengi pamoja na masuria. Kwa kuwa alijishugulisha na biashara alikuwa anatajirika zaidi kila wakati. Ng'ombe thelathini, kondoo mia moja, dazeni za kalungu na paa walikuwa wanachinjwa kila siku ndani ya jumba la ufalme wake. Sulaiman "alaihis-salaam" kila wakati alikuwa analinda amani na kuanzisha urafiki na uhusiano na majirani wake. Alimuoa binti wa Pharaoh ambae ni jirani yake zaidi pia alimuoa Balkis, Malkia wa Sheba na kumwita kwenye dini ya ukweli. Alipanua urafiki wake kwake, na kulingana na wanahistoria wa kiislam, nae pia alimuoa.

Ukweli kwamba Balkis aliitwa kwenye dini ya ukweli na Sulaiman "alaihis-salaam" umeandikwa kwenye aya ya 30-33 ya Sura An-Naml katika Quran tukufu. Sulaiman "alaihis-salaam" alikuwa huru sana kama manabii wengine "alaihis-salaam". "Mahakama ya Solomon" imechukuliwa kama mfano wa haki ulimwenguni kote, na hio ya Umar "radiyallahu anhu". Sulaiman "alaihis-salaam" alivumilia imani nyengine. Licha ya maandamano yaliyofanywa na Wayahudi wenye shauku, alikubali hekalu za dini nyengine kujengwa pia. Hivyo, alipewa heshima kote duniani na kuwa mfano mzuri. Aliendeleza sheria za baba yake Daud "alaihis-salaam". Kuhusu Sulaiman "alaihis-salaam" imeandikwa katika Quran tukufu. Maana ya aya ya 13 ya Sura Saba ni "**Na kwa Sulaimani Tukauitiisha upepo uliokwenda safari yake ya asubuhi mwendo wa mwezi mmoja na safari yake ya jioni mwendo wa mwezi mmoja na Tukamtiririshia chemchem katika shaba. Na katika majinni kulikuwa na waliofanya kazi mbele yake kwa idhini ya Mola wake na kila anayejitenga na amri Yetu miongoni mwao Tunamuonjesha adhabu ya Moto uwakao**." Na maana ya aya 31-40 ya Sura Sad ni: "**Na Tukampa Daudi, Sulaimani, aliyekuwa mtu mwema bila shaka alikuwa mnyenyekevu mno. (Kumbukeni) alipopelekewa jioni farasi walio kimya wasimamapo, wepesi wakimbiapo. Basi akasema `Mapenzi ya farasi ni ya tunu kwangu kwa sababu wananikumbusha kuhusu Mola wangu`. Kwa hiyo aliketi mpaka walipofichika nyuma ya pazia. Warudisheni kwangu, na akaanza kuwapangusa miguu yao na shingo zao. Na hakika Tulimjaribu Sulaimani na Tukauweka mwili juu ya kiti chake, kisha akaelekea kwa mola wake. Akasema `Ee Mola wangu, Unisamehe na Unipe ufalme ambao hataupata yoyote asiyestahili baada yangu. Bila shaka Wewe Ndie mtoaji`. Basi Tukamtiishia upepo ukaenda pole pole kwa amri yake anakotaka kufika. Pia mashetani kila ajengaye na azamiliaye. Na wengine wafungwao minyororoni. Hiki ndicho kipawa Chetu bila ya hesabu, basi fanya ihsani au zuia. Na kwa yakini alikuwa mbele Yetu mwenye cheo cha kukaribiana na mahali pazuri**." Kulingana na uchapishaji wa Wayahudi na Wakristu, sehemu tatu za Bibilia ilioko mikononi mwao imenukuliwa kutoka kwenye kitabu cha Solomon "alaihis-salaam". Hivi ni "Mithali, Mhubiri na Wimbo Ulio Bora." Inasemekana katika Taurat kwamba upepo, ndege na

wanyama wengine walikuwa kwenye milki ya Sulaiman "alaihis-salaam". Alikuwa na uwezo wa kuzungumza lugha zao. Ndege na wanyama wengine walikuwa wanafanya kile walichoamrishwa kufanya kwa haraka. Ujenzi tofauti ulikamilishwa kwenye muda mfupi kwa usaidizi wa majini waliokuwa chini ya amri yake.

Wakati wa enzi za Sulaiman "alaihis-salaam", watu walipewa haki za kiraia sana kuliko wakati wa Daud "alaihis-salaam". Kulingana na sheria mpya baba alikuwa na haki nyingi juu ya mtoto wake. Mtoto, bila kujali umri wake, alipaswa kutimiza maagizo ya baba yake. Mgao wa urithi kwa mtoto mkubwa ulikuwa maradufu. Kwa masuala yanayohusiana na ndoa au ushirikiano watu maarufu katika familia walipewa mamlaka. Wahusika walipaswa kukubali wale waliochaguliwa kwao. Mwanamke aliyeachwa alikuwa anapewa baadhi ya fedha zinazoitwa "**mahr**." Mjane mwenye mtoto au bila mtoto alipaswa kuolewa na shemeji wake. Mtoto wa kwanza baada ya ndoa hi alihukumiwa kuwa mtoto wa marehemu. Kwa hiyo, mtoto ndio alikuwa mrithi wa marehemu. Mwanamme alipewa idhini ya kuoa zaidi ya mwanamke mmoja. Baada ya Sulaiman "alaihis-salaam" kuondoka duniani, waisrael waligawanyika katika makabila kumi na mbili, ambao walipigana wenyewe kwa wenyewe. Mgawanyiko huu ulianza kabla ya kifo cha Sulaiman "alaihis-salaam". Lakini kwa usaidizi wa Allahu taala, Sulaiman alaihsalam aliweza kuwaunganisha pamoja. Rehoboam, mtoto wake Sulaiman "alaihis-salaam" aliibuka mrithi wake. Lakini kabila mbili kati ya kumi na mbili walimfuata. Nchi ya Israel iligawanyika vipande viwili. Moja yake ilipewa jina la "**Israel**" na makabila kumi waliishi humo. Makabila mawili yaliyobakia yaliunda nchi inayoitwa "**Yahuda**." Uongozi huu ndio ulioongoza mji wa Jerusalemu. Hatimaye, walipoteza maadili yao. Allahu taala alikuwa na hasira nao na kuwaadhibu. Waliishi kwa muda chini ya uongozi wa Assyrian. Mnamo mwaka wa 587 B.C (kabla Yesu kuzaliwa) kiongozi wa Assyrian Buhtunnasar aliharibu na kuchoma mji wa Jerusalemu. Kwa nguvu, aliwafukuza kutoka kwenye mji wa Jerusalemu na kuelekea Babylon. Lakini baada ya Khosrow Shaha wa Iran kuwashinda wa Assyrian, aliwaruhusu wa Israel kurudi Jerusalemu. Walijaribu kuukarabati mji wa Jerusalemu ambao ulikuwa umechomwa. Mwanzo waliishi chini ya uongozi wa Iran na baadae chini ya Macedoniya. Warumi waliingia mjini Jerusalemu

mnamo mwaka 64 B.C. waliuharibu na kuuchoma mji tena. Warumi waliuharibu tena mji wa Jerusalemu mwaka 70 A.D. Alikuwa Titus, malikia wa Warumi ambae aliuchoma mji wa Jerusalemu hadi chini ya ardhi bustani na mazao.

Wakati wa Israel wapo chini ya uongozi wa Warumi, Issa "alaihis-salaam" alizaliwa. Wakati wa siku za majanga hizo, Tourah asili iliharibiwa. Baadhi ya vitabu vipya viliandikwa na kupewa jina Tourah. Ndio sababu Allahu taala alimtuma Issa "alaihis-salaam" kama nabii kuwaongoza waisraeli kurudi kwenye njia sahihi. Waisrael hawakutaka kumkubali Issa "alaihis-salaam" kama nabii. Walikuwa wanamsuburi mtume sawa sawa kama yule alielezwa ndani ya Tourah. Walifikiri kwamba atakuwa mtume mwenye nguvu sana, mwenye ujasiri sana na kwamba angefanikiwa kufanya chochote alichotaka, na kwamba wataokolewa kutoka kwa mikono ya Warumi kwa msaada wa mtume huyu. Walipomuona Issa "alaihis-salaam" akiwa mtu mpole, hawakumtaka. Walifikiri ni nabii wa uongo. Walimtukana mama yake, Hadhrat Maryam. Leo kuna kama milion 15 ya watu wanaojulikana kama Wayahudi. Hakuna yoyote miongoni mwao anayefuata Taurat ya ukweli. Kulingana na takwim za kimataifa "**Britannica of the Year**," bado ni rehma kama wote wanaamini kwenye dini moja kwa kuwa kuna makundi mengi miongoni mwa Wayahudi wanaamini dini nyengine au hawana dini asilani.

## DINI YA UKRISTO

Issa "alaihis-salaam" alitumwa kuboresha dini ya Waisraeli. Hiyo ina maana, Ukristo wa kweli ni dini iliyobadilishwa ya Waisraeli.

Issa "alaihis-salaam" anasema katika aya ya kumi na saba sura ya tano ya kitabu cha Mathayo, "Usifikiri kwamba nimekuja kuharibu sheria, au manabii. " Hatutarudia maelezo yaliyotolewa kwenye "Quran tukufu na Biblia," lakini tunaomba wasomaji wetu wapenzi kusoma sehemu hiyo. Biblia ya kwanza iliyokuwa na maandiko ya awali ya Ukristo yaliyotolewa na Hadhrat nabii Issa "alaihis-salaam" ilibadilishwa mara nyingi na maandiko mengi ya kigeni na hadithi za uongo na za kidunia ziliongezwa. Kwa hivyo

hadithi hizo za uongo zilipochanganywa na maneno na maagizo ya Allahu taala, Biblia ilipoteza sifa za kuwa kitabu kitakatifu.

Mwandishi mkuu wa Kiislam Alhaj Abdullah Ibn Dastan Mustafa "rahmatullahi alaih", ambae alikufa mwaka wa 1303 [1885], katika kitabu chake cha Kituruki kiitwacho **Izahulmeram fi Kashfiz-zulam**, anaelezea kitabu gani ambacho kiliteremshwa kwa Hadhrat nabii Issa kilichotajwa katika Quran tukufu. Kitabu hicho kinasema hivi: "Wayahudi walipojaribu kumuua Hadhrat nabii Issa "alaihis-salaam", walimkamata na wakachoma Biblia aliyokuwa nayo. Tangu wakati huo, Biblia ilikuwa haijaenea ulimwenguni kote, na dini yake na sheria (sheria za dini) zilikuwa hazijaanzishwa. Hii lilitokea kwa sababu kwamba Issa "alaihis-salaam" alikuwa amehubiri dini yake kwa muda wa miaka miwili na nusu. Pia hapakuwepo uwezekano wa kuwepo kwa nakala nyingine za Biblia. Wafuasi wa Issa "alaihis-salaam" walikuwa wachache mno na wengi wao walikuwa hawajui kusoma na kuandika. Kwa hivyo, haikuwezekana kwao kuwa na ushahidi wa maandishi ya Biblia. Hadi wakati huo, Biblia ilikuwa haijaandikwa, lakini nabii Issa "alaihis-salaam" peke yake ndie alikuwa ameihifadhi. Huu ni uwezekano mwingine. Katika baraza la kiroho la Nicaea (Iznik), miaka 325 baada ya Kristo, idadi kubwa ya Biblia iliteketezwa kwa sababu ya kuhukumiwa 'uongo na uovu usio na msingi.' Labda, Biblia halisi ya Issa "alaihis-salaam" iliteketezwa kati ya hizo zilizochomwa.

Wakristo ulimwenguni wanakubali kwamba maneno mengi ya kigeni yaliingizwa ndani ya Biblia na kusababisha maagizo halisi ya Allahu taala na maneno ya watumwa wake kuchanganywa pamoja. Bila shaka, Biblia ya awali ilikuwa katika lugha ya Kiebrania. Baadae, ilitafsiriwa kwa Kilatini na Kigiriki. Makosa mengi yalifanywa Wakati walipobadilisha Biblia ya Kiebrania kwa Kigiriki. Hili liliitokea kwa sababu wanao abudu masanamu wa Kigiriki walitafsiri Biblia wakitegemea falsafa ya Plato na walipinga imani ya "upweke wa Allah". Kwa hiyo, mbinu ya Utatu (umoja wa tatu), ambayo ni mbinu ya uongo kabisa, imeletwa ndani ya Biblia. Kwa mujibu wa falsafa ya Plato, si vizuri kuabudu masanamu mengi kwa hivyo ni bora kufanya masanamu maalum kuwa mungu (god).

Falsafa ya Plato pia inadai kwamba mungu (god) ni umoja wa watatu. Kwanza ni "Baba." Huyu ndie muumba mkuu na baba wa miungu (gods) mingine miwili.

Kwa mujibu wa falsafa ya Plato mungu wao wa pili ni muumba anayeonekana ambae ni kizazi cha Baba ambaye asiyeonekana. Neno hili linamaanisha nembo na ufahamu. Falsafa ya Plato inasisitiza kwamba ni ukweli Issa "alaihis-salaam" anaitwa "nembo," neno takatifu, na wakristo, na wanamwamini kuwa yeye ni "mungu" kama wanavyo dai kuwa neno hili limeandikwa mwanzoni mwa kitabu cha Yohana. Falsafa yao ya tatu ni ulimwengu (asili), unaoonekana na unaojulikana. Warumi na Wagiriki walijaribu kuufanya Ukristo kuwa falsafa. Issa "alaihis-salaam" alisema "Mimi ni mtu tu, kama nyinyi." Licha ya hayo, waliamini kuwa ni mwana wa Mungu. Hata walizusha kitu kiitwacho "Roho Mtakatifu." Walisema kwamba kulikuwepo watu watatu wa Mungu - Baba, Mwana na Roho Mtakatifu - umoja wake unamfanya “Mungu Mkristo”. Hata hivyo, neno "Baba" linalotumiwa katika Biblia ya Kiebrania lilimaanisha kwamba Allahu taala ni mwenye nguvu. Na neno "mwana" liliotumiwa kwa Hadhrat nabii Issa maana yake kwamba alikuwa "mtumwa mpendwa wa Allahu taala," sio kitu kingine chochote. Roho Mtakatifu ndiye nguvu ya unabii uliotolewa kwa Hadhrat Issa na Allahu taala. Ukweli huu unafafanuliwa katika Qurani tukufu, katika aya ya kumi na tatu ya Sura ya Tahrim kama ifuatavyo**: “Na Mariamu binti Imrani aliyejilinda utupu wake, na tukampulizia humo roho yetu na akayasadikisha maneno ya Mola wake, na vitabu vyake, na alikuwa miongoni mwa wanyenyekevu.”**

Katika Ukristo wa kwanza, hakukuwa na wazo kama "Utatu." Msomi wa Kiislam Dastan Mustafa "rahmatullahi alaih" anasema: "Wazo la Utatu" lilipendekezwa kwanza na padre aitwaye Sibelius, miaka mia mbili baada ya Issa "alaihis-salaam". Hadi wakati huo, watu waliamini kwamba Allah ni mmoja, na vile kwamba Hadhrat Issa "alaihis-salaam" alikuwa Mtume Wake. Dhana zilizopendekezwa na Sibelius zilikataliwa sana na wakristo wengi. Mapambano yalitokea kati ya makanisa na damu nyingi zilimwagika.

Ukweli huu umethibitishwa katika kitabu cha historia, kilichoandikwa wakati huo na kilichotafsiriwa kutoka Kifaransa hadi

Kiarabu. Katika mwaka wa 200 AD, wazo la 'Baba' na 'Mwana' tu lilipendekezwa. Wazo la 'Roho Mtakatifu' liliongezwa miaka ya 181 baadae na halmashauri ya dini iliyofanyika mwaka 381 wakati wa Theodosius, Mfalme wa Byzantium. Papa wengi, walikuwa kinyume na uamuzi huu. Papa Honorius kamwe hakuamini "Utatu." Ingawa Honorius aliondolewa, miaka kadhaa baada ya kifo chake, vikundi vipya vilianzishwa ambavyo vilipinga wazo la "Utatu. Kuchora picha za Hadhrat Issa, kufanya sanamu yake, na kuziweka katika makanisa, kuona msalaba kama kitu takatifu, na mambo mengine kama hayo yalisababisha shida nyingi na ukatili, hapo awali lakini vilikubaliwa na kanisa miaka 700 baadae.

Wamebadilisha maadili na misingi ya Ukristo. Papa anaamini kuwa hawezi kudhalilishwa, mapadre vile wamepewa mamlaka ya kukiri, pia binaadamu anahukumiwa kuwa alizaliwa na dhambi. Ingawa iliandikwa katika Injil (Biblia), kwamba Muhammad ni "alaihis-salaam" mtume mtukufu wa mwisho, ila walimkataa. Hata leo, wanaendelea kubadilisha maneno katika Biblia. Falsafa zao hizo zote zilimchukiza na kusababisha ghadhabu ya Allahu taala. Na katika Sura an-Nisa aya ya 172 takatifu, Allahu taala anasema hivi: **“Enyi watu wa Kitabu! Msiruke mipaka ya dini yenu, wala msiseme juu ya Allahu taala ila yaliyo ya kweli, Masihi Issa bin Mariamu ni Mtume wa Allahu taala na neno Lake tu Alilompelekea Mariamu, na ni roho iliyotoka Kwake. Basi muaminini Allahu taala na Mitume Wake, wala msiseme watatu, jizuieni, itakuwa bora kwenu, bila shaka Allahu taala ni Mungu Mmoja tu. Ni mbali na utakatifu Wake ya kwamba Awe na mwana. Ni vyake vilivyomo mbinguni na vilivyomo ardhini, na Allahu taala Anatosha kuwa Mlinzi.”**

Katika aya hio neno "Roho" humaanisha "Issa" "alaihis-salaam" limetafsiriwa kwa maana tofauti. Kwanza, lina maana kwamba Jibril "alaihis-salaam" alipumua ndani ya Maria na baada ya kupumua, akawa mjamzito. Kupumua kwa Jibril "alaihis-salaam" inaitwa "Roho". Au, Roho hapa ina maana ya ufunuo kutoka kwa Allahu taala. Mariyam alipewa habari njema kwa njia ya neno hili, na pia Jibril "alaihis-salaam" aliamrishwa kupumua, na Issa "alaihis-salaam" alipewa amri ya "Kuwa!" Au, ni amri ya "Kuwa!" Inasemekana kwamba uhusiano kati ya Allahu taala na roho ni kama uhusiano kati ya hotuba ya mtu na pumzi yake.

Katika Qurani tukufu aya ya themanini ya Suratul Baqarah inatangaza kwa wale waliobadilisha Biblia kwamba: "**Basi ole wao kwa wale waandikao kitabu kwa mikono yao kisha husema hiki kimetoka kwa Allahu** taala **ili wakiuze kwa thamani ndogo, basi ole wao kwa yale iliyoandika mikono yao na ole wao kwa yale wanayoyachuma."**

Maana takatifu ya Aya 1-3 ya Sura Al-Ikhlas: "Sema: **Yeye Allahu** taala **ni Mmoja. Allahu** taala **Asiyehitaji, Ambaye wote wanahitaji Kwake, Hakuzaa wala Hakuzaliwa, Wala Hana anayefanana naye hata mmoja**."

Tulinukuu hadithi iliyo chini kutoka Kitabu cha Kituruki **Dhiyaul-kulub** cha mwandishi Ishaq Ef-fendi "rahmatullahi alaih" kutoka Harput, Uturuki.

Mara ya kwanza mapadre wawili walienda katika mji wa Kanton nchini China ili kuhubiri dini ya Ukristo. Walimuomba gavana wa Kanton ruhusa ya kuhubiri dini ya Kikristo. Gavana hakuwasikiliza kabisa. Lakini mapadri walipomkasirikia na kumwendea kila siku (kuomba ruhusa), mwisho wake alisema, "Mimi lazima nitaomba idhini kutoka kwa Faghfur [Mfalme] wa China. " Kwa hivyo aliripoti jambo hilo kwa Mfalme wa China. Mfalme alijibu kuwa: "Nitumie hao, nataka kujua nini wanachotaka." Baadae aliwambia mapadri kwenda Peking, mji mkuu wa China. Habari hii ilisababisha msukosuko mkubwa kati ya viongozi wa Buddha. [Wao walimuomba mfalme awafukuze mapadre wa kikristo kutoka nchini mwao kwa sababu "Wakristo hao watafundisha watu wetu dini mpya ambayo itaibuka chini ya jina la Ukristo. Wakristo hao hawamtambui Buddha Mtakatifu. Wao watawapotosha watu wetu."] Mfalme akasema," Lazima tuwasikilize kwanza. Halafu tutaamua. "Mfalme alifanya mkutano na wasimamizi wa serikali na wafuasi wa nchi. Aliwaalika wakristo, akawaambia kuelezea kanuni za dini ya Kristo ambayo waliotaka kuanzisha. Baadae mapadri hao wa Kikristo walisema yafuatayo:

"Mungu, Muumbaji wa mbingu na dunia, ni mmoja. Hata hivyo, yeye ni watatu. Mwana pekee wa Mungu na Roho Mtakatifu, pia kila mmoja, ni Mungu." Mungu aliumba Adamu na Hawa na akawaweka katika Pepo. Aliwapa aina zote za baraka, bali aliwaagiza wasile matunda kutoka kwa mti fulani, kwa namna fulani Shetani alimdanganya Hawa. Na yeye, akamdanganya Adamu,

hawakuitii amri ya Mungu kwa kula matunda ya mti waliokatazwa. Kisha walifukuzwa kutoka peponi na kupelekwa duniani. Adamu na Hawa walikuwa na vizazi vya watoto na wajukuu. Wote walikuwa wenye dhambi kwa sababu walikuwa wamepotoshwa na dhambi iliyofanywa na babu yao. Hali hii ilidumu miaka elfu sita. Hatimae Mungu aliwasamehe wanaadamu, hata hivyo hakupata njia nyingine isipokuwa ni kumtoa mwanae sadaka mwenyewe kwa ajili ya ukombozi wa dhambi zao na kumuamrisha mwanae pekee kuja na ufumbuzi wa dhambi hiyo. Mtukufu mtume tunayemwamini ni Yesu mwana wa Mungu. Kuna mji unaoitwa Jerusalemu katika kanda ya Palestina upande wa magharibi mwa Arabuni. Katika Jerusalemu kuna mahali panaitwa Jelila (Galilaya), ambapo kuna kijiji kinachoitwa Nasira (Nazareti). Miaka elfu iliyopita kulikuwa na msichana mmoja aitwaye Maryam (Mary) katika kijiji hicho. Msichana huyu alipigwa kwa binamu yake wa kwanza, lakini msichana huyo alikuwa bikira. Siku moja, akiwa peke yake, Roho Mtakatifu alipumua na kumtia mwana wa Mungu ndani yake. Hivyo msichana huyo alipata ujauzito hali ya kuwa bikira kama alivyokuwa. [Kisha, walipokuwa wanakwenda Jerusalemu, alikuwa na mtoto katika imara huko Beyt-i-lahm (Bethlehemu). Walimuweka mwana wa Mungu ndani ya shamba katika imara. Wakuu wa mashariki, ambao walijua kwamba alizaliwa wakati walipoona kwamba nyota mpya ghafla ilitokea mbinguni, wakamtoa kwa zawadi mikononi mwao, na hatimaye walimkuta katika imara hiyo. Wakainama mbele yake ishara ya kumtukuza. Mwana wa Mungu, aitwaye Yesu, aliwahubiria viumbe vya Mungu mpaka alipokuwa na umri wa miaka thelathini na tatu. Alisema, Mimi ni mwana wa Mungu, muniamini mimi, nimekuja kuwaokoa nyinyi. ' Alionyesha miujiza mingi, kama kufufua wafu, kufanya vipofu kuona tena, kufanya viwete watembee, kuwaponyesha wenye ukoma, kuondosha dharuba za baharini, kulisha watu elfu kumi kwa samaki wawili, kubadili maji kuwa divai, kuifuta mtini na alama moja (mkono) kwa sababu haikutoa matunda yoyote majira ya baridi, na kadhalika. Lakini watu wachache sana walimuamini. Hatimaye, Wayahudi wasio waaminifu walimsaliti kwa Warumi, na hivyo wakamfanya asulubiwe. Hata hivyo, siku tatu baada ya kufa msalabani, Kristo alifufuliwa na kujidhihirisha kwa wale

waliomuamini. Kisha akapanda mbinguni na kukaa upande wa kulia wa Baba yake.

Huo ndiyo msingi wa dini tunayoenda kuhubiri. Wale wanaoamini dini hii watakwenda Peponi, na wale ambao hawataamini wataingia Jahannam."

Baada ya kusikiliza maneno haya, Mfalme wa China alimuambia Padri huyo kwamba "Jibu maswali haya nitakayouliza." Kisha akaanza kuuliza maswali yake, "Swali langu la kwanza ni hili: Unasema kwa upande mmoja kwamba Mungu ni mmoja na kwa upande mwingine kwamba yeye ni wa tatu. Hii ni kama si ya mantiki hivi haingii akilini, kama vile kusema kuwa mbili na mbili hufanya tano. Eleza nadharia hii kwa kiina. "Makuhani **hawakuweza kujibu**. Wakasema, "Hii ni siri ambayo ni ya Mungu pekee. Na ni mbali sana na ufahamu wa binadamu." Faghfur (Mfalme) akasema, "Swali langu la pili ni hili. Mungu ndie Muumbaji wa mbingu na ulimwengu wote, hivyo kwa sababu ya dhambi iliyofanywa na mtu mmoja, inaashiria lawama juu ya watoto wote ambao hawajui kabisa tendo la dhambi lililofanyika na baba zao, je, hii inawezekana? Na kwa nini hakupata njia yoyote kuliko kutoa sadaka mwanawe mwenyewe kama upatanisho kwao? Je! Inastahili Ufalme Wake? Je, utasemaje hili? "Wakuhani, tena, **hawakujibu**." Hii pia ni siri ya Mungu. "Faghfur akasema,"Na swali langu la tatu: Yesu aliuagiza mti kutoa matunda mapema, na kisha akaukata kwa sababu haukuweza kutoa matunda. Haiwezekani mti kutoa matunda nje ya msimu. Pamoja na ukweli huu, ingekuwa si ukatili kwa Yesu kukasirika na mti na kuukata lakini pia kwa nini hakumuambia babaake ambae kaumba kila kitu? Je, Mtukufu Mtume angekuwa mwenye ukatili? "Wakuhani **hawakuweza kujibu hili**, labda, wakasema," Mambo haya ni ya kiroho. na ni siri za Mungu. Hisia za binaadamu haziwezi kuelewa. "Baadae, Mfalme wa China akasema, "Nakupatia ruhusa (unataka). Nenda ukahubiri sehemu yoyote ya China." Walipotoka mbele ya Mfalme, Mfalme akageuka kwa wale waliokuwepo, akasema, "Sidhani kwamba mtu yeyote nchini China anaweza akawa mjinga sana kwa kuamini upotofu huo. Kwa hivyo, sioni ubaya wowote kwa kuruhusu wanaume hao kuhubiri mila hii mbaya. Ninajihakikishia kwamba, baada ya kuwasikiliza, watu wetu wataona kwamba duniani kuna makabila ya kidunia na kufikiri sana kwa imani yao wenyewe ya Buddha."

Faghfur alivyosema ulikuwa ukweli kabisa. Kwa sababu ingawa miaka 2000 imepita tangu siku hio, na licha ya jitihada kubwa zilizofanywa na wamisionari wa Kikristo, hawajaweza kuibadilisha China kuwa na waumini wa Kristo wengi.

Kama vile inavyoeleweka kwa vitabu mbalimbali ambavyo tumesoma kwa lugha tofauti, Hadhrat Maryam (Mary) aliishi peke yake katika Bayt-ul Muqaddas (Masjid-i Aqsa). Hakuna mtu yeyote aliyeingia ndani ya chumba chake isipokuwa Zakaria (Zakariy-ya "alaihis-salaam"). Malaika Jibril "alaihis-salaam" alimuambia Maryam (Mary) kuwa ingawa ni bikira atazaa na mwanawe atakuwa nabii. Mojawapo ya neno katika kitabu cha **Mir'at-i kainat** inasema: "Wakati Hadhrat Mary (Maryam) alipokua akioga katika nyumba ya Zakaria (alaihis-salaam) na shangazi yake, Jibril (alaihis-salaam) alionekana kama mwanaadamu na alimrushia pumzi ndani yake. Matokeo ya pumzi za Jibril, Maryam alishika mimba na akawa mjamzito. Baadae alienda "Bayt-ul-lahm" pamoja na mwana wa mjomba wake, Joseph (Yusuf) Najjar. **Issa** "alaihis-salaam" alizaliwa Bayt-ul-lahm. Kisha, wakaenda Misri. Wakaishi huko kwa miaka kumi na miwili. Hatimae wakahamia Nazareti na waliishi huko kwa kipindi. Wakati Issa alikuwa na miaka thelathini Allah alimteremshia ujumbe na akawa nabii. Kwa sababu hii, watu waliomuamini Issa "alaihis-salaam" waliitwa "**Nasrani**" na watu wote wa Nasrani waliitwa "**Nasara**." Kulingana na Biblia, wakati **Issa** alipozaliwa, nyota mpya nyekundu ilidhihirika mbinguni. Lakini, kulingana na wanafalsafa na wakomunisti wengine hadithi hii yote si sahihi na ni ya uongo mtupu. Hakuna mtu yeyote aliyeitwa Issa. Kulingana na Ernest Renan, profesa katika Chuo Kikuu cha Paris, Mary aliolewa na Yusuf (Joseph). Na Issa "alaihis-salaam" alizaliwa kawaida kama watoto wengine. Hata hivyo Issa alikuwa na ndugu na dada zake pia. Uthibitisho huu wa Renan ulimfanya aondolewe na Papa. Lakini, mwanzoni mawazo yake yalikubaliwa na wasioamini Mungu.

Quran tukufu inaonyesha wazi kwamba Issa "alaihis-salaam" ni mwana wa Hadhrat Maryam (Mary), ambae alikuwa bikira. Kama tulivyosema hapo juu, Allahu taala alimkarimu yeye na akamteremshia Ruh-ul-qudus (Roho Mtakatifu). Lakini ukweli halisi ulifunuliwa katika aya ya 88 na 254 ya Sura Al-Baqarah. Maana takatifu ya aya hizi ni: "**Tumempa Issa mwana wa Mariam ishara wazi na kumtia nguvu na Roho Mtakatifu**." [Aya hii tukufu inasema

kwamba miujiza dhahiri ilitolewa kwake. Na ni wazi wazi katika aya ya 49 ya Sura Aali-Imran, na katika aya ya 47 na 111 ya Sura Al-Maidah, na katika aya ya 28 ya Sura Al-Hadyd kwamba Injil (Biblia) iliteremshwa kwa Issa].

Uthibitisho kwamba Issa alizaliwa kutoka kwa bikira Maria (Maryam) unasemwa katika aya ya 44 hadi 50 ifuatayo ya Aali-Imran **"(Kumbukeni) waliposema Malaika, Ewe Mariamu, bila shaka Allahu taala anakupa habari njema za neno litokalo Kwake, ndani yake muna bishara ya mtoto jina lake Masihi Issa mwana wa Mariamu, mwenye heshima katika dunia na Akhera, na yu miongoni mwa waliokaribishwa. Naye atazungumza na watu katika utoto na katika utu uzima, na atakuwa katika watu wema. (Mariamu) akasema, Mola wangu, nitampataje mtoto na hali ya kuwa mtu yoyote hakunigusa? Akasema: Hivyo ndivyo Allahu taala Huumba Anavyopenda, Anapotaka jambo basi Huliambia tu kuwa, basi huwa. Na (Allahu taala) Atamfunza Kitabu na hekima na Taurati na Injili. Na (Atamfanya) Mtume kwa wana wa Israeli (kuwaambia), Nimewajieni na Ishara kutoka kwa Mola wenu, ya kwamba nawaumbeni katika udongo sawa na matengenezo ya ndege, kisha napulizia ndani yake, mara hua ndege kwa idhini ya Allahu taala. Na ninamponesha kipofu na mwenye ukoma, na kuwahuisha wafu kwa idhini ya Allahu taala, na ninawaambieni mtakavyovila na mtakavyoweka akiba katika nyumba zenu, bila shaka katika hayo imo ishara kwenu ikiwa ninyi mnaamini".**

Kama ilivyoelezwa katika Sura Aali-Imran ayat za juu hapo, Issa "alaihis-salaam" alizungumza na watu wakati alipokuwa mtoto sana. Alipokuwa mtoto alikuwa na hekima ya ajabu. Maswali yaliulizwa kwake na alikuwa anajibu ipasavyo. Hali hii ilionyesha kwamba alikuwa mtu wa ajabu. Wakati wa unabii wake, ulioishi miaka mitatu, alihubiri Jerusalem na alifanya miujiza kadhaa. Kama ilivyoelezwa katika Quran tukufu, aliwafufua wafu. Aliponyesha wenye ukoma. Alirudisha macho ya vipofu. Issa "alaihis-salaam" alikuwa nabii ambae hakuwa na nyumba. Alikuwa anaabudu mola wake usiku na mchana. Issa alikuwa mwenye fadhili, mwenye huruma, na alikuwa anaishi kama mtu wa kawaida. Miujiza aliyotumia ilimfanya atembee mara moja baada ya kumponya mtu ili asimshukuru. [Kwa mfano, siku moja walikuwa wanasafiri katika meli, dhoruba kali ilitokea. Walipohofu kuangamia, abiria

walilalamika, "Kwa nini (Issa) usizuie dhoruba hiyo? Tutaangamia. Je, hujali?" Alikuwa kimya]. Issa "alaihis-salaam" Aliwasamehe abiria hao kwa tabia zao mbaya.

Idadi ya maagizo [amri na makatazo] katika Injil (Biblia) ilikuwa chache sana. Issa "alaihis-salaam" hakudai kuwa alileta dini mpya. Alisema kila siku "Sianzishi dini mpya, ila mimi nilitumwa nirejeshe dini ya ukweli ambayo ililetwa kwa mitume wa Israeli 'alaihim-us-salawatu wa-t-taslimat' na ambayo ukweli wake umeanza kupotea”. Issa alitaka kila mtu amuamini Allahu taala mmoja. Hivyo, haikubaliki kudai kwamba Ukristo ni dini mpya. Ukristo na dini nyingine ambazo zinaamrisha kuamini Allahu taala mmoja zililetwa na Hadhrat Ibrahim "alaihis-salaam" na Musa "alaihis-salaam" ni sawa. Issa "alaihis-salaam" hakuandika mafundisho yake mwenyewe wala Biblia. Na hakuna mtu aliyemilki Biblia halisi iliyoteremshwa na Allahu taala. Biblia iliopo leo na Wakristo imejumuisha maandishi kutoka Torati ya Kale na vitabu vingine vilivyoongezwa baadae na Matayo, Marko, Luka na Yohana na vijitabu na barua za wanafunzi waliitwa mitume (Agano Jipya). Kwa maelezo zaidi [Tazama: **Quran tukufu na Biblia**.] Biblia zilizoandikwa na mitume wengine zilikusanywa na kuchomwa. Tukio hili lilifanyika katika halmashauri za kidini ambazo zilifanyika Istanbul mnamo mwaka wa 381 AD, na ambazo tumewahi kugusa, sio kuwaeleza wale wa awali, kama vile ilivyofanyika katika mwaka wa 325 na 364 [wakati wa utawala ya Constantine na Theodosius].

Ukweli kwamba mtume Muhammad "swallallahu alaihi wa sallam" atatumwa ulielezewa kwenye Biblia na **Barnaba**, lakini ushahidi huo ulifutwa kwenye Biblia. Leo, inajulikana kuwa hakuna mmoja ya waandishi wa vitabu hivi vinne aliyewahi kumuona Issa "alaihis-salaam" isipokuwa Yohana. Kulingana na kitabu cha Ishaq Effendi "rahmatullahi alaih" kutoka Harput nchini Uturuki, anasema kwamba Biblia ya kwanza, ya pili, ya tatu na ya nne ziliandikwa miaka ya 65, 60, 55-60, na 98 baada ya Kristo. Katika kitabu cha Yohana kinasemakana kwamba: "Mwenyezi Mungu aliwapenda wanaadamu sana kiasi kwamba aliwatumia mwanawe mwenyewe." Lakini hakuna shaka kwamba neno "mwanawe mwenyewe" linamaanisha "mtumwa anayempenda." (Yohana alikuwa mwana wa (mjomba wa mama wa Issa wa "alaihis-salaam"). Hata hivyo, ushahidi kama huo haupatikani katika vitabu

vingine vitatu. Lakini katika vitabu hivyo, Issa "alaihis-salaam" anamtambua Allah kama "Baba," neno ambalo bila shaka lina maana ya "mtu mtakatifu na mpenzi". Kipengele kilichotajwa kwenye aya ya tano ya sura ya ishirini na saba ya kitabu cha Mathayo inathibitisha kwamba baadhi ya vitabu (Biblia) viliandikwa baada ya miaka sabini ya kuzaliwa kwa Issa "alaihis-salaam". "Issa "alaihis-salaam" alipokufa, pazia la hekalu lilifunikwa kutoka juu hadi chini, na dunia ilitetemeka, na makaburi yalifunguliwa, na miili mingi ya watakatifu ikaondolewa makaburini baada ya kufufuliwa kwake, aliingia katika mji mtakatifu, na akadhihirika kwa wengi. Maelezo haya ya maafa yalinukuliwa kutoka kitabu cha Myahudi ambae alikuwa na huzuni sana wakati Jerusalemu ilipoharibiwa na kuchomwa na Tito, mfalme wa Kirumi, miaka sabini baada ya kuzaliwa kwa Issa "alaihis-salaam". Norton Andrews (1786-1853), mmarekani na mtetezi wa Biblia, alisema, "Hadithi hio ni ya uongo. Kweli kinachosemwa ni uthibitisho wa kujitegemea. Ulikuwa ni moja ya uongo kuhusu Masjid - Aqsa, uliyotengenezwa na Wayahudi ambao walikuwa katika hali iliyoharibiwa baada ya jiji la Jerusalemu kuharibiwa. Baada ya muda, mtu aliandika hadithi hii kwenye sehemu ya kitabu cha Matayo akifikiria kuwa Issa "alaihis-salaam" alifaa kusulubiwa. Kisha, mwandishi mwingine aliandika katika kitabu cha Matayo. Baadae, maandishi hayo yalitafsiriwa kabisa. "Mathew aliandika tukio hili katika kitabu chake kwamba kilichotokea wakati wake na kama alivyoshuhudia kwa macho yake mwenyewe. Lakini kuna shaka kwamba kitabu cha Matayo kiliandikwa na Matayo yeye mwenyewe au na watu wengine. Wanahistoria wa Ulaya wanasema kuwa kuna mitindo miwili ya maandishi katika kitabu cha Matayo, na wanasema kwamba kitabu hicho kinawezekana kuwa kiliandikwa na watu wawili tofauti. Hata wakristo waaminifu wa kidini wanakubali kwamba Biblia ambazo zilizopo duniani leo sio maneno ya Allahu taala.  Kama tulivyosema hapo awali.

Biblia ina mchanganyiko wa maneno ya Allahu taala pamoja na maneno ya wanaadamu. Usia muhimu kwa Waislamu ni kwamba: Katika Biblia, aya zinazokubaliana na Quran tukufu lazima zikubaliwe, lakini aya ambazo ni kinyume na Quran tukufu lazima (kuwa ni maneno ya wanaadamu) zikataliwe. Ila aya ambazo hazikubaliani wala kukataliwa na Quran tukufu zinaweza kuwa

sahihi baada ya kuchunguzwa vizuri, hizo zinaweza kukubaliwa na imani ya Kiislam.

Issa [alaihis-salaam] alitumwa kurekebisha dini ya Waisraeli.

Lakini, Wayahudi hawakumpenda Issa "alaihis-salaam". Walisema kwamba Issa "alaihis-salaam" alikuwa nabii wa uongo. Walilalamika juu yake kwa Warumi, wakasema "Issa "alaihis-salaam" anataka kuwa Mfalme wa Israeli, anataka kuwashawishi watu kuwaasi dhidi ya Warumi, anajiona kuwa ni mwana wa Mungu." Wakristo wanaamani kwamba, Pilatus, aliekuwa gavana wa Kiyahudi katika mamlaka ya Warumi alimkamata Issa "alaihis-salaam" akampeleka kwa Hirodes. Hirodes alifurahi sana kwa sababu alitaka kukutana na Issa "alaihis-salaam" na vile kuona miujiza yake. Lakini Issa "alaihis-salaam" alinyamaza kimya na hakujibu maswali yaliyoulizwa na Hirodes. Baadae Hirodes alimpeleka tena kwa Pilatus. (Sura ya ishirini na tatu ya Luka). Issa "alaihis-salaam" alihimizwa na wafuasi wa Wayahudi, kisha Pilatus alimpeleka kwa Wayahudi kusulubiwa. Wakristo wanaamini kwamba Issa "alaihis-salaam" alisulubiwa na kufa, baadae alifufuliwa na akapanda Mbinguni. Lakini Waislamu wanaamini kuwa Hadhrat nabii Issa hakukamatwa wala kusulubiwa lakini alipandishwa mbinguni moja kwa moja. Na mtu aliyesulubiwa badala yake alikuwa Yuda (Yahuda, mmoja wa watume wake). Ushahidi huo umefunuliwa katika Quran tukufu, Sura An-Nisaa katika aya ya 156 hadi 159: **"Basi kwa sababu ya kuvunja kwao ahadi yao, na kuzikataa kwao Ishara za Allahu taala, na kuua kwao Manabii bila ya haki, na kwa kusema kwao, mioyo yetu imefunikwa; bali Allahu taala Aliipiga muhuri kwa kufuru zao, kwa hiyo hawaamini ila kidogo tu. Na kwa sababu ya kufuru zao na kusema kwao juu ya Mariamu masingizio makubwa. Na kusema kwao hakika tumemuua Masihi Issa mwana wa Mariamu, mtume wa Mungu hali hawakumuua wala hawakumfisha msalabani, bali alifananishwa kwao (kama maiti). Na kwa hakika wale waliohitilafiana kwa hili wamekuwa wana shaka nalo, wao hawalijui hakika yake isipokuwa wanafuata dhana. Na kwa yakini wao hawakumuua. Bali Allahu taala Alimnyanyua Kwake, na Allahu taala ni Mwenye nguvu, Mwenye hekima. "** Baada ya Issa "alaihis-salaam" kupanda mbinguni, Ukristo ulianza kuenea polepole ulimwenguni kote. Kutoka mwanzo, Warumi na Wagiriki

ambao walikuwa wanaabudu masanamu, walikataa dini hii mpya. Wakristo walikamatwa na kuuliwa. Walitupwa mbele ya wanyama mwitu katika mzunguko. Lakini, dini ya ukweli iliendelea mbele kujulikana na kuheshimiwa. Lakini ni aibu kwamba Injil halisi (Biblia) ilisambaratika muda mchache. Ushawishi wa uongo wa Paulo, ambae alikuwa mnafiki. " Ni sababu ya kusulubiwa kwa Issa. Msingi wa Ukristo wa leo ni kwamba Mungu aliruhusu mwanawe kuuliwa ili akasamehe dhambi za wanaadamu." Ingawa Issa "alaihis-salaam" hakusema kwamba mtu yeyote anaezaliwa kuwa ni mwenye dhambi, Ukristo wa leo unaelezwa kama ifuatavyo:

1. Mtu anazaliwa kama ana dhambi. Adamu, mwanaadamu wakwanza, hakuitii amri ya Allahu taala, Kwa hivyo, alifukuzwa kutoka peponi.

2. Vizazi vya Adamu, hadi sasa, vinaonekana kuwa na dhambi.

3. Issa "alaihis-salaam" ni mwana wa Allahu taala alimtuma ulimwenguni kuwaokoa wanaadamu kutoka kwenye dhambi.

4. Allahu taala aliruhusu mwanawe mwenyewe kusulubiwa kwa sababu alitaka kusamehe dhambi za wanaadamu.

5. Dunia hii ni mahali pa mateso. Furaha na raha ni marufuku katika ulimwengu huu. Mtu aliumbwa kuteseka na kuabudu.

6. Mtu hawezi kuwa na uhusiano wa moja kwa moja (ibada) na Allahu taala. Hawezi kumuomba moja kwa moja. Mapadre tu ndio wanaweza kumuomba Allahu taala. Na mapadre pekee ndio wanaweza kusamehewa dhambi zao.

7. Kiongozi wa Wakristo ni Papa. Papa tu ndie asiyekuwa na hatia wala makosa, chochote anachofanya ni haki.

8. Roho na mwili ni tofauti. Mapadri pekee ndio wanaweza kusafisha roho za watu. Lakini miili ya watu haitakuwa safi, itakuwa daima na dhambi.

Kwa sababu ya masuala haya yasiyokubalika, Ukristo wa kweli ulioletwa na Hadhrat nabii Issa ili kurekebisha dini ya Waisraeli ulipoteza misingi yake ya ukweli, na ikawa ni dini ya uongo au dini inayoitwa Ukristo.

Watu wengine walijaribu kuurejesha Ukristo kwenye utaratibu na mfumo wake wa awali. Wakizingatia lengo hili, Padre aitwaye Luther alianzisha dini mpya iitwayo Uprotestanti, lakini yeye

alifanya Ukristo ukawa mbaya sana kuliko ulipokuwa mwanzoni. Licha ya hao, dini ya Kiislam iliteremshwa ili kurekebisha makosa yote yaliyoingizwa katika Ukristo baada ya Issa "alaihis-salaam" na kuweka dini takatifu katika hadhi yake ya asili kwa sababu ilikuwa imeharibiwa sana na ilikuwa ikizidi kuwa mbaya zaidi. Bila shaka, vitabu vyote vitakatifu vilivyoteremshwa na Allahu taala vimeonyesha kwamba "Mtume mtukufu "alaihis-salaam" atakuja," na atawaongoza wanaadamu wote katika njia sahihi inayoongoza kwenye uokovu. Ujumbe huu unaweza kuonekana katika Torati na katika Biblia pia. Aya ya 12-13 ya Sura ya kumi na sita katika Yohana inasema hivi: "Bado nina mengi ya kuwaambieni, lakini hamuwezi kuyabeba sasa. Ni wakati gani yeye, Roho wa ukweli atakuja, na atawaongoza katika yote ya ukweli". Katika aya ya 72, 96, 136, 163, ukweli huu uliteremshwa pia kwa wafuasi wake na Hadhrat Issa " Mtume mtukufu atakuja, jina lake ataitwa Muhammad, atairejesha Injil (Biblia) katika asili yake sahihi, kwa sababu itakuwa imeharibiwa mpaka atakapokuja, ataleta kitabu kitakatifu". Lakini inasemekana katika kitabu hicho kwamba yeye hakusulubiwa, mtu aliyesulubiwa alikuwa Yuda, ambae aliwaambia maafisa wapi wanaweza kumuona Issa. Ukweli huu pia unathibitishwa na Quran tukufu katika Sura (Sura) Saff. Ayat ya saba inasema **"Na aliposema Issa bin Maryam. Enyi wana wa Israeli, mimi ni Mtume wa Allahu taala kwenu, ninaethibitisha yaliyo mbele yangu katika Taurati na kutoa habari njema ya Mtume atakayefika nyuma yangu jina lake ni Muhammad, lakini alipowafikia kwa Ishara zilizo wazi, wakasema huu ni udanganyifu dhahiri".**

## UISLAMU

Mtukufu Mtume aliyechaguliwa na Allahu taala kueneza dini hii mpya alikuwa Hadhrat Muhammad "swallallahu alaihi wa sallam". Kwenye kitabu hiki kinachoitwa **Quran Tukufu na Bibiliya** kuna maelezo mengi juu ya jinsi Hadhrat Muhammad alivyokuwa, jinsi alivyopewa amri ya kwanza ya Allah, na jinsi alivyoanza kueneza Uislam; hivyo, hakuna haja ya kuyarudia hayo hapa. Hapa tutaongeza ukweli ambao haujaelezewa hapo awali. Uislamu ni dini ya ukweli iliyotumwa na Allahu taala na ambayo Hadhrat Muhammad (swallallahu alahihi wa sallam) alianza kuwahubiria watu wake akiwa na umri wa miaka arobaini na mitatu baada ya kuzaliwa kwake mwaka wa 571 A.D. Kwa namna nyengine, alifikisha Ukristo na Uyahudi uliojitakasa, ambao ulikuwa umeharibika kwa sababu ya kubadilishwa na watu mafundisho yake. Jina la dini hii ni Uislam. Na bila ya shaka, yote haya yalikuwa asili kwa sababu tumewahi kuelezea huko nyuma katika kitabu hiki, kwamba dini ambayo anaitambua Allah, ambayo ilikuwa imejulikana tangu wakati wa Adamu (alaihis-salaam), ilifikia asili yake ya mwisho na "**Uislam**," baada ya Uyahudi na Ukristo. Utafiti wa makini wa maisha ya manabii wengine na dini walizohubiri, ambazo zimeandikwa katika vitabu vya Wakristo, zinafafanua ukweli kwamba wao manabii pia walikuwa na dini moja tu ambayo ni dini ya "**Tawhid**", jambo ambalo, kwa upande wake, linathibitisha hoja yetu ya kwamba "utatu" ni upotofu ulioingizwa katika dini ya Issa 'alaihis-salaam' na Wayahudi na Warumi.

1- Kitabu kitakatifu cha dini ya Uislamu ni **Quran tukufu**. Quran tukufu ni dhahiri kwamba ni neno la Allahu taala. Ingawa vitabu vingine vitakatifu vimebadilishwa kwa muda mrefu na ndani yake baadhi ya maneno ya binaadamu yameingizwa, Quran tukufu imebaki katika hali yake ya awali tangu ilipoteremshwa na hakuna neno, hata moja, ambalo limebadilishwa mpaka sasa hivi. Jambo la "Tawhid" linalohusu imani katika Uislam ni sawa na yale yaliyomo katika dini za manabii wengine. Kwa upande mwingine, na kwa bahati mbaya, baadhi ya hadithi za uongo na maandiko ya watu yaliingizwa kwenye dini zao.

2- Leo, dini ya Kiislamu inatajwa na kuidhinishwa duniani kote. Miaka iliyopita, wasomi wa dini ya Kikristo waliushambulia Uislamu kwa upofu wao waliita 'Dini ya Uislam kwamba iliyoanzishwa na shetani', kwa mfano wapapa, ambao wanashikilia mamlaka ya dini katika Kanisa la Kikristo, walitengeneza safari za kupigana vita ili kuangamiza Waislamu. Baada ya karne ya kumi na nane tu, wanahistoria wa Ulaya walijifunza dini ya Kiislam na hatua kwa hatua wakaanza kutafsiri Quran tukufu katika lugha zao wenyewe za kiulaya.

Licha ya ukweli kwamba baadhi ya tafsiri hizo zilifanywa na Wakristo washupavu, kwa sababu hiyo, tafsiri yao haikuwa sawa kulingana na Quran yenyewe. Pia kulikuwa na tafsiri za kuaminika zilizofanywa na wanahistoria waaminifu miongoni mwa wakristo wa Ulaya. Kwa upande mwingine, kuna baadhi ya tafsiri za Quran tukufu zilizofanywa na Waislamu. Watu ambao walisoma tafsiri sahihi au tafsiri za Quran tukufu na kuelewa vyema, kisha wakaisifu ni Goethe, Carlyle, Lamartine, Tagore na wengineo. Maelezo ya kina juu ya athari ya tafsiri kwao yanaonekana katika vitabu vyetu. Lakini sasa tutafafanua makala kadhaa yaliyoandikwa na watu mbalimbali waliokuja Uturuki baada ya 1266 (1850) kwa ajili ya dini ya Kiislam na Hadhrat Muhammad "swallallahu alaihi wa sallam".

Mheshimiwa Charles Charles, mwandishi wa kwanza wa ubalozi wa Uingereza huko Istanbul kati ya miaka 1311-1316 (1898), katika kitabu chake **Uturuki ipo Ulaya** kilichochapishwa mwaka wa 1900, anasema hivi kuhusu "Dini ya Kiislamu" "Dunia hii haikuwa uwanja wa Issa (alaihis-salaam). Ukristo kama ungelikuwa umeunganishwa na serikali fulani au mashirika yoyote ya serikali, ungeporomoka kabisa. Tunaona kwamba ukweli huu ni kinyume kabisa na Uislam. Muhammad (alaihis-salaam) sio tu mtu wa kidini, alikuwa pia kiongozi mkuu wa umma wake. Aliheshimiwa na wageni wake hata zaidi ya wanavyofanya wafuasi wa kristo wanavyomuheshimu Mfalme Papa. Muhammad (alaihis-salaam) alikuwa daima mjumbe makini na, licha ya shughuli zake za ajabu na miujiza, alisema kuwa alikuwa mtu tu na alikuwa na maisha yake binafsi kama watu wangineo walivyo".

Katika sehemu nyingine ya kitabu hicho cha Mheshimiwa Charles Charles, inasema hivi "Tukizingatia mtindo wa maisha ya watu wakati wa Issa (alaihis-salaam) na dhambi na makosa

waliyoyatenda, itakuwa ajabu kuona kwamba madhambi hayo hayakukatazwa wala kupigwa marufuku katika Biblia. Biblia inapendekeza tu kwamba watu wasifanye dhambi hizo. Haikutaja nini kitatokea kwa watu ambao wameyafanya madhambi hayo vile na adhabu zao zitakuwaje. Kwa upande mwingine, Quran tukufu inaonesha wazi wazi dhambi. Kwa mfano, kuabudu masanamu au kuzika wasichana waliozaliwa (watoto wa kike wachanga) hai, pamoja na adhabu kwa kila mmoja wao huko Akhera imeelezewa wazi wazi.

Kwa hiyo, Quran tukufu ilitoa huduma kubwa sana kwa mataifa ya Arabia kwa kupingana kabisa na dini za uongo za siku hizo za kijahiliyya."

Sir Eliot anasema kuwa: "Moja ya kanuni bora za Uislam ni kwamba Uislam haubaguwi kati ya wananchi na wageni wa nchi, yani watu wote ni sawa. Hakuna mpatanishi kati ya Allahu taala na mja wake katika dini ya Kiislamu. Wapatanishi wa kati (mediator), kama mapadri, wameondolewa katika Uislam."

"Binaadamu anaheshimiwa sana katika Uislamu. Kama vile, askari wa Kituruki ni mfano mzuri wa jambo hili, wao ni nidhamu kabisa wanafanya mpango wa kibinafsi, na mataifa mengine hayana askari kama hawa wa Kituruki. Lakini, nidhamu yao, utii mkali kwa viongozi wao na ujasiri wa maadili hutoka kwenye ukweli kwamba wao ni Waislamu wema. Bila shaka ni Uislam ambao unaingiza ndani ya nyoyo zao sifa hizi nzuri. Zaidi ya hayo, ni Uislamu vile ambavyo umeanzisha "umoja wa mali" kati ya watu, kwa msaada wa "zakat". Zakat inajaribu kuondoa pengo kati ya matajiri na maskini, pengo ambalo linaweza kusababisha mshtuko wa kijamii. Kwa hivyo, dini hii ya ajabu inatosha kwa kila mtu kuelewa mambo ya dunia na akhera. Mtu yeyote atakayejifunza kwa upendeleo na kwa undani maelezo ya Muhammad (alaihis-salaam) atakuwa na heshima kubwa na upendo kwa ajili yake."

Sasa, hebu tuchunguze kitabu kingine. Katika kitabu chake **La Turquie Actuelle** (Uturuki wa Leo), kilichochapishwa Paris mnamo mwaka wa 1267 (1851), Kiongozi wa mkoa wa Kifaransa Henry A. Ubi-cini mwenye asili ya Kiitaliano ambae alizaliwa katika jiji la Touraine, Ufaransa, baada ya kuishi nchini Uturuki kwa miaka kadhaa, anaelezea kuhusu Uislam kama ifuatavyo:

"Dini ya Uislamu inamuamrisha binadamu kuwa na huruma na kuwa na mtazamo mwema. Watu masikini ambao walifukuzwa kutoka Ulaya kwa sababu waliitwa "wajeuri", walikaribishwa kwenye ufalme na wameishi katika uhuru na usalama katika ulimwengu wa Kiislamu wa Kituruki, ambao mwanzoni walinyanganywa walipokuwa Ulaya. Wananchi wote wa kila aina ya dini wameonesha huruma sawa na haki sawa nchini Uturuki. Wazungu, ambao wanasema kuwa Waturuki na Waislamu ni wabaya, walipata masomo ya ubinadamu na ukarimu kutoka kwa Waturuki na Waislamu. Mwandishi aliyeishi katika karne ya kumi na sita akasema 'Ajabu, lakini nimeenda nchi za Kiislam. Sikuona muamala mbaya au ukatili katika miji ya Waislam, ambao tunawaita wakatili. Wanaheshimu haki za wengine. Wao huwasaidia sana watu wapweke.

Inaaminika kwamba katika nchi za Uislamu, wazee, vijana, Wakristo, Myahudi au Waislamu, na hata watu wasioamini Mungu wote hupewa haki sawa. 'Ninakubaliana naye.' (Muandishi Ubicini) anasema katika kitabu hicho kama ifuatavyo:

"Katika mji wa Istanbul matukio machache yalitokea katika sehemu inayoitwa 'Fatih' ambapo Waislamu wengi wanaishi. Lakini, kila siku, wizi na uhalifu ulifanyika katika sehemu inayoitwa Pera (Beyoglu) ambako Wakristo wengi wanapoishi. Hapa, watu huibiana na kuuana, imekuwa tabia ya kawaida kama ilivyo katika miji mikubwa ya Ulaya. Licha ya mamia ya maelfu ya Waislamu wanaishi kwa amani, uaminifu na utulivu katika eneo lililoitwa 'Fatih', Wakristo karibu 30,000 huko ‘Pera’ wanaishi kwa uzito na uovu na ni mfano mbaya wa uaminifu kwa ulimwengu. Waitaliano walitunga wimbo kwa Pera: '**Pera, dei sulirati il nido**', (Pera ni pango la wagonjwa). Wanaimba wimbo huu kwa kuendelea".

Bwana Maxima Rodinson, mtu ambae asiyeamini Mungu alisema juu ya mtume wa Uislamu "swallallahu alaihi wa sallam" yafuatayo; Katika kitabu chake **Muhammad**, kilichochapishwa hivi karibuni na kutafsiriwa katika lugha 25 za kigeni, alibadilisha maana ya mistari fulani akitafsiri Quran kulingana na mawazo yake mwenyewe, lakini bwana huyo Maxima Rodinson, Marxist, mwanakomunisti na mwanzo ni Myahudi, hakubali dini yeyote, na anatambua Waislamu wote (alaihi-mussalawatu wattaslimat) kama ni wagonjwa wa kifafa ambao waliona vizuka. Hata hivyo, juu ya

mtume Muhammad (swallallahu alaihi wa sallam") alisema hivi "Kwa kweli, tunajua kidogo sana juu ya utu wa Muhammad (rahma-Allahu taala alaihi ya sallam) mtu ambae mawazo yake na shughuli zake zilizunguka katika ulimwengu wote. Lakini inawezekana kuona kwamba Muhammad (rahma-Allahu taala alaihi ya sallam) alijaa mwanga wa kibinafsi ambao hauwezi kuonekana kwa mtu mwingine yeyote. Hii ni nuru ambayo iliwafanya watu waliokusanyika kuzunguka kipaji chake. Tunaweza kukubali jambo hili. Mimi nimejaribu kuelezea katika kitabu changu mwanga huu [halo] kama vile ninavyoweza kuona." Kama inavyoonekana, waandishi wa Ulaya nao wanakubali ukamilifu wa dini ya Kiislam, na vile wanavyo msifu mtume "swalallahu alaihi wa sallam" na kuangalia Quran tukufu kama kitabu kamili. Lakini, hao wenyewe wanafikiri kwamba kitabu hiki hakikutumwa na Allahu taala. Wanaamini kwamba" Qurani imeandikwa na mtume wetu "swallallahu alaihi wa sallam", yaani, ilitokea kutokana na uwezo wake wa kufikiria na sio ujumbe wa Allah. Muhammad "alaihis-salaam", ambae alikuwa muaminifu kabisa, aliamini kuwa Quran ilitumwa kwake na Allahu taala. "Baadhi ya wanahistoria hawa wanasema kwamba Muhammad "alaihis-salaam" alijua kusoma na kuandika au kwamba alipata elimu ya dini kutoka kwa Wakristo (au Wayahudi). Rodinson, mwanakomunisti aliyetajwa hapo juu, anajaribu kuthibitisha kuwa neno "**ummi**" (hajasoma), neno ambalo linafafanuliwa katika Quran tukufu kwamba mtume mtukufu kwamba hajui kusoma wala kuandika, halimaanishi kwamba "mtu asiyejua kusoma na kuandika." Rodinson anathibitisha kwamba linamaanisha kitu tofauti kabisa. Anasema kwamba "Bahira" padri moja ndie aliyemfundisha Mtume wetu.

Bahira alikuwa monki wa Kikristo. Katika nakala zingine zinasema kuwa, jina lake halisi linasemekana kuwa Georgius au Sargius. Kwa lugha ya Kiarabu, Bahira [au Behfra] inamaanisha "wanajulikana" na huenda ikawa ni jina la utani lililotumiwa kwa monki hii.

Siku moja mtume wetu "swallallahu alaihi wa sallam", alipokuwa na umri wa miaka kumi na miwili, alimuona Abu Talib akijitayarisha kwa ajili ya safari ya biashara. Wakati Abu Talib alipomwambia kwamba hakutaka kumchukuwa, Mtume wetu alimuambia, "Katika jiji hili unaniacha na nani? Kwa sababu hapa

sina baba, wala mtu yeyote anaenihurumia mimi." Abu-Talib alivutiwa sana na maneno haya ya Mtume wetu, **kwa hivyo aliamua kumchukuwa**. Baada ya safari ndefu, na msafara wa biashara walikaa kwa muda karibu na makao ya Wakristo kutoka Basra. Katika makao hayo kulikuwa na padri aliyeitwa Bahira. padri, huyo alikuwa mwanazuoni wa Kiyahudi aliyejifunza sana na alikuwa amebadilisha Ukristo baadae. Alikuwa na kitabu kilichofikia urithi wake kwa njia ya mlolongo wa vizazi kadhaa na ambacho alikuwa akikiweka kama kitabu cha kutafakari kujibu maswali aliyoulizwa. Ingawa alikuwa ametembelea eneo hili mara kadhaa katika kipindi cha miaka iliyopita, hakuwa na hamu ya msafara wa Quraish wakati wote. Kila asubuhi alikuwa anakwenda kwenye mtaro karibu na monasteri na kuangalia nje kuelekea mwelekeo wa wanaowasili karibu kama kwamba alikuwa akitarajia jambo lisilo la kawaida. Wakati huu kilitokea kitu kwa Bahira na kwa msisimko mkubwa, alisimama na kushangazwa. Aliona wingu, ambalo lilikuwa linazunguka na kufuata msafara wa Quraish. Wingu hili lilikuwa linamlinda Mtume wetu dhidi ya joto la jua. Baada ya msafara kukaa kidogo kwa ajili ya kupumzika, Bahira pia alimuona Mtume wetu pale alipokaa chini ya mti, matawi yake yalimuekea kivuli cha kumsitiri. Msisimko wake uliongezeka. Hapo hapo, aliamrisha maandalizi ya meza kwa chakula cha jioni. Kisha aliwaalika wanachama wote wa msafara wa Quraish kula chakula cha jioni pamoja. Wote walikubali mwaliko huo, wakamuacha Mtume wetu "swallallahu alaihi wa sallam" kutazama msafara wao. Bahira alichunguza wageni wake kwa uangalifu kisha akauliza, "Wapendwa wa Quraish, je, kuna yoyote kati yenu ambaye hakuja kwenye chakula cha jioni?" Wakasema, "Naam, kuna mmoja." Na alivyo tazama juu, wingu lilikuwa bado pale pale lilipo kuwa mwanzoni, ingawa wote katika ma Quraish walikuja. Alipoona jambo hilo, alijua kwamba kuna mtu aliyeachwa kulinda msafara. Bahira alisisitiza juu ya kuja kwake kwenye chakula cha jioni. Mara tu Mtume alipofika, Bahira akamtazama na kumchunguza kwa makini. Baadae Bahira akamuuliza Abu Talib, "Je huyu mtoto ni wako?" Abu Talib akasema, "Yeye ni mwanangu." Bahira alisema, "Kwa mujibu wa vitabu fulani, imeandikwa kwamba baba wa mtoto huyu hayuko hai na huyu si mwanao. Wakati huo Abu Talib akijibu, "Yeye ni mwana wa ndugu yangu." Bahira aliuliza, "Nini

kilichotokea kwa baba yake?" Akajibu, "Baba yake alikufa alipokuwa ni mdogo mno." Bahira: "Wewe umesema ukweli kabisa, nini kilichotokea kwa mama yake?" Abu Talib akajibu, "Alikufa pia." Akihakikishia majibu haya yote, baada ya hayo Bahira alimgeukia Mtume wetu na akamuomba afanye kiapo kwa jina la sanamu. Lakini Mtume wetu akamwambia Bahira "Usiniambie kufanya kiapo kwa jina la masanamu hayo. Katika ulimwengu huu hakuna adui zaidi kuliko haya masanamu, nawachukia wote". Bahira kisha akaomba kiapo kwa jina la Allahu taala na akamuuliza "Je Wewe unalala?" Mtume wetu alimjibu, "Moyo wangu haulali, ingawa macho yangu yanalala". Bahira aliendelea mbele kuuliza maswali mengi na kupata majibu kama alivyo tarajia. Majibu haya yalifanana na yale yaliandikwa katika vitabu ambavyo alikuwa amesoma hapo awali. Kisha, Bahira alitazama macho ya Mtume wetu mpendwa, akamuuliza Abu Talib, "Je! Hii hupendi hukaa daima katika macho haya yanayobarikiwa?" "Ndio" akasema, "Hatukuwahi kuiona kama inatoweka." Kisha, Bahira alitaka kuona Muhuri wa Unabii ili kuimarisha moyo wake baada ya kuona ushahidi huo. Lakini, Mtume wetu "swallallahu alaihi wa sallam" hakutaka kufunua (mgongo) nyuma yake kutokana na hisia zake nzuri.

Lakini mjomba wake akasema, "hee mwanangu, tafadhali fanya yale anayotaka." Hapo hapo, Mtume wetu alifunua mgongo wake na Bahira aliona uzuri wa Muhuri wa Unabii kwa kuridhika sana. Alimbusu kwa msisimko na machozi yalijaa usoni mwake. Kisha, Bahira akasema, "Nakiri kwamba wewe ni Mtume wa Allahu taala." Na kwa sauti kuu aliwaambia maquraish: "Huyu ndie Mwalimu wa ulimwengu wote ... Huyu ni Bwana wa Ulimwengu ... Huyu ndie Mtume mkuu ambae Allahu taala amemtuma kama baraka kwa ulimwengu wote. " Lakini wana biashara walishangaa. Wakasema, "Kwa mtazamaji wa padri huyu jinsi Muhammad (alaihis-salaam) anakadiriwa kuwa juu na mkubwa kuliko wengineo." Bahira kisha akamwambia Abu Talib kwamba, "Huyu ni mtume wa mwisho na anaheshimiwa zaidi kuliko watume wote, na vile dini yake ya Uislamu itaenea ulimwenguni pote na kuondosha dini zote za awali. Kwa hivyo usiende nae Dameski. Kwa sababu Wana wa Israeli (Wayahudi) ni maadui wake. Ninaogopa watamletea madhara mtu huyo mpendwa na waheshima, vile viapo vingi na ahadi nyingi zilifanyika kwa kumheshimu yeye Mtume wa Mungu. " Abu Talib

aliuliza, " Maana ya maapo hayo na ahadi?" Bahira alijibu: "Allahu taala aliwaagiza Mitume wote ikiwa ni pamoja na Issa (alaihis-salaam) kuwajulisha umma wao (wafuasi) kuhusu mtume wa mwisho "swallallahu alaihi wa sallam" ambae atakuja.

Abu Talib, baada ya kusikia maneno haya kutoka kwa Bahira, alibadilisha mawazo yake juu ya kwenda Dameski. Aliuza bidhaa zake zote za kibiashara huko Busra na kurudi Makka. Mkutano huu wa mtume wetu "swallallahu alaihi wa sallam" na Bahira ulikuwa wa kwanza na wa mwisho. Kwa hivyo, ilikuwa haiwezekani kwa mvulana mwenye umri wa miaka kumi na mbili kupokea kiasi chochote cha habari kuhusu dini kwa kipindi cha muda mfupi huo aliokuwa pamoja na Bahira.

Ingawa baadhi ya wanahistoria wa Kikristo wanasema kwamba mtume wa mwisho "swallallahu alaihi wa sallam" alipata masomo kutoka kwa padri aitwaye Mastura (lakini, kama walivyokiri) hawana ushahidi kwa hilo. Labda, huu pia ulikuwa mkutano mfupi.

Je! Inawezekanaje kwamba Quran tukufu, ambayo ni kubwa sana na maneno yake halisi ni maneno ya Allahu taala, yanaweza kuhesabiwa na mtu? Wakati Quran tukufu ikichunguzwa, inaonekana kwamba inafafanua kwa undani sheria za asili, ambazo siri zake zimejulikana hivi karibuni tu, na mageuzi ya maisha yenyewe. (Kwa mfano fomu ya maisha ya kwanza ilitoka kwenye maji, chakula cha ubinaadamu kimetengenezwa na vipengele vinashuka kutoka angani nk. Zaidi ya hayo, mifumo ya kijamii tunayojaribu kuikuza leo imeelezewa kwa njia ya mantiki zaidi na ya kuaminika. Haki ya kuwa na mali inafanyika chini ya jina "zakat." Kanuni za maadili bora na namna bora ya kuabudu hufundishwa. Hata kama alikuwa mtu mjanja sana, ufahamu huu na maarifa yake haiwezekani kuamini kwa mtu ambae hajawahi kusoma kitabu, au habari hii imejulikana au imeandikwa miaka 1400 iliyopita. Wakati aya za Quran tukufu zikishuka, Mtume hakujua maana yake yote, lakini alikuwa akimuuliza Jibril (alaihis-salaam) ili apate kujifunza. Ikiwa Wazungu wanakubali utume wake, hakuna shaka kwamba watakuwa Waislamu na hivyo kupata furaha ya milele. Tunatarajia kwamba siku moja baadae wataiamini na kuingia kwenye dini ya ukweli na hivyo watapata furaha isiyo na mwisho (mbinguni).

## JE, FALSAFA INAKUBALIWA KATIKA UISLAMU?

Hadi sasa, tumeelezea kwa ufupi kanuni za dini tofauti na tulivyoelezea dini nyengine hapo juu.

Sasa, tutaelezea kuhusu dini ya Uislam. Kwanza, tunajiuliza kwamba, je, tunaruhusiwa kutumia falsafa katika Uislamu?

Falsafa ni jina la matokeo ya uchunguzi na utafiti wa masomo fulani yanayotambuliwa na mtu kwa kutumia hekima, mantiki na majaribio. Kwa kifupi, “Falsafa” inamaanisha "Kutafuta asili ya kila kitu na kutafuta sababu ya kuwepo kwake". Katika lugha ya Kiyunani, Falsafa inamaanisha "Filosofia" (upendo wa maarifa) na inategemea msingi wa kufikiri kwa undani, kutafuta, kulinganisha, na kuchunguza. Ni muhimu kwa wale wanaohusika na falsafa kuwa na ujuzi wa kina katika sayansi na katika saikolojia. Hata hivyo, bila kujali ujuzi gani mtu anao, anaweza kuwa na hitilafu katika mawazo yake mwenyewe, au, mwisho wa majaribio yake, hitimisho lake linaweza kuwa baya pia. Ndiyo sababu hitimisho linalofanywa kwa njia ya falsafa haliwezi kuthibitishwa moja kwa moja.

Katika Quran tukufu kuna aina mbili za aya (mistari). Ayaat (Aya) ambazo maana yake zipo wazi sana. Hizi huitwa "**muhkam**" (ayat imara).

Na maana ya baadhi ya ayat haziwezi kueleweka kwa urahisi. Zinahitaji kuelezewa. Aya hizi zinaitwa "**muteshabih**" (ayat ya kimapenzi). Hadithi, maneno ya nabii "swallallahu alaihi wa sallam", yamegawanywa katika sehemu mbili, yaani, yale yalio imara na yale yanaofaa. Katika dini ya Uislam, umuhimu wa kufafanua hadithi hizo ulisababisha uanzishaji wa sayansi inayoitwa "**Ijtihad**". Mtume wetu "swallallahu alaihi wa sallam" pia, alifanya ijtihad mwenyewe. Ijtihad zilizofanywa na Mtume wetu na sahaba (marafiki [radiyallahu taala alaihim ajmain]) ni vyanzo vikuu vya ujuzi wa Kiislam.

Waislamu wapya waliuliza nini kitatokea kwa mambo waliyokuwa wanayafanya kabla kusilimu kwao na mwelekeo wa Uislamu wao, wasomi wa Kiislam walipaswa kujibu maswali yao. Majibu ya maswali kuhusu masuala ya sifa yaliunda tawi la elimu ya Kiislam linaloitwa **Kalam** (**itiqani**). Wataalamu wa "Kalam"

walithibitisha kimantiki kwa nini dini za awali zilikuwa si za ukweli. Wasomi hawa "rahmatullahi alaihim" walijitahidi sana kutatua mambo haya kwa kina. Walitumia sana ukweli pamoja na maarifa ya thamani sana ya "mantiki". Kwa upande mwingine, ilikuwa ni muhimu sana kuwaambia Waislamu wapya ukweli huu juu ya Allah. Kwamba Allah ni mmoja, aliyehai, hakuzaa mtu yeyote wala hakuzaliwa.

Hili lilifanyika kwa namna ambayo inawezakana kueleweka kwa urahisi. Wasomi wa Kalam walifanikiwa sana katika jitihada zao. Hata hivyo, wanasayansi wa Kiislam waliwasaidia katika kazi hii takatifu. Kwa mfano, Yaqub Ibn Ishaq al-Kindi, mwanazuoni wa mantiki na astronomy, alisoma kwa miaka mingi ili aigeuze imani ya wanaoabudu masanamu Sabi'i na Va-san'a, ambao waliona nyota kuwa takatifu, kwa imani yao hii isiyo sahihi. Hatimae, alithibitisha kuwa imani yao ilikuwa mbaya kwa kuwaonesha ushahidi tofauti. Jambo linalosikitisha kusema, ni kwamba, yeye mwenyewe aliathiriwa na mawazo ya falsafa ya kale ya Kigiriki na akajiunga na kundi lililoitwa "Muu'tazila." Alikufa Baghdad katika mwaka wa 260 (873).

Wakati wa Harun Rashid ", Khalifa wa tano kwa khilafat ya Abbasid, walianzisha taasisi inayoitwa" **Darulhikma**" katika mji wa Baghdad. Taasisi hii ilitumiwa kama kituo kikuu cha kutafsiri sio tu huko Baghdad, bali pia Damasko, Harram na Antiokia (Antakya) ambako vituo vile vya sayansi vilianzishwa. Kazi zilizoandikwa kwa Kigiriki na Kilatini zilitafsiriwa katika ofisi hizi pamoja na vitabu vilivyoandikwa katika lugha za Kihindi na Kiajemi.

Kwa kweli, Renaissance halisi (kurudi kwenye kazi za kale za thamani) ilianzia katika mji wa Baghdad. Kwa mara ya kwanza, kazi za Plato, Porphyrios na Aristotle zilifasiriwa katika lugha ya Kiarabu. Kazi hizi zilizingatiwa kwa makini na wasomi wa Kiislam "rahmatullahi alaihim". Walihitimisha kuwa baadhi ya maoni ya wanafalsafa wa Kigiriki na Kilatini walikuwa sahihi, lakini wengi wao walikuwa na uharibifu. Kwa sababu wao walikuwa kinyume na "Muhkam ayat, hadiths, mantiki na hekima". Iligunduliwa kuwa hawakujua ukweli wa sayansi na dini, na kwamba walifanya makosa zaidi katika mambo ambayo hayaeleweki kwa kutumia hekima. Wataalam halisi wa Kiislam, kwa mfano Imam-i Ghazali na Imam-i Rabbani "rahmatullahi alaih" walisema kuwa hawa wanafalsafa

hawakuamini misingi muhimu ya imani; Kwa hiyo, wataalam wa Kiislam waliripoti kwa undani imani isio sahihi ambayo iliaminiwa na wanafalsafa wasioamini dini ya ukweli.

Kuna maelezo zaidi juu ya jambo hili katika kitabu kinachoitwa **Al-Munkizu Aniddalal** kilichoandikwa na Imam-i Ghazali. Wataalam wa Kiislam wakati walikuwa wakielezea aya za "**mutashabi**" (aya) na hadithi, walifuata (walitegemea) tu ijtihad zilizotolewa na mtume Muhammad "swallallahu alaihi wa sallam" na sahaba zake. Wataalam wa Kiislam walikataa kabisa maoni ya falsafa ya kale yaliyo kwenda kinyume na Uislam, kwa hivyo waliulinda Uislam kutoharibiwa kama Ukristo ulivyokuwa. Lakini, watu wasiojua dini walichukuwa kutoka kwa wanafalsafa maneno mengi wakifikiri kwamba kila maneno ya wanafalsafa hao yalikuwa ya ukweli. Kwa hivyo, imani ya uharibifu ikaundwa katika Uislamu." Mtume wetu (swallallahu alayhi wa sallam) amebainisha kwamba vikundi sabini na mbili vitatokea katika Uislam. Wanafalsafa wengine, walijitokeza na waliongozwa na falsafa za Kigiriki, Kihindi, Kiajemi na Kilatini, kama vile Ibn Sina, Farabi, Ibn Tufayl, Ibn Rushd, na Ibn Bajje. Wanafalsafa hao katika mambo mengine walienda kinyume na ukweli wa Quran tukufu. Ibni Khaldun aliigawanya elimu ya Kiislamu katika sehemu mbili, yaani, "**Ulum-i Nak-liya**" [Tafsir, Qiraat, Hadithi, Fiqh, Farai, Kalam, Tasawuf] na **Ulum-i akliyya** [Mantiki, Fizikia, Hali, Kemia, Hesabu, Jiometri, Upimaji, Munazara, falaki]. Kundi la kwanza linaitwa "Maarifa ya Kidini." Matawi machache katika kundi la pili, ambalo linaweza kueleweka kwa majaribio, huitwa "ujuzi wa kisayansi."

Imam-i Muhammad Ghazali "rahmatullahi alaih" alijitahidi dhidi ya Wagiriki wa kale. Alichunguza falsafa ya Kigiriki na kukataa mawazo yao ambayo hakukubaliana nayo. Falsafa iliyochanganywa na imani za Kiislam wakati wa Harun Rashid "rahmatullahi alaih" ilikuwa ni mwongozo wa falsafa kama vile Montesquieu na Spinoza. Ambao walikiri waziwazi kwamba walikuwa chini ya Farabi, ambaye falsafa yake ilikuwa inaitwa "Farabius."

Imam-i Ghazali "rahmatullahi alaih" alijitahidi dhidi ya kundi la Dai ambalo ni la wa Shia. Kundi hilo lilikuwa ni la kwanza miongoni mwa makundi sabini na mbili ambayo mtume alitutahadharisha. Kulingana na falsafa ya Dai, wanadai kwamba Qurani tukufu ina mambo mawili, yaani, kipengele cha ndani (batini [isiyoonekana] na

kipengele cha nje (zahiri [inayoonekana]). Walijiita wenyewe "kundi la batini." Imam-i Ghazali "rahmatullahi alaih" anapinga falsafa zao na hakubaliani nao hata kidogo. Baada ya kushindwa, walitoka kwanye Uislamu kwa kusema na kutoa maana za uongo kwenye ayat (Aya) na Hadithi sharif ambazo maana zake hazikuwa wazi.

Hatimaye, washia hao wakawa "**Mulhids**" (wasioamini). Baadae, kwa kuwa walikuwa pia ni wana siasa, walipoteza uaminifu wao mkubwa kwa Waislam (Waislamu wa kweli).

Mashia walichanganya dini ya Kiislam na falsafa zao na wakajiita wenyewe kuwa ni wafuasi wa Hadhrat Ali "radiyallahu anhu". Baadae matawi mbalimbali ya Kishia yaliibuka. Kwa mfano kundi liloitwa Khawarij lilisema kuwa ni wafuasi wa Hadhrat Ali, lakini baadae wakaibuka kuwa adui wake. Kulingana na falsafa ya hao Mashia "Muislamu yeyote atakae fanya dhambi kubwa huwa kafiri." Ndiyo maana wanadai kwamba Hadhrat Ali na Hadhrat Muawiya (radiyallahu anhuma) ni makafiri (wasioamini).

Baadae, fikira mpya ilizuka kupinga wazo hili. Wao walitegemea mantiki yao tu na wakasema, "Hapa duniani mtu hawezi kumuhukumu Muislamu ambae amefanya dhambi kubwa, kama vile kumuua Muislamu mwingine. Hukumu juu yao itatolewa na Allahu taala siku ya Akhera. Kwa sababu hii, kundi hili la Washia halihisabiwi kuwa la wakafiri (wasioamini). "Na wafuasi wa falsafa hii mpya waliitwa jina la "**Mu'tazila**."

Falsafa nyengine iliyotokea kwenye Mashia iliitwa "**Galiya**," jina ambalo linamaanisha "wenye kuenea." Mashia wanasema kuwa Pepo na Jahannamu zipo duniani. Wao ni makafiri kabisa (wasioamini). Kwa sababu hakuna uhusiano kati yao na dini ya Uislam.

Maadui wa dini yetu ya Uislamu waliotaka kuubomoa walitoka ndani ya Uislamu na waliunda vikundi vidogo vidogo lakini vibaya sana, na wakajifanya kuwa chini ya jina la Uislam. Kwa mfano Bahai, Qadian na Tabligh-i Jama'at ni makundi maarufu sana waliotaka kuubomoa Uislamu.

1- BAHAIYA: Mfalme wao ni Mfarisi aitwaye Albab 'Ali. Mfalme huyo alikuwa anajiita kioo. Alikuwa anasema, Allahu taala anaonekana katika kioo chake hicho. Baha-ullah Alipokufa,

mwanae Abbas, alimrithi na akawa mkuu wa kikundi hicho. Abbas alipokufa mwaka 1339 (1921 A.D.), mwanawe Shawqi alichukuwa nafasi yake. Bahaullah alijidai kwamba alikuwa nabii. Katika falsafa yao, nambari kumi na tisa ni nambari takatifu. Aina zote za uasherati huhesabiwa kuwa heshima. Nawalichapa vitabu vingi katika lugha tofauti. Na wanadanganya watu kwa urahisi sana.

2- QADIANI: Hawa pia huitwa 'Ahmadiya'. Mheshimiwa profesa Abu Zuhra, wa Jami-ul-azhar, anasema, "Mirza Ahmad, muanzilishi wa Uhamadiya alikufa mwaka wa 1326 (1908 A.D.), alizikwa katika jiji la Qadian karibu na Lahore. Waqadian wanasema, kuwa Issa (alaihis-salaam) alikuja Kashmir baada ya kukimbia kwa Wayahudi na wanadai kwamba Issa (alaihis-salaam) alikufa kipindi alipo kuwa Kashmir. Maqadian hao wanamwita Ahmad Qadian kuwa mtume wao na wanasema, "Quran tukufu inafafanua kuwa Wayahudi na Wakristo ni watu wema.

Kwa hiyo, Waqadian wanaamini kuwa ni tendo la ibada kuwapenda Waingereza. Wanasema," Amri zinazohusiana na Jihad ni za kale, zimeharibika na ziko wazi. Wanasema: "Ikiwa mtu hatatuita 'kafiri,' hatutamwita kafiri. Hatukuruhusiwa kukubali binti zetu kuolewa na watu wasio wa Qadiani lakini tunaweza kuoa binti wao."

Allama Husain Muhammad (rahmatullahi alaih), aliyekuwa mwalimu katika shule ya Dir-i zur, aliandika katika kitabu chake **Ar-raddu' Alal-qadianiyya** kwa undani maneno ya Qadiani ambayo yanawafanya wawe makafiri. Kuna makafiri ambao wanajitambulisha kwa majina fulani kama ya Waislam. Hao wanapinga Wakristo na Wayahudi na kuthibitisha ukweli kwamba Uislamu ni dini pekee ya ukweli na ni muongozo pekee wa furaha. Hata hivyo Bahai, Qadian, Shia na mawahhabi huwadanganya watu hawa masikini kwa vikundi vyao vibaya. Msomi wa Fizikia Abdussalam, ambae alishinda tunzo la Nobel, ni Qadian. Ahmad Deedat, ambae aliwavutia Wakristo kuingia kwenye Uislamu mwaka 1980 na kujadiliana nao, sio Muislamu wa kisunni. Watu hao huzuia waislamu wapya kutofikia njia ya kweli ya kiislamu na furaha ya milele.

Masufi ni kundi la Waislamu wa kweli ambao huitwa Ahl as-Sunnat Watu hawa, msimamo wao mkuu sio falsafa. Kwa mujibu wao, ufahamu kamili wa Quran tukufu, na kuwa Muislam wa kweli,

inahitaji kufanya ibada kamili, na mtume wetu "swallallahu alaihi wa sallam", sio tu katika kufuata amri zake na makatazo yake, lakini pia kwa kujilazimisha kikamilifu kufuata mwenendo wake wa kitabia.

**Wanaume wenye sifa za Tasawuf**: Watu wanaoitwa Sufi walijitokeza katika kundi la Waislamu, kwa neno jingine huitwa Waislam wa "Ahl as-Sunna". Sufi haihusishwi na falsafa. Wanasema ili kuwa Muislamu halisi ni bora uelewe Quran tukufu, na vile sio tu ni muhimu kufuata amri na makatazo ya mtume wetu "swallallahu alaihi wa sallam", lakini pia tabia zake zote pamoja na kanuni zake za maadili ni vyema kuzitekeleza.

## Ifuatayo ni misingi ya Kisufi

1) **Faqr**, (Utafakari) ambayo ina maana, "Kufahamu kwamba daima unahitaji msaada wa Allahu taala." Kwao, "hakuna mtu isipokuwa Allahu taala ambae anauwezo wa kuumba viumbe vyote au kitu chochote. Allahu taala ni Muumba wa yote."

2) **Zuhd** na taqwa, "Kujihusisha na Uislam, kuzingatia kanuni zote za Uislamu katika maisha yako, kuwa na manufaa na kumwabudu Mola wakati wote.", neno "sofu" linatumika badala ya "sufi".

3) **Tafakkur**, utulivu na dhikr: "Kufikiria daima juu ya Allahu taala na baraka zake, na kutozungumza bila mpango wowote, na kutozungumza na mtu yeyote, bali kuzungumza kwa kadiri iwezekanavyo, na daima kurudia jina la Allahu taala kila wakati."

4) **Hal** na **Maqam**: "Kuelewa, kwa njia ya nuru (ujuzi) unaokuja kwako, kwa moyo wako na roho yako, na kujua kwamba imetakaswa kwa kiasi gani." "Kuwa na ufahamu wa mapungufu yako."

Mtu wa kwanza na maarufu sana kwa "sufi" alikuwa Hasan al-Basri "radiyallahu anhu" 21-100 (624-727). Hasan al-Basri alikuwa mchungaji mkubwa wa Kiislamu alikubaliwa kama imam (mujtahid) na Waislamu wote. Yeye ni maarufu kwa tabia zake nzuri na pia ujuzi wake usioweza kupatikana kwa watu wa kawaida. Hasan al-

Basri wakati alipohubiri aliweka hofu ya Allahu taala ndani ya mioyo ya wasikilizaji wake, na alikuwa mwanazuoni mzuri wa Hadithi kupitia kwa Hadithi nyingi zilizotumiwa.

**Wasil bin Ata**, muanzilishi wa falsafa ya Mu'tazila; alikuwa mwanafunzi wa Hasan-i Basri. Lakini, aliacha mafundisho ya al Basri. **Mu'tazil** inamaanisha kutengwa. Jina jingine linalotumiwa kwa **Mu'tazila ni Qadariyya**. Linatumika kwa sababu wanakataa qadar (hatima). Wanasema "Mtu ndiye muumbaji wa kile anachofanya. Wala Allahu taala hajui uovu au wema kabla hakujafanywa. Kwa hiyo, akitenda tendo baya atakuwa na jukumu kamili kwa hilo. Haiwezekani kuepuka jukumu hilo "Dhana hii, inayoitwa" qadariyya, "ilipendekezwa na Wasil bin Ata, ambae alikuwa mwanafunzi wa Hasan al-Basri na ambaye aliendelea kuhudhuria masomo yake. Kwa sababu hii Hasan al Basri, ambaye aliamini sana Qadar za Allahu taala, hakumkataa Wasil bin Ata kuwa mwanafunzi wake.

Lengo la Tasawwuf ni kufikia "Ma’rifat-Ilahiyya." Ma’rifat Ilahiyya maana yake ni kujua sifa za Allahu taala. Haiwezekani kwa mtu kutambua tabia za Allah za kipekee. Mtume wetu "swallallahu alaihi wa sallam" alisema: "**Msifikirie kuhusu tabia za Allahu** taala **za kipekee. Fikirieni kuhusu neema zake**." Mfano, hatupaswi kufikiria kuhusu Allahu taala yuko wapi, ila inafaa kufikiria kuhusu sifa na neema alizopewa binadamu katika kumjua Allah. Mara alisema: "**unapofikiria kuhusu tabia za Allah za kipekee, basi kile kinachokuja akilini mwako sio Allah**." Kipimo cha kufikiria na uwezo wa busara ya binadamu unamwisho wake. Hawezi kufahamu vitu vilivyopo juu ya kikomo hicho.

Anapofikiria sana anakosea. Hawezi kufikia ukweli. Busara na mawazo ya binaadamu haviwezi kufahamu siri na mambo ya elimu ya dini yenye kutatanisha. Ndio sababu watu wanaochanganya falsafa na elimu ya dini walitoka kwenye njia ya kweli iliyooneshwa na Uislam hatimaye wakawa **watu wa uzushi**. Watu wazushi sio makafiri, ni waislamu. Lakini walitoka kwenye njia ya kweli, na wamekuwa moja kati ya makundi sabini na mbili ya uzushi. Tunafaa kufikiria hivi: Hakuna kitu kwa jina la falsafa ya kiislamu. Kuna watu ambao wamechanganya falsafa na Uislam. Kulingana na wanazuoni wa Ahl as-Sunna, chimbuko la elimu ya kiislamu ni muhkam ayat (zenye maana ya wazi wazi) na hadithi za mtume, wala sio busara

za binaadamu au mawazo ya mtu. Msingi wa Tasawufu ni kujitambua mwenyewe. Tasawuf pia msingi wake ni mapenzi ya Allah. Haya yanaweza kufikiwa na kujirekebisha na kumfuata mtume Muhammad. Mtu anapojiendeleza kwenye njia ya Tasawuf, matukio mbali mbali yanajitokeza kwenye moyo wake. Watu wa tasawuf wanahisi muonekano wa Allahu taala kwenye nyoyo zao. Ndio maana kifo sio janga kwao, ila ni kitu kizuri na kitamu. Ina maanisha kurudi kwa Allahu taala kinawafanya kuwa na furaha. Mevlana Celaleddin Rumi "rahmatullahi alaih", msufi mkubwa, alikiita kifo "Shab-i Arus". Hakuna huzuni au kutokuwa na matumaini kwenye Tasawuf. Kuna mapenzi na muonekano tu. Maulana anasema: "mlango wetu sio mlango wa watu wasiokuwa na matumaini.

Dawa zinazotakiwa kutibu moyo zinatengenezwa kutokana na vitu vitatu. Kumiliki imani ya ukweli kama walivyofundisha wanazuoni salafu swaleh, kuabudu na kujilinda dhidi ya vitu vilivyokatazwa. Ni huzuni kusema, hao wasiojua dini ya kiislamu au Tasawuf ni kwa nini wanatumia dini kama njia ya kupata faida za dunia. Wanachanganya njia ya Tasawufu pamoja na vitendo vya kuabudu, na muziki ili kuzichanganya kwenye Tasawuf lionekane kama lilikuemo, hawajielewi hawa wamegeuza ibada za kidini kuwa kucheza ngoma kwa kusikiliza miziki kama sherehe za Mewlewi. Ingawa vitendo hivi havina uhusiano na Uislam, na havijatajwa kwenye aya au hadithi yoyote, watu hawa wanavionesha kutumia jina la dini ya sufi na sherehe za kiislamu. Mtume wetu "swallallahu alaihi wa sallam" na hakuna mmoja kati ya masahaba zake waliotekeleza sherehe kama hizi. Hawa ilikuwepo Tasawufu kwenye enzi zao. Lakini hakukuepo sherehe za derwish. Leo, Falsafa hii ya kizushi imetajwa katika vitabu vyote vya kigeni vilivyoandikwa kuhusu Tasawuf. Imam Ghazali "rahmatullahi alaih" alikuwa mwanazuoni wa kiislam katika elimu ya "Kalam" vile vile mtaalamu wa kweli kwenye nyanja ya Tasawuf. Inasemekana kwamba mwanazuoni wa kiislamu mkubwa pia Shaikh-ul Islam wa mfalme Sulaiman the Magnificent "rahmatullahi alaih", Abussu'ud Effendi "rahmatullahi alaih" 896-982 (1490-1574), aliwatesa sana watu wa Tasawuf na alifika hatua ya kutoa uamuzi rasmi kuwaua kwa kuwanyonga. Madai haya sio kweli. Abussu’ud Effendi aliwatesa vibaya wale derwish waliopotea na wanaojichanganya na watu wa

Tasawuf wa kweli au wale waliokuwa wanadai kwamba: "Watu ambao wamefika daraja ya juu kwenye Tasawuf hawatii amri za kidini. Hawatakiwi kujishugulisha wenyewe na mambo yalioruhusiwa na yaliokatazwa. Kwao hakuna tofauti. Abussu'ud alitoa uamuzi rasmi wa kifo kwa wale wanaotenda dhambi zinazosababisha ugomvi nchini kote.

Kiongozi wa watu waliokataa wale wanaochanganya falsafa na elimu ya kiislamu ni mtume Muhammad "swallallahu alaihi wa sallam". Hadithi hii ni maaruf sana: "**Umma wangu utagawika katika makundi sabini na tatu. Sabini na mbili ya makundi hayo yatakwenda kwenye moto wa Jahannam, na kundi moja tu litakuwa salama. Na hao ndio wale wanaonifuata na Sahaba zangu**." Hadithi hii tukufu, inayotabiri ya baadae, ni muujiza mkubwa. Ilitokea kama alivyotabiri. Wanazuoni wa kiislamu wamefafanua makundi sabini na mbili haya kwa upana, waliochanganya falsafa na itikadi za kiislamu na wakaacha njia ya ukweli iliokuwa ya masahaba wa mtume. Chini ya muangaza wa hadithi ya mtume Muhammad "alaihis-salaam" iliotajwa hapo juu, wanazuoni wa kiislam walipinga makundi hayo kwa kutumia ushahidi mwingi sana. Mmoja wa wanazuoni wa kiislam wakubwa ni Sayyid Sherif Jur-jani "rahmatullahi alaih". Mwanazuoni wa kiislam huyu, aliyekuwa amefikia daraja la Wilayat kwenye Tasawuf alikufa mnamo mwaka 816 (1413) kwenye mji wa Shiraz. Kitabu chake **Sherh-i Ma-waqif** kimejaa ushahidi wa aina hii. Pia, Sa'daddin-i Taftazani, "rahmatullahi alaih", aliefikia daraja la juu kwenye elimu ya Kalam, alifuta falsafa za kizushi kwa kutumia kitabu chake chenye thamani kinachoitwa **Sherh-i aqaid**. Alikufa kwenye mji wa Samarkand mnamo mwaka 792 (1389). Na kitabu **Al-Milal wan nihal** kilichoandikwa na Muhammad Shehrestan "rahmatullahi alaih", aliyekufa mwaka 548 (1153), kimejaa dalili za kupinga hilo. Kitabu hiki kilichopo kwenye lugha ya kiarabu na tafsiri yake ya kwenye lugha ya kituruki vimechapishwa mara kwa mara. Kilitafsiriwa kwenye lugha za Ulaya na UNESCO; kwa hivyo, imeeleweka na ulimwengu wote kwamba hakuna falsafa katika asili ya Uislamu, na sio sahihi kusema "falsafa ya kiislamu."

Imam Muhammad Ghazali "rahmatullahi alaih" alichunguza Tasawuf na metaphysics na akafafanua kwenye vitabu vyake **al-Munkiz** na **at-Tahafut-ul falasifa** kwamba hawa wanafalsafa

walitegemea kwenye akili tu, kwamba walikosea sana, na watu wa Tasawuf kwa kufuata ayat na hadithi walifikia imani ya kweli na neema za milele. Alichunguza kila moja ya falsafa za makundi ya uzushi sabini na mbili, ambao kama tulivyosema awali, ni waislamu, na kuona kwamba makundi hayo yote yameshawishika na wanafalsafa wa kigiriki.

Ikiwa sisi ni waaminifu tutaona vizuri kwamba falsafa ya wanaoitwa "**makundi ya kizushi**" haiendani sambamba na ukweli, tuseme kwa mfano haiendani na Quran al-kerim na Hadithi sharif za mtume. Katika karne yetu, vifungu walivovitoa kwenye falsafa za kigiriki za zamani havipewi umuhimu. Tukilinganisha falsafa za makundi ya wazushi moja na jengine, tutaona kwamba wote wanakubaliana kwa ukweli kwamba Allahu taala ni mmoja, kila kitu kinatoka kwake, ndie mtawala kabisa. Uislam ndio dini ya ukweli kabisa na ndio dini ya mwisho; Quran tukufu ni neno la Allahu taala na Muhammad (alaihis-salaam) ndie mtume wake wa mwisho. Ukweli huu wote umesemwa na makundi yote yenye uzushi. Wanamtazama binaadamu kuwa kiumbe mtakatifu sio muasi. Wakrisito nao wanadai hivyo hivyo. Makundi sabini na mbili yote ni waumini na waislamu. Hata hivyo, kwa mtazamo wao, akili, falsafa na dini ni kitu kimoja. Ndio maana kuna baadhi ya tofauti katika itikadi zao. Kwa kuwa wanategemea falsafa tofauti, baadhi ya mgawanyiko wa wazi wazi na mapambano yameanza kati yao. Yupi kati yao ni sahihi anafahamika kwa kuwatathmini kwa kutumia taarifa sahihi kutoka kwenye hadithi sharif za mtume "alaihis-salaam". Haiwezekani kulitambua kundi sahihi kwa kutumia nguvu au kwa kujifanya adui au kwa mtu mmoja kuwatukana watu wengi kwamba ni makafiri.

Kulingana na wanazuoni wa kiislam, Uislam unakataza kuvamia mambo matano. Na haya ndio: 1) Uhai, 2) Mali, 3) Akili, 4) Kizazi, 5) Dini. Mzushi akisema kwamba falsafa yake ndio ilio sahihi kuliko zingine zote na kwa ajili hio anaua na kuangamiza kiunyama na hasikilizi ushauri wowote, basi kwa hali hiyo, tunasema kwamba mtu huyu ana upungufu wa dini au akili. Sasa, acha tuangalie tena mengi kuhusu yapi anayotaka Allahu taala kutoka kwa Muislamu wa ukweli na yale aliyomuamrisha kufanya kupitia aya za Quran tukufu wakati tunaacha falsafa hizi zilizochanganywa na elimu ya imani na watu wazushi huko nyuma. Jambo la ukweli ni kwamba

hakuna falsafa kwenye Uislam. Makundi sabini na mawili ya uongo yaliujeruhi Uislamu kwa kuchanganya falsafa na Uislam. Kwa upande mwengine, walichanganya falsafa ya Kigiriki ya zamani na itikadi za Uislam, na kwa upande mwengine walibadilisha itikadi za kidini kulingana na mawazo yao na misimamo yao. Lakini kikundi cha hii ni kwa sababu imani ya kiislamu inalingana na akili ya kawaida. Hekima ya mtu ikiwa na shaka na kitu chochote katika Uislam, basi inafahamika kwamba hekima ya mtu huyu ni sakim sio salim. Kwa kawaida, hekima yoyote au mawazo ambayo yanauchukulia Uislamu kuwa wenye upungufu na kwa hivyo yanajaribu kuukamilisha kwa kutumia falsafa lazima ieleweke kama yana kasoro. Kundi sahihi ni lile ambalo haliangalii matakwa yake ya kibinafsi bali linaangalia haki zaidi atafuata akili yake ya kawaida, maadili yake na huenda yatakuwa sawa na amri za Allahu taala. Imeelezewa kwenye mwisho wa mlango wa kitabu cha tafsiri cha **Riih-ul Beyan** kilichoandikwa na Ismail Hakki kwamba Allahu taala atampa mtu huyu imani ya ukweli. Wanazuoni "rahmatullahi alaihim" waliwataja wanafalsafa wa Kigiriki katika vitabu vyao kwa kuwapinga tu. Makundi ya uzushi na yaliyopotea yalijaribu kuchanganya falsafa ya Kigiriki na imani za Kiislam, lakini kundi la Ahl as-Sunna lilijaribu kuzitenganisha na kuziweka nje ya dini ya Uislam. Kisha mtu ambae anataka kujifunza Uislam kwa usahihi ili kuelewa kile Allahu taala amemaanisha kwenye maneno yake lazima asome vitabu vilivyoandikwa na wasomi wa Ahl as-Sunna wa Jamaat.

Sura Yunusu aya 45: **Hakika Allahu taala Hawadhulumu watu chochote, lakini watu wanajidhulumu wenyewe.**

Sura Ar-Raad aya 12: **Hakika Allahu taala Habadili yaliyoko kwa watu mpaka wabadili yaliyomo ndani ya nafsi zao.**

Sura Yunus 109: **basi najiongoza na kufuata njia nzuri ya Allah, anaeongoka ni kwa faida ya nafsi yake, na anayepotea, basi anapotea kwa hasara ya nafsi yake, na mimi si mlinzi juu yenu.**

Sasa tunafaa kuwa watu wa aina gani? Allahu taala anafafanua watu wanaomuamini katika qur-an:

Sura Furqan aya 64-75: **Na watumishi wa Rahmani ni wale wanaotembea ardhini kwa unyenyekevu, na wajinga wakisema nao husema: Amani** (iwe juu yenu)**, Na wale wanaokesha usiku kwa ajili ya Mola wao kwa kusujudu na kusimama. Na wale**

**wanaosema: Mola wetu, Utuondolee adhabu ya Jahanamu, bila shaka adhabu yake ndio iendeleayo. Hakika (Jahanamu) hiyo ni kituo kibaya na mahali (pabaya) pa kukaa. Na wale ambao wanapotumia hawatumii kwa fujo wala hawafanyi ubahili, na wanakuwa waadilifu baina yao. Na wale wasiomwabudu mungu mwingine pamoja na Allahu taala, wala hawaui nafsi aliyoiharimisha Allahu taala isipokuwa kwa haki, wala hawazini, na atakayefanya hilo bila shaka atakutana na adhabu ya dhambi yake. Atazidishiwa adhabu siku ya kiama, na atakaa humo kwa kufedheheka. Ila yule aliyetubia na kuamini na kufanya vitendo vizuri, basi hao ndio Allahu taala Atawabadilishia maovu yao kuwa mema na Allahu taala ni Msamehevu, Mrehemevu. Na aliyetubia na kufanya wema, basi kwa hakika yeye anatubu kwa Allahu taala toba hasa. Na wale ambao hawashuhudii uwongo, na wanapopita penye upuuzi, hupita kwa heshima. Na wale ambao wanapokumbushwa Aya za Mola wao hawazipuuzi kwa uziwi na upofu. Na wale wanaosema: Mola wetu! Utupe katika wake zetu na watoto wetu yanayoburudisha macho, na Utujaalie kuwa viongozi kwa wamchao (Mungu).**

Sura Al-Maidah aya 9: ... **Na uadui wa watu baina yenu usiwashawishi kuacha kufanya uadilifu…**

Sura Al-Maidah aya 90: **Allahu taala Hatawakamateni kwa viapo vyenu vya upuuzi, lakini Atawakamateni kwa viapo mlivyoviapa kwa nia…**

Maana ya tafsiri ya baadhi ya sura kama Naml na Sura Al-Baqara ni: **Allah yuko pamoja na wenye subira. Vumilieni. Kuwa mvumilivu. Kwa ajili ya Allah.**

Sura Al-Baqarah aya 218: ... **Na fitina ni mbaya zaidi kuliko kuua...**

Sura Al-Baqarah aya 265: **Enyi mlioamini, msiharibu sadaka zenu kwa masumbulizi na udhia...**

Sura Al-Baqarah aya 272: **Kama mkitoa sadaka kwa dhahiri ni vizuri, na kama mkitoa kwa siri na kuwapa mafakiri, basi huo ni ubora kwenu...**

Sura Al-An-am 152 na Sura Furqan aya 68: **...Usiue nafsi...**

Sura Aaraf aya 32: **...kuleni na kunyweni wala msifanye is-rafu hakika Yeye Hawapendi wanao fanya israfu.**

Sura Aaraf aya 57: **Wala msifanye uharibifu katika nchi ikiisha tulia…**

Sura Ibrahim aya 27: **Na mfano wa neno baya ni kama mti mbaya ambao umeng'olewa ardhini, hauna uimara.**

Sura Nahl aya 90: **Kwa hakika Allahu taala Anaamuru uadilifu, na hisani, na kuwapa (watu kama uwapavyo) ndugu, na Anakataza upunjufu, na uovu, na uasi...**

Sura Al-Isra 22-24 na Ahqaf aya 15: **Na Tumemuusia mwanaadamu afanye wema kwa wazazi wake, mama yake amechukuwa mimba yake kwa taabu na akamzaa kwa taabu na kumbeba na kumwachisha ziwa ni miezi thelathini, hata anapofikia baleghe yake na akawa mwenye umri wa miaka arobaini, akasema: Ee Mola wangu, Uniwezeshe kushukuru neema Zako ulizonineemesha mimi na wazazi wangu, na ili nifanye vitendo vizuri Unavyovipenda, na Unifanyie wema katika watoto wangu, kwa yakini ninatubia Kwako, na hakika mimi ni miongoni mwa waliosilimu.**

Sura Al-Isra aya 27: "**Na umpe ndugu haki yake, na maskini na msafiri, wala usitumie (mali yako) kwa ubadhirifu.**"

Sura Al-Isra aya 29: "**Na kama unatengana nao kwa kutafuta rehma ya Mola wako unayoitumai, basi sema nao kwa maneno laini.**"

Sura Ta Ha aya 132: "**Wala usivikodolee macho yako Tulivyowafaidisha watu wengi miongoni mwao ni mapambo ya maisha ya dunia ili Tuwajaribu. kwahivyo, na riziki ya Mola wako (Akupayo) ni bora mno na iendeleayo sana)**".

Sura Ar-Rum aya 33: "**Katika wale waliotenga dini yao wakawa makundi-makundi, kila kundi hufurahia waliyo nayo.**"

Sura Ash-Shuura aya 14: "**simamisheni dini wala msifarakiane nayo…**"

Sura Al-Jathiya aya 19-20: "**Kisha Tumekuweka juu ya sheria hasa katika amri, basi ifuate, wala usifuate matamanio ya wale wasiojua. Kwa yakini hao hawatakufaa chochote mbele ya Allahu taala, na hakika wadhalimu ni marafiki wao kwa wao, na Allahu taala ni rafiki wa wamchao.**"

Sura Al-Fat-h aya 29: "**Allahu taala Amewaahidi walioamini na kutenda mema msamaha na ujira mkubwa.**"

Sura Al-Hujurat aya 10: "**Na ikiwa makundi mawili katika waaminio wanapigana, basi fanyeni suluhu kati yao…**"

Sura Ash-Shuura aya 41: "**Na malipo ya ubaya ni ubaya ulio sawa nao, lakini anayesamehe na kusuluhisha, basi ujira wake ni juu ya**
**Allahu taala, bila shaka Yeye Hawapendi wadhalimu.**"

Sura Al-Hujurat aya 7: "**Enyi mlioamini! Kama fasiki akiwajieni na habari yoyote, basi pelelezeni, msije mkawadhuru watu kwa ujahili na mkawa wenye kujuta juu ya yale mliyoyatenda.**"

Sura Al-Hujurat aya 11: "**Kwa hakika waaminio ni ndugu, basi fanyeni suluhu baina ya ndugu zenu, na mcheni Allahu taala ili mrehemewe.**"

Sura Al-Hadyd aya 24: "**Ili msihuzunike juu ya kitu kinachowapoteeni wala msijigambe juu ya Anachowapeni. Na Allahu taala Hampendi kila ajivunaye, ajifaharishaye.**"

Sura Al-Isra aya 36: "**Na timizeni kipimo mpimapo, na pimeni kwa mizani iliyo sawa. Hayo ni wema na bora mwishoni.**"

Sura Ar-Rahman aya 10: "**Na pimeni kipimo kwa haki wala msipunguze mizani.**"

Sura Al-Mutaffifyn aya 2-5: "**Maangamizo kwa wapunjao! Ambao wanapojipimia kwa watu hupokea (kipimo) kamili, Lakini wanapowapimia kwa kipimo au mizani, wao hupunguza. Je! wao hawafikiri ya kwamba watafufuliwa.**"

Zaidi, ingawa waja wake wanaweza kuchukuwa tahadhari juu ya amri zake, anajua kwamba watafanya, kama binaadamu, wanakosea, na anatueleza katika Quran tukufu kwamba atawahukumu kwa usawa na rehma.

Sura Nahl aya 62: "**Na lau Allahu taala Angaliwakamata watu kwa sababu ya dhuluma yao, Asingaliacha hata mnyama mmoja...**"

Sura Ankabuut aya 8: "**Na walioamini na kufanya vitendo vizuri, kwa yakini Tutawaondolea maovu yao, na Tutawalipa mema ya yale waliyokuwa wakiyafanya.**"

Sura Az-Zumar aya 36: "**Ili Allahu taala Awafutie ubaya walioufanya na kuwalipa ujira wao kwa wema waliokuwa wakifanya.**"

Sura Ash-Shuura aya 26-27: "**Naye ndiye Anayepokea toba za watu wake, na Husamehe makosa, na Huyajua mnayoyatenda. Na Huwajibu wanaoamini na kutenda wema na Huwazidishia fadhili Zake, lakini makafiri wana adhabu kali.**"

Sura Muhammad aya 3: "**Na wale walioamini na wakatenda mema na wakaamini yaliyoteremshwa juu ya Muhammad, nayo ni haki iliyotoka kwa Mola wao, Atawaondolea maovu yao na atarekebisha mienendo yao.**"

Sura An-Najm aya 33: "**Ambao wanajiepusha na madhambi makuu na vitendo vibaya isipokuwa makosa hafifu, bila shaka Mola wako ndiye Mwenye maghufira tele...**"

Sura An-Naziat aya 41-42: "**Na ama yule aliyeogopa Enzi ya Mola wake, na akaikataza nafsi matamanio maovu, Basi kwa hakika**
**Pepo ndiyo makao.**"

Sura Saba aya 18: "**Nasi Hatumwadhibu ila anayekufuru.**"

Kwa ufupi, msingi wa Uislam ni kutii maamrisho matukufu ya Allahu taala ambayo yanautuliza moyo, yanaisafisha nafsi, na ni rahisi kwa kila mtu kuifahamu. Misingi ya falsafa inayojengwa na mawazo ya binaadamu tu. Tunafaa kuzisoma kwa ajili ya ya kuzifuata, na tunafaa kukubali na kutekeleza maamrisho ya Allahu taala yalioandikwa kwenye Quran tukufu. Hivi ndio Uislam wa kweli. Allahu taala anawakataza waislam kuwa na itiqad nyingi, kuanzisha vikundi mbali mbali, au kuwa na tofauti za kiitiqad miongoni mwao.

Allah anawakataza waislamu kufanya vikao vya siri au kuanzisha jumuiya za siri kwa lengo la kuhujumiana. Aya kuhusu jambo hili ni kama zifuatazo:

Sura Al-Mujadilah aya 10-11: "**Enyi mlioamini! Mnaposhauriana kwa siri, basi msishauriane juu ya dhambi na jeuri na kumwasi Mtume, bali shaurianeni juu ya wema na uchamungu, na mcheni Allahu taala Ambae Kwake mtakusanywa. Kwa yakini kushauriana kwa siri kunatokana na Shetani ili awahuzunishe wale walioamini, lakini hawezi kuwadhuru chochote ila kwa idhini ya Allahu taala, na waaminio, basi wamtegemee Allahu taala tu.**"

Sura Al-Jathiya aya 18: "**Na Tukawapa maelezo ya amri, basi hawakuhitilafiana ila baada ya kuwafikia elimu, kwa uasi baina**

**yao, hakika Mola wako Atahukumu kati yao siku ya kiama katika yale waliyokuwa wakihitilafiana.**"

Sura Ar-Rum aya 33: "**Katika wale waliogawa dini yao wakawa makundi-makundi, kila kundi hufurahia waliyo nayo.**"

Sura Al-Hadyd aya 21: "**Jueni ya kwamba maisha ya dunia ni mchezo na upuuzi na pambo na kujifurahisha baina yenu, na tamaa ya kuzidiana katika mali na watoto. Mfano wake ni kama mvua ambayo huwafurahisha makafiri maotesho yake, kisha yanakauka na unayaona yenye rangi ya manjano, kisha yanakuwa yenye kuvunjika-vunjika, na katika Akhera ni adhabu kali na maisha ya dunia sio ila ni starehe idanganyayo.**"

Kuna jambo lengine zaidi ya hili linaloweza kuelezea ukweli kwamba dunia hii ni njia tu ya kupata dunia ya pili.

Tunafaa kutekeleza maamrisho ya dini yetu ya Uislam kwa nguvu zetu zote kuliko kudanganywa na matamanio ya dunia na hatimaye kupotea. Muislam ambae ana itiqadi sahihi na ana elimu sahihi ya dini na ambae hajadanganywa na wale waliopotea kutoka kwenye njia ya ukweli anategemewa kuwa mtu mwaaminifu, mwanazuoni wa kweli, mwananchi mwenye uzalendo na mtiifu wa sheria za nchi. Ni mzuri yeye mwenyewe na ni mzuri kwa nchi yake.

Uislam unamuheshimu mtu. Allahu taala anasema: "**Nimemuumba binadamu katika umbo lililo bora zaidi katika viumbe.**" Maisha ya binaadamu ni muhimu sana mbele yake. Allahu taala Anasema: "**Usiue nafsi...**" Wakristo wanadai kwamba binaadamu ni kiumbe duni, mwenye dhambi, lakini madai haya yanakataliwa kabisa na Uislam. Binaadamu wote wanazaliwa wakiwa waislamu. Wanazaliwa pia wakiwa safi.

Waislamu nao pia wanazaliwa wakiwa watukufu. Maana ya aya arubaini za mwanzo za Sura Az-Zumar ni: "**Kwa yakini Tumekuteremshia Kitabu kwa ajili ya watu kwa haki, basi anayeongoka ni kwa nafsi yake, na anayepotea bila shaka anapotea kwa hasara (ya nafsi) yake...**" Allahu taala alimtuma mja wake mpendwa Muhammad "alaihis-salaam" kama mtume pamoja na kitabu chake Quran tukufu kama muongozo wa binaadamu. Wale wasiofuata njia ya wazi iliyooneshwa na Quran tukufu na mtume wa mwisho Muhammad "alaihis-salaam" kwa sababu hawataki basi watapewa adhabu kali.

Sasa tuangalie aya zifuatazo kwa uangalifu:

Sura Sad aya 88: "**Huu sio chengine chochote ila ni ukumbusho kwa walimwengu.**"

Sura al-Isra aya 16: "**Anayeongoka, basi anaongoka kwa ajili ya nafsi yake tu, na anayepotea, basi anapotea kwa hasara (ya nafsi) yake. Wala hatabeba yeyote mzigo wa mwingine. Na hatukuwa wenye kuadhibu mpaka Tumepeleka Mtume.**"

Kwa hiyo tunafaa kumuomba Allahu taala kutuongoza kwenye itiqad ya kweli. Ili hili kuwezekana tunastahiki kuifahamu dini ya kiislam ambayo ni dini ilio sahihi na dini ya mwisho, pia na kusoma vitabu vilivyoandikwa na wanazuoni wa **kiislam** ambao wameufafanua Uislam vizuri.

Allahu taala hawafanyi binaadamu kuwa waislamu au waumini isipokuwa kwa wale wanao taka kuwa hivyo kwa maana nyengine maisha yake ya baadae mtu huyachagua mwenyewe. Vyote viwili rehma yake na adhabu zake ni za milele. Pia uadilifu wake ni wa milele. Allahu taala akipenda, anamuongoza mtu yoyote kwenye itiqad sahihi bila sababu yoyote au mahitaji yoyote kutoka kwa mtu huyo. Imeripotiwa awali kwamba atawapa mwongozo na itiqad sahihi watu ambao vitendo vyao na tabia zao ni nzuri kulingana na akili zao za kawaida. Itajulikana pale anapoondoka duniani kwamba amekufa na itiqadi yake. Mtu ambae anaishi na itiqadi yake sahihi lakini akaipoteza itiqadi yake kwenye siku za mwisho kwenye maisha yake basi mtu huyu anakufa bila itiqadi na atafufuliwa miongoni mwa watu wasiokuwa na itiqadi. Kila siku tunafaa kumuomba Allahu taala kutuwezesha kufa tukiwa na itiqadi zetu sahihi. Kwa kuwa Allahu taala ana rehma ya milele, amewatuma mitume kwa waja wake kuwaelezea kuhusu uwepo wake na umoja wake yaani kuwa hana mshirika wala msaidizi, na kuwaelezea vitu ambavyo anataka waja wake waviamini.

Itiqadi maana yake ni kukubali vile alivyosema mtume "swallallahu alaihi wa sallam". Yoyote asiemuamini mtume na vile alivyokuja navyo, mtu huyu atakuwa kafiri.

Na kwa ajili hio basi kafiri huyo atakuwa hakufuata alio amrishwa na atachomwa na moto wa milele baada ya kifo chake.

Mtu ambaye hakupata taarifa kuhusu mtume lakini kwa kutumia akili zake mwenyewe akafikiria na akaona kwamba "Allah

yupo na ni mmoja" na akafariki na itiqadi hio, ataingizwa kwenye pepo pia.

Kuchomwa milele ni natija ya kumkanusha mtume "alaihis-salaam" hali ya kuwa umepata taarifa kuhusu yeye. Hata hivyo, kuna wanazuoni wa kiislam wakubwa wanaosema kwamba "yoyote ambaye hafikirii na kuamini kwamba Allahu taala yupo, basi moja kwa moja atakwenda jahannam," lakini maneno yao inamaanisha yule ambaye hajafikiria baada ya kupata habari za mtume "alaihis-salaam". Yule mwenye akili timamu hatomkanusha mtume. Atamuamini moja kwa moja bila kusita.

Abu Talib, ammi yake mtume Muhammad "alaihis-salaam", mara kwa mara alikuwa anasema kwamba mapenzi aliyonayo kwa mtume mtoto wa ndugu yake ni makubwa kuliko kwa wanawe, kwa kiasi kuwa anamtetea sana. Ni ukweli wa kihistoria, kwamba kuambatana kwake kukubwa na utamaduni alikokuwa nako kulimzuia kukubali Uislam licha ya juhudi zake mtume Muhammad "alaihis-salaam" lakini hadi kufikia kufa bila kuukubali Uislam ni mtihani mkubwa sana.

Kukabiliwa na viambatanishi kama hivi ni ugonjwa mkubwa wa nafsi. Na watu wengi wameanguka kwenye mtego huu kwa sababu ya nafsi zao, na mwisho wake zimewazuia kupata furaha ya milele. Allahu taala anasema katika hadithi qudsi, "**Itambue nafsi yako kama adui wako, na ndio adui Wangu!**" mkaidi huyu sio rahisi kumkimbia hasa kwa mtu ambae kazaliwa na wazazi wakiristo na kalelewa chini ya mafunzo ya kikiristo. Rafiki zake wanaweza kumuonea au familia yake kumtenga akibadilisha dini. Pengine labda atakosa kazi au cheo akiwa Muislam. Kweli, kila mfano hapo juu ni sababu, lakini sababu kuu ni: leo waislam hawafahamu dini yao. Zaidi ya hayo, habari mbaya kuhusu Uislamu, tafsiri mbaya, hadithi na wajinga wa dini waliogeuka na kuingia kwenye moja ya makundi ya uzushi sabini na mbili, kama vile wadanganyifu, maandishi ya kiburi yalioandikwa na wanasayansi wasioamini chini ya jina la sayansi. Kwa upande mwengine, kila tunapozungumza na mkiristo msomi kuhusu yalioandikwa ndani ya kitabu hiki, tunakuta kwamba anahisi mapenzi ya Uislam.

Kuhusu mada ya kuelezea Uislam kwa njia isio sahihi, nchi za kiislam ndio wamekuwa hatari sana kwa Uislam. Watu waliotengana na dini kwenye baadhi ya nchi, ambazo idadi yake ni

kama thelathini, wameufanya ulimwengu kupata sura na habari zisizo sahihi na hisia mbaya kuhusu Uislam. Quran tukufu inatafsiriwa vibaya katika nchi za kiislam ambazo waislam wametengana na dini yao. Zaidi ya hayo baadhi ya mitume, kwa mfano Adam "alaihis-salaam" anakataliwa. Bila shaka, baada ya muda, viongozi wa serikali za nchi hizo watatambua ukweli na kuacha njia hizo zenye makosa na watagunduwa njia ya ukweli iliyooneshwa na mamilioni ya vitabu vyenye thamani vilivyoandikwa na wanazuoni wa ahlu haki wa kiislam. Lakini, kwa sasa kutokana na siasa zao za uongo na namna wanavyoongozwa, wanaujeruhi Uislam sana.

Mtume wetu Muhammad "swallallahu alaihi wa-sallam" alisema kwamba, yeyote ambaye hana imani atachomwa kwenye moto milele. Ujumbe huu ni sahihi. Tunafaa kuukubali ujumbe huu kama tunavyoamini kwamba Allahu taala yupo na ni mmoja. Kuchomwa kwenye moto milele maana yake ni nini?

Yeyote anayefikiria msiba wa kuchomwa milele inawezekana kupoteza akili zake kwa sababu ya hofu atakayopata. Angalau, ataanza kutafuta njia za kuepuka janga hili. Dawa yake ni rahisi sana. "**Kuamini kwamba Allahu taala yupo na ni mmoja, Muhammad "alaihis-salaam" ni mtume wake wa mwisho na kwamba kila alichosema ni ukweli**" inamlinda mtu dhidi ya janga la kudumu. Ikiwa yoyote atasema kwamba haamini kwenye janga kama hilo la kuchomwa milele eti lipo, na kwamba haogopi kitu chochote kama hicho, na kwamba hawezi kutafuta njia ya kujikinga na janga hilo, basi mtu huyu tutamuuliza: una ushahidi wowote au dalili ya kutoamini? Ukweli gani au ushahidi gani wa sayansi unaokuzuia kuamini ujumbe huu? Kiukweli hawezi kutoa dalili yoyote. Inakuwaje nifikirie ambalo halijaegemea kwenye dalili yoyote au ushahidi liitwe elimu au sayansi? Neno la namna hiyo huitwa dhana au uwezekano. Sio jambo zuri kujiepusha na kuogopa janga kama hilo la kuchomwa milele kwenye moto japokuwa kuna moja kati ya milioni moja au moja kati ya bilioni moja uwezekano wake kutokea? Mtu mwenye akili timamu asijaribu kujiepusha?

Asijaribu kutafuta njia ya kujiokoa mwenyewe dhidi ya uwezekano huu wa kuchomwa kwenye moto milele?

Kama unavyoona, kila mtu mwenye akili timamu ana imani. Ili kuwa na imani, huwezi kujiweka kwenye matatizo, kama kulipa

ushuru au kutoa mali kwa ajili ya kuupiga vita na kuuhujumu Uislam, kubeba matatizo na balaa ya kuabudu, au kushikamana na utamu na vitu vya kufurahia. Inatosha kuamini kwa moyo. Hutakiwi kuweka wazi wazi imani yako kwa wasio amini dini. Hali ya kuwa ni binadamu na viumbe wenye akili, watu wasioamini kuwepo kwa moto wa milele wanategemewa angalau kukubali uwezekano wake.

Kuwa dhidi ya uwezekano wa kuchomwa kwenye moto milele sio ujinga ila ni masikitiko makubwa kujiepusha kuwa na **IMAN** ambayo ndiyo dawa pekee ya janga hili. Sanaullah Pani-Puti "rahmatullahi alaih" alieleza katika kitabu chake **Huquq-ul-Islam**, "kuwepo kwa Allahu taala. Sifa zake na vitu vinavyokubaliwa na kuhakikishwa na yeye vinaweza kufahamika kwa njia ya ujumbe wa mitume. Haviwezi kueleweka kwa njia ya kuelezea. Mtume Muhammad "alaihis-salaam" alitueleza vitu hivyo. Na vilisambazwa kila sehemu kwa juhudi za Khulafa-i Rashidin. Kila mmoja wa Ashabu-al-Kiram alikuwa amesoma baadhi ya elimu. Waliikusanya elimu hii. Katika suala hili, Ashab-i Kiram wana haki juu yetu. Kwa sababu hii, tumeamrishwa kuwapenda, kuwashukuru na kuwatii wote. Kitabu hiki kwenye Lugha ya Persian (kiajami) kilichapishwa Lahore na pia İstanbul mnamo mwaka 1410 [1990] na Hakikat Kitabevi.

## HÜSEYN HILMI IŞIK “rahmatullahi alaih“

Hüseyn Hilmi Işik, "rahmatullahi alaih", mchapishaji wa Hakikat Kitabevi Publications, alizaliwa katika Eyyub Sultan, Istanbul mwaka 1329 (1911 A.D.).

Miongoni mwa vitabu mia na arobaini na nne alivyochapisha, sitini ni vya Kiarabu, ishirini na tano vya Kiajemi, vya Kituruki kumi na nne, na vilivyobaki ni vitabu vya Kifaransa, Kijerumani, Kiingereza, Kirusi na lugha zingine.

Huseyn Hilmi Işik, "rahmatullahi alaih" (aliyoongozwa na Sayyid' Abdulhakim Arwasi, "rahmatullahi alaih", mwanazuoni maarufu wa dini na sifa kamilifu katika Tasawuf na uwezo wa kuwaongoza wanafunzi kwa kukomaa kikamilifu, mwenye utukufu na hekima), alikuwa mwanazuoni mwenye uwezo mzuri wa Kiislam mwenye uwezo wa kuongoza furaha, alifariki wakati wa usiku kati ya Oktoba 25, 2001 (8 Sha'ban 1422) na Oktoba 26, 2001 (9 Sha'ban 1422). Alizikwa katika Eyyub Sultan, ambako alizaliwa.

## Mwisho

Hitimisho la kitabu hichi kimelenga kuelimisha jamii ya kiislamu katika nchi ya za Afrika. Nimejaribu kutumia lugha ambayo ni rasmi katika nchi za mashariki pia nimejaribu kutafsiri baadhi ya maneno ambayo ni ya kielimu zaidi ili kuja kwenye lugha ya kiswahili kwa lengo la kuwafaidisha wasomaji wa rika zote. Pia nimetumia uslubu ya kielimu nyingi ya fiqhi kwa baadhi ya mada lakini pia nimejaribu kutumia uslubu wa mijadala kwa baadhi ya vifungu nilivokuwa natoa hoja au kujibu hoja kwa wanaokwenda kinyume na mtazamo wangu pia nimejaribu kunukuu vitabu tofauti vya zamani na vya sasa ili kuonesha ushahidi wa ninayoyazungumza lakini pia nimetumia aya za Qur-an na hadithi ili kubainisha hoja zangu na nilipoelezea kuhusu Uislamu nimeingia ndani zaidi kuelezea kuhusu masufi ili kubainisha yale ambayo masufi wanayafanya na kuyaamini na kuweka wazi ili kama kuna vitendo vinanasibishwa nao ambavyo haviko katika hayo ambayo nimeyataja hapo juu basi itakuwa ni uzushi tu juu ya Uislam lakini nilikuwa simaanishi kama Uislamu ni usufi tu bali nilikuwa najaribu kuonesha uhalisia ulivyo na ukweli wa mambo.

**BOOKS PUBLISHED BY HAKIKAT KITABEVI**

**ENGLISH:**

1– Endless Bliss I, 304 pp.

2– Endless Bliss II, 400 pp.

3– Endless Bliss III, 336 pp.

4– Endless Bliss IV, 432 pp.

5– Endless Bliss V, 512 pp.

6– Endless Bliss VI, 352 pp.

7– The Sunni Path, 128 pp.

8– Belief and Islam, 128 pp.

9– The Proof of Prophethood, 144 pp.

10– Answer to an Enemy of Islam, 128 pp.

11– Advice for the Muslim, 352 pp.

12– Islam and Christianity, 336 pp.

13– Could Not Answer, 432 pp.

14– Confessions of a British Spy, 128 pp.

15– Documents of the Right Word, 496 pp.

16– Why Did They Become Muslims?, 304 pp.

17– Ethics of Islam, 240 pp.

18– Sahaba ‘The Blessed’, 560 pp.

19– Islam’s Reformers, 320 pp.

20– The Rising and the Hereafter, 112 pp.

21– Miftah-ul-janna, 288 pp.

22– Book of Namaz, 240 pp. 23– O Son, 352 pp.

**DEUTSCH:**

1– Islam, der Weg der Sunniten, 128 Seiten

2– Glaube und Islam, 128 Seiten

3– Islam und Christentum, 352 Seiten

4– Beweis des Prophetentums, 160 Seiten

5– Geständnisse von einem Britischen Spion, 176 Seiten

6– Islamische Sitte, 288 Seiten

**EN FRANÇAIS:**

1– L'Islam et la Voie de Sunna, 112 pp.

2– Foi et Islam, 160 pp.

3– Islam et Christianisme, 304 pp.

4– L'évidence de la Prophétie, et les Temps de Prières, 144 pp.

5– Ar-radd al Jamil, Ayyuha'l-Walad (Al-Ghazali), 96 pp.

6– Al-Munqid min ad'Dalal, (Al-Ghazali), 64 pp.

**SHQIP:**

1-Besimi dhe Islami, 96 fq.

2-Libri Namazit, 208 fq.

3-Rrefimet e Agjentit Anglez, 112 fq.

**ESPAÑOL:**

1-Creencia e Islam, 112.

2-Libro Del Namaz, 224. PO

**BOSHNJAKISHT:**

1-Iman i Islam, (128) str.

2-Odgovor Neprijatelju Islama, (144) str.

3-Knjiga o Namazu, (192) str.

4-Nije Mogao Odgovoriti, (432) str.

5-Put Ehl-i Sunneta, (128) str.

6-Ispovijesti Jednog Engleskog Spijuna, (144) str.

**Swahili:**

1-Iman na Uislam

2-Dini ya Kiislam